Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 31 Mei, 2014**

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne. S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa naomba tukae.

Katibu tuendelee?

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Bunge na Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 Pamoja na Maoni nya Kamati Kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara hiyo, kwa Mwaka 2014/2015.

**MHE. PROF. PETER MAHAMUDU MSOLLA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. MOSES J. MACHALI K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA MAJI:**

Taarifa ya Msemeji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Maji Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu tuendelee?

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 - Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia**

**SPIKA:** Mheshimiwa Rajabu?

Mheshimiwa Waziri, kidogo tu naomba ukae.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba Mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 68(7) ya Kanuni zetu za Bunge na kwa kuzingatia vilevile Kanuni ya 64(1)(a), lakini vilevile Kifungu kidogo cha (f).

Mheshimiwa Spika, jana wakati Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Profesa Muhongo, anahitimisha Hoja yake, alitoa shutuma kali dhidi ya Wabunge wa Kambi ya Upinzani ya kwamba, Wabunge wa Kambi ya Upinzani wako baadhi ambao wamehongwa na *IPTL.* Ushahidi anao na *CD* kupitia *CCTV* anayo.

Kwa hiyo, hizi shutuma ni nzito na zinadhalilisha Kambi ya Upinzani na zinadhalilisha Wabunge wako. Tunaamini kwamba, Wabunge wa Kambi ya Upinzani wako *clean* kabisa na hawajihusishi na mambo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakuomba Mwongozo Wako kwamba, kama kweli ushahidi anao na hiyo *CD* anayo basi aiwasilishe kwako. Ikiwezekana ichezwe hapa, ili waonekane au wajulikane wale ambao wamefanya udhalimu huo dhidi ya Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo Wako.

**SPIKA:** Kwamba, *CD* itachezwa hapa haiwezekani ndio maana tuna Kamati inaitwa Kamati ya Haki na Maadili ya Wabunge, ndio sababu hiyo. Lakini Mwongozo Wako tutaushughulikia wakati unaofaa.

Mheshimiwa Mtoa Hoja?

Wabunge wanavyopenda ubishani humu ndani, aah! Tuendelee na kazi.

Mheshimiwa Mtoa Hoja? *(Makof/Kicheko)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia Taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako na Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Wizara yangu, naomba kutoa Hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi

na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Malengo ya Wizara katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia Pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha, 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana leo kushiriki katika Mkutano huu wa Bunge unaojadili Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, niruhusu sasa niungane na Waheshimiwa Wabunge, Ndugu na marafiki katika kuwafariji na kuwapa pole familia, Ndugu, na wapiga kura wa Marehemu Mheshimiwa William Mgimwa aliyekuwa Mbunge wa Kalenga na Mheshimiwa Saidi Ramadhani Bwanamdogo, aliyekuwa Mbunge wa Chalinze.

Napenda pia, kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, Ndugu na marafiki wa marehemu. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Godfrey Mgimwa kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Kalenga na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Chalinze. Ushindi wao ni kielelezo tosha kuwa wananchi wana imani kubwa na Chama cha Mapinduzi (CCM) katika kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 imetekeleza majukumu na mipango yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2013/2014, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010–2015.

Aidha, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imezingatia Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Nyuklia ya Mwaka 2013, Sera ya Taifa ya Bayoteknolojia ya mwaka 2010, Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo ya mwaka 2010, Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996, Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya mwaka 2003, Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu ya mwaka 1997 na Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2013/2014. Mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ilitengewa jumla ya Sh. 63,147,599,460. Kati ya fedha hizo, Sh. 27,218,364,000 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Sh. 20,212,187,000/= zilikuwa ni kwa ajili ya Mishahara na Sh. 7,006,177,000 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Fedha za Maendeleo zilizoidhinishwa zilikuwa Sh. 35,929,235,460 ambapo fedha za ndani zilikuwa Sh. 30,295,482,000 na fedha za nje zilikuwa Sh. 5,633,753,460/=.

Mheshimiwa Spika, majukumu yaliyotekelezwa na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na Taasisi zake katika kipindi cha mwaka 2013/2014 ni kama yafuatayo. Kwanza UTEKELEZAJI KATIKA SEKTA YA MAWASILIANO, Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unatekelezwa kwa awamu tano ambapo awamu ya I na II zimekamilika na zinatumika tangu mwaka 2012 zikiwa na jumla ya kilomita 7,560. Kwa sasa Wizara ipo katika utekelezaji wa awamu ya III inayohusisha ujenzi wa vituo vitatu mahiri vya kutunza kumbukumbu *(Internet Data Centres)* vitakavyojegwa Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar.

Pia, katika awamu hii utajengwa mtandao wa intaneti wa kasi *(Internet Protocol/Multiprotocol Label Switching Network (IP/MPLS)* pamoja na kuunganisha Unguja na Pemba katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Utekelezaji wa sehemu ya kwanza (I) ya awamu ya tatu (III) umeanza rasmi Desemba, 2013 ambapo hatua za ujenzi wa kituo mahiri cha kutunza kumbukumbu katika eneo la Kijitonyama, Dar es Salaam zimeanza.

Mheshimiwa Spika, Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi Katika Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Ujenzi wa Mikongo ya Mijini *(Metro Networks)*. Wizara kwa kutambua umuhimu wa kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma za mawasiliano inatekeleza Awamu ya IV ya Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa kushirikiana na makampuni ya simu *Tigo, Airtel* na *Zantel.*

Awamu hii itagharimu jumla ya Dola za Kimarekani milioni 80 ambazo zitagharamiwa na makampuni hayo ambapo serikali itatoa ruhusa ya kutumia hifadhi ya njia *(Right of Way)*. Umiliki wa mikongo ya mijini inayojengwa kwa utaratibu huu utakuwa ni wa serikali wakati makampuni hayo yatapewa sehemu ya mikongo hiyo kwa ajili ya matumizi yao binafsi. Aidha, utekelezaji katika Jiji la Dar es Salaam umekamilika ukiwa na jumla ya kilomita 91 zilizogharimu Dola za Kimarekani milioni sita. Hatua inayofuata ni utekelezaji katika Miji ya Morogoro, Arusha, Mwanza na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika Njia ya Reli. Katika kuhakikisha kuwa Mkongo unafika katika maeneo mengi zaidi, serikali kwa kushirikiana na kampuni za simu *(Airtel, Tigo* na *Zantel)* wamekamilisha taratibu za kuanza ujenzi wa mkongo katika njia za reli kuanzia Dar es Salaam hadi Mwanza, Tabora hadi Kigoma na Dar es Salaam hadi Arusha.

Mheshimiwa Spika, juhudi za Serikali katika Kupeleka huduma za *TEHAMA* kwa Watumiaji wa Mwisho. Serikali katika kuhakikisha kuwa inakuza matumizi ya *TEHAMA* nchini hususan katika kutumia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, inatekeleza yafuatayo. Kwanza, Uunganishwaji wa Vyuo vya Elimu ya Juu na Taasisi za Utafiti katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, wizara inaratibu utekelezaji wa mradi wa kuunganisha Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Madhumuni ya mradi huu ni kuimarisha mfumo wa utoaji wa huduma katika Taasisi za elimu ya juu na utafiti kwa kuimarisha matumizi ya *TEHAMA* kwa njia ya kuwekeza katika miundombinu ya *TEHAMA* inayoziunganisha Taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya mradi huu ilikusudia kuunganisha Taasisi 28; hadi kufikia mwezi Mei, mwaka huu 2014 tayari Taasisi 18 zilikuwa zimeunganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Uwezeshaji wa Matumizi ya *TEHAMA* kwa Gharama Nafuu. Katika kuhakikisha kuwa matumizi ya *TEHAMA* yanaongezeka hasa katika taasisi za serikali, shule, hospitali na vyuo vya elimu, Wizara inatekeleza mradi wa *Regional Communication Infrastructure Program (RCIP)* unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ukiwa na lengo la kuwezesha Taasisi hizi kutumia intaneti kwa bei nafuu, kuongeza upatikanaji wa huduma za *Broadband,* kuongeza ufanisi na uwazi wa Serikali kupitia matumizi ya serikali mtandao. Wizara imekamilisha ujenzi wa mtambo wa *Internet Bandwidth* na ununuzi wa *Internet Bandwidth* yenye ukubwa wa *1.55Gb* kwa sekunde ambayo tayari imeanza kutumika. Hadi kufikia mwezi Mei, 2014 jumla ya taasisi 42 zimeunganishwa na zingine 25 zipo katika utaratibu wa kuunganishwa.

Mheshimiwa Spika, Uwezeshaji wa Serikali Kufanya Mikutano kwa Kutumia *TEHAMA*. Wizara inaendelea na juhudi za kuhakikisha kuwa matumizi ya *TEHAMA* katika ofisi za Serikali yanaongezeka. Wizara imenunua mitambo ya *Video*

*Conferencing* 26 kwa ajili ya kuendeshea vikao kwa njia ya mtandao. Hadi kufikia mwezi Novemba, 2013 mitambo 25 ilikuwa imefungwa katika Makao Makuu ya Mikoa 21, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na *TAMISEMI*.

Aidha, taratibu za kufunga mitambo ya aina hiyo katika makao makuu ya mikoa mitano ya Zanzibar pamoja na Ofisi ya Rais wa Zanzibar zimekamilika na inatarajiwa kufungwa mwishoni mwa mwezi Juni, mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Kukuza Matumizi ya *TEHAMA* kwenye Shule za Msingi na Sekondari. Katika kuhakikisha kuwa matumizi ya *TEHAMA* katika shule yanaongezeka kwa kasi na kuweka mazingira ya kutumia elimu mtandao. Wizara inatekeleza mradi wa majaribio wa shule mtandao *(E-schools)* ukiwa ni sehemu ya juhudi za Serikali katika kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kuunganisha Shule.

Mpaka sasa vituo 49 zikiwemo shule 43, vituo vya posta vitatu na vyuo vya afya vitatu vimepelekewa na kufungiwa vifaa vya *TEHAMA* pamoja na kufanyiwa mafunzo ya matumizi bora ya vifaa hivyo. Aidha, taratibu za kumpata mzabuni kwa ajili ya shule nyingine 80 zipo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, Usalama Katika Matumizi ya *TEHAMA*. Kukua kwa kasi kwa matumizi ya *TEHAMA* kumeleta mafanikio mengi katika nyanja mbalimbali za maisha ya kila siku, kama vile, mabadiliko katika huduma za mawasiliano, huduma za kibenki na mitandao ya kijamii. Sambamba na hilo mafanikio hayo yameleta changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na uhalifu katika mitandao *(Cyber Crimes)*.

Katika kulitambua hili, Wizara imekamilisha rasimu ya miswada mitatu ya Sheria za Usalama wa Mtandao *(Cyber Security Laws)*. Kwanza ikiwa Sheria ya Kulinda Taarifa Binafsi *(Personal Data Protection)*, Sheria ya Miamala ya Ki-Elektroniki *(Electronic Transaction)* na Sheria ya Kudhibiti Uhalifu wa Mitandao na Kompyuta *(Computer and Cyber Crime)*. Rasimu hizi zimewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ili ziweze kuandaliwa kwa mujibu wa taratibu za uandishi wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Kufikisha Huduma za Mawasiliano Vijijini. Wizara imeendelea kushawishi sekta binafsi kufikisha mawasiliano kwenye maeneo yasiyo na mvuto kibiashara. Kupitia juhudi hizi kampuni za simu zimeridhia kwa hiari yao kupeleka mawasiliano kwenye jumla ya Kata 163 kwa awamu ya kwanza "A" na awamu ya kwanza "B". Katika awamu ya kwanza "A", kampuni za simu zitapeleka mawasiliano kwenye Kata 44 kwa gharama zao na Kata 33

kwa ruzuku ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kupitia mkopo wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kampuni za simu zimeshiriki kwenye zabuni ya awamu ya kwanza "B" ambapo jumla ya Kata 86 zimepata wazabuni kwa ruzuku ya Mfuko wa Mawasiliano kwa wote. Ushiriki wa kampuni za simu kwenye zabuni za Mfuko wa Mawasiliano kwa wote umeongezeka kwa asilimia 213 kutoka Kata 52 mwaka 2012/2013 hadi kufikia Kata 163 mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, mfuko upo katika hatua za mwisho za ujenzi wa miundombinu ya Mawasiliano katika Kata 52 zenye jumla ya vijiji 316 na wakaazi laki saba thelathini na saba elfu mia tatu na sabini na nane. Mara baada ya kukamilika awamu yote ya kwanza huduma ya mawasiliano inategemea kufikia vijiji 1,268 vyenye wakaazi milioni moja laki tisa arobaini na tisa elfu mia mbili na kumi na tisa katika Kata 215 zenye ukubwa wa eneo la kilomita za mraba laki moja, thelathini na tatu elfu mia mbili na themanini na tisa. Eneo hili likiwa sawa na asilimia kumi na nne ya eneo lote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imefanya tathmini na kubaini kuwa jumla ya Kata 1,365 zina tatizo la mawasiliano ambapo jumla ya Shilingi bilioni 328 zinahitajika ili kuweza kulipatia ufumbuzi tatizo hili. Kwa takwimu hizi, ni dhahiri kuwa hitaji la mawasiliano bado ni kubwa ikilinganishwa na kasi tunayokwenda nayo kwa kutegemea fedha za mkopo wa Benki ya Dunia na makusanyo kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote. Katika kukabiliana na changamoto hii Serikali inaangalia vyanzo vingine vya fedha ndani na nje ya nchi, ikiwa ni pamoja na kuwasilisha andiko la mradi kwa lengo la kuomba fedha za mkopo nafuu kutoka Serikali ya India ili kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, Ukuaji na Mchango wa Sekta ya Mawasiliano. Mazingira mazuri yaliyowekwa na Serikali kwenye Sekta ya Mawasiliano yameonesha matokeo makubwa. Idadi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano nchini imeendelea kuongezeka kutoka laini za simu za mikononi milioni 2.96 mwaka 2005 hadi kufikia milioni 27.45 mwezi Desemba mwaka jana. Watumiaji wa mfumo wa intaneti nao wameongezeka kutoka milioni 3.56 mwaka 2008 hadi kufikia milioni 9.3 mwezi Desemba 2013. Pia, kuna ongezeko kubwa la huduma kupitia mawasiliano ya simu za mkononi. Huduma hizo ni pamoja ununuzi wa bidhaa mbalimbali na miamala ya kifedha ambayo ina watumiaji wapatao 12,330,962. Kati ya kipindi cha Julai, 2013 hadi Aprili, 2014 jumla ya miamala 972,641,605 yenye thamani inayofikia shilingi Trilioni 28.3 imefanyika kupitia mitandao ya simu za mkononi.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji Mpana wa Mpango wa Kubadilisha Teknolojia ya Utangazaji Kutoka Analojia kwenda Dijitali. Mambo yaliyofanyika ni pamoja na tathmini ya utekelezaji wa awamu ya kwanza katika maeneo ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Moshi, Mwanza na Tanga ili kubaini mafanikio na changamoto. Matokeo ya tathmini yanaonyesha kuwa zoezi la uhamaji katika awamu hiyo lilifanikiwa kwa asilimia 89. Mafanikio hayo yaliwezeshwa na uelewa wa kutosha kupitia elimu kwa umma iliyotolewa katika maeneo husika, kuwepo kwa ving'amuzi vya kutosha katika maeneo ya uzimaji na gharama ya ving'amuzi wakati wa uzimaji kuwa chini ikilinganishwa na hapo awali.

Mheshimiwa Spika, baada ya tathmini hii, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaendelea na utekelezaji mpana katika maeneo yaliyosalia ili kukamilisha zoezi hili ndani ya muda tuliojiwekea. Hadi hivi sasa zoezi la uzimaji wa mitambo ya analojia kwa awamu ya pili, lililoanza tarehe 31 Machi, 2014 limekwishafanyika katika miji ya Tabora, Singida, Musoma na Bukoba. Leo hii ninaposoma hotuba hii uzinduzi wa mitambo ya dijitali unaendelea katika mji wa Kahama. Aidha, taratibu za uzimaji katika miji ya Iringa, Kigoma, Lindi, Morogoro, Mtwara na Songea zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Septemba, 2014.

Mheshimiwa Spika, mpango huu umetekelezwa kwa mafanikio makubwa na hivi sasa wananchi katika miji yenye matangazo ya dijitali wanaweza kupata *chaneli* nyingi za televisheni ikilinganishwa na hapo awali na hivyo kuwa na wigo mpana wa kupata habari. Utekelezaji huu umeifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza katika Afrika kutekeleza makubaliano ya nchi wanachama wa Umoja wa Kimataifa wa Mawasiliano ya kuzima mitambo ya analojia ifikapo tarehe 17 Juni, 2015.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya yanaifanya Tanzania kuwa mfano wa kuigwa na mataifa mengine ambapo nchi za Uganda, Kenya, Zambia, Lesotho na Malawi zimekuja kupata uzoefu. Aidha, Afrika ya Kusini hivi sasa inajiandaa kuwaita wataalam wetu kwenda kutoa uzoefu nchini humo. Vilevile, mwezi Februari, 2014 Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa nchi wanachama wa Taasisi ya mawasiliano ya nchi za Jumuiya ya Madola kuhusu mabadiliko ya teknolojia ya utangazaji kwa lengo la nchi hizo kupata uzoefu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kulishukuru Bunge lako Tukufu, wadau wa sekta na wananchi kwa ujumla kwa ushirikiano katika utekelezaji wa zoezi hili muhimu. Aidha, nirudie tena kutoa wito kwamba, zoezi hili ni muhimu na lina lengo la kuifanya nchi yetu iendane na mabadiliko ya teknolojia yanayotokea

duniani ambayo hayaepukiki. Naomba kutoa wito kwa wadau wote watoe ushirikiano kwa vyombo vinavyohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuimarisha mfumo wa udhibiti katika sekta ya mawasiliano. Wizara imeendelea na mpango wa kuboresha mazingira ya udhibiti kwa kuanzisha mtambo wa kuhakiki na kusimamia huduma za mawasiliano nchini yaani *Telecommunication Traffic Monitoring System (TTMS)* kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Mtambo huu wa *TTMS* ulipatikana kwa kushirikiana na sekta binafsi kwa utaratibu wa *Build Operate and Transfer* ulioanza kufanya kazi mwezi Oktoba, 2013. Katika kufanikisha azma hii Wizara ilitengeneza Kanuni zinazosimamia mawasiliano kupitia Mitandao ya simu yaani *Poca TTMS Regulation* 2013. Kwa mujibu wa Kanuni hizi kampuni za nje ya nchi zinatakiwa kulipa senti ishirini na tano (25) za kimarekani kwa kila dakika moja ya mazungumzo ya simu inayoingia nchini.

Pia Kanuni hizi zimeweka mgawanyo wa mapato hayo ya senti ishirini na tano (25) ambapo Serikali kupitia Hazina inapata senti saba (7), watoa huduma wanapata senti kumi na tatu (13) na senti tano (5) ni kwa ajili ya uendeshaji wa mitambo ikiwa ni pamoja na kumlipa mwekezaji wa mtambo huo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Januari, 2014 mfumo huu umeweza kuiingizia Serikali jumla ya Shilingi Bilioni 6.8 ambazo hapo awali hazikuwepo. Malipo haya ni kipindi cha Oktoba, 2013 mpaka Januari, 2014. Kwa hivi sasa mtambo unaratibu dakika za maongezi kwa simu za kimataifa na kufuatilia udanganyifu yaani *fraud* kwa simu zinazoingia nchini ambapo mpaka sasa hivi udanganyifu umepungua kutoka asilimia 60 kabla ya mtambo kufungwa hadi chini ya asilimia 2 hivi sasa. Wahusika wa udanganyifu wamefikishwa mahakamani na kesi zinaendelea. Kazi nyingine zinazokamilishwa ni kuuwezesha mtambo huu kuratibu dakika za maongezi kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine yaani *interconnection* pamoja na kufuatilia miamala yaani *money transactions* inayopitia kwenye mitandao ya simu za mkononi.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano inasimamia mfumo madhubuti wa Taifa wa kuhakikisha usalama wa mitandao wa mawasiliano ya komputa. Mradi huu ulianzishwa rasmi mwezi Septemba, 2012 na hadi hivi sasa umekuwa ukiendelezwa hatua kwa hatua. Kikosi maalum cha Ulinzi cha Kielektronic yaani *Computer Emergence Respond Team* kimeanzishwa na kinahusika na uhakiki wa usalama katika matumizi ya TEHAMA hapa nchini. Kikosi hiki kinawataalamu wenye ujuzi wa hali ya juu kuhusu usalama wa mitandao ya mawasiliano na kimekwisha anza kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta yaani *POCA* mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Matibabu Mtandao. Wizara kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam inaendelea na utekelezaji wa mradi wa Matibabu Mtandao unaounganisha *DIT,* hospitali za Muhimbili, Amana, Temeke, Mwananyamala, Tumbi, Bagamoyo na Hospitali ya Rufaa ya Mbeya kwa kushirikiana na Wizara za Afya na Ustawi wa Jamii na wadau wengine wa maendeleo. Usimikaji wa mitambo na vifaa na mafunzo kwa madaktari wanaohusika na mradi huu vimekamilika. Majaribio ya Mradi yanaendelea yakihusisha madaktari wa hospitali zilizotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji Mpana wa kuweka Miongozo ya Mpango wa Anuani ya Makazi na Misimbo ya Posta. Baada ya kukamilika kwa utekelezaji kwa hatua ya majaribio ya Mpango wa Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta katika miji ya Arusha na Dodoma, Wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kushirikiana na wadau wengine imeanza utekelezaji mpana wa mpango huu yaani *roll out* kwa kuanzia mkoa wa Dar es Salaam ambapo umeanza mwezi Desemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru wadau wote wanaohusika na mpango huu hususan uongozi wa mkoa wa Dar es Salaam na Manispaa zote tatu za mkoa huu kwa ushirikiano mkubwa waliouonyesha katika utekelezaji wa mpango huu. Kimsingi, Halmashauri zimeshiriki kikamilifu katika kubainisha majina ya mitaa, kukusanya, kuweka vibao vya namba za nyumba na majina katika mitaa kumi zilizochaguliwa kuanza utekelezaji Kata tano Ilala, Kata mbili Temeke na Kata tatu Kinondoni. Lengo ni kukamilisha utekelezaji wa mpango huu katika Kata zote za Mkoa wa Dar es Salaam ifikapo mwezi Desemba mwaka huu. Sambamba na hilo, Wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeziwekea Wizara zote na baadhi ya Taasisi Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta ambazo tayari zimeanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, kupitia uzoefu uliopatikana katika Mkoa wa Dar es Salaam, wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inakamilisha uandaaji wa mwongozo unaoweka mfumo bora wa kitaasisi wa kutekeleza mpango huu katika maeneo mengine nchini. Aidha, rasimu ya mpango wa utekelezaji katika maeneo mengine ya nchi umeandaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kuendelea Kuweka Mifumo ya Kisera na Kuimarisha Uratibu wa Sekta ya Mawasiliano. Katika kuweka mazingira mazuri ya kukuza sekta ya mawasiliano na kuimarisha uratibu, Wizara imekamilisha uandaaji wa rasimu ya sera mpya ya TEHAMA inayohuishwa na rasimu ya mkakati wa Utekelezaji wa sera hiyo ambapo kwa pamoja vipo katika hatua ya uwasilishwaji ili kuridhiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mfumo wa uratibu wa kisekta, wizara imeendelea kukamilisha taratibu za kuanzisha Tume ya TEHAMA. Uchambuzi wa majukumu ya Tume na mlinganisho baina yake na Taasisi nyingine umefanyika kwa umakini. Aidha, rasimu ya Tamko la Rais la kuanzisha Tume hiyo limekwisha pitia hatua mbalimbali za ukamilishwaji. Tume inatarajiwa kuwa imeanza kazi mwezi Septemba, mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Jamii Habari. Kwa kutambua umuhimu wa kuwa jamii iliyojengwa kwa misingi ya maarifa katika kufanikisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Finland imeendelea kutekeleza mpango wa kujenga jamii habari mpango huu unahusisha utekelezaji wa programu ya kuimarisha uwezo wa Wizara katika kusimamia sekta ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia na programu ya kukuza ubunifu nchini kupitia TEHAMA. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 programu hii kupitia wataalam wa Taasisi ya Menejimenti ya Mashariki na Kusini mwa Afrika yaani ESAMI imefanya tathmini ya kubaini mahitaji ya kuimarisha uwezo wa Wizara ikiwa ni pamoja na mpango kazi wa utekelezaji wa mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza ubunifu nchini mpango huu umeendelea kusaidia juhudi za kukuza ujasiriamali kwa kuwezesha kituo cha ubunifu kinachoitwa Buni kilichoko *COSTECH* ambapo takribani wajasiriamali 300 hushiriki katika makongamano mbalimbali kwa wiki. Katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Aprili, 2014 jumla ya makongamano arobaini na tano yamefanyika katika kituo cha Buni. Aidha mpango huu umeendelea kusaidia uendelezaji wa vituo saba vya utatuzi wa changamoto za kijamii yaani *living labs* vilivyopo Kigamboni, Iringa, Mwanza, Sengerema, Mbeya, Arusha na Zanzibar. Vilevile, mradi huu umeratibu jumla ya ziara nne za kubadilishana uzoefu baina ya wataalam wa Tanzania na Finland ambapo wataalam na viongozi kutoka Tanzania walitembelea taasisi wenza nchini Finland na wataalam na wafanyabiashara kutoka Finland walitemebelea Tanzania. Idara na Taasisi zilizohusika na mpango huu za elimu ya juu ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam, Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* na wasimamizi wa vituo vya *living labs*. Kupitia mpango huu, hivi sasa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela vimeanza ushirikiano na vyuo vyilivyoko huko nchini Finland.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji Katika Sekta ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Maboresho katika Mfumo wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini yaani *National Innovation System Reform Programme.* Maendeleo ya uchumi na jamii yanaendana sambamba na ongezeko la matumizi mapana ya

Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Pamoja na ukweli huu, katika nchi yetu sayansi, teknolojia na ubunifu havichangii ipasavyo katika maendeleo hayo kutokana na jinsi na mfumo wa ubunifu ulivyo hapa nchini. Kimfumo, sayansi, teknolojia na ubunifu ni dhana mtambuka na manufaa yake makubwa yanapatikana pale ambapo wadau wote nchini wanatumia maarifa, udadisi au utafiti na ubunifu kwa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa, ubunifu na utafiti umeachwa kuwa ni jukumu la taasisi chache hususan, vyuo vikuu na taasisi za utafiti, ambazo hazizungumzii baina yao na watumiaji wa matokeo ya utafiti huo, jambo ambalo limedumaza mchango wa sayansi, teknolojia na ubunifu katika maendeleo ya jamii na uchumi. Ili kukabiliana na hali hiyo na kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani, Wizara kupitia programu ya mageuzi ya Sayansi na Teknolojia imekamilisha uundwaji wa mfumo mahsusi wa Sayansi, Teknolojia na ubunifu nchini. Chini ya mfumo huu, mabadiliko makubwa ya kiutendaji yatafanyika, mifumo mipya ya kitaasisi itaanzishwa na sheria mpya ya sayansi, teknolojia na ubunifu itatungwa ambayo itaweka mazingira mazuri ya namna ya kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu nchini. Kuwepo kwa mambo haya kwa pamoja ndani ya mfumo huu kutavutia wadau mbalimbali kuchangia maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu tofauti na ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeanza kutekeleza baadhi ya mambo yaliyopendekezwa kwenye mfumo huu. Baadhi ya mambo hayo ni kupitia upya Sheria Namba 7 ya Mwaka 1986 iliyounda Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia kwa kuandaa rasimu ya sheria ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Pia kupitia Sheria Namba 7 ya Mwaka 2003 iliyounda Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kuzipa Taasisi za Sayansi na Teknolojia Zilizo Chini ya Wizara, Mwelekeo Mpya wa Kitaalam. Kama sehemu ya kwanza ya maboresho ya mfumo wa ubunifu nchini, Taasisi zilizo chini ya Wizara zimeendelea kujielekeza katika kuanzisha na kuweka mifumo mipya ya kitaaluma itakayowezesha kujenga wataalam wenye ubunifu na ambao sio tu watategemea kuajiriwa, bali watakuwa na uwezo wa kuzalisha ajira mpya wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela – Arusha, kulifanywa kwa mtazamo huu wa kutayarisha wataalam wenye ujuzi maalum watakaochangia katika maendeleo ya kitaaluma, uzalishaji na utengenezaji wa ajira mpya.

Mheshimiwa Spika, tayari Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela ambayo ilianza mwaka 2012 imeanza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kutatua tatizo sugu la uhaba wa wataalam katika taasisi za elimu ya juu na za utafiti.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia yaani *COSTECH* imefikia makubaliano na kampuni ya kimataifa ya *FESTO* ili kuanzisha kituo cha mafunzo ya fani ya *mechatronics*, ambapo wanafunzi wa *DIT* na wafanyakazi wa viwandani wataweza kujifunza ujuzi mpya katika taaluma ya *mechatronics* kwa kutumia maabara.

Ujuzi huu mpya utasaidia kuwawezesha vifaa vyetu kubadilisha teknolojia za kizamani na kutumia teknolojia hii mpya inayotumia TEHAMA na kuleta maendeleo endelevu viwandani. Pia wanafunzi wa *DIT* watapata fursa ya kujifunza teknolojia hii ya kisasa ambayo itawasaidia kukabiliana na ushindani katika soko la ajira hapo watakapohitimu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iko katika mchakato wa kutafuta fedha zitakazowezesha kuboresha majengo ya kufundishia katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya ili dhana ya Chuo Kikuu hichi kupandishwa kuwa hadhi kutoka taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Mbeya na kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia iwe dhahiri. Katika ujenzi huo Chuo kinategemea kuzigeuza maabara zake ziwe kitovu cha uzalishaji bidhaa na kongano ambazo zitawasaidia wahitimu kuwa na uwezo wa kujiari na kutengeneza ajira kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, Uratibu na Maendeleo na Uendelezaji wa Sayansi Teknolojia na Ubunifu. Kwa kutambua kuwa Sayansi, teknolojia na ubunifu. Ni dhana mtambuka. Wizara kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia, imeendelea kuratibu kuendeleza utafiti na ubunifu utakaotekelezwa katika sekta mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Kuanzisha vipaumbele na kusimamia ugawaji wa fedha za utafiti kutoka Serikali kwenye maeneo mbalimbali ya kuendeleza utafiti na ukuaji wa sayansi na teknolojia kupitia mfuko wa Taifa wa uendelezaji wa Sayansi na teknolojia yaani TUSATE.

(ii) Kuendeleza rasilimali watu kupitia ufadhili wa wanafunzi wa shahada ya udhamili na udhanifu katika vyuo vikuu mbalimbali hapa nchini.

(iii) Kutafuta fedha uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia kutoka kwa wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kwa mfano mwaka 2013/2014 *COSTECH* wameratibu matumizi ya *EURO* milioni 1.8 sawa na shilingi bilioni 4.07 za mfuko wa pamoja kati ya Tanzania, Sweden na Uholanzi.

Vile vile *COSTECH* kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Uingereza, yaani *UK Department for International Development* wamezindua mfuko wa kuendeleza ubunifu, yaani *Human Development Innovation Fund* wenye thamani ya *Pound* za Kiingereza Milioni 30 sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 83.9 utakaosaidia kuchochea na kuendeleza ubunifu katika sekta za elimu, Afya na Maji.

Mheshimiwa Spika, kupitia Tamizi ya Dar es Salaam *Business TEKNOHAMA incubator* iliyopo pale *COSTECH* kampuni 52 zimefadhiliwa ambazo nyingi ziko katika hatua mbalimbali za kujiimarisha katika soko la ndani na nje ya nchi. Hadi mwezi Septemba, 2013 kampuni hizi zilikuwa zimetengeneza ajira 211 za moja kwa moja na ajira 7000 zisizokuwa ni za moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Tume ya nguvu za *Atomic Tanzania* kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi imeendelea kuratibu miradi miradi mbalimbali ya utafiti inayotumia teknolojia za *nuclea*r katika sekta ya kilimo, afya na mifugo.

Katika mwaka wa fedha 2013/2014 jumla ya miradi mitano yenye thamani ya *EURO 642,400* sawa na shilingi bilioni 1.45 ilifadhiliwa kupitia shirika la nguvu za *atomic* duniani. Pia miradi mingine yenye thamani ya shilingi milioni 40 inayofadhiliwa kupitia shirika la Kimataifa la kuzuia matumizi ya silaha za *nuclear* inatekeleza na *TAEC*.

Mheshimiwa Spika, Changamoto zilizopo katika sekta ya mawasiliano Sayansi na Tekonolojia, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu na malengo ya sekta ya mawasiliano Sayansi na Teknolojia ziko pia changamoto kadha ambazo zimechangia kutofikiwa kwa malengo ya sekta kama ifuatavyo:-

Mtiririko Mdogo wa Fedha Ndani za Maendeleo; mtiririko mdogo wa Fedha Miradi ya Maendeleo na upatikanaji wake kwa wakati umeleta changamoto katika kukamilika kwa baadhi ya shughuli zilizopangwa kwa mwaka fedha 2013/2014. Katika mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni 30,295,000,485/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Mei, 2014 Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 5,033,387,500/= sawa na asilimia 16.62 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, taasisi zinazoendesha *program* ya mafunzo katika ngazi ya *diploma* kutokuwa na stahili ya mkopo, Chuo kikuu cha Sayansi na Teknolojia ya Mbeya na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam zinaendesha *program* za mafunzo katika ngazi za Cheti na *Diploma* ambazo wanafunzi wake hawana stahili ya kupata mikopo kutoka Bodi ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na dhamira ya dhati ya Serikali ya kusomesha wataalam wengi wa kutosheleza mahitaji ya Taifa katika kada hii ya *diploma* kukosekana kwa fedha kutosha hususan za matumizi mengineyo, zinaziweka taasisi hizi katika hali ya wasiwasi, hususan kwenye huduma zinazogharamiwa na vyuo hivyo zikiwemo za chakula cha wanafunzi kutishiwa kusitishwa. Huduma hizo kuendelea kutolewa na vyuo kumepelekea vyuo kuwa malimbikizo ya madeni kwa watoa huduma za chakula na vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Aidha, kwa upande wa taaluma kutopatikana kwa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo kunasababisha wanafunzi kuchelewa kwenda kwenye mafunzo ya vitendo viwandani. Hali hii imekuwa ikichelewesha kufikia kwa azma ya Serikali ya kuandaa rasilimali watu ya kutosha katika sekta ya sayansi na teknolojia ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa wataalam katika Nyanja ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, sekta ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, inakabiliwa na uhaba wa wataalam kuwepo na hali hii kunakizana na utashi wa kuwa na jamii inayoongozwa na maarifa. Jitihada zinafanywa na taasisi za elimu kupanua udahili, ni moja kati ya mkakati wa kupunguza tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, shughuli za utafiti na maendeleo kutotengewa fedha za kutosha, upungufu wa fedha umeendelea kuathiri utekelezaji wa malengo na ufanisi wa shughuli za utafiti na maendeleo. Azma ya Serikali ni kuongeza tengo la fedha za utafiti na maeneleo katika Bajeti ya Serikali ya kufikia asilimia moja ya pato ghafi la Taifa.

Pamoja na azma hii kuwepo, kumekuwa na changamoto katika kufikia lengo hili ambapo fedha zinazotengwa pamoja na kuongezeka ikilinganishwa na miaka ya nyuma hazijaweza kufikia kiwango hiki. Wizara kupitia uboreshaji wa mfumo wa sayansi, tekonlojia na ubunifu umeandaa vivutio ili kuongeza mchango wa sekta binafsi na wadau wengine kuchangia utafiti, maendeleo ya sayansi na teknolojia na ubunifu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, maazimio na mwelekeo wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Malengo katika Mpango wa Kati na muda Mrefu. Sekta ya

Mawasiliano Sayansi na teknolojia inaazimia kutekeleza mpango wa muda wa kati na muda mrefu ambao umetilia mkazo maeneo yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, kwanza sekta ya mawasiliano, katika sekta ya TEHAMA, Wizara inaazimia kutekeleza yafuatayo.

Kwanza kuendelea na ujenzi na kuimarisha miundombinu ya TEHAMA nchini, ikiwa ni pamoja na ushiriki, utekelezaji na uendelezaji wa mradi wa ujenzi wa awamu ya tatu ya mkongo wa Taifa wa mawasiliano unaojumuisha uunganisha wa Ugunja na Pemba katika mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upanuzi wa mkongo wa baadhi ya maeneo ambayo hayakufikiwa na awamu ya kwanza na ya pili, ujenzi wa mtandao wa *internet* wa kasi na vituo mahiri vya kutunza kumbukumbu yaani *data center* katika miji ya Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar.

Pili, kuendelea kueneza mkongo wa Taifa wa mawasiliano na kupanua matumizi yake katika maeneo mbalimbali hapa nchini na katika nchi jirani.

Tatu, kuendelea kuratibu utekelezaji wa mradi wa kuunganisha katika mkongo wa Taifa wa mawasiliano vituo 200 vikiwemo shule za msingi, shule za sekondari, vyuo vya afya, vituo vya posta pamoja na taasisi zilizoainishwa kwenye mradi wa *ESCOL* ujulikanao kama *Tanzania Beyond Tomorrow.*

Nne, kuratibu zoezi la uwekaji na matumizi ya mfumo wa anwani za makazi na simbo ya posta katika maeneo mbalimbali nchini.

Tano, kuendelea kupanua mtandao na kuboresha huduma za mawasiliano ya simu na *internet* nchini kuratibu utekelezaji wa sera ya Taifa ya TEHAMA na kuimarisha ujenzi wa vituo vya jamii vya mawasiliano nchini.

Sita, kutunga sera ya Taifa ya menejimenti ya masafa na kuandaa mfumo wa kukuza utoaji wa huduma mbalimbali kupitia makampuni mengine ya TEHAMA yaani *ICT Business process outsourcing.*

Saba, kutunga sheria ya tume ya TEHAMA.

Nane, kuendelea mkakati wa kuweka mtandao wenye kasi na uwezo mkubwa yaani *broad band* nchini.

Tisa, kuanza uhuishaji wa Sera ya Taifa ya posta.

Kumi, kukamilisha uanzishwaji wa Tume ya TEHAMA na kufuatilia utendaji wa Taasisi mbalimbali za sekta ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Sayansi Teknoloja na Ubunifu, kwa upande wa sekta ya sayansi, teknolojia na ubunifu, Wizara imeazimia kutekeleza yafuatayo:-

Kwanza, kuendelea na utekelezaji wa *program* ya mageuzi ya mfumo wa ubunifu nchini yaani *National Innovation system reform.*

Pili, kuimarisha na kuboresha Taasisi za Utafiti Sayansi na Teknolojia.

Tatu, kuendelea kuimarisha miundombinu, mifumo, Taasisi na rasilimali katika Nyanja za Utafiti, Sayansi na Teknolojia nchini.

Nne, kubuni kuandaa na kusimamia Sera, Mipango ya Utekelezaji Miongozi, mikataba itifaki, sheria na Kanuni zinazolenga kuendeleza Sayansi na Ubunifu nchini. *(Makofi)*

Tano, kuimarisha uhusiano wenye tija na wadau mbalimbali katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ndani ya nchi kikanda na kimataifa.

Mwisho, kuhamasisha jamii kuhusu Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa ujumla kwa Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii.

Mheshimiwa Spika, shukrani, napenda sasa nitumie fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia na kuwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Ni ukweli usiopingika kwamba mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2013/2014 yametokana na jitihada za pamoja kwa kushirikiana na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa mashirika ya maendeleo ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa makampuni ya simu za mkononi kwa utayari wao katika kushughulikia changamoto za mawasiliano katika maeneo yasiyo na mawasiliano hapa nchini. Pia ninazishukuru kwa jinsi zinavyoshiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilinufaika na itaendelea kupokea misaada mikopo na ushirikiano kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo kwa kipindi cha fedha cha mwaka 2014/2015 kwa niaba ya Serikali ninapenda kutoa shukrani zangu kwa Serikali za Marekani, *Sweden, Norway, Finland, Uholanzi, Japan, Italy,* Afrika ya Kusini, Jamhuri ya Korea Kusini, Jamhuri ya Watu wa China na India. *(Makofi)*

Vilevile natoa shukrani zangu kwa benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya *Exim* ya Jamhuri ya Watu wa China, pamoja na taasisi na Mashirika wahisani ya Umoja wa Mataifa, Jumuiya ya Madola, Shirika la Kimataifa la Nguvu za *Atomic, KOICA, UNESCO, UNCTAD, UPU* na *ITU.*

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2014/2015, Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia, katika mwaka wa fedha 2014/2015 yamekadiriwa kuwa shilingi bilioni 67,221,001,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Katika ya fedha hizo, shilingi bilioni 37,844,668,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yaani Mishahara na Matumizi Mengineyo. Ambapo shilingi bilioni 26,838,491,000 ni kwa ajili ya Mishahara na shilingi bilioni 11,600,177,000/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni 29,376,333,000/= ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo za Maendeleo shilingi bilioni 26,000,000,000/= ni Fedha za Ndani na shilingi bilioni 3,376,333,000/= ni Fedha za Nje.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kutekeleza mipango yake iliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2014/2015 sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuidhinisha Matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 67,221,001,000/= kwa mchanganuo ulioelezwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inavyo viambatanisho kuanzia namba moja hadi namba kumi na sita vinavyotoa takwimu vielelezo na taarifa mbalimbali zinazohusu sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za Bunge, pamoja na Bunge lako Tukufu kwa kunisikiliza wakati nikiwakilisha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Hotuba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia Kama Ilivyowasilishwa Mezani**

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA MHESHIMIWA PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA (MB), WAKATI WA KUWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA**

**FEDHA KWA MWAKA 2014/2015**
**Mei, 2014**

## A. UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba (Mb) kuhusu Wizara yangu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2013/2014 na malengo ya Wizara katika bajeti ya mwaka 2014/2015.

Aidha, naliomba Bunge lako tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana tena kushiriki katika mkutano huu wa bunge unaojadili bajeti ya Serikali.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** niruhusu sasa niungane na Waheshimiwa Wabunge, ndugu na marafiki katika kuwafariji na kuwapa pole familia, ndugu, na wapiga kura wa Marehemu Mheshimiwa William Augustao Mgimwa aliyekuwa Mbunge wa Kalenga (CCM) na Mheshimiwa Saidi Ramadhani Bwanamdogo, aliyekuwa Mbunge wa Chalinze (CCM). Napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia, wewe Mhe. Spika, Bunge lako Tukufu, ndugu na marafiki wa marehemu. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema peponi, Amina.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** nachukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Godfrey Mgimwa (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Kalenga (CCM) na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Chalinze (CCM). Ushindi wao ni kielelezo tosha kuwa wananchi wana imani kubwa na CCM katika kuwaletea maendeleo.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima na taadhima nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu vyema na kwa utekelezaji mahiri wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 pamoja na mipango na programu mbalimbali za kuiletea nchi yetu maendeleo. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Mohamed Ghalib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter

Pinda, Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo wamemsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia na kuongoza shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, nawapongeza Mawaziri wenzangu walionitangulia kuwasilisha hotuba za bajeti kwa mwaka 2014/15. Hotuba hizo zimeelezea mafanikio, changamoto, matukio mbalimbali na hali ya uchumi wa taifa letu kwa mwaka 2013/14 na mipango kwa mwaka 2014/15. Aidha, nawashukuru Mawaziri wote walionitangulia kwa kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ambazo zinahusu Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Vilevile, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu makini mliyoitoa kwa nia ya kuboresha mikakati ya utekelezaji wa mipango iliyowasilishwa na Serikali kwa maendeleo ya wananchi wa Tanzania.

**6. *Mheshimiwa Spika,*** napenda sasa kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za pekee kwa wale wote walioniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa kipindi kilichopita, na ambao wameniwezesha kuandaa mpango wa mwaka wa fedha 2014/2015 na kuboresha hoja hii ambayo ninaiwasilisha katika Bunge lako tukufu. Aidha, nawashukuru Mheshimiwa January Yusuph Makamba (Mb), Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na Mbunge wa Jimbo la Bumbuli; Prof. Patrick James Makungu, Katibu Mkuu; Ndugu John Mngodo, Naibu Katibu Mkuu; watendaji wote katika Wizara, Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara kwa ushirikiano wao katika kufanikisha uwasilishaji wa hotuba hii.

**7. *Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini (CCM), kwa ushauri wao unaotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa tija na ufanisi zaidi. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mhe. Eng. Habib Juma Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni (CUF) ambaye ni Waziri Kivuli wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa ushirikiano wake na mchango wake katika kuiboresha hoja hii ninayoiwasilisha katika Bunge lako tukufu.

**8. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inayo dhamana ya kusimamia, kuimarisha na kuendeleza Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili viweze kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya nchi. Vilevile, Wizara inayo dhamana ya kusimamia na kutoa miongozo ya kiutendaji kwa taasisi, mashirika, tume na kampuni ambazo zinafanya kazi chini yake. Taasisi hizo ni: (i) Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam;

(ii) Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha;

iii) Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya;

iv) Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania;

(v) Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia;

vi) Shirika la Posta Tanzania;(vii) Kampuni ya Simu Tanzania;

(viii) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; na (ix) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote.

**9. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 imetekeleza majukumu na mipango yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2013/2014, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2010–2015.

Aidha, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imezingatia Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Nyuklia ya mwaka 2013, Sera ya Taifa ya Bayoteknolojia ya mwaka 2010, Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo ya mwaka 2010, Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996, Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya mwaka 2003, Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu ya mwaka 1997 na Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2013/2014

**10. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ilitengewa jumla ya Sh. 63,147,599,460. Kati ya fedha hizo, Sh. 27,218,364,000 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo za Matumizi ya Kawaida Sh. 20,212,187,000 zilikuwa ni kwa ajili ya Mishahara na Sh. 7,006,177,000 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Fedha za Maendeleo zilizoidhinishwa zilikuwa Sh. 35,929,235,460 ambapo fedha za ndani zilikuwa Sh. 30,295,482,000 na fedha za nje zilikuwa Sh. 5,633,753,460.

**11. *Mheshimiwa Spika,*** majukumu yaliyotekelezwa na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na taasisi zake katika kipindi cha mwaka 2013/14 ni haya yafuatayo:

### B.1 UTEKELEZAJI KATIKA SEKTA YA MAWASILIANO

### B.1.1 Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

**12. *Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unatekelezwa kwa awamu tano (5) ambapo awamu ya I na II zimekamilika na zinatumika tangu mwaka 2012 zikiwa na jumla ya kilomita 7,560. Kwa sasa Wizara ipo katika utekelezaji wa awamu ya III inayohusisha ujenzi wa vituo vitatu (3) mahiri vya kutunza kumbukumbu (internet data centres) vitakavyojegwa Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar.

Pia, katika awamu hii utajengwa mtandao wa intaneti wa kasi (*Internet Protocol/Multiprotocol Label Switching Network – IP/MPLS) pamoja na* kuunganisha Unguja na Pemba katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Utekelezaji wa sehemu ya kwanza (I) ya awamu ya tatu (III) umeanza rasmi Desemba, 2013 ambapo hatua za ujenzi wa kituo mahiri cha kutunza kumbukumbu katika eneo la Kijitonyama, Dar es Salaam zimeanza.

**13. *Mheshimiwa Spika,*** awamu ya tatu (III) itakapokamilika italeta manufaa makubwa kwa Taifa kwa kurahisisha upatikanaji wa huduma za kielektroniki kama vile shule mtandao, biashara mtandao, serikali mtandao. Vilevile, itaongeza na kukuza matumizi ya mtandao, kuwezesha utunzaji wa taarifa ndani ya nchi na kuimarisha matumizi salama ya mtandao.

**B.1.2 Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi Katika Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

**Ujenzi wa Mikongo ya Mijini (Metro Networks**

**14. *Mheshimiwa Spika,*** wizara kwa kutambua umuhimu wa kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma za mawasiliano inatekeleza Awamu ya IV ya Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa kushirikiana na makampuni ya simu za kiganjani ya Airtel, Tigo na Zantel. Awamu hii itagharimu jumla ya Dola za Kimarekani milioni 80 ambazo zitagharamiwa na watoa huduma ambapo serikali itatoa ruhusa ya kutumia hifadhi ya njia (**Right of Way**).

Umiliki wa mikongo ya mijini inayojengwa kwa utaratibu huu utakuwa ni wa serikali wakati watoa huduma watapewa sehemu ya mikongo hiyo kwa ajili ya matumizi yao binafsi. Aidha, utekelezaji katika jiji la Dar es Salaam umekamilika ukiwa na jumla ya kilomita 91 zilizogharimu Dola za Kimarekani milioni sita (6). Hatua inayofuata ni utekelezaji katika miji ya Morogoro, Arusha, Mwanza na Mbeya.

**Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika Njia ya Reli**

**15. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa Mkongo unafika katika maeneo mengi zaidi, serikali kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano

(Tigo, Airtel na Zantel) wamekamilisha taratibu za kuanza ujenzi wa mkongo katika njia ya reli kuanzia Dar es Salaam hadi Mwanza, Tabora hadi Kigoma na Dar es Salaam hadi Arusha.

**B.1.4 Juhudi za Serikali katika Kupeleka huduma za TEHAMA kwa Watumiaji wa Mwisho**

**16. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika kuhakikisha kuwa inakuza matumizi ya TEHAMA nchini hususan katika kutumia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, inatekeleza yafuatayo:

**B.1.4 Uunganishwaji wa Vyuo vya Elimu ya Juu na Taasisi za Utafiti katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

**17. *Mheshimiwa Spika,*** wizara inaratibu utekelezaji wa mradi wa kuunganisha Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Madhumuni ya mradi huu ni kuimarisha mfumo wa utoaji wa huduma katika taasisi za elimu ya juu na utafiti kwa kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwa njia ya kuwekeza katika miundombinu ya TEHAMA inayoziunganisha Taasisi hizi.(**Kiambatanisho Na. 16**)

**18. *Mheshimiwa Spika,*** awamu ya kwanza ya mradi huu ilikusudia kuunganisha taasisi 28. Hadi kufikia mwezi Mei, 2014 tayari taasisi 18 zilikuwa zimeunganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

**B.1.5 Uwezeshaji wa Matumizi ya TEHAMA kwa Gharama Nafuu**

**19. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa matumizi ya TEHAMA yanaongezeka hasa katika taasisi za serikali, shule, hospitali na vyuo vya elimu, Wizara inatekeleza mradi wa *Regional Communication Infrastructure Program* (RCIP) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ukiwa na lengo la kuwezesha taasisi hizi kutumia intaneti kwa bei nafuu na kuongeza upatikanaji wa huduma za *broadband* na kuongeza ufanisi na uwazi wa Serikali kupitia matumizi ya serikali mtandao. Wizara imekamilisha ujenzi wa mtambo wa *Internet Bandwidth* na ununuzi wa *Internet Bandwidth* yenye ukubwa wa 1.55Gbps ambayo tayari imeanza kutumika. Hadi kufika mwezi Mei, 2014 jumla ya taasisi 42 zimeunganishwa na zingine 25 zipo kwenye utaratibu wa kuunganishwa.**(Kiambatanisho Na. 6)**

**B.1.6 Uwezeshaji wa Serikali Kufanya Mikutano kwa Kutumia TEHAMA**

**20. *Mheshimiwa Spika,*** wizara inaendelea na juhudi za kuhakikisha kuwa matumizi ya TEHAMA katika ofisi za Serikali yanaongezeka. Wizara imefunga mitambo ya *Video Conferencing* 26 kwa ajili ya kuendeshea vikao kwa njia ya mtandao. Hadi kufikia mwezi Novemba, 2013 mitambo 25 ilikuwa imefungwa katika Makao Makuu ya Mikoa 21, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na TAMISEMI. Aidha, taratibu za kufunga mitambo ya aina hiyo katika makao makuu ya mikoa mitano (5) ya Zanzibar pamoja na Ofisi ya Rais wa Zanzibar zimekamilika na inatarajiwa kufungwa mwishoni mwa mwezi Juni, 2014.

### B.1.7 Kukuza Matumizi ya TEHAMA kwenye Shule za Msingi na Sekondari

**21. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa matumizi ya TEHAMA katika shule yanaongezeka kwa kasi na kuweka mazingira ya kutumia elimu mtandao, Wizara inatekeleza mradi wa majaribio wa shule mtandao (*E-schools*) ukiwa ni sehemu ya juhudi za Serikali katika kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kuunganisha Shule. Mpaka sasa vituo 49 zikiwemo shule 43, vituo vya posta vitatu (3) na vyuo vya afya vitatu (3) vimepelekewa na kufungiwa vifaa vya TEHAMA pamoja na kufanyiwa mafunzo ya matumizi bora ya vifaa hivyo. Aidha, taratibu za kumpata mzabuni kwa ajili ya shule nyingine 80 zipo katika hatua za mwisho.

### B.1.8 Usalama Katika Matumizi ya TEHAMA

**22. *Mheshimiwa Spika,*** kukua kwa kasi kwa matumizi ya TEHAMA kumeleta mafanikio mengi katika nyanja mbalimbali za maisha ya kila siku, kama vile, mabadiliko katika huduma za mawasiliano, huduma za kibenki na mitandao ya kijamii. Sambamba na hilo mafanikio hayo yameleta changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na uhalifu katika mtandao (*Cyber Crimes*). Katika kulitambua hili, Wizara imekamilisha rasimu ya miswada mitatu ya Sheria za Usalama wa Mtandao (*Cyber Security Laws*). Sheria ya Kulinda Taarifa Binafsi (*Personal Data Protection*), Sheria ya Miamala ya Ki- Elektroniki (*Electronic Transaction*) na Sheria ya Kudhibiti Uhalifu wa Mtandao na Kompyuta (*Computer and Cyber Crime*). Rasimu hizi zimewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili ziweze kuandaliwa kwa mujibu wa taratibu za uandishi wa sheria.

**23. *Mheshimiwa Spika,*** mbali na uandaaji wa sheria hizi, Wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inasimamia uwekaji wa mfumo madhubuti wa kitaifa wa kupambana na uhalifu katika mitandao ya mawasiliano ya kompyuta. Ndani ya mfumo huu ambao utekelezaji wake ulianza rasmi mwezi Septemba 2012 kimeanzishwa Kikosi Maalum cha Ulinzi wa

Kielektroniki (*Computer Emergency Response Team*) kinachohusika na uhakiki wa usalama katika matumizi ya TEHAMA hapa nchini. Kikosi hiki kina wataalam wenye ujuzi wa hali ya juu kuhusu usalama wa mitandao ya mawasiliano na kimekwisha anza kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta.

### B.1.9 Kufikisha Huduma za Mawasiliano Vijijini

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** wizara imeendelea kushawishi sekta binafsi kufikisha mawasiliano kwenye maeneo yasiyo na mvuto kibiashara. Kupitia juhudi hizi kampuni za simu zimeridhia kwa hiari kupeleka mawasiliano kwenye jumla ya Kata 163 kwa awamu ya kwanza "A" na awamu ya kwanza "B". Katika awamu ya kwanza "A", kampuni za simu zitapeleka mawasiliano kwenye Kata 44 kwa gharama zao na Kata 33 kwa ruzuku ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kupitia mkopo wa Benki ya Dunia. Vilevile, kampuni za simu zimeshiriki kwenye zabuni ya awamu ya kwanza "B" ambapo jumla ya kata 86 zimepata wazabuni kwa ruzuku ya UCSAF. Ushiriki wa kampuni za simu kwenye zabuni za UCSAF umeongezeka kwa asilimia 213 kutoka kata 52 mwaka 2012/13 hadi kufikia kata 163 mwaka 2013/2014.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** wizara kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imefanya tathmini na kubaini kuwa jumla ya kata 1365 zina tatizo la mawasiliano ambapo jumla ya Shilingi bilioni 328 zinahitajika ili kuweza kulipatia ufumbuzi tatizo hili. Kwa takwimu hizi, ni dhahiri kuwa hitaji la mawasiliano bado ni kubwa ikilinganishwa na kasi tunayokwenda nayo kwa kutegemea fedha za mkopo wa Benki ya Dunia na makusanyo kupitia UCSAF. Katika kukabiliana na changamoto hii inayokwamisha kufikiwa kwa malengo ya kufikisha mawasiliano vijijini ifikapo 2015, Serikali inaangalia vyanzo vingine vya fedha ndani na nje ya nchi, ikiwa ni pamoja na kuwasilisha andiko la mradi kwa lengo la kuomba fedha za mkopo nafuu kutoka nchi wahisani ili kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo haya ambayo mahali pengine ni madogo au wakazi wake ni wachache mno kiasi cha kutowavutia kibiashara watoa huduma za simu.

### B.1.10 Ukuaji na Mchango wa Sekta ya Mawasiliano

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** mazingira mazuri yaliyowekwa na Serikali kwenye Sekta ya Mawasiliano yameonesha matokeo makubwa. Idadi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano nchini imeendelea kuongezeka kutoka laini za simu za kiganjani milioni 2.96 mwaka 2005 hadi kufikia milioni 27.45 mwezi Desemba 2013. Watumiaji wa mfumo wa intaneti nao wameongezeka kutoka milioni 3.56 mwaka 2008 hadi kufikia milioni 9.3 mwezi Desemba 2013. Pia, kuna ongezeko kubwa la huduma kupitia mawasiliano ya simu za kiganjani. Huduma hizo ni pamoja na miamala ya kifedha ambayo ina watumiaji wapatao 12,330,962 na

ununuzi wa huduma na bidhaa kwa kutumia miamala ya kibenki. Hivi sasa, wananchi wanaweza kufanya malipo ya huduma mbalimbali wanazozitumia kupitia simu za kiganjani ambapo katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Aprili, 2014 jumla ya miamala 972,641,605 yenye thamani inayofikia shilingi Trilioni 28.3 imefanyika. Maendeleo haya yamesaidia kuokoa muda na kupunguza msongamano sehemu za kulipia na kupata huduma hizo **(Kiambatanisho Na.11)**.

**B.1.11 Utekelezaji Mpana wa Mpango wa Kubadilisha Teknolojia ya Utangazaji Kutoka Analojia Kwenda Dijitali**

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu zoezi la kubadilisha teknolojia ya utangazaji kutoka mfumo wa analojia kwenda dijitali. Mambo yaliyofanyika ni pamoja na tathmini ya utekelezaji wa awamu ya kwanza katika maeneo ya Dar es Salaam, Mbeya, Tanga, Mwanza, Arusha, Dodoma na Moshi ili kubaini mafanikio na changamoto. Matokeo ya tathmini yanaonyesha kuwa zoezi la uhamaji katika awamu hiyo lilifanikiwa kwa asilimia 89. Mafanikio hayo yaliwezeshwa na uelewa wa kutosha kupitia elimu kwa umma iliyotolewa katika maeneo husika, kuwepo kwa ving'amuzi vya kutosha katika maeneo ya uzimaji na gharama ya ving'amuzi wakati wa uzimaji kuwa chini ikilinganishwa na hapo awali.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya tathmini, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaendelea na utekelezaji mpana katika maeneo yaliyosalia ili kukamilisha zoezi hili ndani ya muda tuliojiwekea. Hadi hivi sasa zoezi la uzimaji wa mitambo ya analojia kwa awamu ya pili, lililoanza tarehe 31 Machi 2014, limekwishafanyika katika miji ya Tabora, Singida, Musoma na Bukoba wakati uzinduzi wa mitambo ya dijitali unaendelea katika mji wa Kahama. Aidha, taratibu za uzimaji katika miji ya Kigoma, Iringa, Songea, Morogoro, Sumbawanga, Lindi na Mtwara zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Septemba, 2014.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mpango huu umetekelezwa kwa mafanikio makubwa na hivi sasa wananchi katika miji yenye mtangazo ya dijitali wanaweza kupata *chaneli* nyingi za televisheni ikilinganishwa na hapo awali na hivyo kuwa na wigo mpana wa kupata habari. Utekelezaji huu umeifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza katika Afrika kutekeleza makubaliano ya nchi wanachama wa umoja wa kimataifa wa mawasiliano ya elektroniki (*International Telecommunications Union- ITU*) ya kuzima mitambo ya analojia ifikapo tarehe 17 Juni, 2015.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio haya yanaifanya Tanzania kuwa mfano wa kuigwa na mataifa mengine ambapo nchi za Uganda, Kenya, Zambia,

Lesotho na Malawi zimekuja kupata uzoefu. Aidha, Afrika ya Kusini hivi sasa inajiandaa kuwaita wataalam wetu kwenda kutoa uzoefu nchini humo. Vilevile, mwezi Februari, 2014 Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa nchi wanachama wa taasisi ya mawasiliano ya nchi za Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Telecommunications Organization- CTO*) kuhusu mabadiliko ya teknolojia ya utangazaji kwa lengo la nchi hizo kupata uzoefu wa Tanzania.

**31. *Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kulishukuru Bunge lako tukufu, wadau wa sekta na wananchi kwa ujumla kwa ushirikiano katika utekelezaji wa zoezi hili muhimu. Aidha, nirudie tena kutoa wito kwamba, zoezi hili ni muhimu na lina lengo la kuifanya nchi yetu iendane na mabadiliko yanayotokea duniani ambayo hayakwepeki. Wadau wote watoe ushirikiano kwa vyombo vinavyohusika.

**B.1.12 Kuimarisha Mfumo wa Udhibiti Katika Sekta ya Mawasiliano**

**32. *Mheshimiwa Spika,*** wizara yangu imeendelea na mpango wa kuboresha mazingira ya udhibiti kwa kuanzisha mfumo wa kuhakiki na kusimamia huduma za mawasiliano nchini (*Telecommunication Traffic Monitoring System- TTMS*) kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Katika kufanikisha azma hii, wizara imetengeneza kanuni mpya zinazosimamia mawasiliano kupitia mitandao ya simu (*EPOCA (TTMS) Regulation 2013*). Mtambo huu wa TTMS ulipatikana kwa kushirikiana na sekta binafsi kwa utaratibu wa *Build Operate and Transfer (BOT)* ulianza kufanya kazi mwezi Oktoba 2013. Kwa mujibu wa kanuni za TTMS, kampuni za nje ya nchi zinatakiwa kulipa senti ishirini na tano (25) za kimarekani kwa kila dakika moja ya mazungumzo ya simu zinazoingia nchini. Kanuni ya TTMS imeweka mgawanyo wa mapato hayo ya senti ishirini na tano (25) ambapo Serikali kupitia Hazina inapata senti saba (7), watoa huduma wanapata senti kumi na tatu (13) na senti tano (5) ni kwa ajili ya uendeshaji wa mitambo ikiwa ni pamoja na kumlipa mwekezaji wa mtambo huu.

**33. *Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Januari 2014 mfumo huu umeweza kuiingizia Serikali jumla ya **Shilingi Bilioni 6.8.** Kwa hivi sasa mtambo unaratibu dakika za maongezi kwa simu za kimataifa na kufuatilia udanganyifu (*fraud*) kwa simu zinazoingia nchini ambapo mpaka sasa udanganyifu umepungua kutoka asilimia 60 kabla ya mtambo kufungwa hadi chini ya asilimia 2 hivi sasa. Wahusika wa udanganyifu wamefikishwa mahakamani na kesi zinaendelea. Kazi nyingine zinazokamilishwa ni kuuwezesha mfumo huu kuratibu dakika za maongezi kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine (*interconnection*) pamoja na kufuatilia miamala (*transactions*) inayopita kwenye mitandao ya simu.

**B.1.13 Matibabu Mtandao (*Telemedicine*)**

**34. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) inaendelea na utekelezaji wa mradi wa Matibabu Mtandao (*Telemedicine*) unaounganisha DIT, hospitali za Muhimbili, Amana, Temeke, Mwananyamala, Tumbi, Bagamoyo na Hospitali ya Rufaa ya Mbeya kwa kushirikiana na Wizara za Afya na Ustawi wa Jamii na wadau wengine wa maendeleo. Usimikaji wa mitambo na vifaa na mafunzo kwa madaktari wanaohusika na mradi huu vimekamilika. Majaribio ya Mradi yanaendelea yakihusisha madaktari wa hospitali zilizotajwa.

**B.1.15 Utekelezaji Mpana na Kuweka Miongozo ya Mpango wa Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta**

**35. *Mheshimiwa Spika,*** baada ya kukamilika kwa utekelezaji kwa hatua ya majaribio ya Mpango wa Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta katika miji ya Arusha na Dodoma, wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kushirikiana na wadau wengine imeanza utekelezaji mpana wa mpango huu (*roll out*) kwa kuanzia mkoa wa Dar es Salaam ambao umeanza mwezi Desemba 2013.

**36. *Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuwashukuru wadau wote wanaohusika na mpango huu hususan uongozi wa mkoa wa Dar es Salaam na Manispaa zote tatu za mkoa huu kwa ushirikiano mkubwa waliouonyesha katika utekelezaji wa mpango huu. Kimsingi, Halmashauri zimeshiriki kikamilifu katika kubainisha majina ya mitaa, kukusanya taarifa za wakazi na kuweka vibao vya namba na majina ya mitaa katika kata kumi (10) zilizochaguliwa kuanza utekelezaji – kata tano (5) Ilala, mbili (2) Temeke na tatu (3) Kinondoni. Lengo ni kukamilisha utekelezaji wa mpango huu katika kata zote za Dar es Salaam ifikapo Desemba mwaka huu. Sambamba na zoezi hili, Wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imeziwekea wizara zote na baadhi ya taasisi Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta ambazo tayari zimeanza kutumika.

**37. *Mheshimiwa Spika,*** kupitia uzoefu uliopatikana katika Mkoa wa Dar es Salaam, wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inakamilisha uandaaji wa mwongozo unaoweka mfumo bora wa kitaasisi wa kutekeleza mpango huu katika maeneo mengine nchini. Aidha, rasimu ya mpango wa utekelezaji katika maeneo mengine ya nchi umeandaliwa.

**B.1.16 Kuendelea Kuweka Mifumo ya Kisera na Kuimarisha Uratibu wa Sekta ya Mawasiliano**

**38. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuweka mazingira mazuri ya kukuza sekta ya mawasiliano na kuimarisha uratibu, Wizara imekamilisha uandaaji wa rasimu ya sera mpaya iliyohuishwa na rasimu ya mkakati wa Utekelezaji wa sera hiyo ambapo kwa pamoja vipo katika hatua ya uwasilishwaji kuridhiwa.

**39. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mfumo wa uratibu wa kisekta, wizara imeendelea kukamilisha taratibu za kuanzisha Tume ya TEHAMA. Uchambuzi wa majukumu ya Tume na mlinganisho baina yake na Taasisi nyingine umefanyika kwa umakini. Aidha, rasimu ya Tamko la Rais la kuanzisha Tume hiyo limekwisha pitia hatua mbalimbali za ukamilishwaji. Tume inatarajiwa kuwa imeanza kazi mwezi Septemba mwaka huu.

### B.1.17 Ujenzi wa Jamii Habari

**40. *Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa kuwa na uchumi uliojengeka kwenye misingi ya maarifa (*knowledge economy*) katika kufanikisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi, wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Finland imeendelea kutekeleza mpango wa kujenga jamii habari (*information society and ICT development program*). Mpango huu unahusisha utekelezaji wa programu ya kuimarisha uwezo wa Wizara katika kusimamia sekta ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia na programu ya kukuza ubunifu nchini kupitia TEHAMA. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14 programu kupitia wataalam wa Taasisi ya Menejimenti ya Mashariki na Kusini mwa Afrika (*Eastern and Southern Africa Management Institute – ESAMI*) imefanya tathmini ya kubaini mahitaji ya kuimarisha uwezo wa wizara (*institutional situation analysis*) ikiwa ni pamoja na mpango kazi wa utekelezaji wa mapendekezo hayo.

**41. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza ubunifu nchini mradi umeendelea kusaidia juhudi za kukuza ujasiriamali kwa kuwezesha kituo cha ubunifu (*Innovation Space*) kinachoitwa "Buni" kilichoko COSTECH ambapo takribani wajasiriamali 300 hushiriki katika makongamano mbalimbali kwa wiki. Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Aprili 2014 jumla ya makongamano arobaini na tano (45) yamefanyika katika kituo cha Buni. Aidha mpango huu umeendelea kusaidia uendelezaji wa vituo saba (7) vya utatuzi wa changamoto za kijamii (*living labs*) vilivyopo Kigamboni, Iringa, Mwanza, Sengerema Mbeya, Arusha na Zanzibar. Vilevile, mradi huu umeratibu jumla ya ziara nne (4) za kubadilishana uzoefu baina ya wataalam wa Tanzania na Finland zimefanyika ambapo wataalam na viongozi toka Tanzania walitembelea taasisi wenza nchini Finland na wataalam na wafanya biashara toka Finland walitemebelea Tanzania. Idara na Taasisi zilizohusika na mpango huu za elimu ya juu ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST), Taasis ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT) na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na wasimamizi wa vituo vya

*living labs*. Kupitia mpango huu, hivi sasa Chuo cha Kikuu cha Dar es Salaam na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela vimeanza ushirikiano na vyuo vyilivyoko nchini Finland.

## B.2 UTEKELEZAJI KATIKA ENEO LA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU

### B.2.1 Maboresho katika Mfumo wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini (*National Innovation System Reform Programme*)

**42. *Mheshimiwa Spika,*** maendeleo ya uchumi na jamii yanaenda sambamba na ongezeko la matumizi mapana na yanayotegemeana ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika sekta mbali mbali nchini. Pamoja na ukweli huu, katika nchi yetu sayansi, teknolojia na ubunifu havijachangia ipasavyo katika maendelo hayo kutokana na jinsi mfumo wa ubunifu nchini (*National Innovation System-NIS)* ulivyokaa. Kimfumo, sayansi, teknolojia na ubunifu ni dhana mtambuka na manufaa yake makubwa yanapatikana pale ambapo wadau wote nchini wanatumia maarifa, udadisi (utafiti) na ubunifu kwa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

**43. *Mheshimiwa Spika,*** hali ilivyo sasa, ubunifu na utafiti umeachwa kuwa ni jukumu la taasisi chache hususan, vyuo vikuu na taasisi za utafiti, ambazo hazizungumzi baina yao na watumiaji wa matokeo ya utafiti huo, jambo ambalo limedumaza mchango wa sayansi, teknolojia na ubunifu katika maendeleo ya jamii na uchumi. Ili kukabiliana na hali hiyo na kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani, Wizara kupitia programu ya mageuzi ya Sayansi na Teknolojia (*National Innovation System Reform Programme)* imekamilisha uundwaji wa mfumo mahsusi wa Sayansi, Teknolojia na ubunifu nchini.

Chini ya mfumo huu, mabadiliko makubwa ya kiutendaji yatafanyika ikiwemo mapendekezo ya mifumo mipya ya kitaasisi na maamuzi ya kuundwa kwa sheria mpya ya sayansi, teknolojia na ubunifu itakayoweka mazingira mazuri ya namna ya kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu nchini. Kuwepo kwa mambo haya kwa pamoja ndani ya mfumo huu kutavutia wadau mbalimbali kuchangia maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu tofauti na ilivyo sasa. Kuwepo kwa mfumo kutawezesha pia kujengeka ndani ya taifa letu utamaduni wa ubunifu, udadisi na utafiti kuwa sehemu ya maisha ya kila siku ya jamii na kuondoa mipaka ya kisekta na kitaaluma iliyopo hivi sasa na inayodumaza ubunifu.

**44. Mheshimiwa Spika**, wizara yangu imeanza kutekeleza baadhi ya mambo yaliyopendekezwa kwenye mfumo huu. Baadhi ya mambo hayo ni kupitia Sheria Na. 7 ya mwaka 1986 iliyounda Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia kwa kuandaa rasimu ya sheria ya sayansi, teknolojia na ubunifu na kupitia Sheria Na. 7 ya mwaka 2003 iliyounda Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania. Aidha, utekelezaji mpana wa mfumo huu utahusisha sekta zote na jamii yote ya Kitanzania na utachangia kwa kiasi kikubwa kufikiwa kwa malengo yaliyo kwenye Dira ya Taifa ya mwaka 2025 inayolenga kujengwa kwa jamii yenye maarifa (*knowledge society*).

**B.2.2 Kuzipa Taasisi za Sayansi na Teknolojia Zilizo Chini ya Wizara Mwelekeo Mpya wa Kitaaluma**

**45. *Mheshimiwa Spika,*** kama sehemu ya kwanza ya maboresho ya mfumo wa ubunifu nchini, Taasisi zilizo chini ya Wizara zimeendelea kujielekeza katika kuanzisha na kuweka mifumo mipya ya kitaaluma utakaoziwezesha kujenga wataalam wenye ubunifu na ambao sio tu watategemea kuajiriwa, bali watakuwa na uwezo wa kuzalisha ajira mpya wenyewe.

**46. *Mheshimiwa Spika,*** kuanzishwa kwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha kulifanywa kwa mtazamo huu wa kutengeneza wataalam wenye ujuzi maalum watakaochangia katika maendeleo ya kitaaluma, uzalishaji na utengenezaji wa ajira mpya.

**47. *Mheshimiwa Spika,*** tayari Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela ambayo ilianza mwaka 2012 imeanza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kutatua tatizo sugu la uhaba wa wataalum katika taasisi za elimu ya juu na utafiti. Vile vile, matokeo ya tafiti zilizofanywa na wahitimu wa taasisi hii kwa mwaka 2012/13 zimewawezesha kuwepo kwa machapisho ya kitaaluma 70. Mambo haya ni muhimu katika kuinua hali na mizania ya taifa letu katika sayansi na teknolojia miongoni mwa nchi za Afrika na ulimwenguni.

**48. *Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT) kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imefikia makubaliano na kampuni ya kimataifa ya FESTO ili kuanzisha kituo cha mafunzo ya fani ya *mechatronics*, ambapo wanafunzi wa DIT na wafanyakazi wa viwandani wataweza kujifunza ujuzi mpya katika taaluma ya umakenika kwa kutumia maabara na vifaa vya kisasa. Ujuzi huu mpya utawasaidia kuwezesha viwanda vyetu kubadlisha teknolojia za kizamani na kutumia teknolojia hizi mpya zinazotumia TEHAMA na kuleta maendeleo endelevu viwandani, ikiwa ni pamoja na wanafunzi wanaohitimu DIT kukabili ushindani katika soko la ajira pindi watakapohitimu. Vilevile, maabara zingine za kisasa za *Electrical Automation lab* na *Hydraulics lab* zitaanzishwa chini ya mradi huu.

**49. *Mheshimiwa Spika,*** wizara yangu ipo katika mchakato wa kutafuta fedha zitakazowezesha kuboresha majengo ya kufundishia katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) ili dhana ya chuo hiki kupandishwa hadhi kutoka Chuo cha Ufundi Mbeya, kwenda Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya (2005) na kwa sasa kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (Julai 2012) iwe dhahiri. Katika ujenzi huo chuo kinategemea kuzigeuza maabara zake ziwe kitovu cha uzalishaji bidhaa ili kubadili dhana ya sasa ya mafunzo viwandani na ujenzi wa kongano (*incubators*) ndani ya chuo ambapo wahitimu watatoka na uwezo wa kujiajiri na kutengeneza ajira kwa wengine.

**B.2.3 Uratibu wa Utafiti na Maendeleo na Uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

**50. *Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua kuwa sayansi, teknolojia na ubunifu ni dhana mtambuka, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imeendelea kuratibu na kuendeleza utafiti na ubunifu unaotekelezwa katika sekta mbalimbali kama ifuatavyo:-

i. Kuanisha vipaumbele na kusimamia ugawaji wa fedha za utafiti kutoka serikalini kwenye maeneo mbalimbali yanayoendeleza utafiti na ukuaji wa sayansi teknolojia na ubunifu kupitia Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia (MTUSATE);

ii. Kuendeleza rasilimali watu kupitia ufadhili wanafunzi wa shahada ya uzamili na uzamivu katika vyuo mbali mbali ndani ya nchi; naiii. Kutafuta fedha za uendelezaji wa Sayansi na teknolojia kutoka kwa wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kwa mfano mwaka 2013/14 COSTECH wameratibu matumizi ya Yuro milioni 1.8 za mfuko wa pamoja kati ya Tanzania, Sweden na Uholanzi (TASENE). Vilevile, COSTECH kwa kushirikiana na Shirika la Ushrikiano wa Kimataifa la Uingereza (*UK Department for International Development (DFID))* wamezindua mfuko wa kuendeleza ubunifu - *Human Development Innovation Fund (HDIF*) wenye thamani ya *Pound* za Uingereza milioni 30, utakaosaidia kuchochea na kuendeleza ubunifu katika sekta za Elimu, Afya na Maji.

**51. *Mheshimiwa Spika,*** kupitia kongano ya *Dar es Salaam Technology Busness incubator* (DTBi) iliyopo katika jengo la Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kampuni 42 zimefadhiliwa ambazo nyingi zipo katika hatua mbalimbali za kujiimarisha katika soko la ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Septemba, 2013 kampuni hizi zilikuwa zimetengeneza ajira 211 za moja kwa moja na 7,000 zisizokuwa za moja kwa moja.

**52. *Mheshimiwa* Spika**, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi, imeendelea

kuratibu miradi mbalimbali ya utafiti inayotumia teknolojia za nyuklia katika sekta za kilimo, afya na mifugo. Katika mwaka 2013/14 jumla ya miradi mitano (5) yenye thamani ya Yuro 642,400 ilifadhiliwa kupitia Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA) na miradi mingine yenye thamani ya Shilingi milioni 40 inayofadhiliwa kupitia Shirika la Kimataifa la Kuzuia Matumizi ya Silaha za Nyuklia (*Comprehensive Test Ban Treaty Organization (CTBTO*)).

### B.3 UTEKELEZAJI WA MASUALA YA UJUMLA KATIKA WIZARAB.

### 3.1 Uendelezaji wa Rasilimali Watu

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa kuendeleza rasilimali watu, Wizara imeratibu mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa kuwapeleka mafunzoni watumishi sita (6) kwenye mafunzo ya muda mrefu na mfupi, ambapo kati ya hao, watumishi watano (5) wamehudhuria mafunzo ndani ya nchi na mmoja (1) nje ya nchi.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza kanuni za maadili za kiutendaji katika utumishi wa umma  kwa kuwaelimisha watumishi kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma Na 8 ya mwaka 2002, marekebisho ya sheria ya Utumishi wa Umma Na.18 ya mwaka 2007, Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, Kanuni za Kudumu za utumishi wa Umma Toleo la mwaka 2009, Nyaraka za Serikali na taratibu za utendaji kazi kupitia Baraza la Wafanyakazi, TUGHE na Mikutano mbalimbali.

### B.3.2 Uandaaji wa Sera na Miongozo Mbalimbali katika Sekta

***55. Mheshimiwa Spika,*** kama ambavyo nimekwishaeleza hapo awali, Wizara iko katika hatua za mwisho za kurejea Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ya mwaka 2003. Sera hii inategemewa kukamilika katika mwaka wa fedha 2014/2015. Pia, uandaaji wa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera hiyo (*Implementation Strategy*) unafanywa sambamba na uhuishaji wa sera hiyo.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, wizara inafanya marejeo ya Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996 kutengeneza sera ya taifa ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Kazi hii inafanyika sambamba na Programu ya Mageuzi ya Mfumo wa Ubunifu nchini (*National Innovation System Reform Programme*).

### B.4 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KWENYE TAASISI ZA MAWASILIANO

### B.4.1 Shirika la Posta Tanzania (TPC)

**57. *Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Posta Tanzania katika jitihada zake za kuongeza na kuimarisha matumizi ya TEHAMA limeunganisha ofisi za Posta 112 katika mtandao wa kompyuta kwa lengo la kuboresha mazingira ya utoaji wa huduma kwa kutumia teknolojia za kisasa **(Kiambatanisho Na. 7)**. Juhudi za kuunganisha ofisi zilizobaki zinaendelea. Aidha, Shirika limeendelea kukuza biashara katika huduma za kutuma barua za kawaida kutoka milioni 13 mwaka 2010 hadi milioni 17 mwaka 2013. Idadi ya barua na vifurushi vya haraka nayo imeongezeka kutoka 419,990 mwaka 2010 hadi 621,561 mwaka 2013. Vile vile, Shirika limekamilisha ujenzi wa jengo la Posta Kibondo.

**B.4.2 Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)**

**58. *Mheshimiwa Spika,*** TTCL imeendelea kujenga na kuimarisha Mtandao Muhimili (*Core Network*) wa simu za mezani na kiganjani kwa kutekeleza Mradi wa Njia Mpya ya Mawasiliano Dar es Salaam-Unguja-Pemba (*Microwave Link*) utakaogharimu Dola za Kimarekani milioni 2.8. Mradi huu uliozinduliwa tarehe 13 Februari 2014 Chake Chake, Pemba, unalenga kuongeza uwezo wa njia ya Mawasiliano kati ya Dar es Salaam -Unguja-Pemba ambayo ilikuwa inasababisha msongamano (*congestion*) kwa wateja wa sauti (*voice*) na "*data*". Msongamano huu umesababishwa na mahitaji makubwa ya huduma za mawasiliano kwa watumiaji hasa taasisi za fedha, elimu ya juu na wafanyabiashara wakubwa. Kwa kutumia njia hii mpya ya mawasiliano, wateja wa Unguja na Pemba watapata huduma bora na inayokidhi mahitaji yao.

**59. *Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) imeendelea na juhudi za kuimarisha na kuongeza uwezo wa mtambo wa intaneti. Mradi huu unahusu uwekaji wa vifaa vya kuongeza uwezo wa mitambo (*Asymmetric Digital Subscriber Line - ADSL*) ili kuunganisha wateja katika mkongo wa TTCL katika maeneo muhimu ya kibiashara kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma bora ya simu na 'data' kwa wateja. Chini ya mradi huu, uwezo wa mtambo wa intaneti uliboreshwa imefungwa katika maeneo ya Bukoba, Kidatu, Tunduru, Tanga, Rombo, Same na Chukwani-Zanzibar. Mitambo mingine ambayo uwezo wake uliboreshwa imefungwa katika jengo la NSSF Kaloleni (Arusha), Mufindi (Iringa), jengo la VIVA Tower (Dar es Salaam) na Mbamba Bay (Ruvuma). Ufungaji wa mitambo mipya ya mawasiliano aina ya *Multi Service Access Node (*MSAN) katika mji wa Dodoma (Nane Nane) na Wilaya za Kongwa, Mpwapwa, Kishapu na Ushirombo unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni 2014.

**B.4.3 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**

**60. *Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kudhibiti mawasiliano nchini. Aidha,

Mamlaka inatekeleza mambo mengine kwa maelekezo ya serikali na taasisi za kikanda na za kimataifa zinazosimamia mawasiliano. Mambo hayo ni pamoja na kusimamia mpango wa kubadili teknolojia ya utangazaji kutoka mfumo wa analojia kwenda dijitali. Utekelezaji wa awamu ya pili umeanza baada ya utekelezaji wa awamu ya kwanza kufanyiwa tathmini na watalaam kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na matokeo kupendekeza awamu ya pili kufanyika. Kupitia utekelezaji wa awamu ya pili tayari miji ya Singida, Tabora, Musoma na Bukoba imepatiwa matangazo ya dijitali baada ya mitambo ya analojia kuzimwa.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kuongeza kasi ya mawasiliano kwa njia ya intaneti, wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kuratibu na kuwezesha ujenzi wa mitambo ya vituo vya kubadilishana mawasiliano ya intaneti (*Internet Exchange Points - IXP)* katika kanda mbalimbali nchini. Kupitia mitambo hii, mawasiliano ya intaneti kwa watumiaji wa kanda husika yanafanyika papo hapo badala ya kutoka nje ya nchi. Hadi hivi sasa mitambo imefungwa katika kanda ya kaskazini (Arusha), kanda ya kati (Dodoma) na mtambo wa kitaifa wa kubadilishana mawasiliano uliopo Dar es Salaam (*Tanzania Internet Exchange Point - TIX*). Mpango huu umepata mwitikio mzuri kutoka kwa watoa huduma za intaneti (*Internet Service Provider – ISP*) ambapo jumla ya watoa huduma ishirini na sita (26) wamejiunga na mtambo wa Dar es Salaam na watoa huduma sita (6) wamejiunga na mtambo wa Arusha. Kwa upande wa kanda ya nyanda za juu kusini (Mbeya), kanda ya ziwa (Mwanza) na kanda ya Zanzibar, mitambo imekwisha nunuliwa na taratibu za kuifunga zinaendelea kwa kushirikiana na watoa huduma husika.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imenunua mtambo wa kupima masafa ambao umegharimu Sh. 800,000,000 kwa ajili ya Zanzibar.

### B.4.4 Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa fedha 2013/14, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) umeendelea kusimamia utekelezaji wa mpango wa kufikisha mawasiliano kwenye kata 215 zilizopata wazabuni katika awamu ya kwanza (kata 52), awamu ya kwanza A (kata 77) na awamu ya kwanza B (kata 86). Kata hizo 215 zina jumla ya vijiji 1,268 vyenye wakazi zaidi ya 1,949,219 ambao hawafikiwi na huduma ya mawasiliano **(Kiambatanisho Na.8,9 na 10)**

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini iliyofanywa na Wizara kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote inaonyesha kuwa Tanzania ina jumla ya kata 1365 zisizo na mawasiliano au zinapata mawasiliano kwa shida. Jiografia ya baadhi ya

maeneo haivutii uwekezaji wa sekta binafsi kwa teknolojia iliyopo hata kama Serikali itatoa ruzuku ya asilimia mia moja (100%) kwani gharama kubwa zinahitajika katika uendeshaji. Kwa kutambua hilo Wizara inaangalia uwezekano wa kutumia teknolojia rahisi zenye ubora unaofaa kwa maeneo hayo.

Juhudi zinazofanywa na Serikali ni pamoja na kutafuta fedha kutoka nchi Wahisani ili kufikisha mawasiliano katika kata zenye eneo dogo na wakazi wachache ambazo hazivutii uwekezaji wa watoa huduma za simu.

**65. *Mheshimiwa Spika,*** dhana ya kufikisha mawasiliano kwa wote ni pana na inalenga maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara na vijiji vilivyo kwenye hali dhaifu (disadvantage) ikiwemo shule hususan zenye watoto wenye mahitaji maalum. Kupitia dhana hii Mfuko umeainisha shule 8,500 za Sekondari na Msingi na kutathmini namna ya kufikisha huduma za intaneti. Kwa kuanzia shule 25 zimeainishwa zikiwemo shule tano (5) za watoto wenye mahitaji maalum. Shule hizo ni pamoja na Shule ya Msingi ya Kisiwandui (Zanzibar), Shule ya watoto wasiosikia Buguruni (Dar es Salaam), Patandi (Arusha), Mtanga Maalum (Lindi) na Dumila Mchanganyiko (Morogoro) ambazo zitapelekewa huduma ya intaneti kwa njia ya setilaiti. Vifaa vya setilaiti tayari vimekwishaingia nchini. Dhumuni la mradi huu wa majaribio ni kuona namna gani mfuko unaweza kushirikiana na wadau wengine kama Halmashauri katika kuufanya kuwa mradi endelevu baada ya mwaka wa kwanza ambao mfuko utalipia gharama za intaneti.

### B.5 Utekeleaji wa Shughuli za Maendeleo Kwenye Taasisi za Sayansi na Teknolojia

### B.5.1 Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT)

**66. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa masomo 2013/14 Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT) imeanza ufundishaji katika kozi mpya za Shahada ya Uzamili katika Uhandisi Utawala (*Masters of Engineering in Maintenance Management*); Shahada ya Teknolojia katika Sayansi za Maabara (*Bachelor of Technology in Laboratory Sciences)* Stashahada ya Uhandisi wa Mifumo ya Mawasiliano (*Communication Systems Engineering*); Stashahada ya *Multimedia and Film Technology*; Stashahada ya *Renewable Energy Technology* na Stashahada ya Teknolojia ya Sayansi ya Chakula (*Food Science Technology*).

**67. *Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam imeendelea kufanya upanuzi wa udahili na uanzishaji wa programu mpya za stashahada kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Katika mwaka wa masomo 2013/2014, Taasisi ilidahili wanafunzi 1,633 kati yao wanafunzi wa

stashahada ni 939 (wa kiume 804 na wa kike 135) na wa shahada ya uhandisi ni 699 (wa kiume 616 na wa kike 83) sawa na asilimia 108 ya lengo.

**68.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kampasi ya Mwanza iliyokuwa ikijulikana kama Tanzania Institute of Leather Technology (TILT), DIT imekamilisha ukarabati wa karakana mbili (2). Aidha, ukarabati wa maabara mbili (2), hosteli mbili (2), bwalo la chakula (Cafeteria). Aidha, ukarabati wa nyumba sita (6) za wafanyakazi uko katika hatua za makabidhiano.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) inaendelea na utekelezaji wa mradi wa Matibabu Mtandao (*Telemedicine*) kama nilivyoeleza hapo awali. Jitihada hii kama ilivyo ile ya kuanzisha maabara za *mechatronics* kwa kushirikiana na kampuni ya FESTO ni utekelezaji wa maboresho wa taasisi za elimu kupitia maboresho ya mfumo wa sayansi teknolojia na ubunifu ambapo shughuli za taasisi za elimu zinaunganishwa na sekta zingine za uzalishaji na huduma nje ya utamaduni wa kawaida wa vyuo vya elimu ya juu. Kupitia mradi huu DIT itachangia moja kwa moja katika kuboresha huduma ya afya na hivyo kuwaongezea wanafunzi watakaohitimu katika taasisi hii kuwa na ujuzi wa viwandani na hivyo kuvutia katika soko la ajira.

### B.5.2 Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST)

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukidhi mahitaji ya Chuo kufuatia kupandishwa hadhi kutoka Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Mbeya (MIST) kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Chuo kimeajiri jumla ya watumishi 40; kati yao 38 ni wanataaluma na 2 ni waendeshaji.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kuleta uwiano wa jinsia katika sekta ya sayansi na teknolojia, MUST ilitoa mafunzo ya awali kwa wanafunzi wa kike 183, kati yao 161 walifaulu na kujiunga na masomo katika mwaka 2013/14. Vilevile, Chuo kimeendelea na upanuzi wa udahili na uanzishaji wa programu mpya. Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika mwaka wa masomo 2013/14 ni 3,442, kati yao wanafunzi wa stashada ni 2333 (533 wa kike na 1,800 wa kiume) na wanafunzi wa shahada ni 1,109 wanafunzi. Kati ya wanafunzi hao 107 wa kike na 1,002 wa kiume Chuo kinaendelea na juhudi za kubadilisha uwiano huu wa kijinsia.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kufanikisha upanuzi wa Chuo, Chuo kimeanzisha *college* mpya zikiwemo *College of Engineering and Technology*, *Institute of Science and Technology and School of Business Studies*. Vilevile, Chuo kiko mbioni kuanzisha *College of Science and Education* ambayo

itaanzishwa hivi karibuni. Aidha, Chuo kimepokea vifaa vya kufundishia kutoka Serikali ya Italia kupitia mradi wa *Tanzania Labour Market Support Programme* ili kuongeza ufanisi katika ufundishaji hususan katika kozi mpya zinzotegemea kuanza mwaka wa masomo 2014/15.

**73. *Mheshimiwa Spika,*** Chuo kinaendeleza ushirikiano na vyuo vya ufundi barani Afrika chini ya Shirikisho la *Commonwealth Association of Polytechnics in Africa (CAPA)*. Pia, Chuo kinaendeleza ushirikiano na umoja wa vyuo vikuu vya sayansi na teknolojia Afrika yaani "*African Network of Scienctific and Technical Institutions (ANSTI)*". Aidha, Chuo kinaendeleza ushirikiano na vyuo mbali mbali vya ufundi ikiwa ni pamoja na Chuo cha Ufundi Arusha (ATC); *Kilimanjaro International Institute of Telecommunications and Computer (KIITEC); Lilongwe Technical College (LTC)* cha Malawi na *Bielefeld University of Applied Science and Technical University of Dortmund* cha Ujerumani. Pia, Chuo kimeanzisha ushirikiano na *Commonwealth of Learning (COL*) katika nyanja za ufundishaji.

**B.5.3 Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha**

**74. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha, ilipata Hati Idhini (*Charter*) tarehe 19 Agosti, 2013, ambayo ilikabidhiwa kwa Mkuu wa Chuo na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 20 Agosti, 2013.

**75. *Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela- Arusha imeongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 83 mwaka 2011/2012 hadi kufikia wanafunzi 336 kwa mwaka wa masomo 2013/2014. Kati yao, wanafunzi 81 ni wanawake na 255 ni wanaume. Hili ni ongezeko kubwa la udahili katika masomo ya juu ikilinganishwa na hali ilivyokuwa kabla.

**76. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha utendaji na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Taasisi unazingatia kanuni na taratibu za Serikali, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela – Arusha imekamilisha-uandaaji wa miongozo na sera za ndani zikiwemo Mpango Mkakati wa Chuo wa mwaka 2013–2027; Kanuni za Fedha za Taasisi za mwaka 2013; Mwongozo wa Ukaguzi wa Hesabu za Ndani wa mwaka 2013 na Sera ya ndani ya Maendeleo ya Rasilimali Watu ya mwaka 2013.

**77. *Mheshimiwa Spika,*** aidha, tarehe 19 Desemba 2013 Taasisi ya Sayansi na Teknolojjia ya Nelsoni Mandela – Arusha ilifanya mahafali yake ya kwanza. Jumla ya wanafunzi 44 kati ya 53 wa shahada ya uzamili waliodahiliwa mwaka 2011/12 walitunukiwa shahada zao. Idadi hii ni sawa na asilimia 83 ya wanafunzi wote wa uzamili waliodahiliwa. Ufaulu huu ni mkubwa ilinganishwa na vyuo

vingine ambapo asilimia kubwa ya wanafunzi huhitimu nje ya muda uliopangwa awali.

**78. *Mheshimiwa Spika***, vilevile, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 Taasisi imeendelea kutekeleza miradi ya utafiti inayofadhiliwa na wafadhili mbalimbali yenye thamani ya Sh.9,907,930,782. Taasisi pia imeajiri wafanyakazi 35 wakiwemo wanataaluma 32 na waendeshaji 3; kati yao wanawake ni watano (5) na wanaume ni 30.

**79. *Mheshimiwa Spika***, ili kuinua kiwango cha taaluma kwa wataalam na wanafunzi wake, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha imeimarisha na kuendeleza ushirikiano na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi zikiwemo *University of Califonia System, Washington State University, University of Illinois at Urbana-Champaign, Purdue University, Michigan State University, Kennesaw State University in USA, East China Normal University, Indian Institute of Technology at Bombay and Delhi (ITT Bombay and Delhi), Korean Institute of Science and Technology (KIST), Hanyang University (HYU), Pohang University of Science and Technology (POSTECH), University of Saskatchewan-Canada, Belgium Universities(KU Leuven, VUB & U Antwerp), Ifakara Health Institute, The Tropical Pesticide Research Institute (TPRI), National Institute for Medical Research (NIMRI), Southern African Centre for Infectious Diseases Surveillance (SACIDS).*

**B.5.4 Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC)**

**80. *Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) imeendelea kusimamia matumizi salama ya mionzi katika hospitali na vituo vya afya, viwandani, kwenye migodi na kufanya tafiti mbalimbali. Juhudi hizi zimeleta matokeo mazuri ikiwemo (i) kuboresha huduma za tiba ya saratani, (ii) uboreshaji wa mazao ya kilimo na mifugo, na (iii) kuhakiki usalama wa vyakula na kwenye pembejeo za kilimo zisiwe na mionzi yenye madhara.

**81. *Mheshimiwa Spika,*** Tume imeshirikiana na vyuo vikuu nchini kupitia maabara zake ambapo wanafunzi wapatao kumi (10) wanaosoma shahada za uzamili na uzamivu wamefanya tafiti za teknolojia ya nyuklia katika maabara hizo. wanafunzi hao wametoka katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela. katika kuimarisha mahusiano na taasisi za elimu na utafiti, Tume imeanza mchakato wa kuanzisha mtandao wa wataalam wa nyuklia walio kwenye vyuo na taasisi mbalimbali zinazotumia teknolojia ya nyuklia unaoitwa *Tanzania Nuclear Educational Network for Science and Technolgy- TAN-NEST*. Mtandao huu ambao utasaidia kuwaunganisha wataalam na kuongeza kasi za tafiti.

**82. *Mheshimiwa Spika,*** Tume vilevile hufanya tafiti zenye lengo maalum na zinazohitaji kuhakiki usalama wa makundi maalum. Kupitia utaratibu huu wa kuchunguza kiwango cha dozi ya mionzi katika matumizi ya mashine za *X-ray* na *Computed Tomography* yaani CT scan kwa watoto wadogo (*Pediatric Patients)*. Utafiti huu imeonyesha kuwa kiwango cha mionzi katika mashine hizi kipo kati ya 22 - 146µGy.$cm^2$ ambacho kipo chini ya viwango vilivyowekwa kimataifa na hivyo kuwahakikishia watumiaji usalama wa mashine hizo kwamba hazina madhara kwa watoto.

**83. *Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua mchango wa Tume katika tafiti mbalimbali, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki Duniani (International Atomic Energy Agency (IAEA)) limeipatia TAEC kifaa cha kuhakiki ubora wa machine za X-ray (*Modern Quality Control Equipment)* chenye thamani ya Yuro 7,327.20.

Aidha, Tume imekagua vituo vyenye vyanzo vya mionzi vipatavyo 118 na migodi 7 na kubaini kuwa hali ya usalama wa wafanyakazi na mazingira ni salama kwa sababu vipo chini ya viwango vya kimataifa kama inavyotakiwa kisheria. Mpaka sasa Tume imesajili vituo 607 vyenye vyanzo vya mionzi vikiwa na jumla ya vyanzo vya mionzi 997.

**84. *Mheshimiwa Spika,*** Tume vilevile imeendelea na kuhakiki viwango vya mionzi isiyoayonisha katika minara ya simu (*Mobile phone base stations*). Mpaka sasa vituo 122 vimepimwa nchi nzima na kuonyesha kuwa kiwango cha mionzi inayotoka katika minara ya simu iko ndani ya viwango vinavyokubalika na Tume inayoratibu viwango vya mionzi isiyoayonisha kimataifa *International Commission on Non-Ionizing Radiation Protection* (ICNRP).

Aidha, Tume inaendelea na uandaaji wa kanuni za kudhibiti matumizi ya mionzi isiyoayonisha kitaifa.

**85. *Mheshimiwa Spika,*** baada ya kukamilisha uandaaji wa sheria na kanuni za uchimbaji wa madini ya urani, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania iliomba msaada kutoka kwa Shirika la Kimatifa la Nguvu za Atomiki (*International Atomic Energy Agency*) ili kutathmini utayari wa nchi katika kusimamia uchimbaji wa urani. Mkazo uliwekwa kwenye mradi wa urani wa mto Mkuju ambao ulishapata leseni ya uchimbaji ili athari kwa watu na mazingira zisitokee. Msaada wa tathmini ulioombwa IAEA ni katika maeneo ya utafutaji, tathmini ya rasilimali, ujenzi wa mgodi, usindikaji, usafirishaji. Kufukia mashimo, kusafisha na kurejesha mazingira baada ya uchimbaji kufikia ukomo.

### B.5.5 Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imeendelea kuratibu miradi ya utafiti 59 inayofadhiliwa na Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia (MTUSATE) **(Kiambatanisho Na.13)**. Aidha, Tume imesimamia pia miradi mingine 4 inayofadhiliwa na Mfuko wa pamoja kati ya Tanzania, Sweden na Uholanzi (TASENE). Baadhi ya matokeo ya tafiti hizo ni: ugunduzi wa vinasaba vya mimea ya Tanzania, ubunifu katika tiba ya kupunguza makovu yatokanayo na upasuaji baada ya kurekebisha mdomo wa sungura, utunzaji wa lugha na utamaduni wa Wangoni.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** wizara kupitia Ofisi ya COSTECH Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Utoaji Huduma za Kujitolea (VSO) na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume imeanzisha mradi wa kutengeneza kifaa cha kutumia mwanga wa jua (*solar drier*) kwa ajili ya kukaushia matunda mbalimbali pamoja na mwani. Kwa sasa kifaa cha awali (*prototype*) kinajaribiwa kwa ajili ya kuthibitisha joto lake na mambo mengine ya kiufundi.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** wizara kupitia COSTECH, imefadhili jumla ya watafiti 130 katika vyuo mbalimbali nchini ambapo watafiti 82 wanachukua shahada ya uzamili na watafiti 48 wanachukua shahada ya uzamivu **(Kiambatanisho Na.12)**. Kati ya wanafunzi hao, 22 wanatoka Zanzibar. Tangu mwaka 2010 mpaka sasa, wizara kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imefanikiwa kuwasomesha watafiti 517 katika vyuo vikuu 13 vya hapa nchini.

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** wizara kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imefanikisha kukarabati vituo vya utafiti 20, ambapo vituo 19 ni vya Tanzania Bara na kituo kimoja (1) ni Zanzibar. Ujenzi wa jengo la ofisi katika Kituo cha Utafiti wa Kilimo Naliendele, Mtwara na ujenzi wa maabara ya nyama na nyumba tatu (3) kwa ajili ya wafanyakazi katika Kituo cha Utafiti wa Mifugo cha TALIRI cha Mabuki Misungwi Mwanza umekamilika.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** wizara kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imeanzisha jumla ya kongano bunifu za uzalishaji 54, ambapo kongano 23 zilizokidhi vigezo vya kuwa bunifu zimewezeshwa kwa kupewa shilingi milioni 8 kila moja ili kuweza kukuza uwezo wao wa ubunifu na kuongeza ushindani **(Kiambatanisho Na.14)**. Idadi ya kongano zilizowezeshwa kwa mikoa ni pamoja na Morogoro (7); Singida (2) Manyara (3), Shinyanga (2) Dar es Salaam (4), Ruvuma (1), Rukwa (1) na Zanzibar (5). Aidha, zaidi ya watu 250 wameajiriwa kutokana na kongano hizo kuimarisha shughuli zake kupitia uwezeshaji huu.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Zanzibar, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia inaendelea kuzisimamia kongano 5 ikiwemo kongano ya

mwani, kuku, mbogamboga, viungo, utalii na ufugaji wa samaki. Kongano ya mwani imetoa ajira ya watu kama 30,000 kwa Zanzibar wengi wao wakiwa akina mama, na pia imelifanya zao la mwani kuwa ni sekta ya pili kwa kuingiza fedha za kigeni Zanzibar.

**92. *Mheshimiwa Spika,*** wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia inaendelea na juhudi za kuanzisha Kijiji Mahiri cha TEHAMA (*Smart ICT Village*). Kijiji hiki, ambacho kitaanzishwa kwa utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi kinakusudia kuhawilisha maarifa na teknolojia kutoka nje ya nchi na kuyaleta hapa nchini na pia kukuza uwezo wa wanasayansi, watafiti na wajasiriamali chipukizi katika sekta ya TEHAMA. Kwa sasa Tume ipo katika hatua za mwisho za kusaini mkataba wa makubaliano (MoU) na Mamlaka ya Uwekezaji (EPZA), kwa lengo la kupata eneo lenye ukubwa wa ekari 438 katika eneo la EPZA lililopo Bagamoyo Mkoa wa Pwani ili kuanza shughuli za ujenzi.

## C. CHANGAMOTO ZILIZOPO KATIKA SEKTA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

**93. *Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu na malengo ya Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia zipo pia changamoto kadhaa ambazo zimechangia kutofikiwa kwa malengo ya sekta kama ifuatavyo:

### C.1 Mtiririko Mdogo wa Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo

**94. *Mheshimiwa Spika,*** mtiririko mdogo wa fedha za miradi ya maendeleo na upatikanaji wake kwa wakati umeleta changamoto katika kukamilika kwa baadhi ya shughuli zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2013/14. Katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 30,295,485,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambazo zilijumuisha fedha za utafiti na maendeleo (*Research and Development*). Hadi kufikia tarehe 30/05/2014, wizara ilikuwa imepokea **Sh. 5,033,387,500** sawa na asilimia **16.62** ya fedha zilizoidhinishwa.

### C.2 Taasisi Zinazoendesha Programu za Mafunzo Katika Ngazi za Diploma Kutokuwa na Stahili ya Mkopo

**95. *Mheshimiwa Spika,*** Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) zinaendesha programu za mafunzo katika ngazi za cheti na diploma ambazo wanafunzi wake hawana stahili ya kupata mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HELSB) kama ilivyo kwa wanafunzi wanaosoma katika ngazi ya shahada.

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na dhamira ya dhati ya Serikali ya kusomesha wataalam wengi wa kutosheleza mahitaji ya taifa katika kada hii ya diploma, kukosekana kwa fedha za kutosha hususan za Matumizi Mengineyo (OC) huduma za utendaji wa taasisi hizi na kuziweka katika hali ya wasiwasi hususan kwenye huduma zinazogharamiwa na Chuo zikiwemo za chakula kutishiwa kusitishwa. Hali hii isingejitokeza kama huduma hii ingechukuliwa na wanafunzi wenyewe kupitia mikopo yao binafsi. Huduma hizi kuendelea kutolewa na na vyuo kumepelekea taasisi kuwa na malimbikizo ya madeni kwa watoa huduma za chakula na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Aidha, kwa upande wa taaluma, kutopatikana kwa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo kuna sababisha wanafunzi kuchelewa kwenda kwenye mafunzo kwa vitendo viwandani (*industrial pratical training*). Hali hiyo imekuwa ikichelewesha kufikiwa kwa azma ya Serikali ya kuandaa rasilimali watu ya kutosha katika kutumia sayansi na teknolojia katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

### C.3 UHABA WA WATAALAM KATIKA NYANJA ZA SAYANSI, TEKNOLOJIA ZA UBUNIFU

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu inakabiliwa na uhaba wa wataalam, kuwapo kwa hali hii kunakinzana na utashi wa kuwa na jamii inayoongozwa na maarifa (*knowledge-led society*). Jitihada zinafanywa na taasisi za elimu kupanua udahili ni moja ya mkakati wa kupunguza tatizo hili.

### C.4 USALAMA KATIKA MITANDAO YA MAWASILIANO

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na mafanikio makubwa hasa kufuatia kuongezeka kwa matumizi ya TEHAMA ulimwenguni na kasi kubwa ya mabadiliko na matumizi ya teknolojia ya mawasiliano imeleta hofu kwa watumiaji kutokana na kuongezeka kwa uhalifu wa mtandao na uvunjifu wa maadili katika jamii. Serikali kwa kutambua changamoto hizi imeanzisha mikakati mbalimbali ikiwemo kutunga sheria, kuanzisha kikosi maalum cha kupambana na uhalifu katika mtandao na kutoa elimu kwa wananchi. Wizara inaamini kuwa suluhishi madhubuti katika eneo hili utatokana na ushiriki wa jamii yenyewe katika kukabili kadhia hizi na kuongeza matumizi ya teknolojia kukabili hali hii.

### C.5 SHUGHULI ZA UTAFITI NA MAENDELEO KUTOTENGEWA FEDHA ZA KUTOSHA

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** upungufu wa fedha umeendelea kuathiri utekelezaji wa malengo na ufanisi wa shughuli za utafiti na maendeleo. Azma ya Serikali kuongeza tengeo la fedha za utafiti na maendeleo katika Bajeti ya Serikali kufika asilimia moja (1%) ya Pato Ghafi la Taifa. Pamoja na azma hii kuwepo, pamekuwa na changamoto katika kufikia lengo hili ambapo fedha

zinazotengwa pamoja na kuongezeka ikilinganishwa na miaka ya nyuma hazijaweza kufikia kiwango hiki. Wizara kupitia Uboreshaji wa Mfumo wa Sayansi, Teknolojia imeandaa vivutio ili kuongeza mchango wa sekta binafsi na wadau wengine kuchangia utafiti na maendeleo ya sayansi na teknolojia na ubunifu kwa ujumla. Hata hivyo ili kufanikisha jambo hili, tengeo la fedha kupitia bajeti ya Serikali linapaswa kuongezeka kugharamia utekelezaji wa programu hii.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na changamoto nilizozieleza, wizara itaendelea kutekeleza majukumu yake ili na kuzipatia ufumbuzi changamoto hizi ili kuongeza mchango wa sayansi, teknolojia na ubunifu katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi wote kwa ujumla.

## D.MALENGO YA BAJETI KWA MWAKA 2014/2015

**D.1 SEKTA YA MAWASILIANO101.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2014/2015 katika Sekta ya Mawasiliano, wizara itatekeleza yafuatayo:

(i) Kuendelea na Ujenzi wa Awamu ya III ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Utekelezaji wa Awamu ya III ya ujenzi wa Mradi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unajumuisha: uunganishaji wa Zanzibar katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; upanuzi wa Mkongo kwenye baadhi ya maeneo ambayo hayakufikiwa katika Awamu ya I na II; na ujenzi wa Mtandao wa IP/MPLS na Vituo Mahiri vya kutunzia kumbukumbu (*Data Centres*) katika miji ya Dar es salaam, Dodoma na Zanzibar;

(ii) Kuweka na kusimamia mtandao wa TEHAMA mkubwa na wenye kasi zaidi (*Broadband strategy*);

(iii) Kukamilisha utungaji wa Sheria ya Matumizi Salama ya Mtandao (*Cyber Security Law*);

(iv) Kuendelea kuunganisha taasisi za elimu ya juu na utafiti katika Mkongo wa Taifa Mawasiliano chini ya mradi wa STHEP kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo hususan Benki ya Dunia;

(v) Kuanza mchakato wa uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 pamoja na kutunga Sera mpya ya Taifa ya Menejimenti ya Masafa;

(vi) Kuanzisha programu ya kukuza upatikanaji na utoaji wa huduma kupitia ugatuzi wa baadhi ya huduma za taasisi na kampuni kufanywa na wajasiriamali wa nje au wa kujitegemea kupitia TEHAMA (*Business Process Outsourcing*);

(vii) Itakamilisha utekelezaji wa Mradi wa Kitaifa wa Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta katika Mkoa wa Dar es Salaam na kuanza utekelezaji Zanzibar pamoja na mikoa ya Arusha, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Moshi na Tanga;

(viii) Kuendelea na awamu ya pili ya zoezi la kuhama kutoka Mfumo wa Utangazaji wa Analojia kwenda Dijitali; Awamu hii inahusisha miji ya Tabora, Singida, Kigoma, Musoma, Bukoba, Morogoro, Iringa, Kahama, Songea, Lindi na Mtwara;

(ix) Itaratibu utekelezaji wa Mradi wa Jamii Habari pamoja na kuanzisha mpango mkakati wa kitaifa wa kupeleka matokeo yaliyojitokeza kupitia mradi huu katika sehemu zingine za nchi. Aidha, mkakati wa kupanua Mradi wa Jamii Habari kuingiza eneo la kukuza uchumi kupitia teknolojia (*knowledge economy*) baina ya Tanzania na Finland utatekelezwa;

(x) Itakamilisha uanzishaji wa Tume ya TEHAMA na kuiwezesha kuanza kufanya kazi;

(xi) Itaratibu na kusimamia utendaji kazi wa Taasisi za Mawasiliano zilizo chini ya Wizara ambazo ni Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), Shirika la Posta Tanzania (TPC), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Baraza la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA - CCC) na Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF); pamoja na kuratibu utekelezaji wa Sera za Mawasiliano kwa kampuni binafsi zinazotoa huduma hizo nchini;

(xii) Itaendelea kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa ili kuchochea ukuaji wa sekta ya mawasiliano nchini; Aidha, itakamilisha uridhiaji wa mabadiliko ya mikataba ya Umoja wa Posta Duniani (UPU); Umoja wa Mawasiliano Duniani (ITU) na matumizi ya huduma za mawasiliano wakati wa majanga (*Tampere Convention on emergence telecommunications*);

(xiii) Itaratibu mpango wa Mawasiliano kwa Wote pamoja na kuimarisha vituo vya mawasiliano ya kijamii na kusimamia uetekelezaji wa mpango wa utabibu kwa njia ya TEHAMA (*telemedicine*) kupitia mradi wa *Pan African e-Network* unaofadhiliwa na Serikali ya India.

(xiv) Itaendelea kuweka miongozo itakayoboresha huduma za mawasiliano nchini ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora (*Quality of Services*) na kuandaa Mkakati wa Taifa wa Posta (*National Postal Strategy*) utakaoendana na viwango vya kimataifa.

### D.2 SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU

**102. *Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa sayansi, teknolojia na ubunifu katika mwaka wa fedha 2014/15, Wizara itatekeleza yafuatayo:

(i) Kuendelea na utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Mfumo wa Ubunifu nchini (*National Innovation System Reform*);

(ii) Kuendelea na uimarishaji wa mifumo, taasisi na rasilimali watu ili kukuza utafiti na matumizi ya sayansi na teknolojia nchini;

(iii) Kuimarisha na kuboresha taasisi za utafiti, sayansi na teknolojia nchini;

(iv) Kubuni, kuandaa na kusimamia sera, mipango ya utekelezaji, miongozo, mikataba, itifaki, sheria na kanuni zinazolenga kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu nchini;

(v) Kukamilisha andiko la programu ya matumizi ya nyuklia;

(vi) Kuimarisha uhusiano wenye tija na wadau mbalimbali katika sayansi, teknolojia na ubunifu ndani ya nchi, kikanda na kimataifa;

(vii) Kuhamasisha jamii kuhusu sayansi, teknolojia na ubunifu kwa ujumla kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

(viii) Kuratibu uendelezaji wa miundombinu na rasilimali watu katika sayansi na teknolojia; na

(ix) Kuandaa sheria ya sayansi, teknolojia na ubunifu, kukamilisha sera taifa ya sayansi, teknolojia na ubunifu pamoja na mkakati wa utekelezaji na kuandaa Sera ya Taifa ya Teknolojia za Nyuklia ya mwaka 2013.

### D.3 MASUALA YA UJUMLA

**103. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara itatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuajiri na kuwapandisha vyeo watumishi wenye sifa na wanaokidhi vigezo mbalimbali vilivyo kwenye nyaraka za maendeleo ya

utumishi wa umma za mwaka 2002 pamoja na Tathmini ya Utendaji Kazi kwa Uwazi (OPRAS);

(ii) Kusimamia utekelezaji wa mkakati wa uadilifu kwa kutekeleza kanuni za maadili ya kiutendaji katika utumishi wa umma, kwa kuwaelimisha watumishi kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002, kanuni na taratibu za uendeshaji katika utumishi wa umma na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007 ili utumishi wa umma uwe wenye ufanisi na wa kuheshimika;

(iii) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Waraka Na. 2 wa Mwaka 2006 kwa kuhamasisha watumishi kupima afya zao ili wale watakaoonekana kuwa na upungufu katika afya zao waweze kupatiwa huduma;

(vi) Kuendela kutekeleza Mpango wa Mafunzo kwa kuwapeleka kwenye mafunzo watumishi katika maeneo ya sayansi, teknolojia na mawasiliano ili kuwaongezea ujuzi, maarifa na ufanisi katika utendaji wao wa kazi;

(xv) Kuendelea kuimarisha sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia utekelezaji wa mifumo ya kimenejimenti mathalani Miundo ya TEHAMA, mgawanyo wa majukumu pamoja na mpango wa kurithishana madaraka;

(xiii)Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano 2011/2012-2015/2016;

(xiv)Kuratibu uandaaji wa Taarifa ya Kusimamia, Kudhibiti na Kuratibu Mapato na Matumizi ya Serikali;

(xv) Kuratibu uandaaji wa Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010-2015;

(xvi) Kuratibu usimamizi na tathmini ya miradi inayotekelezwa na Wizara na Taasisi zilizo chini yake;

(xix) Kushirikiana na vyombo vya habari kuelimisha umma kupitia redio, runinga, magazeti, machapisho na tovuti ili kuongeza uelewa wa jamii kuhusu masuala ya TEHAMA, sayansi, teknolojia na ubunifu.

## D.4 MALENGO YA TAASISI

### D.4.1 Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT)

**104. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/2015, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kudahili wanafunzi wapya 1600 wakiwemo wa stashahada 1,090 (wa kiume 690 na kike 400) na shahada ya uhandisi 450 (wa kiume 320 na kike 130) na shahada ya uzamili 60 na kuendelea kuwa na jumla ya wanafunzi 3,250;

(ii) Kuendesha programu maalum kwa wanafunzi wa kike ili kuwezesha wanafunzi 100 wa kike wapate sifa za kudahiliwa katika kozi mbalimbali za uhandisi;

(iii) Kuanzisha kozi mpya za stashahada za; *Civil and Highway Engineering* na *Food Science and Technology;*

(iv) Kumalizia ujenzi wa *DIT Teaching Tower*;

(v) Kuanzisha kozi ya elimu ya juu katika *Sustainable Energy Engineering* kwa ushirikiano na *ACP-EU Cooperation Program in Higher Education EDULINK II: ENERGISE (Enlarged Network in Education and Research for Growing Impact of Sustainable Energy)*. Pia, kuanzisha programu ya masomo ya juu katika *Computational Engineering under the Weather Information Management in East Africa (WIMEA-ICT) programme*;

(vi) Kuendelea na ukarabati wa majengo, miundombinu ya maji, umeme na mawasiliano katika Kampasi ya DIT Mwanza;

(vii) Kuendelea kufundisha programu za muda mfupi za kitaalam za kutengeneza viatu, kutengeneza bidhaa za ngozi, kusindika ngozi na matumizi ya kompyuta.

(viii) Kuendeleza mradi wa matibabu mtandao kwa kuunganisha Hospitali ya Bugando, Hospitali ya Seliani Arusha, Hospitali ya Kilimanjaro Christian Medical Centre (KCMC) na Mnazi Mmoja, Zanzibar kwenye mtandao.

**D.4.2 Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST)**

**105. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/2015, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kitatekeleza mambo yafuatayo:-

(ix) Kudahili jumla ya wanafunzi 3,700 katika ngazi ya stashahada na shahada;

(x) Kuendelea kutoa mafunzo ya awali (*pre-entry*) kwa wanafunzi wa kike kwa lengo la kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike kufikia 100 katika fani za uhandisi , sayansi na teknolojia;

(xi) Kuanzisha kozi mpya za fani za mekatroniki, sayansi na teknolojia ya vyakula, uhandisi mawasiliano na uhandisi madini;

(xii) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya chuo ikiwemo kuendelea na ujenzi wa maktaba; kuanza ujenzi wa *College of Engineering and Technology, College of Science and Education na School of Business Studies*; na kuanza ujenzi wa jengo la utawala, hosteli za wanafunzi pamoja na nyumba za wafanyakazi.

**D.4.3 Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela-Arusha**

**106. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/2015, Taasisi ya Nelson Mandela itatekeleza mambo yafuatayo:

(xiii) Itadahili jumla ya wanafunzi wapya 100 katika fani mbalimbali za sayansi na uhandisi; kati yao 60 ni wa shahada za uzamili na 40 ni wa shahada za uzamivu, pamoja na kuendelea kufadhili wanafunzi 278 wanaoendelea, kati yao 165 ni wa shahada za uzamili na 113 wa shahada za uzamivu;

(xiv) Itaanzisha progamu mpya saba za Shahada za Uzamili na Uzamivu;

(xv) Itaajiri wafanyakazi 84, ikiwa ni wanataaluma 37, mafundi 21 na waendeshaji 26;

(xvi) Itaimarisha kituo cha TEHAMA na ununuzi wa vifaa vyake pamoja na ununuzi wa vifaa vya mafunzo, maabara na maktaba; na

(xvii) Itaendeleza ujenzi wa maabara na majengo ya ofisi;

**D.4.4 Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)**

**107. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/2015, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) itatekeleza mambo yafuatayo:

(xviii) Itaendelea na juhudi za kuimarisha matumizi ya matokeo ya tafiti mbali mbali ili zitumike kufanya maamuzi kwa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na watoa maamuzi, watunga sera, sheria, mikakati na mipango itakayoboresha huduma za sekta hapa nchini;

(xix) Itaratibu shughuli za utafiti nchini, ikiwa ni pamoja na zile zinazofadhiliwa na mfuko wa Taifa wa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia (MTUSATE) na Tanzania Sweden and Netherlands (TASENE);

(xx) Itaendelea na jitihada za uendelezaji na uhawilishaji wa teknolojia mbalimbali nchini;

(xxi) Itagharamia tafiti za kisayansi ikiwa ni pamoja na:-

(a) Uendelezaji wa rasilimali watu;

(b) Kuboresha mazingira ya utafiti miundombinu na vitendea kazi; na

(c) Miradi mipya ya utafiti na ile inayoendelea kulingana na vipaumbele vya taifa.

(xxii) Itaanzisha atamizi mpya ya biashara na kilimo (*Agri-business Incubator*) ili kukuza ujasiriamali na uwekezaji katika sekta ya kilimo hususan usindikaji wa mazao;

(xxiii) Itaendeleza uboreshaji wa jumla katika kongano 45 ili ziweze kufanya vizuri zaidi katika soko la ushindani kwa kutengeneza bidha zenye ubunifu na ubora zaidi;

(xxiv) Itahamasisha mfumo wa kuendeleza teknolojia mbalimbali katika vyuo vikuu na taasisi za utafiti;

(xxv) Itaanzisha mfuko wa kusaidia maendeleo ya teknolojia (*Funds for Technology Development*) mbalimbali kwa njia ya ushindani;

(xxvi) Itarusha vipindi 30 vya runinga, vipindi 20 vya redio kwa kushirikiana na TBC, kuchapisha makala 30 katika magazeti, kuchapisha jarida la kielektroniki la kila mwezi na kushiriki maonyesho 15 yanayohusu sayansi, teknolojia na ubunifu;

(xxvii) Itaboresha shughuli za kuratibu tafiti katika ofisi ya Zanzibar kwa kushirikiana na SMZ;

(xxviii) Kuendelea na ujenzi wa kijiji cha kisasa cha mawasiliano (*ICT Technology Park*) ambacho kitachangia kuleta makampuni makubwa ya kimataifa na hatimaye kuweza kukuza uchumi wenye kutumia maarifa (*knowledge base economy*); na

(xxix) Itaendeleza jitihada za kutumia mfuko wa MTUSATE kama kichocheo cha kuwavutia wafadhili wengine ili waweze kuchangia mfuko wa utafiti na maendeleo ikiwa ni pamoja na sekta binafsi.

(xxx) Itaratibu uanzishwaji wa "*channel*" ya luninga ya Sayansi na Teknolojia na Ubunifu.

### D.4.5 Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC)

**108. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/2015, Tume ya Taifa ya Nguvu za Atomiki Tanzania itatekeleza mambo yafuatayo:

(i) Itafanya tathmini ya maombi 370 ya leseni mbalimbali ili kuona kama yanakidhi matakwa ya sheria na kanuni za usalama na kinga ya mionzi ya mwaka 2004;

(ii) Kuendelea na upimaji wa viwango vya mionzi (*Personnel Dosimetry Service*) kwa Wafanyakazi 1,600;

(iii) Kutafuta na kukusanya mabaki ya vyanzo vya mionzi na kuyahifadhi katika maabara maalumu (*Central Radioactive Waste Management Facility- CRWMF*) iliyoko Arusha;

(iv) Kutoa elimu kwa wananchi waishio maeneo yenye madini ya urani kwa kupitia makongamano manane (8) ili kuongeza uelewa na kuweka tahadhari pale inapostahili;

(v) Kuendelea na upimaji wa vyanzo vya mionzi katika sampuli angalau 6,000 za vyakula na mbolea;

(vi) Kuimarisha upimaji wa mionzi kwenye mazingira katika vituo 24 ambavyo vimekuwa vikiendeshwa kwa ushirikiano na Taasisi nyingine;

(vii) Kuendelea na ukaguzi wa migodi mitano (5) mikubwa inayofanya kazi ili kubaini hali ya usalama inayoendelea katika migodi hiyo;

(viii) Kuendesha kituo cha kupima mionzi katika hewa ya anga kupitia *Radionuclide Monitoring Station (TZP-RN64*) iliyopo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) chini ya mkataba wa kimataifa wa *Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty of Nuclear Weapons (CTBT*);

(ix) Kuratibu miradi ya kitaifa na kikanda (AFRA) inayogharamiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki Duniani (*International Atomic Energy Agency-IAEA*) na kusimamia mchakato wa kuandaa miradi mipya kwa kipindi cha mwaka 2015/2016;

(x) Kuendelea kuimarisha uendeshaji wa shughuli na majukumu ya TAEC, kwa kuendelea na juhudi za kuanzisha ofisi ya kanda katika mkoa wa Ruvuma (Namtumbo) ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Tume;

(xi) Kuandaa kanuni, taratibu na viwango ili kuhakikisha usimamizi wa mionzi isiyoayonisha katika nyanja na sekta mbalimbali nchini;

(xii) Kufanya kaguzi kwenye vituo 120 vinavyotoa mionzi isiyoayonisha (*non-ionizing radiation*) kwenye minara ya simu, redio, luninga, na vifaa vingine vya mionzi ili kubaini usalama wa wakazi wa maeneo husika; na

(xiii) Kuanza mradi wa ujenzi wa maabara za kisasa ili kukidhi majukumu na mahitaji ya sasa na baadae. Pamoja na ujenzi huu, mkakati wa kupeleka huduma karibu na wananchi utaanza kwa kuweka maabara katika vituo vya Dar es Salaam na Zanzibar; na

(xiv) Kuendelea kukagua vituo vyenye vyazo vya mionzi 150 na migodi 20 ili kubaini hali ya usalama.

**D.4.6 Shirika la Posta Tanzania (TPC)109.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Shirika la Posta Tanzania litatekeleza mambo yafuatayo:

(xxxi) Kuunganisha ofisi za Posta katika mtandao wa kielektroniki kutoka 112 (mwaka 2013/14) hadi 147 ili kuongeza matumizi ya TEHAMA katika kutoa huduma zake;

(xxxii) Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi 295 yatakayohusisha uendeshaji (60), TEHAMA (95), huduma kwa wateja/ masoko (105) na uongozi (35);

(xxxiii) Kuanza ujenzi wa miradi mipya ya Posta - Bariadi, Sumbawanga na upanuzi wa jengo la posta Babati;

(xxxiv) Ukarabati wa jengo la Makao Makuu (*Posta House*) Dar es Salaam na majengo ya yaliyoko Wete, Mahonda, Moshi na Lindi;

(xxxv) Kuimarisha na kuboresha duka la kununua na kuuza fedha za kigeni (*Posta Bureau De Change*) katika Posta Kuu ya Dar-es-Salaam na kuanzisha duka kama hilo katika ofisi ya Posta Shangani /Zanzibar;

(xxxvi) Kuendelea kuimarisha na kuboresha huduma za EMS – *courier* na *City Urgent Mail (pCUM*); na

(xxxvii) Kupanua huduma za kibenki kwa uwakala kupitia Benki ya Posta na CRDB katika ofisi za Posta zilizoko wilayani.

**D.4.7 Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)110. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/2015, Kampuni ya Simu Tanzania itatekeleza mambo yafuatayo:

(xxxviii) Kuboresha mapato kutoka Sh. bilioni 91.3 mwaka 2013 hadi Sh. bilioni 149 mwaka 2015 (ongezeko la 63.2%);

(xxxix) Kuongeza idadi ya wateja wake wa huduma mbalimbali za simu (*voice and data*) kutoka 259,106 mwaka 2013 hadi 1,200,000 mwaka 2015 (ongezeko la 363%);

(xl) Kuboresha makusanyo ya mapato na madeni ya kampuni yanayotokana na huduma za simu zinazotolewa kila mwezi kwa wateja wake kupitia kampuni za kukusanya madeni (*debt collectors*);

(xli) Uboreshaji wa huduma kwa wateja kwa kuweka mifumo ya huduma kwa wateja na kupanua uwezo wa mtandao wa simu (*capacity*)(xlii) Upanuzi wa mtandao kwa kutumia teknolojia ya 4G LTE katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Mwanza, Morogoro, Kilimanjaro, Tanga, Iringa pamoja na Zanzibar;

(xliii) Kusimamia ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano Awamu ya Tatu; na,

(xliv) Kuendeleza Rasilimali Watu kwa kujenga uwezo wa kiutendaji (*Capacity Building*).

**D.4.8 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**

**111. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/2015, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

(xlv) Kufanya tathmini ya gharama za huduma za simu za mkononi.

(xlvi) Kufanya utafiti kuhusu utoaji wa huduma za intaneti na matumizi ya masafa yanayowezesha mawasiliano ya intaneti (*Broadband*).

(xlvii) Kuelimisha watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhusu sheria, haki na wajibu wa watumiaji: kuhusu mfumo mpya wa Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta; uhamaji kutoka mfumo wa utangazaji wa analojia kwenda dijitali; usajili wa laini za simu za kiganjani; haki na wajibu wa watumiaji na masuala ya tahadhari dhidi ya uhalifu kupitia mtandao;

(xlviii) Kutekeleza awamu ya kwanza na ya pili ya kituo cha kusimamia usalama wa mitandao ya mawasiliano (TZ-CERT) pamoja na kuanzisha mfumo wa kumbukumbu za simu za mkononi kwa kushauriana na watoa huduma wa simu za mkononi (CEIR);

(xlix) Kuratibu uanzishwaji wa kituo cha taifa cha uokozi na kukabiliana na majanga, ikiwa ni pamoja na kuwezesha kutumika kwa namba za kuokoa na za dharura ambazo ni 110, 115 na 118. Pia, kufuatilia utendaji wa namba 111 na 112;

(l) Kupitia upya upangaji wa masafa yatakayopatikana baada ya kuhamia utangazaji wa dijitali – masafa ya 694 MHZ hadi 790 MHZ;

(li) Kuweka kanuni za utangazaji wakati wa uchaguzi, na matangazo ya televisheni na redio na kuhimiza uendelezaji wa uandaaji wa vipindi vyenye maudhui ya Kitanzania;

(lii) Kusimamia na kuendesha mtambo wa TTMS pamoja na kusimamia matumizi ya masafa;

(liii) Kusimamia uzingatiaji wa Kanuni na masharti ya leseni;

(liv) Kuratibu tathmini ya mionzi ya mawasiliano kwenye maeneo mbalimbali na uanzishaji wa utaratibu wa kusimamia mifumo ya utendaji wa Mamlaka ili kuhakikisha ufanisi;

(lv) Kufanya utafiti kuhusu satelaiti na mifumo ya mawasiliano kwenye masafa ya 3.5 GHZ; n

(lvi) Kusimamia mfumo wa kumbukumbu, takwimu na taarifa zinazohusu mfumo wa kitaifa wa Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta.

**D.4.9 Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)**

**112. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2014/2015, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) utatekeleza mambo yafuatayo:

(vii) Kutathmini mahitaji ya huduma za mawasiliano katika maeneo yasiyo na mvuto kibiashara nchini kwa lengo la kuyajumuisha katika miradi ya Mfuko;

(lviii) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kufikisha mawasiliano ya simu katika Kata mia mbili (200) ili kuona huduma iliyokusudiwa inawafikia wananchi;

(lix) Kuunganisha shule 55 za umma kwenye mtandao wa intaneti Tanzania bara na Zanzibar;

(lx) Kuanzisha vituo vinne vya majaribio vya radio jamii (*Community Radio*);

(lxi) Kutathmini na kufikisha matangazo ya runinga ya digitali katika mikoa minne (4) mipya ambayo haijafikiwa na huduma hiyo; na

(xii) Kuanzisha Vituo vya TEHAMA katika visiwa vya Unguja na Pemba.

## E. MAAZIMIO NA MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

### E.1 MALENGO KATIKA MPANGO WA MUDA WA KATI NA MREFU

**113. *Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inaazimia kutekeleza Mpango wa Muda wa Kati na Muda Mrefu ambao umetilia mkazo katika maeneo yafuatayo:

### E.1.1 Sekta ya Mawasiliano

**114. *Mheshimiwa Spika,*** katika Sekta ya Mawasiliano, wizara imeazimia kutekeleza yafuatayo:

(i) Kuendelea na ujenzi na kuimarisha miundombinu ya TEHAMA nchini ikiwa ni pamoja na ushiriki, utekelezaji, uendeshaji na uendelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Awamu ya III ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unayojumuisha uunganishaji Zanzibar na Pemba katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, upanuzi wa Mkongo kwa baadhi ya maeneo ambayo hayakufikiwa na Awamu ya I na II, Ujenzi wa Mtandao wa IP/MPLS na Vituo Mahiri vya kutunzia kumbukumbu (*Data Centres*) katika miji ya Dar es salaam, Dodoma na Zanzibar;

(ii) Kuendelea kueneza Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kupanua matumizi yake katika maeneo mbalimbali nchini na katika nchi jirani;

(iii) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa mradi wa kuunganisha katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano vituo 200 zikiwemo shule za msingi, shule za sekondari, vyuo vya afya, vituo vya Posta pamoja na taasisi zilizoainishwa kwenye mradi wa e-Schools unaojulikana kama *Tanzania Beyond Tomorrow-TBT.*

(iv) Kuratibu zoezi la uwekaji na matumizi ya Mfumo wa Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta katika maeneo mbalimbali ya nchi;

(v) Kuendelea kupanua mtandao na kuboresha huduma za mawasiliano ya simu na intaneti nchini na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA na kuimarisha ujenzi wa vituo vya kijamii vya mawasiliano nchini;

(vi) Kutunga Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Masafa na kuandaa mfumo wa kukuza utoaji wa huduma mbalimbali kupitia kampuni nyingine za TEHAMA (*ICT-Business Process Outsourcing*);

(vii) Kutunga Sheria ya Tume ya TEHAMA;

(viii) Kuandaa Mkakati wa kuweka mtandao wenye kasi na uwezo mkubwa (*Broadband*) nchini;

(ix) Kuuanza uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Posta; na

(x) Kukamilisha uanzishaji wa Tume ya TEHAMA na kufuatilia utendaji wa taasisi za mawasiliano hususan *TTCL, UCSAF, TPC* na *TCRA;*

### E.1.2 Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

**115. *Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Sayansi Teknolojia na Ubunifu, Wizara imeazimia kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendelea na utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Mfumo wa Ubunifu Nchini (*National Innovation System Reform*);

(ii) Kuimarisha na kuboresha Taasisi za Utafiti, Sayansi na Teknolojia nchini;

(iii) Kuendelea kuimarisha mifumo, taasisi na rasilimali watu katika nyanja za utafiti, sayansi na teknolojia nchini;

(iv) Kubuni, kuandaa na kusimamia sera, mipango ya utekelezaji, miongozo, mikataba, itifaki, sheria na kanuni zinazolenga kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu nchini;

(vi) Kuimarisha uhusiano wenye tija na wadau mbalimbali katika sayansi, teknolojia na ubunifu ndani ya nchi, kikanda na kimataifa;

(vii) Kuhamasisha jamii kuhusu sayansi, teknolojia na ubunifu kwa ujumla kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii; na

lxiii) Kuratibu uendelezaji wa miundombinu na raslimali watu katika sayansi na teknolojia.

**F. SHUKRANI**

**116. *Mheshimiwa Spika,*** napenda sasa kutumia fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia na kuiwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Ni ukweli usiopingika kwamba mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2013/2014 yametokana na jitihada za pamoja, ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa washirika wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi.

**117. *Mheshimiwa Spika*,** naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa kampuni za simu za kiganjani kwa utayari wao katika kushughulikia changamoto za mawasiliano katika maeneo yasiyo na mawasiliano hapa nchini. Ninazishukuru kwa jinsi zinavyoshiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii kama vile uchangiaji wa damu salama, ujenzi wa vituo vya afya, ununuzi wa vitabu vya ziada na kiada vinavyotumika mashuleni na vyuoni, ununuzi wa madawati na ujenzi wa madarasa.

**118. *Mheshimiwa Spika*,** wizara ilinufaika na itaendelea kupokea misaada, mikopo na ushirikiano kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015. Kwa niaba ya Serikali, napenda kutoa shukrani kwa Serikali za Marekani, Sweden, Norway, Finland, Uholanzi, Japan, Italia, Afrika Kusini, Jamhuri ya Korea, Jamhuri ya Watu wa China na India. Vilevile, natoa shukrani kwa Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Exim ya Jamhuri ya Watu wa China, pamoja na taasisi na mashirika wahisani ya Umoja wa Mataifa, Jumuiya ya Madola, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki, *KOICA, UNESCO, UNCTAD, UPU na ITU.*

**G. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

**119.** ***Mheshimiwa spika,*** makadirio ya matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia katika mwaka wa fedha 2014/15 yamekadiriwa kuwa **Sh. 67,221,001,000.** Kiasi hicho cha fedha kimepangwa kutumika kama mchanganuo unavyooneshwa katika jedwali hapa chini:

**Jedwali Na.1 Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/15**

| **Na.** | **Maelezo** | | **Makadirio Ya Matumizi Ya Fedha Kwa Mwaka 2014/2015** |
|---|---|---|---|
| 1. | Mishahara | Makao Makuu | 1,622,814,000 |
| | | Taasisi | 25,215,677,000 |
| 2. | Matumizi Mengineyo *(OC)* | | 11,006,177,000 |
| | **Jumla ya Matumizi ya Kawaida** | | **37,844,668,000** |
| 3. | Fedha za Maendeleo za Ndani | | 26,000,000,000 |
| 4. | Fedha za Maendeleo za Nje | | 3,376,333,000 |
| | **Jumla ya Fedha za Maendeleo** | | **29,376,333,000** |
| | | **JUMLA KUU** | **67,221,001,000** |

***120.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kutekeleza mipango yake iliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2014/15, sasa naliomba Bunge lako tukufu lipokee, lijadili na kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Sh. 67,221,001,000** kwa mchanganuo ulioelezwa.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii inavyo viambatisho kuanzia **Na.** 1 hadi **Na.**16 vinavyotoa takwimu, vielelezo na taarifa mbalimbali zinazohusu Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho kabisa napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za Bunge pamoja na Bunge lako tukufu kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha Hotuba yangu. Hotuba hii itapatikana pia katika tovuti ya wizara ambayo ni ***www.mst.go.tz***

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Sasa nitamwita Msemaji wa Kamati ya Bunge ya Kudumu iliyohusika na suala hili, msemaji wa Kamati, Mheshimiwa Prof. Kapuya, wale

wanaohusika wawe karibu tunatumia muda. Mheshimiwa Prof. Juma Athumani Kapuya.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa mujibu wa kifungu namba 99.

**SPIKA:** Haisikiki vizuri.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA MIUNDOMBINU):** Kifungu kidogo namba 9 za kanuni ya Bunge toleo Namba 20…

**SPIKA:** Haisikiki.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo muda wangu uutunze. Kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa mujibu wa kifungu Namba 99(9) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2013 Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa ujumla kwa ushirikiano na mawasilisho mazuri yaliyofanywa na Wizara hii mbele ya Kamati kuhusu utekelezaji wa ushauri wa Kamati kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2013/2014 pamoja na Makadirio ya Mapato ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa ushauri wa Kamati uliotolewa wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2013/2014. Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2013/2014 na kuchambua utekelezaji wa ushauri na maagizo ya Kamati kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Bajeti hii ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2013/2014, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali kwa Serikali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa Serikali kupitia Wizara hii imeufanyia kazi ushauri na maagizo yaliyotolewa na Kamati isipokuwa

katika maeneo ambayo utekelezaji wake ulikwamishwa kutokana na ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa mwaka 2013/2014, Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 63,147,599,460/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 20,212,187,000/= ni kwa ajili ya Mishahara na shilingi bilioni 7,006,177,000/= kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Aidha, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 35,929,235,460/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 30,295,482,000/= ni Fedha za Ndani na shilingi bilioni 5,633,753,460/= ni Fedha za Nje. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014 Wizara imepokea jumla ya fedha za ndani za Maendeleo shilingi bilioni 3,077,025,000/= sawa na asilimia 10.15 tu ya fedha yote ya ndani iliyoidhinishiwa na Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa fedha za nje kiasi cha shilingi bilioni 1,772,127,527.52 zimepokelewa sawa na asilimia 31.45 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati. Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Mwelekeo wa Bajeti kwa Wizara hii kwa Matumizi ya Kawaida kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ni mzuri kwani Bajeti imepanda kidogo kwa ongezeko la shilingi bilioni 4,073,401,540 sawa na asilimia 6.4 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2013/2014. Kinachosikitisha ni kwamba, Bajeti kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2014/2015 imeshuka sana ambapo Wizara hii imetengewa shilingi bilioni 28,376,333,000 tu ukilinganisha na shilingi bilioni 35,929,235,460 za mwaka 2013/2014. Upungufu huu ni wa takribani shilingi bilioni 7,552,902,640 sawa na asilimia 21.02 ya kiasi kilichotengwa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Katika utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2013/2014, Kamati ilibaini kuwa kiasi ya utekelezaji wa Wizara iliathirika kutokana na ama kutotolewa kabisa kwa Bajeti iliyoidhinishwa, ama kutolewa kiasi kidogo au kutotolewa kwa wakati Fedha za Maendeleo. Tafsiri ya hali hii ni kwamba nchi yetu haiyapi kipaumbele kabisa masuala ya Sayansi na Teknolojia kama ambavyo nchi zinazoendelea. Mfano, India, Korea Kusini, Malaysia na China zinavyofanya. Kwa kuwekeza katika Sayansi na Teknolojia nchi hizo zimeweza kuinua uchumi wao kwa haraka kupitia tafiti mbalimbali za kilimo, madawa, elimu, usafirishaji, afya, nishati mawasiliano na mengineyo mengi.

Mwanasayansi aliyekuwa maarufu katika miaka ya 1970-1980 aitwaye *Carl Sagan* alisema Nanukuu: "*We live in a society absolutely dependant on science and technology and yet have cleverly arranged things so that almost no one understands science and technology. That is a clear description for*

*disaster*" mwisho wa kunukuu. Kwa tafsiri isiyo rasmi alisema tunaishi katika jamii ambayo inategemea sana sayansi na teknolojia, lakini tunafanya vitu kana kwamba kila mmoja haelewi umuhimu wa sayansi na teknolojia. Hizi ni alama tosha ya kuashiria kuingia katika janga.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu zitolewe kwa wakati ili kasi ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Wizara hii iwe kubwa na maendeleo yaweze kuonekana haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania yaani *TCRA*. Katika kuongeza ufanisi kwa mitandao yote ya mawasiliano ya simu nchini, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kufunga mtambo wa kuhakiki na kusimamia huduma za mawasiliano yaani *Telecommunication Traffic Monitoring System* pamoja na upatikanaji wa Kanuni mpya zinazohusiana na uhakiki wa mapato yatokanayo na simu zinazoingia nchini kote toka nje ya nchi yaani *TTMS Regulation 2013*.

Mheshimiwa Spika, kati ya faida za kufungwa kwa mtambo huu ni pamoja na kutoa takwimu za mawasiliano yanayofanyika ndani na nje ya nchi, kutambua mapato na miamala ya fedha mtandao yaani *mobile money transaction*, kufuatilia na kugundua mawasiliano ya ulaghai yaani *fraudulent traffic* na kutambua taarifa za laini ya simu yaani *Sim Card Profile*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa mtambo wa kuhakiki na kusimamia huduma za mawasiliano nchini, unafanya kazi kwa kushirikisha sekta binafsi kwa njia ya Kujenga, Kuendesha na Kuhamisha yaani *Build*, *Operate* and *Tranfer*. Kutokana na Sheria hii makampuni ya nje yanatakiwa kuyalipa makampuni ya ndani senti 25 za Kimarekani kwa kila dakika moja ya simu zinazopigwa hapa nchini kutoka nje. Kati ya fedha hizo, Serikali inapata senti saba (7) kwa kila dakika, watoa huduma wanapata senti kumi na tatu (13), na senti tano (5) zinatumika kwa uendeshaji ikiwa ni pamoja na kumlipa mwekezaji wa mtambo huu.

Tangu kuanzishwa kwa mtambo huu, mwezi Oktoba 2013, hadi kufikia mwezi Machi 2014, mfumo huu umeiingizia Serikali jumla ya shilingi bilioni 5.2 zilizolipwa kwa kipindi cha miezi mitatu yaani mwezi Oktoba, Novemba na Desemba.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri fedha za Mfumo wa Kuhakiki na Kusimamia Huduma za Mawasiliano yaani *Telecommunication Traffic Monitoring System* ambazo ni senti 7 za Kimarekani kwa kila dakika zinazopelekwa Serikalini kwa sasa zipelekwe kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili kusaidia

kupunguza pengo la upatikanaji wa huduma ya mawasiliano kati ya vijiijini na mijini.

Aidha, Kamati inaendelea kushauri kuwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania -*TCRA* kufanikisha zoezi la kusimamia miamala ya malipo ya fedha kupitia simu za mkononi inayofanywa na makampuni ya simu yaani *Mobile Money Transaction Monitoring*. Hii itasaidia kutambua mapato yatokanayo na miamala ya fedha mtandao yaani *Mobile Money Transaction*.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri pia, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania - *TCRA* kuendelea kusimamia na kuwa na mfumo madhubuti wa taifa kuhakikisha usalama mawasiliano ya mtandao wa kompyuta kwani hali ilivyo sasa siyo nzuri, kumekithiri wizi na utapeli katika mitandao jambo ambalo linawaathiri wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kuongezeka kwa Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano. Kamati inaipongeza Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania - TCRA kwa kuendelea kusimamia sekta ya mawasiliano kwani imeweza kuongeza idadi ya watumiaji wa huduma ya mawasiliano kutoka idadi ya laini za simu 2,963,737 mwaka 2005 hadi kufikia idadi ya laini za simu 27,450,789 Desemba, 2013.

Pia watumiaji wa mfumo wa intaneti wameongezeka kutoka 3,563,732 mwaka 2008 hadi kufikia 9,312,271 mwezi Desemba, 2013. Sambamba na hilo kumekuwa na ongezeko la huduma kupitia mawasiliano ya simu za mkononi kama vile miamala ya kifedha kwa kutumia simu za mkononi, ununuzi wa huduma au bidhaa na miamala ya kibenki inaweza kufanyika kupitia simu za mkononi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo Kamati inashauri mamlaka itoe elimu kwa wananchi watumiaji wa huduma hizi za simu kuhusu namna nzuri ya kutumia mitandao na huduma zake ili kuepukana na adha ya utapeli. Vilevile elimu itolewe kwa wananchi ili kuondoa dhana iliyojengeka miongoni mwao ya kuwa kampuni za simu wamekuwa wakiwaibia fedha zao kupitia miamala na mawasiliano wanaiyofanya kwa kutumia simu. Aidha, Serikali isimamie kikamilifu utoaji wa taarifa wakati wa usajili wa laini za simu ili kuepuka udanganyifu wakati wa usajili. Pia, serikali ihakikishe mawasiliano ya simu yanakuwa na ubora hususani katika suala la usikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta, Mradi wa Postikodi na Simbo za Posta yaani *Postal Code*. Anuani za Makazi na Simbo za Posta ni muhimu katika Maendeleo ya nchi kiuchumi, kibiashara, kisiasa na katika utoaji huduma mbalimbali za jamii. Faida za kuwa na anuani inayoeleweka zinamgusa kila mtu kuanzia Serikali na Taasisi zake, makampuni, wafanyabiashara, watoa

huduma mbalimbali za jamii kama huduma za umeme, maji, gesi, huduma za kifedha kama benki, wasambazaji wa barua na vifurushi, ulinzi na usalama wa raia, watoa huduma za dharura kama vile zimamoto na magari ya wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Wizara imekamilisha mwongozo wa uwekaji majina ya mitaa na uwekaji namba za nyumba yaani *street addressing manual* katika Mkoa wa Dar es Salaam. Kata kumi (10) zilizochaguliwa kwa ajili ya kuanza utekelezaji katika Manispaa ya Ilala ni Kata tano (5), Kinondoni Kata (3) na Temeke Kata (2). Uwekaji wa vibao vya Namba za nyumba na majina umeanza mwezi Desemba, 2013 ambapo Wizara zote na Taasisi za Serikali zilizopo Dar es Salaam tayari zimekabidhiwa vibao vyenye misimbo ya Posta na namba za Majengo yao na baadhi zimeanza matumizi ya anuani hizo mpya.

Mheshimiwa Spika, Kamati hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi huu kwani fedha zinazotolewa ni ndogo mno ukilinganisha na mahitaji pamoja na umuhimu wa mradi huu kwa Taifa. Kwa mwaka 2013/2014 pesa iliyoidhinishwa ilikuwa ni shilingi bilioni 1,000,000,000 ambazo hadi kufikia Machi, 2014 ni shilingi Milioni 300,000,000/= tu ndio zilizokuwa zimetolewa sawa na asilimia 30 ya fedha yote zilizokuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri fedha zilizoidhinishwa kwa utekelezaji wa mradi huu kwa mwaka 2013/2014 zitolewe zote kabla ya kwisha kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano – TEHAMA. Matumizi ya teknolojia katika jamii inayoendelea kama hii ya Tanzania hayaepukiki, sambamba na hilo, matumizi ya mtandao katika shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi yameongezeka ikiwemo kufanya biashara, kupata elimu, kulipia ankara mbalimbali na mengineyo. Ikizingatiwa kwamba Tekinolojia ya Habari na Mawasiliano ni moja ya mradi wa Matokeo Makubwa Sasa, yaani *Big Result Now*. Kupitia TEHAMA Wizara imefanya miradi ifuatayo:-

Moja, Mradi wa *Video Conferencing* kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha mawasiliano katika Ofisi za Serikali kwa kununua mitambo ya *video conferencing* 26 kwa ajili ya kuifunga katika Makao Makuu ya Mikoa 21 ya Tanzania Bara, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, TAMISEMI na Ofisi ya Rais Ikulu. Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia Novemba 2013, mitambo 25 ilifungwa na mafunzo ya matumizi ya mitambo hii yalitotolewa kwa wataalam, sehemu zote mitambo ilipofungwa. Aidha taratibu za kufunga mitambo katika mikoa mitano (5) ya Tanzania Visiwani pamoja na Ofisi ya Rais Ikulu zimekamilika

na inatarajiwa kufungwa kabla ya kumalizika kwa mwaka huu wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kasi iongezwe katika kutekeleza mradi huu kwani utasaidia na kurahisisha maamuzi na maelekezo katika ngazi mbalimbali za uongozi Serikalini kutolewa kupitia mtandao hivyo kuongeza ufanisi na kupunguza urasimu katika Ofisi za Serikali. Vilevile utapunguza gharama za matumizi ya karatasi yaani *paper work*.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Shule Mtandao yaani *e-schools*. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuratibu mradi wa majaribio wa shule mtandao yaani *e-schools*, ambao unatekeleza mpango wa Taifa wa kuunganisha shule *National School Connectivity Plan*. Mpaka sasa vituo arobaini na tisa (49) zimekwisha fungiwa vifaa vya TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali katika kutekeleza mradi huu isiwe na upendeleo katika uchaguzi wa shule za kufanyia majaribio ili kuwepo na uwakilishi sawa wa shule za mijini na vijijini. Kwa mfano, Wilaya ya Kaliua mkipeleka itapendeza sana.

Mheshimiwa Spika, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Kamati inatoa pongezi kwa Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia vema mradi wa mkongo wa Taifa kwa awamu ya kwanza na ya pili ambapo umeweza kuunganisha mikoa yote ya Tanzania Bara. Kukamilika kwa awamu ya kwanza na ya pili kumesaidia watoa huduma za mawasiliano kufikisha huduma kwa wananchi kwa uharaka, uhakika mkubwa na kwa gharama nafuu hivyo kuharakisha maendeleo ya Taifa.

Vilevile, kukamilika kwa awamu ya kwanza na ya pili ya Mkongo wa Taifa kumeleta mabadiliko makubwa kwa kushusha gharama na kuongeza ubora wa mawasiliano. Kwa mfano, hapo awali gharama ya kuunganisha mawasiliano kati ya Dar es Salaam na Mwanza umbali usiozidi kilometa 1000 kwa kiwango cha *2Mbps* kwa njia ya *Microwave* ilikuwa ni dola za Kimarekani 16,790 kwa mwezi. Hivi sasa bei ya kuunganisha mawasiliano kati ya Dar es Salaam na Mwanza ama kwengine kokokote nchini bila kujali umbali ni Dola za Kimarekani 160 tu kwa mwezi ambayo ni sawa punguzo la karibu asilimia 80.

Aidha, mkongo huu umeweza kuunganisha nchi zote jirani hasa zile ambazo hazipakani na bahari, nchi hizo ni kama vile Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia na Malawi. Pia mkongo umeunganisha Tanzania na Mikongo ya baharini yaani *SEACOM* na *EASSy*. Awamu ya tatu ilianza mwezi Desemba 2013 na inayotarajiwa kukamilika ndani ya miezi kumi na nane (18) ambapo Mikoa ya Unguja na Pemba itakamilika ndani ya muda huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea Ofisi za Mkongo wa Taifa mnamo mwezi Januari, 2014 ilielezwa kwamba hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2013, Mkongo umesaini Mikataba yenye thamani ya Dola 47,348,295.06 kupitia kwa wateja waliounganishwa. Baadhi ya wateja waliounganishwa ni pamoja na Makampuni ya simu ya *TTCL*, *TiGO, Zantel, Airtel, Vodacom, Simbanet na Infinity* Africa. Makampuni ya nje kumi (10) ambayo ni *MTL* (Malawi), *MTN* (Zambia), *BCS* (Kenya), *MTN, RDB*, *Rwanda Tel*, *Airtel* na *BCS* (Rwanda), *UCOM* na *ECONET* (Burundi).

Mheshimiwa Spika, bado Serikali inaweka mradi wa mkongo wa Taifa kuwa kati ya miradi ambayo ni ya kipaumbele kwa Taifa. Mpango wa Maendeleo Taifa 2014/2015. Hata hivyo, kasi ya utoaji fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu si ya kuridhisha. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 mradi uliidhinishiwa jumla shilingi bilioni 1,100,000,000 hadi kufikia Aprili, 2014 fedha iliyotolewa ni shilingi milioni 300,000,000, sawa na asilimia 27.2 ya fedha yote iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inajiuliza ikiwa sasa umebaki mwezi mmoja tu ili kumalizika kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Je, Serikali bado ina nia ya dhati ya kuendelea kuuweka ujenzi wa Mkongo wa Taifa kuwa katika vipaumbele vyake? Aidha, Kamati inashauri Serikali kuharakisha kuleta Sheria ya Usalama katika Mtandao yaani *Cyber Security Law*.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF)*. Lengo la kuanzishwa kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote yaani *Universal Communication Service Access Fund* ilikuwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya mawasiliano katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu. Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ilifanya tathmini ya mahitaji ya huduma za mawasiliano katika maeneo mbalimbali yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara.

Hata hivyo, Kamati inaona mwitikio wa watoa huduma ambao ni Makampuni ya Simu kwenda katika maeneo hayo ni mdogo mno ukilinganisha na mahitaji ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza ya mradi huu iliyotangazwa tarehe 11 Oktoba, 2012 Mfuko ulitangaza Zabuni katika Kata 152 lakini zilizopata Wawekezaji au Wazabuni ni Kata 52 tu. Awamu ya kwanza "A" iliyotangazwa tarehe 31 Julai, 2013 Mfuko ulitangaza Zabuni katika Kata168 lakini ni Kata 77 tu zilizopata Wazabuni. Awamu ya kwanza "B" ya Mradi huu iliyotangazwa tarehe 4 Desemba, 2013 Mfuko ulitangaza Zabuni katika Kata 124, lakini zilizopata

Wazabuni ni Kata 86 tu. Hali hii inasababisha kupungua kasi na kutokamilika kwa haraka kwa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeanza kutekeleza Mfumo wa Kuhakiki na Kusimamia Huduma za Mawasiliano yaani *Telecommunication Traffic Monitoring System*. Na kwa kuwa kutokana na Sheria hii Makampuni ya simu ya nje yanatakiwa kuyalipa Makampuni ya ndani senti 25 za kimarekani kwa kila dakika moja ya simu zinazopigwa hapa nchini kutoka nje na Serikali kupata senti 7 kwa kila dakika. Na kwa kuwa tangu mfumo huu ulipoanzishwa mwezi Oktoba, 2013 hadi mwezi Machi, 2014, Mradi huu umeiingizia Serikali shilingi bilioni 5.2 zilizolipwa kwa kipindi cha miezi mitatu tu.

Kamati inaona kuwa kama kipindi cha miezi mitatu tu zimeweza kupatikana shilingi bilioni 5.2 zilizoelekezwa Serikalini, fedha hizo zingeweza kujenga takribani minara 31 ambapo inakadiriwa bei ya ujenzi wa mnara mmoja kuwa ni shilingi milioni 166. Minara hii baada ya kujengwa itakodishwa kwa watoa huduma na fedha itakayopatikana itatumika kuendeleza ujenzi wa minara kwenye maeneo mengine kama vile Kata ya Mwongozo, Kata ya Ichemba, Ilindwanoni, Sasu na maeneo mengine. *(Makofi)*

Hivyo, Kamati inashauri fedha za Mfumo wa Kuhakiki na Kusimamia Huduma za Mawasiliano ambazo zinagawiwa Serikali zipelekwe kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili kuharakisha upatikanaji wa mawasiliano Vijijini na katika maeneo yenye Mawasiliano hafifu. Aidha, Serikali iendelee kushirikisha na kushawishi makampuni ya simu ili yapeleke mawasiliano katika maeneo yalioainishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL)*. Kampuni ya Simu Tanzania inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 65 na asilimia 35 inamilikiwa na mmiliki mwenza *Bharti*. Kampuni hii kwa sasa inakabiliwa na hali ngumu ya kifedha na uwezo mdogo wa kukabiliana na ushindani katika soko. Hii imetokana na mbia mwenza *Bharti Airtel* kushindwa kuwekeza katika Kampuni kwa muda mrefu. Ili kuinusuru Kampuni hii, Taasisi mbalimbali za fedha zimeweka masharti ya kuikopesha *TTCL* kwa sharti la Serikali kutoa dhamana kwa asilimia mia moja (100). Serikali imeonesha nia ya kuidhamini *TTCL* ili mradi mbia mwenza ambaye ni *Bharti Airtel* aondoke.

Kwa kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2014 pande zote mbili zimekamilisha zoezi la uthamini. Kamati inashauri kuharakishwa kuondolewa kwa mmiliki mwenza wa *TTCL* yaani *Bharti Airtel* ili Serikali iweze kuidhamini *TTCL* kwa asilimia 100 jambo litakalowezesha Taasisi zingine za fedha kuikopesha *TTCL*.

Changamoto nyingine kubwa inayoikabili *TTCL* ni madeni ambayo kwa kiasi kikubwa yanaathiri ufanisi wake. Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL)* imekuwa ikizidai Taasisi nyingi za Serikali madeni ambayo ni malimbikizo ya muda mrefu. Katika taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati ilieleza kuwa hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2014 *TTCL* inazidai Wizara na Taasisi za Serikali kiasi cha shilingi billion 2,431,040,809.37/= na dola za kimarekani 1,488,153.38. Vilevile, *TTCL* imekuwa ikidaiwa madeni mengi na Taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za kiserikali ambapo jumla ya madeni yote inayodaiwa ni shilingi bilioni 105, 237,881,863.02/=.

**SPIKA:** Tunaendelea lakini kwa nini wengine mnafanya kazi kama mko nje? Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti endelea!

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL)* na Wizara ya Fedha zishirikiane kwa karibu na kuhakikisha madeni yote yanakusanywa. Wizara ya Fedha ilipe madeni hayo kwa kukata moja kwa moja kwenye *OC* za Wizara na Taasisi zinazodaiwa kwani ni aibu kuona wadaiwa sugu wa *TTCL* ni Wizara na Mashirika ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (*MUST)*. Taasisi zinazotoa mafunzo zimekuwa zikiongeza wanafunzi kulingana na matakwa ya kitaifa katika fani mbalimbali huku Bajeti za Taasisi husika zikiendelea kushuka na kutokutolewa kwa wakati. Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kilianzishwa kwa madhumuni ya kuziba pengo la soko la ajira katika nafasi za wanasayansi, mafundi sanifu, pamoja na wahandisi ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia. Pamoja na umuhimu wa Chuo hiki kwa Taifa, bado ni vigumu kwa Chuo hiki kufikia hadhi ya Chuo Kikuu kutokana na ufinyu wa Bajeti itolewayo kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Bajeti ya fedha za Maendeleo iliyoidhinishiwa chuo hiki ilikuwa ni shilingi bilioni 2,500,000,000 ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2014 ni shilingi milioni 543,637,500 tu ndizo fedha zilizotolewa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri ili kukipa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia uwezo na hadhi ya Chuo Kikuu, Serikali itenge Bajeti inayoendana na ongezeko la wanafunzi katika chuo hiki na kukiepusha na madeni yanayotokana na huduma mbalimbali kutoka kwa wazabuni. Pia, Kamati inashauri fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya chuo hiki pamoja na ufinyu wake zitolewe kwa wakati ziweze kusaidia utekelezaji wa Miradi na Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela. Madhumuni ya kuanzisha kwa Taasisi ya Nelson Mandela ni kuzalisha wataalam waliobobea katika nyanja mbalimbali za sayansi na teknolojia ikiwa ni pamoja na watafiti kwa lengo la kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi yetu na kuleta maendeleo kwa ujumla.

Ni dhahiri kuwa maendeleo ya kiuchumi duniani yanapatikana kwa kutumia sayansi na teknolojia inayoibuliwa baada ya kufanya tafiti mbalimbali. Taasisi ya Nelson Mandela imeanzishwa kwa ajili kutoa mafunzo ya aina hii kwa nchi yetu na Afrika kwa ujumla.

Hata hivyo, inaelekea kuwa dira ya Taasisi hii haiwezi kufikiwa kutokana na Bajeti ndogo inayotengwa. Kwa mfano mwaka wa fedha wa 2013/2014 Taasisi ilipangiwa jumla ya shilingi bilioni 4,500,000,000 kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Hata hivyo, hadi kufikia Aprili, 2014 fedha iliyokuwa imetolewa ni shilingi milioni 300,000,000 tu. Aidha, mwaka 2014/2015 Bajeti ya Maendeleo iliyopangwa kwa ajili ya Taasisi hii imeshuka hadi kufikia shilingi bilioni 1,500,000,000.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia utoaji huu wa fedha, Kamati inajiuliza. Je, Serikali ina nia ya kuifanya Taasisi hii kufikia dira yake ya kuwa miongoni mwa Taasisi Bora ya Elimu ya Juu Duniani?

**SPIKA:** Jamani tunaomba utulivu!

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA MIUNDOMBINU):** *(Centre of Excellency)*. Kamati inaishauri Serikali iazimie kuiboresha Taasisi hii kwa kuiongezea Bajeti ya Maendeleo ili iweze kutimiza malengo ya kuanzishwa kwake, vinginevyo itakuwa haina tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam kimsingi inalo jukumu la kutoa mafunzo ya uhandisi na teknolojia hapa nchini. Taasisi hii imepata mafanikio mbalimbali na hasa ikizingatiwa kuwa ni taasisi ya kwanza kupata ithibati ya Baraza la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* mwaka 2005. Changamoto kubwa inayoikabili Taasisi hii ni fedha, ambapo katika mwaka wa fedha 2013/2014, Taasisi hii ilitengewa shilingi bilioni 2,500,000,000, hadi kufikia mwezi Aprili, 2014 ilikuwa imepata jumla ya Sh.843,637,500 tu. Aidha, changamoto zingine ni upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kununulia chakula cha wanafunzi na fedha za mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi kwa kuwa zote hizi pia hutegemea Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili Taasisi hii iweze kuendelea kuimarika katika utoaji wa elimu nchini, Kamati inashauri, Taasisi hii nayo ipewe *Skills Development Levy* kama inavyopewa *VETA*.

Vilevile, Kamati inashauri Taasisi za Elimu ya Juu na Vyuo Vikuu vipewe uhuru wa kutafuta wafanyakazi na Walimu wa vyuo hivyo wenyewe kwani kuingizwa kwenye ajira ya pamoja ya Wizara ya Utumishi inachelewesha, inapotosha na wakati mwingine kuajiri watu wasiofaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)*. Kamati inaipongeza Tume ya Sayansi na Teknolojia kwa ubunifu wa kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha ambavyo vimeisaidia kujiendesha mpaka sasa. Kamati imekuwa ikisikitishwa na fedha zinazotengwa kwa ajili ya utafiti na maendeleo kuwa ni kidogo ukilinganisha na umuhimu wa utafiti na sayansi katika jamii yetu. Hata hivyo, pamoja na fedha hizo kuwa ndogo, pia hazitolewi kwa wakati jambo linalosababisha Tume ya Sayansi na Teknolojia kuchelewa kutekeleza majukumu yake.

Jedwali linaloonyesha mtiririko wa Bajeti ya Tume ya Sayansi na Teknolojia kwa miaka mitano mfululizo:-

| **MWAKA** | **FEDHA ILIYOIDHINISHWA** | **FEDHA ILIYOTOLEWA** |
|---|---|---|
| 2010/2011 | Bilioni 30 | Bilioni 19 |
| 2011/2012 | Bilioni 25.7 | Bilioni 7.3 |
| 2012/2013 | Bilioni 21.4 | Bilioni 12.8 |
| 2013/2014 | Bilioni 16.4 | Hakuna fedha iliyotolewa |

Aidha, katika bajeti ya mwaka 2014/2015 kiasi cha fedha kilichotengwa kimezidi kushuka hadi kufikia Sh.14,000,000,000.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa inajiuliza, kwa utengaji na kasi ya utoaji huu wa fedha ni kweli tutafikia asilimia moja (1) ya Pato Ghafi la Taifa lililokusudiwa? Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kabla ya kuisha kwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014, ili Tume hii iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Nguvu za *Atomic*. Tume hii sasa ina mpango wa kujenga maabara ya kuhifadhi mabaki au makapi yanayobaki baada ya madini yenye mionzi ktumiwa. Kwa hali ya Taasisi yetu ilivyo sasa, kama hili litafanikiwa, tunayo nafasi ya pekee katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati, upekee huu unaweza kutupa nafasi ya hata taasisi hii kujiingizia fedha kutumia maabara hii. Kinyume chake tunatengeneza mazingira ambayo ni

hatari sana kwa maisha ya binadamu hasa akina mama wajawazito na hata mifugo na mimea. Kamati inashauri umuhimu wa maabara hii uzingatiwe na wapewe fedha za kutosha ili kukamilisha ujenzi huu mapema.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mipango hii mizuri, Tume hii ina changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha. Hadi Kamati ilipokutana mwezi Mei, 2014 ambapo umebakia mwezi mmoja tu kumalizika, kati ya Sh.1,000,000,000 iliyokuwa imeidhinishwa kwa Tume ya Nguvu za Atomic, hakuna fedha yoyote iliyotolewa. Kamati inashauri kuzingatia umuhimu wa taasisi hii na majukumu yake na ni muhimu fedha hizi zitolewe kabla ya mwaka huu wa fedha kumalizika.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka wa Fedha 2014/2015. Katika Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia imeomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.67,221,001,000/=. Shilingi 37,844,668,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yaani Mishahara na Matumizi Mengineyo. Ambapo kati yake Sh.26,828,491,000 ni kwa ajili ya mishahara na Sh.11,006,177,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia imetengewa jumla ya Sh.28,376,333,000/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kati ya hizo Sh.26,000,000,000/= ni fedha za ndani na Sh.3,376,333,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii kifungu kwa kifungu na sasa inaliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha maombi hayo yenye jumla ya Sh.67,221,001,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, nawashukuru pia Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Naibu Waziri, Profesa Patrick Makungu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; pamoja na Wataalam wote wa Wizara hii na Taasisi zilizo chini yake kwa ushirikiano wao ambao walikuwa wametupa Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao, hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini mkubwa, majina yao yatatokea katika *Hansard.*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nachukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dokta Thomas Kashilillah, Katibu wa Kamati Ndugu Hosiana John na Ndugu Francisca Haule kwa kuihudumia Kamati na kufanikisha maandalizi ya Taarifa hii. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya pekee naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Waziri Hawa Ghasia, Waziri Celina Kombani kwa kumshauri vizuri Mheshimiwa Waziri Mkuu ili kumshauri Rais kutupatia Wilaya mpya ya Kaliuwa na Halmashauri ambavyo sasa vyote vimekwishaanza.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu naomba niwashukuru sana viongozi wa Wilaya ya Urambo, Halmashauri kupitia Mwenyekiti wake, Mbunge wao Mheshimiwa Samuel Sitta na wananchi wa Urambo kwa kukubali Wilaya ya Kaliuwa kuzaliwa na kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kuwasahau wananchi wa Wilaya ya Kaliuwa, nawashukuru kwa ushirikiano wanaonipa na kwa majukumu tunayotekeleza pamoja kuongeza kasi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya na mengine yamechomekewa. *(Kicheko)*

**Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu Kuhusu Makadirio ya Mapato na Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Wayansi na Teknolojia kwa mwaka wa Fedha 2014/2014 kama ilivyowasilishwa Mezani**

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KWA MWAKA WA FEDHA WA**
**2013/2014; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA**
**MWAKA WA FEDHA WA 2014/2015**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa Mujibu wa kifungu Na 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013 kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa ujumla kwa ushirikiano na mawasilisho mazuri yaliyofanywa na Wizara hii mbele ya Kamati kuhusu utekelezaji wa ushauri wa Kamati kwa kazi zilizopangwa kufanyika katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI ULIOTOLEWA WAKATI WA KUJADILI BAJETI YA WIZARA HII KWA MWAKA 2013/2014

**Mheshimiwa Spika.** Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Tekinolojia kwa mwaka 2013/2014 na kuchambua utekelezaji wa ushauri na maagizo ya Kamati kwa kipindi hicho.

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa kupitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali kwa Serikali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa, Serikali imefanyia kazi ushauri na maagizo yaliyotolewa na Kamati, isipokuwa katika maeneo ambayo utekelezaji wake ulikwamishwa kutokana na ukosefu wa fedha.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI YA MWAKA 2013/2014

### 3.1 Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 Wizara iliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 63,147,599,460** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 20,212,187,000** ni kwa ajili ya Mishahara na **shilingi bilioni 7,006,177,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Aidha, Wizara iliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 35, 929,235, 460/=** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 30,295,482,000/=** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 5, 633,753,460/=** ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014 Wizara imepokea jumla ya fedha za ndani za Maendeleo **shilingi bilioni**

**3,077,025,000** sawa na **asilimia 10.15** ya fedha yote ya ndani iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa fedha za nje kiasi cha **shilingi bilioni 1,772,127,527.52** zilitolewa sawa na **asilimia 31.45** ya fedha za nje zilizoidhinishwa.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Tekinolojia

**Mheshimiwa Spika,** mwelekeo wa bajeti kwa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ni mzuri kwani bajeti imepanda kidogo kwa ongezeko la **shilingi bilioni 4,073,401,540** sawa na **asilimia 6.4** ukilinganisha na mwaka wa fedha 2013/2014. Aidha, bajeti kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2014/2015 imeshuka sana ambapo Wizara hii imetengewa **shilingi bilioni 28,376,333,000** tu ukilinganisha na **shilingi bilioni 35,929,235,460** za mwaka 2013/2014. Upungufu huu ni wa takribani **shilingi bilioni 7,552,902,640** sawa na **asilimia 21.02** ya kiasi kilichotengwa 2013/2014.

**Mheshimiwa Spika**, Katika utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2013/2014, Kamati ilibaini kuwa kasi ya utekelezaji wa Wizara iliathirika kutokana na ama kutotolewa kabisa kwa bajeti iliyoidhinishwa, ama kutolewa kiasi kidogo au kutotolewa kwa wakati fedha za maendeleo.

Tafsiri ya hali hii ni kwamba nchi yetu haiyapi kipaumbele kabisa masuala ya sayansi na teknolojia kama ambavyo nchi zinazoendelea mfano, India, Korea Kusini, Malaysia na China zinavyofanya. Kwa kuwekeza katika sayansi na teknolojia nchi hizo zimeweza kuinua uchumi kupitia tafiti mbalimbali za kilimo, madawa, elimu, usafirishaji, afya, nishati mawasiliano na mengine mengi.

Mwanasayansi aliyekuwa maarufu katika miaka ya 1970-1980 aitwaye ***Carl Sagan*** alisema Nanukuu "***we live in a society absolutely dependant on science and technology and yet have cleverly arranged things so that almost no one understands science and technology. That is a clear description for disaster"*** mwisho wa kunukuu. Kwa tafsiri isiyo rasmi alisema "tunaishi katika jamii ambayo inategemea sana sayansi na teknolojia, lakini tunafanya vitu kana kwamba kila mmoja haelewi umuhimu wa sayansi na teknolojia. Haya ni maelezo tosha ya kuashiria kuingia katika janga"

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasisitiza fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu zitolewe kwa wakati ili kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iwe kubwa na maendeleo yaweze kuonekana kwa haraka zaidi.

### 4.2 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

**Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza ufanisi kwa mitandao yote ya mawasiliano ya simu nchini, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Mawasiliano

Tanzania kwa kufunga mtambo wa kuhakiki na kusimamia huduma za mawasiliano (*Telecommunication Traffic Monitoring System*) pamoja na upatikanaji wa kanuni mpya zinazohusiana na uhakiki wa mapato yatokanayo na simu zinazoingia nchini toka nje ya nchi (TTMS Regulation 2013).

**Mheshimiwa Spika**, kati ya faida za kufungwa kwa mtambo huu ni pamoja na kutoa takwimu za mawasiliano yanayofanyika ndani na nje ya nchi, kutambua mapato na miamala ya fedha mtandao (*mobile money transaction*), kufuatilia na kugundua mawasiliano ya ulaghai (*fraudulent traffic*) na kutambua taarifa za laini ya simu (*Sim Card profile*) na za kifaa cha mawasiliano (*terminal equipment identification details*)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa mtambo wa kuhakiki na kusimamia huduma za mawasiliano nchini, unafanya kazi kwa kushirikisha sekta binafsi kwa njia ya Kujenga, Kuendesha na Kuhamisha (*Build*, *Operate* and *Tranfer*). Kutokana na Sheria hii makampuni ya nje yanatakiwa kuyalipa makampuni ya ndani **senti 25 za Kimarekani** kwa kila dakika moja ya simu zinazopigwa hapa nchini kutoka nje. Kati ya fedha hizo, **Serikali inapata senti saba (7) kwa kila dakika, watoa huduma wanapata senti kumi na tatu (13), na senti tano (5) zinatumika kwa uendeshaji wa mitambo** ikiwa ni pamoja na kumlipa mwekezaji wa mtambo huu.

Tangu kuanzishwa kwa mtambo huu, mwezi Oktoba 2013, hadi kufikia mwezi Machi 2014, mfumo huu umeiingizia Serikali jumla ya **shilingi bilioni 5.2** zilizolipwa kwa kipindi cha miezi mitatu yaani mwezi Oktoba, Novemba na Desemba. Kwa kiasi kikubwa mfumo huu umesaidia kupunguza kasi ya udanganyifu kuhusu simu zinazoingia nchini kwa lengo la kuongeza makusanyo ya mapato.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri fedha za Mfumo wa Kuhakiki na Kusimamia Huduma za Mawasiliano (*Telecommunication Traffic Monitoring System*) ambazo ni senti 7 za Kimarekani kwa kila dakika zinazopelekwa Serikalini kwa sasa zipelekwe kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili kusaidia kupunguza pengo la upatikanaji wa huduma ya mawasiliano kati ya vijiijini na mijini hatimae kufikia kwa haraka malengo yaliyowekwa na Serikali.

Aidha, Kamati inaendelea kushauri kuwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kufanikisha zoezi la kusimamia miamala ya malipo ya fedha kupitia simu za mkononi inayofanywa na makampuni ya simu (*Mobile Money Transaction Monitoring*). Hii itasaidia kutambua mapato yatokanayo na miamala ya fedha mtandao (*Mobile Money Transaction*).

Vilevile, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuendelea kusimamia na kuwa na mfumo madhubuti wa taifa kuhakikisha usalama mawasiliano ya mtandao wa kompyuta kwani hali ilivyo sasa kumekithiri wizi na utapeli katika mitandao jambo ambalo linawaathiri wananchi.

### 4.2.1 Kuongezeka kwa Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kuendelea kusimamia sekta ya mawasiliano kwani imeweza kuongeza idadi ya watumiaji wa huduma ya mawasiliano kutoka idadi ya laini za simu 2,963,737 mwaka 2005 hadi kufikia idadi ya laini za simu 27,450,789 Desemba, 2013. Pia watumiaji wa mfumo wa intaneti wameongezeka kutoka 3,563,732 mwaka 2008 hadi kufikia 9,312,271 mwezi Desemba, 2013. Sambamba na hilo kumekuwa na ongezeko la huduma kupitia mawasiliano ya simu za mkononi kama vile miamala ya kifedha kwa kutumia simu za mkononi, ununuzi wa huduma au bidhaa na miamala ya kibenki inaweza kufanyika kupitia simu za mkononi.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio hayo kamati inashauri mamlaka itoe elimu kwa wananchi watumiaji wa huduma hizi za simu kuhusu namna nzuri ya kutumia mitandao na huduma zake ili kuepukana na adha ya utapeli.

Vilevile elimu itolewe kwa wananchi ili kuondoa dhana iliyojengeka miongoni mwao ya kuwa kampuni za simu wamekuwa wakiwaibia fedha zao kupitia miamala na mawasiliano wanaiyofanya kwa kutumia simu.

Aidha, Serikali isimamie kikamilifu utoaji wa taarifa wakati wa usajili wa laini za simu ili kuepuka udanganyifu wakati wa usajili. Pia serikali ihakikishe mawasiliano ya simu yanakuwa na ubora hususani katika suala la usikivu.

### 4.3 Shirika la Posta, Mradi wa Postikodi na Simbo za Posta (*Postal Code*)

**Mheshimiwa Spika,** Anuani za Makazi na Simbo za Posta ni muhimu katika maendeleo ya nchi kiuchumi, kibiashara, kisiasa na katika utoaji huduma mbalimbali za jamii. Faida za kuwa na anuani zinamgusa kila mtu kuanzia Serikali na taasisi zake, makampuni, wafanyabiashara, watoa huduma mbalimbali za jamii kama huduma za umeme, maji, gesi, huduma za kifedha kama benki, wasambazaji wa barua na vifurushi, ulinzi na usalama wa raia, watoa huduma za dharura kama vile zimamoto na magari ya wagonjwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Wizara imekamilisha mwongozo wa uwekaji majina ya mitaa na uwekaji namba za nyumba (*street addressing manual*) katika Mkoa wa Dar es Salaam. Kata kumi (10) zilizochaguliwa kwa ajili ya kuanza utekelezaji katika manispaa ya Ilala ni kata tano (5), Kinondoni kata

(3) na Temeke kata (2). Uwekaji wa vibao vya namba za nyumba na majina umeanza mwezi Desemba, 2013 ambapo Wizara zote na Taasisi za Serikali zilizopo Dar es Salaam tayari zimekabidhiwa vibao vyenye misimbo ya Posta na namba za Majengo yao na baadhi zimeanza matumizi ya anuani hizo mpya.

**Mheshimiwa Spika,** kamati hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi huu kwani fedha zinazotolewa ni ndogo mno ukilinganisha na mahitaji pamoja na umuhimu wa mradi huu kwa Taifa. Kwa mwaka 2013/2014 pesa iliyoidhinishwa ilikuwa ni **shilingi bilioni 1,000,000,000** ambazo hadi kufikia Machi, 2014 ni **shilingi Milioni 300,000,000/=** tu ndio zilizokuwa zimetolewa sawa na **asilimia 30** ya fedha yote zilizokuwa zimetolewa.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inashauri fedha zilizoidhinishwa kwa utekelezaji wa mradi huu kwa mwaka 2013/2014 zitolewe zote kabla ya kuisha kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

### 4.4 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano -TEHAMA

**Mheshimiwa Spika,** matumizi ya teknolojia katika jamii inayoendelea kama hii ya Tanzania hayaepukiki, sambamba na hilo, matumizi ya mtandao katika shughuli mbalimbali za kijamii na uchumi yameongezeka ikiwemo kufanya biashara, kupata elimu, kulipia ankara mbalimbali na mengineyo hufanyika kwa njia hii ya mtandao. Ikizingatiwa kwamba Tekinolojia ya Habari na Mawasiliano ni moja ya mradi wa Matokeo Makubwa Sasa (Big Result Now), kupitia TEHAMA Wizara imefanya miradi ifuatayo:-

#### 4.4.1. Mradi wa Video Conferencing kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha mawasiliano katika Ofisi za Serikali kwa kununua mitambo ya "*video conferencing*" 26 kwa ajili ya kuifunga katika Makao Makuu ya Mikoa 21 ya Tanzania Bara, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, TAMISEMI na Ofisi ya Rais Ikulu. Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia Novemba 2013, mitambo 25 ilifungwa, na mafunzo ya matumizi ya mitambo hii yalitotolewa kwa wataalamu sehemu zote mitambo ilipofungwa. Aidha taratibu za kufunga mitambo katika mikoa mitano (5) ya Tanzania Visiwani pamoja na Ofisi ya Rais Ikulu zimekamilika na inatarajiwa kufungwa kabla ya kumalizika kwa mwaka wa Fedha 2013/2014.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kasi iongezwe katika kutekeleza mradi huu kwani utasaidia na kurahisisha maamuzi na maelekezo katika ngazi mbalimbali za uongozi Serikalini kutolewa kupitia mtandao hivyo kuongeza

ufanisi na kupunguza urasimu katika Ofisi za Serikali. Vilevile utapunguza gharama za matumizi ya karatasi (*paper work*).

### 4.4.2. Mradi wa Shule Mtandao (e-schools).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa kuratibu mradi wa majaribio wa shule mtandao (*E - Schools*), ambao unatekeleza mpango wa Taifa wa kuunganisha shule (*National School Connectivity Plan*). Mpaka sasa vituo arobaini na tisa (49) zimekwisha fungiwa vifaa vya TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika**, kamati inaishauri Serikali katika kutekeleza mradi huu isiwe na upendeleo katika chaguzi wa shule za kufanyia majaribio ili kuwepo na uwakilishi sawa wa shule za mijini na vijijini.

### 4.5. Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa pongezi kwa Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia vema mradi wa mkongo wa Taifa kwa awamu ya kwanza na ya pili ambapo umeweza kuunganisha mikoa yote ya Tanzania bara. Kukamilika kwa awamu ya kwanza na ya pili kumesaidia watoa huduma za mawasiliano kufikisha huduma kwa wananchi kwa uharaka, uhakika mkubwa na kwa gharama nafuu hivyo kuharakisha maendeleo ya Taifa. Vilevile, kukamilika kwa awamu ya kwanza na ya pili ya Mkongo wa Taifa kumeleta mabadiliko makubwa kwa kushusha gharama na kuongeza ubora wa mawasiliano. Kwa mfano, hapo awali gharama ya kuunganisha mawasiliano kati ya Dar es Salaam na Mwanza (umbali usiozidi kilometa 1000) kwa kiwango cha 2Mbps kwa njia ya "Microwave" ilikuwa ni dola za Kimarekani 16,790 kwa mwezi. Hivi sasa bei ya kuunganisha mawasiliano kati ya Dar es Salaam na Mwanza ama kwengine o kokote nchini bila kujali umbali ni Dola za Kimarekani 160 tu kwa mwezi ambayo ni sawa punguzo la karibu asilimia 80. Aidha, mkongo huu umeweza kuunganisha nchi zote jirani hasa zile ambazo hazipakani na bahari, nchi hizo ni pamoja na Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia na Malawi. Pia mkongo umeunganisha Tanzania na Mikongo ya baharini yaani SEACOM na EASSy. Awamu ya tatu ilianza mwezi Desemba 2013 na inayotarajiwa kukamilika ndani ya miezi kumi na nane (18) ambapo Mikoa ya Unguja na Pemba itakamilika ndani ya muda huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipotembelea Ofisi za Mkongo wa Taifa mnamo mwezi Januari, 2014 ilielezwa kwamba hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2013, Mkongo umesaini Mikataba yenye thamani ya **Dola 47,348,295.06** kupitia kwa wateja waliounganishwa. Baadhi ya wateja waliounganishwa ni pamoja na Makampuni ya simu ya *TTCL*, *TiGO, Zantel, Airtel, Vodacom, Simbanet, na Infinity* Africa. Makampuni ya nje kumi (10) ambayo ni *MTL* (Malawi), *MTN*

(Zambia), *BCS* (Kenya), *MTN, RDB*, *RwandaTel*, *Airtel* na *BCS* (Rwanda), *UCOM* na *ECONET* (Burundi).

**Mheshimiwa Spika**, bado Serikali inaweka mradi wa mkongo wa Taifa kuwa kati ya miradi ambayo ni ya kipaumbele kwa Taifa (Mpango wa Maendeleo Taifa 2014/2015). Hata hivyo, kasi ya utoaji fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu si ya kuridhisha. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 mradi uliidhinishiwa jumla **shilingi bilioni 1,100,000,000** hadi kufikia Aprili, 2014 fedha iliyotolewa ni **shilingi milioni 300,000,000**, sawa na **asilimia 27.2** ya fedha yote iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inajiuliza ikiwa sasa umebaki mwezi mmoja tu ili kumalizika kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, je Serikali bado ina nia ya dhati ya kuendelea kuuweka ujenzi wa Mkongo wa Taifa kuwa katika vipaumbele vyake? Aidha, Kamati inashauri Serikali kuharakisha kuleta Sheria ya Usalama katika Mtandao (*Cyber Security Law*). Pia, elimu kwa wananchi iendelee kutolewa ili waweze kujua namna nzuri ya kutumia mtandao ili kuepuka utapeli ambao kwa sasa umekithiri katika mitandao.

**4.6. Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)**

**Mheshimiwa Spika**, lengo kuanzishwa kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*Universal Communication Service Access Fund)* ilikuwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya mawasiliano katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu. Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ilifanya tathmini ya mahitaji ya huduma za mawasiliano katika maeneo mbalimbali yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara. Hata hivyo, Kamati inaona muitikio wa watoa huduma ambao ni Makampuni ya Simu kwenda katika maeneo hayo ni mdogo mno ukilinganisha na mahitaji ya mawasiliano.

**Mheshimiwa Spika**, katika awamu ya kwanza ya mradi huu iliyotangazwa tarehe 11 Oktoba, 2012 Mfuko ulitangaza Zabuni katika **Kata 152** lakini zilizopata Wazabuni ni **Kata 52** tu. Awamu ya kwanza **"A"** iliyotangazwa tarehe 31 Julai, 2013 Mfuko ulitangaza Zabuni katika **Kata168** lakini ni **Kata 77** tu zilizopata Wazabuni. Awamu ya kwanza **"B"** ya Mradi huu iliyotangazwa tarehe 04 Disemba, 2013 Mfuko ulitangaza Zabuni katika **Kata 124,** lakini zilizopata Wazabuni ni **Kata 86** tu. Hali hii inasababisha kupungua kasi na kutokamilika kwa haraka kwa mradi huu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeanza kutekeleza Mfumo wa Kuhakiki na Kusimamia Huduma za Mawasiliano (*Telecommunication Traffic Monitoring System*). Na kwa kuwa kutokana na Sheria hii Makampuni ya simu ya nje yanatakiwa kuyalipa Makampuni ya ndani **senti 25 za kimarekani** kwa kila dakika moja ya simu

zinazopigwa hapa nchini kutoka nje, na Serikali kupata **senti 7** kwa kila dakika**.** Na kwa kuwa tangu mfumo huu ulipoanzishwa mwezi Oktoba, 2013 hadi mwezi Machi, 2014, Mradi huu umeiingizia Serikali **shilingi bilioni 5.2** zilizolipwa kwa kipindi cha miezi mitatu. Kamati inaona kuwa kama kipindi cha miezi mitatu tu zimeweza kupatikana **shilingi bilioni 5.2** zilizoelekezwa Serikalini, fedha hizo zingeweza kujenga takribani **minara 31** ambapo inakadiriwa bei ya ujenzi wa mnara mmoja kuwa ni **shilingi milioni 166.** Minara hii baada ya kujengwa itakodishwa kwa watoa huduma na fedha itakayopatikana itatumika kuendeleza ujenzi wa minara kwenye maeneo mengine yenye uhitaji. Hivyo, Kamati inashauri fedha za Mfumo wa Kuhakiki na Kusimamia Huduma za Mawasiliano (*Telecommunication Traffic Monitoring System*) ambazo zinagawiwa Serikali zipelekwe kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili kuharakisha upatikanaji wa mawasiliano vijijini na katika maeneo yenye mawasiliano hafifu. Aidha, Serikali iendelee kushirikisha na kushawishi makampuni ya simu ili yapeleke mawasiliano katika maeneo yalioainishwa.

**4.7 Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)**

**Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Simu Tanzania inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 65 na asilimia 35 inamilikiwa na mmiliki mwenza *Bharti Airtel*. Kampuni hii kwa sasa inakabiliwa na hali ngumu ya kifedha na uwezo mdogo wa kukabiliana na ushindani katika soko. Hii imetokana na mbia mwenza *Bharti Airtel* kushindwa kuwekeza katika Kampuni kwa muda mrefu. Ili kuinusuru Kampuni hii, taasisi mbalimbali za fedha zimeweka masharti ya kuikopesha TTCL kwa sharti la Serikali kutoa dhamana kwa asilimia mia moja (100). Serikali imeonesha nia ya kuidhamini TTCL ilimradi mbia mwenza ambae ni *Bharti Airtel* aondoke. Kamati ilijulishwa kwamba suala hili limefikia hatua nzuri baada ya kufanyika vikao viwili vya majadiliano kati ya Serikali kupitia kamati za majadiliano ya Serikali (*Government Negotiating Team- GNT*) na wawakilishi wa *Bhart Airtel*. Hadi kufikia mwezi Februari 2014 pande zote mbii zimekamilisha zoezi la uthamini.

Kamati inaendelea kushauri kuharakishwa kuondolewa kwa mmiliki mwenza wa TTCL yaani Bharti Airtel ili Serikali iweze kuidhamini TTCL kwa asilimia 100 jambo litakalowezesha taasisi zingine za fedha kuikopesha TTCL.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine kubwa inayoikabili TTCL ni madeni ambayo kwa kiasi kikubwa yanaathiri ufanisi wake. Kampuni ya Simu Tanzania -TTCL imekuwa ikizidai taasisi nyingi za Serikali madeni ambayo ni malimbikizo ya mda mrefu. Katika taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati ilieleza kuwa hadi kufikia tarehe 28 February, 2014, TTCL inazidai Wizara na Taasisi za Serikali kiasi cha **shilingi billion 2,431,040,809.37/=** na **dola za kimarekani 1,488,153.38.** Vilevile, TTCL i mekuwa ikidaiwa madeni mengi na Taasisi

mbalimbali za Serikali na zisizo za kiserikali ambapo jumla ya madeni yote inayodaiwa ni **shilingi bilioni 105, 237,881,863.02/=**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Kampuni ya Simu Tanzania- TTCL na Wizara ya Fedha zishirikiane kwa karibu na kuhakikisha madeni yote yanakusanywa. Wizara ya Fedha ilipe madeni hayo kwa kukata moja kwa moja kwenye OC za Wizara na Taasisi zinazodaiwa kwani ni aibu kuona wadaiwa sugu wa TTCL ni Wizara na Mashirika ya Serikali.

**4.8 Chuo Kikuu cha Sayansi na Tekinolojia Mbeya (MUST)**

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi zinazotoa mafunzo zimekuwa zikiongeza wanafunzi kulingana na matakwa ya kitaifa katika fani mbalimbali huku bajeti za taasisi husika zikiendelea kushuka na kutokutolewa kwa wakati. Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kilianzishwa kwa madhumuni ya kuziba pengo la soko la ajira katika nafasi za wanasayansi, mafundi sanifu pamoja na wahandisi ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia. Pamoja na umuhimu wa Chuo hiki kwa Taifa, bado ni vigumu kwa Chuo hiki kufikia hadhi ya Chuo Kikuu kutokana na ufinyu wa bajeti itolewayo kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 bajeti ya fedha za maendeleo iliyoidhinishiwa chuo hiki ilikuwa ni **shilingi bilioni 2,500,000,000** ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2014 ni **shilingi milioni 543,637,500** tu ndizo fedha zilizotolewa.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, katika jitihada za kuendeleza miundombinu ya taasisii hii, Serikali ilifanya maamuzi ya upanuzi wa eneo la chuo. Uthamini ulifanyika na kubaini kiasi cha **shilingi bilioni 3,100,000,000** kinahitajika kwa ajili ya zoezi la fidia kwa wananchi ambazo zinatakiwa zilipwe katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014. Hata hivyo hadi kufikia mwezi Machi, 2014 kiasi kilicholipwa ni **shilingi bilioni 1,100,000,000** tu, kiasi kilichosalia ni **shilingi bilioni 2,000,000,000** ambacho kinahitajika kwa ajili ya kukamilisha ulipaji wa fidia ili kuepusha Serikali kupata hasara itakayotokana na gharama za riba.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri ili kukipa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia uwezo na hadhi ya Chuo Kikuu, Serikali itenge bajeti inayoendana na ongezeko la wanafunzi katika chuo hiki na kukiepusha na madeni yanayotokana na huduma mbalimbali kutoka kwa wazabuni.

Pia, kamati inashauri fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya chuo hiki pamoja na ufinyu wake zitolewe kwa wakati ziweze kusaidia utekelezaji wa miradi na maendeleo.

**4.9 Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha**

**Mheshimiwa Spika,** madhumuni ya kuanzisha kwa Taasisi ya Nelson Mandela ni kuzalisha wataalam waliobobea katika nyanja mbalimbali za sayansi na teknolojia ikiwa ni pamoja na watafiti kwa lengo la kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi yetu na kuleta maendeleo kwa ujumla. Ni dhahiri kuwa maendeleo ya kiuchumi duniani yanapatikana kwa kutumia sayansi na teknolojia inayoibuliwa baada ya kufanya tafiti mbalimbali. Taasisi ya Nelson Mandela imeanzishwa kwa ajili kutoa mafunzo ya aina hii kwa nchi yetu na Afrika kwa ujumla.

Hata hivyo, inaelekea kuwa dira ya Taasisi hii haiwezi kufikiwa kutokana na bajeti ndogo inayotengwa. Kwa mfano mwaka wa fedha wa 2013/2014 Taasisi ilipangiwa jumla ya **shilingi bilioni 4,500,000,000** kwa ajili ya shughuli za maendeleo hata hivyo, hadi kufikia Aprili, 2014 fedha iliyokuwa imetolewa ni **shilingi milioni 300,000,000** tu. Aidha, mwaka 2014/2015 bajeti ya maendeleo iliyopangwa kwa ajili ya taasisi hii imeshuka hadi kufikia **shilingi bilioni 1,500,000,000.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia utoaji huu wa fedha, Kamati inajiuliza, je Serikali inania ya kuifanya Taasisi hii kufikia dira yake ya kuwa miongoni mwa Taasisi bora ya elimu ya juu duniani (*centre of excellency)*? Kamati inaishauri Serikali iazimie kuiboresha taasisi hii kwa kuiongezea bajeti ya maendeleo ili iweze kutimiza malengo ya kuanzishwa kwake vinginevyo itakuwa haina tija.

### 4.10 Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam kimsingi inalojukumu la kutoa mafunzo ya uhandisi na teknolojia hapa nchini. Taasisi hii imepata mafanikio mbalimbali na hasa ikizingatiwa kuwa ni taasisi ya kwanza kupata ithibati ya Baraza la Elimu ya Ufundi (NACTE) mwaka 2005. Changamoto kubwa inayoikabili Taasisi hii ni fedha, ambapo katika mwaka wa fedha 2013/2014, Taasisi hii ilitengewa **shilingi bilioni 2,500,000,000**, hadi kufikia mwezi Aprili 2014 ilikuwa imepata jumla ya **shilingi milioni 843, 637,500**. Aidha changamoto zingine ni upatikanaji wa fedha kwaajili ya kununulia chakula cha wanafunzi na fedha za mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi kwa kuwa zote hizi pia hutegemea Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, ili Taasisi hii iweze kuendelea kuimarika katika utoaji wa elimu nchini, Kamati inashauri, Taasisi hii nayo ipewe "*Skills Development Levy*" kama inavyopewa VETA.

Vilevile, Kamati inashauri Taasisi za Elimu ya Juu na Vyuo Vikuu vipewe uhuru wa kutafuta wafanyakazi na waalimu wa vyuo hivyo wenyewe kwani

kuingizwa kwenye ajira ya pamoja ya Wizara ya Utumishi inachelewesha, inapotosha na wakati mwingine kuajiri watu wasiofaa.

**4.11 Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa ubunifu wa kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha ambavyo vimeisaidia kujiendesha mpaka sasa. Kamati imekuwa ikisikitishwa na fedha zinazotengwa kwa ajili ya utafiti na maendeleo kuwa ni kidogo ukilinganisha na umuhimu wa utafiti na sayansi katika jamii yetu. Hata hivyo, pamoja na fedha hizo kuwa ndogo, pia hazitolewi kwa wakati jambo linalosababisha Tume ya Sayansi na Teknolojia kuchelewa kutekeleza majukumu yake.

*Jedwali lifuatalo linaonesha mtiririko wa Bajeti ya Tume ya Sayansi na Teknolojia kwa miaka mitano mfululizo:-*

| MWAKA | FEDHA ILIYOIDHINISHWA | FEDHA ILIYOTOLEWA |
|---|---|---|
| 2010/2011 | Bilioni 30 | Bilioni 19 |
| 2011/2012 | Bilioni 25.7 | Bilioni 7.3 |
| 2012/2013 | Bilioni 21.4 | Bilioni 12.8 |
| 2013/2014 | Bilioni 16.4 | Hakuna fedha iliyotolewa |

Aidha, katika bajeti ya mwaka 2014/2015 kiasi cha fedha kilichotengwa kimezidi kushuka hadi kufikia **shilingi bilioni 14,000,000,000**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imekuwa inajiuliza Je, kwa utengaji na kasi ya utoaji huu wa fedha ni kweli tutafikia asilimia moja (1) ya Pato Ghafi la Taifa kama ilivyokusudiwa? Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kabla ya kuisha kwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014, ili Tume hii iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**4.12 Tume ya Nguvu za Atomic**

**Mheshimiwa Spika**, Tume hii sasa inampango wa kujenga maabara ya kuhifadhi mabaki au makapi yanayobaki baada ya madini yenye mionzi ktumiwa. Kwa hali ya Taasisi yetu ilivyo sasa, kama hili litafanikiwa, tunayo nafasi ya pekee katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati. Upekee huu unaweza kutupa nafasi hata ya kuiingizia fedha taasisi hii. Kinyume chake tunatengeneza mazingira ambayo ni hatari sana kwa maisha ya binadamu hasa akina mama wajawazito na hata mifugo na mimea. Kamati inashauri umuhimu wa maabara hii uzingatiwe na wapewe fedha za kutosha ili kukamilisha ujenzi huu mapema.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mipango hii mizuri Tume hii ina changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha. Hadi Kamati ilipokutana na Wizara mwezi Mei, 2014 ambapo umebakia mwezi mmoja tu kumalizika kwa mwaka wa fedha 2013/2014, kati ya **shilingi bilioni 1,000,000,000** iliyokuwa imeidhinishwa kwaajili ya Tume ya Nguvu za Atomic, hakuna fedha yoyote iliyotolewa. Kamati inashauri kwa kuzingatia umuhimu wa taasisi hii na majukumu yake ni muhimu fedha hizi zitolewe kabla ya mwaka huu wa fedha kumalizika.

## 5.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia imeomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 67,221,001,000.**

**a)** **Shilingi bilioni 37,844,668,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yaani Mishahara na Matumizi Mengineyo. Ambapo kati **yake shilingi bilioni 26,828,491,000** ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi bilioni 11,006,177,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**b)** Aidha, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Tekinolojia imetengewa jumla ya **shilingi bilioni 28,376,333,000/=** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kati ya hizo **shilingi bilioni 26,000,000,000/=** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 3,376, 333,000/=** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii kifungu kwa kifungu na sasa inaliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kupitisha maombi hayo yenye jumla ya **shilingi bilioni 67,221,001,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuhitimisha napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu mbele ya Bunge lako tukufu. Aidha nawashukuru pia Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa, Mb, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Mhe. January Yusufu Makamba Mb, Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na Prof. Patrick J. Makungu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; pamoja na Wataalam wote wa Wizara hii na Taasisi zilizo chini yake kwa ushirikiano wao ambao umeiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao, hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini mkubwa. Sasa naomba kwa heshima kubwa, niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Peter Joseph Serukamba, Mb -Mwenyekiti
2. Mhe. Prof. Juma Athuman Kapuya, Mb-M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Hussein Mussa Mzee, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Zarina Shamte Madabida, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Rebecca Michael Mngodo, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Aliko Nikusuma Kibona, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Eng. Ramo M. Makani, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Dkt. Pudenciana W. Kikwembe, Mb- Mjumbe
12. Mhe. Mussa Haji Kombo, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Mtutura Abdallah Mtutura, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Abdul Rajab Mteketa, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Elizabeth Nkunda Batenga, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Suleman Masoud Nchambi, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Said Amour Arfi, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Haroub Mohamed Shamis - Mjumbe
19. Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashilillah, katibu wa Kamati Ndugu Hosiana John na Ndugu Francisca Haule kwa kuihudumia Kamati na kufanikisha maandalizi ya Taarifa hii. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono Hoja.

Prof. Juma A. Kapuya, (Mb)
**MAKAMU MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU**
31 Mei, 2014

**SPIKA:** Sasa naomba nimuite Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara hii. Mheshimiwa Injinia Mnyaa. *(Makofi)*

**Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa Fedha 2014/2015 kama ilivyosomwa Bungeni**

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA -MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mola Mtukufu Subhana Wataala kwa kunijalia mimi na ninyi mnaonitizama na kunisikiliza kuwa na afya, uzima na kutimiza wajibu wetu uliotuweka hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kumuomba Mwenyezi Mungu atujaalie sote wenye nia njema na nchi hii, atupe moyo wa uvumilivu na subira na azijalie nyoyo zetu kutatua matatizo yetu kwa njia ya busara, amani na upendo kwa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano na atubainishie wabaya wetu kama alivyokwishatubainishia baadhi yao ili na wao tuweze kuwanasihi na Mola atusaidie kuwabadili nia zao mbaya ili Tanganyika na Zanzibar zifaidike na ziwe na haki sawa kwa pande zote mbili za Muungano bila ya ubaguzi wa ukubwa wa eneo, rangi za watu , tamaduni na dini zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kwa ruhusa yako niwashukuru wananchi wa Mkanyageni kwa ushirikiano wanaonipa na uvumilivu wao wakati sipo Jimboni kwa shughuli za Kibunge. Pia nawashukuru wananchi wote wa Majimbo ya Zanzibar kwa uvumilivu wao waliposubiri fedha ya Mfuko wa Jimbo iliyofanyiwa *varange,* sasa fedha zimeshawekwa katika akaunti za kila Jimbo baada ya kucheleshwa kwa miezi mitano kwa sababu wazijuwazo wao Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na yale tulioahidi sasa yatatekelezwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kutoa mtazamo wetu juu ya bajeti ya Wizara hii, naomba kutoa pongezi na shukrani zangu za dhati kwa viongozi wetu wakuu wa vyama hususani *CUF*, CHADEMA na *NCCR* MAGEUZI na kwa kuamua kwa dhati kufanya kazi ya kuwasaidia Watanzania kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Freeman Mbowe, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuniteua kuwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na kuwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Wizara hii muhimu. Naamini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, nitatumikia kwa uaminifu ili kuweza kulikwamua Taifa letu na kuitendea haki Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshiwa Spika, baada ya dua hiyo na shukrani kwa Jimbo, sasa nianze kuihoji na kuishauri Serikali kuhusu Bajeti ya Wizara hii ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimwa Spika, majukumu na dhamana ya Wizara hii. Kabla ya yote, ni vyema kudurusu majukumu ya msingi ya Wizara hii ili Waheshimiwa Wabunge wako wapate nafasi ya kukumbuka ili wakichangia waitendee haki Wizara hii. Pamoja na mambo mengine ambayo ni utaratibu wa kawaida wa kila Wizara, majukumu ya msingi ni kama yafuatayo:-

Moja, kuhakikisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Sayansi, Teknolojia na Ubunifu vinachangia katika kukuza maendeleo ya taifa hili na mengine ni kama ilivyoelezwa katika (i)-(ix) ya kitabu changu.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii pia inao wajibu na dhamana ya kusimamia Mashirika, Tume na makampuni zilizo chini yake ambazo zinachangia katika kuyafikia malengo na matarajio ya wananchi. Taasisi zenyewe zilizo chini ya Wizara hii ni Taasisi ya Teknolojia Dar-es-salaam *(DIT),* Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia - Mbeya, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela na kama ilivyoelezwa katika kitabu changu kuanzia (a) - (i).

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo, Wizara hii iliasisiwa tarehe 7 Februari, 2008 kwa kuunganishwa kwa Idara ya Mawasiliano iliyokuwa chini ya Wizara ya Miundombinu na Idara ya Sayansi na Teknolojia iliyokuwa chini ya Wizara ya Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia. Halikadhalika, Wizara iliundwa tena tarehe 17 Disemba, 2010 kupitia Tangazo la Serikali Na.494, Wizara ikakabidhiwa tena majukumu niliyoyataja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya jumla kuhusu Wizara ya Muungano, Mashirika au Taasisi zake za Muungano. Katika kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kilichokaa tarehe 31 Mei, 2011 na tarehe 1 Juni, 2011 kujadili utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na Bajeti ya mwaka 2011/2012, miongoni mwa maagizo ya Kamati ilikuwa ni kuitaka Wizara hii ya Muungano iwe na sura ya Muungano na ionekane wazi. Hilo lilikuwa ni agizo namba saba la Kamati na majibu Waziri akatoa mwezi Juni, 2012, akasema:-

"Katika utekelezaji wa agizo hilo, Serikali ilijibu kwamba Wizara hii inasimamia masuala ya Muungano kama ilivyoorodheshwa katika Ibara ya Nne (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kama ilivyofafanuliwa katika Nyongeza ya Kwanza ya Katiba hii kuhusu mambo ya Muungano."

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa jibu hilo la Serikali, mambo mengine yaliyotajwa katika Nyongeza ya Kwanza ni Elimu ya Juu, Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania na mambo yote yanayohusika na kazi za Baraza hilo na utafiti.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, hapa tunapata maswali mengi ya kujiuliza ambayo yanahitaji majibu sahihi ya Serikali, nayo ni kuwa *DIT* na Chuo Kikuu cha Mandela na kile Chuo Kikuu cha Mbeya, kimsingi vyote vilikuwa ni vyuo vya ufundi sawa na *Karume Technical College* cha Zanzibar ambacho sasa hivi kinajulikana kama *Karume Institute of Science and Technology* na vyote hivyo hapo mwanzo vilikuwa vinatoa *FTC*. Kwa nini basi Chuo hiki kisijumuishwe katika majukumu ya msingi ya Wizara hii kama hivyo vingine? Ikiwa sababu ni ya umiliki kwamba kinamilikiwa na SMZ basi na hivyo vyingine kwa upande mwingine vilikuwa vinamilikiwa na Tanzania Bara lakini kwa nini huduma zinazotolewa na Wizara hii ya Muungano pamoja na ujenzi wa majengo mapya, vifaa vya utafiti, maabara za uchunguzi na mambo mbalimbali, Wahadhiri na kadhalika zinatofauti kubwa au hazipo kabisa kwa upande wa *KIST - Karume Institute of Science and Technology*? Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri anaweza akasema *TEA* inasaidia teknolojia lakini inasaidia vijisenti tu.

Mheshimiwa Spika, kama hayo hayatoshi pia katika taarifa ya Wizara hii ya tarehe 1 Mei, 2014, uko mradi wa kuunganisha Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti *(Last Mile Connectivity*) kwa ajili ya kufanikisha elimu mtandao ambao umejumuisha taasisi 27 za Tanzania Bara vikiwemo vyuo vikuu binafsi lakini ni Chuo Kikuu kimoja tu cha Zanzibar ambacho ni *SUZA* ndicho kilichotajwa kuwemo katika mpango huu. Sababu zipi zilizotumika hata ikawa *Karume Institute of Science and Technology (KIST)* na vyuo vikuu vingine vya Zanzibar visijumuishwe katika mpango mtandao huo? *(Makofi)*

Moja kati ya jukumu kuu la Wizara hii tumeshaona hapo awali kuwa ni kusimamia kwa kuziimarisha taasisi za sayansi na teknnolojia. Kwa kuwa haikutajwa popote kusimamia na kuziimarisha taasisi za sayansi na teknolojia za Tanzania Bara pekee maana yake tatizo linakuja katika utendaji wa Wizara ambapo pamoja na wale waliosababisha siku za nyuma lakini na wewe mwenyewe Waziri mmeshindwa kusimamia ipasavyo majukumu ya Wizara hii uliyopewa ikiwa na sura ya Muungano kama agizo la Kamati nililosoma mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa ya Bunge lako *KIST* kilijengwa kwa msaada wa Serikali ya Marekani kilikusudiwa kuwa Chuo Kikuu ambacho mimi mwenyewe na Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na Mheshimiwa Rajab ni matunda ya chuo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, elimu ya juu toka 1964 kwenye Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ni suala la Muungano, hakikuendelezwa hadi hivi leo na eneo liko wazi. Je, ni nini kama si kudhoofisha elimu upande mmoja wa Muungano? Hii elimu ya juu ambayo ni ya Muungano wapi ilipoelezwa mipaka yake na sheria ipi maana katika Katiba limetajwa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa bajeti. Ili kujua vizuri utaratibu wa fedha zinazoombwa na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu na zile zinazopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, ni vyema tuangalie mtiririko wa miaka mitano iliyopita ili sote tujiridhishe na ufanisi wa Wizara hii muhimu katika kukuza wataalam, tafiti na maendeleo ya kisayansi na teknolojia kwa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, angalia jedwali namba moja, linatoa ufafanuzi wa hali halisi ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako na iliyotolewa,na maelezo ya ziada yanafafanuliwa katika kifungu 4.2.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo iliyofuata, mambo yalianza kuharibika ambapo Wizara hii imeshindwa kutoa taarifa kwa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusiana na kiasi gani kilichotolewa na Serikali kulinganisha na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako katika matumizi ya kawaida. Jambo hili haliwezi kuwa ni bahati mbaya yumkini kuna jambo linalofichwa kwa kuwa ni desturi iliyozoeleka kwa Wizara zote na kwa miaka yote kuonyesha mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka uliopita kabla ya kupitisha bajeti ya mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, yumkini matumizi ya kawaida yalizidi kiwango kilichoombwa katika *OC* kwa kuwa hatujawahi kusikia wafanyakazi kulalamika kukosa mishahara kwa maana hiyo hakukuwa na upungufu wa fedha bali kulikuwa na matumizi yaliyozidi kiwango kilichoidhinishwa na ndiyo maana Waziri akashindwa kutoa kiwango cha asilimia ya fedha zilizopatikana. Kwa maana hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi wa jambo hili kwa kuwa katika viambatisho vyake vyote kwa miaka mitatu matumizi hayo yamefichwa na hili limetokea yeye akiwa Waziri wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maendeleo, angalia jedwali namba mbili, linajieleza lenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa jedwali namba mbili linavyoonesha, kwa muda wa miaka mitano iliyopita ni mwaka 2009/2010 na mwaka 2012/2013

tu ndiyo kazi zilifanyika na miradi ya maendeleo ikatekelezwa kama ilivyo pangwa. Haizuru baadhi yake haikuweza kukamilika vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini miaka ya 2010/2011, 2011/2012 na mbaya zaidi 2013/2014 fedha za maendeleo zilizopatikana iwe za ndani au za nje zilikuwa chini ya asilimia 30 na nyingine hadi asilimia 10. Huu ni utendaji mbovu unaosababisha miradi takribani yote ya Wizara hii kukwama na kusababishwa kuachwa nyuma na hata majirani zetu wasio na rasilimali kama sisi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inahitaji majibu kwa maswali yafuatayo, kwamba malengo ya Dira ya Wizara hii yatafikiwa? Malengo ya Dhima ya Wizara yatatimizwa?

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Taasisi na miradi mbalimbali. Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ilitoa agizo katika Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 la kuanzishwa kwa anuani za makaazi na postikodi ambapo kila mwananchi ataweza kujitambulisha kwa kutumia jina la mtaa, nambari ya nyumba pamoja na postikodi ya eneo analoishi. Katika kutekeleza agizo hili, Wizara hii iliiagiza Mamlaka ya Mawasiliano *(TCRA)* kusimamia utekelezaji wa mfumo huu. Kamati ya Kitaifa ya Uratibu na utekelezaji wa mfumo huu iliundwa na wajumbe wake ni Makatibu Wakuu wakubwa wafuatao, kwa kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge na wananchi, Makatibu Wakuu wa Wizara za Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha, Wizara ya Ardhi, ni wengi tu.

Mheshimiwa Spika, mpango huu ulianza kwa majaribio mwaka 2008/2009 katika Kata nane huko Arusha na mwaka 2010/2011 katika Kata nane za Manispaa ya Dodoma. Changamoto zilizojitokeza hasa za mipango miji holela na ujenzi holela zilisaidia kuboresha mipango ya utekelezaji katika miji mengine. Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa *TCRA*, aliwahi kusema kwamba wamemaliza kutengeneza mfumo wa "*Programing*" wa *Postal Code* katika "*Global Positioning*" *(GPS)* ambapo nchi iligawanywa katika anuani saba za posta. Waligawa katika Dar es Salaam ikapewa namba moja, Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Mnyara namba mbili, Mwanza, Kagera Shinyanga, Mara namba tatu, Kigoma, Dodoma na Tabora namba nne, Iringa, Mbeya, na Rukwa namba tano, Mtwara, Ruvuma na Lindi sita na Zanzibar saba.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa za Mkurugenzi Mkuu wa *TCRA* za tarehe 5/6/2012, alisema baada ya majaribio ya Arusha na Dodoma na kumaliza kazi ya *GPS* sasa wako tayari kwa nchi nzima na *TCRA* itatenga fedha katika bajeti ya mwaka ujao yaani 2012/2013 kupitia Serikal za Mitaa. Fedha hizo zitatengwa kwa mpangilio kupitia TAMISEMI hadi mwaka 2014 ambapo mradi huu utamalizika. Makadirio ya mwaka 2009 mradi huu ulitarajiwa

kugharimu Sh.158,000,000,000 na kwa mujibu ya hotuba hii ya Waziri makadirio hayo bado hayajaongezeka.

Mheshimiwa Spika, jedwali namba 3 hapa chini linafafanua fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako na fedha halisi iliyopatikana kwa utekelezaji wa mradi huu. Mheshimiwa Spika unaweza ukajionea mwenyewe hapo, ni hiyo mwaka 2011/2012 tu angalau asilimia 66 ilipatikana, lakini 2012/2013 asilimia 28.8, 2013/14 asilimia 30, 2014/2015 hii tuliyo nayo Bunge lako litaidhisha milioni mia tano lakini sijui kitapatikana kipi *wallah aalam*.

Mheshimiwa Spika, leo tunapitisha bajeti ya Wizara hii ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia, mwaka wa fedha wa 2014 unamalizika na kuanza mwaka mwingine. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu na Watanzania wasikie, kuanzia mwaka 2009 wa majaribio na ahadi zote za Wizara hii ni kanda ngapi kati ya hizo saba zilizokamilisha anuani za makazi na simbo za Posta? Kwa kuwa Kamati ya Kitaifa ya Uratibu na Utekelezaji wa mfumo huu ni nzito sana, ambayo mimi sijawahi kuona katika maisha yangu ikiongozwa na Makatibu Wakuu niliowataja hapo mwanzoni, akiwemo Katibu Mkuu Wizara ya Fedha; nini basi kimekwamisha mradi huu ambao ulitakiwa kumalizika mwaka huu 2014? Ikiwa tutapewa jibu la kwamba mwaka 2014 bado haujamalizika, je, huo muda uliobakia Waziri atalihakikishia Bunge lako hili kwa muda uliobakia upo uwezekano wa kukamilisha mradi huu mzima wakati maeneo ulikokamilika ni machache mno?

Mheshimiwa Spika, nimeuliza maswali hayo yote kutokana na umuhimu wa juu na faida za mradi huu kiuchumi, kibiashara, kisiasa, kiusalama na utoaji huduma mbalimbali za jamii ikiwemo umeme, maji, gesi, huduma za kifedha na usambazaji wa barua na vifurushi. Mfano mzuri ni mabenki na ukusanyaji wa kodi mbalimbali. Katika shida moja kubwa sana ambayo mabenki yetu wanaipata katika utoaji mikopo na huduma ni suala la KYC *(Know Your Customer* - kumtambua mteja wako *(physical addresses)* ambapo wateja wote kuwa na mfumo unaolingana wa *KYC* hasa katika uzuiaji wa fedha haramu *(Anti Money Laundering)* bila ya kujali nchi anayotoka.

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa Anuani na Simbo ulitakiwa uende sambamba na Mradi wa Vitambulisho vya Taifa (*National Identification Cards)*. Haya yote yakitekelezwa yatasaidia ukuaji wa Uchumi wa Taifa kwa kuwatambua walipa kodi na ndio maana jirani zetu wa Kenya wanalipia asilimia 95 ya bajeti yao kupitia kodi wanazozitoza kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika hatua hii, Kambi Rasmi ya Upinzani inashindwa kufahamu ni kwa nini miradi yote hii miwili inasuasua hadi hivi leo? Sera ya Taifa ya Posta inafahamika tangu mwaka 2003, taratibu za kuanza Mradi huu zilianza

mwaka 2008, hadi hivi leo ni miaka sita, saba, tayari ni chini ya asilimia 5 kama zinafika utekelezaji wake. Je, Wizara yako au Serikali haijui umuhimu wa Mradi huu? Je, Zanzibar imetekeleza kiasi gani? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo ya kina kwa hatua zote zilizochukuliwa na Serikali na Serikali inaahidi nini na lini Miradi hii yote miwili itakamilika? Vinginevyo tuseme Serikali ya CCM imeshindwa? Je, hatuoni aibu kwamba katika Mkutano wa Umoja wa Posta Duniani uliofanyika Oktoba 2012 huko Doha, Qatar uliozungumzia uhamasishaji wa Mfumo wa Anuani za Makazi kutumika katika nchi zote wanachama ambapo Mheshimiwa Anna Kajumulo Tibaijuka, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi ya Makazi aliteuliwa kuwa Balozi Maalum wa uhamasishaji wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta Duniani lakini nchi yake mwenyewe bado haijakamilisha na wala haijahamasisha vizuri na utekelezaji unasuasua?

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Posta Afrika *(PAPU)*. Kifungu 6.1, kinaonesha namna Bunge lilivyoridhia Azimio la PAPU. Azimio la Mkataba wa Posta wa Afrika wa mwaka 2009 uliridhiwa kwa kauli moja na Bunge lako na kwa kuwa kiwanja cha kujenga Makao Makuu ya PAPU kilipatikana na kuzungushiwa uzio huko Arusha. Ni kwa nini sasa jengo hilo halijajengwa hadi hivi leo? Mbona maendeleo ya ujenzi huo hayajaripotiwa tena na Wizara yako Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* pamoja na Mkongo wa Taifa. Ni jambo linalotia matumaini na kuleta faraja na kwa maana hiyo tuipongeze Wizara kwa kufanikisha kwa kiasi fulani mradi wa Mkongo wa Taifa, kama inavyoelezwa katika kifungu hiki cha 7.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika taarifa zilizotolewa katika hotuba ya Waziri katika bajeti ya 2009/2010 kuwa faida za mkongo ni pamoja na kuboresha matumizi ya simu za viganjani, kusimamia mfumo mpya wa digitali, kuanzisha rejesta ya utambuzi wa vifaa vya mawasiliano, kusimamia usajili wa simu za viganjani, kuhimiza na kuwezesha matumizi ya pamoja ya miundombinu ya mawasiliano. Halikadhalika Mkongo huu utaziunganisha na mikongo ya kimataifa ya baharini ikiwemo *SEACOM*, *UHURU NET, UMOJA NET ESSY* na *TEAMS*. Wakati huohuo, katika taarifa ya mwezi Mei 2014 kwa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu kwa ajili ya matayarisho ya bajeti ya mwaka huu, Mkongo huu umeunganishwa na mikongo ya baharini ya *SEACOM* na *EASSy* tu. Wananchi waliamini kauli hizo za Wizara hii na tulifahamu kitendo cha kuunganishwa na mikongo mingi ya baharini ni kitendo cha kuaminika kwa kuongeza *reliability*, ubora wa huduma *(efficiency)* na kuzuia kukatika mawasiliano kwa kuwa na "*ring circuit*".

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ubora wa mawasiliano haujapatikana, picha katika runinga au TV zetu nyingi nchini zinakatikakatika, zinaganda

zinaonesha vivuli vya ajabu, mawasiliano katika mabenki mara nyingi unaambiwa usubiri mtandao uko chini. Pia katika *ATMs* na huduma nyingine zinazotumia teknolojia ya mawasiliano pamoja na kuhakikishiwa kwamba Mkongo wetu umejengwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vinavyosimamiwa na ITU, hapa tunapata mashaka na kujiuliza maswali mengi ambayo Mheshimiwa Waziri hana budi kulielezea Bunge lako kwa viwango vinavyoridhisha pia.

Kwanza, ni kwa nini Mkongo wetu umeunganishwa na mikongo ya kimataifa miwili tu ya *SEACOM* na EASSy, vipi kuhusu mikongo mengine tuliyoarifiwa mwanzoni ya *UHURU NET*, *UMOJA NET* na *TEAMS*.

Pili, kwa nini basi kutokee udhaifu wa mawasiliano nilioutaja hapo juu.

Tatu, kwa nini kuwe na viwango tofauti baina ya kampuni za simu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, udhaifu huu nilioutaja ulikwisharipotiwa na Kamati ya Bunge ya Miundombinu na kutoa agizo kwa Mheshimiwa Waziri na majibu ya Waziri kwa Kamati alisema; ubora wa mawasiliano umewekewa kanuni *EPOCA (Quality of Service Regulations)* ambazo zinaainisha kiwango cha ubora lakini hadi hivi leo Waheshimiwa Wabunge na wananchi wanashuhudia kuendelea kuona matatizo hayo hayo yakiendelea. Kwa hivyo, nini kauli ya Serikali kwa wananchi kuhusiana na matatizo hayo kuendelea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amri ya Serikali kuhama kutoka kwenye Mfumo wa Analojia kwenda kwenye mfumo wa dijiti. Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* iliamuru vituo vyote vya televisheni nchini kuzima mitambo ya analojia na kuvilazimisha kuingia kwenye mfumo mpya na wa kisasa wa dijiti ambao unatumia ving'amuzi *(receivers)* kupata mawimbi ya televisheni. Katika taarifa ya Waziri mbele ya Kamati ameiambia Kamati juu ya tathmini ya utekelezaji wa amri ya Serikali. Katika taarifa yake pamoja na Serikali kutoa takwimu zisizo sahihi kwa mujibu wa uhalisia wa jinsi zoezi hili lilivyoathiri wananchi hususani katika kupata haki yao ya kupata habari ambayo ipo Kikatiba, bado Serikali imekiri kuwa takwimu hizo ambazo hazina uhalisia kuwa asilimia 5.5 ya wananchi walibainika kushindwa kumudu gharama za ving'amuzi licha ya Serikali kuondoa *import duty* katika ving'amuzi hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa zoezi hili lilifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Tanga, Moshi, Mbeya na Arusha. Pamoja na tathmini hiyo kufanyika, Serikali iliingia katika utekelezaji wa kuzima mitambo katika Mikoa mingine kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 8.2.

Mheshimiwa Spika, pamoja na tathmini iliyofanywa na Serikali, haijaeleza matatizo yaliyojitokeza katika ving'amuzi ambavyo vimeuzwa kwa wananchi. Taarifa inaeleza juu ya takwimu za wananchi walionunua na walioshindwa lakini ukweli ni kwamba hata walioweza kununua pia wamekutana na changamoto ya ving'amuzi hivyo. Kuzima au kukatika mara kwa mara lakini Kambi ya Upinzani katika kipindi cha mwaka 2013 ilipohoji juu ya kukatika kwa matangazo majibu ya Serikali yalikuwa ni kama ifuatavyo na pia yalinukuliwa katika hotuba ya Upinzani, "Wananchi wawasiliane mara moja na watoa huduma za ving'amuzi ili kuwasaidia kupata ufumbuzi". Hilo ndilo lilikuwa jibu. Taarifa hii ilitolewa na kutiwa saini na Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Waziri wa Wizara hii tarehe 2 Aprili, 2013 kauli ambayo iliisikitisha Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwani Serikali ilitoa leseni kwa watoa huduma kwa umma hivyo ilitakiwa kuwajibika kuhakikisha kuwa watoa huduma wanatoa huduma hiyo kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa tatizo la kukatika kwa matangazo bado linaendelea katika maeneo ambayo yamefikiwa na huduma hii. Hivyo ni wazi kuwa wananchi wengi hukosa habari kutokana na kukatika kwa matangazo hayo, hivyo kutopata haki yao Kikatiba ambayo kimsingi Serikali haijaweka mazingira wezeshi ya kuwapa wananchi wake haki ya kupata habari ambayo ni ya Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwanza inaitaka Serikali kufanya tathmini ya ufanisi wa huduma hii kabla ya kujielekeza kuangalia takwimu za wananchi walionunua vifaa hivyo vya mfumo mpya.

*TCRA* ifanye ukaguzi wa uwezo wa matangazo kwa ving'amuzi vyote katika makampuni yaliyopewa leseni ya kufanya biashara hiyo nchini.

Tatu, Serikali iliambie Bunge lako Tukufu je nini tafsiri asilimia 5.5 ya wananchi. Kwa sababu asilimia 5.5 katika idadi ya milioni arobaini na tano maana yake ni wananchi 2,475,000. Je, hawa kukosa huduma ni kidogo?

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Wizara kwa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusiana na gharama au bei za huduma za Mkongo, alisema zilipatikana baada ya kufanya utafiti wa kina na zilifanywa na mshauri mwelekezi OVUM ya Uingereza kwa kushirikiana na *TTCL* na mapendekezo ya bei hizo kuridhiwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, sekta ya mawasiliano inakua kwa kasi kubwa na huenda Tanzania ikawa ya pili kwa Afrika ya Mashariki na Kati ikitanguliwa na Kenya katika fedha za *mobile money.* Pamoja na mafanikio hayo, bado matumizi ya TEHAMA yana nafasi kubwa katika kunyanyua uchumi wa kila raia na Taifa kwa jumla. Matumizi hayo ni pamoja na '*electronic procurement*'

kama Dubai kupitia Shirika lao la TEJARI ambapo limeweza kupunguza gharama za manunuzi kwa asilimia 30, *Tele Medicine* kama India hasa Jimbo la Hydrabad ambapo wananchi vijiji wanapata tiba bila ya kufika Hospitali Kuu, *Eco farming* Zimbabwe ambayo inatumika kwa kuwapatia mikopo na pembejeo wakulima wa vijijini. Pia katika kukuza mapato, kudhibiti wizi wa fedha na ufisadi. Uanzishwaji wa *Tele-Visa* na *E-passport* yote hayo wenzetu wanayafanya kuongeza mapato, hapa sisi tunafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati *TCRA* ikiwahamasisha wawekezaji, utowaji wa mawimbi *(frequencies)* yalikuwa yakitolewa kulingana na uwepo wake. Matokeo yake walipewa lakini wapo wawekezaji ambao wameshindwa kuwekeza. Kambi Rasmi ya Upinzani inatamka wazi, wale wote waliohodhi mawimbi hayo wanyang'anywe na kuanzisha utaratibu wa kuyauza kwa mnada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mawimbi ya 4G/LTE (*Long Technical Evolution)* ambayo mawimbi yake yana bei kubwa na inashangaza kuona baadhi ya nchi mawimbi hayo yanauzwa kati ya dola milioni hamsini hadi milioni mia moja na kumi na kwa dunia ya kwanza milioni mia tisa hamsini, wakati hapa petu yanauzwa kwa dola milioni tatu. Hili ni jambo la kushangaza, hivyo tunamtaka Waziri atoe ufafanuzi ili aweke wazi kwamba, je, hakuna harufu ya rushwa katika jambo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuanza kutumia Mkongo wa Taifa na unafuu ukapatikana kwa kiwango alichotoa mfano Mheshimiwa Waziri cha 2Mbps kwa njia isiozidi kilomita 1000 kutoka Dar es Salaam mpaka kufikia dola 160 bado inaonekana gharama hizi ziko juu.

Mheshimiwa Spika, pia Kambi ya Upinzani tunamtaka Waziri atueleze kwa nini ving'amuzi kama vile vya *ARISAT, MEDIACOM*, STAR TRAC, *TECHNOSAT* vinapatikana na vinaonesha *TVs* zote za ndani bila ya gharama yoyote ya mwezi lakini vingamuzi vya *STAR TIME, CONTINENTAL*, *DIGITECH*, vilipiwe kwa kila mwezi. Je, huu ndio nafuu ya Mkongo wa Taifa? Maana makampuni haya baada ya kuhamasishwa na *TCRA* kwa nini basi kuwe na *multiplex* nyingi, tatu mpaka nne, kwa nini isiwe *multiplex* moja.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri kurekebisha *TCRA* iwe na sura ya Muungano na sio kwa kuwa na Wajumbe wa Bodi tu bali kwa uwakilishi kiutendaji, isirudie makosa yaliyopita wakati ule haijaunganishwa wakati Tume ya Mawasiliano na Tume ya Utangazaji ambazo ndizo zimefanya *TCRA*, wakati Zantel ilipowekeza Zanzibar na kuwekewa vikwazo vingi hata Zanzibar kudai kurejeshewa *code* namba yake ya 259 kutoka ITU.

Mheshimiwa Spika, Baada ya *COSTECH* kufunguliwa Juni 2012 na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na sasa ofisi imeazimwa sehemu yake ya ndani ya jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais huko Tunguu. Mchakato wa kupata ofisi yake upo lakini matatizo yaliyopo zaidi ni ufinyu wa watendaji wa ofisi hiyo kwani kuna wafanyakazi watatu tu ambapo wawili wakiwa wa muda.

Mheshimiwa Spika, Suala la fedha za utafiti nalo limekuwa ni tatizo kwa upande wa ofisi hii Zanzibar na uwezo wake kwa sasa kufanya tafiti ni mdogo kwani hakuna fedha za utafiti. Hivyo mheshimiwa Waziri naomba katika majibu yake aseme ni kwa vipi ofisi hii imekuwa haiwezeshwi kifedha na pia aweke wazi sasa Serikali ina mpango gani wa kuiwezesha kwa sasa ili ufanisi uwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Tanzania *Atomic Energy Commision* kwa Zanzibar ipo ndani ya Ikulu ya Zanzibar na imekuwa ikishindwa kutoa huduma kwa wahitaji kutokana na eneo hilo kiusalama. Ni kwa nini Serikali haioni umuhimu wa ofisi hii kuwekwa katika maeneno ambayo itawahudumia wahitaji kwa uhuru zaidi? Je, serikali ina mpango gani wa kuipatia *TAEC* ardhi ya kudumu ili waweze kujenga ofisi zao za kudumu huko Zanzibar? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TAEC* haina maabara na hivyo kwa wahitaji wa huduma kutoka *TAEC* hulazimika kupeleka Arusha na hawapati huduma yoyote Zanzibar kwani hakuna huduma ya maabara Zanzibar. Je, Serikali haioni upo umuhimu kwanza wa kutambua kuwa ofisi hii inatakiwa kupewa hadhi sawa kama ya Arusha kwani ni ofisi ya upande mmoja wa Muungano na sio ofisi ya kikanda *(zonal office)*. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kujenga maabara ndogo kwa ajili ya…

*(Hapa kengele ililia kuashiria*
*kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kipande kilichobakia kirekodiwe kwenye *Hansard* kama kilivyo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

**Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa Fedha 2014/2015 kama ilivyowasilishwa Bungeni**

## HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MHESHIMIWA MOHAMED HABIB JUMA MNYAA (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA- WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

(Inatolewa chini ya kanuni za kudumu za Bunge, kanuni ya 99(9) toleo la Mwaka 2013).

### 1.0 UTANGULIZI

**1.1 Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote namshukuru Mola mtukufu Subhana wa taala kwa kunijaalia mimi na nyinyi mnao nitizama na kunisikiliza kuwa na afya, uzima na kutimiza wajibu wetu uliotuweka hapa Bungeni.

**1.2. Mheshimiwa Spika,** pia nichukue nafasi hii kumuomba Mwenyezi Mungu atujaalie sote wenye nia njema na nchi hii atupe moyo wa uvumilivu na subira na azijaalie nyoyo zetu kutatua matatizo yetu kwa njia ya busara, amani na upendo kwa pande zote mbili za jamuhuri ya muungano na atubainishie wabaya wetu kama alivyokwisha tubainishia baadhi yao ili na wao tuweze kuwanasihi na mola atusaidie kuwabadili nia zao mbaya ili Tanganyika na Zanzibar zifaidi haki sawa kwa pande zote mbili za Muungano bila ya ubaguzi wa ukubwa wa eneo rangi za watu , utamaduni na dini zetu.

**1.3. Mheshimiwa Spika**, Naomba pia kwa ruhusa yako niwashukuru Wananchi wa Mkanyageni kwa ushirikiano wanaonipa na uvumilivu wao wakati sipo jimboni kwa shughuli za kibunge,pia nawashukuru wananchi wote wa Majimbo ya Zanzibar kwa uvumilivu wao waliousubiri fedha ya mfuko wa Jimbo iliyofanyiwa varange sasa fedha
zimeshawekwa katika akaunti za kila Jimbo baada ya kucheleshwa kwa miezi mitano kwa sababu wazijuzo wao Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na yale tulioahidi sasa yatatekelezwa vizuri.

**1.4. Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuanza kutoa mtazamo wetu juu ya bajeti ya Wizara hii, naomba kutoa pongezi na shukrani zangu za dhati kwa viongozi wetu wakuu wa vyama hususani CUF, CHADEMA na NCCR MAGEUZI na kwa kuamua kwa dhati kufanya kazi ya kuwasaidia watanzania kwa pamoja, lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Freeman Mbowe Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuniteua kuwa Waziri kivuli wa Wizara ya Mawasiliano sayansi na Tekinolojia na kuwa msemaji wa kambi rasmi ya upinzani katika wizara hii muhimu, ninaamini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nitatumika kwa uaminifu ili kuweza kulikwamua taifa letu na kuitendea haki Kambi ya Upinzani.

**1.5. Mheshiwa Spika**, baada ya dua hiyo na shukrani kwa Jimbo sasa nianze kuichambua, kuihoji na kuishauri Serikali kuhusu Bajeti ya Wizara hii ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

## 2.0 MAJUKUMU NA DHAMANA YA WIZARA

**2.1 Mheshimwa Spika**,Kabla ya yote ni vyema **KUDURUSU** majukumu ya msingi ya Wizara hii ili Waheshimiwa Wabunge wako wapate nafasi ya kukumbuka ili wakichangia waitendee haki Wizara hii. Pamoja na mambo mengine ambayo ni utaratibu wa kawaida wa kila wizara, majukumu ya msingi ni kama yafuatayo:-

i. Kuhakikisha teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Sayansi, Teknologia na Ubunifu vinachangia katika kukuza maendeleo ya taifa hili.

ii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera za Posta na Mawasiliano ya simu.

iii. Kuandaa na kusimamia Sera ya Sayansi, Teknologia na Ubunifu.

iv. Kusimamia upatikanaji na matumizi ya Sayansi na Teknologia katika uzalishaji na huduma

**v.** **KUHAULISHA** (transfer into practice) matokeo ya utafiti yenye kuchochea ukuaji wa Sayansi na Teknologia.

vi. Kuratibu na kusimamia uandaaji na upatikanaji wa wataalam wa ndani katika fani za Sayansi na Teknologia.

vii. Kusimamia kwa kuziimarisha taasisi za Teknologia kimaendeleo nchini.

viii. Kusimamia maswala ya Teknologia ya Habari na Mawasiliano nchini.

ix. Kurejea na kusimamia utekelezaji wa sera ya Teknologia ya Habari na Mawasiliano ili sekta hii iweze kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**2.2 Mheshimiwa Spika**, wizara hii pia inayo wajibu na dhamana ya kusimamia **MASHIRIKA**, Tume na kampuni zilizo chini yake ambazo zinachangia katika kuyafikia malengo na matarajio ya wananchi . Taasisi zenyewe zilizo chini ya Wizara ni zifuatazo:-

a. Taasisi ya Teknologia Dar-es-salaam (DIT).

b. Chuo kikuu cha Sayansi na Teknologia Mbeya

c. Taasisis ya Sayansi na Teknologia ya Nelson Mandela (NM- AIST)
d. Tume ya nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC)
e. Tume ya Sayansi naTeknologia(COSTECH)
f. Kampuni ya simu Tanzania (TTCL)
g. Shirika la Posta Tanzania (TPC)
h. Mamlaka ya mawasiliano Tanzania (TCRA)
i. Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCAF)

**2.3. Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo,Wizara hii iliasisiwa tarehe 7 Februari 2008 kwa kuunganishwa kwa Idara ya Mawasiliano iliyokuwa chini ya Wizara ya Miundombinu na Idara ya Sayansi na Technolojia iliyokuwa chini ya Wizara ya Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia. Halkadhalika, Wizara iliundwa tena tarehe 17 Disemba 2010 kupitia tangazo la Serikali Na 494, Wizara ilikabidhiwa tena majukumu niliyoyataja hapo awali.

## 3.0 MAELEZO YA JUMLA KUHUSU WIZARA YA MUUNGANO MASHIRIKA AU TAASISI ZAKE ZA MUUNGANO.

**3.1 Mheshimiwa Spika**, Katika kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kilichokaa tarehe 31/05/2011 na tarehe 01/06/2011 kujadili utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mawasiliano,Sayansi na Teknolojia pamoja na Bajeti ya mwaka 2011/2012, ***miongoni mwa maagizo ya Kamati ilikuwa ni kuitaka Wizara hii ya Muungano iwe na sura ya Muungano na ionekane wazi.***

Katika utekelezaji wa agizo hili, Serikali ilijibu kwamba Wizara hii inasimamia masuala ya Muungano kama ilivyoorodheshwa katika Ibara ya Nne (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kama ilivyofafanuliwa katika nyongeza ya kwanza ya Katiba hii kuhusu mambo ya muungano.

**3.2 Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa jibu hilo la Serikali mambo mengine yaliyotajwa katika nyongeza ya kwanza ni la (14)-Elimu ya Juu, (16)-Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania na mambo yote yanayohusika na kazi za Baraza hilo na ( 18)-Utafiti.

**3.3 Mheshimiwa Spika,** Kwa maana hiyo, hapa tunapata maswali mengi ya kujiuliza ambayo hapana budi yanahitaji majibu **sahihi ya Serikali**,nayo ni kuwa DIT, NM-AIST na MUST kimsingi vyote vilikuwa ni vyuo vya ufundi sawa na Karume Technical Colleague cha Zanzibar ambacho sasa hivi kinajulikana kama **Karume Institute of Science and Technology** na vyote ni vya elimu ya juu. Ni kwanini basi Chuo hiki kisijumuishwe katika majukumu ya msingi ya Wizara hii

kama hivyo vyengine? Ikiwa sababu ni ya umiliki kwamba kinamilikiwa na SMZ basi na hivyo vyengine vinamilikiwa na upande mwengine wa Muungano (Tanganyika au Tanzania Bara) lakini kwa nini **huduma** zinazotolewa na Wizara hii ya Muungano pamoja na ujenzi wa majengo mapya, vifaa vya utafiti, maabara za uchunguzi na mambo mbali mbali, Wahadhiri na kadhalika zinatafauti kubwa au hazipo kabisa kwa upande wa KIST?

**3.4. Mheshimiwa Spika,** Kama hayo hayatoshi pia katika taarifa ya Wizara hii ya tarehe 1/5/2014 uko mradi wa kuunganisha Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti (Last Mile connectivity –STHEP) kwa ajili ya kufanikisha elimu mtandao ambao umejumuisha taasisi 27 za Tanzania Bara vikiwemo vyuo Vikuu binafsi lakini ni Chuo Kikuu kimoja tu cha Zanzibar ambacho ni SUZA ndicho kilichotajwa kuwemo katika mpango huu? Sababu zipi zilizotumika hata ikawa Karume Institute of Science and Technology (KIST) na Vyuo Vikuu vyengine vya Zanziba visijumuishwe katika mpango mtandao huo? Moja kati ya jukumu kuu la Wizara hii tumeshaona hapo awali kuwa ni … ***Kusimamia kwa kuziimarisha taasisi za Sayansi na technolojia.*** Kwa kuwa haikutajwa popote kusimamia na kuziimarisha taasisi za Sayansi na Teknoloji za Tanzania Bara pekee maana yake tatizo linakuja katika utendaji wa Wizara yako ambao pamoja na wale walio sababisha siku za nyuma lakini na wewe mwenyewe Waziri mmeshindwa kusimamia majukumu ya Wizara hii uliyopewa ipasavyo? Ikawa na sura ya Muungano kama agizo la kamati tulilolisoma mwanzo.

**3.5. Mheshimiwa Spika,** Kwa taarifa ya Bunge lako KIST kilijengwa kwa msaada wa Serikali ya Marekani kilikusudiwa kuwa Chuo Kikuu ambacho mimi mwenyewe na Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ni matunda ya Chuo hicho. Elimu ya Juu toka 1964 kwenye nyongeza ya kwanza ya Katiba ni suala la Muungano hakikuendelezwa hadi hivi leo na eneo liko wazi, je ni nini kama si kudhoofisha elimu upande mmoja wa muungano? Hii elimu ya juu ambayo ni ya muungano wapi ilipoelezwa mipaka yake na sheria ipi? Maana katika katiba limetajwa tu.

## 4.0 UCHAMBUZI WA BAJETI

**Mheshimiwa Spika,** Ili kujua vizuri utaratibu wa fedha zinazoombwa na kuidhinishwa na Bunge lako tukufu na zile zinazopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia ni vyema tuangalie mtiririko wa miaka mitano iliyopita ili sote tujiridhishe na ufanisi wa Wizara hii muhimu katika kukuza wataalam,tafiti na maendeleo ya kisayansi na teknolojia kwa ukuwaji wa uchumi wa nchi yetu.

**4.2. Mheshimiwa Spika**, Ukiangalia jedwali namba 1 kwa umakini utagundua kwamba katika kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita yaani kuanzia mwaka fedha 2009/2010 hadi 2013/2014, ni miaka miwili (2) ya mwanzo tu Wizara hii iliweza kutimiza malengo yake ya kimaendeleo ambapo fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako iliweza kutolewa kwa asilimia 97.4 katika matumizi ya kawaida na asilimia 74 katika matumizi ya maendeleo. Hii inatokana pamoja na mambo mengine ni uwezo wa Serikali kupanga bajeti ya maendeleo kwa kiwango ambacho ilikaribia kukimudu cha bilioni 13.9. Katika mwaka uliofuata 2010/2011 hali haikuwa mbaya sana kwakuwa matumizi ya kawaida yaliweza kupatikana kwa asilimia 82 ambapo kwa upande wa maendeleo fedha iliweza kupungua na kukaribia angalau asilimia 50.

**4.3 Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha miaka mitatu (3) mfululizo iliyofuata mambo yalianza kuharibika ambapo Wizara hii imeshindwa kutoa taarifa kwa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusiana na kiasi gani

kilichotolewa na Serikali kulinganisha na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako katika matumizi ya **kawaida(**mishahara na matumizi mengineyo**)**.Jambo hili haliwezi kuwa ni bahati mbaya yumkini kuna jambo linalofichwa kwakuwa ni desturi iliyozoeleka kwa Wizara zote na kwa miaka yote kuonesha mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka uliopita kabla ya kupitisha bajeti ya mwka husika.

**4.4 Mheshimiwa Spika,** Yumkini matumizi ya kawaida yalizidi kiwango kilichoombwa katika OC kwakuwa hatujawahi kusikia wafanyakazi kulalamika kukosa mishahara kwa maana hiyo hakukuwa na upungufu wa fedha bali kulikuwa na matumizi yaliyozidi kiwango kilichoidhinishwa na ndio maana Waziri akashindwa kutoa kiwango cha asilimia ya fedha zilizopatikana. Kwa maana hiyo Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi wa jambo hili kwa kuwa katika viambatisho vyake vyote kwa miaka mitatu matumizi hayo yamefichwa na hili limetokea yeye akiwa Waziri wa Wizara hii.

**4.5 Mheshimiwa Spika,** Kwa kuchambua bajeti ya maendeleo ya Wizara hii muhimu ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia ndiyo itakayotoa mwangaza wa kuona nini kinafanyika kule ndani ya Wizara hii. Mfano huu unaoonyesha mtiririko wa miaka mitano ya utendaji wa Wizara hii utatoa picha fulani ya kujitambua namna ya malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na kuondoa Umasikini (Mkukuta) yanavyo tekelezwa na kwa kiasi gani kama upo uwezekano wa kufika huko tulikokusudia kwa kipindi tulicho jiwekea.

**4.6 Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa jedwali No 2 linavyoonyesha kwa muda wa miaka mitano iliyopita ni mwaka 2009/2010 na mwaka 2012/2013 tu ndio kazi zilifanyika na Miradi ya Maendeleo ikatekelezwa kama ilivyo pangwa haizuru baadhi yake haikuweza kukamilika vizuri. Lakini miaka ya 2010/2011, 2011/2012 na mbaya zaidi 2013/2014 fedha za maendeleo zilizopatikana iwe za ndani au za nje zilikuwa chini ya asilimia 34 na nyengine hadi asilimia 10. Huu ni utendaji mbovu unaosababisha miradi takriban yote ya Wizara hii kukwama na kusababishwa kuachwa nyuma na hata majirani zetu wasio na rasilimali kama sisi.

**4.7. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inahitaji majibu kwa maswali yafuatayo:

a. Malengo ya Dira ya Wizara hii yatafikiwa?
b. Malengo ya Dhima ya Wizara yatatimizwa?

***Dira ya Wizara***: Kuwa na Jamii yenye maarifa yaliyojengwa katika misingi thabit yenye kuipa Jamii Uwezo,Ustadi na Umahiri ili kuweza kunufaika na Sayansi , Teknolojia na Ubunifu, katika kuleta mageuzi yatakayotupatia uchumi endelevu wenye kuhimili ushindani wa Kimataifa.

***Dhima ya Wizara***: Kuwezesha upatikanaji wa Rasilimali Watu na uibuaji wa maarifa mapya ili viweze kusaidia katika kuleta utajiri wa nchi uliojengwa juu ya misingi imara na endelevu inayotokana na sera zenyekutoa fursa ya kuiendeleza Sayansi, teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

## 5.0 UCHAMBUZI WA TAASISI NA MIRADI MBALI MBALI

### 5.1 Mradi wa Anuani za Makaazi na Simbo za Posta

**5.2. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ilitoa agizo katika Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 la kuanzishwa kwa anuani za Makaazi na postikodi ambapo kila mwananchi ataweza kujitambulisha kwa kutumia jina la mtaa, nambari ya nyumba pamoja na postikodi ya eneo analoishi.Katika kutekeleza agizo hili, Wizara hii iliiagiza Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) kusimamia utekelezaji wa mfumo huu. Kamati ya Kitaifa ya Uratibu na utekelezaji wa mfumo huu iliundwa na wajumbe wake ni Makatibu Wakuu wafuatao kwa kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge na Wananchi:-

-Katibu Mkuu Wizara ya Mawasiliano,Sayansi na Teknologia -Mwenykiti.
- Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) – Mjumbe
- Wizara ya Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makazi – Mjumbe
- Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano Zanzibar –Mjumbe
-Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa Zanzibar - Mjumbe
- Wizara ya Mambo ya Ndani - Mjumbe
- Wizara ya Fedha - Mjumbe
- Mkurugenzi Mkuu TCRA - Mjumbe
-Postamasta Mkuu - Mjumbe
- Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) -Mjumbe
-Mkurugenzi Mkuu, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) – Mjumbe.

**5.3 Mheshimiwa Spika,** Mpango huu ulianza kwa majaribio mwaka 2008/2009 katika kata nane huko Arusha na mwaka 2010/2011 katika kata nane za Manispaa ya Dodoma na changamoto zilizojitokeza hasa za mipango miji na ujenzi holela zilisaidia kuboresha mipango ya utekelezaji katika miji mengine. Kwamujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa TCRA aliwahi kusema kwamba wamemaliza kutengeneza mfumo wa "Programmimng" wa POSTAL CODE katika "Global Positioning System" (GPS) ambapo nchi iligawanywa katika anuani za posta saba(7) kama ifuatavyo:-

- Dar es Salaam - 1
- Arusha,Kilimanjaro,Tanga na Mnyara - 2
- Mwanza,Mara,Kagera na Shinyanga - 3
- Kigoma,Dodoma na Tabora - 4
- Iringa,Mbeya, na Rukwa - 5
- Mtwara, Ruvuma na Lindi - 6
- Zanzibar (Unguja na Pemba) - 7

**5.4 Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa taarifa za Mkurugenzi Mkuu wa TCRA za tarehe 5/6/2012 alisema baada ya majaribio ya Arusha na Dodoma na kumaliza kazi ya GPS sasa wako tayari kwa nchi nzima na TCRA itatenga fedha katika bajeti ya mwaka ujao yaani 2012/2013 kupitia Serikal za Mitaa. Fedha hizo zitatengwa kwa mpangilio kupitia TAMISEMI hadi mwaka **2014 ambapo**

**mradi huu utamalizika.** Makadirio ya mwaka 2009 ulitarajiwa kugharimu Tsh bilioni 158,na kwa mujibu ya hotuba hii ya Waziri makadirio hayo bado hayajaoongezeka.

Jedwali Namba 3 hapa chini linafafanua fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako na fedha halisi iliyopatikana kwa utekelezaji wa mradi huu.

**5.5 Mheshimiwa Spika,** Leo tunapitisha bajeti ya Wizara hii ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia, mwaka wa fedha wa 2014 unamalizika na kuanza mwaka mwengine.Kambi Rasmin ya Upinzani inataka kufahamu na Watanzania wasikie kuanzia mwaka 2009 wa majaribio na ahadi zote za Wizara hii ni kanda ngapi kati ya hizo saba zlizokamilisha anuani za makazi na simbo za Posta? Kwakuwa Kamati ya Kitaifa ya Uratibu na Utekelezaji wa mfumo huu ni nzito sana ambayo mimi sijawahi kuona katika maisha yangu ikiongozwa na Makatibu Wakuu niliowataja hapo mwanzoni akiwemo Katibu Mkuu Wizara ya Fedha nini basi kimekwamisha mradi huu ambao ulitakikana kumalizika mwaka huu 2014? Ikiwa tutapewa jibu la kwamba mwaka 2014 bado hauja malizika jee huo muda uliobakia Waziri atalihakikishia Bunge lako hili muda uliobakia upo uwezekano wa kukamilisha Mradi huu kwa Tanzania nzima wakati maeneo uliokamilika takribani ni machache mno?

**5.6 Mheshimiwa Spika,** Nimeuliza masuala hayo yote kutokana na umuhimu wa juu na faida za mradi huu kiuchumi,kibiashara,kisiasa,kiusalama na utoaji huduma mbali mbali za jamii(umeme,maji,gesi,huduma za kifedha,usambazaji wa barua na vifurushi n.k). Mfano mzuri ni Mabenki na

ukusanyaji wa kodi mbali mbali. Katika **shida** moja kubwa ambayo **mabenki** yetu wanaipata katika utoaji mikopo na huduma ni suala la KYC (know your customer)- kumtambua mteja wako(physical addresses) ambapo wateja wote kuwa na mfumo unaolingana wa KYC hasa katika uzuiaji wa fedha haramu (Implementation of Anti money Laundering Regulations (AML) bila ya kujali nchi anayotoka.

**5.7 Mheshimiwa Spika**, Mradi huu wa Anuani na Simbo ulitakikana uende sambamba na Mradi wa Vitambulisho vya Taifa (National Identification Cards). Haya yote yakitekelezwa yatasaidia ukuaji wa Uchumi wa Taifa kwa kuwatambua walipa kodi na ndio maana jirani zetu wa Kenya wanalipia asilimia 95 ya bajeti yao kupitia kodi wanazozitoza kwa Wananchi.

**5.8. Mheshimiwa Spika,** Katika hatua hii, Kambi Rasmin ya Upinzani inashidwa kufahamu ni kwanini miradi yote hii miwili inasuasua hadi hivi leo? Sera ya Taifa ya Posta inafahamika tangu mwaka 2003, taratibu za kuanza Mradi huu zilianza mwaka 2008/2009 hadi hivi leo ni miaka 6 tayari ni chini ya asilimia 5 kama zinafika utekelezaji wake.

1. Jee Wizara yako au Serikali haijui umuhimu wa Mradi huu?
2. Je Zanzibar imetekeleza kiasi gani?
3. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo ya kina kwa hatua zote zilizochukuliwa na Serikali inaahidi nini na lini Miradi hii yote miwili itakamilika? Vinginevyo tuseme Serikali ya CCM imeshindwa?
4. Jee hatuoni aibu kwamba katika Mkutano wa Umoja wa Posta Duniani uliofanyika Oktoba 2012 huko Doha,Qatar uliozungumzia uhamasishaji wa Mfumo wa Anuani za Makazi kutumika katika nchi zote wanachama ambapo Mhe Anna Kajumulo Tibaijuka(Mb),Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi aliteuliwa kuwa Balozi Maalum wa uhamasishaji Anwani za Makazi na Simbo za Posta Duniani lakini nchi yake mwenyewe bado haijahamasika na utekelezaji unasuasua?

## 6.0 MKATABA WA POSTA AFRIKA (PAPU)

**6.1. Mheshimiwa Spika**, Habari nyengine inayohusiana na posta ambayo nitaizungumza kwa kifupi sana ni Azimio la kuridhia Mkataba wa Posta Afrika (PAPU) lilopitishwa na Bunge lako hapa Dodoma mwaka 2012. Serikali ilieleza kwamba iwapo Bunge litardhia Azomio hilo la Mkataba wa PAPU basi nchi yetu itapata manufaa makubwa.Tanzania ni Makao Makuu ya Umoja huu na imeshatoa eneo la kujenga ofisi za kudumu jijini Arusha kama ilivyoelezwa katika ibara ya 4 ya Mkataba huo na kwamba Bunge likiridhi Tanzania itanufaika na kuwa mwenyeji wa Umoja huo.Pia ilielezwa kunufaika katika kubadilishana utaalamu,mafunzo,ufundi na tafiti mbali mbali zitakazoongeza tija kwenye

shirika letu la posta. Hizo ni faida chache kati ya faida nyingi zilizoelezwa na Serikali.

**6.2. Mheshimiwa Spika**, Azimio la Mkataba wa Posta wa Afrika wa mwaka 2009 uliridhiwa kwa kauli moja na Bunge lako na kwakuwa kiwanja cha kujenga Makao Makuu hayo ya PAPU kilipatikana na kuzunguushiwa uzio huko Arusha ni kwanini sasa jengo hilo halijajengwa hadi hivi leo mbona maendeleo ya ujenzi huo haujaripotiwa tena na wizara yako.

## 7.0 MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA(TCRA) & MKONGO WA TAIFA

**7.1. Mheshimiwa Spika**, Ni jambo linalotia matumaini na kuleta faraja na kwa maana hiyo tuipongeze Wizara kwa kufanikisha kwa kiasi fulani mradi wa Mkongo wa Taifa. Mradi ambao ulianza mwaka 2004 na utekelezaji ukaanza mwaka 2005 katika ngazi ya upembuzi yakinifu,utekelezaji wa kazi halisi ya kuchimba na kulaza Mkongo wenyewe awamu ya kwanza Februari 2009 hadi Juni 2010 ambapo jumla ya kilomita 4330 zilikamilika.Awamu ya pili iliyoanza Agosti 2010 hadi Machi 2012 ambapo jumla ya kilomita 3230 zilikamilika. Kwa upande wa gharama za Mkongo imeripotiwa kwamba awamu ya kwanzana ya pili zimegharimu fedha za nje USD milioni170 ambzo ni mkopo wa masharti nafuu kutoka Exim Bank ya China pamoja na fedha za ndani Tsh.17.712.000.000/-

**7.2. Mheshimiwa Spika**, Katika taarifa zilizotolewa katika hotuba ya Waziri katika bajeti ya 2009/2010 kuwa faida za mkongo ni pamoja na kuboresha matumizi ya simu za viganjani,kusimamia mfumo mpya wa digitali,kuanzisha rejesta ya utambuzi wa vifaa vya mawasiliano,kusimamia usajili wa simu za viganjani ,kuhimiza na kuwezesha matumizi ya pamoja ya miundombinu ya mawasiliano. Halkadhalika Mkongo huu utaziunganisha na mikongo ya kimataifa ya baharini ikiwemo SEACOM,UHURUNET,UMOJANET,EASSy na TEAMS. Wakati huo huo katika taarifa ya mwezi Mei 2014 kwa kamati ya kudumu ya Miundombinu kwa ajili ya matayarisho ya bajeti ya mwaka huu, Mkongo huu umeunganishwa na mikongo ya baharini ya SEACOM na EASSY tu.

**7.3. Mheshimiwa Spika**, Wananchi waliamini kauli hizo za wizara hii na tulifahamu kitendo cha kuunganishwa na mikongo mingi ya baharini ni katika kuleta kuaminika (reliability),ubora wa huduma(efficiency) na kuzuia kukatika mawasiliano kwa kuwa na “ring circuit”. Kwakuwa ubora wa mawasiliano haujapatikana, picha katika runinga(TVs) nyingi nchini zinakatika katika,zinaganda zinaonyesha vivuli vya ajabu, mawasiliano katika Mabenki mara nyingi unaambiwa usubiri mtandao uko chini, pia katika ATMs na huduma nyingine zinazotumia teknolojia ya mawasiliano pamoja na kuhakikishiwa kwamba Mkongo wetu umejengwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa

vinavyosimamiwa na ITU(International Telecommunication aaaunion). Hapa tunapata mashaka nakujiuliza maswali mengi ambayo Mheshimiwa Waziri hanabudi kulielezea Bunge lako kwa viwango vinavyoridhisha pia. Kwanza , ni kwanini Mkongo wetu umeunganishwa na mikongo ya kimataifa miwili tu (SEACOM na EASSy) vipi kuhusu mikongo mengine tuliyoarifiwa mwanzoni ya **uhurunet**,**umojanet** na **teams** ?Pili ,kwa nini basi kutokee udhaifu wa mawasiliano nilioutaja hapo juu? Tatu, kwa nini kuwe na viwango tofauti baina ya kampuni za simu?

**7.4. Mheshimiwa Spika,** Udhaifu huo nilioutaja ulikwisha kuripotiwa na Kamati ya Bunge ya Miundombinu na kutoa agizo kwa Mheshimiwa Waziri na majibu ya Waziri kwa Kamati alisema ubora wa mawasiliano umewekewa kanuni EPOCA Quality of Service Regulations ambazo zinaainisha kiwango cha ubora lakini hadi hivi leo Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wanashuhudia kuendelea kuona matatizo hayoyakiendelea.Kwa hivyo nini kauli ya Serikali kwa Wananchi kuhusiana na matatizo hayo kuendelea?

## 8.0 AMRI YA SERIKALI KUHAMA KUTOKA KWENYE MFUMO WA ANALOJIA KWENDA KWENYE MFUMO WA DIJITI

**8.1. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) iliamuru vituo vyote vya Televisheni nchini kuzima mitambo ya analojia na kuvilazimisha kuingia kwenye mfumo mfumo mpya na wakisasa wa dijiti ambao unatumia ving'amuzi (Receivers) kupata mawimbi ya televisheni, katika taarifa ya Waziri mbele ya kamati ameiambia kamati juu ya tathmini ya utekelezaji wa amri ya serikali, katika taarifa yake pamoja na serikali kutoa takwimu zisizo sahiohi kwa mujibu wa uhalisia wa jinsi zoezi hili lilivyoathiri wananchi hususani katika kupata haki yao ya kupata habari ambayo ipo kikatiba, bado serikali imekiri kuwa takwimu hizo ambazo hazina uhalisia kuwa asilimia 5.5 ya wananchi walibainika kushindwa kumudu gharama za ving'amuzi licha ya serikali kuondoa import duty katika ving'amuzi.

**8.2. Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kuwa zoezi hili lilifanyika katika mikoa ya Dar Es Salaam, Dodoma, Mwanza,Tanga, Moshi, Mbeya na Arusha, Pamoja na tathmini hiyo kufanyika serikali iliingia katika utekelezaji wa kuzima mitambo katika mikoa mingine kama Singida, Tabora, Musoma , Bukoba, Kigoma, Morogoro, Kahama, Iringa na Songea, Serikali hii ya CCM sasa imekuwa ni kawaida kwake kuamua kuvunja katiba na kuwanyima haki wananchi wake kupata habari, ni vema sasa serikali hii kutambua kuwa swala la wananchi kupata habari ni la lazima kwani lipo kikatiba na hivyo serikali lazima itambue kuwa ipo kwa ajili ya kulinda katiba ya nchi na hivyo inawajibika kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**8.3. Mheshimiwa Spika**, pamoja na tathmini iliyofanyika na serikali, haijaeleza matatizo yaliyojitokeza katika ving'amuzi ambavyo vimeuzwa kwa wananchi, taarifa inaeleza juu ya takwimu za wananchi walionunua na walioshindwa, lakini ukweli ni kwamba hata walioweza kununua pia wamekutana na changamoto ya ving'amuzi hivyo kuzima na kukatika mara kwa mara, lakini kambi ya upinzani katika kipindi cha mwaka 2013 ilipohoji juu ya kukatika kwa matangazo majibu ya serikali yalikua ni kama ifuatavyo, na pia yalinukuliwa katika hotuba ya upinzani "***Wananchi wawasiliane mara moja na watoa huduma za ving'amuzi ili kuwasaidia kupata ufumbuzi***" taarifa hii ilitolewa na kutiwa saini na Mh. Profesa Makame Mbarawa waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia tarehe 2 April,2013 kauli ambayo iliisikitisha kambi rasmi ya upinzani Bungeni kwani Serikali ilitoa leseni kwa watoa huduma kwa umma hivyo ilitakiwa kuwajibika kuwa watoa huduma wanatoa huduma hiyo kwa uhakika.

**8.4. Mheshimiwa Spika**, hadi sasa tatizo la kukatika kwa matangazo bado limeendelea katika maeneo ambayo yamefikiwa na huduma hii, hivyo ni wazi kuwa wananchi wengi hukosa habari kutokana na kukatika kwa matangazo hayo, hivyo kutopata haki yao kikatiba ambayo kimsingi serikali haijaweka mazingira wezeshi ya kuwapa wananchi wake haki ya kupata habari ambayo ni ya kikatiba.

**8.5. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwanza inaitaka serikali kufanya tathmini ya ufanisi wa huduma hii kabla ya kujielekeza kuangalia takwimu za wananchi walionunua vifaa hivyo vya mfumo mpya, Pili TCRA ifanye ukaguzi wa uwezo wa matangazo kwa ving'amuzi vyote katika makampuni yaliyopewa leseni ya kufanya biashara hiyo nchini, Tatu serikali iliambie bunge lako tukufu je nini tafsiri asilimia 5.5 ya wananchi walioshindwa kumudu kuhama kutoka mfumo wa analojia kuelekea digiti? Haioni kuwa idadi kamili ya asilimia 5.5 ya watanzania ni watu 2,475,000 ambao kuwanyima haki wananchi hawa hawastahili kupata habari? Je watu hawa ni kidogo leo kwa CCM wakati wa kura mtu mmoja anathamani lakini kukosa habari haina tija.

## 9.0 GHARAMA ZA MATANGAZO BAADA YA KUPATA MKONGO

**9.1. Mheshimiwa Spika,**Katika taarifa ya Wizara kwa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusiana na gharama au bei za huduma za Mkongo, alisema zilipatikana baada ya kufanya utafiti wa kina na zilifanywa na mshauri mwelekezi OVUM ya Uingereza kwa kushirikiana na TTCL na mapendekezo ya bei hizo kuridhiwa na Wizara.

**9.2. Mheshimiwa Spika,** Sekta ya mawasiliano inakua kwa kasi kubwa na huenda Tanzania ikawa ya pili kwa Afrika ya Mashariki na Kati ikitanguliwa na

Kenya katika fedha za mtandao(mobile money).Pamoja na mafanikio hayo bado matumizi ya TEHAMA yana nafasi kubwa katika kunyanyua uchumi wa kila Raia na Taifa kwa jumla. Matumizi hayo ni pamoja na 'electronic procurement' kama Dubai kupitia Shirika lao la TEJARI ambalo limeweza kupunguza gharama za manunuzi kwa asilimia 30,tele medicine kama India hasa Jimbo la Hydrabad ambapo Wananchi vijiji wanapata tiba bila ya kufika Hospitali Kuu,eco farming Zimbabwe ambayo inatumia kwa kuwapati mikopo na pembejeo wakulima wa vijijini.Pia katika kukuza Mapato kudhibiti wizi wa Fedha na ufisadi,uanzishwaji wa Tele Visa na E passport yote hayo wenzetu wanayafanya kuongeza mapato.

**9.3. Mheshimiwa Spika**, Wakati TCRA ikiwahamasisha wawekezaji, utowaji wa mawimbi (frequencies) yalikuwa yakitolewa kulingana na uwepo wake. Matokeo yake walipewa lakini wapo wawekezaji ambao wameshindwa kuwekeza. Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri awanyanganye wale wote waliohodhi mawimbi hayo na kuanzisha utaratibu wa kuyauza kwa mnada. Mheshimiwa Spika Mawimbi ya 4G/LTE ni teknolojia ambayo mawimbi yake yana bei kubwa na inashangaza kuona baadhi ya nchi mawimbi hayo yanauzwa kati ya USD Milioni 50 hadi USD Milioni 110, na kwa dunia ya kwanza milioni 950, wakati hapa petu yanauzwa kwa USD Milioni 3. Hili ni jambo la kushangaza, hivyo tunamtaka Waziri atoe ufafanuzi ili aweke wazi kwamba hakuna harufu ya rushwa katika jambo hili?

**9.4. Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kuanza kutumia Mkongo wa Taifa na unafuu ukapatikana kwa kiwango alichotoa mfano Mheshimiwa Waziri cha 2Mbps kwa njia isiozidi kilomita 1000 kutoka Dar es Salaam kuwa USD 160 badala ya zamani ya USD 16790 kwa nji ya 'microwave'bado yanayofaidika ni makampuni ya katikati yanayounganishwa na mkongo sio wateja wa mwisho wa kawaida. Mfano mzuri ni viwango vinavyo tafautiana hadi hivi sasa baina ya makampuni ya simu ,kutoka mtandao mmoja kupiga simu mtandao mwengine na kubwa zaidi pale watu wlipokua wanatumia Settelite Dish ambapo tulikuwa tunatumia 'receiver'(kingamuzi) na LNB na hakuna malipo mengine yoyote. Lakini leo hii watu wanalazimika kununua kingamuzi(receiver) ndiyo aone matangazo ya TVs na kulazimika kulipia ada ya mwezi ya Tsh 10.000/- hadi Tsh50.000 kamailivyo kwa Startimes. DSTV na kadhalika tena bila ya ahadi yakupatikana TVs zote za ndani kama vile CH 10,ITV,TBC,Star TV n.k. Kwa nini TCRA inashindwa kudhibiti hali hiyo? Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri alitolee ufafanuzi na kulirekebisha mara moja jambo hili kwa kuwa haki ya kupata habari ni ya kikatiba. Pia Kambi ya Upinzani tunamtaka Waziri atueleze kwa nini vingamuzi kama vile vya ARISAT,MEDIACOM,STAR TRAC,TECHNOSAT vinapatikana na vinaonesha TVs zote za ndani bila ya gharama yoyote ya mwezi lakini vingamuzi vya STAR TIME,CONTINENTAL,DIGITECH,AZAM TV vilipiwe

kwa kila mwezi? Jee hii ndio nafuu ya Mkongo wa Taifa tulioletewa? Maana makampuni haya baada ya kuhamasishwa na TCRA.

**9.5. Mheshimiwa Spika**, Kambi ya Upinzani pia inamtaka Waziri kurekebisha TCRA iwe na sura ya muungano na sio kwa kuwa na wajumba wa Bodi tu bali kwa uwakilishi na kiutendaji isirudie makosa yaliyopita wakati ule haijaunganishwa kwa Tume ya Mawasiliano na Tume ya Utangazaji ambazo ndizo zimefanya TCRA wakati Zantel ilipowekeza Zanzibar na kuwekewa vikwazo vingi hata Zanzibar kudai ITU irejeshee namba yake ya kimataifa ya 259.Pamoja na juhudi hafifu zinazo fanywa vile vile kwa COSTECH na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC)

**9.6. Mheshimiwa Spika**, Baada ya COSTECH kufunguliwa June 2012 na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, na sasa ofisi imeazimwa sehemu yake ya ndani ya jengo la ofisi ya makamu wa Rais huko Tunguu, mchakato wa kupata ofis yake upo lakini matatizo yaliyopo zaidi ni ufinyi wa watendaji wa ofisi hiyo kwani kuna wafanyakazi watatu tu, ambao wawili wakiwa wa muda.

**9.7. Mheshimiwa Spika**, Swala la fedha za utafiti nalo limekuwa ni tatizo kwa upande wa ofis hii Zanzibar na uwezo wake kwa sasa kufanya tafiti ni mdogo kwani hakuna fedha za utafiti, hivyo mheshimiwa Waziri naomba katika majibu yake aseme ni kwa vipi ofisi hii imekuwa haiwezeshwi kifedha na pia aweke wazi sasa serikali inampango gani wa kuiwezesha kwa sasa ili ufanisi uwepo?

**9.8. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Tanzania Atomic energy Commision kwa Zanzibar ipo ndani ya Ikulu ya Zanzibar na imekuwa ikishindwa kutoa huduma kwa wahitaji kutoakana na eneo hilo kiusalama, ni kwa nini serikali haioni umuhimu wa ofisi hii kuwekwa katika maeneno ambayo itawahudumia wahitaji kwa uhuru zaidi? Lakini pia Je serikali ina mpango gani wa kuipatia TAEC ardhi ya kudumu ili waweze kujenga ofisi zao za kudumu?

**9.9. Mheshimiwa Spika**, TAEC haina maabara na hivyo kwa wahitaji wa huduma kutoka TAEC hulazimika kupeleka Arusha na hawapati uamyeyote Zanzibar kwani hakuna huduma yamaabara Zanzibar, Je serikali haioni upo umuhimu kwanza wa kutambua kuwa ofisi hii inatakiwa kupewa hadhi sawa kama ya Arusha kwani ni ofisi ya upande mmoja wa muungano na sio ofisi ya kikanda (zonal office), hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni inaitaka serikali kujenga maabara ndogo kwa ajili ya kuwezesha huduma kupatikana Zanzibar sio kuwa na kiini macho kilichopo sasa?

## 10.0 UDHIBITI WA MATUMIZI MABAYA YA VYOMBO VYA MAWASILIANO

**10.1. Mheshimiwa Spika,** katika moja ya matukio yaliyowahi kutokea duniani ni pamoja na tukio hili la Marekani mwanzoni mwa miaka ya 1970 enzi

za utawala wa Richard Nixon wa Republican, mwezi Juni 17, 1972 Nixon aliyekuwa anahaha kupata kurejea madarakani kipindi cha pili alijikuta kwenye kashfa baada ya kuhusika kufunika na kuwalinda waliovunja na kuiba siri kwa wapinzani wake,tukio hilo lililokuja kubatizwa baadaye kama kashfa ya Watergate lilijulikana baada ya watu watano kunaswa kwa tuhuma za kuingia kijasusi kupata siri kwenye makao makuu ya ofisi za Democratic zilizoko Hoteli ya Watergate, Washington, D.C, Uchunguzi wa awali wa gazeti la The Washington Post lililopelekewa taarifa kwa siri na Shirika la Upelelezi la Marekani (FBI) ulionyesha watu hao wanahusishwa na ikulu ya White House,hii ilitokana na ukweli kwamba katika kashfa hiyo kamati ya uchaguzi ya Nixon ilihusika.

**10.1. Mheshimiwa Spika**, Kama kawaida ya viongozi wengi, Nixon alitupilia mbali habari hizo akidai kuwa ni propaganda za kisiasa tu na ikulu ilikanusha vikali ikidai ni habari za upande mmoja na za kupotosha,Lakini baadaye FBI ilithibitisha pasipo shaka kwamba wasaidizi wa Nixon walijaribu kuihujumu Democrats na baadhi yao wakaanza kujiuzulu,Nixon aliwekwa katika wakati mgumu bada ya hati ya kiapo ya John Dean kuonyesha rais huyo alihusika na Alexander Butterfield alionyesha katika kiapo kuwa Nixon alikuwa na mfumo wa kurekodi mazungumzo ya simu ndani ya ofisi maarufu kama Oval Office,Kesi ikanguruma, ushahidi ukatolewa na baadaye Aprili 1974, Nixon akasalimu amri akawasilisha mkanda huo wenye kurasa 1,200 aliorekodi mazungumzo hayo, Agosti 8, 1974 Nixon akatangaza wazi kupitia kwenye vyombo vya habari kwamba anajiuzulu na siku iliyofuata yaani Agosti 9, 1974 akaondoka na kumwachia madaraka makamu wake Gerald Ford.

**10.2. Mheshimiwa Spika,** tukio hili linafanana wazi na tukio la Ikulu ya Dar es Salaam kuhusika kulipia tangazo la kukashifu wapinzani wake katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 kupitia mitandao ya simu na magazeti huku TCRA ikikaa kimya kulinda uovu wa wakubwa,  hii ilitokana na SERIKALI kutokutoa tamko la kulaani au kusikitishwa na tukio lile, kampuni za simu za mkononi nazo zilikaa kimya, na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) haikuwa na jibu,ujumbe ambao ulitumwa kupitia Na. +3588976578 na Na. +3588108226 ukikashifu wagombea wa Upinzani na TCRA kukaa kimya.

**10.3. Mheshimiwa Spika,** Nimeeleza undani wa hili na kufanya rejea ya uchaguzi wa mwakla 2010 si kwa lengo la kutaka turudi huko ila ni kuonesha Matukio haya kwa kuendelea kukaliwa kimya ni wazi yanaliingiza taifa katika migogoro isiyo ya lazima, kumekuwepo na taarifa nyingi za ujumbe mfupi zinazotolewa ama na makampuni ya simu au watu binafsi ambao wamesajili kadi za simu na kutuma ujumbe mfupi wa kuchochea chuki dhidi ya dini Fulani Fulani tofauti, kwa kipindi kirefu sasa TCRA haijaweza kuchukua hatua dhidi ya taarifa hizi ambazo madhara yake ni kuligawa taifa na kuondoa mshikamano uliopo, kama TCRA iliamua kwa hiari kuto kukemea vitendo hivi katika uchaguzi

mkuu wa mwaka 2010, kwa kuzingatia taarifa zilitolewa katika vyombo vya habari hususani magazeti kwa lengo la kuficha uovu wa serikali ili irudi madarakani, ni wazi kwa sasa kuna haja ya kuliona hili kwa maono tofauti kwani hakuna ushindani tena lengo ni kujenga mshikamano wa kitaifa na kuheshimiana kwa minajili ya itikadi zetu na imani zetu kwa pamoja.

## 11.0. HUDUMA ZA MAWASILIANO YA SIMU ZA VIGANJANI.

**11.1. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia mamlaka ya mawasiliano Tanzania TCRA ndiyo yenye mamlaka ya kudhibiti huduma za mawasiliano, mamlaka hii imeanza kutekeleza mfumo wa kuhakiki na kusimamia huduma za mawasiliano (Telecommunication Traffic Monitoring System (TTMS), Pamoja serikali kuanza utekelezaji wa mfumo huu, kumekuwepo na malalamiko ya wananchi kukatwa fedha na makampuni ya simu kwa huduma ambazo hazijaombwa na hili lipo wazi mitandao inafanya bishara ya lazima kwa wamiliki wa simu kwa kuwapa huduma kwa lazima na kuwakata fedha, pamoja na serikali katika taarifa yake kuwa imepata mapato ya shilingi billion 5.2 zilizolipwa kwa kipindi cha miezi miwili ya Oktoba,November na Desemba 2013, hii ni fedheha kwa serikali wakati wananchi wanaibiwa mamia ya mabilioni ya shilingi, inajisifu kupata bilioni tano, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali sasa kuyadhibiti makampuni haya ya simu ambayo kwa sasa ni kawaida kwa wateja wake kukatwa fedha kwa huduma ambazo hazijaombwa na mteja.

**11.2. Mheshimiwa Spika**, gharama za mawasiliano ya simu za viganjani hususani kwa kupiga simu kwa mitandao tofauti (Interconnection Charges) hali ambayo imekuwa ikisababisha wananchi kumiliki kadi za simu zaidi ya moja, lakini pia makampuni haya yamekuwa yakiwatoza wateja pale wanapopiga simu kwenda huduma kwa mteja na hakuna viwango vyenye mlingano kati ya kampuni moja na nyingine na TCRA ipo na jukumu lake la kudhibiti huduma za mawasiliano, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali sasa, kwa kuwa limezungumzwa sana humu bungeni na kambi rasmi ya upinzani imesema sana, sasa vema serikali ikatambua wananchi hawa wa kipato cha chini ambao hawawezi kumudu gharama hizi ukilinganisha na sisi wabunge hapa, sio wananchi wa Wapinzani ila ni watanzania ambao wanategemea serikali hii iwe mstari wa mbele katika kutetea maslahi yao, hivyo ni wakati muafaka sasa kwanza serikali kutoa kauli hapa bungeni je, hiki kinachofanywa na haya makampuni ni sahihi kwa mujibu wa leseni walizopewa au mikataba ya utoaji huduma ya mawasiliano kwa wananchi? Pili iseme ni hatua gani sasa itachukua ili kuweza kuokoa fedha za wananchi ambao wamekuwa wakitozwa kwa huduma wasizozitaka? Tatu Wizara iseme nini kazi ya TCRA kama haya yanafanyika na mamlaka ipo kimya bila kuchukua hatua dhidi ya makampuni haya ya simu za viganjani?

## 12.0. SHIRIKA LA TTCL

**12.1. Mheshimiwa Spika**, ukisoma taarifa ya waziri mbele ya kamati utakuta ajenda ya shirika la TTCL aliyoiweka katika taarifa yake ni MADENI YA TTCL, kwa kuyainisha jinsi serikali ilivyoshiriki kufilisi shirika hili la TTCL hadi kufikia sasa kazi ya Wizara imekuwa kama ni kuanisha madeni yake kwa TTCL tuu, ni aibu kwanza kwa serikali lakini pia udhalilishaji kwa waziri kuwa moja ya majukumu yake ni kuainisha madeni ya serikali yako kwa shirika hilo, kwa mara kadhaa wabunge wamepiga kelele juu ya utendaji na mwenendo wa shirika hili, kama bunge tunaweza kuelekeza nguvu za hoja na kutuhumu weledi wa watendaji wa TTCL na bila aibu tukaomba serikali kufufua shirika hili kama ndio msaada uliobaki kwa shirika lakini tukasahau kwa makusudi kuwa muuaji wa shirika hili ndio huyo tunaemtaka leo afufue.

**12.2. Mheshimiwa Spika,** Ni vema tukawa waungwana na kusema kweli, Mchawi wa TTCL ni serikali ya CCM, kwani kwa tatarifa zake tuu inadaiwa shilingi za kitanzania 2,431,040,809.37 kujumlisha na Dola za kimarekani 1,488,153.38 ambayo madeni haya yamelifanya shirika lijiendeshe kwa tabu na hadi kufikia shirika lenmyewe kuanza kukopa na hadi kudaiwa mamilioni ya fedha.

**12.3. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutoa kauli hapa je ina mpango gani na kulipa madeni haya ya TTCL? Pili serikali iweke wazi kama inayo nia ya kulipoteza kabisa shirika hili kama madeni yote haya hayalipwi hadi sasa na nini mategemeo yake kwa shirika? Bunge liazimie hapa na kuitaka seriikali kuweka kipaumbele kwa TTCL na kulipa madeni yake ilishirika liweze kutoa huduma kwa wananchi.

## 13.0. MFUMO MPYA WA TEKNOLOJIA YA UPIGAJI KURA (BIOMETRIC TECHNOLOGY)

**13.1. Mheshimiwa Spika,** Kuingia katika teknolojia ni swala muhimu sana kwa taifa lakini swala la matokeo ya kuingia huko ni vema tafakuri kubwa ikafanyika tunapoelekea huko, wizara hii haifanyi siasa hivyo ushauri wa kitaalamu ni muhimu sana kwa serikali ili isije kuliingiza taifa katika migogoro amabayo sio ya lazima, kuna mchakato wa maandalizi ya siri unaoendeshwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wa kuandaa utambuzi wa wapiga kura kwa kutumia mfumo wa “biometric” kwa maana ya kumtambua mpiga kura kwa alama za mwili kama alama za vidole na au mboni ya jicho kama sehemu ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu ujao wa 2015",kama ilivyoelezwa katika hotuba ya kiongozi wa upinzani bungeni wakati wa kujadili hotuba ya waziri mkuu.

**13.2. Mheshimiwa Spika,** teknolojia hii kwa siku za karibuni imetumika katika chaguzi nchini Ghana na Kenya na hivi juzi Malawi, Kote huko, ilifeli, na chupuchupu iingize mataifa hayo katika vurugu kubwa za uchaguzi. Mataifa haya yalilazimika kurudia mfumo wa upigaji na kuhesabu kura kwa mkono, hali iliyosababisha hofu kubwa,si kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani haiafiki matumizi ya teknolojia mpya kurahisisha na kuboresha mfumo mzima wa uchaguzi katika nchi yetu, bali inatambua athari kubwa zinazoweza kutokea siku za usoni kama suala lililo "sensitive" namna hii linafanywa kwa fitina za usiri na kufanywa ni swala la kisiasa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka serikali sasa kulitazama hili kwa busara na kuona haja ya kutafakari kwa kujifunza madhara ya mfumo huu.

## 14.0. ILANI YA CCM NA SAYANSI NA TEKNOLOJIA

**4.1. Mheshimiwa Spika**, Katika ilani ya CCM ya mwaka 2010 ibara ya 69 inayozungumzia juu ya sayansi na tekinolojiainasema nanukuu

*"Mapinduzi ya kilimo, ufugaji, uvuvi na viwanda ambayo Taifa linataka yafanyike ili tuweze kuleta modenaizesheni ya uchumi wetu, yatawezekana na kasi yake itakua kwa njia ya nchi kuwekeza vema katika ujenzi wa msingi imara wa maendeleo ya sayansi na teknolojia (building a solid scientific and technical base), Msingi imara wa sayansi na teknolojia katika uhandisi wa chuma na madawa (kemikali) utaiwezesha nchi kupanua haraka matumizi ya sayansi na teknolojia katika shughuli za uzalishaji mali na utoaji huduma katika sekta mbalimbali za uchumi wetu"*

Lakini ukisoma katika randama ya mapato na matumizi ya wizara katika ukurasa wa 9 ibara ya 3.1.2 Idara ya Sera na Mipango inasema idara itaratibu uandaaji wa taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2010-2015, lakini pia ukisoma katika taarifa ya Mheshimiwa Prof Makame M Mbarawa (Mb) Waziri wa Mawasiliano Sayansi na Teknolojia kwenye kamati ya bunge ya kudumu ya miundombinu kuhusu utekelezaji wa bajeti wa mwaka 2013/2014 na makadirio ya bajeti ya mwaka 2014/2014, Waziri anaonesha matatizo ya wizara ikiwa ni pamoja na uhaba wa wataalamu katika Nyanja za Sayansi , Teknolojia na Ubunifu.

**14.2. Mheshimiwa Spika**, Leo hii ni mwaka wa 4 tangu ilani ianze kutekelezwa, waziri anasema wizara imeanza kuandaa rasimu ya program ya mageuzi ya sayansi teknolojia na ubunifu kwa maana ya "**RASIMU**" ikiwa ni mwaka mmoja tu umebaki kumaliza mpango wa Ilani, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ikisema serikali hii haina uwezo wa kututoa hapa tulipo kwa kasi iliyopo katika maandishi yake itakuwa inaionea serikali? Kwa nini serikali hii inakana

ukweli mara zote huku taarifa zake na utekelezaji wa ilani yake unaonesha wazi hakuna kinachofanyika zaidi ya kujinadi kwa kauli tupu?

**4.3. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi hiki ambacho nchi imeamua kwa dhati kujenga uchumi wa kisasa na kuutokomeza umaskini, ni lazima sasa tulipatie kipaumbele cha kwanza suala la maendeleo na matumizi ya sayansi na teknolojia ili tuweze kuondokana na uchumi ulio nyuma na pia uchumi tegemezi, maneno haya yapo kwenye Ilani ya CCM utadhani ni maneno ya serikali ya Kenya kwani serikali hii hii ya CCM maneno haya iliyaweka katika ilani mwaka 2010 ukiangalia kasi ya utegemezi wa bajeti imeendelea kuwa kubwa zaidi kufikia sasa, sasa ikiwa mipango hii ya serikali kufanya maboresho katika sekta ya sayansi ya teknolojia kwa lengo la kuikwamua serikali na kuitoa katika utegemezi, Kambio rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka waziri hapa bungeni aseme kwa dhati mana serikali yake imempa wizara hii kwa mategemeo makubwa kwa kuwa yeye ni Profesa hivyo atafanya kazi kwa kuzingatia uwezo wake mkubwa kitaaluma na anao ujuzi wa mambo haya ya sayansi na teknolojia hivyo ni kwa vipi sasa kwa kipindi hiki kifupi ambacho serikali imebakiwa nacho kabla ya kupokelewa kuongoza serikali nini yawe matumaini ya watanzania angalau hicho kidogo wakati wakisubiri utawala mpya?

**14.4. Mheshimiwa Spika**, ilani ya CCM Ibara ya 71 inasema nanukuu

*"Hivyo, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2010-2015, Chama Cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali kuweka msisitizo mkubwa katika suala la maendeleo na matumizi ya sayansi na teknolojia kwa kuchukua hatua zifuatazo:-*

*(a) Kutenga kila mwaka kiasi kisichopungua asilimia 1.0 ya pato ghafi la Taifa (GDP) kwa ajili ya Utafiti, Maendeleo na Maonyesho ya Matokeo ya Utafiti (R,D&D). (b) Kuchukua hatua za makusudi za kuimarisha Tume ya Sayansi na Teknolojia ili kiwe chombo kinachowaunganisha watafiti na wagunduzi wote nchini ili waweze kukaa kubadilishana uzoefu na kuwa na msukumo wa pamoja katika ujenzi wa msingi wa sayansi na teknolojia tunaouhitaji. (c) Kuishirikisha sekta binafsi katika kuchangia maendeleo na matumizi ya sayansi na teknolojia kwenye uzalishaji mali na utoaji wa huduma. (d) Kuandaa programu mahusus ya wataalamu wa kada mbalimbali kama vile za uhandisi, uganga wa binadamu na wanyama, madini, jiolojia na kilimo n.k. watakaojaza nafasi ambazo ni muhimu na za lazima katika kuyafikia malengo hayo ya dira. (e) Kufufua, kupanua na kuanzisha viwanda ili kukuza uzalishaji viwandani na kuongeza ajira ya wanasayansi. (f) Kuimarisha shughuli za kuatamia teknolojia (technology incubation) kabla ya kuzipeleka sokoni. (g) Kuandaa mazingira bora ya kusambaza teknolojia kwa watumiaji. (h) Kutumia vyombo vya habari kutoa taarifa muhimu za sayansi, teknolojia na ubunifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. (i) Kuwatambua wagunduzi wetu na kuwapa rasmi*

*hakimiliki za ugunduzi wao. (j) Kuboresha kwa kiwango kikubwa mishahara, marupurupu na mafao ya watafiti na wagunduzi wetu".*

**14.5. Mheshimiwa Spika**, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, ina maswali kwa serikali ya CCM na vyema hata Chama kikawaeleza wananchi kwa kujibu maswala haya katika mikutano yake huko nje, Kwanza haya maelekezo ya ya chama kwa serikali je yalichelewa klutolewa kwa serikali ili yaweze kutekelezwa mapema? Kwani hadi sasa hakuna utekelezaji wa ahadi hizi ambazo CCM iliahidi, Pili Serikali iseme hapa ni kwa nini hadi sasa maagizo haya hayajatekelezwa kwani bado takribani mwaka mmoja kipindi chake kumalizika na utekelezaji hauonekani na watanzania bado ni maskini, hakuna maboresho ya huduma kwa kuzingatia teknolojia inayozungumzwa katika ilani na mipango ya serikali hii.Tatu serikali iseme hapa ni wagunduzi wangapi ambao serikali imewatambua na wa aina gani lakini pia imewawezasha vipi kuendeleza ugunduzi huo hadi kufikia kiwango cha kuleta mabadiliko ya teknolojia nchini? Nne serikali iseme ni kwa kiasi gani imefufua, imepanua na kuanzisha viwanda ili kukuza uzalishaji viwandani na kuongeza ajira ya wanasayansi Viwanda ambavyo vilikufa kwa sera mbovu na ufisadi wa serikali hii hii ya CCM?.

…………………………………

**MOHAMED HABIB JUMA MNYAA (MB)**
**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA**
**YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA.**
**May 30, 2014.**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia kwenye mjadala, yupo Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba na Mheshimiwa Naomi Kaihula. Mheshimiwa Brig. Gen. Ngwilizi!

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nianze kusema kwamba naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili labda niseme kwamba hotuba ya Kambi ya Upinzani tumeipata sasa hivi. Tokea mwanzo anasoma mpaka tumefika ukurasa wa 23 tulikuwa hatuna hotuba hiyo, sijui ilikuwa ni sehemu mbinu zao ili tusielewe wanasema kitu gani?

Mheshimiwa Spika, lakini labda nianze na suala bajeti ya Wizara hii. Bajeti ya Wizara hii ni ndogo wala haikidhi. Cha kushangaza zaidi ni kwamba tokea mwanzo, miaka miwili iliyopita kumekuwa na ongezeko kidogo sana la bajeti hii. Mwaka juzi walipata shilingi bilioni 26, mwaka uliofuata walipata shilingi bilioni 27

na mwaka huu wameongezewa zimekuwa shilingi bilioni 37. Kutokana na majukumu ya Wizara hii fedha hizi ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, nadhani tutapata maelezo vizuri zaidi tukija kuzungumzia bajeti ya Wizara ya Fedha kwa sababu kinachoonekana hapa ni kwamba kuna kucheleweshwa kwa kutolewa fedha. Sasa hili limekuwa likijitokeza katika kila Wizara. Kwa hiyo, masuala haya ya kuchelewesha fedha na kuzifanya Wizara zishindwe kutekeleza majukumu yao ni wazi kwamba itabidi tupate majibu halisi kutoka Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Kamati ya Miundombinu, imefanya kazi nzuri sana na kwa kweli ushauri ulioko pale, kama utazingatiwa na Serikali utaweza kuleta maendeleo ya haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la anuani za makazi na simbo za Posta. Hili linahitaji lifanyike kwa kasi zaidi kwa sababu jinsi tunavyochelewa ndivyo tunavyochelewesha sisi wenyewe maendeleo yetu. Ni lazima tuhakikishe kwamba Wizara hii inawezeshwe ili anuani za makazi ziweze kupatikana haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, nijikite kwenye Jimbo langu la Mlalo. Kwanza, niishukuru Wizara wamefanya jitihada, kuna Kata zangu kwa ujumla kama robo tatu ziko kwenye mawasiliano. Hata hivyo, ziko Kata tatu ambazo bado hazijaingia katika mawasiliano ya simu. Kata hizo ni Rwangi, Mbaramo na Shume, eneo la Gologholo. Kata hizi zina wakazi wengi sana, kuna shughuli za kiuchumi nyingi sana zinaendelea huko, kukosekana kwa mawasiliano katika maeneo hayo, kwa kweli kunakwamisha maendelo ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile katika Jimbo la Mlalo, katika Tarafa ya Mlalo, kuna ukanda wa kutokea Malindi, kuteremka mpaka Majulai, mpaka Nyasa, kule tuko kwenye kivuli cha mawasiliano. Minara ipo lakini eneo linalofuata barabara ile hakuna mawasiliano kabisa. Naomba Wizara izungumze na watoa huduma ili angalau kuwepo na mnara katikati ya bonde lie la Mlalo ambao utawezesha kutoa mawasiliano katika eneo zima lile.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo, mimi naomba nirudie kusema kwamba naunga mkono hoja ya Wizara hii, bajeti yao tuipitishe pamoja na kwamba tunajua haitoshi, hilo ni suala ambalo tutalizungumza wakati tukichangia kwenye Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa ni Mheshimiwa Juma Njwayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba na Mheshimiwa Naomi Kaihula ajiandae.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi asubuhi hii ili niungane na wenzangu kuchangia kidogo hotuba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa changamoto kubwa anazoweza kukabiliana nazo, pia Naibu wake na Watendaji wote walioko kwenye Taasisi anazoziongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani nimekushusha cheo kidogo pole, ulimi tu umeteleza. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Wala usijali, cheo kipo palepale. *(Kicheko)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, leo naomba nichangie machache yafuatayo. La kwanza, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii lakini nina matatizo makubwa sana kwangu ya mawasiliano, ninazo Kata saba, hali ni mbaya sana. Kata za Mihambwe, mahali hapa walikuwa wameahidiwa mnara tangu mwaka 2005 lakini sehemu hiyo ni nzuri na muhimu sana kibiashara. Maeneo haya yana uzalishaji mkubwa wa korosho na watu wengi wanakaa huko.

Mheshimiwa Spika, kama mnavyojua, kwenye maeneo ambayo yana uchumi na watu ni wengi, kukitokea adha kidogo ya kuwasiliana na vyombo vya ulinzi na usalama na vitu vingine inakuwa shida. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara hii ishirikiane na *operator* wa simu za mikononi ili wakaweke minara pale Mihambwe, Mkoreha, Naputa, Maundo, Namikupa na Chaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanasema ukilalamika sana haifai hata kidogo ukipata nacho ushukuru. Naomba niwashukuru walitoa minara mitatu mwaka jana pale Nanyanga, Kitama na Chaume. Pamoja na uzuri huo wa minara mitatu, naomba Kata hizo nilizozitaja tafadhali mnisaidie maana hali siyo nzuri sana katika maeneo hayo. *(Mkakofi)*

Mheshimiswa Spika, jambo la pili, naomba nifurahi, kwenye hotuba ya Waziri, ukurasa wa 12, leo ameliambia Bunge hili na Taifa kwa ujumla kwamba sheria zifuatazo rasimu yake iko tayari. Nazo ni Sheria ya Usalama wa Mitandao *(Cyber Security Laws)*, Sheria ya Kulinda Taarifa Binafsi *(Personal Data Protection)* na Sheria ya Miamala ya Kieletroniki *(Electronic Transaction)* na Sheria ya Kudhibiti Uhalifu wa Mtandao na Komputa *(Computer and Cyber Crime)*.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni muhimu sana. Rai yangu kwa Serikali wafanye haraka ili sheria hizi zije Bungeni hapa tuzipitishe ili ziweze kufanya kazi. Kwa sababu Watanzania wamekuwa wakigubikwa kwa namna moja au nyingine na maovu mengi yanayotokana na kutokuwepo kwa sheria hizi. Kwa kuzileta haraka sheria hizi, zitatuondolea matatizo mengi. Watu wanaibiwa kwenye simu, hakuna namna mtu binafsi na siri zake zikiibiwa, zikipotoshwa unaweza kuji-*protect* yaani mambo ya hovyohovyo yako mengi tu. Kwa kuwepo sheria hii, kutasaidia sana kpunguza sana adha, matatizo na shida zinazowapa Watanzania na wengine wanaoingia nchini kwetu. Kwa hiyo, juhudi za makusudi na za haraka zifanyike ili sheria iletwe ili sasa Tanzania tuwe na sheria hizi zitumike kuwalinda Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuongelea *TCRA,* kwanza tuisaidie vya kutosha lakini na wenyewe wafanye kazi ya ziada ya kudhibiti matatizo hasa uhalifu unaotokea lakini pia wadhibiti makampuni ya simu. Kwa mfano, yako matatizo, unaweka leo *voucher* ya Sh.10,000/= baada ya muda mfupi tu unaambiwa *voucher* ile imeisha. Yako matatizo unaongea ghafla unaingiliwa, unasimamishwa, unaondolewa kwenye mpango wa maongezi yako pasipo mwelekeo wowote. Jambo hili na mengine ya namna hiyo yamekuwa adha. Kwa hiyo, tunawaomba *TCRA,* isimamie vizuri *mobile operators* hawa ili mambo yaende kama yanavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko jambo moja. Serikali, imekuwa ikipata kama sikosei kati ya senti 7 - 10 zinazoendea Serikalini kutokana na makusanyo haya na tulipitisha hapa Bungeni. Fedha hiyo mimi sioni mantiki ya kuendelea kubakia Serikalini. Kwa nini isipelekwe kwenye ule Mfuko wa Mawasiliano kwa wote *(UCAF)* ili usaidie kuboresha mawasiliano vijijini. Huku Mihambwe ambako kwa namna moja au nyingine hakujapata mnara, kwa sababu hapa wakati mwingine tunaambiwa ni ufinyu wa pesa na kweli minara hii ni ya gharama sana lakini fedha hii itakapokwenda moja kwa moja kwenye Mfuko huu utasaidia kupunguza matatizo ya ukosefu wa minara. Mimi sioni haja ya kukaa Serikalini inafanya nini, tupeleke mahali kunakofanana nayo.

Mheshimiwa Spika, kwa leo nilikuwa na mchango huo mdogo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi lakini nirudie kusema nafurahishwa na namna viongozi walioko kwenye Wizara hii wanavyowatumikia Watanzania vizuri. Mungu awabariki sana, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimuite Mheshimiwa Albert Ntabaliba.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia mjadala ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja hii lakini la pili nawapongeza Mawaziri wa Wizara hii kwa kupanua mawasiliano katika nchi yetu ya Tanzania na sasa vijiji vingi vimeanza kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa niwapongeze kwenye Jimbo langu la Manyovu, Wilaya ya Buhigwe, minara imeongezeka na yale matatizo mengi tuliyokuwa nayo mipakani kwamba mawasiliano hayapo, tumeshapata minara katika maeneo ya Kilelema, Muyama, kule tunaenda vizuri. Tunayo matatizo kama kwenye bajeti mliivyoonesha, ile minara mnayotaka kujenga Nyamgali ili iweze kusaidia matatizo tuliyo nayo katika kijiji cha Kibande, kijiji cha Bwelanka na Nyamgaliyake. Kwa hiyo, tunaomba hilo liweze kutekelezwa. Kwenye bajeti, mmeonesha kwamba mnara utakaojengwa Nyamgali, utashughulikia vijiji 14. Sasa nilitaka kuvijua ni vipi hivyo ambavyo Wizara imeviorodhesha.

Mheshimiwa Spika, tunayo matatizo kwenye Kata nyingine tatu. Tunayo matatizo ya minara katika kijiji cha Kinazi, Kata ya Rusaba, tunayo matatizo ya mawasiliano Kata ya Munzeze, tunayo matatizo ya mawasiliano Kata ya Kajana. Kwa hiyo, naomba mtusaidie na pale paweze kuwa na mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho mimi sifurahi na ambacho nafikiri lazima kifanyike vizuri zaidi, *simcard* yangu inabeba watu 250, watu wengine inabidi wawekwe kwenye simu. Je, teknolojia haiwezi kuongezwa ikabeba watu hata kama watu 100,000. Kwa nini *megabyte* ya *simcard* isiongezeke? *Simcard* yangu na ya mwanangu zinalingana uwezo wa ku-*store* watu, nafikiri muangalie jinsi teknolojia hapa inaweza kuongeza uwezo huo. *(Makofi)*

Mheshmiwa Spika, kama hamuongezi, mruhusu basi *simcard* mbili zitumike kwenye namba moja, hata *simcard* ziwe tatu lakini zitumike kwa namba moja. Kama hatutaki ku-*install* kwenye simu ziwepo kwenye *simcard* hata kama ni nane, kumi ziweze kuwa na uwezo huo. Naomba hilo nalo mliangalie mtakavyoweza kufanya. Kama mlifikia 250, kwa nini msifikie 5,000, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, lingine ni namna ambavyo ukimpigia mtu simu unaanza kupewa matangazo ya Shirika lile halafu ndiyo inaita. Je, zile gharama nani analipa? Huenda ndiyo chanzo watu kukuta tunaweka hela nyingi na mara moja zimeisha. Kwa hiyo, hilo nalo naomba mliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni hizi *promotion* zinazofanywa na Makampuni haya, kwamba *Tigo* kwenda *Tigo* bei kadhaa, *Tigo* kwenda mitandao mingine

bei kadhaa, kwa kweli hilo nalo bado linatuumiza. Kwa sababu sasa ilivyo huwezi kuwa na *list* ya watu wa kwenda kwenye mtandao wako peke yako, lazima kuwe na uhuru wa kwenda mahali popote na gharama zilingane.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sina mengi, nawapongeza. Naomba vijiji vya Kinazi, wanalalamika kwelikweli. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa January Makamba uliahidi kwamba utayashughulikia na nina imani mtashughulikia pamoja na Waziri wako makini kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nilisema nitamuita Mheshimiwa Naomi Kaihula, ataufatiwa na Mheshimiwa Jerome Bwanausi na Mheshimiwa Abdul Mteketa pia ajiandae.

**MHE. NAOMI A.M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuzungumza katika Bunge lako Tukufu. Zaidi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Rehema na Wema wake kuniwezesha kuwa na uhai na afya hata kuweza kuzungumza na Wabunge wako.

Mheshimiwa Spika, nina vitu viwili nitakavyozungumzia ambavyo ni vya kukera na kimoja kizuri. Kuna jambo moja ambalo limezungumzwa na wenzangu lakini pia napenda niongezee, Wizara, mnasimama kwa ajili ya wananchi na kama mnasimama kwa ajili ya wananchi ni lazima mjue mazingira ambayo tuko sasa hivi ni ya kibepari. Kwa kuwa ni ya kibepari, ni lazima hata mifumo yake na sheria zake ziende kibepari. Kwa bahati mbaya sana ni kwamba mifumo imebadilika kijanjakijanja imekuwa ni ya kibepari lakini wananchi wake siyo wabepari ni wajamaa, ni watu *innocent*. Kutokana na hilo lazima nyie Serikali mfikiri mbali zaidi jinsi gani ya kuwasaidia na kuwalinda watu wenu dhidi ya mifumo ya kinyonyaji kama inavyoendelea katika simu.

Mheshimiwa Spika, moja kubwa kama walivyosema watu wengi, unakuta hawa watu wanaoshughulika na hayo mambo ya mawasiliano katika simu, wanatuibia sana sisi, namaanisha hata Serikali inaibiwa. Unakuta unajirusha yaani unajiunga na vifurushi vyao, wanakuambia utamaliza tarehe fulani na saa fulani. Kitu cha ajabu unakuta wala haifiki na wakati mwingine umejiunga hapohapo tayari wanakuambia salio limekwisha, limekwishaje na mimi wala sijaongea, hili jambo limekuwa la kawaida sasa hivi. Huu ni wizi kabisa, sasa wanatuibia hata sisi tunaojua, sasa wananchi wetu na ndugu zetu kule vijijini inakuwaje? Tunakuomba sana na tuliwaomba Serikali mtutetee, mtafute jinsi gani mtaweza kuwabana hawa jamaa waaache kutuibia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nililosema nataka nizungumzie na ambalo ni kero, unakuta kwamba wewe una haraka zako, unakwenda benki, unafika pale wanakuambia mitandao iko chini, sasa mitandao iko chini inahusiana nini na mimi? Mimi nataka huduma kwa hiyo wewe ni lazima utafute njia za kuhakikisha kwamba ikitokea hii mitandao inakuwa chini, huyu mteja nitamhudumia hivi. Ndiyo maana nasema hii mifumo ni ya kinyonyaji, ni ya kibepari *perse*. Ni vinjia unaviona vidogovidogo lakini vinaiba pesa nyingi sana, siyo hivyo tu lakini vinahatarisha hata maisha ya mtu yule. Mtu unataka kuchukua fedha harakaharaka pengine kuna hatari inahitaji fedha unakuta kwamba huo mtandao unakaa mpaka jioni mtandao hakuna. Unakuta pesa zimekaa njiani wanasema mitandao, jamani, jamani, tunawaomba mtusaidie, mtulinde ndiyo wajibu wenu, kutulinda dhidi ya mitandao kama hiyo na tabia na utamaduni unaotaka kujengeka wa kutuibia. Ni kazi ya Kimungu kwa kweli lazima mtuonee huruma sisi ambao tunaibiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine linalohusiana nalo, kwa mfano unasafiri, sasa sehemu nyingine zenye mapori hakuna mawasiliano, sasa sijui inakuwaje? Naomba mtuambie, inakuwaje na mtafanyaje maana pale pasipokuwa na mitandao mara nyingi ndiyo unakuta majambazi wamekaa hapo wawavizie, sasa mtawasiliana

vipi harakaharaka wakati katika sehemu kama hizo hakuna mawasiliano? Naomba mliangalie hili na muone ni jinsi gani ambavyo mtasaidia katika kupunguza ujambazi na uharamia, hilo naomba sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Wizara yenu na kazi yenu siyo mbaya sana, kazi yenu ni nzuri, wanaowaangusha ni wale ambao hawawapi fedha za kutosha kusudi muweze kufanya kama mnavyohitaji. Kwa mfano, suala la kuhakikisha kwamba kwenye vyuo kunakuwa na *computers*, wanatangaza utapata na masomo ya *computers* na kadhalika lakini hakuna. Je, mna njia yoyote mnayotumia kuhakikisha kwamba masomo haya yanakuwa kweli na vifaa ili wanapotangaza watu waende kusoma kwenye shule hizo ni kweli zipo au ni kwa ajili ya kuvutia tu watu wawanyonye? Kwa sababu *computer* kwa kweli ni lazima uwe na vifaa vya kutosha ili uweze kupata elimu ya kutosha. Hilo naomba pia mliangalie na mlishughulikie ni jinsi gani ambavyo mnaweza kutoa elimu ambayo ni *effective*, *the competence* ya hiyo elimu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa napenda niwashukuru na mmenifurahisha sana yaani ni Wizara ya kwanza kabisa ambayo imefikiria kuhusu wanawake, kuhusu jinsia, tena *technically* nawashukuru na nataka niwashauri zaidi.

Wizara hizi nazisifu kutoka moyoni, mimi kama mwanajinsia na mwanaharakati, wameongeza idadi ya wanawake, mkisoma kuanzia ukurasa

wa 37 mpaka 38 wameongeza idadi ya wanawake kuingia katika masomo ya teknolojia ya sayansi, siyo kawaida. Naomba mtueleweshe ni jinsi gani mnawapata hawa watu ili sisi kama wanaharakati na kama watu wa jinsia tuone jinsi gani tunaweza kusaidia pia kutangaza na kuona ni watu gani wanaweza kujiunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, pia kwa sababu ….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mwanaharakati bahati mbaya umemaliza muda wako.

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Jerome Bwanausi atafuatiwa na Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa na Mheshimiwa Esther Lukago Midimu naye ajiandae.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hotuba ya Waziri lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa ya kuchangia. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo langu la Lulindi naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii, hongereni sana. Kwa hakika katika kipindi cha uongozi wao, jitihada kubwa zimefanyika katika kuhakikisha kwamba mambo mengi yanafanyika. Kwanza, kusimamia kuhusu Mkongo wa Taifa kwa awamu zote mbili yaani awamu ya kwanza na ya pili kwa mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni juhudi zinazoendelea kufanywa kuhakikisha kwamba mawasiliano yanapatikana nchi nzima pamoja na vikwazo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutopata fedha za kutosha kufanyia shughuli hii ya usambazaji wa mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, la tatu, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuzindua mtambo wa kufuatilia na kuhakiki mawasiliano ya simu hapa nchini. Kwa kweli jambo hili lilikuwa ni muhimu sana na niipongeze *TCRA* kwa kuhakikisha wanadhibiti jambo hili na sasa hata zile meseji zilizokuwa zinatumwa za uchochezi na

vitisho ndani ya mitandao yetu zimeanza kupungua. Kwa hiyo, naiomba Wizara iendelee kusisitiza jambo hili kuhakikisha jambo hili ambalo lilikuwa linataka kuhatarisha nchi linadhibitiwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulieleza ni kwamba kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri imeeleza kwamba Tanzania ina Kata 1,365 zisizo na mawasiliano ama zina mawasiliano hafifu. Kwa kasi inayoendelea hivi sasa kupitia kwenye Mfuko wetu wa Mawasiliano kasi ni ndogo sana, itachukua miaka mingi sana kuhakikisha hizi Kata 1365 zinapata mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ameeleza mikakati ambayo Wizara inatarajia kuifanya, kuhakikisha yale maeneo ambayo hayana vivutio kwa wawekezaji hawa wanaoweka mitandao kutafuta aina nyingine ya teknolojia ili kuhakikisha kwamba maeneo haya yanapatiwa mawasiliano. Kwa hiyo, napongeza juhudi hizi lakini naomba kasi iendelee.

Mheshimiwa Spika, nimeona juhudi zinazofanywa na Mfuko katika kutangaza zabuni. Zabuni ya kwanza ilitangazwa Kata 152 lakini ni Kata 52 tu ambazo zilifanikiwa. Ikatangazwa tena kwenye Kwanza A, Kata 168 lakini ni Kata 77 peke yake ndizo zilifanikiwa kupata wazabuni. Mwisho, kwenye awamu ya Kwanza B, Kata 124 lakini zinafanikiwa kupata Kata 86 tu.

Naiomba Wizara, ni lazima kuangalia ni kwa nini wazabuni hawana vivutio sana vya kutaka kuomba katika maeneo mbalimbali pamoja na lile lililoelezwa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla waliangalie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la Jimbo langu la Lulindi. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote na hasa Mfuko wa Mawasiliano kwa juhudi walizofanya kuhakikisha wanaleta matumaini kwenye Kata za Chiwata, Nkululu na Mpindimbi ambazo zimepata wazabuni ambao ni *Tigo*. Ni imani yangu kuwa wananchi wamesikia hotuba ya Mheshimiwa Waziri lakini pia kupitia maelezo ninayoyasema ni kwamba maeneo haya yamepata kampuni ya *Tigo*. Naiomba sana kampuni ya *Tigo* iweze kufanya kazi hii kwa wakati na kwa sababu inasimamiwa na Mfuko wa Mawasiliano basi Mfuko uhakikishe kwamba maeneo haya yanapatiwa mtandao huu haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho nataka kuchangia kuhusu mawasiliano mipakani. Jimbo langu la Lulindi lina Kata nne zilizo mpakani mwa Tanzania na Msumbiji. Maeneo yote ya hizi Kata nne hayana mawasiliano kabisa na

mawasiliano yaliyopo ni mawasiliano yanayopatikana kutokea kwenye mitandao ya nchini Msumbiji. Sasa wananchi wanajiuliza, sisi tupo Tanzania ama tupo Msumbiji? Kwa sababu vocha na *line* zote zinatoka Msumbiji kuwauzia wananchi wa Tanzania. Naomba Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wizara kwa ujumla, hebu toeni kipaumbele kwenye Kata hizi za Chikolopola, Mchauru, Sindano na Mnavira ambazo zipo mpakani.

Mheshimiwa Spika, jambo hili halisaidii tu wananchi wale lakini pia linasaidia katika suala la ulinzi wa nchi yetu. Kwa hiyo, suala la mipakani kupata mawasiliano ni jambo ambalo wala halina mbadala. Kwa hiyo, namwomba Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho hebu atoe maelezo na wananchi wa maeneo haya ya Chikolopola, Mchauri, Sindano na Mnavira wapate maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, ni mipango gani ambayo Serikali inayo katika bajeti hii ya mwaka 2014/2015 kuhakikisha mawasiliano yanapatikana katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nilitaka kuchangia haya na naomba kuunga mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Midimu.

**MHE. ABDUL RAJAB MTEKETA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza napenda kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi toka niingie Bunge hili tatizo langu kubwa ilikuwa katika Kata zangu mbili za Tanganyika Masagati na Uchindile na *form* alizotoa Waziri tujaze kuonyesha sehemu ambazo tunataka tupeleke minara nilizijaza hizo lakini nimepiga kelele mpaka leo hii kelele zangu hazijazaa matunda. Naomba Waziri na Naibu wake wanishughulikie suala hili ambalo linaniangusha sana. Sasa hivi kila kitu kipo katika mitandao, watu wa Tanganyika Masagati wanaona kweli wako Tanganyika maana mpaka sasa hivi wanapata taabu sana. Simu mpaka watu wapande miti, wapande kwenye milima, waende kwenye sehemu nyingine mbalimbali na akina mama wanateseka sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sasa hivi kuna ugonjwa wa Fistula ambao *CCBRT* wanaushughulikia wanawatumia wagonjwa wao fedha kwenye MPESA, sasa wao wanakosa hizi huduma zote. Naomba sana, najua kabisa sekta ya mawasiliano imeshikwa na watu binafsi na watu binafsi kama *Airtel, Tigo, Vodacom* wanafanya kazi kwa kutafuta faida. Kwa hiyo, sehemu hizo nyingine

Serikali iangalie yaani itoe fedha zake zenyewe ili kusudi wananchi wale wapate mawasiliano bila matatizo. Kwa sababu kila kitu sasa hivi kinaingia kwenye mitandao, vitu kama matangazo ya kazi na kadhalika wananchi hawa wanakosa fursa hizo. Mimi kusema sana sipendi kwa sababu nimeshasema kutoka mwaka 2010 mpaka leo, wananchi hawa wanateseka sana, naomba sana wapelekewe minara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile katika mji wa Ifakara muda mwingi utakuta mawasiliano yanakatika na hasa Tigo na Airtel. Naomba wahusika watengeneze vitu hivyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Inakuwa ngumu kuijadili Wizara hii eeh! Mheshimiwa Esther Midimu atafuatiwa na Mheshimiwa Gregory George Teu.

**MHE. ESTHER L. M MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, namshukuru Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. Nawashukuru sana wanachapa kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia naipongeza Wizara kwa kuruhusu huduma ya MPESA, TIGOPESA na AIRTEL MONEY kwani imesaidia sana kupunguza msongamano kwenye benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuomba minara kwenye Mkoa wangu wa Simiyu. Naomba mawasiliano kwenye Wilaya ya Busega, Kata ya Badugu, Ngasamo, Shigala, Busami. Wilaya ya Maswa, Kata ya Nguliguli, Sanami, Mwanenge, Budekwa na Kadoto. Wilaya ya Itilima, Sagata, Mwaswale, Migato na Munze lakini Kata nyingine nitawasilisha kwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kuhusu wizi wa kwenye mitandao. Kwa kweli wananchi wengi sana suala hili linawakera kwani wakiweka vocha ndani ya muda mfupi vocha zinakuwa zimeshaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nakerwa sana na mitandao ya *facebook* na *Jamii Forum* kwani inadhalilisha viongozi hata wakubwa, inasikitisha sana. Pia, mitandao ya *facebook* inaharibu watoto wetu kwani inaonyesha picha cha utupu na picha za binadamu kufanya mapenzi na mnyama. Hiki ni kitu ambacho hakiwezekani na inasikitisha sana na mimi kinanikera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuongelea ni kuhusu usajili wa simu. Wananchi wengi wanasajili simu kwa udanganyifu. Akienda kusajili simu anasajili kwa jina la mtu mwingine na uhalifu ukitokea hakamatwi yeye bali anakamatwa mtu mwingine. Inasikitisha sana kwa kitendo hicho.

Mheshimiwa Spika, mimi sina mengi ya kusema bali naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Ignas Malocha atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Meshack Opulukwa.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kuipongeza Wizara hii, Waziri na Naibu Waziri kwa jinsi wanavyowajibika katika Wizara hii. Tatizo kubwa tunaloliona ni upungufu wa fedha lakini kama ni kuwajibika kwa kweli wanawajibika. Japokuwa tuna matatizo mengi kwenye maeneo yetu na tangu tumeingia Bungeni wamekuwa wakituahidi kwamba watapeleka mawasiliano, unashindwa kudadisi zaidi kulingana na uchache wa pesa lakini jitihada unaziona, kwa kweli nawapongeza kwa jitihada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mawasiliano ni miongoni mwa nguzo muhimu katika kuleta maendeleo ya nchi yetu na nchi nyingine duniani. Kwa umuhimu wa huduma hii, ni vema Serikali ihakikishe maeneo yote yanapata mtandao wa simu za mkononi. Umuhimu wa mawasiliano kiuchumi, kijamii, kiusalama na kiutumishi, sisi wote tunafahamu mawasiliano ni nguzo muhimu kiuchumi. Sasa hivi vijana wetu wanatumia simu za mkononi kuagiza bidhaa, kujua masoko ya bidhaa mbalimbali, kutuma fedha na kadhalika, kwa hiyo, jambo hili ni muhimu sana. Kijamii vilevile kiafya inasaidia sana maeneo yenye vituo vya afya kama zahanati kutoa taarifa mbalimbali, mahitaji ya gari, kutoa taarifa kwa ndugu na

jamaa. Katika sekondari vijana wetu wanapata huduma mbalimbali ya kujua mambo ya kidunia yanakwendaje, yanamsogeza duniani hata kama yuko kijijini. Kwa hiyo, ni vema kabisa tunakatambua umuhimu wa jambo hili. Vilevile

kuwarahisishia wazazi katika kutuma pesa za ada za shule. Kwa hiyo ni muhimu sana jambo hili likatiliwa umuhimu maeneo yote yakapata mtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiusalama, yapo maeneo ambayo ni hatarishi wananchi wanaweza wakavamiwa, wakakosa mawasiliano. Kwa mfano, mwaka jana wananchi wa Chombe Kipeta walivamiwa Mlima Kipara, masaa matatu majambazi waliwavamia wakawanyang'anya pesa, hakuna mawasiliano. Kwa hiyo, ni jambo muhimu sana kwa Serikali kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiutumishi vilevile, yapo maeneo ambayo wako mbali na benki na hii inawafanya watumishi wengine waanze kukataa maeneo ya kuishi kwa sababu ya umbali. Anaona kutumia nauli yake mpaka kufika maeneo ya benki anatumia zaidi ya shilingi 40,000/ au 50,000/= lakini kama mawasiliano ya simu yapo inamrahisishia katika kupata huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niyataje maeneo ambayo hayana mtandao katika Jimbo langu yaani Kata ya Milepa, kijiji cha Kisa, Msiha, Milepa; Kata ya Mfinga, Msila, Kasekela Mfinga, Mtapenda, Kwilo na Mpete; Kata ya Kaoze na Kipenta vijiji vya Chombe, Kaoze, Kapenta, Kawila, Kiyandaigonda, Mkusi na Tululu. Katika Kata hizi mbili, niishukuru Serikali nimesoma katika kitabu wameshatenga shilingi milioni 75,440,000 kwa ajili ya kupeleka mtandao katika maeneo hayo, naishukuru sana Serikali. Pia napenda kutoa wito kwa makampuni yote ya *Vodacom, Airtel* na *Tigo* kuwa maeneo yetu ni ya kibiashara na tunafahamu makampuni haya yanafanya biashara. Kwa hiyo, natoa wito wapeleke huduma hii kwa sababu hii ni biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini namwomba sana Mheshimiwa Waziri, nimezungumza naye sana tangu nimeingia Bunge hili anisaidie mtandao Makao Makuu ya Kata ya Milepa kwa sababu kuna huduma muhimu, kituo cha Polisi, kituo cha afya, sekondari na mimi ndipo ninapoishi pale, nikienda na mimi napanda mtini, wananchi wananicheka sana, wanadhani wakati mwingine mimi ndiyo nina fedha mkononi. Naomba mlichukulie kwa uzito jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina mengi zaidi bali naipongeza Wizara, Waziri na Naibu Waziri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nilisema namwita Mheshimiwa Meshack Opulukwa atafuatiwa na Mheshimiwa Gregory George Teu.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, kwanza ningependa kumpongeza Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Eng. Mnyaa kwa kazi kubwa ambayo yeye akishirikiana na Kambi ya Upinzani wameweza kuifanya ili kuweza kuwasilisha mawazo ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusiana na bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, napenda pia kuwapongeza Wabunge wote wa Upinzani Bungeni ambao kwa kweli kwa kutokuridhika na jinsi ambavyo Wizara ya Nishati na Madini ilivyokuwa ikiendelea hapa jana waliamua kutoka nje na hatimaye kuwaachia wenzetu waweze kuendelea kupitisha bajeti hii ili wasiweze kuwa ni sehemu ya lawama au sehemu ya matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee, mimi na Makamu wangu, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, tunawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Kwa heshima kubwa, ninaomba *Hansard* irekodi majina yao kama yanavyoonekana kwenye taarifa yetu kikamilifu. Aidha, ninapenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kulisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Pia ninawashukuru Ndugu Matamusi Fungo na Ndugu Maria Mdulugu, kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria Kama Ilivyowasilishwa Mezani**

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014, PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

## 1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni 99 (5),(9) na 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inahusisha mafungu saba ambayo ni: Fungu 12-Tume ya Utumishi wa Mahakama, Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Fungu 35 - Mkurugenzi wa Mashtaka, Fungu 40- Mahakama, Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria, Fungu 55- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Fungu 59- Tume ya Kurekebisha Sheria.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 3 Mei, 2014 Kamati yangu ilichambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Mtengeti Migiro (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria akishirikiana na Naibu Waziri Mheshimiwa Angela Jasmine Kairuki (Mb), pamoja na Watendaji wa Wizara. Katika maelezo yake Waziri aliieleza Kamati kuhusu utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa kipindi cha Mwaka 2013/2014.

**UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014**

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Kamati yangu ilitoa Maoni na Ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utendaji kazi wa Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa kiasi kikubwa ushauri huo umezingatiwa na ushauri mwingine upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ifuatilie kwa makini utendaji kazi wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba bila kuathiri uhuru wa Tume na kuiwezesha nchi kufikia lengo la kupata Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Wizara ilikuwa karibu na Tume katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na kufuatilia utekelezaji bila kuingilia uhuru wake. Kutokana na jitihada hizo Tume ilikamilisha maandalizi ya Rasimu ya Katiba pamoja na taarifa nyinginezo muhimu, na kuikabidhi rasimu hiyo Serikalini. Aidha, Rasimu ya katiba imeishawasilishwa katika Bunge Maalum la Kutunga Katiba.

(ii) Bajeti ya Bunge la Katiba ifahamike na iletwe Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Sura ya 83, masuala yote ya Bunge la Katiba yapo chini ya Bunge Maalum la Katiba ambapo fedha kwa ajili ya Bunge hili zinatolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.

(iii) Tume ya Utumishi wa Mahakama iongezewe Bajeti yake kwa kutengewa fedha za Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Tume ya Utumishi wa Mahakama haikutengewa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Bajeti iliyopewa Tume ya Utumishi wa Mahakama kwa mwaka 2014/2015 imefuata ukomo wa Bajeti ya Tume ya Shilingi 2,871,716,000.

(iv) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iimarishe Kitengo cha Mikataba kwa kuwajengea uwezo wa kuwapatia Rasilimali Watu na fedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilielezwa kuwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inao mpango wa kuwasomesha Mawakili waliopo na watakaoajiriwa ili kuwajengea uwezo kitaaluma katika kushughulikia masuala ya mikataba na masuala mengine ya kisheria. Kutokana na uwezo wa Serikali kifedha uliopo katika mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imepanga kumsomesha Wakili mmoja katika ngazi ya Shahada ya Uzamili katika nyanja za mikataba inayohusu mafuta na masuala ya shughuli za ujenzi. Kwa sasa eneo hili la mikataba kwa Muundo wa ofisi ya Mwansheria Mkuu wa Serikal limepewa hadhi ya kuwa Divisheni na kuongozwa na Afisa mwenye cheo cha Mkurugenzi.

Mheshimiwa Spika, Divisheni hii kwa sasa inao Mawakili wa Serikali kumi na nane (18) na inatarajia kuajiri wengine wawili katika mwaka wa fedha 2014/2015. Sambamba na jitihada hizi, eneo la mikataba limetengewa kasma yake ya Bajeti ya kiasi cha Shilingi bilioni 1.34 katika mwaka wa fedha 2013/2014 kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa (UNDP) chini ya Mradi wa UNDP Support Programme wamekuwa wakifadhili Programu ya Mafunzo ya muda mfupi ili kuwawezesha mawakili wa Serikali na wadau wengine wa Sekta nyingine kuwajengea uwezo wa kuchambua, kujadili, kuandika, kuhakikisha na kusimamia mikataba.

(v) Kitengo cha Uandishi wa Miswada kiweke utaratibu wa kundaa Miswada kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili ili hatimaye inapokuwa

imepitishwa na Bunge, kuwepo na sheria moja yenye Lugha ya Kiingereza na Kiswahili na hii itawasaida wananchi wengi kunufaika na sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kwamba Serikali imeendelea kuzingatia maelekezo ya Kamati na kuyafanyia kazi kila mara. Kwa hivi sasa Miswada ya Sheria inayowasilishwa Bungeni imekuwa katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Mfano, Sheria ya Marekebisho ya Katiba na Sheria ya Vyama vya Ushirikia.

(vi) Serikali iiwezeshe kibajeti Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuajiri watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitengewa bajeti ya Shilingi bilioni 1.86 kwa lengo la kuajiri watumishi wapya 489. Hata hivyo, kibali cha kuajiri watumishi hao wapya hakikutolewa kutokana na sababu za kibajeti zilizojitokeza. Hivyo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imewasilisha tena maombi ya ajira mpya kwa watumishi 489 kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

(vii) Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2013/2014 ni kidogo. Hivyo Serikali inashauriwa kuitengea ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali fedha nyingi za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inakubaliana na maoni ya Kamati kuwa bajeti ya miradi ya maendeleo inayotengwa ni kidogo. Hata hivyo, kumekuwepo na jitihada za kuwasilisha maombi Wizara ya Fedha ya kutengewa fedha za maendeleo za ndani lakini jitihada hizi bado hazijafanikiwa kutokana na uwezo wa Serikali kuwa mdogo. Mfano, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeomba jumla ya Shilingi bilioni 50.0 fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi za Makao Makuu na Ofisi mpya za Mikoani ili kuondokana na tatizo la kupanga katika majengo binafsi kwa gharama kubwa. Hata hivyo fedha zilizotengwa ni shilling 457,149,000 ambazo ni fedha za nje.

(viii) Serikali iboreshe maslahi ya watumishi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuwapa motisha ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Serikali imeendelea na jitihada za kuboresha maslahi ya watumishi wake kwa kutoa motisha mbalimbali ili kuongeza tija na ari ya utendaji kazi. Kwa upande wa Mawakili wa Serikali, mishahara imeboreshwa, Mawakili wanalipwa posho kwa ajili ya kodi ya pango

la nyumba, na posho ya mavazi. Aidha, watumishi wote wanalipwa posho ya muda wa ziada baada ya saa za kazi na siku za mapumuziko.

(ix) Kurugenzi ya Mashtaka iongezewe uwezo kifedha ili iweze kutekeleza vyema Mpango wake wa kutenganisha suala la Upelelezi na uendeshaji wa Mashtaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa Fedha 2013/2014 Serikali iliongeza bajeti ya Divisheni ya Mashtaka kutoka Shilingi 10,844,037,000 hadi Shilingi 20,844,037,000 kwa ajili ya kutekeleza malengo yaliyopangwa. Kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 Divisheni ya Mashtaka imetengewa jumla ya shilingi bilioni 22,144,326,000/=.

(x) Wizara inunue vifaa vya kisasa kama kompyuta na Samani za ndani kwa Mahakama zote nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilielezwa kuwa Wizara kupitia Mahakama ya Tanzania itahakikisha kuwa Mahakama zake zinapata vitendea kazi muhimu ili kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kulingana na uwezo wa Serikali kifedha uliopo.

(xi) Serikali itoe fedha za maendeleo zilizotengwa kwa mahakama ili kuwezesha miradi ya ujenzi wa mahakama kuendelea kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia mwezi wa Machi, 31, 2014 Mahakama ilikuwa imepokea fedha kiasi cha shilingi 5,508,842,840 kati Tshs. 42, 716, 668, 000/= ikiwa ni bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kutekeleza bajeti, ambazo zimetumika katika kufanya kazi zifuatazo:-

- Kufanya uchambuzi wa kumpata mshauri elekezi kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Mahakama Tanzania.

- Kufanya ukaguzi wa ukarabati wa mahakama nchi nzima kwa kutumia mshauri elekezi (TBA).

- Kuendelea kufanya ukarabati wa Mahakama Kuu, Dar es Salaam na Mtwara ambao unategemea kumalizika ifikapo mwei Juni, 2014.

- Ujenzi wa Mahakama Kuu Bukoba awamu ya Tatu unaendelea na unategemea kumalizika ifikapo Juni, 2014.

(xii) Mahakama ipewe fedha za kujengea majengo ya Mahakama Kuu kwenye Mikoa ya Kigoma, Mara, Lindi, Morogoro, Singida, Manyara, Katavi, Njombe, Simiyu na Pwani ili kupunguza kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa ni azma ya Serikali kuhakikisha kuwa kila mkoa unakuwa na Mahakama Kuu katika kipindi kifupi iwezekanavyo. Hivyo, Mahakama imejizatiti kuhakikisha kwamba dhamira hiyo ya Serikali inatimizwa kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

(xiii)) Mahakama ibuni njia bora zaidi za upimaji wa utendaji kazi wa Mahakimu na Majaji ili kuongeza ufanisi na utendaji wa Mahakama kwenye kazi zake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Mahakama imeshaweka utaratibu bora, shirikishi na wa uwazi katika upimaji wa utendaji kazi wa Mahakimu na Majaji kwa kuwa na viwango na idadi maalum vya uondoshaji wa mashauri kwa mwaka.

(xiv) Serikali iharakishe kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa Mradi wa tele justice ili Mahakama iweze kuondokana na mfumo wa zamani wa kerekodi mienendo ya kesi kwa njia ya mkono.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Taarifa ya upembuzi yakinifu wa Mradi huu imekamilishwa na kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais - Tume ya Mipango kwa hatua za kupata fedha na hatua nyingine za utekelezaji.

(xv) Serikali iimarishe Mfuko wa Mahakama kibajeti ili mfuko huo uweze kukidhi mahitaji ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Mfuko wa Mahakama umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Mahakama Sura ya 237. Kwa mwaka 2013/2014 Mfuko huu umetengewa Shilingi Bilioni 129.69. Hata hivyo, Mfuko huu umekuwa ukiidhinishiwa fedha kidogo na pia kutolewa kwa kuchelewa na hivyo kutokidhi mahitaji yake ya msingi. Hali hii inaufanya mfuko huu kutokutekeleza kazi zake kulingana na malengo ya kuanzishwa kwake.

(xvi) Serikali iweke utaratibu wa kutoa motisha kwa Mahakimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilielezwa kwamba Mahakama inajitahidi kutoa motisha kwa watumishi wake wa ngazi mbalimbali kwa kadri bajeti inavyoruhusu. Watumishi wamekuwa wanapatiwa motisha ya aina mbalimbali kama vile kulipa kodi ya pango, kutoa vyombo vya usafiri, kulipa stahili kwa wakati kama fedha za likizo, posho za ziada, matibabu, mazishi; kutoa fursa za mafunzo na kubadilishana uzoefu kwa kuhamia katika vituo vingine kwa muda.

(xvii) Sera ya Mabaraza ya Ardhi ya vijijini kuwa chini ya Wizara ya Ardhi iangaliwe upya na ikiwezekana Mabaraza hayo yawe chini ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa hili ni suala la kisera ambalo linahitaji muda wa kutosha kulishughulikia kwa kushirikisha vyombo mbalimbali vya maamuzi. Hata hivyo, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria ilifanya utafiti wa Mabaraza hayo na taarifa yake ipo tayari.

(xviii) Serikali iipatie Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini kiasi cha Shilingi Bilioni 17 ambacho kilitakiwa kutolewa na Serikali kama ubia katika ujenzi wa Jengo la Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA TOWER).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Wizara iliwasilisha maombi yake Hazina ya kupatiwa kiasi hicho cha fedha katika mwaka wa fedha 2013/14 ambacho ni sehemu ya malipo ya ada ya usimamizi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuahidiwa kiasi cha shilingi bilioni 2 katika bajeti ya mwaka 2014/2015. Kiasi hiki cha fedha kingechangia katika ujenzi wa jengo la Wakala. Hata hivyo, kiasi hicho cha fedha hakikutengwa katika makadirio ya bajeti ya mwaka husika. Jengo la RITA Tower linajengwa kwa ubia kati ya RITA na Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF).

(xix) Mpango wa kusajili watoto wa chini ya umri wa miaka mitano (U5BRI) usambazwe katika Wilaya zote nchini ili kuhakikisha watoto wote wanasajiliwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Mpango wa usajili wa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano (U5BR) ulizinduliwa rasmi tarehe 23 Julai, 2013 katika Halmashauri 10 za Mkoa wa Mbeya na kusajili zaidi ya watoto 132,387. Mpango huu unatarajiwa kuenezwa katika mkoa wa Mwanza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 na baadae kuenezwa katika mikoa ya Shinyanga, Geita na Simiyu. Hadi sasa Wakala umetambulisha Mpango katika ngazi ya Sekretarieti ya Mkoa na kufanya vikao vya hamasa na Makatibu Tawala wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Waganga Wakuu wa Wilaya na wa Mkoa, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya awali. Kazi hii imefanyika sanjari na kufanya utafiti wa awali (baseline) kama hatua za awali za kuusambaza mfumo huo katika Mkoa husika.

(xx) Matukio ya uvunjwaji wa haki na kutoa ripoti zake mapema ili kuwawezesha Wananchi kujua hali ya Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kwamba utaratibu wa usuluhishi na upatanishi kama mbinu mbadala za kuharakisha utatuzi wa baadhi ya migogoro umeanzishwa.

Kwa kutumia njia hii, Tume imeweza kufanya usuluhishi na upatanishi katika mashauri 25 kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ambapo ufumbuzi wa haraka wa mashauri hayo ulipatikana. Aidha:-

(i) Tume imeendelea kutoa elimu katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kuiwezesha jamii kujua misingi ya haki za binadamu na utawala bora;

(ii) Kuendelea kuboresha mfumo wa kompyuta katika kushughulikia malalamiko (Case Management System) pamoja na maboresho katika mfumo wa kompyuta unaopokea malalamiko kwa njia ya ujumbe wa simu (SMS for Human Rights);

(iii) Tume imezindua Mpango kazi wa kitaifa wa Haki za Binadamu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Mpango kazi huu utasaidia jamii kutambua na kuzingatia misingi ya haki za binadamu katika kutekeleza majukumu yao; na

(iv) Tume imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake hasa katika fani mbalimbali hasa za uchunguzi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

(xxi) Serikali iipatie Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora fedha za kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, ikiwa ni pamoja na kuchapa Ripoti za Haki za Binadamu za kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2014/15, Serikali imeongeza Bajeti ya Tume kutoka Shillingi 3,795,802,000 hadi Shilingi 4,795,802,000 fedha za matumizi mengineyo ambapo Tume imepanga kutumia ongezeko hili katika kuboresha utekelezaji wa majukumu yake.

(xxii) Serikali iangalie uwezekano wa kurekebisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi kutokana na mifumo iliyopo kutokidhi mahitaji na hali halisi ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Tume imekamilisha Taarifa ya Mapitio ya Sheria zinazohusiana na Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi. Taarifa hiyo imekwisha wasilishwa kwa Waziri wa katiba na sheria kwa hatua za maamuzi.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA KATIBA NA SHERIA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE**

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Wizara ya Katiba na Sheria ilikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

(i) Ukomo wa bajeti kwani kiasi cha fedha kinachotengwa kwa Wizara kimekuwa hakikidhi mahitaji halisi ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake hakizingatii mpango kazi wa wizara. Kwa mfano kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 Tume ya Utumishi wa Mahakama imetengewa Tsh 2,871,738,000 wakati mahitaji halisi ni Tsh 4,341,738,000. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imetengewa Tsh 8,332,865,000 wakati mahitaji halisi ni Tsh 13,400,000,000.

(ii) Baadhi ya Taasisi kutegemea majengo ya Ofisi za kupanga kwa gharama kubwa hivyo kupunguza uwezo wa kuboresha huduma zake hali hii inayopunguza ari ya kufanya kazi miongoni mwa watumishi wa wizara . Mfano wa Ofisi zilizo katika majengo ya kupanga ni Ofisi karibu zote zilizoko Mikoani zinazotumiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliyopo Jengo la Sukari House, jijini Dar es Salaam.

(iii) Kukosekana kwa fursa ya kupatiwa mikopo kwa wanafunzi wa Taasisi ya mafunzo ya Uanasheria kwa vitendo(The Law School of Tanzania). Hali hii inapunguza uwezo wa Taasisi hiyo wa kudahili idadi kubwa ya wanafunzi pamoja na kusababisha migogoro na migomo ya mara kwa mara kwa wanafunzi waliodahiliwa.

(iv) Watumishi wa Wizara kuacha kazi na kujiunga na Taasisi nyingine kwa lengo la kutafuta maslahi bora na kusababisha kuongezeka kwa tatizo la uhaba wa watumishi.

(v) Uhaba wa rasilimali watu umeendelea kuwa tatizo katika Taasisi, Idara na Vitengo mbalimbali hivyo kuathiri kiwango cha ufanisi katika utoaji huduma kwa wananchi. Mfano, mahitaji halisi ya Watumishi katika Wizara na Taasisi zake ni 9,351 wakati Watumishi waliopo sasa ni 6,913.

(vi) Vitendo vya rushwa kuendelea kujitokeza miongoni mwa watumishi na kusababisha Wizara ya Katiba na Sheria kuwekwa katika nafasi ya pili katika Taasisi ambazo watumishi wake wanahusishwa na rushwa hapa nchini.

(vii) Mazingira duni ya kufanyia kazi kwa Watumishi wa Wizara pamoja na Taasisi zake hususan ukosefu wa majengo ya Mahakama za Mwanzo, Ofisi za Mawakili wa Serikali pamoja na taasisi nyingine. Hali hiyo inapunguza ari ya kufanya kazi miongozi mwa watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

(viii) Uwezo mdogo wa wananchi walio wengi kutumia vyombo vya kutoa haki na huduma za kisheria pamoja na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu mfumo uliopo wa Sheria na Mahakama nchini. Jambo hilo linasababisha baadhi ya Wananchi kujichukulia sheria mkononi kisha kupelekea kuongezeka kwa vitendo vya uvunjifu wa amani na ukiukwaji wa haki za Binadamu.

(ix) Kutotolewa kwa wakati na kwa ukamilifu fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake. Wizara na Taasisi zilizo chini yake zimekuwa zikichelewa kupata fedha zinazoidhinishwa na serikali au zimekuwa zikipata pungufu au kutopata kabisa. Mfano kwa Mwaka wa Fedha 2013/214 Mahakama ya Tanzania ilitengewa kiasi cha Shilingi 42.8 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Machi 31, Mahakama ilikuwa imepokea kiasi cha Tsh Bilioni 5.5 tu.

**UFAFANUZI WA SERIKALI KUHUSU HOJA MBALIMBALI ZA KAMATI**

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia taarifa ya utekelejaji wa bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2013/2014 na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Kamati yangu iliomba ufafanuzi kwa baadhi ya mambo ambayo yalionekana yanahitaji ufafanuzi wa ziada.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeyatolea ufafanuzi mambo hayo kama ifuatavyo:-

(a) Ufafanuzi kuhusu kufahamika kwa bajeti ya Bunge Maalumu la Katiba kwa Mwaka wa fedha 2013/2014 na kama ilipelekwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilielezwa kwamba bajeti ya Bunge Maalum ya Jumla ya Sh.Bilioni 24.4 ilipitishwa na Bunge lako Tukufu kwa Mwaka huo wa fedha kupitia Fungu-21 Hazina kwenye kifungu cha" Special Expenditure". Serikali ilitenga fedha hizo kwa kutambua kwamba Bunge Maalum lingeanza kazi kwa mwaka huo wa fedha na kwa wakati huo mahitaji halisi ya Bunge Maalum yalikuwa hayafahamiki. Aidha, kwa kutumia uzoefu uliopatikana katika uendeshaji wa Bunge hilo, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 20.0 katika Fungu 21 – Hazina kwenye kifungu cha "Special expenditure" katika mwaka wa fedha 2014/2015 ili kukamilisha kazi hiyo.

(b) Wizara kutoa maelezo kuhusu hatua zilizochukuliwa na Serikali kutokana na athari za operation Tokomeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa kufuatia Azimio la Bunge lililoitaka Serikali kuunda Tume ya Uchunguzi ili kuchunguza athari na hatua za kuchukua kwa wale waliohusika na usababishaji wa madhara yaliyojitokeza katika zoezi la Operation Tokomeza, Serikali imeunda Tume ya Uchunguzi Chini ya Sheria ya Commision of Inquiry Act, Sura ya 32 na kuitangaza kupitia Gazeti la Serikali Namba 131 la tarehe 2 Mei, 2014. Kupitia Tume hiyo, Makamishna watatu wameteuliwa kufanya kazi hiyo kwa mujibu wa hadidu za rejea walizopewa.

(c) Hatua zilizochukuliwa katika kupunguza mashauri mahakamani na msongamano wa mahabusu na wafungwa magerezani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Wizara na Taasisi zake wamechukua hatua mbalimbali za kupunguza mashauri mahakamani na idadi ya mahabusu na wafungwa magerezani. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji mashtaka na kudhibiti kesi zinazopelekwa Mahakamani,

(ii) Kutembelea magereza na maeneo ya vizuizi,

(iii) Kuanzisha mifumo ya kielektroniki ya utunzaji wa kumbukumbu za mashauri,

(iv) Kuweka mipango ya kuajiri idadi kubwa zaidi ya mawakili wa Serikali, mahakimu na watumishi wa kada nyingine,

(v) Kuwa na muda maalum wa kumaliza mashauri mapya kwa kila ngazi ya mahakama kwa mwaka,

(vi) Kuhakikisha kwamba mashauri yote yaliyosajiliwa yanamalizika katika kipindi kisichozidi miaka miwili,

(vii) Kutekeleza mkakati wa kujipima kwa wastani wa idadi ya mashauri yanayotolewa uamuzi kwa kila jaji na hakimu,

(viii) Msukumo unaofanyika kupitia Kamati za Kusukuma Kesi, na

(ix) Jukwaa la Haki Jinai la Taifa - Kuchukua hatua madhubuti kuondoa msongamano wa wafungwa na mahabusu.

(d) Kuhusu iwapo nakala ya Hati ya Muungano kuthibitishwa na Msajili wa Mahakama badala ya Katibu Mkuu Kiongozi ni ukiukwaji wa Sheria (vifungu vya 83 na 85 vya Sheria ya Ushahidi ) Sura ya 6.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa ufafanuzi kuhusu suala hili kwamba vifungu vya 83 na 85 vya Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 vinahusiana na nyaraka zinazowasilishwa Mahakamani kama Sehemu ya ushahidi. Kulingana na matakwa ya vifungu hivyo, nyaraka hizo zinazowasilishwa mahakamani ndizo zinazopaswa kuthibitishwa na Mhifadhi (Custodian) wa nyaraka husika. Kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Sheria ya Viapo, Sura ya 12, Msajili wa Mahakama ni mmoja kati ya watu wenye mamlaka ya kuthibitisha nakala ya Hati/Nyaraka. Hivyo, Msajili wa Mahakama kuthibitisha Hati ya Muungano haikuwa ukiukwaji wa Sheria yoyote.

(e) Maelezo kuhusu sababu za kupungua kwa bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2014/2015 kutoka Bilioni 260 kwa mwaka 2013/2014 hadi kufikia Bilioni 230.9 kwa Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 260. Fedha hizo zilijumuisha Sh. Bilioni 33,994,588,000 za Iliyokuwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Fungu-8, ambapo kwa mwaka huu wa Fedha Tume ya Mabadiliko ya Katiba imemaliza shughuli zake hivyo haikutengewa Fedha. Aidha, program ya Maboresho ya Sekta ya Sheria imemalizika hivyo kufanya fedha za nje kwa mwaka huu kupungua sana.

(f) Ufafanuzi juu ya maelekezo ya Mahakama kuhusu kifungu cha 148 cha sheria ya mwenendo wa Makosa ya Jinai na Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye kesi ya Balozi Prof. Costa Mahalu

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifafanuliwa kuwa katika kesi ya Prof. Mahalu Mahakama ilikitamka kifungu cha 36(4)(e)cha Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200 kuwa ni cha kibaguzi kwa kuwa kinatoa unafuu kwa watu wenye fedha kupata dhamana na kuwanyima haki hiyo wale wasio na fedha. Mahakama haikukitolea maelezo kifungu cha 148 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20. Katika kesi hiyo, Mahakama ilielekeza kifungu cha 36(4)(e) kifanyiwe marekebisho ili kiendane na matakwa ya Katiba. Serikali haikuridhika na uamuzi huo na hivyo iliamua kukata rufaa katika Mahakama ya Rufani kwa kutoa notisi ili kupinga uamuzi huo kwa misingi kwamba kifungu cha 36(4)(e) hakikinzani na Katiba. Marekebisho ya kifungu hicho hayajafanywa kwa kuwa rufaa dhidi ya uamuzi huo haijasikilizwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliendelea kuelezwa kuwa chanzo cha kesi hii ni kwamba Prof. Mahalu na mwenzake walishtakiwa kwa kosa la jinai Na.1/2007 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu ambapo dhamana ilizuiliwa kwa mujibu wa kifungu cha 36(4)(e) kinachoweka sharti la kuweka nusu ya kiasi cha fedha kinachohusika katika kesi kwa ajili ya dhamana. Hatua hii ilipelekea Prof. Mahalu kufungua shauri la Kikatiba na kuomba mahakama kutamka kuwa kifungu hicho ni cha kibaguzi. Wakati Serikali ikiendelea na mchakato wa rufaa kuhusu shauri la kikatiba, shauri la jinai lililokuwa Kisutu lilitolewa uamuzi ambapo Prof. Mahalu aliachiwa huru. Serikali ilikata Rufaa dhidi ya uamuzi wa kuachiwa Prof. Mahalu kupitia rufaa Na.135/2012 ambapo baadaye rufaa hii iliondolewa na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP).

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Kamati yangu iliridhika na ufafanuzi huu wa Serikali.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati pamoja na majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zilizo chini yake, Kamati inatoa maoni na ushauri kwa Wizara na Taasisi zilizo chini yake ili kuboresha utendaji kazi kwa lengo la kuleta ufanisi kwa manufaa ya Taifa kama ifuatavyo:-

**TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA - FUNGU 12**

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 113 ya Katiba ya Jamhuri Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake, ikisomwa pampja na Sheria ya Utumishi wa Mahakama, Sura ,237, ikiwa na majukumu ya kusimamia maadili na nidhamu kwa watumishi wa Tume/Mahakama pamoja na kuboresha menejimenti ya watu ndani ya Tume na Utumishi wa mahakama. Kutokana na umuhimu wa Taasisi hii, Kamati inashauri kama ifuatavyo :-

Kwa kuwa katika mwaka wa fedha 2013/2014 Tume haikutengewa fedha za maendeleo, Kamati inaendelea kushauri Tume itengewe fedha za kutosha na fedha zilizoidhinishwa zitolewe kwa wakati.

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara, baadhi ya watumishi wa Wizara wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya rushwa hivyo kusababisha Wizara kuwa katika nafasi ya pili kwa kujihusisha na rushwa,kamati ina shauri Tume ya Utumshi wa mahakama kujengewa uwezo ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kuthibiti hali hii hatari'

Kutokana na uhaba wa fedha Serikalini na ukomo wa bajeti iliyopewa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Kamati inashauri Wizara kufanya utaratibu wa kuhamishia kiasi cha Shilingi Bilioni moja na Millioni mia nne(1,400,000,000/=)kutoka mfuko wa Mahakama mapema kwenda Tume ya Utumishi wa Mahakama ili kuiwezesha Tume hiyo kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Kwa kuwa bado hakuna uelewa wa kutosha kwa wananchi kuhusu uwepo wa Tume na Kamati za Maadili za Mahakama pamoja na Majukumu ya yake, Kamati inashauri kuwa Elimu kuhusu uwepo wa Tume pamoja na majukumu yake iendelee kutolewa hasa vijijni ili kuwawezesha wananchi kuitumia kwa kupeleka malalamiko wakiona kuna ukiukwaji wa maadili.

**OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**
**Fungu 16**

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia utekelezaji wa majukumu na makisio ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kamati ilibaini changamoto mbalimbali zinazokabili ofisi ya mwanasheria mkuu wa Serikali, hivyo inashauri ifuatavyo ili kuboresha utendaji wake:-

(i) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ijengewe uwezo katika kitengo cha mikataba kwa kuwapatia mafunzo Mawakili wa Serikali katika masuala ya mikataba ya mafuta na gesi ili kuhakikisha kuwa watendaji hao wanatumika ipasavyo kuishauri Serikali kuingia mikataba yenye tija kwa taifa kuhusu sekta hizo na nyingine.

(ii) Kwa kuwa kumekuwa na kuongezeka kwa matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaosababisha uvunjifu wa amani, Kamati inashauri Serikali iimarishe mfumo wa utoaji haki ili kuhakikisha kwamba amani na utulivu vinaendelea kuwepo na kuimarika kwa wananchi kupata haki sawa na kwa wakati.

(iii) Kwa kuwa Serikali imeendelea kuijengea uwezo Mahakama ya Tanzania kupitia Mfuko wa Mahakama na kwa kuzingatia kuwa Mwasheria Mkuu wa Serikali ni mdau mkubwa katika utekelezaji wa shughuli za Mahakama, Kamati inashauri kwamba maboresho ya Mahakama yaende sambamba na maboresho ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha kuwa vyombo hivi vinafanya kazi kwa ufanisi katika kuhakikisha kuwa azma ya utoaji haki sawa na kwa wakati inafikiwa.

(iv) Serikali iendelee kuboresha maslahi ya watumishi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hususan Mawakili wa Serikali ili kuwapa motisha watumishi hao kufanya kazi kwa bidii na kwa uadilifu mkubwa.

(v) Kamati inashauri Serikali itenge fedha za ndani za kutosha na kutoa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili iweze kujenga ofisi na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Taasisi hii.

**MKURUGENZI WA MASHITAKA (DPP) - Fungu 35**

Mheshimiwa Spika, Divisheni ya Mashtaka katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeanzishwa kupitia Ibara ya 59B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake kwa ajili ya kutekeleza jukumu muhimu katika Taifa la kuendesha Mashtaka na kuratibu kazi zinazofanywa na vyombo vya uchunguzi kama yalivyoainishwa na Katiba na sheria zingine. Kutokana na umuhimu huo, ili kuimarisha na kuboresha Divisheni hii, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Divisheni ya Mashtaka ijengewe uwezo kwa kupewa kibali cha kuajiri watumishi 489 na kuwapatia mafunzo ili waweze kutekeleza majukumu yao kama ilivyokusudiwa.

(ii) Serikali itoe fedha za matumizi ya kawaida ili Ofisi hii iweze kutekeleza majukumu yake ikiwemo kutembelea magereza, kuendesha mashtaka na kuratibu shughuli zinazofanywa na vyombo vya upelelezi Nchini.

**MAHAKAMA - Fungu 40**

Mheshimiwa Spika, Kamati iliitembelea Mahakama ya Tanzania mnamo Mwezi Februari, 2014 ili kupokea taarifa ya utekelezaji wa Majukumu ya taasisi hii katika Mwaka wa Fedha 2013/2014. Katika ziara hiyo Kamati ilielezwa kuhusu mikakati iliyopangwa na inayotekelezwa juu ya namna ya kupunguza mlundikano wa mashauri Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, moja ya Mikakati ya Mahakama ya kupunguza mlundikano wa mashauri ni kuwa na takwimu sahihi na zinazoaminika za mashauri nchini kote. Mahakama imeainisha mashauri yote kwa miaka yake ya kusajiliwa na kuanza kuyashughulikia kwa kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine ni kuanzishwa kwa mpango wa ufanyaji kazi kwa kujipima utendaji kazi (performance based).Katika mpango huo kila ngazi ya mahakama imejiwekea wastani wa idadi ya mashauri itakayo yamaliza kwa mwaka. Mfano, mahakama ya rufani imeweka lengo la kumalliza

mashauri 1200 hadi 1400 kwa mwaka,mahakama kuu 220 hadi 250 kwa kila Jaji kwa mwaka na mahakama za hakimu mkazi na Wilaya kesi 250 hadi 300 kwa kila hakimu kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa kazi za mahakama kwa kuongeza vitendea kazi na rasilimali watu ni mkakati mwingine uliochukuliwa na Taasisi hii ili kupunguza mlundikano wa mashauri

Mheshimiwa Spika, sote tunatambua kuwa Mahakama sio miongoni mwa maeneo sita ya vipaumbele vya Taifa yaliyomo katika mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN). Hata hivyo, mahakama katika mpango wake wa ndani imeweza kuandaa na kutekeleza mpango unaofanana na mpango wa BRN na kupata mafaniko makubwa kwa muda mfupi ikiwemo kupunguza mashauri mahakamani. Kamati inapongeza juhudi hizo zinazofanywa na uongozi wa mahakama katika kukabiliana na changamoto ya mlundikano wa mashauri Mahakamani (back logs) na nyingine ili kufikia azma ya kutoa haki kwa wote na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na kasi hii na tunaamini kwamba kama kasi hii itaendelea Mahakama inaweza kumaliza kabisa tatizo la mlundikano wa mashauri mahakamani. Pamoja na jitihada hizi Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Fedha zinazotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama ziwekewe wigo (ring fenced) ili kuhakikisha kuwa zinatumika kwa malengo yanayokusudiwa. Aidha, Fedha za Mfuko wa Mahakama zisifananishwe na fedha za matumizi ya kawaida (OC) bali zipewe uzito stahiki na kutolewa kwa wakati.

(ii) Kwa kuwa kumekuwa na tatizo la ufinyu wa bajeti na kuchelewa kutolewa au kutotolewa kabisa kwa Fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya mahakama. Mfano katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 Mahakama iliidhinishiwa Sh. Bilioni 42. Hadi kufikia Machi 31, 2014, ni kiasi cha shilingi bilioni 5.5 tu ndizo zilikuwa zimetolewa, Kamati inashauri kuwa bajeti ya Mahakama iongezwe na fedha zinazoidhinishwa zitolewe kwa wakati ili kuiwezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

(iii) Mahakama ipewe kibali cha kuajiri watumishi wengine wakiwemo mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ili kupunguza tatizo la upungufu wa watumishi sambamba na kuboresha maslahi ya Watumishi hao.

(iv) Kutokana na upungufu na uduni wa Ofisi pamoja na vitendea kazi, Kamati inashauri hatua za makusudi na za haraka zichukuliwe ili kujenga

majengo ya Mahakama na kuweka vitendea kazi bora na vya kisasa ili kuamsha ari ya utendaji kazi miongoni mwa watumishi wa Mahakama.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA – Fungu 41**

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria ndiyo mhimili mkuu wa Serikali katika masuala yote ya kisheria katika nchi ikiwa na jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa kunakuwa na utawala wa sheria unaozingatia Katiba na kuwepo kwa mfumo wa sheria unaotoa fursa sawa kwa watu wote katika jamii ili kuweza kuendesha shughuli zao kwa ufanisi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, amani na utulivu uliopo nchini ni matunda ya usimamizi makini wa mfumo wa utawala wa Sheria, hivyo, ni dhahiri kuwa Wizara hii ni muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu. Kwa kuzingatia unyeti wa Wizara hii na ili iendelee kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Kamati imebaini kwamba utoaji wa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Wizara hii hauridhishi. Kwa Mfano kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 Wizara ilitengewa Sh. 7,069, 331,500. Hadi kufikia Machi, 2014, ni kiasi cha sh 2,355,175,821 tu sawa na asilimia 29 tu ndizo zilizokuwa zimetolewa. Kamati inashauri kuwa kasi ya utoaji wa fedha zinazotengwa na Wizara na kupitishwa na Bunge iongezwe na zitolewe kwa wakati ili kuwezesha ufanikishaji wa utekelezaji wa shughuli hizo.

(ii) Serikali kuweka kipaumbele miradi ya maendeleo na kutenga fedha za ndani kwa ajili hiyo kuliko kutegemea fedha za nje.

(iii) Kwa kuwa Wizara imekwishapelekewa na Tume ya Marekebisho ya Sheria, Taarifa ya Mapendekezo ya mfumo bora wa utatuzi wa migogoro ya ardhi ,Kamati inashauri taarifa hiyo ifanyiwe kazi mapema ili mfumo bora wa utatuzi wa migogoro uanze kutumika kwa lengo la kumaliza migogoro ya ardhi inayoendelea hapa nchini.

(iv) Kamati ilielezwa kwamba Wizara ina upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali. Katika kukabiliana na changamoto hiyo Wizara iliomba kibali cha kuajiri watumishi 22 kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 lakini hakikutolewa. Hivyo Kamati inashauri kwamba vibali hivyo vitolewe ili kuijengea uwezo Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**TUME YA KUREKEBISHA SHERIA - Fungu 59**

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria ni Taasisi ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria iliyoanzishwa kwa mujibu Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura 171. Majukumu ya Tume ni kufanya mapitio ya Sheria Mbalimbali na kufanya utafiti kisha kuandaa mapendekezo na kuyawasilisha kwa Waziri wa Katiba na Sheria ambaye huyawasilisha Bungeni kwa ajili ya utunzi wa Sheria au kuzifanyia mabadiliko Sheria zinazokuwa zina mapungufu katika kuhakikisha kuwa Sheria za nchi zinaenda sanjari na mazingira ya sasa katika kudumisha utawala wa Sheria na usimamizi wa Haki nchini.

Ili kuboresha utendaji kazi wa Tume, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Tume ijengewe uwezo kwa kupewa kibali cha kuajiri Watumishi wa kutosha wenye ujuzi katika masuala stahiki ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, watumishi waliopo wajengewe uwezo kwa kupewa mafunzo katika fani zao.

(ii) Serikali ihakikishe inatoa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Tume ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

(iii) Kwa kuwa Utafiti ni moja ya majukumu ya Tume, Kamati inashauri kwamba Tume ipewe vitendea kazi vya kutosha ikiwemo magari ili kurahisisha usafiri kwenda kufanya utafiti maeneo mbalimbali.

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA - Fungu 55**

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni idara huru ya Serikali ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria iliyoundwa kwa mujibu wa Ibara ya 129 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake ikisomwa pamoja na Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Sura 391. Majukumu ya Tume yameainishwa katika Ibara ya 130 (1) ya Katiba. Jukumu kubwa la Tume hii ni kulinda, kutetea na kuhifadhi haki za binadamu nchini. Ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati yangu inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iimarishe idara hii kwa kuitengea bajeti ya kutosha na kuhakikisha kuwa fedha zinazotengwa na kuidhinishwa na Bunge zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake na kufikia lengo na Taifa lililokusudiwa; na

(ii) Kwa kuwa rasilimali watu ni nyenzo muhimu katika ufanisi wowote wa maendeleo,Kamati inashauri Tume ijengewe uwezo kwa kuongeza watumishi wenye ujuzi katika masuala mbalimbali na kupewa vitendea kazi stahiki ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**WAKALA WA USAJILI, UFILISI NA UDHAMINI**
**(Registration, Insolvency and Trusteeship Agency-RITA)**

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usajili ,Ufilisi na Udhamini (RITA) ni idara ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria yenye jukumu la kusajili na kuweka kumbukumbuku muhimu za maisha ya binadamu nchini kwa maendeleo ya Taifa. Kwa kuzingatia umuhimu wa idara hii kamati inatoa ushauri ufuatao ili kuimarisha na kuboresha idara hii:-

(i) Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) iliingia ubia wa kujenga jengo lake katika mtaa wa Makunganya jijini Dar es salaam. Gharama za ujenzi ilikuwa shilingi bilioni 35 ambapo kati ya fedha hizo, RITA walipaswa kutoa shilingi bilioni 17, lakini hadi sasa wametoa bilioni 1 tu. Kamati inashauri kuwa Serikali itoe kiasi cha Fedha kinachodaiwa ili kuepuka riba kubwa itakayotokea endapo fedha zitachelewa kulipwa.

(ii) Kwa upande mwingine, Kamati inaipongeza RITA kwa kazi nzuri wanayoifanya na mafanikio makubwa waliyoyapata katika kutekeleza mpango wa kusajili watoto chini ya umri wa miaka mitano unaojulikana kama U5BRI-Under five Birth Registration Initiative katika Mkoa wa Mbeya na maeneo mengine nchini. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuuwezesha kibajeti Wakala ili uweze kutekeleza mpango wake ilioubuni wa U5BRI (Underfive Birth Registration Initiatives) na kuusambaza katika mikoa mingine nchini.

**MAOMBI YA FEDHA NA MALENGO YA BAJETI KWA**
**MWAKA WA FEDHA 2013/2014**

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu ipasavyo,Wizara ya Katiba na Sheria inaomba fedha kwa mwaka 2014/2015 kwa muhtasari kwa mafungu kama ifuatavyo:- Fungu 12 –Tume ya Utumishi ya Mahakama (Tsh 3.080.480.000); Fungu 16 –Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Tsh,11.216.912.000); Fungu 35-Kurugenzi ya Mashtaka (Tsh. 22.144.326.000); Fungu 40 – Mahakama (Tsh.166.388.093.000); Fungu 41-Wizara ya Katiba na Sheria (Tsh.16.231.914.000); Fungu 55 –Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Tsh. 7.339.564.000); na Fungu 59-Tume ya kurekebisha Sheria (Tsh.8.577.362.121) kama alivyoeleza Mheshimiwa waziri wa Katiba na Sheria alipokuwa anawasilisha hoja yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

**HITIMISHO**

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii muhimu ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu. Pia,

namshukuru Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Dkt Asha- Rose Migiro, (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Angela Jasmine Kairuki (Mb), Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Jaji Frederick Werema, (Mb), na Naibu Mwansheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa George M. Masaju kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Vile vile nawashukuru Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria na Wakuu wa Taasisi pamoja na Maafisa Waandamizi wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano waliotupatia.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Uzoefu wao wa muda mrefu katika masuala mbalimbali kuhusu sekta ya sheria, Haki za Binadamu na Utawala Bora umesaidia kufanikisha kazi hii kwa ufanisi. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. William Mganga Ngeleja, (Mb) - Mwenyekiti
2. Mhe. Gosbert Begumisa Blandes, (Mb)- M/Mwenyekiti
3. Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu,(Mb)- Mjumbe
4. Mhe. Nimrod Elirehema Mkono,(Mb) - Mjumbe
5. Mhe. Halima James Mdee, (Mb) - Mjumbe
6. Mhe. Fakharia Khamis Shomar,(Mb) - Mjumbe
7. Mhe. Nyambari C.M Nyangwine, (Mb) - Mjumbe
8. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, (Mb ) - Mjumbe
9. Mhe. Felix Francis Mkosamali, (Mb) - Mjumbe
10. Mhe. Rukia Khasim Ahmed, (Mb) - Mjumbe
11. Mhe. Mustapha Boay Akunaay,(Mb) - Mjumbe
12. Mhe. Ramadhan Haji Saleh, (Mb) - Mjumbe
13. Mhe. Tundu Antipas Mughwai Lissu,(Mb) - Mjumbe
14. Mhe. Deogratias Aloys Ntukamazina,(Mb)- Mjumbe
15. Mhe. Jason Samson Rweikiza, (Mb) - Mjumbe
16. Mhe. Ali Khamis Seif,(Mb) - Mjumbe
17. Mhe. Abdallah Sharia Ameir,(Mb) - Mjumbe
18. Mhe. Mariam R. Kasembe,(Mb) - Mjumbe
19. Mhe. Zahra Ali Hamad, (Mb) - Mjumbe
20. Mhe,Shamsi Vuai Nahodha, (Mb) - Mjumbe

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru ndugu Matamus Fungo na ndugu Maria Mdulugu, kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kiidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake, kama yalivyowasilishwa na Mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

William Mganga Ngeleja (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA
Mei, 2014

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa ninamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni Maoni ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Mpango, Makadirio na Mapitio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka 2014/2015:-

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ninaomba irekodiwe katika *Hansard* kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri wa Katiba na Sheria imeanzishwa kwa mujibu wa kipengele cha 12 cha Nyongeza ya Waraka wa Rais uliochapishwa kama Tangazo la Serikali Na. 494 la tarehe 17 Desemba 2010. Majukumu ya Ofisi hii yameainishwa katika Tangazo la Ukasimishaji wa Majukumu ya Kiuwaziri la Mwaka 2010 *(The Ministers (Assignment of Ministerial Functions) Notice, 2010),* lililochapishwa katika Gazeti la Serikali kama Tangazo la Serikali Na. 494A la tarehe 17 Desemba, 2010. Kwa mujibu wa Nyongeza ya Pili ya Tangazo hilo, pamoja na mengine, Ofisi ya Waziri wa Katiba na Sheria imekasimiwa majukumu ya masuala ya kikatiba, uendeshaji, utoaji wa haki, uendeshaji mashtaka na haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, majukumu haya ni mazito katika hali ya kawaida, kwani mfumo wa kikatiba, haki za binadamu na utoaji haki katika nchi yenye kufuata mfumo wa kidemokrasia ndiyo roho ya mfumo mzima wa utawala. Mfumo wa kikatiba na wa utoaji haki ndiyo unaotofautisha dola iliyoparaganyika (*a failed state*) na dola inayoongozwa kikatiba (*a constitutional state*) na utawala wa sheria (*rule of law*). Majukumu haya ni mazito zaidi katika nchi ambayo, kama ilivyo nchi yetu, inatengeneza Katiba Mpya. Hapa, vilevile, mfumo unaotumika kutengeneza Katiba Mpya ndiyo

utakaotofautisha nchi hiyo kuwa *a failed state* au kuwa nchi yenye mfumo imara wa kikatiba na wa kisiasa. Kwa sababu hiyo, kwa vyovyote vile, majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria ni mazito na yenye umuhimu mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Bunge Maalum na Harufu ya Ufisadi: Vyombo vya habari mbalimbali hapa nchini vimemnukuu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, akisema kwamba, hadi kuahirishwa kwake, Bunge Maalum limetumia zaidi ya Shilingi bilioni 27. Kama kauli ya Waziri wa Fedha ni sahihi, kiasi hiki cha fedha kitakuwa kikubwa kuliko fedha za Matumizi ya Kawaida ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Divisheni ya Uendeshaji Mashtaka na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kwa ujumla wao kwa mwaka unaoisha wa fedha. Hiki siyo kiasi kidogo cha fedha katika nchi kama yetu ambayo shughuli mbalimbali za huduma za jamii zimekwama kwa ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati Bunge lako Tukufu linajadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala iliagiza bajeti ya Bunge Maalum iletwe Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa. Kamati ilitoa agizo hilo kwa sababu wakati Wizara ilikuwa imewasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba, yaani Fungu 08, hakukuwa na Fungu lolote linalohusu Bunge Maalum. Hii ni licha ya ukweli kwamba, hadi kufikia mwaka jana, tayari ilikuwa inajulikana kwamba kutakuwa na Bunge Maalum, kwa sababu vifungu husika vya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba vilikwishapitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Agizo la Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala lilipuuzwa mwaka jana kwani Serikali hii sikivu ya CCM, haikuleta makadirio ya mapato na matumizi ya Bunge Maalum kwa ajili ya kujadiliwa na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Mwaka huu pia agizo hilo limepuuzwa kwani hakuna Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bunge Maalum ambayo yameletwa kwa ajili ya kujadiliwa na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Ili kuhalalisha vitendo vyake vya kupuuza agizo la Bunge lako Tukufu, Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Mtengeti Migiro, alidai mbele ya Kamati kwamba, masuala yote ya Bunge la Katiba yapo chini ya Bunge Maalum la Katiba, ambapo fedha kwa ajili ya Bunge hili zinatolewa na Mfuko Mkuu wa Hazina. Kwa jibu hili, Waziri alitaka kuiaminisha Kamati kwamba, hakukuwa na haja ya fedha za Bunge Maalum kujadiliwa na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu, kwa sababu tu fedha hizo zilikuwa zinatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuoneshwa kwamba, fedha zinazolipwa kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina hazina budi kuidhinishwa na sheria iliyotungwa na Bunge na matumizi yake kuidhinishwa na Sheria ya Matumizi ya Serikali, sasa Waziri amebadili kauli na kudai kwamba, fedha za matumizi ya Bunge Maalum ziliidhinishwa na Bunge lako Tukufu! Katika Majibu yake ya Hoja za Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala wakati wa kupitia Makadirio ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Mheshimiwa Waziri amesema yafuatayo: "Bajeti ya Bunge Maalum ya shilingi bilioni 24.4 ilipitishwa na Bunge katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 kupitia Fungu 21 – Hazina kwenye kifungu cha *Special Expenditure*. Serikali ilifanya hivyo kwa kutambua kwamba, Bunge Maalum lingeanza kazi zake katika mwaka huo wa fedha. Wakati huo mahitaji halisi ya uendeshaji wa Bunge hilo yalikuwa hayafahamiki." Waziri ameongeza kusema kwamba, kwa kutumia uzoefu uliopatikana katika uendeshaji wa Bunge hilo, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 20 kwenye Fungu 21 –Hazina kwenye kifungu cha *Special Expenditure* katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 ili kukamilisha kazi zilizosalia.

Mheshimiwa Spika, kauli za Waziri wa Katiba na Sheria juu ya masuala yote yanayohusu Bajeti ya Bunge Maalum, hazina ukweli wowote. Kwanza, kuhusu kiasi cha fedha kilichokwishatumika kwa ajili ya Bunge Maalum. Kauli ya Waziri kwamba, kiasi hicho ni shilingi bilioni 24.4, inapingana moja kwa moja na kauli iliyotolewa na Waziri wa Fedha ndani ya Bunge Maalum. Kwa mujibu wa Taarifa Rasmi *(Hansard)* ya Majadiliano ya Bunge Maalum ya Kikao cha Ishirini na Tisa cha tarehe 24 Aprili, 2014, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, alisema yafuatayo kuhusu matumizi ya Bunge Maalum: "Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwamba, hatutumii fursa hii, nasikitika tumechukua fedha, yaani kodi ya Wananchi ambao kila siku wanalia na wameweza ku-*sacrifice* tunakwenda kwenye *twenty seven billions* kwa ajili ya *session* hii, tumeweza ku-*sacrifice* kupeleka umeme kwa Wananchi, hususan vijijini." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiasi kilichotajwa na Waziri wa Fedha kinalingana na kiasi kilichotajwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Utaribu na Bunge), Mheshimiwa William Lukuvi, aliyeiambia Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwamba, hadi linaahirishwa tarehe 25 Aprili mwaka huu, Bunge Maalum lilikwishatumia takribani shilingi bilioni 27.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu linahitaji majibu ya kuridhisha kuhusu mkanganyiko huu katika kauli za Waziri wa Katiba na Sheria na Mawaziri wenzake wa Fedha na Sera, Uratibu na Bunge. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM ilieleze Bunge lako Tukufu ni kauli ya Waziri yupi kati ya hawa watatu ndiyo iaminiwe na kuchukuliwa kuwa ndiyo kauli sahihi na Bunge lako Tukufu? Aidha, kama itajulikana kwamba mmojawapo kati ya Mawaziri hawa watatu ametoa taarifa za uongo kwa

Kamati ya Bunge lako Tukufu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka mamlaka ya uteuzi, yaani Rais wa Jamhuri ya Muungano, awawajibishe kwa kuwafukuza kazi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, Waziri anayedanganya Bunge lako Tukufu au Kamati zake siyo tu analidharau Bunge, bali pia anaidharau mamlaka ya uteuzi wake, yaani Rais. Vinginevyo, Bunge lako Tukufu liambiwe kwamba Waziri huyo ametumwa na Rais kuja kudanganya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uongo wa pili wa kauli ya Waziri wa Katiba na Sheria unahusu madai yake kwamba, Bajeti ya Bunge Maalum iko kwenye Fungu 21 – Hazina. Uthibitisho wa uongo huu uko kwenye Kitabu cha II cha Makadirio ya Matumizi ya Umma ya Huduma za Mfuko Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, kilichowasilishwa Bungeni mwaka jana; na Kitabu hicho hicho kilichowasilishwa Bungeni mwezi huu kwa ajili ya Mwaka wa Fedha 2014/2015. Katika Vitabu vyote viwili, hakuna kifungu chochote kinachoitwa *Special Expenditure* au kasma yoyote inayohusu Bunge Maalum. Aidha, hakuna kifungu chochote chenye makadirio ya matumizi ya shilingi bilioni 24.4 kwa ajili ya Bunge Maalum au kwa ajili nyingine yoyote katika Kitabu cha mwaka 2013/2014; na wala hakuna makadirio ya matumizi ya shilingi bilioni 20 kwa ajili ya matumizi ya Bunge Maalum katika Kitabu cha mwaka 2014/2015. Vilevile kwenye Vitabu vya Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Mwaka wa Fedha 2014/2015, hakuna kifungu chochote kinachoitwa *Special Expenditure* au chenye kiasi cha fedha kilichotajwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, kama hakuna vifungu vyovyote vya *Special Expenditure* kwa ajili ya Bunge Maalum na kama hakuna kiasi chochote kilichooneshwa kwenye Vitabu vya Bajeti, maana yake ni kwamba, Bunge lako Tukufu halijaidhinisha bajeti yoyote kwa ajili ya Bunge Maalum. Kwa kifupi, Waziri wa Katiba na Sheria amelidanganya Bunge lako Tukufu na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itaona ajabu sana endapo Bunge lako Tukufu litaamua, licha ya ushahidi wote huu, kufunika kombe ili mwanaharamu apite! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maoni yake juu ya Hotuba ya Waziri Mkuu kuhusu Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka 2014/2015, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, aliliambia Bunge lako Tukufu kwamba, fedha zote zilizotumika kwa ajili ya gharama mbalimbali za Bunge Maalum hazikuidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Ukweli ni kwamba, hadi sasa Bunge lako Tukufu halijui bajeti yote ya Bunge Maalum, halijui fedha kiasi gani zimetumika kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya miundombinu ya Bunge hili, kwa ajili ya posho, mishahara na stahili mbalimbali za Wajumbe na Watumishi wa Bunge Maalum hadi

lilipoahirishwa tarehe 25 Aprili, 2014. Aidha, Bunge lako Tukufu halina ufahamu wowote juu ya gharama za Bunge Maalum pale litakaporudi tarehe 5 Agosti, 2014, kuendelea kujadili Rasimu ya Katiba Mpya.

Katika hali hiyo, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni alitaka maswali yafuatayo yapatiwe majibu:-

(i) Je, bajeti ya matumizi ya Bunge Maalum ni kiasi gani na kwa ajili ya matumizi gani?

(ii) Je, ni kiasi gani cha fedha hizo kimeshatumika hadi sasa na kwa ajili ya matumizi gani?

(iii) Je, ni nani aliyejadili na kupitisha bajeti hiyo?

(iv) Je, ni Sheria gani iliyotungwa na Bunge lipi iliyoidhinisha matumizi haya ya fedha za umma?

(v) Je, ni lini na kwa Waraka gani Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliidhinisha matumizi haya?

Mheshimiwa Spika, maswali haya hayajapatiwa majibu yoyote. Badala yake, Waziri wa Katiba na Sheria amelipa Bunge lako Tukufu sababu za kuuliza maswali mengine yafuatayo:-

(a) Je, ni ukurasa upi kati ya kurasa za 55 - 60 zenye makadirio ya Fungu 21 – Hazina kwenye Kitabu cha II ambapo kuna kifungu cha *Special Expenditure* chenye makadirio ya matumizi ya shilingi bilioni 24.4 kwa ajili ya Bunge Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014?

(b) Je, ni ukurasa upi kati ya kurasa za 68 - 73 zenye makadirio ya Fungu 21 – Hazina kwenye Kitabu cha II ambapo kuna kifungu cha *Special Expenditure* chenye makadirio ya matumizi ya shilingi bilioni 20.0 kwa ajili ya Bunge Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015?

(c) Je, kati ya kauli yake kwamba hadi linaahirishwa Bunge Maalum limekwishatumia shilingi bilioni 24.4 na kauli ya Waziri wa Fedha kwamba Bunge hilo limekwishatumia shilingi bilioni 27, ipi ndiyo kauli ya kweli?

(d) Mwisho, kama itajulikana kwamba kauli yake kuhusu masuala yanayohusu Bajeti ya Bunge Maalum ni ya uongo; yuko tayari kulinda heshima yake iliyobaki kwa kujiuzulu au atasubiri mamlaka yake ya uteuzi imwajibishe kwa kumfukuza kazi kwa kulidanganya Bunge?

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania: Ibara ya 4(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, inaelekeza kwamba, Vyombo vyenye Mamlaka ya kutekeleza utoaji haki ni Mahakama ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Mahakama ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ibara ya 107A(1) inaweka wazi kwamba, mamlaka ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama. Maoni haya yanahusu Mahakama ya Tanganyika kwa sababu mbali na Mahakama ya Rufani ya Tanzania, masuala ya mahakama siyo mambo ya Muungano.

Katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Mahakama iliidhinishiwa shilingi bilioni 117.580 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 86.600 zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 30.980 kwa ajili ya mishahara. Aidha, Mahakama iliidhinishiwa shilingi bilioni 42.716 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kwa mujibu wa maelezo ya Makadirio ya Mapato, Matumizi ya Kawaida na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2014/2015, hadi Machi 2014, Mahakama ilikuwa imepokea shilingi bilioni 72.106, sawa na asilimia 61 (siyo 56 zilizotajwa katika maelezo ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kati ya hizo, shilingi bilioni 36.253 au asilimia 42 zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 26.652 au asilimia 86 zilikuwa kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia Machi, 2014, Mahakama ilikuwa imepokea shilingi bilioni 5.508 au asilimia 13 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Mahakama imeeleza katika Maelezo yaliyoletwa mbele ya Kamati kwamba, kutopelekewa fedha zilizoidhinishwa kumeisababishia Mahakama kuendesha shughuli zake kwa ugumu mkubwa. Aidha, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo umekuwa si wa kuridhisha na hivyo kuashiria kukwama kwa utekelezaji wa Miradi ya Mahakama ambayo mchakato wake umefikia ukingoni.

Mheshimiwa Spika, Ndimi Mbili za Mahakama: Lugha iliyotumika katika maelezo ya Mahakama kuelezea matatizo ya kutopatiwa fedha zinazoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ni ya kidiplomasia, ambayo pengine ndiyo lugha sahihi kwa mamlaka ya utoaji haki katika nchi. Hata hivyo, lugha hiyo haitoi picha kamili na halisi ya ukubwa wa matatizo hayo na inaweza kuwa inapotosha ukweli wa hali halisi. Kwa mfano, Maelezo ya Mahakama yanadai kwamba, Mahakama ya Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuondoa mlundikano wa mashauri *(backlog clearance)* na kuonesha ongezeko kubwa la wastani wa uondoaji wa mashauri katika ngazi zote za Mahakama. Hata hivyo, Taarifa ya Waziri inatoa picha kinyume kabisa. Hivyo basi, kwa mujibu wa Taarifa ya Waziri, upungufu huu wa bajeti umesababisha kukwama kwa shughuli za uendeshaji na usikilizaji wa mashauri na kusababisha kuongezeka kwa

msongamano wa mahabusu na wafungwa magerezani. Vivyo hivyo tunaambiwa kama tulivyoambiwa miaka miwili iliyopita kwamba, suala la usafiri kwa ajili ya shughuli za Mahakama limepewa uzito unaostahili. Ili kuthibitisha uzito huo unaostahili, Mahakama inatuambia kwamba, mwaka 2013/2014 Mahakama ilipanga kununua magari 218 na pikipiki 200 kwa ajili ya kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama.

Hata hivyo, kwa mujibu wa maelezo hayo hayo ya Mahakama, hadi sasa tayari Mahakama imenunua magari saba na imeingia mkataba wa ununuzi wa magari mengine 211 na pikipiki 200 ambayo yanatarajiwa kupatikana mwishoni mwa mwezi Juni, 2014. Kwa maneno mengine, magari saba au asilimia tatu ya matarajio ndiyo yaliyokwishanunuliwa na bado Mahakama inaona huu ni uzito unaostahili! Kwa upande mmoja, Mahakama inatuambia kwamba, umalizaji wa mashauri katika Mahakama ya Ardhi ulikuwa asilimia 99, lakini kwa upande mwingine Wizara inatuambia imeshindwa kufuatilia migogoro ya ardhi. Ulimi mmoja wa Wizara unaliambia Bunge lako Tukufu juu ya kuimarika kwa usimamizi na ukaguzi wa kazi za Mahakama kwa kuongeza vitendea kazi na rasilimali watu. Ulimi mwingine wa Wizara hiyo hiyo, unakiri mbele ya Bunge lako Tukufu juu ya kupungua kwa imani ya Wananchi kwa Serikali kutokana na kukosekana kwa huduma au huduma hafifu!

Mdomo mmoja wa Wizara unasema kwamba, ukaguzi wa Mahakama uliofanywa na Viongozi wa Mahakama ya Tanzania, umesaidia kusikiliza maoni na malalamiko mbalimbali ambayo yamesaidia kuboresha utendaji kazi katika Mahakama husika. Mdomo mwingine wa Wizara hiyo hiyo unakanusha kwa kusema kwamba, Vikao vya Kamati za Maadili vimekwama hivyo kupelekea kuongezeka kwa malalamiko dhidi ya vyombo vya kutoa haki. Aidha, wakati Mahakama inadai, imeendelea kuwapatia motisha na kuboresha masilahi ya wafanyakazi kwa kuwapatia posho za saa za ziada, mikopo, zawadi wakati wa sikukuu za kitaifa na za kidini, mafunzo na usafiri kazini. Wizara inakanusha mambo hayo mazuri kwa kudai kuna kupungua kwa ari ya watumishi kufanya kazi! *Contradictions* hizi kati ya kauli za Wizara na Taasisi yake Kuu zinahitaji maelezo ya kuridhisha kwa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizorembeshwa: Mahakama ya Tanzania imekuwa na matatizo mengi na sugu yanayotokana na ukosefu wa mgawo wa kibajeti. Matatizo haya yanafahamika na tumeyazungumza sana katika Bunge hili Tukufu. Hata hivyo, takwimu zinazotolewa na Wizara na hasa Mahakama yenyewe zinaleta tatizo lingine ambalo halihitajiki katika mazingira tuliyonayo. Hili ni tatizo la *sexed up statistics,* yaani takwimu zilizorembeshwa. Kuna msemo wa Kiingereza kuhusu takwimu unaosema *statistics are like a woman's bikini. What they reveal is interesting, but what they conceal is vital*! Yaani, takwimu

zinafanana na vazi la kuogelea la mwanamke. Zinachokionesha kinapendeza, lakini zinachokificha ndiyo muhimu zaidi! *(KIcheko)*

**SPIKA:** Kwa nini mwanamke siyo mwanaume; si kuogelea tu?

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Msemo huu unajidhihirisha katika takwimu zilizoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mahakama ya Tanzania juu ya utendaji kazi wake. Tunaambiwa, kwa mfano kwamba, mwaka 2013 mashauri 168,068 ya aina zote yalisajiliwa. Hata hivyo, kwa mujibu wa takwimu hizo, mashauri 182,237 ya aina zote yalisikilizwa na kutolewa hukumu kwa kipindi hicho na kubaki na mashauri 100,109 ya aina zote hadi ilipofika Disemba, 2013.

Hata kwa mtu asiyekuwa na shahada ya uzamivu ya takwimu, kama ilivyo kwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni anayewasilisha Maoni haya, hesabu hizi za Mahakama ya Tanzania zina walakini mkubwa. Haiwezekani kwa mashauri 168,000 kufunguliwa katika mwaka mmoja, halafu mashauri 182,000 yasikilizwe na kutolewa maamuzi na bado yabaki mashauri 100,000 katika mwaka huo huo!

Mheshimiwa Spika, tatizo la *sexed up statistics* linaelekea kuwa sugu katika Mahakama ya Tanzania. Miaka miwili iliyopita, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ililalamika kwamba, takwimu za mafanikio ya Mahakama ya Tanzania katika kusikiliza na kutoa maamuzi ya mashauri zinapotosha ukweli.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilisema wakati ule kwamba, kama hali halisi ingekuwa ndiyo hii inayoelezewa na Wizara, basi ni wazi kwamba, nchi yetu ya Tanzania isingekuwa na tatizo la mlundikano wa kesi katika Mahakama zetu zote. Kwa hiyo, Wizara isingekuwa na changamoto za bajeti finyu isiyokidhi majukumu ya Mahakama au ya fedha kutokutolewa kadiri ya mpango wa kazi wa mwaka na kwa wakati kama inavyodaiwa katika Maelezo ya Wizara hayo hayo yanayotangaza mafanikio makubwa katika usikilizaji wa mashauri na utoaji wa maamuzi ya mashauri hayo.

Tofauti na Taarifa ya Waziri ya sasa, Maelezo ya Wizara ya mwaka 2012/2013, yalitoa takwimu zilizoonesha mlundikano wa mashauri ya aina zote katika ngazi mbalimbali za Mahakama. Hivyo, ilikuwa siyo vigumu kugundua kwamba, takwimu za mafanikio makubwa zilikuwa hazilingani na takwimu za mlundikano wa mashauri.

Ndiyo maana tuliweza kusema kwamba, kwa sababu ya kutopatiwa fedha za kukidhi mahitaji yake halisi, Mahakama ya Tanzania imeshindwa kabisa kutatua tatizo la mlundikano mkubwa wa kesi katika ngazi zote. Kwa

sababu ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kuzijua, mwaka huu Maelezo ya Mahakama hayana takwimu zozote za mlundikano wa mashauri katika ngazi zote za Mahakama ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutokuwa na taarifa za mlundikano mashauri katika Taarifa ya Waziri na Maelezo ya Mahakama, bado zipo ishara kwamba, hali siyo nzuri. Hivyo, kwa mfano, Taarifa ya Waziri inaonesha kwamba, idadi ya mahabusu magerezani imepungua kutoka 18,203 mwezi Juni, 2012 na kufikia mahabusu 17,284 mwezi Machi, 2014. Hili ni punguzo la mahabusu 919 au asilimia tano tu katika kipindi cha karibu miaka miwili!

Takwimu hizi zinaonesha kwamba, badala ya kupungua, tatizo la mlundikano wa mahabusu linaweza kuwa limeongezeka kwa kiasi kikubwa. Katika hali hii, hitimisho letu kuhusu masuala haya katika bajeti ya mwaka 2012/2013 bado ni sahihi. Kwa ushahidi huu ni wazi kwamba, Mahakama ya Tanzania imeshindwa kutekeleza wajibu wake huu wa Kikatiba kwa sababu ya kunyimwa fedha na vitendea kazi vingine na Serikali hii hii inayodai kwamba dira yake ni haki kwa wote na kwa wakati!

Mheshimiwa Spika, miaka miwili iliyopita Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Mohamed Chande Othman, aliiambia semina juu ya Kudhibiti Ucheleweshaji wa Utatuzi wa Migogoro ya Kibiashara: Usuluhishi Kama Njia ya Kuharakisha Utoaji Haki, iliyofanyika Dar es Salaam tarehe 20 Julai, 2012, kwamba, *case delay is a sign of an inefficient judicial system. Excessive case delays may amount to a denial of justice*. Yaani, ucheleweshaji wa kesi ni ishara ya mfumo wa kimahakama usiokuwa na ufanisi. Ucheleweshaji mkubwa wa kesi unaweza kuwa udhulumaji wa haki. Kauli hiyo ya Jaji Mkuu imerudiwa na Waziri ambaye amesema katika Taarifa yake kwamba, msingi wa dhima ya Wizara yake ni kuwa haki iliyocheleweshwa ni sawa na haki iliyodhulumiwa.

Kama kauli hizi ni za kweli na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini ni za kweli, basi ni kweli vilevile kwamba, maelfu ya mahabusu na wafungwa ambao wamejaa katika magereza yetu wakisubiri maamuzi ya kesi zao na maelfu ya wadaawa ambao kesi zao zimelundikana katika mahakama zetu zote, watakuwa wamedhulumiwa haki zao na Serikali hii ya CCM ambayo sera za utoaji haki za hazitekelezeki.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake ya mwaka 2011/2012, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilielezea upungufu mkubwa wa watumishi wa ngazi mbalimbali wa Mahakama ya Tanzania ambao ni matokeo ya moja kwa moja ya kunyimwa fedha na Serikali. Tulirudia maelezo yetu katika maoni yetu ya mwaka 2012/2013. Miaka mitatu baadaye, tatizo hili halijapatiwa ufumbuzi wowote na kuna uwezekano linazidi kuwa kubwa zaidi.

Kwa mujibu wa takwimu za Wizara, kwa ujumla wake Wizara ina upungufu wa watumishi 2,521 au asilimia 27 ya mahitaji yake, ambayo ni watumishi 9,351. Kwa upande wa Mahakama, upungufu huo ni asilimia 25 au watumishi 1,891 kati ya 9,627 wanaohitajika. Ili kushughulikia tatizo hilo la uhaba wa watumishi, Serikali hii ya CCM imetoa kwa Mahakama kibali cha ajira mpya kwa ajili ya watumishi 148, ambayo ni sawa na asilimia nane tu ya wanaohitajika ili kuondoa upungufu huo!

Mheshimiwa Spika, katika Maoni yetu ya miaka miwili iliyopita tulieleza jinsi ambavyo Mahakama ya Tanzania imeendelea kufedheheka kwa kuwa mdeni mkubwa na sugu. Wakati tunaandika Maoni hayo, Mahakama ya Tanzania inadaiwa na Majaji na Watumishi wengine wa Mahakama, watoa huduma, wenye nyumba za kupangisha Majaji, Wajenzi na Wazabuni mbalimbali jumla ya shilingi bilioni 5.2. Fedha zote hizo zilikuwa ni madeni ya miaka ya nyuma hadi kufikia Mwaka wa Fedha 2010/2011. Hadi Machi, 2014, kwa mujibu wa Taarifa ya Waziri, madeni ya Wizara kwa watoa huduma na wakandarasi yamefikia zaidi ya shilingi bilioni tano. Kwa maana nyingine, madeni ya Wizara hayajapungua kwa kiasi chochote cha maana tangu Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, tulipendekeza, wakati wa mjadala wa Sheria ya Uendeshaji Mahakama, miaka mitatu iliyopita kwamba, badala ya Mahakama kutegemea ukomo wa bajeti unaowekwa na Hazina, sheria ielekeze kama ilivyo kwa Bunge na Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi Bungeni na nchi jirani ya Kenya kwamba, bajeti ya Mahakama ya kila mwaka isiwe pungufu ya asilimia tatu ya bajeti ya kila mwaka ya Serikali ili kuiwezesha Mahakama kuwa na uhakika wa fedha zake na kuiwezesha kupanga mipango yake kwa uhakika zaidi.

Pendekezo letu lilikataliwa na limeendelea kukataliwa na Serikali hii sikivu ya CCM. Matatizo ya bajeti ya Mahakama ambayo tumeyaeleza hapa na ambayo tumeyaeleza kwenye Maoni yetu ya kila mwaka, yanathibitisha wazi kwamba, utaratibu wa sasa wa kutegemea mgawo wa Hazina hauwezi kutatua matatizo ya fedha ya Mahakama ya Tanzania.

Kwa mara nyingine tena, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli Bungeni ni kwa nini inakataa kuihakikishia Mahakama fedha zake kwa kurekebisha Sheria ya Uendeshaji Mahakama ili kuweka *a minimum percentage* ya bajeti ya Serikali kwa ajili ya Mahakama kama ilivyofanya kwa Bunge na kwa Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, hali ya haki za binadamu katika nchi yetu inatisha. Mauaji na mashambulio dhidi ya Viongozi wa Kidini na Waumini wao na sehemu zao za ibada yaliyotokea kati ya mwaka 2012 na 2013 hayajatatuliwa hadi leo. Hakuna mtu yeyote ambaye ameadhibiwa kwa mauaji ya padri mmoja wa Kanisa Katoliki Zanzibar. Hakuna aliyeadhibiwa kwa shambulio la risasi na la tindikali dhidi ya Mapadri wengine wawili wa Kanisa hilo huko huko Zanzibar, wala kwa shambulio la tindikali dhidi ya Msaidizi wa Mufti wa Zanzibar.

Hakuna aliyetiwa hatiani wala kuadhibiwa kwa kuhusika na shambulio la bomu katika Kanisa Katoliki Olasiti Arusha lililoua watu watatu na kujeruhi wengine wengi. Serikali ya CCM haijatoa taarifa yoyote rasmi hadharani au Bungeni juu ya wahusika wa mauaji na mashambulio hayo na sababu zake. Hakuna mtu aliyepatikana na hatia ama kuadhibiwa kwa kuhusika na mauaji na mashambulio hayo hadi sasa.

Mauaji na mashambulio ya waandishi wa habari na wanaharakati wengine kama madaktari yaliyotokea kati ya 2012 na 2013 hayajatatuliwa. Pia Maafisa wa Jeshi la Polisi walioamuru mauaji ya mwandishi wa habari Daudi Mwangosi, hawajachukuliwa hatua yoyote. Badala yake, aliyekuwa Kamanda wa Polisi amepandishwa cheo na kuhamishiwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi. Huu ni ushahidi wa wazi kabisa kwamba, mauaji hayo yalipangwa na/au yalifanywa kwa maelekezo ya Serikali ya CCM.

Maafisa wa Idara ya Usalama wa Taifa na wa Jeshi la Polisi waliohusika kumteka nyara na kumtesa Mwenyekiti wa Chama cha Madaktari Tanzania, Dkt. Steven Ulimboka hawajakamatwa hadi leo licha ya majina yao kujulikana. Raia wa Kenya aliyebambikiziwa kesi ya kumteka Dkt. Ulimboka amekwishaachiliwa huru na mahakama. Serikali ya CCM haijatoa taarifa yoyote rasmi hadharani au Bungeni kuhusu jambo hili. Huu ni ushahidi wa kuhusika kwa Serikali ya CCM katika shambulio hilo. Hakuna aliyekamatwa wala kuadhibiwa kwa kumteka nyara na kumtesa aliyekuwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri, Absalom Kibanda. Serikali ya CCM haijatoa taarifa yoyote rasmi hadharani au Bungeni kuhusu shambulio hilo linalofanana na shambulio dhidi ya Dkt. Ulimboka. Serikali hii ya CCM ina wajibu kisheria na kisiasa wa kulinda maisha ya Watanzania na mali zao. Imeshindwa kutekeleza wajibu huo kwa Watanzania.

Serikali ya CCM imeitia demokrasia kitanzini na inatishia kuinyonga na kuiua. Mikutano halali ya Vyama vya Siasa vya Upinzani imeshambuliwa kwa mabomu na risasi za moto na Jeshi la Polisi. Watu wengi wameuawa katika mashambulizi hayo na wengine wengi wamejeruhiwa. Viongozi, Wanachama na hata wapita njia tu wamepigwa, kukamatwa na kufunguliwa mashtaka ya jinai kwa kushiriki mikutano halali ya Vyama vya Siasa vya Upinzani.

Jeshi la Polisi likishirikiana na Watumishi wa Idara ya Usalama wa Taifa na Viongozi na Makada wa CCM, wameshirikiana kuwabambikizia Viongozi na Wanachama wa CHADEMA kesi za uongo za ugaidi. Wengi wameteswa kwa ukatili mkubwa baada ya kukamatwa na kuhojiwa katika Vituo vya Polisi katika kesi hizi. Hadi sasa Serikali hii ya CCM haijasema chochote juu ya kufutwa kwa kesi za uongo za ugaidi walizofunguliwa Viongozi na Wanachama wa CHADEMA kama vile Wilfred Lwakatare na Henry Kilewo. Walioshiriki kutunga mashtaka hayo ya kidhalimu hawajachukuliwa hatua yoyote.

Serikali ya CCM imewageuka Watanzania walioipigia kura na kuwaua, kuwatesa na kuwatia vilema vya maisha, kuwabaka, kuwafukuza kwenye maeneo yao na kuwafanya wakimbizi wa ndani au *internally displaced persons (IDPs)*. Badala ya kulinda mali zao, Serikali ya CCM imekuwa mwizi wa mali za Wananchi. Serikali ya CCM imeendesha Operesheni Kimbunga kwa kisingizio cha kuondoa wahamiaji haramu nchini. Matokeo ya Operesheni hiyo ni kwamba, maelfu ya watu wasiokuwa na hatia wa Mikoa ya Kagera na Kigoma, inayopakana na Burundi na Rwanda, walikamatwa, kuteswa na kuporwa mifugo, fedha na mali zao nyingine na makazi yao kuharibiwa.

Utaratibu wa kisheria wa kuwakamata watuhumiwa, kuwapeleka mahakamani, kuwapata na hatia na kuwaadhibu kwa mujibu wa sheria umepuuzwa. Cha kushangaza, Operesheni Kimbunga haikuihusu Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mara, Mbeya, Mtwara, Rukwa na Ruvuma ambayo inapakana na nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Malawi, Msumbiji na Zambia ambayo nayo pengine ina wahamiaji haramu. Katika mazingira haya, ni sahihi kuamini kwamba, Operesheni Kimbunga ilikuwa ni lengo la kuwaadhibu watu wenye asili ya Rwanda kwa sababu ya mgogoro wa kidiplomasia kati ya Rais Jakaya Kikwete na Rais Paul Kagame wa Rwanda.

Hata kabla vumbi lililotimuliwa na Operesheni Kimbunga halijatulia, Serikali ya CCM ilianzisha vita nyingine kubwa dhidi ya Watanzania; hii ni Operesheni Tokomeza Ujangili. Licha ya jina lake, Operesheni hiyo imetokomeza maisha ya Watanzania wasiokuwa na hatia yoyote. Makumi ya watu wameuawa, mamia wamejeruhiwa, maelfu wamekamatwa na kuteswa, vijiji vizima vimechomwa moto na makazi ya Wananchi kuharibiwa, mifugo imeuawa ama kuporwa kwa mtutu wa bunduki, mashamba na mazao yameharibiwa na maelfu ya Wananchi wametiwa umaskini mkubwa na Serikali hii ya CCM.

Hatimaye, baada ya kelele kubwa ndani na nje ya Bunge, Operesheni Tokomeza ilisitishwa na Mawaziri wa Ulinzi, Mambo ya Ndani, Maliasili na Utalii na Mifugo wakaondoshwa madarakani kwa sababu ya Operesheni hiyo. Walioua,

kutesa na kulemaza Watanzania na kuwaibia au kuharibu mali zao hawajakamatwa wala kuchukuliwa hatua zozote za kisheria.

Operesheni Kimbunga na Tokomeza zilikuwa Operesheni za Kijeshi. Zilianzishwa, kuongozwa na kutekelezwa na Maafisa na Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na vikosi vingine vya ulinzi na usalama. Operesheni hizi za kijeshi zimefanyika wakati Tanzania haiko vitani na wala haiko katika hali ya vita. Rais Kikwete hakutangaza vita wala kuwepo kwa hali ya vita kwa mujibu wa Katiba ili kuweza kuamuru kutekelezwa kwa Operesheni hizi za kijeshi.
Hakukuwa na maasi au vurugu zozote zozote za kijamii. Kwa sababu hiyo, hakuna Mkuu wa Mkoa yeyote aliyeomba msaada wa kijeshi ili kuwezesha matumizi ya Majeshi ya Ulinzi katika kusaidia mamlaka za kiraia kama inavyotakiwa na Sheria ya Ulinzi wa Taifa, 1970 na Kanuni zake. Kwa kila namna inavyoonekana, Operesheni Kimbunga na Operesheni Tokomeza zilikuwa ni matumizi haramu ya nguvu za kijeshi dhidi ya raia. Kama hii haitoshi, sasa Serikali hii ya CCM inazungumza kuianzisha tena Operesheni hii dhidi ya Wananchi wa Tanzania!

Mheshimiwa Spika, Tume ya Uchunguzi iliyoahidiwa Bungeni na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuchunguza masuala yanayohusu ukiukwaji huu wa haki za binadamu, imeundwa na Rais kupitia Tangazo la Serikali Na. 131 la tarehe 2 Mei, 2014. Tume hiyo inaongozwa na Jaji Kiongozi Mstaafu Hamisi Amir Msumi na Makamishna wenzake, Majaji wastaafu Stephen Ihema na Vincent Kitubio Damian Lyimo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu na kutambua utumishi uliotukuka wa Jaji Kiongozi Msumi. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina imani kabisa na uteuzi wa Makamishna Ihema na Lyimo. Itakumbukwa kwamba, tarehe 13 Julai, 2012, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ililalamikia uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu wakiwa wamekaribia muda wao wa kustaafu kwingineko katika utumishi wa umma (na) wanapewa zawadi ya Ujaji kuwawezesha kupata mafao ya Majaji wastaafu ambayo yameboreshwa sana katika miaka ya karibuni.

Ushahidi tuliouwasilisha mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge baada ya Msemaji wa Kambi kushtakiwa kwenye Kamati hiyo kwa kile kilichoitwa kuwadhalilisha Majaji, uliwahusisha Majaji Wastaafu Ihema na Lyimo katika kundi la Majaji ambao uteuzi wao tuliupigia kelele. Sehemu ya ushahidi huo inaonesha kwamba, tarehe 16 Juni, 2003, aliyekuwa Mwenyekiti CCM wa Mkoa wa Singida, Mzee Joram Allute, alimwandikia Rais Benjamin Mkapa, maombi ya kumwondoa Jaji Ihema kama Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania kwa uzembe na kukosa maadili. Mzee Allute alikuwa na kesi kwa Jaji Ihema ambapo Jaji huyo alikalia uamuzi kwa zaidi ya miaka minne hadi

aliponyang'anywa faili la kesi hiyo na kukabidhiwa Jaji mwingine aliyeandika uamuzi huo ndani ya wiki tatu!

Mwezi mmoja kabla ya barua ya Mzee Allute kwa Rais Mkapa, Mawakili wake walikuwa wamemwandikia Jaji Mkuu Barnabas Samatta kulalamikia ucheleweshaji wa uamuzi wa kesi hiyo. Mawakili hao walidai hadhi na heshima ya Mahakama inaporomoka vibaya kama inachukua zaidi ya miaka mitatu kwa Jaji kutafakari na kutoa uamuzi kwa jambo jepesi kama maombi ya pingamizi.

Mheshimiwa Spika, siyo tu kwamba, Jaji Mstaafu Ihema ana rekodi mbaya ya kijaji, bali pia ana rekodi ya kutumiwa na Serikali hii ya CCM kuisafisha Serikali kwa matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na Watendaji wa Serikali. Mwaka 2012, mara baada ya Jeshi la Polisi Mkoani Iringa kumuua Daudi Mwangosi, aliyekuwa Mwandishi wa Habari wa Kituo cha Televisheni cha Channel Ten, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, alimteua Jaji Ihema kuongoza Kamati iliyoundwa na Waziri Nchimbi kuchunguza mauaji ya Marehemu Mwangosi. Taarifa ya Uchunguzi wa Kifo cha Mwandishi wa Habari wa Channel Ten Bw. Daudi Mwangosi, iliyoandaliwa na Kamati ya Jaji Ihema ni mfano wa namna ya kuisafisha Serikali kutoka kwenye lawama ya mauaji ya raia wake.

Taarifa hiyo ilitofautiana kimsingi na Taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya Uchunguzi wa Tukio Lililopelekea Kifo cha Daudi Mwangosi Kilichotokea Septemba 2, 2012 Kijijini Nyololo, iliyoandaliwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na *Ripoti ya* Timu Maalum ya Uchunguzi Iliyoteuliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) Kuchunguza Mazingira Yaliyopelekea Kuuawa kwa Mwandishi wa Habari Daudi Mwangosi Septemba 2, 2012 Katika Kijiji cha Nyololo, Wilaya ya Mufindi, Mkoani Iringa, iliyotolewa na Baraza la Habari Tanzania *(MCT)* na Jukwaa la Wahariri Tanzania *(TEF)*.

Kwa upande wake, Jaji Lyimo aliteuliwa tarehe 28 Machi, 2007, mwaka mmoja kabla ya muda wake wa kustaafu kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo, ilipofika tarehe 26 Oktoba, 2007, Katibu Mkuu Kiongozi wa wakati huo Phillemon Luhanjo, alimtaarifu Jaji Mkuu kwamba, Rais Kikwete ameamua kusogeza mbele muda wa kustaafu wa Mheshimiwa Jaji Vincent Kitubio Damian Lyimo kwa miaka mitatu kuanzia tarehe 28 Machi, 2008, siku ambayo angestaafu kwa lazima.

Uteuzi wa Majaji hawa na wengineo wenye sifa kama hizo, ulilalamikiwa mno na Majaji wengine kiasi kwamba, Kikundi Kazi kwa Ajili ya Kuchambua na Kushauri Kuhusu Ajira ya Majaji Baada ya Kustaafu chini ya Ofisi ya Rais,

kilihitimisha katika Taarifa yake tarehe 7 Machi, 2008, inaonekana wazi kuwa suala la ajira za mikataba kwa Majaji ambao wamekuwa wakifanya kazi za Jaji baada ya kufikia umri wa kustaafu ni kinyume cha Katiba.

Sasa Majaji hawa ndiyo wamepewa jukumu la kuchunguza matukio ya ukiukwaji haki za binadamu ambayo hayana mfano katika historia ya Tanzania tangu Uhuru. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina imani yoyote na uteuzi wa Majaji Ihema na Lyimo na inapendekeza uteuzi wao ufutwe na Majaji wenye sifa bora zaidi wateuliwe kwa ajili ya kazi hii muhimu. Vinginevyo, matokeo ya Tume ya Msumi hayatakubaliwa na Umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya uendeshaji wa mashtaka ya jinai yamekasimiwa kwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mujibu wa Ibara ya 59B(2) ya Katiba. Mamlaka haya yamefafanuliwa na kutiliwa nguvu na kifungu cha 16(1) cha Sheria ya Utumishi wa Mashtaka ya Taifa, Na. 27 ya 2008 (*National Prosecutions Service Act, 2008*). Kwa mujibu wa kifungu hicho, Mkurugenzi wa Mashtaka ana mamlaka siyo tu ya kudhibiti mashtaka yote ya jinai, bali pia kuratibu shughuli za upelelezi wa makosa ya jinai. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 17(1) na (3), Mkurugenzi ana uwezo wa kutoa maelekezo ya maandishi kwa Ofisa yeyote wa Umma ili apatiwe taarifa yoyote inayohusu upelelezi au uendeshaji wa mashtaka ya jinai na Ofisa huyo anatakiwa kutii maelekezo hayo.

Ili kumwezesha Mkurugenzi wa Mashtaka kutekeleza wajibu wake wa kikatiba kwa uhuru kamili na bila woga au upendeleo, Mkurugenzi wa Mashtaka amewekewa kinga ya ajira yake. Hivyo, kwa mfano, Ibara ya 59B(4) ya Katiba inaelekeza kwamba, katika kutekeleza mamlaka yake, "Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa huru, hataingiliwa na mtu yeyote au mamlaka yoyote na atazingatia nia ya kutenda haki, kuzuia matumizi mabaya ya taratibu za utoaji haki na masilahi ya umma. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 19(1) na (2) cha Sheria ya Utumishi wa Mashtaka ya Taifa, sifa, masharti na mafao ya ajira ya Mkurugenzi wa Mashtaka yatakuwa sawa na yale ya ajira ya Jaji wa Mahakama Kuu. Vilevile, kufuatana na kifungu cha 19(3), Mkurugenzi wa Mashtaka hawezi kuondolewa kwenye madaraka yake isipokuwa kwa kushindwa kutimiza wajibu wake kwa sababu ya ugonjwa au kwa kukiuka Kanuni za Maadili ya Kitaaluma chini ya Sheria ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 ya Sheria za Tanzania. Hii ndiyo kusema kwamba, kwa mujibu wa Sheria Na. 27 ya 2008, utaratibu wa kumwondoa Mkurugenzi wa Mashtaka kwenye ajira yake hauna tofauti na utaratibu wa kumwondoa Jaji wa Mahakama Kuu kwenye ajira yake.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, utaratibu huu wa kikatiba na kisheria umempa Mkurugenzi wa Mashtaka nyenzo

za kutosha kisheria za kupambana na uhalifu mkubwa hapa nchini na vilevile kuzuia matumizi mabaya ya mfumo wa uendeshaji na utoaji haki na hasa hasa ya mfumo wa mashtaka ya jinai. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashangazwa na kusikitishwa na kushindwa kwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kufungua na/au kuendesha mashtaka yanayohusu matukio makubwa ya uhalifu ambayo yametikisa Taifa letu katika mwaka huu wa fedha na kabla ya hapo.

Tarehe 16 Juni, 2013, mkutano wa hadhara wa kampeni za uchaguzi wa madiwani uliokuwa unafanywa na Viongozi Wakuu wa CHADEMA katika eneo la Soweto Mjini Arusha, ulishambuliwa kwa mabomu na risasi za moto. Watu watatu waliuawa pale pale na mwingine alifia hospitalini baadaye. Wengine wengi walijeruhiwa vibaya. Hadi sasa Serikali hii ya CCM haijatoa taarifa yoyote rasmi, ndani ya Bunge hili au nje, juu ya waliohusika na mashambulizi haya ya kigaidi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kufahamu hatua zozote, kama zipo, zilizochukuliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka kuchunguza tukio hilo la kigaidi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua matokeo yoyote, kama yapo, ya uchunguzi wa tukio hilo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo linahitaji majibu linahusu utekelezaji wa maelekezo ya Mahakama Kuu ya Tanzania juu ya marekebisho ya sheria ambazo Mahakama Kuu imetamka kwamba zinakiuka Katiba. Kama tulivyosema katika Maoni yetu miaka miwili iliyopita, mfumo wa dhamana chini ya kifungu cha 148(5)(a) cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai ambao unakataza dhamana kwa idadi kubwa ya watuhumiwa wa makosa yaliyotajwa katika aya (e) ndiyo sababu kubwa ya magereza kufurika mahabusu na mlundikano wa kesi za jinai kwa ujumla. Kwa sababu hiyo, Mahakama Kuu ilitamka, katika kesi ya *Jackson s/o ole Nemeteni @ ole Saibul @ Mdosi @ Mjomba na wenzake 19 dhidi ya Mwanasheria Mkuu, Shauri la Madai Na. 117 la 2004*, kwamba bila kuwepo utaratibu uliowekwa na sheria kama inavyoelekezwa na Ibara ya 15(2)(a) ya Katiba, utekelezaji wa masharti ya kifungu cha 148(5)(a) umetumiwa vibaya. Kwa sababu hiyo, Mahakama Kuu ilitamka kwamba, kifungu hicho kinachokataza dhamana kwa watuhumiwa wa makosa ya wizi wa kutumia silaha ni kinyume cha Ibara ya 15(2)(a) ya Katiba.

Kuhusiana na kifungu cha 148(5)(e) cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai kinachoweka masharti ya dhamana yasiyotekelezeka kwa watuhumiwa wa makosa ya uhujumu uchumi, Mahakama Kuu katika kesi ya Prof. Dkt. Costa Ricky Mahalu & Mwenzake dhidi ya Mwanasheria Mkuu, Shauri la Maombi Na. 35 la 2007, ilitamka kwamba, kifungu hicho ni cha kibaguzi kwa watuhumiwa maskini na kinakiuka matakwa ya Ibara ya 13(2) ya Katiba inayokataza ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira.

Kwa kutumia mamlaka yake chini ya ibara ya 30(5) ya Katiba, badala ya kukifuta kifungu hicho, Mahakama Kuu katika kesi zote mbili iliielekeza Serikali ifanye marekebisho katika kifungu cha 148(5)(a) na (e) vya Sheria ya Mwenendo wa Jinai ili kuweka utaratibu bora zaidi wa kushughulikia dhamana za watuhumiwa wa makosa ya wizi wa kutumia silaha na wa uhujumu uchumi. Katika Kesi ya Jackson s/o ole Nemeteni, Mahakama Kuu ilitoa muda wa miezi kumi na nane kuanzia tarehe 13 Julai, 2007. Katika Kesi ya Prof. Dkt. Costa Ricky Mahalu, Mahakama Kuu ilitoa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 4 Oktoba, 2010. Hii ina maana kwamba, Serikali ilitakiwa iwe imetekeleza maelekezo ya Mahakama Kuu juu ya kifungu cha 148(5)(a) kufikia tarehe 12 Desemba, 2008. Aidha, Serikali ilitakiwa kutekeleza maelekezo ya Mahakama Kuu kuhusu kifungu cha 148(5)(e) kufikia tarehe 3 Oktoba, 2011.

Huu ni mwaka wa tano na nusu tangu kwisha kwa muda uliowekwa katika Kesi ya Jackson s/o ole Nemeteni lakini Serikali haijafanya marekebisho tajwa ya Sheria ya Mwenendo wa Jinai. Aidha, huu ni karibu mwaka wa tatu tangu muda uliowekwa katika Kesi ya Prof. Dkt. Costa Ricky Mahalu lakini Serikali haijatekeleza maelekezo hayo.

Kuhusiana na utekelezaji wa maelekezo ya Mahakama Kuu katika Kesi ya Prof. Dkt. Costa Ricky Mahalu, Mwanasheria Mkuu ametoa maelezo kwamba, Serikali haikuridhika na uamuzi huo na hivyo iliamua kukata rufaa katika Mahakama ya Rufani kwa kutoa notisi ili kupinga uamuzi huo. Mwanasheria Mkuu ameeleza kwamba, marekebisho ya kifungu hicho hayajafanywa kwa kuwa rufaa dhidi ya uamuzi huo haijasikilizwa.

Mheshimiwa Spika, Mwanasheria Mkuu hajasema ni lini Serikali ilitoa notisi ya rufaa dhidi ya uamuzi wa Mahakama Kuu. Aidha, Mwanasheria Mkuu hajasema kama tayari Serikali imeshakata rufaa hiyo, ijapokuwa maelezo yake yanaashiria kwamba, rufaa hiyo bado haijawasilishwa kwenye Mahakama ya Rufani. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, Serikali hii ya CCM inaweza kuwa inatumia vibaya masharti ya kifungu cha 14(3) cha Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Binadamu, Sura ya 3 ya Sheria za Tanzania, yaani The Basic Rights and Duties Enforcement Act, Chapter 3 of the Laws of Tanzania. Kifungu hicho kinazuia utekelezaji wa uamuzi wowote wa Mahakama Kuu pale ambapo Serikali imewasilisha notisi ya rufaa yenye kuonesha nia ya kupinga uamuzi husika.

Kwa kutumia kifungu hicho, Serikali inaweza kuzuia uamuzi huo kwa kutoa notisi ya rufaa tu bila kulazimika kukata rufaa yenyewe na utaratibu mzima wa kurekebisha sheria mbovu na za kikandamizaji kwa kutumia Mahakama ukasitishwa. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali

hii ya CCM itoe nakala ya notisi ya rufaa iliyoiwasilisha katika Mahakama ya Rufani katika Kesi ya Prof. Dkt. Costa Ricky Mahalu. Hii ni muhimu ili kuhakikisha kwamba, taarifa ya Mwanasheria Mkuu ni ya kweli. Aidha, kama itathibitika kuwapo kwa notisi hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM kutoa kauli rasmi mbele ya Bunge hili Tukufu ni lini inatazamia kuwasilisha rufaa ambayo tayari imekwishaitolea notisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Kesi ya Jackson s/o ole Nemeteni, Serikali haijatoa maelezo yoyote kwa nini haijatekeleza maelekezo ya kikatiba ya Mahakama Kuu kwa karibu miaka sita. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli rasmi kama na lini, inatarajia kutekeleza maelekezo hayo ya Mahakama Kuu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji kama hii siyo dharau ya Serikali hii ya CCM kwa Mahakama ya Tanzania ni kitu gani?

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha maoni haya, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Viongozi Wakuu wa Vyama vyetu vitatu vinavyounda Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa kufanya maamuzi ya kuendeleza ushirikiano ulioanzia ndani ya Bunge Maalum, kwenye Bunge lako Tukufu. Kwa sababu ya maamuzi hayo, imewezekana kwa Naibu Waziri Kivuli wa Sheria na Katiba, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, kushirikiana nami katika kuandaa na kuwasilisha Maoni haya. Naomba nitumie fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Rashid Abdallah, kwa kuteuliwa kwenye nafasi hiyo na kumshukuru kwa ushirikiano wake katika kuandaa Maoni haya.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya marefu, naomba kukushukuru na wewe binafsi na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitawaita wachangiaji wafuatao; yupo Mheshimiwa William Ngeleja, halafu Fakharia Shomar na Mheshimiwa Raya, tufike hapa kwanza.

Mheshimiwa Ngeleja!

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia fursa hii na kwa heshima hii, ninaomba kusema yafuatayo kuhusu bajeti iliyoko mbele yetu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, kama ambavyo imejitokeza kwenye taarifa na ni taarifa za pande zote mbili, upande wa Serikali lakini pia kwa TAARIFA za Kamati; wote tunakubaliana kwamba, Wizara hii ya Katiba na Sheria ni mhimili muhimu sana katika uendeshaji wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tumeelezwa katika taarifa zetu na uzoefu unaonesha kwamba, bila kuwepo kwa utawala bora ambapo utawala wa Sheria ni

sehemu ya utawala bora, nchi haiwezi kutulia na haiwezi kuwa na amani. Sasa tunachokisema hapa ni kusisitiza tu kuhusu ugawaji wa rasilimali fedha, kuwezesha Wizara hii ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake ziweze kupata mafungu yanayowezesha kutekeleza wajibu wake; kwa sababu kinyume chake itakuwa ni tatizo kwa Taifa letu.

Sasa tunaona kuna mambo makubwa yanayoendelea ikiwemo hii migogoro ya ardhi ambayo inaendelea katika maeneo mbalimbali. Kwa kiasi kikubwa, wasimamizi wa shughuli hizi ni Wizara ya Katiba na Sheria. Sasa ombi langu, tunatambua ufinyu bajeti, *ceiling* tunazo, lakini ni muhimu sana kuzingatia utoaji rasilimali fedha kwa Wizara hii. Tunafahamu kwamba Wizara hii haimo katika ule Mpango wa *BRN,* lakini bajeti yao siyo kubwa kihivyo na mtu angesema unadhani fedha zingetoka wapi? Kamati ya Bajeti itusaidie sana kutoa mafungu yanayohitajika kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

La pili, ninalotaka kulisema sasa kwa sababu lilikuwa la jumla ni kuhusu Taasisi zilizokuwa chini ya Wizara hii. Moja ni ile Kurugenzi ya Mashitaka. Tatizo ni kubwa, mwaka jana tumejadili, tumekubaliana Taasisi hii iwezeshwe ipate watumishi wengine zaidi ya 489. Ninafahamu kwamba, kuna changamoto mbalimbali katika upande wa Serikali; lakini kama tunavyosema, tusipowawezesha hawa haki za watu hazitopatikana na matokeo yake nchi hii haitatawalika. Kwa hiyo, ninachosisitiza tuangalie sana vibali tutoe lakini pia uimarishaji wa bajeti. Katika taarifa yetu tumesema na mimi kwa sababu naunga mkono hoja hii iliyokuwa mbele yetu, tumesikia habari nzuri ambazo zimesemwa kuhusu utendaji wa baadhi ya Taasisi zilizoko chini ya Wizara hii. *(Makofi)*

Nataka nisemee moja kwa sababu ya ufinyu wa muda, Taarifa yetu imejieleza kwa mambo mengi mazuri na sisi ambao tumebahatika kukaa na hizi Taasisi na Wizara kwa ujumla, tunafahamu kazi kubwa wanayofanya, lakini siyo rahisi kwa dakika saba kusema yote.

Nataka kuzungumzia habari ya Mahakama. Mahakama wanafanya kazi kubwa sana na tunampongeza kwa nafasi hii Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Tanzania pamoja na Taasisi yake na Mtendaji Mkuu, Bwana Katanga. Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru sana kwa usimamizi wa Taasisi zako wewe na Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inafanya kazi kubwa, lakini wakati mwingine katika mazingira magumu. Sasa nataka kusemea uwezeshaji wa Mhimili huu wa Mahakama. Inaonesha Mhimili huu pamoja na kwamba, tunatambua Mahakama ni Mhimili unaojitegemea na unahitaji kutendewa kama

inavyotendewa Mihimili mingine, lakini bado kuna changamoto katika rasilimali fedha.

Nilichokuwa naomba, ombi letu ambalo tumeweka kwenye Kamati yetu, kwa rasilimali zinazotolewa hasa rasilimali fedha, Mhimili huu uwezeshwe. Fedha zake kwa vyovyote itakayotengwa, isiguswe na isitendewe kama ambavyo imejitokeza wakati mwingine, fedha inayotengwa upande wa Mahakama inatumika kama *OC*. Sasa hii si haki, wengine wanaweza wakadhani kwa sababu sasa tuna mchakato wa Katiba pengine haya mambo tutayaweka sawa wakati wa mjadala wa Katiba mpya, lakini tunasema, kwa sababu maisha hayasubiri ukamilishwaji wa Katiba mpya, sisi kwa bajeti hii tuanze kuhakikisha kwamba fedha tunazozitenga tunaziwekea wigo kama tulivyopendekeza kwenye Kamati zisiguswe.

Katika mtiririko wa *allocation,* fedha ziwafikie hawa walengwa na ziwafikie kwa wakati unaohitajika. Tuna tatizo kubwa, kwa sababu ya kutokuwa na utaratibu mzuri, mwaka jana tumepitisha makadirio kwa mpango wa maendeleo, kwa huu Mhimili wa Mahakama shilingi bilioni 42, lakini zilizowafikia mpaka sasa hivi ni bilioni tano tu.

Sasa migogoro yote hii hawa ndiyo wasimamizi; tunafanyaje katika mazingira haya? Naomba sana huu ushauri wa kuwatengea fedha na kuziwekea wigo zisiguswe, tuutekeleze kuanzia sasa ili waendelee kutekeleza majukumu yao.

Lingine ambalo nataka kulisema, kwenye utaratibu wao waliojiwekea wa *BRN,* ku-*fast track* kesi, mashauri mbalimbali yaliyoko Mahakamani. Kwa kweli Mahakama wanahitaji kuungwa mkono kwa kila namna kwa sababu wamefanya kazi kubwa na wakati mwingine katika mazingira magumu kama nilivyosema.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kwa sababu nimesikia kengele ya kwanza inatuarifu; nilikuwa napitia hapa na kwa sababu wenzetu wametumia, siwezi kusema ujanja kwa sababu neno hili linaudhi; Taarifa hii imetufikia wakati mjadala unaanza. Taarifa hii ya wenzetu wa Kambi ya Upinzani ina kurasa 24, lakini ukiziangalia zaidi ya asilimia 70 ya hii Taarifa ni malalamiko.

Sasa wote tunafahamu kwamba, jambo hili, kuwepo kwa taarifa hizo za upande wa pili maana yake ni kwamba, ni kuwa na mawazo mbadala. Watanzania wanasikia wataendelea kuyachambua, tunafahamu kwamba Serikali haiwezi kuyafanya yote kwa pamoja na tunafahamu upungufu uliopo. Sisi kwa pamoja tunaendelea kuishauri Serikali itemize wajibu wake, lakini itimize kwa kadiri ambavyo mambo yanawezekana.

Taarifa hii imejaa malalamiko, haitoi mawazo mbadala nini tufanye sasa, zaidi ya yale ambayo wanalalamikia. Ninaomba niseme kwamba, katika siasa ni kama vita na kwa sababu ni kama vita, wakati wote wanapopata nafasi wapiganaji wataitumia. Sisi tunafahamu dunia nzima, upande wowote ambao haupo Serikalini ni rahisi sana kui- *challenge* Serikali.

Leo ukienda Marekani pamoja na kwamba, tunaambiwa uchumi umeanza kukua na taarifa zipo hivyo, lakini ambao hawapo Serikalini, *Republicans* sasa hivi wanapiga kelele. Hawakubali pamoja na kwamba Wananchi wanaelewa, lakini wakipata fursa kwa kutumia majukwaa kama haya wanalalamika.

Naomba wenzetu muendelee kutafakari, tunafahamu Baraza la Mawaziri la Upinzani hivi karibuni limefanyiwa marekebisho, endeleeni kujipanga vizuri, muisaidie Serikali nini kifanyike badala ya kulalamika tu hapa bila kutoa mawazo mbadala kama ambavyo inakusudiwa kutoka kwenye kanuni zetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba wenzangu pia tuendelee kuiunga mkono hoja ya Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Halima Mdee!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza, Mheshimiwa Ngeleja ukisaidiwa fikra asilimia 30 inabidi ushukuru na hizo 70 lazima tuziseme kwa sababu nchi inaelekea kuwashinda, matatizo yamekuwa ni mengi kuliko faraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka Waziri wa Sheria anijibu na ninashukuru Naibu wake alikuwepo kipindi kirefu, ni muda mrefu sana Wizara hii imekuwa ikilidanganya hili Bunge kuhusiana na ujenzi wa Mahakama, hususan Mahakama ya Jimbo la Kawe. Ninaomba nipate majibu kuhusiana na hiyo Mahakama. Pili, hii Wizara ndiyo inasimamia mchakato wa Katiba kuanzia hatua za awali. Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011 ililetwa na Wizara hii kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Inasikitisha kwamba ni Wizara hii hii ambayo imekuwa inaongoza katika kusigina utekelezaji wa Sheria mabadiliko hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge Maalum la Katiba tumeshuhudia ni kwa namna gani Wizara hii kupitia Mawaziri wake, wamekuwa makuwadi wa kuivunja ile Sheria. Sheria iko wazi, inaeleza michakato mine; inaeleza mchakato wa kwanza wa maoni, inaeleza mchakato wa pili wa Mabaraza, inaeleza mchakato wa tatu wa Bunge Maalum la Katiba na inaeleza mchakato wa nne wa Kura ya Maoni.

Mheshimiwa Spika, masikitiko yangu, chini ya Uongozi wa Viongozi hawa wawili hapa mbele, Bunge Maalum la Katiba likajigeuza sehemu ya kutoa maoni upya. Spika, ulikuwepo, Sheria hii inavunjwa, badala ya Bunge litekeleze wajibu wake wa kujadili na kuboresha na kupitisha, likaanza kufanya utaratibu mpya wa maoni, kinyume na hii sheria. Bunge akiwepo Waziri Mkuu, akiwepo Mwanasheria Mkuu, wanazungumzia Mabaraza kwamba, Sheria hii imeipa mamlaka Mabaraza kubadilisha kabisa maoni ambayo yametolewa na Wananchi; kitu ambacho ni kinyume na sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume imetumia zaidi ya shilingi bilioni 70 …

**SPIKA:** Mimi siyo Mwenyekiti ni Spika.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, napata mzuka.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu sisi inaisimamia Tume ya Warioba. Tume ya Warioba imetumia zaidi ya shilingi bilioni 70. Bunge Maalum la Katiba tunaambiwa limetumia shilingi bilioni 24 na huku kuna shilingi bilioni 27. Hapa kuna utata ambao tunataka mtujibu! Fedha nyingi zinatumika, tunaenda kufanya kazi ya kisanii kwenye Bunge Maalum la Katiba wakati Sheria imeeleza wazi.

Mheshimiwa Spika, nataka leo Mwanasheria Mkuu wa Serikali atueleze hii Sheria, nafasi ya kifungu cha tisa ilikuwa ni nini? Nafasi ya kifungu cha 18 ilikuwa ni nini? Nafasi ya kifungu cha 25 ilikuwa ni nini? Na nafasi ya kifungu cha 28(b) ni nini? Ninasema hivyo kwa nini?

Mheshimiwa Spika, haiwezekani mfanye usanii wa kuturudisha kwenye Katiba iliyopo sasa, wakati Katiba ya mwaka 1977 inaturuhusu kama tunataka kufanya mabadiliko, tufanye chini ya kifungu cha 98 cha Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasikia Mheshimiwa Rais ameongeza siku 60. Hizi siku 60 kama watu wanaenda kuvunjavunja misingi ya Rasimu ya Pili ya Katiba, misingi ambayo ni chimbuko la maoni ya Wananchi, huo ni usanii na uharibifu wa hela. Mimi sitarajii kabisa kwamba, kuna watu na akili zao timamu, wataenda kwenye lile Bunge wakati Sheria hii imevunjwa, wakati wanajua wanaenda kuvunja ile misingi. Kama dhamira ingekuwa Bunge Maalum ndiyo

tutunge, tungeweza tusianzishe mchakato wa Wananchi, tusianzishe mchakato wa Mabaraza, tukaamua sisi wenyewe ndiyo tufanye kila kitu kwa kadiri ambavyo tungetaka. *As long as* kuna hatua nne zilizotambuliwa kisheria, hatua zote nne ni lazima ziheshimiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuhoji uhalali wa hatua ya kwanza, ukahoji uhalali wa hatua ya pili, halafu eti ninyi Makada wa CCM asilimia 95 mmejikusanya huku, mjione ndiyo mna mamlaka ya kubadilisha yale yote yaliyomo kwenye hatua mbili. Hili halikubaliki na tutapambana nje na ndani mpaka kieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la *DPP; DPP* amekuwa akilalamikiwa sana; mbaya zaidi analalamikiwa pia na Afisa Mwandamizi wa Serikali, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, anasema linapokuja suala la kushughulikia rushwa kubwa kubwa, *DPP* amekuwa ni kikwazo. Juzi tuliambiwa hapa suala la *Escrow Account* milioni 200 mnapeleka TAKUKURU, mnapeleka CAG. TAKUKURU wamenukuliwa na Sheria ya 2007 iko wazi, inatamka bayana kwamba, hawezi kutaja wala rushwa wakubwa, mafisadi, haruhusiwi kuwataja kwa majina. Pili, akitaka kufungua shauri la rushwa kubwa kubwa mpaka akaombe kibali kwa *DPP*. Analalamika kwamba, *DPP* amekuwa akibania vibali kwa masilahi yake binafsi. Zaidi wanasema siku sitini zikipita ndiyo imetoka hiyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatarajia kwamba, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Waziri wakiwa wanatujibu, watuambie ni kwa kiwango gani Sheria ya TAKUKURU mwaka 2007, italetwa kwa ajili ya kuifanyia mabadiliko. Vilevile ni kwa kiwango gani hizi rushwa kubwa ambazo majalada yamekuwa yanapelekwa kule, *DPP* kwa masilahi yake anayaficha zitapelekwa mahakamani?

Tatu, limeulizwa suala la UDA leo, aliyekuwa mshtakiwa mkuu, aliyeisababishia UDA hasara kubwa …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Tumemaliza tayari, sasa ninamwita Mheshimiwa Ali Khamis Seif

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuwa hai na uzima huu kusimama katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pili, nina ushauri kuhusiana na suala zima la upatikanaji wa Katiba Mpya. Ninavyoona mimi ni kuwa, utakapoondoka na Rasimu

ambayo imeletwa na Tume ya Jaji Warioba, kwa maana ya kuwa tuwe na Muungano wa Serikali mbili, Bunge la Katiba litakuwa halina maana, hili ambalo tunaliita Bunge Maalum. Kwa sababu gani? Bunge lile lipo kwa sababu ya mambo ya Mungano na unapokuwa na Serikali mbili ina maana mambo ya Tanzania Bara, kwa lugha nyingine Tanganyika, yatakuwemo katika Katiba ile. Kwa hiyo, Bunge halali la kubadilisha mambo yale ni Bunge hili. Bunge Maalum la Katiba litakuwa halistahili. Huo ni ushauri.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara ambayo inategemewa kuwapatia Wananchi haki sawa tena kwa wakati. Taasisi ambazo zinahusika zaidi ni Mahakama, *Division* ya Mashtaka na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Dola ina Mihimili mitatu; kuna Serikali ambayo ndiyo Mtendaji, kuna Mahakama na kuna Bunge. Inavyoonekana, Mhimili wa Mahakama unapuuzwa. Inachukuliwa kama ni Wizara au kama ni Idara wakati ule ni Mhimili muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, ushahidi wa kwanza, tuangalie majengo ya Mihimili mitatu. Bunge tumo humu na majengo mengine yako nje ya Ukumbi huu. Utajua kuwa hapa pana hadhi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na inawakilisha miaka hamsini ya Muungano. Ukienda Ikulu hali kadhalika, lakini nenda alipo Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Tanzania, jengo alilopo, Ofisi aliyonayo, inasikitisha kweli kweli. Kwa hiyo, hii inaonesha kuwa Mahakama bado haijapewa nafasi inayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo suala la majengo tu, hata uwasilishaji wa fedha za kibajeti baina ya Mihimili hii mitatu, ukiangalia katika suala zima la fedha za maendeleo, Ofisi ya Rais, Ikulu, ambayo tunategemea ndiyo Makao Makuu ya Serikali hapa, katika bajeti ya mwaka 2013/2014, fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya maendeleo ni shilingi bilioni 59.58, zilizopokelewa na Ofisi ya Rais, Ikulu, ni shilingi bilioni 40.90, hii ni sawa na asilimia 69. Bunge, fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge ni shilingi bilioni 8.88, iliyopokelewa ni bilioni 2.95, hii ni sawa sawa na asilimia 36. Mahakama fedha iliyoidhinishwa na Bunge ni shilingi bilioni 42.71, fedha iliyopokelewa mpaka mwezi Machi, 2014 ni shilingi bilioni 5.50, ni asilimia 13 tu.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la msingi kwenye Mhimili huu na Serikali ilione hili. Katika hali hiyo itakuwa hakuna majengo, hakuna Mahakama za Mwanzo zinazostahiki, hakuna Mahakama za Wilaya, hakuna Mahakama Kuu. Ikulu 69, Bunge 36, Mahakama 13.

Mheshimiwa Spika, fedha za uendeshaji au fedha za matumizi mengine; Ofisi ya Rais Ikulu asilimia 74 wakati haupo na fedha zipo hapa, Bunge ambalo na mimi nimo ni asilimia 76.1, Mahakama asilimia 56. Hivyo, ni ushahidi mwingine kuonesha kuwa, Mahakama bado hatujaipa nafasi inayostahiki. Inawezekana Mahakama tunaihitaji tukiwa na matatizo yetu lakini hali halisi haishughulikiwi kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, leo Mhimili unaomba wafanyakazi 1,264 kwa bajeti ya mwaka 2013/2014 Mhimili huo unapewa kibali cha watu 148, maana kama Wizara au kama Idara.

Mheshimiwa Waziri anasema kuwa, ili kesi zipungue na mahabusu wapungue, ni lazima Mahakama pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na *Division* ya Mahakama …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Tunashukuru. Mheshimiwa Raya Khamis, nilimtaja kwanza.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pili, ningependa kuchangia Hotuba hii ya Katiba na Sheria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ningependa kuendeleza ambapo Mheshimiwa Mdee ameishia, kuhusiana na suala zima lililopo katika UDA na kesi yake katika Mahakama. Tunaona kwamba, Mahakamani tayari kesi ya UDA ilikuwepo na kiutaratibu kesi lazima iwe imefanyiwa uchunguzi, tayari kuna kila kitu, ndiyo kesi inafunguliwa. Jambo la kushangaza ni kwamba, katika suala hili, hii kesi imefunguliwa *then DPP* akaifuta! Tunataka kujua ni sababu zipi zilizopelekea kesi hii kufutwa na ni lini inatarajiwa kuendelezwa ama kufunguliwa ili tujue ni nini kinaendelea na kitu gani kipo hapo katikati ambacho tunafikiri labda kinataka kufichwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, katika suala ambalo amelizungumzia Halima Mdee na suala ambalo ninaunga mkono Hotuba ya Kambi ya Upinzani ni *issue* nzima ya Bunge Maalum la Katiba. Cha kusikitisha, katika Bunge la Katiba changamoto zake ukurasa wa 33 na 34; nilifikiri kwamba, miongoni mwa changamoto ni jinsi ambavyo tunaliendeleza, Muundo wake haujaridhisha baadhi ya Wabunge ambao ni Wajumbe. Vilevile tunaona kwamba, Bunge hili bado lina mzozo, Muundo wake kwa ujumla bado inakuwa ni utata na haueleweki katika jamii ni kitu gani. Wananchi wengi wanahitaji kujua kuna nini na ni kitu gani na Muundo mzima wa hili Bunge unakwendaje na unakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo yangu na maoni yangu, naomba myachukue na myazingatie. Kwa kuwa Bunge hili bado lina utata, napendekeza Waziri pamoja na kuishauri Serikali, hatuoni umuhimu wa kuleta Muswada katika Bunge hili wa kuamua kulisimamisha Bunge hili la Katiba mpaka pale ambapo Muundo wa Bunge utakapokuwa unaeleweka na kuridhisha. Katika Bunge tuwe tuna mjadala ambao unajadili mawazo ya Wananchi na tuwe na mjadala ambao unaleta masilahi ya Wananchi katika Taifa hili na siyo kujadili itikadi ya watu fulani, ama vyovyote ambavyo ilivyo, kujadili mawazo ya kikundi cha watu wachache badala ya mawazo ya Wananchi kama ambavyo inatarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuelezea *delay* za kesi Mahakamani. Katika Hotuba ya Waziri, ukurasa wa 13, ameelezea vizuri kwamba, wanajitahidi kufanya taratibu mbalimbali kuondokana na mrundikano wa kesi ama *delaying* za kesi katika Mahakama zetu. Ningependa nijue ni kesi ngapi katika kesi ngapi ambazo tayari zimesikilizwa ndani ya muda ambao Waziri ameueleza hapa ndani ya miaka miwili?

Ningependa kujua ni kesi ngapi katika kesi ama watuhumiwa ambao wako ndani si chini ya miaka mitano mpaka sasa zilizosikilizwa katika hizo kesi ambazo anasema zimesikilizwa ndani ya miaka miwili; ama tunakuwa tunasikiliza kesi ambazo tunaangalia huyu ambaye amekuja na hii kesi yupo katika *position* gani ya maisha, tunampa *priority* katika kusikiliza kesi zake. Ningependa kujua, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atuambie ni kesi ngapi ka ya hizi ambazo mmesema mnajitahidi kuondoa mlundikano wa kesi mahakamani zimesikilizwa ambazo zipo ndani ya miaka mitano bado zilikuwa hazijafunguliwa?

Mheshimiwa Spika, vilevile tunaona kwamba, tuna Tume ya Haki za Binadamu na kuna watu ambao wanashughulika na hiki Kitengo. Bado kuna Watanzania ambao wapo Mahakamani si chini ya miaka tisa mpaka kumi kesi zao hazijasikilizwa. Hakuna utaratibu wowote na hatujui ni lini kesi zao zitafunguliwa kusikilizwa mahakamani. Ningependa kusisitiza kuundwe *Special Unit* ambayo itakwenda kwenye mahabusu kuwahoji wale wafungwa wana muda gani na kesi zao zitaisha lini? Kwa sababu kuna baadhi ya mahabusu mpaka leo hawajui wana makosa gani na hawajui kesi zao zitaanza lini kusikilizwa na bado mafaili ya kesi zao hayajafunguliwa. Hatuoni kwamba tunawanyanyasa hawa watu kwa kuwaweka ndani kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningependa nitoe ushauri na ningependa kujua suala zima la hao mahabusu ambao wanachukua muda

mrefu kukaa ndani. Tume ya haki za binadamu inaliona vipi hili suala na inasema nini kuhusiana na watu kukaa ndani muda mrefu na muda wa unapofika wa kesi zao kufunguliwa na kuanza kusikilizwa watu wale wanaonekana hawana makosa na kuambiwa hawana mashtaka ya kujibu na kuachiwa warudi nje, wakati wameshapoteza muda mrefu wakiwa ndani; ni kitu gani ambacho wenzetu hawa wanalipwa kutokana na kupotezewa muda wao mrefu wakiwa ndani?

Mheshimiwa Spika, ningependa nizungumzie suala zima la rushwa katika Mahakama zetu. Katika *system* nzima na mfumo mzima wa Mahakama zetu, tunaona hizi *delaying* zipo. Unakwenda Mahakamani, Jaji anajua *hearing* leo inatakiwa ama leo kuna *ruling* ya kesi fulani na yeye ndiye ambaye anakupa tarehe, unafika Mahakamani unaambiwa Jaji hayupo. Mbaya zaidi na cha kusikitisha, hakuna taarifa zozote za upande ambao unakwenda kusikiliza *ruling* ama *judgment* inayosimamiwa na yule Jaji, hakuna taarifa zozote zilizopo upande wa pili kwamba Jaji huyu hatakuwepo ana dharura ama ana kitu fulani.

Kwa kweli tunasikitishwa na hili, unakuta kesi tayari imeshafikia *ruling,* inachukua labda miezi sita, saba, mpaka Jaji aje apatikane. Inapelekwa kwa mwingine inapewa tarehe, tarehe ambayo inapewa akirudi anaambiwa tena hayupo ama kama ni *hearing* tayari mashahidi wamepatikana na ni vigumu na inachukua g harama nyingi. Kwa hiyo, tunazidi kuwashushia mzigo watu ambao ilibidi kesi zao ziwe ndani ya muda fulani na tunaona kwamba, zinazidi kuchelewa zinaendelea kuchukua muda zaidi kwa sababu ya Jaji kutokuwepo na kutokutoa taarifa yoyote kwa upande wa pili. Muda mwingine mashahidi wanatoka mikoa mbalimbali ama wengine wako nchi nyingine wanakuja kutoa ushahidi, wakifika wanakuta Jaji hayupo na taarifa hakuna kujua nini ambacho kimetokea, haileti picha nzuri.

Mheshimiwa Spika, bado tunarudi tena katika *system* nzima ya mtindo wa rushwa Mahakamani, *anyway* au vyovyote ambavyo tunaweza kuita kwamba tuna …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** *Time!* Mheshimiwa Fakharia nilimtaja kabla ya hapo.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwanza, naunga mkono hoja ya Wizara. Pili, nataka kuuliza hivi hapa tunazungumzia Bunge la Katiba au tunazungumzia Bajeti? *(Makofi)*

Kwa sababu ninashangaa wanapozungumza watu wakati tulikuwa nao kwenye Bunge la Katiba, wakachukua mpira wakaweka kwapani wakatoka, leo kwenye kipindi cha Bunge la Bajeti wameanza kufufua yale yaliyokuwa yamejificha! Wameondoka hawakuaga na kurudi wanaweza wakarudi sisi hatuna matatizo. Bunge la Katiba litakuwepo mwezi wa nane, rudini tuje tutangaze hoja humu ndani, tujue nini kinachoendelea. Siyo iwe kuchupia chupia katika masuala mengine kuzungumzia mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nataka kuzungumzia Wizara ya Katiba yenyewe, Wizara Mama. Wizara ya Katiba ndiyo Wizara Mama iliyobeba Taasisi kadhaa. Wizara ya Katiba katika bajeti yake ya mwaka 2013/2014, ilipangiwa shilingi 7,066,331,500. Cha kushangaza, hii fedha huwa hawaipati yote na kama mtu hupati kitu cha kutosha hata kufanya kazi yako kwa ukamilifu haiwezekani. Wamepewa shilingi 2,355,175,821. Utaona hapa kama pana mchezo, hatuitaki Wizara ifanye kazi. Eti Wizara hiyo ina Mahakama, Wizara hiyo ina Afisa Mwanasheria, Wizara hiyo ina Tume ya Haki za Binadamu. Wizara hiyo ina Ofisi nyeti nyeti tunazozitaka ziweze kuweka utawala bora katika nchi yetu na ndiyo hizo Mafungu yake hayapati fedha. Tunategemea wafanye kazi au bado tuwe tunasuasua na kucheza wakati wenzetu watakuwa wanasonga mbele sisi bado tunarudi nyuma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukija mazingira duni ya kufanyia kazi; Wizara pamoja na Taasisi zake, sehemu za kufanyia kazi ziko duni. Imezungumzwa hapa, Ofisi ya Jaji Mkuu ukienda usiombe kuzimwe umeme, maana hata ukifungua madirisha ndani hamwonani. Sasa utakuta vituko vinavyokuweko; sijui tunaangalia Mhimili au tunaangalia kwamba hii ni Mahakama kwa sababu Mahakama ni sehemu inayokwenda kutia watu adabu. Sijui tuzungumze kitu gani! Mahakama haimtii mtu adabu. Kwa sababu sisi tuko nje huku, kama hujatenda maovu huwezi kufika na kila aliyefika kule huwa kama anakwenda kupata elimu ya kuondosha lile alilolitenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakuta sasa hivi elimu tunayoipata ni duni. Unajua sasa hivi mitaani mtu akiiba kuku au kibaka kafanya jambo kaiba simu, mtu huyu akipatikana atakamatwa achomwe moto, badala ya kupelekwa kwenye Vyombo vya Sheria. Sasa mimi naomba elimu itolewe na watoaji elimu ni hii sehemu ya Sheria na hawa kutoa elimu ni fedha hawapewi, tutegemee maadili yetu yatakuwaje? *(Makofi)*

Itakuwa tukikamatana badala ya kupelekana kwenye Vyombo vya Sheria tunatiana moto. Ina maana baada ya kuweka amani na utulivu, tutaanza kuwa na mazingira ambayo siyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho ninataka kukizungumzia ni kuhusu rushwa. Unajua hii ni Taasisi nyeti au Wizara nyeti. Kwa hali halisi ilivyo ni sehemu ya pili katika Taasisi zenye watumishi ambao wanaongoza kwa rushwa. Naiomba Wizara pamoja na Taasisi zake, kwa sababu sisi tunakutegemeeni ninyi, sisi tunakuangalieni ninyi, ikiwa mtaongoza kwa rushwa sasa wanaokuangalieni huku nyuma watafanya nini?

Hali halisi tukiangalia wakati mwingine tunakuoneni ninyi ndiyo mnaotaka rushwa; kumbe na sisi wenyewe huku Wananchi tunaongoza kuwafanya wao wapende rushwa. Sasa bado naendelea kusema, elimu itolewe ili kwa mpokeaji na mtoaji kitu hiki kiwe kimoja hakiwezekani na Tanzania bila ya rushwa inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nitazungumzia kuhusu mahabusu wetu. Mahabusu ni sehemu mbaya na si nzuri kupelekwa kiongozi, raia au kupelekwa watoto. Hivi sasa mahabusu wamejaa katika magereza yetu, kesi haziendi kwa utaratibu uliopangwa. Mwaka jana nilizungumza nikaambiwa imepangwa ratiba ambapo kila mmoja anatakiwa kiasi fulani cha kesi azitekeleze, lakini wanashindwa kutekeleza; sehemu ya kufanyia kazi hawana na fedha za kufanyia kazi hakuna. Sasa naomba atakapokuja Mheshimiwa Waziri atuambie mbinu gani watakazotumia ili hii Wizara iweze kufanya kazi zake kwa uhakika na Watendaji waweze kupata mafao yao kwa uhakika na fedha za maendeleo zipatikane kwa uhakika ili waweze kutekeleza majukumu yao na kujenga maofisi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Elizabeth Batenga; nafikiri yupo?

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie machache katika Hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo ningependa kuliungumzia ni kasi ya kurekebisha Sheria mbalimbali ambazo zinaonekana zina upungufu. Kwa muda mrefu tumedai Sheria mbalimbali zirekebishwe hasa zile ambazo zinaonesha zinakandamiza wanawake na watoto. Sheria ya Mirathi, Sheria ya Ndoa na nyinginezo ambazo zinakandamiza wanawake na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazidi kusisitiza na kuomba kwamba, kasi ya kurekebisha Sheria hizi iongezwe. *(Makofi)*

La pili, elimu kuhusu Sheria. Bunge hili kazi yake kubwa ni kutunga Sheria. Zinapotungwa Sheria, zinawahusu Wananchi wote kwa namna moja au nyingine. Sasa kama Wananchi hawaelimishwi kuhusu hizi Sheria, utekelezaji wake unakuwa ni mgumu. *(Makofi)*

Tunajua kwamba, kutokujua Sheria hakukupi wewe unafuu au haki ya kusema kwamba, hukujua ndiyo maana umekosea. Kwa hiyo, mtu unaweza kutenda kosa bila kutambua unaadhibiwa, lakini kumbe Wizara hii ndiyo inapaswa kutoa elimu kuhusu Sheria zote zinazotungwa na hasa ndugu zetu wa huko vijijini mambo mengine hawayajui. Mheshimiwa Waziri, ameeleza katika Hotuba yake kwamba, wanatoa elimu ya Sheria, lakini niseme tu kwamba haitoshelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mahakama ndiyo inayotafsiri Sheria na kutoa haki, lakini haki haipatikani mpaka uidai, mpaka uitafute. Katika kutafuta na kudai ni lazima uwe na uelewa. Katika Mahakama inategemea ni jinsi gani utakavyojitetea au utakavyojieleza ndipo utaweza kupata ile haki. Kwa hiyo, mtu wa kawaida kwenda kusimama Mahakamani na kutetea haki yake wakati mwingine inakuwa ni vigumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iendeleze mpango huu ambao imeuanzisha wa kuwapa watu msaada wa kisheria ili watu wasipoteze haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nivipongeze Vyama Visivyo vya Kiserekali, katika shughuli hii ya kusaidia watu ambao wanahitaji msaada wa kisheria. Nitambue Chama cha Wanasheria Wanawake *(TAWLA)*, kwa namna wanavyojitahidi kuwasaidia Wananchi na hasa Wanawake katika kudai haki zao. Wameanzisha Mradi wa *Paralegals.* Sasa naomba Wizara iisaidie *TAWLA* katika kuendeleza huu Mpango wa *Paralegals* ili uweze kuenea katika maeneo mbalimbali hasa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niseme tu kwamba, Opereseni Kimbunga haikulenga watu wenye asili ya Kinyarwanda. Operesheni Kimbunga ililenga watu wote ambao wako nchini kinyume cha Sheria. Sasa kama mtu yuko Tanzania anakaa isivyo halali kurudishwa kwenu inakuwa nongwa kwa sababu gani? *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba watu wasizidi kupotosha kwamba, Operesheni Kimbunga ilianzishwa kwa sababu ya kuwaadhibu Wanyarwanda baada ya kinachoitwa mgogoro kati ya Rais wa Tanzania na Rais wa Rwanda. Operesheni hii ililenga watu wote ambao walikuwa Tanzania kinyume cha

utaratibu. Tanzania inawakaribisha watu wote wanaopenda kuishi kwa amani na kwa kufuata Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri ili …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Amesikia. Waheshimiwa Wabunge, naomba niwakumbushe jambo moja; utaratibu wetu wa kuchangia ni wa kujaza fomu siyo kuleta hapa. Kama jina lako halipo katika fomu zile hupati nafasi hapa. Hata ukisema unampa nafasi yangu mwingine, huyo mwingine lazima awe humu kwenye fomu zangu. Akiwa kwenye fomu zangu hiari yenu kama mnataka azungumze atazungumza, isipokuwa pia nitaangalia aliyechangia mara nyingi kwa mujibu wa Kanuni hawezi kupewa nafasi kama wengine wapo katika orodha ile ile. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nakuombeni sana msiniletee vibarua mimi sasa sichangii atachangia mwingine badala yangu aah, tafadhali mkajaze fomu vizuri. Tumesema mtu unaweza ukajaza mpaka Wizara sita unazofikiria unazipenda kwa kulingana na ya kwanza, ya pili ya tatu, vile unavyotaka. Kwa hiyo, hii inakuwa vizuri kwa sababu hata kama anachangia mwingine, lakini si aliomba na yeye. Alistahili kupata lakini labda nafasi haikutosha na wewe ukasema naomba achangie mwingine lakini yumo katika maombi ya siku ya Wizara ile na katika kundi.

Nawaombeni hili mlizingatie kwa sababu niliona vinoti vingi vinasema basi wachangie, hapana. Ambao wanaweza kuchangia bila kuwa wamejaza fomu ni Mawaziri, nao pia watachangia eneo linalohusiana na Wizara zao siyo popote pale na ataondoka mwingine kati yao, atasema ataondoka fulani kwa ajili ya huyu mpaka idadi ile itimie.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako!

**SPIKA:** Mheshimiwa Kombo!

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa Ibara ya 68(7). Jana wakati Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini alimshutumu Balozi wa Uingereza akidai anaingilia mambo ya ndani ya nchi na kumtaka kwenda kujieleza Wizarani.

Mheshimiwa Spika, suala hilo tayari vyombo vya habari vimeanza kuandika taarifa hiyo jambo ambalo kitaifa litaitia doa nchi yetu katika nyanja za Kimataifa na kutokuwa na uelewano mzuri na Uingereza. Hii ni *diplomatic crisis.*

Mheshimiwa Spika, Waingereza na Tanzania…

**SPIKA:** Naomba, habari ya Waingereza, mimi ninawajua!

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakuomba kuitaka Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Uhusiano wa Kimataifa kutoa maelezo ya kina juu ya sakata hili.

**SPIKA:** Kwa sababu mlikuwa mmeondoka, Waziri Mkuu alishasema hilo! Mheshimiwa Dkt. Kikwembe!

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana name kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Mawasiliano kwa niaba ya wananchi wa Katavi.

Mheshimia Spika, kwanza kabisa napenda niwapongeze Prof. Mbarawa pamoja na Ndugu yangu Mheshimiwa Januari kwa kazi yao nzuri wanayoifanya. Ninawapongeza kwa sababu nimeona hata katika huu mradi wa kuunganisha shule za umma na mtandao wa *internet* hata shule yetu moja ya Mpanda Ndogo Sekondari imo, kwa hiyo nawapongeza kwa hilo.

Pia niwapongeze kwa kuweza kutupa kupaumbele Mikoa mipya ikiwemo Katavi, Njombe, Simiyu na Geita kutupatia ving'amuzi katika Mikoa mipya na katika Mkoa wa Katavi Wilaya ya Mpanda mmetupa Ilembo, Misunkumilo,

Shanwe, Kajense, Kashaulili, Nsemlwa, lakini mmeiacha Kata mmoja ambayo ni muhimu sana ina watu wengi kule, watu wenye mifugo na wakulima wa mpunga, Kata ya Kakese. Kwa hiyo na yenyewe ninaomba kama mnaweza mtuingizie ile Kata. Ninawashukuru pia katika kutuweka katika Mpango wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote.

Mheshimiwa Spika, mimi ninachoshangaa tu ni kwamba, pamoja na kwamba nawapongeza, lakini kwa kweli sijajua ni uwiano gani wa Kata walioutumia kuzipatia Kata hivyo vipaumbele. Kwa mfano, katika Mkoa wa Katavi tuna Kata moja tu ya Ikola kwa awamu ya kwanza. Awamu ya pili tuna Kata ya Katuma. Nawapongeza kwa juhudi zenu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Januari anakumbuka nilivyokuwa nampigia kelele kuhusu Kata ya Katuma na ninashukuru Mungu kwa sababu pale patakuwa ni Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda Vijijini, namshukuru sana kwa hilo na wananchi hivi wanavyosikia wanafurahia na tunaomba mkandarasi aende pale, kama ni *Vodacom* au ni nani basi wajitahidi wananchi wale waweze kupata huduma kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivi? Ninasema hivi kwa sababu Kata zetu zimekaa mbalimbali sana, sehemu kubwa ya Mpanda ni pori. Kwa hiyo tunaomba sana mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali iweze kutuweka katika huu Mpango wa Awamu ya Kwanza B. Naomba mnipatie Kata ya Ilunde. Kata ya Ilunde ipo Kisiwani. Kutoka Ilunde mpaka Inyonga Makao Makuu ni karibu saa sita, pana pori la hifadhi pale katikati. Pale mtu atoke ndiyo aje kupanda mti, na picha ninayo. Unapanda mti pale, ndiyo unapiga simu. Kwa mwanamke huwezi kukwea mti ni parefu, kwanza kuna wanyama kuna tembo, kuna faru, kuna nyati, kwa hiyo unamtuma mtu anaenda kukusomea siri zako, apande juu ya mti, tena anakuacha kijijini kwa sababu huwezi kwenda naye ni porini. Kwa hiyo kidogo kwa kweli inatuletea adha.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, Kata ya Ilunde wanategemea hospitali ya Inyonga (Kituo cha Afya cha Inyonga) ni mbali sana pale. Nakumbuka hata wakati wa kuchangia mwaka jana kwenye afya niliomba *ambulance*, pikipiki pale haifai ni pori la hifadhi. Kwa hiyo mimi ninaomba Ilunde mtupatie mawasiliano kwa kweli, wametesema kiasi cha kutosha wale watu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nije pale Inyonga Makao Makuu ya Wilaya Mlele. Inyonga Makao Makuu ya Wilaya ya Mlele wanatumia mnara mmoja nafikiri ni wa *Vodacom* ambao sasa nafikiri wameingia *share* na aidha ni *Airtel*, au nini. Sasa ule mnara unazidiwa kwa hiyo inaonesha kabisa Inyonga hakuna

mawasiliano. Kwa hiyo mimi niwaombe mtupelekee mnara pale Inyonga Makao Makuu ya Wilaya ya Mlele.

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, Kata zingine mmezitenga. Katika Kata zote 42, Kata karibu 24 zote mmeziacha hazina mpango wowote wa kuingizwa kwenye huu mpango wa mawasiliano ya mwaka huu. Sasa basi, mimi niombe katika hizo mlizoziacha, naomba pia Kata ya Mwamapuli. Kata ya Mwamapuli ni Kata muhimu sana, kule kuna bonde la mpunga, kuna mashine ya kisasa kwa juhudi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu ni Jimbo lake, ameweka mtambo wa kisasa wa kupembua mpunga, kuukoboa, kuu-*grade* na kuupaki. Kuna kituo cha mawasiliano kwa ajili ya biashara, kutangaza nchi nzima.
Kwa hiyo, ninaomba pale napo muwape kipaumbele muwapatie mnara.

Mheshimiwa Spika, lakini pia narudi Itenka. Itenka nako ni wakulima hao hao. Naomba muwape mnara.

Mheshimiwa Spika, machimboni ambako ndiko wananchi wengi wanafanya shughuli zao za uchimbaji mdogo mdogo, eneo lile ni hatari, bila mawasiliano kwa kweli ni tatizo. Naomba muwapatie mnara pale waweze kupata mawasiliano kwa urahisi kwa sababu mara nyingi wamekuwa wakitekwa hata mchana hata saa ngapi.

Hivi tu karibuni imebidi tuweke kituo cha Polisi pale kwa ajili ya kuwalinda hawa wachimbaji wadogo ambao wanatoka mjini kwenda machimboni kuchimba na kurudi. Kwa hiyo, naomba pia kule muwapatie mnara ambao utawasaidia kupata mawasiliano ya haraka na Askari pindi wanapokuwa wanavamiwa kwa sababu yale maeneo ni ya wachimbaji.

Mheshimiwa Spika, pia kuna Kata nyingine ambayo ni muhimu sana Kata ya Ugala, pale pia ni eneo la pori, ni eneo pia treni inapita na mara nyingi panapata matatizo ya kujaa maji na treni inashindwa kupita. Mimi naona kwa umuhimu wa mawasiliano, pia Kata ya Ugala napenda muwapatie kipaumbele katika hii Awamu ya Kwanza B ili tuweze kuwa na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, lakini na Kata zingine pia za Litapunga, Mamba, Mbede, Stalike ambao wapo karibu na Mbuga ya Katavi ni rahisi pale kuvamiwa na majangiri, kwa hiyo nao pia wanatakiwa kupata minara pale na Kata zingine zote, ikiwemo Karema, Kapalamsenga, Mishamo, Kabungu, Utende, Usevya, Urwila, Ugala, Majimoto, Sibeswa, Mwese na Mishama, kwa

sababu ni mpakani na bado tuna makambi ya Wakimbizi, kwa hiyo napenda tuwe na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine limeangalia orodha ya makongamano ambayo yanafanywa na Wizara hii nafikiri kupitia *COSTECH*. Mheshimiwa Spika, bado nashangaa ni uwiano upi unaotumiwa katika kugawanya hivi vitu.

Niwaombe basi, naomba mimi makongamano katika hayo mliyoyapanga, Mkoa wa Katavi hamkuupa kabisa, mliipa Nkansi ufugaji wa ng'ombe wa nyama. Sasa naomba Mkoa wa Katavi ikiwezekana katika mpango wenu, mimi niwaombe tuna Mbuga kule ya Katavi *National Park,* tuleteeni makongamano ya utalii, ufugaji nyuki na kurina asali.

**SPIKA:** Muda wako umekwisha.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasikila!

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii uliyonipatia niweze kuzungumza machache kuhusu Wizara hii muhimu sana ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na niwapongeze Waziri, Naibu Waziri, lakini na watendaji wote katika Wizara nyeti hii.

Meshimiwa Spika, nilikuwepo katika Kamati ya Miundombinu mara ya mwisho, sasa hivi nipo TAMISEMI, lakini najua changamoto nyingi wanazozipata Wizara hii kwa sababu ni Wizara pia inayojitahidi kufanya tafiti na kuzalisha wanasayansi kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, kwa vile muda ni mfupi, niende moja kwa moja kwenye hotuba ya Waziri ukurasa wa 96, imeonesha kwamba katika mwaka 2013/14 Kata 77 zilizopata Wazabuni kwa Mkoa wetu wa Rukwa kwa awamu ya kwanza (A) ilikuwa ni Nkansi Kata ya Wampembe tu ambayo vijiji sita vilinufaika na Voda. Kwa awamu ya pili (B) Nkansi tena, Namanyere lakini na Sumbawanga vijijini Kata ya Kaoze. Hivyo unaweza kuona kwamba katika awamu mbili ni Kata tatu tu ambazo zilikuwa zimenufaika.

Mheshimiwa Spika, hizi ni Kata chache ukilinganisha na maeneo yalivyokaa vibaya na ukiangalia kwamba Mkoa wetu wa Rukwa upo pembezoni mno, umepakana na nchi ya Congo na Zambia, hivyo tunahitaji mawasiliano kwa ukaribu sana ili tuweze kuwasiliana na Makao Makuu mara tunapokuwa tumepata shida.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kwamba ni Nkansi na Sumbawanga Vijijini waliokuwa wamefikiriwa zaidi, lakini inawezekana Sumbawanga Mjini kwa

sababu mawasiliano siyo mabaya sana ndiyo maana haiku-*appear* kwenye mlolongo huu wa awamu ya kwanza na ya pili.

Mheshimiwa Spika, tukizungumzia Wilaya ya Kalambo ni Wilaya mpya imezaliwa na Wilaya ya Sumbawanga Vijijini, hivyo ukiangalia hata katika mgawo wa zabuni kwenye hizi Kata, Kalambo haijaoneshwa mahali popote. Lakini Wilaya ambayo mpakani kweli kweli, ni mpakani kwa Zambia lakini tena mpakani kwa *DRC*. Kwa hiyo, utakuta *movement* kutoka Zambia na *DRC* ni kubwa mno kwamba hata kama uhalifu utakuwa unaingia nchini, siyo rahisi kuwakamata kwa sababu mawasiliano ni mabaya sana.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika Wilaya hii ya Kalambo kuna Kata ambazo mawasiliano yake ni mabaya sana, Kata ya Mwimbi ina mawasiliano ya kusuasua, lakini Mnamba ni karibu hakuna. Mambwekenya, Madibila karibu hakuna mawasiliano kabisa, Legezamwendo na Mambonkoswe, Kalembe hakuna, Katete hakuna na ukipata ni ya kusuasua, ukifika hapa utapata mawasiliano, lakini ukisogea hatua kumi mbele hamna. Kituo cha Afya Ngorotwa ndiyo mbaya zaidi hata wauguzi na waganga kupata mawasiliano siyo rahisi.

Mheshimiwa Spika, kuna Kijiji kipo katikati Ziwa Tanganyika kinaitwa Kipwa wale wanategemea *Airtel* Zambia, hivyo mawasiliano na huku ng'ambo siyo rahisi. Kilewani wana mnara wa *Voda* lakini wa *Airtel* hamna. Kijiji cha Samazi na Kipanga pia hawana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Vijiji hivi viweze kupatiwa mawasiliano. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amesema *the way forward* wana mpango wa kufanya tathmini kuangalia mahitaji ya huduma za mawasiliano katika maeneo yasiyo na mvuto kibiashara nchini kwa lengo la kuyajumuisha katika mradi wa mfuko wa *UCAF*.

Mheshimiwa Spika, Kalambo au Mkoa wa Rukwa una mvuto wa kibiashara sana tu, kwa sababu wananchi wale wanalima, wanauza, wana pesa mfukoni, hawawezi kukosa pesa ya kununua simu au *airtime* na *population* yake ni kubwa. Hivyo watakapokuwa wanafanya tathmini wakifika maeneo ya Kalambo, wasisahau Wilaya hii ambayo ina Kata 17 lakini haionekani hata kwenye taarifa hii ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano kupitia redio, kule redio wanayoipata zaidi ni redio Zambia na hata kwenye simu ukifika maeneo yale unakutana tu na masafa unaambiwa *welcome to Airtel* Zambia. Inawezekana minara michache iliyopo kule haina nguvu sana inavutwa na minara ya Zambia. Kwa hiyo nilikuwa naomba mtakapofanya tathmini kule Kalambo mpitie muangalie

ile minara ina upungufu gani. Kwa sababu utakuta kuna mnara wa *Voda* lakini unaambiwa *welcome to Airtel* Zambia. Ukifika kufanya kazi kule ujue siku saba nzima utakuwa huwasiliani na watu wa Morogoro au Tabora.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 68 wa hotuba pia naona kuanzisha vituo vinne vya majaribio ya redio jamii *(community radio)*. Nilikuwa naomba basi, sijui kama vimeshatengwa hivi vituo vine! Kama havijatengwa, basi waweze kuwafikiria wananchi wa Kata ya Mkali kule Kalambo kwa sababu wao hawasikii redio ya aina yeyote, wametengwa wapo kisiwani kabisa hawajui kinachoendelea hapa Tanzania. Hivyo, watakapokuwa wanaanzisha hii *community radio* chonde chonde, Mheshimiwa Waziri Mbarawa, wafikirieni watu wa Kalambo, tupo mbali mno kule, tuwafikirie na wao, hakuna wanachokisikia huku, runinga ni taabu.

Tushukuru tu kwamba Nishati na Madini jana wamesema watakuwa wakieneza sasa umeme vijijini kote kwa maana ya *REA* labda watapata runinga. Lakini kuna sehemu runinga inapatikana kwa shida sana, wanasema pengine ving'amuzi. Naomba muweze kuangalia hili suala.

Mheshimiwa Spika, nikiendelea na mawasiliano ya aina nyingine; tumeweza kuona kwamba mawasiliano ni mazuri yakiwepo yanaweza yakasaidia hata kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi. *Otherwise* watumishi ni wachache sana kwenye zahanati zetu.

Kama mgonjwa, mzazi yupo kitandani anahudumiwa na muuguzi na muunguzi yupo peke yake na anahitaji mawasiliano, inabidi amuache mzazi aende mahali ambapo mtandao kidogo unapatikana ili aweze angalau kuita gari la wagonjwa au aweze kutafuta msaada. Matokeo yake sasa kama hali ilikuwa mbaya kwa huyu mama ndiyo hapo tunapopoteza wajawazito.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache nilikuwa najaribu kuikumbusha Wizara kwamba mnapoifikiria Sumbawanga Vijijini mfikirie kwamba kuna Kalambo ambayo imezaliwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MICHANGO YA MAANDISHI**

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, ombi langu la siku zote ni kuhusu minara katika maeneo yafuatayo:-Kata ya Bugando (Nyamigamba na Leheja), Kata ya Mantare (Mwanekeyi), Kata ya Ngulla (Nyambuyi) na Kata ya Sukuma Jimbo la Magu katika vijiji vya Isemi, Lumeji, Kitongo, Nyauhanga na Buhumbi.

Mheshimiwa Spika, maeneo hayo hayana mawasiliano yenye uhakika, ukitaka kuwasiliana ni mpaka uende sehemu ya mwinuko. Naomba Serikali iviambie vyombo vinavyomiliki huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano katika karne ya leo ni mkombozi mkubwa kutokana na teknolojia ya sasa na siku zijazo, msisitizo ni kwamba sekta hii iwe makini katika kupunguza upatikanaji wa mawasiliano ya simu wakati mtumiaji anaongea ili kupunguza gharama kwa mlaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, natambua uwezo na dhamira ya Waziri na Naibu ingawa mnakwamishwa zaidi na bajeti ndogo ya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, naomba kushukuru japo kwa hatua ya awali nianze kuona minara inajengwa katika vijiji vya Sunuka, Kalya na Igalula kwa Ukanda wa Ziwa.

Mheshimiwa Spika, ombi langu bado vijiji vya Kanda ya Ziwa vya mpakani na *DRC* havijapata mawasiliano vyote. Vijiji hivyo ni Sigunga, Sibwesa, Kashagalu na Konkwa. Ombi langu pia ni Kata za Ukanda wa barabara ambao vijiji vya Kandaga, Mtego, Ilalangulu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ijitahidi kuharakisha mchakato wa kufanya makampuni ya simu kuwa na uwazi wa mapato yao kwa faida ya kodi sahihi na mapato ya wasanii.

Mheshimiwa Spika, nashauri msukumo katika tafiti uongezwe, bado bajeti ni ndogo sana.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, kupitia maandishi nichangie bajeti/hotuba ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ni chachu ya maendeleo kwa kuwa shughuli yoyote inayoendeshwa kwa kutegemea sayansi na teknolojia inakuwa na tija ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, ushauri kwa Serikali ni kuwa Wizara hii ichukue jukumu la kuwa kiongozi kwa kuhimiza Idara, Taasisi, Asasi na Wizara zote za Serikali zinawekeza sana kwenye sayansi na teknolojia. Matumizi na ufundishaji wa sayansi na teknolojia kwa upande wa elimu utasaidia kuwa na raia wenye

uelewa na hali ya juu. Hii iwe ni kwa hao wanaoelimishwa wataajiriwa au watajiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya sayansi na teknolojia katika shughuli kwa kiasi kikubwa itasaidia kupunguza gharama, kuongeza ubora wa bidhaa/huduma. Rasilimali muda kidogo hutumika pale sayansi na teknolojia inapotumika. Ili tusonge mbele kwa kasi tunayotegemea lazima tuwekeze katika sekta hii na Wizara hii ibebe jukumu ka kuwa kiongozi.

Mheshimiwa Spika, katika kampuni za simu, *TTCL* ni kampuni ambayo inamilikiwa na umma kwa asilimia 50. Umiliki huu kwa kushirikiana na huyu mbia binafsi kimsingi unasigina ukuaji wa kampuni hii. Pamoja na upungufu huu mwananchi walio wengi wanamashaka na hawafurahii aina hii ya ushirika.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha *TTCL* kuwa na nguvu na uthubutu wa kukua na kushindana, Serikali ichukue hisa zote za *TTCL*. Ili kukusanya mtaji, hisa hizo za wamiliki binafsi zinaweza kuuzwa kwa wananchi kwa ujumla wake. Katika dunia ya sasa Tanzania kama Taifa lazima tuwe na kampuni yetu ambayo itaweza kuendesha shughuli kwa kuzingatia maslahi ya Taifa zaidi.

Mheshimiwa Spika, nasikitika Kata zangu za Rutoro na Ng'eng'e zimeendelea kuwa maeneo yasiyokuwa na mawasiliano ya simu. Katika kitabu cha Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ukurasa wa 59 Kata hizi zimeorodheshwa. Naendelea kushauri maeneo haya yapate minara ya simu, kwanza mbali ya kuwa kuna watu wengi zipo shughuli nyingi za maendeleo. Zaidi haya ni maeneo ambayo yanahatarisha usalama kutokana na kuwepo watu wengi wageni toka nchi jirani bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali ya Kata hizi mbili naomba na kushauri Kata za Rutoro na Ng'eng'e zijengwe minara ya simu za mkononi.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo au tuseme utaratibu wa kujenga minara kila kampuni na mnara wake. Kimsingi hii ni vurugu na tunaweza kuita uchafuzi wa mazingira. Ushauri ni kuwa tuwe na utaratibu wa kujenga minara ambapo kampuni nyingi zitachangia mnara mmoja. Utaratibu huu utawezesha minara mingi kusambazwa sehemu nyingine ikiwa ni pamoja na faida ya kupunguza gharama.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri, naomba mgao wa minara katika Jimbo la Lushoto na Wilaya kwa ujumla uimarishwe. Naomba usikivu uongezwe hasa kwa kuzingatia kwamba Wilaya ya Lushoto iko milimani na inahitaji minara mingi.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo naomba katika Jimbo langu yaongezwe minara ni katika Kata za Makanya, Malibwi, Mlola, Kwekanga na Kata ya Kwai maeneo ya Kireti, Kwefingo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mitandao ya kijamii idhibitiwe kwa kutoa matusi na kuandika maneno ya uchonganishi. Najua sio rahisi kudhibiti mawazo na tabia za watu ili kupata mafanikio katika kudhibiti mawasiliano ya mitandao ni budi kubadilisha sheria ya mawasiliano. Nashauri adhabu ziongezwe ili watakaopatikana na makosa ya matusi na uchonganishi watozwe faini kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara na makampuni ya mawasiliano kwa kuongeza ubunifu mfano, Tigo-Pesa, M-Pesa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara na Serikali kwa ujumla kutenga fedha za kutosha kwa tafiti mbalimbali zinazofanywa na taasisi za utafiti kama *COSTECH*. Wizara isimamie utafiti wa mazao kwa kutumia *Bio-Tecknowledge,* nchi jirani zetu wanakwenda kwa kasi kutafiti njia mbalimbali za kukuza kilimo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Wizara nikianza na Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara.

Pamoja na pongezi hizo naomba nitoe pongezi za dhati na za pekee kwa *TCRA* ikiongozwa na mkuu wao Profesa Nkoma, ukweli kazi yao si tu ni kubwa bali ni nzuri na bora kwani kila mwaka wamepiga hatua kubwa licha ya changamoto nyingi wanazokumbana nazo ikiwamo upungufu wa fedha kwa kulingana na azma yao au mikakati yao. Hivyo naiomba Serikali iongeze bajeti ya *TCRA*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maoni yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *TCRA* ndiyo wadau wakubwa ma watoa leseni kwa makampuni ya utangazaji wachukue hatua ya kusimamia makampuni haya kwa kuwakagua kama wametekeleza sheria inayowataka walipe mirabaha ya kazi zote za sanaa zilizotumika katika vyombo hivyo vya utangazaji.

Mheshimiwa Spika, ninawaamini *TCRA* kwani wapo makini kwenye kazi zao. Hivyo kwa hatua hiyo watakayoichukua *TCRA* itakuwa imesaidia *COSOTA* kupata fedha za mirabaha ambazo ni mali ya wasanii.

Mheshimiwa Spika, bado kuna tatizo kubwa sana kwenye makampuni ya kuuza milio ya simu hasa nyimbo na kadhalika. Mikataba inayowekwa haipo wazi kati ya wasanii na makampuni hayo. Pia bado malipo hayatekelezeki kama sheria inavyosema, sasa naomba Waziri atusaidie ni nini hicho?

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, makampuni ya simu yamekuwa yakiuza miito hiyo bila ridhaa ya mwenye simu. Kila baada ya ama wiki au siku nne utaambiwa umekatwa shilingi 400/= kuwekewa mlio wako upya kwa mwezi lakini hata mwezi haujaisha ndani ya siku nne au saba unauziwa tena bila ridhaa yako, kweli huo ni wizi.

Pia unaweza ukawekewa wimbo ambao hukuuomba, kwa mfano Shekhe kuwekewa *gospel* au Padri qaswida. Hali hii ni mbaya sana, ni wizi! Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba minara zaidi Wilaya mpya ya Mkalama. Nimeona Kata moja tu ya Mwanga, tafadhali tunaomba minara.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwanza fedha za kuendeleza kueneza Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili nchi nzima itoke kwa nje ulimwengu wa zamani.

Pili, fedha zitolewe za kuendeleza mradi wa uwekaji anwani za makazi na misimbo ya Posta katika maeneo yote nchini ili tuingie kwenye ulimwengu wa kisasa.

Tatu, *TCRA* fanyeni muwezalo kudhibiti picha za matusi kwenye mitandao, kwani nchi kama China, India na kwingine wameweza. Watoto wetu wanaathirika jamani, *please*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nawatakia baraka za Mungu katika kuifanya kazi hii.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, Shirika la Simu Tanzania ni shirika ambalo lipo muda mrefu. Shirika hili limekuwepo muda mrefu kabla ya kuwepo Mashirika ya Simu binafsi kama Zantel, Tigo, Vodacom, Airtel na kadhalika. Mashirika haya binafsi yanaendelea kupata faida na kuimarika kila leo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusitiksha Shirika letu la umma *(TTCL)* kila leo linaendelea kupata hasara, hivi sasa *TTCL* linadaiwa shilingi bilioni 105,237,881,863.02.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kujua deni kwa kiasi hicho limesababishwa na nini na je, hao waliosababisha Kampuni ya Simu *(TTCL)* kuwa na deni kiasi hicho wamechukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kuhama kutoka *analogue* kwenda kwenye *digital.* Hali hiyo sio mbaya, haidhuru wananchi wengi hivi sasa wanakosa mawasiliano lakini ninategemea hapo baadaye wananchi watapata mawasiliano yaliyo bora. Katika hayo maeneo ambayo yanapata mawasiliano ya *digital* bado mawasiliano hayo kweye *television* yanaharibika mara kwa mara kinyume na mategemeo ya wananchi kuwa watapata mawasiliano yaliyo safi.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa kuna tatizo gani la mawasiliano kwenye *television* hukatika mara kwa mara. Ninaomba Serikali inieleze matatizo hayo yataondoka lini?

Mheshimiwa Spika, nchi haiwezi kuendelea bila ya utafiti na baada ya utafiti kupatikana matokeo yake yanaweza kufanyiwa kazi. Ni jambo la kusikitisha kuwa nchi yetu fedha za kufanyia utafiti ni chache mno wakati inavyotakiwa angalau asilimia moja ya Pato la Taifa fedha zake ziende kwenye utafiti, bahati mbaya hali sivyo ilivyo. Ni lini Serikali itahakikisha asilimia moja ya Pato la Taifa fedha yake inatumika katika utafiti?

Mheshimiwa Spika, ulimwengu wa leo unaongozwa na sayansi na teknolojia na tayari Waziri ameshasema kuwa kuna upungufu mkubwa wa wataalam wa sayansi, lakini bahati mbaya sana vyuo ambavyo vitatupatia wataalam hao fedha inayopelekwa kwenye vyuo hivyo ni kinyume na fedha inayoidhinishwa na Bunge. Je, katika hali hiyo kweli Serikali ina nia ya kutaka nchi yetu sayansi na teknolojia iwe ndiyo kipaumbele katika kuleta maendeleo katika nchi hii?

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ifanye marekebisho ili vyuo vyetu vipatiwe fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge.

**MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, wataalam pamoja na watumishi wote wa Wizara kwa kutekeleza majukumu yao vizuri, hususan kusambaza mawasiliano nchini (mawasiliano kwa wote).

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mpwapwa inayo majimbo mawili (Mpwawa yenyewe na Jimbo la Kibakwe). Kata zilizopata wazabuni wa kuunganisha mawasiliano tangu mwaka 2012/2013 Jimbo la Mpwapwa (Mjini) halimo katika awamu zote. Kata zilizopata mwaka 2013/2014 ni kutoka Jimbo la Kibakwe tu (Mlundizi, Wotta na Berege).

Mheshimiwa Spika, Kata ambazo hazina mawasiliano kabisa katika Jimbo la Mpwapwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kaya ya Matomondo katika vijiji vya Tambi, Wembule, Mwenzele, Mbori, Makutupa.

(ii) Kata ya Mima katika vijiji vya Mina, Sazima, Igoji, Chamanda na Iwondo.

Mheshimiwa Spika, naomba Kata hizi mbili za Mtomondo na Mina zenye vijiji nilivyovitaja vipewe kipaumbele ya kwanza kwa kuzingatia muda mrefu umepita tangu mwaka 2012/2013. Kata hizi mbili hazina mawasiliano kabisa, hivi sasa. Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho yako lisemee hili.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara hii kwa kuweka mfumo wa mawasiliano kwa kuwekewa mtandao wa *post global* katika Jimbo la Mpwapwa. Mheshimiwa Waziri mfumo huu wa mawasiliano ni mpya, bado elimu itahitajika katika maeneo au ofisi zilizowekwa mtandao, je, Jimbo la Mpwapwa mtandao huu umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alielezee Bunge wakati wa majumuisho kuhusu *post global* ni huduma gani?

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nawapongeza kwa kazi nzuri Waziri na Naibu Waziri, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, kilio changu ni kuhusu ukosefu wa mawasiliano kwenye Kata ya Zirai, Tarafa ya Amani, Wilaya ya Muheza. Pia tunaomba minara Wilayani Muheza ikiwezekana Vodacom na Airtel, tulionao ni wa Tigo tu.

Mheshimiwa Spika, naomba majibu ya kilio changu.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni suala la mitandao, hakuna maadili kabisa, kwenye *facebook,* utakuta uchafu mwingi sana. Naomba Wizara ilifanyie kazi suala hili.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, nimepitia orodha ya Kata zisizo na mawasiliano ya simu Tanzania nzima na kugundua Kata zote zilizo katika mpaka wa Tanzania na Malawi kandokando ya Ziwa Nyasa hazina mawasiliano ya simu kabisa wakati Wizara hii inajitahidi kusambaza huduma hii katika nchi nzima, lakini ni pamoja na maombi ya muda mrefu kwa Mawaziri wote kuhusu umuhimu wa kupeleka mawasiliano mpakani.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji unaelekezwa zaidi katika maeneo yanayofikika kwa magari na kuziacha Kata ambazo ni tishio kiusalama kama Kata za Lupingu, Lifuma, Makonde, Kilondo na vijiji vyake vyote, sehemu ambazo wakati wa mgogoro na nchi jirani na Malawi wanakuwa wa kwanza kupata matishio ya kiusalama.

Mheshimiwa Spika, hawana mnara wa mawasiliano hata ya barabara, hivi Wizara ina malengo gani kwa maeneo haya? Ikumbukwe kwamba maeneo yote hayana mvuto wowote wa kiuchumi, hata iweje ni lazima Serikali isaidie kusukuma.

Namuomba Waziri au Naibu wake watembelee wenyewe wakajionee hali ilivyo mbaya. Hata usafiri unaotumika hivi sasa wa mashua *(boats)* hauna uhakika hata kidogo, kwa kweli inasikitisha. Kama Mawaziri wangekuwa wamefika Ziwa Nyasa (mwambao) naamini wangeziweka Kata hizi katika mpango wa awamu ya kwanza 'B' kwa mwaka 2014 badala ya Luduga na Madope ambako kunafikika kwa usafiri wa magari.

Mheshimiwa Spika, nitakachotaka kufahamu wakati Waziri anajibu hoja baadaye aeleze je, ni lini basi Kata nne na vijiji vyake nilivyovitaja hapo awali vitapata huduma ya simu chini ya mpango wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maombi hayo na maelezo yake naunga mkono hoja hii na nawatakia kazi njema kwa mwaka 2014/2015.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na hongereni sana kwa kazi nzuri Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa sekta ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kodi katika sekta ya mawasiliano, Wizara ipunguze kodi ya mawasiliano hasa *excise duty 17%* ambayo ni ya juu na huumiza ushindani na kukua kwa sekta ya mawasiliano *(growth)*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuweka fedha za kutosha katika utafiti, nchi yetu haitengi fedha za kutosha katika utafiti na maendeleo. Ni lazima tuwekeze angalau asilimia moja ya Pato la Taifa katika utafiti Serikali iliamua kutenga bilioni 30 kila mwaka, lengo hili litekelezwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu minara ya mawasiliano, tunashukuru kwa mpango wa kujenga mnara katika Kata ya Mkalama, Wilaya ya Pangani.
Bado tunahitaji minara ya mawasiliano katika vijiji vya Kigurusimba, Mrozo/Kituro na Ubangaa.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri asubuhi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa nitoe kilio changu kwa Wizara hii kuhusu matatizo makubwa ya kutokuwa na mawasiliano kabisa katika Kata zote za Delta yaani Kisingononi, Mbuchi, Maparoni na Salale. Kwa kifupi tu ni kuwa Kata hizi kwa kiasi kikubwa wakazi wake ni wavuvi na huvua sana samaki aina ya kamba na wengineo mawasiliano kwao ni kitu cha muhimu sana kwa ajili ya kutafuta masoko. Naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia wananchi hao zaidi ya 30,000 kuwasaidia kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, katika Kata za Dimani, Mchukwi na Mwambao nazo pia hazina mawasiliano ya simu. Umetimia muda sasa wa kuweza kuboresha mawasiliano katika Kata hizi ili wananchi waweze kuwasiliana kwa madhumuni mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nipongeze Wizara na Waziri pamoja na Naibu wake kwa kuchapa kazi kwa bidii na uzalendo wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, niombe Wizara iharakishe uwekaji wa *video conference* haraka sana kwa upande wa Zanzibar.

Kuhusu *TTCL* ningeshauri Serikali kuharakisha mipango ya kumalizana na mbia wa *TTCL* ambaye imeonekana dhahiri kuwa ni mbabaishaji na si mwekezaji ili shirika limilikiwe kwa asilimia mia moja na Serikali ili liwezeshwe na kuweza kuingia kwenye ushindani wa kibiashara kama makampuni mengine ya

simu yanavyoweza kuendesha biashara hii kwa faida kubwa na kuweza kuchangia Pato la Taifa.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Korogwe Vijijini kuna matatizo mengi ya mawasiliano, nimetoa taarifa kwenye Bunge hili toka mwaka 2011 hadi leo hakuna muafaka wowote. Katika mwaka 2012 mwezi wa Juni nilienda na Naibu Waziri wa Mawasiliano Mheshimiwa Charles Kitwanga hadi Kata ya Kizara na kampuni ya Airtel na kuahidi Kata hiyo ikifika mwezi wa 12 mwaka 2012 itakuwa mnara umefungwa katika Kata ya Kizara.

Katika ratiba ya maeneo yatakayopata mawasiliano Kata ya Kizara haimo kwa nini hadi leo na pia kuna vijiji vya Kigwasi, Kata Mashewa na Usambara Kata ya Chekelei hadi leo vijiji hivi havina mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atakapojibu maswali yake anieleze kuwa hii ahadi ya Serikali ya kupatia vijiji hivyo mawasiliano yatakamilika lini, kwani wananchi wamesubiri kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali inijibu suala hili ambalo limechukua muda mrefu.

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, sasa umeme unakuja Jimbo la Igalula, TEHAMA mashuleni sasa ije shule zote za msingi na sekondari katika Kata zote kumi. *Education* ni muhimu sana si kwa *IT* tu, lakini pia kwa kufundishia masomo ya sayansi, fizikia, kemia, baiolojia, hisabati na jiografia, uelewa mpana na ufaulu utaongezeka.

Mheshimiwa Spika, *Business Parks* kwa *IT* vitawezesha ajira nyingi kuongezeka kwa ku-*outsource* wateja Marekani, Ulaya, Australia na New Zealand hasa Mkongo wa Taifa ikifika Wilayani na Katani hivyo hakuna uhitaji waajiriwa kuja mijini kama umeme na mawasiliano huduma zikifika vijijini. Mtu anaweza kufanya kazi hata akiwa nyumbani kwake ili mradi ana kompyuta.

Mikoa ya Pwani mwa Bahari ya Hindi pamoja na Unguja na Pemba ina nafasi kubwa *(Indian Ocean Rim)* ya biashara ya TEHAMA kama zilivyo Jamaica, Indonesia, Malaysia, Singapore, Porto Rico, *Dominican Republic* na kwingineko ambako wanafaidika pia katika *IT Hardware/Software Assemblies* ambako vijana wengi wanakuwa *outsourced* na makampuni makubwa ya Magharibi, *HP, IBM, Microsoft*, kampuni za simu, *Nokia, Samsung*.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa majini (baharini) ni rahisi kuleta malighafi Tanzania na kutuma bidhaa funganishwa *(assembled products)* kwenye masoko duniani. Elimu ya TEHAMA tuanze tangu shule za msingi kupata vijana walio tayari na weledi mkubwa ili waajiriwe kirahisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfuko wa mawasiliano kwa wote Jimbo la Igalula, napongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Mfuko kwa Ujenzi wa Minara ya Miyenze/Lutende na Loya, ninaamini mwezi Julai, 2014 yote miwili itawashwa, ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Kata/Vijiji vifuatavyo pia vipate mawasiliano:-

(1) Kata ya Goweko, Kijiji cha Kamama, hakina mawasiliano kwa 10%.

(2) Kata ya Kigwa, Kijiji cha Nzigala, hakina mawasiliano kwa 21%.

(3) Kata ya Miswaki, Kata ya Igudi, hakina mawasiliano kwa 60%; Kijiji cha Kalangale, hakina mawasiliano kwa 88%;Kijiji cha Mdalaigwa, hakina mawasiliano kwa 100% na Kijiji cha Miswaki, hakina mawasiliano kwa 32%.

(4) Kata ya Miyenze, Kijiji cha Idekamiso, hakina mawasiliano kwa 100%; Kijiji cha Miyenze, hakina mawasiliano kwa 100%; Kijiji cha Nyankombe, hakina mawasiliano kwa100% na Kijiji cha Songambele, hakina mawasiliano kwa 100%.

(5) Kata ya Nsolo, Kijiji cha Ntalasha, hakina mawasiliano kwa 47%.

(6) Kata ya Tura, Kijiji cha Karangasi, hakina mawasiliano kwa 43%; Kijiji cha Munyu, hakina mawasiliano kwa 100%, Kijiji cha Mwamlela, hakina mawasiliano kwa 100%; Kijiji cha Nkongwa, hakina mawasiliano kwa 100% na Kijiji cha Tura, hakina mawasiliano kwa 33%.

(7) Kata ya Kizengi, Kijiji cha Mwakadola, hakina mawasiliano kwa 100%.

**MHE. DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa - Waziri, Mheshimiwa January Makamba, Naibu Waziri, Profesa Patrick Makungu - Katibu Mkuu, Wakuu wa

Idara na watumishi wa Wizara, Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu na watumishi wa taasisi zilizo chini ya Wizara kwa mafanikio walioyapata katika mwaka 2013/2014.

Natoa wito kwao kuwa waendelee na mshikamano na jitihada hizo ili kuweza kufikia malengo yote waliyowekewa na Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mawasiliano naipongeza Wizara na *TCRA* kwa ubunifu uliowezesha ujenzi wa *Telecom Traffic Monitoring System (TTMS)* kwa kushirikiana na sekta binafsi ambao utawezesha Serikali kufuatilia mawasiliano ya ndani na nje ya nchi. Ubunifu wa aina hii uendelezwe katika nyanja nyingine ili kuharakisha utekelezaji wa mipango ya kueneza mawasiliano nchini na kuboresha upatikanaji wa huduma.

Kwa mfano udhibiti wa vifaa (kama simu) visivyo na ubora unahitaji maabara ya kupima kama Serikali/*TCRA* haina fedha za kutosha basi ishirikishe sekta binafsi kujenga maabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *number portability,* ushindaji wa kweli baina ya watoa huduma za mawasiliano ya simu utafikiwa pale watumiaji wa huduma watakapokuwa na uhuru wa kuhama kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine bila kupoteza namba zao na hivyo kuendelea kuwasiliana bila tatizo. Katika mipango ya maendeleo ya sekta *number portability* ilikuwa ajenda muhimu. Naomba Serikali iwajulishe Watanzania hatua iliyofikiwa katika uanzishaji wa huduma hiyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masafa, naipongeza sana Serikali kwa kuwa moja ya nchi za kwanza Afrika kutekeleza uamuzi wa kubadili teknolojia ya utangazaji kutoka analojia kwenda *digital.* Naamini kuwa hatua hiyo itatuwezesha kupata masafa ya kutosha kupanua wigo wa mawasilianio ya simu. Hata hivyo nimekuwa na maoni kuwa bei ya masafa ambayo ndiyo nyezo muhimu sana katika mawasiliano haijapewa thamani inayosatahili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa hii ni rasilimali adimu nashauri kuwa Serikali kupitia *TCRA* ipitie upya bei ya masafa ili kuhakikisha kuwa Taifa linanufaika na rasilimali hiyo. Aidha, nashauri kuwa pamoja na *TCRA* kushiriki *study groups* za *ITU* ianzishe utafiti juu ya uwezekano wa kutumia masafa ambayo bado yanaonekana kutokuwa na mahitaji. Vilevile tufanye uthamini wa masafa yetu ili tujue thamani yake kama ilivyo kwa rasilimali nyingine zisizohamishika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Posta, utekelezaji wa mradi wa anwani za makazi ni simbo za Posta unaweza kuharakishwa kwa Serikali kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kushiriki katika utekelezaji. Kwa maoni yangu

wananchi/wakazi wanaweza kulipia gharama za kuweka namba kwenye majengo yao, kuchangia gharama za kuweka vibao kwenye mitaa yao na kadhalika.
Hii itapunguza gharama kwa Serikali na kufanya mradi huo kuwa wa jamii badala ya kuwa wa Serikali na *TCRA*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubora wa huduma za mawasiliano, hivi karibuni ubora wa huduma za mawasiliano ya simu umekuwa ukipungua kwa karibu mitandao yote. Nashauri Serikali kupitia mdhibiti wa mawasiliano ifuatilie na kuhimiza watoe huduma kurekebisha upungufu uliojitokeza ili wananchi wapate huduma bora.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utafiti, nampongeza sana Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH kwa jitihada anazofanya kuimarisha shughuli za utafiti nchini. Taifa letu limekuwa likitegemea matokeo ya utafiti unaofanywa na wanasayansi wa nchi nyingine kwa maendeleo yake. Utegemezi huo umekuwa na athari kubwa kwani mazingira yalikofanyikia utafiti ni tofauti na mazingira yetu na hivyo kufanya baadhi ya matokeo hayo yasifae kwa mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, ili kukuza utafiti na uwezo wa wataalam wetu, nashauri kuwa Serikali ithamini utafiti. Hiyo iambatane na kutengewa fedha za kutosha na kuhakikisha kuwa kiasi kilichotengwa kinatolewa kwa wakati ili taasisi zote zenye jukumu la kufanya utafiti katika sekta mbalimbali ziweze kufanya hivyo. Tukumbuke kuwa hata kama tunayoandikia ilipatikana kupitia utafiti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Ufundi Arusha, chuo hiki chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Richard Massika kimekuwa kikifanya kazi nzuri sana ya ubunifu wa teknolojia ikiwemo umwagiliaji na nyinginezo ambayo imenufaisha sana jamii. Ili kukuza ubunifu huo nashauri kuwa wahadhiri na watumishi wote wanaoshiriki katika utafiti wenye mafanikio watunzwe. Aidha, chuo kiongezewe fedha ili waweze kuhawilisha teknolojia hizo kwa wananchi kwa madhumuni ya kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na narudia kusema kuwa naunga mkono hoja.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kumshukuru Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha nami niweze kuchangia katika hotuba ya bajeti hii ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ya mwaka wa fedha 2014/2015. Vilevile nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa kuandaa bajeti yao nzuri na yenye kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano, sayansi na teknolojia ni vitu vinavyoshahabiana na ni muhimu katika maendeleo ya Taifa lolote lile duniani. Ingawa mfumo mzima wa teknolojia tokea uingie duniani umepunguza nafasi za ajira kwa wananchi wengi katika mataifa mbalimbali, lakini hatuna budi kubadilika na kwenda na jinsi dunia inavyokwenda. Hapa kwetu athari hizo pia zilitokea baada ya mfumo huo kuingia nchini.

Naiomba Serikali kutilia mkazo katika kukuza tekenilojia nchini ili tupate wataalam wa kutosha ambao watatuletea mafanikio katika fani hiyo. Serikali iwekeze zaidi katika vyuo vya teknolojia ili tuweze kuzalisha wataalam zaidi kila mwaka, kwani hivi sasa ukilinganisha idadi ya vyuo hivyo bado hailingani na mahitaji halisia kwa nchi yetu. Ingefaa zaidi vyuo hivi viwepo kila mkoa kwani mikoani kuna vijana wenye vipaji na uwezo mkubwa katika fani hizo pale tu wakiwezeshwa kwa kupatiwa elimu nzuri basi watasaidia Taifa hili kupiga hatua kubwa sana katika sekta nzima ya teknolojia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tumekuwa na takwimu ndogo sana katika fani ya ugunduzi wa teknolojia hivyo basi naishauri Serikali kuweka mkakati katika hili kwani kuna vijana wengi wamegundua mambo mbalimbali lakini wamekosa fursa ya kuendelezwa ili kuleta tija kwa Taifa letu, naomba tuige mifano katika nchi zingine zilizoendelea kwa kuwaendeleza wagunduzi wao katika fani ya teknolojia na kuwaletea faida kubwa kama nchi.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano hivi sasa yamekuwa si anasa kama ilivyokuwa hapo awali, tukianzia mawasiliano ya simu, mitandao ya kompyuta na kadhalika. Tukianzia mitandao ya simu hivi sasa wananchi kumiliki simu mbili au tatu ni jambo la kawaida kwani mitandao hii imekuwa na msaada mkubwa katika kuleta maendeleo nchini na kwa mtu mmoja mmoja. Kutokana na huduma za mitandao hii imetoa ajira kwa wananchi mbalimbali na hivyo kupunguza suala zima la tatizo la ajira nchini. Hii yote ni faida ya mawasiliano, hivi sasa wananchi wamerahisishiwa huduma nyingi zinapatikana kwenye simu za mikononi, huduma za kifedha, huduma za kununua bidhaaa mbalimbali pia hupatikana hivyo hata wale wananchi ambao hawana akaunti za kibenki wamekuwa wakipata huduma hizo katika simu zao za mikononi.

Hata hivyo kila jambo huwa lina changamoto zake na ndiyo ilivyo pia katika sekta hii. Kuna baadhi ya watu wamekuwa wakitumia vibaya mawasiliano ya simu za mikononi kwa kujisajili kwa kutumia majina ya uongo ili wasijulikane, hivyo kusababsha dhana nzima ya usajili wa namba za simu kuwa hauna tija kwa kiasi fulani. Naishauri Serikali kuangalia kwa namna nyingine ni jinsi gani wataweza kudhibiti hali hii. Umuhimu wa mawasiliano nchini hivi sasa

umezidi kukua hivyo basi hakuna budi kwa Serikali sasa kutilia mkazo suala zima la kuhakikisha yale maeneo yote ambayo mawasiliano yamekuwa magumu, hayapatikani kabisa au *network* kusumbua yashughulikiwe ipasavyo ili wananchi wa maeneo hayo waweze na wao kupata huduma hiyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, Jimboni kwangu nami kumekuwa na tatizo la mawasiliano kwa baadhi ya maeneo. Hali hiyo imegeuka kuwa kero kwa wananchi wangu na hivyo kuwafanya kukosa kabisa mawasiliano ambayo ni haki yao ya msingi kwa wakati wote, maeneo hayo pia niliyazungumzia katika Bunge lililopita na kuiomba Serikali kuyaangalia katika namna ya kipekee ili mawasiliano yaweze kupatikana kwa wakati wote. Maeneo hayo ambayo bado yamekuwa na tatizo la kutokuwepo kwa mawasiliano ni:-

(i) Kata ya Magindu, Lukenge, Miombo, Mkonga, Mzizima, Gwata, Gumba na Kigoda, Kata ya Soga, Vikuge, Ngoingo, Misufini, Kipangege, Boko, Mnemela, Mpiji, Mkarambati na Kibaoni;

(ii) Kata ya Ruvu, *Ruvu Station,* Minazi Mikinda, Mnazi Lubungo na Kitomondo; na

(iii) Kata ya Kwala, Dutumi, Madege, Mwembe Ngozi, Msua, Mpera Mumbi na *Kwala Station.*

Mheshimiwa Spika, maeneo hayo yana matatizo makubwa ya mawasiliano kwa muda mrefu sasa, hivyo naiomba Wizara kwa mara nyingine tena kuyatafutia ufumbuzi ili wananchi waweze kupata mawasiliano kwa wakati wote, vivyo hivyo waweze kuyatumia katika kujiingizia kipato kwa kufungua miradi midogo midogo ya huduma za kifedha zinazotolewa na makampuni hayo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mazingira ya nchi yetu katika suala zima la nishati ya umeme maeneo ya vijijini, kuna baadhi ya Watanzania wameweza kutumia vipaji vyao kwa kugundua vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme. Wananchi hao wamekuwa wakiachwa ili hali wana uwezo mkubwa wa ubunifu katika sekta nzima ya teknolojia hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuweka utaratibu wa kuwajali wagunduzi wa aina hii si kwa umuhimu wao bali ni kutokana na kwamba ubunifu wao unasaidi kutatua kero kubwa inayoikabili Serikali katika sekta nzima

ya nishati ya umeme, wabunifu hawa Wizari ingewawezesha kwa kuwaendeleza ili kuweza kufanya ubunifu wa kisasa zaidi unaoendana na teknolojia ya sasa tofauti na ubunifu wao wanaoufanya sasa hivi wakitumia vifaa duni lakini vinaleta tija.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya wabunifu hawa wameweza kujikwamua kiuchumi kutokana na ubunifu wao huo wa kiteknolojia kwa kutoa huduma kwa wananchi wengine, hii ni mifano mizuri ambayo hata katika nchi zilizoendelea kuwachukua watu kama hawa na kuwaendeleza kwa manufaa ya nchi. Tanzania tumebarikiwa sana kuwa na vipaji, hivyo Wizara haina budi kufanya tafiti za kutosha na kuchukua hatua thabiti ili kuviendeleza vipaji hivyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyozungumza hapo awali kuhusu suala zima la kuwawezesha watu wetu katika fani nzima ya sayansi, Wizara inaweza kushirikiana na sekta nyingine za Serikali katika kuweka mikakati mizuri ambayo baadaye itatupatia wanasayansi wengi ili wakidhi mahitaji, hivi sasa kuanzia mashuleni vijana wetu wamekuwa wakikimbilia masomo ya sayansi na hivyo kutokupata wahitimu wa kutosha katika fani hiyo.

Vilevile nichukue fursa hii kuipongeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* kwa kazi nzuri inayoifanya, ingawa wamekuwa wakikutana na changamoto mbalimbali lakini wamekuwa wabunifu katika utendaji wao kazi wa kila siku.

Hata hivyo napenda kuipongeza mamlaka hii pia kwa hatua kubwa waliyofikia ya mafanikio ya awamu ya kwanza ya matumizi ya dijitali na hivi sasa kupelekea kuingia awamu ya pili ya uzimaji wa mitambo ya analojia ambayo awamu hii itakamilisha awamu mbili na hivyo kubakiza awamu ya mwisho itakayopelekea nchi nzima kutumia mfumo wa dijiti.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kuwapongeza kwa kuzindua mtambo wa kuhakiki takwimu za mawasiliano yaani *Telecommunication Traffic Monitoring System,* hiyo ni hatua nzuri na ya mafanikio kwa Taifa letu, kwani duniani ni teknolojia ambayo inatumika ili kusaidia Serikali kupata mapato.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kugusia kidogo masuala yanayotokea katika mitandao, imekuwa ni kawaida kwa wananchi wetu kutumia mitandao hii katika njia ambazo hazina tija. Wizara ina jukumu kubwa kupitia wataalam wake kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi kuweza kutumia uhuru huu wa mitandao kama fursa ya kujiendeleza, kupata maendeleo, kujikwamua kiuchumi na kujielimisha. Duniani kote katika nchi zilizoendelea wamekuwa wakitumia sekta hii kama fursa pekee katika kuleta maendeleo katika nchi zao, lakini hapa kwetu imekuwa ni tofauti kabisa kwani watu wamekuwa wakitumia

mitandao hii kupotosha, kutukana na kufanya mambo yasiyofaa katika jamii na hata wakati mwingine kuweka picha zisizofaa na hivyo kupelekea kuporomoka kwa maadili.

Kwa hali ilivyo ni wajibu sasa wa Wizara kupitia sekta husika kuanza kuelimisha wananchi kuona mitandao hii ni fursa kwao ya kujiletea maendeleo na hata na kuacha kuitumia tofauti, kwa mfano sasa hivi kuanzisha *blogs* imekuwa ni kitu cha kawaida na kumekuwa na *blogspot* nyingi sana, hii inatokana na *blogspot* haina gharama yoyote kuirusha hewani, kikubwa kinachohitajika ni ubunifu wako tu wa kuitengeneza katika njia iliyokuwa rahisi sana.

Hivyo basi kutokana na utaratibu huo mamlaka husika inaweza kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi wenye uwezo wa kufanya hivyo sana sana kwa wale vijana wetu ambao wamemaliza elimu zao na hawajabahatika kupata kazi kutengeneza *blog* hizi na kujiingizia kipato kidogo na hivyo kuondokana na tatizo la ajira kwa kiasi fulani. Unawezaje kujiingizia fedha kidogo kulipa *blog*?

Mheshimiwa Spika, kuna makampuni megi sana yanahitaji kujitangaza hapa nchini, hivyo wanatafuta watu wanaoweza kutangaza bidhaa zao kupitia wao, mfano mdogo ni kwamba ili uweze kuyapata makampuni haya ni lazima kwenye *blog* yako iwe na uwezo wa kutembelewa na watu mia mbili na zaidi kwa siku, ukiweza fikisha idadi hiyo basi inakuwezesha kuingia mikataba na makampuni hayo.

Naiomba Wizara kutumia fursa hii ipasavyo kwa kuwapa elimu ya kutosha vijana wetu kuweza kutumia njia hii na kujiingizia kipato, kwani kuna baadhi ya wananchi ambao tayari wananufaika na fursa hii kwa kupata kipato. Teknolojia, sayansi na mawasiliano kuna fursa nyingi sana ambazo zipo wazi kabisa, bahati mbaya iliyopo hapa nchini kwetu ni kwa wataalam wetu kutokuwa wabunifu na kuweza kutoa elimu kwa vijana wetu na baadhi ya vijana wetu kutoweza kujengwa toka wakiwa vyuoni kuziona fursa katika sekta hizi muhimu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nami nitoe mchango wangu katika Wizara hii kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kuhusu kusimamia sera ya posta na mawasiliano ya simu ni muhimu sana. Nikianza na posta zilizopo hapa nchini imeanza kuzorota kwani

huduma yake haiendi sawa na zamani kwani majengo hayo yamekuwa kama ya mtu binafsi.

Mheshimiwa Spika, suala la simu, kwa kweli mawasiliano ni muhimu sana kwa matumizi ya nyumbani, kazini na hata kwa biashara, naomba nitoe pendekezo langu hapa ili nipate ufafanuzi kama litafaa litumike.

Mheshimiwa Spika, pendekezo hizi simu ziangaliwe upya, matumizi yake hayatenganishwi kwani wengine ni kuwapunja wananchi. Napenda simu za ofisi, Mashirika na wafanyakazi katika muda wa maongezi upewe angalizo la bei na wananchi wakulima ni vema pia ikatengwa muda na kiwango cha fedha yake ya maongezi maana simu zimekuwa zikiiba hasa pale unapoongeza salio hata ukijiunga pesa inaonekana imeisha kabla ya maongezi.

Mheshimiwa Spika, katika kusoma taarifa ya maendeleo ya shughuli za maendeleo ya shughuli za Mfuko wa Mawasiliano kwa wote hadi Aprili, 2014.

Mheshimiwa Waziri, Mkoa wa Dodoma una Wilaya 11 na inahitaji mawasiliano katika mgao wenu mmeipunja sana Wilaya ya Kondoa Mjini, hatuna mawasiliano hasa Kata ulizotaja na ambazo hukutaja, mfano Kondoa – Chemba nimewapatia, Chemba, Gwandi, Lalta Ovada, Mpendo, Sanzawa, Kondoa Mjini na Kwadelo tu.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza "B" nimeona Kondoa, Itambi, Kikilo, Kikore, Kingare, Mnenia, Busi, Changaa, Hondomairo, Bumbuta, Itaswi, Kalamba, Kisese, Serya, Thawi.

Mheshimiwa Spika, naomba angalau mawasiliano hata kama mtandao mmoja tu inatosha angalau wapate mawasiliano hasa ukiangalia sera ni karibu mno na Kondoa Mjini haina mawasiliano ikifuatiwa Kata ya Changaa na vijiji vyake hata hapo tu Tumbelo wanapochimba madini hakuna mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi ya Wilaya hii haina mawasiliano ya kutosha nikiorodhesha ni kama Wilaya nzima tu niombe hata mpeleke Thawi, Kikilo, Changaa, Hondomairo, Busi, Pahi, Bumbuta na kama Waziri unavyofahamu tuna kuomba wananchi wa Kondoa kwa niaba yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii ila iongezewe pesa za kutosha ili ikamilishe maeneo yote kwani ni muhimu sana Wizara hii hivyo kuipa fedha kuduchu ni kuendelea kuyafuja maendeleo ya wananchi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Waziri na Naibu Waziri wake kwa kazi ngumu na yenye umuhimu.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii na kumpongeza Waziri - Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa na timu yake kwa namna wanavyotekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo ningeomba Wizara hii ni kuboresha mawasiliano ya simu makao makuu ya Wilaya ya Wangingo'mbe pale Igwachanya.

Sehemu ile hakuna mawasiliano ya uhakika mpaka upande kwenye mlima au mti mrefu, hata hivyo ni kwa taabu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii ichukue hatua mara moja katika bajeti ya mwaka 2013/2014 Waziri alitoa ahadi ya kupewa minara miwili lakini hadi leo sijaona utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Waziri wakati atakapohitimisha hotuba yake anijibu ni lini ataweka mnara Igwachanya na Saja kama alivyoahidi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningeshauri Wizara hii ichukue hatua ni pale makampuni ya simu hulazimisha ku-*charge* mteja bila idhini yake, kuingiza nyimbo za milio ya simu.

Mheshimiwa Spika, wametoa ujumbe kuwa umeingiziwa nyimbo fulani na kwa gharama fulani.

Mheshimiwa Spika, naomba makampuni haya yachukuliwe hatua kwani wanawaonea sana wateja wao na sijui kama Serikali inapata kodi yake kwenye huduma ya aina hii.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa Mnyaa (Mb) Waziri na Mheshimiwa January Makamba (Mb) Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa kazi nzuri sana na hotuba nzuri ya bajeti. Nampongeza pia Katibu Mkuu na wafanyakazi wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa utekelezaji wa Mkongo wa Taifa na faida ambazo tunaendelea kuzipata nchini, simu kushuka bei, mawasiliano kujengeka mjini na kuelekea vijijini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara kwa kutujengea minara miwili katika eneo la Nyumba ya Mungu, Kata ya Lang'ata na namna mnara mwingine katika eneo la Jipe - Ndea Kata ya Jipe inayopakana na nchi ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, bado lipo eneo kubwa la Kata ya Ngujini eneo la Kisangara juu ambalo halina mawasiliano ya simu. Naiomba Wizara iwasaidie Wilaya ya Mwanga kukamilisha kazi nzuri waliyoianza kwa kujenga mnara wa simu katika Kata ya Ngujini.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani zangu.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wao wote kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutujengea mnara katika Kata ya Tomunguo, wananchi wanashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, aidha ninaomba sana Wizara isaidie kutujengea minara katika Kata za Matuli na Mkulasi kuwepo na mawasiliano utasadia sana kuokoa maisha ya akina mama wajawazito kwani zanahati zinapiga simu makao makuu *ambulance* kila itokeapo dharula ya uzazi. Vilevile shughuli nyingi za kiuchumi zinategemea sana kuwepo kwa mawasiliano ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Wizara hii iangalie uwezekano wa kuwashauri wamiliki wa mashirika ya simu kwamba utekelezaji wa *corporate responsibility* uonyeshe sura ya kitaifa zaidi, maana yake ni kwamba watengeneze misaada ya kijamii kwa uwiano, Watanzania wote wanatumia huduma zao.

Mheshimiwa Spika, naomba kulikaribisha Shirika la Posta kutoa huduma za kiposta na kibenki katika makao makuu ya Halmashauri ya Morogoro yaliyopo Mvuha. Viwanja vya kujenga ofisi vipo vingi tu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja.

Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa kufanya kazi nzuri katika mazingira magumu ya bajeti finyu.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu nimeeleza kwamba Wilaya ya Ngara inapakana na nchi za Rwanda na Burundi nchi ambazo mipaka yake na Tanzania haikutulia hasa Burundi ambako wapinzani wa Serikali ya Rais Nkurunziza wameweka makazi yao katika milima ambayo inapakana na Wilaya yangu ya Ngara.

Katika hali hiyo kunahitajika usikivu mzuri wa simu ili wananchi wa Ngara wanaoishi mpakani waweze kutoa taarifa kwa polisi mara waonapo matukio ambayo siyo ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, nimeshaleta orodha ya vijiji muhimu vya mpakani ambavyo havina minara tangu mwaka 2011 lakini mpaka sasa Wizara haijafanya lolote kuhusu kuweka minara.

Mheshimiwa Spika, naomba niorodheshe tena vijiji ambavyo havina usikivu kabisa, vijiji vya Nyakisasa, Bukiriro, Muganza, Mabawe, Ntobeye, Mbuba na Keza.

Mheshimiwa Spika, tafadhali sana naomba muifanye Wilaya ya Ngara kuwa a *priority district*.

Mheshimiwa Spika, nawatakia kila la heri.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kusoma hotuba yako vizuri, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, suala la mawasiliano ya simu za mkononi ni muhimu sana nchini kote kwa wakulima, wavuvi, wafugaji, wafanyabiashara, viongozi na wapiga kura na wote wanahitaji simu katika karne ya 21. Tunaiomba Serikali, mfuko wa pamoja wa *YUCAF* wa simu vijijini uanzie kutumika katika mikoa ya pembezoni.

Mheshimiwa Spika, hapa ninazungumzia Mkoa wa Lindi na vijiji vyake ni pembezoni sana, Lindi Vijijini mpaka sasa hakuna simu za mkononi baadhi ya sehemu. Vijiji ambavyo havina minara Lindi Vijijini ni Mvuleni, Kijiweni, Mipingo, Kiwawa, Rutamba, Milola. Matimba, Kilolambwani na Namkongo.

Mheshimiwa Spika, Lindi Mjini mitaa ambayo haina minara ni pamoja na Kihwetu, Mbauja, Likong'o, Tandangongoro, Narunyu, Nandambi na Mkanga.

Mheshimiwa Spika, vijiji hivi vya mijini ni kioo cha mkoa, tunaomba mawasiliano.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, suala la mawasiliano ni muhimu kwa maendeleo ya nchi na watu.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano huokoa vifo vya mama na mtoto na watu kwa ujumla, hupunguza umaskini kwa kutumia muda mchache kufuatilia

masuala mbalimbali, pia kupunguza wananchi waliozoea kuweka hela ndani na huzihifadhi simu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa lakini bado kuna Watanzania bado wanaishi kama wakati wa ujima, mfano Mkoa wa Morogoro zipo Wilaya, Kata, Vijiji ambazo hazifikiki kwa barabara wala treni, mfano Wilaya ya Kilombero katika Kata ya Tanganyika Masagati na vijiji vyake hakuna mawasiliano ya barabara wala simu, hakuna mawasiliano ya barabara wala simu, pia Kata ya Uchindile na vijiji vyake hakuna mawasiliano hata ya barabara na hata treni ya *TAZARA* ambayo ndiyo usafiri pekee unaopita katika Kata hiyo iliyopo Wilaya ya Kilombero.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kuangalia kwa jicho la karibu na uharaka kupeleka mawasiliano katika kata hizo za Uchindile na Tanganyika Masagati. Ni matumaini yangu mtachukua hatua za haraka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na msisitizo wa Kata hizo mbili tajwa hapo juu, Wilaya ya Kilombero kwa miundombinu ya barabara ambapo ni mibovu na haipitiki kwa urahisi hivyo tegemeo kubwa ni mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi naomba niorodheshe maeneo ambayo yenye mitandao hafifu. Maeneo ambayo hayana mawasiliano kabisa katika Kata ya Masagati ni katika vijiji vya Ipinde, Tanganyika na Taweta; na katika Kata ya Uchindile ni katika vijiji vya Uchindile, Kitete pamoja na Lugala.

Pia katika Kata ya Kamwene ni katika vijiji vya Matema, Jaribu na katika Kata ya Chita hakuna mawasiliano katika vijiji vya Udagaji na Makutano.

Mheshimiwa Spika, Kata zenye baadhi ya mitandao *(Vodacom* na *Tigo)* ni katika Kata ya Chisano kwenye vijiji vya Chisano, Kifinye na Mgugwe, wakati katika Kata ya Mbingu mawasiliano hayapo kabisa katika kijiji cha Chiwachiwa. Aidha katika vijiji vya Londo na Vigaeni mawasiliano hayana uhakika.

Katika Kata ya Idete vijiji vya Kisegese na Namwawala (bado *Airtel*); Kata ya Mkula vijiji vya Msufini, Sole, Katulukila; Kata ya Kidatu katika kijiji cha Msolwa Station, hakuna; Kata ya Sanje katika vijiji vya Sanje na Miwangani.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ndiyo maeneo yenye shida ya mawasiliano pia katika Kata ya Mlimba katika kijiji cha Ngwasi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kupata majibu ya Serikali namna mashirika yanavyofanya kazi na kuleta usumbufu mkubwa kwa watumiaji huduma za kifedha.

Mfano mteja alituma fedha kwa jamaa yake toka tarehe 24/01/2014 hadi leo fedha haijamfikia, aliyetumiwa na aliyetuma hajarudishiwa na kumuacha anahangaika yeye binafsi alijitahidi kufuatilia akashindwa pia mimi nilimfuatilia hadi leo hakuna majibu na muamala wenyewe ni kama: *Trans ID; 14010584228499 you have received 200,000.00 Tzs from 255789189819 visit any airtel money outlets to withdraw Pin is 016308. You need to redeem the money in 7 days*."

Mheshimiwa Spika, mtumiaji jina lake ni Isaka Mzunda, alituma tarehe 24/01/2014. Naomba nijue ni lini atarudishiwa fedha zake? Ahsante.

**MHE. *CAPT*. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote niunge mkono hoja hii. Pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yale kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kusambaza mawasiliano ya simu hadi vijijini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ambazo hazina mawasiliano ya simu (Manyoni) napenda kuishukuru Wizara kwamba kata zangu mbili yaani Kata ya Makondo na Kata ya Senza ambazo hazina mawasiliano ya simu, zimewekwa katika awamu ya kwanza ya kupatiwa mawasiliano ya simu. Nasisitiza wakandarasi wa kujenga minara hiyo *(Vodacom)* waanze kazi haraka ili kumaliza kilio cha wananchi wa kata hizo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo awamu ijayo itumike kuimarisha maeneo ambayo hayajafikiwa na *network,* maeneo hayo ni Kata ya Majiri hasa kijiji cha Majiri, Mahaka na Mpandagoni, pia Kata ya Makulu hasa kijiji cha Hika na Ilaloo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya sayansi na teknolojia lengo la kutenga kila mwaka 1% ya pato ghafi la Taifa kwa ajili ya kugharamia shughuli za sayansi na teknolojia bado hadi sasa halijatekelezwa, hii ni habari mbaya.

Mheshimiwa Spika, ushauri kwa Serikali ni kwamba kwa kuwa maendeleo ya sayansi na teknolojia ndiyo ufunguo wa maendeleo ya kisasa katika sekta zote basi ni muhimu kabisa kuwekeza kwa kiwango kinacholingana na uzito wa suala hili.

Mheshimiwa Spika, fedha za utafiti zinazopitia *COSTECH* na kupelekwa kwenye taasisi mbalimbali za utafiti, nashauri pia zigawiwe kwa taasisi za utafiti za sekta ya ulinzi kama vile Kituo cha Nyumbu (Kibaha) na Kituo cha Mazao (Morogoro) kwani vituo hivi havipati fedha za utafiti kutoka COSTECH. Hii ni dosari ambayo inahitaji kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, mwisho narudia kusema kwamba naunga mkono hoja hii.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Waziri Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Naibu Waziri Mheshimiwa January Makamba, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote kwa kazi nzuri sana wanayofanya, tatizo linalowasibu ni uhaba wa fedha kwani takribani miaka yote wanapewa fedha kidogo ukilinganisha na majukumu waliyonayo. Naomba Serikali waipatie fedha Wizara hii ili itekeleze majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa kupeleka mawasiliano vijijini Jimbo langu la Singida Magharibi katika awamu ya kwanza vijiji katika Tarafa ya Sepuka yaani Mwaru, Mlandaga, Ufanang'ungira, Iyumbu na kadhalika wanatarajiwa kuwekewa minara na kampuni ya Airtel. Nashukuru kwamba Airtel wanaendelea na ujenzi wa minara na hadi sasa minara miwili inajengwa lakini bado wananchi wanalalamika mawasiliano sio mazuri na usikivu sio mzuri. Naomba wataalam wafanye marekebisho yanayohitajika ili usikivu mzuri upatikane.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha ni kuwa Kampuni ya Tigo iliyoshinda zabuni ya kupeleka/kujenga minara katika vijiji vya Mchintiri, Kinyampembee, Iglanson na vijiji vingine vya Tarafa ya Ihanja haijaanza kazi hiyo wakati walitakiwa kukamilisha kazi hiyo mwezi Machi, 2014. Wananchi wanauliza kumetokea nini, kwani wenzao wa Tarafa ya Sepuka wameshaanza kujengewa minara na Kampuni ya Airtel lakini Kampuni ya Tigo hakuna kitu, kulikoni?

Mheshimiwa Spika, kutokana na tatizo hilo la Tigo yupo kiongozi mmoja mpuuzi anaeneza *propaganda* kuwa mimi Mbunge nimesimamisha zoezi la kuwapatia minara/mawasiliano vijiji vya Muhintiri, Inglanson, Kinyampembee kujua kwa nini Tigo hawajatimiza kazi yao.

Naomba *UCAF* waongezewe fedha ii wakamilishe majukumu yao. Pia naomba Wizara ifuatailie wizi unaofanywa na makampuni ya simu ya Tigo na Voda.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. REBECA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Sayansi na Teknolojia ni Wizara muhimu sana katika kuharakisha maendeleo ya nchi yetu

endapo itatengewa fedha za kutosha na kutolewa kwa wakati ili kufanikisha miradi iliyo chini ya Wizara hii kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Msemaji wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa kwa hotuba aliyoiwasilisha. Aidha, Wizara iyachukue yote ya muhimu kwa ajili ya kufanikisha shughuli za Wizara. Aidha, nawapongeza pia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi zao za kila siku wanazozifanya bila ya bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Wizara hii ni kidogo sana. Jumla ya shilingi bilioni 67.2 ni fedha zitakazotosha miradi michache licha ya miradi mingi iliyo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, makampuni ya simu yanatakiwa kulipa *service levy,* kwa hivi sasa yanalipa moja kwa moja makao makuu Kinondoni. Napendekeza *service levy* ilipwe moja kwa moja katika Halmashauri zetu ili kuchangia maendeleo ya wananchi na mipango ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ngezeko la gharama za mawasiliano, Serikali ilipandisha tozo ili kupata fedha ya kupeleka umeme vijijini. Wananchi wanataabika, wengi hawana uwezo wa kulipia *voucher* wanabaki ku-*beep.* Serikali iangalie uwezo wa watumiaji na hivyo kwa kubadilisha *rate* iliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipanua eneo la Chuo Kikuu Mbeya cha Sayansi na Teknolojia (MUST) ili kupanua miundombinu ya taasisi. Katika mwaka wa fedha 2013/2014 fedha iliyohitajika kufidia wananchi ilikuwa shilingi bilioni 3.1 lakini hadi kufikia Machi 2014 ni shilingi bilioni 1.1 tu ilikuwa imetolewa, fedha iliyobaki itolewe yote. Serikali ilipe wananchi kuondoa usumbufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, ahsante.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa hii ya kuchangia katika Wizara hii.

Awali ya yote napenda kuwapongeza Mawaziri pamoja na hotuba makini ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, hakikika bila ya mawasiliano hakuna maendeleo na kama maendeleo hayapo ina maana umaskini utaendelea kuwa umetawala na kukithiri.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kutenga fedha ya kujenga mnara Biharamulo Mjini ambao utahudumia Kata za Ruziba, Bisibo, Nyarubungo na Biharamulo Mjini. Pamoja na kuwepo kwa mawasiliano toka mnara wa Airtel lakini natumaini sasa mawasiliano yatazidi kuimarika zaidi.

Pia napongeza taarifa ya maendeleo ya shughuli za mfuko wa mawasiliano kwa wote hadi Aprili, 2014. Kwa Jimbo la Biharamulo Magharibi jumla ya Kata tisa ambazo ni Bisibo, Kalenge, Lusachunga, Nemba, Nyabusozi, Nyakahura, Nyantekera, Nyarubungo na Ruziba zimetambuliwa kama nilivyoomba mwaka jana. Naomba juhudi za makusudi na makini kukamilisha kazi hiyo muhimu ya kuharakisha mawasiliano mazuri.

Naomba niongelee suala zima ambalo mwaka jana limejitokeza kwa kiasi kikubwa sana la wizi wa mitandao. Kuna wizi mkubwa uliokuwa unafanikiwa kwa kushirikisha wafanyakazi wa kampuni ya Airtel na kuiba fedha kwenye benki mbalimbali mfano *NBM*.

Mheshimiwa Spika, watumishi hawa wezi wamekuwa wakipiga simu na kujitambulisha kuwa wanashughulikia suala zima la kuhuisha programu mbalimbali kwenye kampuni yao ya Airtel, lakini jambo la kushangaza ni pale kampuni hii imeonekana kutotoa ushirikiano wa kuwatambua wafanyakazi wake wanaoendesha vitendo hivi vya wizi. Naomba Waziri unapohitimisha atueleze suala hili limeshughulikiwa kwa kiasi gani na hawa wahusika wamechukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Spika, suala la lugha chafu na picha chafu kutumwa katika mtandao, hakikia suala hili linapaswa kufanyiwa kazi kwa umakini mkubwa, si kwa vijana tu bali hata kwa watu wazima.

Mheshimiwa Spika, leo hii suala la *whatsapp* limeteka akili za watu kwani ni picha chafu tu ndizo zinarushwa katika mtandao huu. Hakika suala hili litazidi kuporomosha maadili ya Watanzania kwani huo sio utamaduni uliozoeleka kwa walio wengi au utamaduni tunaopaswa kurithi Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, changamoto ni minara ya simu inaleta madhara kwa wananchi mfano ni Temeke katika mtaa wa Wailes, wananchi watapata mivutano isiyoeleweka na hasa wakati wa usiku.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *DSTV* mara unapomaliza fedha tu *channel* utakazopata ni *TBC1* na *Channel Ten* tu, hupati *Star Tv,* wala *ITV*.

Mheshimiwa Spika, watu wanapigwa picha bila ridhaa mfano, picha yako unapigwa wakati unaongea Bungeni au sehemu yoyote na inaunganishwa na mwingine ukatengenezewa kitu kisichofaa kabisa.

Mheshimiwa Spika, hali hii ni hatari, Serikali itafute njia ya kunusuru ugomvi na migogoro isiyo na sababu.

Mheshimiwa Spika, Airtel hazishiki Mbagala, simu zinakatikakatika. Maeneo ya Mbagala, Nzasa, Kilungule mitandao kutoshika simu zinakoroma hovyo hata maneno hayasikiki hasa Tigo.

Pia ving'amuzi havishiki maeneo ya Mbagala, picha zinaganda na kuvurugika tu, hali hiyo imeanza toka tuanze kutumia ving'amuzi.

Mheshimiwa Spika, Tigo-Pesa na mitandao ya M-Pesa pale pesa zinapoenda kwa mtu ambaye haeleweki unapoenda makao makuu unachukua muda mrefu kupata majibu ya shida yako na foleni kubwa na hasa kituo cha *Mlimani City.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Mitandao ya kijamii idhibitiwe inaonyesha picha za hovyo sana.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pongezi kwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wengine wa Wizara hii kwa uchapaji na utendaji kazi. Kazi yao inaonekana dhahiri.

Mheshimiwa Spika, suala la simu Wilayani Tarime pamoja na maendeleo ya dhahiri yanayoonekana katika Wilaya ya Tarime, kuna minara kadhaa katika baadhi ya kata. Hata hivyo bado kuna uhitaji mkubwa wa minara katika kata zifuatazo; Nyandoto, Manga, Komaswa, Nyansicha, Gorong'a, Bumera, Itiryo, Mbogi, Kihore, Nyakonga, Matongo, Nyanungu, Kibasuka, Susuni, Muriba, Mwema, Nyarukoba, Pemba, Nyamaraga, Kitale, Nyarero , Nyamwaga, Ganyange, Kemambo, Nyamaraga na Sirari.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuwa vijiji vya kata hizi vikipatiwa mnara mmoja tu kwa kila kata vitasukuma mbele gurudumu la maendeleo hasa ukizingatia kuwa kata hizi zipo mpakani mwa Kenya na Tanzania na

shughuli kuu ya biashara, ulinzi na mawasiliano ni muhimu. Hivyo napendekeza na kusisitiza Wizara kupeleka haraka iwezekanavyo minara katika kata hizi zote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mawaziri kwa kazi nzuri naomba tupate minara katika Kata za Chuno, Mingumbi, Mitohe, Miguruwe na Kandawale.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, shida yangu kubwa kwa Wizara hii ni kushindwa kuyashawishi makampuni ya simu kupeleka mnara katika Kata ya Mwamagembe. Nimehangaika takribani miaka mitano sasa bila mafanikio yoyote isipokuwa ahadi tu za hapa na pale kutoka Wizara hii.

Tatizo la Mwamagembe ni kwamba wao walirukwa baada ya minara kuwekwa Kata ya Mitundu, wakaruka Kata ya Mwamagembe wakaenda kuweka Kata ya Rungwa. Ushindani kati ya Vodacom na *Airtel* katika kuweka minara ulipelekea Kata ya Mwamagembe kukosa huduma ya mnara kutoka Airtel baada ya *Airtel (Celtel)* kusimamisha upelekaji minara wakati Vodacom wakafanikiwa kupeleka mnara Kata ya Rungwa.

Mheshimiwa Spika, hatua hii imeacha malalamiko makubwa kwa wananchi wa Mwamagembe kwamba wanabaguliwa kihuduma. Kata hii ina uchumi mkubwa kutokana na kilimo cha tumbaku na mazao yatokanayo na misitu. Hata Bwana Ulanga anakiri hili baada ya kufanya utafiti.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kupitia Wizara hii itatue tatizo hili sugu, vinginevyo tutaona kuna ubaguzi katika kutoa huduma hii.

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kujua ni lini minara itawekwa Kata ya Idodyanide, Kata ya Kitaraka, Kata ya Mgandu, Kata ya Ipande na Kata ya Sanjaranda.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu suala la kufikisha huduma za mawasiliano vijijini. Umuhimu wa maeneo ambayo hayana mawasiliano kuyapata ni jambo lisiloepukwa na Serikali. Hitaji la mawasiliano kwa Watanzania walio vijijini bado ni kubwa ikilinganishwa na fedha zinazotengwa na Wizara ili kupeleka mawasiliano vijijini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Wizara kutafuta fedha za kupeleka umeme vijijini ni lazima Serikali ione umuhimu wa kuipatia fedha Wizara ili itekeleze upelekaji wa mawasiliano vijijini. Karatu ni miongoni mwa Wilaya ambazo baadhi ya vijiji vyake havina kabisa mawasiliano au kuwa na mawasiliano hafifu.

Je, ni lini vijiji hivyo vitapata umeme?

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti wa mfumo wa sekta ya mawasiliano, ukuaji wa mawasiliano nchini ni jambo linalokuwa kwa haraka sana. Hata hivyo ukuaji huo ndivyo mawasiliano hayo yanaweza kutumika kwa matumizi mabaya au mazuri na hivyo udanganyifu katika mitandao ni jambo linalokuwa kwa kasi sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Wizara za kutengeneza kanuni mpya zinazosimamia mawasiliano kupitia mtandao ili kuongeza mapato ya Serikali ni jambo jema. Nashauri Wizara kutokuangalia upande mmoja tu wa kupata mapato bali itazame upande mwingine wa kuthibiti matumizi mabaya katika sekta ya mawasiliano hii ni pamoja na kuwatambua watu wanaotukana, kukashifu, kuchafuana katika mitandao ya mawasiliano nchini na kuwachukulia hatua.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo bado wananchi waathirika wa matumizi mabaya ya mawasiliano hawana uelewa wa kujua wafanye nini au kuchukua hatua gani wanapokutana na hayo? Nashauri Wizara na/au itupe majibu wanajipanga vipi kudhibiti hali hiyo? Na je, itachukua hatua gani kutoa elimu kwa wananchi kuacha tabia hiyo na wakiathirika wafanye nini?

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kupata nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri kwa hotuba yake, niwapongeze pia watendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe shukrani zangu kwa Waziri kwa jinsi ambavyo anajitahidi kutupatia mawasiliano, lakini pia nitoe malalamiko yangu makubwa sana katika Mkoa wangu wa Geita kwani mawasiliano hakuna kabisa.

Mheshimiwa Spika, hata kwenye kitabu cha hotuba kinaonyesha maeneo ambayo yamepata mitandao ya Vodacom ni sehemu mbili tu katika mkoa mzima yaani ni Wilaya ya Bukombe Kata ya Mbogwe na Nyang'hwale Kata ya Shabaka.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine kama Chato, Geita, Nyang'hwale ambayo ni makao makuu ya Wilaya hakuna mawasiliano, pia kuna vijiji vingi katika Wilaya ya Nyang'hwale mpaka sasa wananchi wanapanda kwenye miti ndiyo wapate mawasiliano vijiji hivyo ni Nyijundu, Nyarubele, Kakora, Nyantukuza, Kabiga, Ligembe, Kitongo, Ikangara na Karumwa, maeneo haya yote yapo katika Wilaya mpya ya Nyang'hwale

Mheshimiwa Spika, nimuombe Waziri aweze kuyapa kipaumbele maeneo ya mikoa mipya na Wilaya mpya ili kuweza kuhalalisha mawasiliano katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa mtazamo wangu juu ya bajeti hii basi naanza kwa kutoa pongezi na shukrani zangu za dhati kwa Waziri Mheshimiwa Makame Mnyaa Mbarawa, kwa juhudi na kazi nzuri anayoifanya yeye na Naibu Waziri wake Mheshimiwa January Makamba kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyopangiwa Wizara hii ni ndogo sana hivyo basi naishauri Serikali iongeze bajeti ya Wizara hii ili nchi yetu iweze kuwa na mawasiliano ndani ya vijiji vyote. Wananchi wengi vijijini wanahitaji mawasiliano ili waweze kujikwamua kiuchumi pamoja na huduma kwa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itekeleze ule mradi wa kuunganisha Taasisi za Elimu ya Juu na utafiti kule Zanzibar kwa ajili ya kufanikisha elimu mtandao katika vyuo vikuu kama vile *Karume Institute of Science* na *Technology (KIST)* pamoja na vyuo vingine ili nayo Zanzibar ifaidike na matunda haya yaliyopatikana kutokana na juhudi na mafanikio ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ilianzisha Mradi wa Anuani za Makazi na Postikodi ambapo kila mwananchi ataweza kujitambulisha kwa kutumia jina la mtaa, nambari za nyumba pamoja na postikodi ya eneo analolishi. Je, mpango huu wamefikia wapi kama Wizara mbona hatujaona kutekelezwa kwake?

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuipongeza Wizara kwa mafanikio makubwa tuliyoyapata Wazanzibar hasa Pemba kwa kupata mradi wa Mkongo

wa Taifa. Tumepata faraja na matumaini makubwa sana kwani tatizo sugu la umeme limeondoka na sasa Wapemba tunapata umeme wa kutosha.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, kukuza matumizi ya TEHAMA kwenye shule za msingi na sekondari, napenda kujua katika shule hizi za majaribio Wilaya ya Misenyi imepata shule ngapi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu usalama katika matumizi ya TEHAMA, kumekuwepo na wizi wa hali ya juu kupitia mitandao hasa benki na *sim banking*, watu wanaibiwa vibaya sana hasa kwa kupigiwa simu au kutumiwa *message* ili kuelekeza kuwa umeshinda kupata fedha na inataja kiwango kikubwa na ina kuelekeza ufuate maelekezo mpaka unatuma fedha kwa mtu usiye mjua, matokeo yake unakuwa umehamisha fedha zako toka kwenye *Account* yako na kwenda kwenye *Account* ya huyu mnayewasiliana, na mhusika hutoa fedha haraka sana na ukifuatilia hapatikani tena.

Napenda kujua lini wizi huu utadhibitiwa?

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la kuibiwa kupitia simu hasa ukikosea, ukifuatilia uliyemtumia wakati mwingine unafanikiwa kuzipata na mara nyingi hupati kwa sababu wengi hawajasajiliwa. Napenda kujua, kwa nini mpaka leo kuna watu wanaotumia simu bila kusajiliwa wakati hilo ni kinyume cha sheria, lini *line* hizo zitaondolewa katika mtandao?

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Nkenge, Wilaya ya Misenyi, mawasiliano ni hafifu sana na tumekuwa tukiahidiwa kuwa tutapewa minara, lakini mpaka leo hatujapata. Napenda kujua lini Kata hizi zitapata mawasiliano Kata za Kibobo, Buyangu, Ruzinga, Ishozi, Ishunju, Mabale, Kilimilile, Kakunyu, Minziro, Bugandika na Mtukula.

Mheshimiwa Spika, napenda ijulikane kuwa Wilaya hii ipo mpakani, ni vyema tukapewa minara ili Watanzania watumie mitandao ya Tanzania.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza kwa masikitiko makubwa siungi mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nimefuatilia sana suala la mnara wa mawasiliano nimeshauliza swali Bungeni na kuahidiwa kupewa mnada lakini kwa bahati mbaya katika bajeti mbili mfululizo mwaka 2013/2014 na 2014/2015 sijapata mnara lakini Jimbo la pili Wilaya hiyo hiyo ya Uyui, mimi Tabora Kaskazini sijapata mnara ila mwenzangu wa Jimbo la Igalula kapewa minara mitatu je, hii ni haki?

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Tabora Kaskazini lina makao makuu ya Wilaya ya Uyui lakini hapo hapo makao makuu Kata ya Isikizya hatuna mawasiliano ya uhakika kabisa. Kata ya Ibiri na Ufuluma ambapo tuna wakulima wengi na wenye uwezo mzuri lakini hatuna mawasiliano ya simu isipokuwa Kata ya Ufuluma mnara upo ila haifikishi huduma vijiji vya jirani ndani ya kilometa 15, ni lawama tupu

Mheshimiwa Spika, Kata yangu ya Shitage na Bukumbi ambazo zipo kilometa 160 kutoka makao makuu ya Wilaya hazina na zipo pembeni kabisa mwa Jimbo nimeomba sana kupewa huduma ya mawasiliano ya simu lakini sijasikilizwa!

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kufuatilia ili nijue maeneo uliyonisaidia kupata mnara wa simu Jimbo la Tabora Kaskazini. Kwa bahati mbaya hujanitendea haki katika orodha ya minara sina hata mnara mmoja kuanzia mwaka 2013/2014 na 2014/2015. Nimesikitika sana lakini naomba msaada wa kupewa mnara Tabora Kaskazini tafadhali sana.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja!

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Uyui minara mitatu umepeleka Jimbo la Igalula na mimi hata mmoja sijapewa!

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya licha ya kuwa na matatizo makubwa ya upungufu mkubwa wa ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii tukiitaka ifanye kazi nzuri na ya kuonekana ni lazima Serikali iwatengee bajeti ya kutosha itakayoendana na uhalisia wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa mawasiliano ya Kata ya Katuma, Jibwesa na Kabungu toka nimeingia katika Bunge hili nimekuwa nikipiga kelele juu ya maeneo haya ambayo hayana mawasiliano na kufanya wananchi wanaoishi katika kata hizo kujiona kama hawana haki ya kuishi katika nchi yao. Kata hizi zina sifa zote za kupelekewa mawasiliano ukilinganisha na baadhi ya maeneo ambayo unapita unakuta kuna minara ya simu wakati hata idadi ya watu wanaotumia huduma hiyo kuwa ndogo kuliko maeneo ambayo nimeyataja. Najiuliza maswali mengi ni kwa nini Kata hizo za Kabungu, Katuma na Sibwasa hazipatiwi huduma ya mawasiliano na kuna tatizo gani? Nitahitaji kupata majibu kutoka kwa Waziri mwenye dhamana anijibu vinginevyo nitashika shilingi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mawasiliano hafifu. Pamoja na kuwa na baadhi ya Kata chache zilizo na mawasiliano kuna tatizo kubwa la kutokuwa na mawasiliano mazuri katika Kata za Karema, Ikola, Mwese na Kata ya Mpangogo. Maeneo hayo mawasiliano yako hafifu sana kiasi kwamba mnawaletea usumbufu mkubwa katika kata hizo. Niliiomba sana Wizara yako iwaagize wahusika hasa katika Kata ya Mpandandogo na Kata ya Ikola, waende wakarekebishe minara iliyo kwenye kata hizo ili wananchi wapate mawasiliano yaliyo bora.

Mheshimiwa Spika, suala la wizi wa fedha katika mitandao, eneo hili lazima Serikali iliangalie kwa makini sana, kuna matukio mengi yanayojitokeza mara kwa mara kiasi kuwa kunawaletea usumbufu mkubwa na kupoteza fedha zao kupitia wizi ambao unafanywa kitaalamu zaidi. Ni vizuri Wizara ikafuatilia ili kukomesha wizi unaofanywa kupitia mitandao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi mabaya ya mawasiliano, nashauri Serikali iwadhibiti sana wale ambao wana matumizi mabaya ya simu kwa kuzitumia kusambaza ujumbe wa uchochezi, matusi na udhalilishaji. Naomba sana kupitia chombo cha kudhibiti mawasiliano kifanye kazi yao.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja hiyo pale tutakapopata majibu hasa ya mawasilino kwenye Kata zangu.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii. Naipongeza Wizara/Serikali kwa kuwa na *force market* katika *telecommunication* kwani imerahisisha huduma mbalimbali, makampuni mengi ya simu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo hizo kampuni za simu ulipaji wake wa kodi kwa Serikali ni utata ukilinganisha na kipato wanachopata, Serikali budi ipitie upya sheria hii.

Makampuni haya tunayapongeza kwa ubunifu mbalimbali lakini hata hivyo ukiangalia kwa umakini gharama zake hizo za jirushe ni kubwa sana na zinafanyika kiujanja ujanja hivyo wateja kuamini kuwa wanaibiwa *voucher,* pia ukiweka tu zimekwisha mara moja.

Mheshimiwa Spika, juhudi za makusudi zifanyike katika suala zima la *cyber* ili kuwepo na udhibiti wa siri ndani ya simu ya mteja.

Mheshimiwa Spika, suala la anuani za makazi limefikia wapi? Kasi yake hakuna, kulikoni?

Mheshimiwa Spika, Serikali/Wizara ina mkakati gani wa ku-*control* mitandao ya kijamii? Imekuwa ikitumika sana katika kuchafua watu hususan viongozi. Iwepo *mechanism* ya ku-*control* hili.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali/Wizara kwa kupandisha hadhi Taasisi ya Teknolojia Mbeya na kuwa Chuo Kikuu. Kipekee na kwa umuhimu wake ingeangalia sana suala la miundombinu. Barabara ya kuelekea kwenye chuo hiki imekuwa inaleta aibu kwani inapita kwenye vichochoro visivyojulikana ndani ya makazi ya wananchi. Njia mbadala ifanyike katika kurekebisha hili.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano ya leo ndiyo yenye kuleta dira ya kuharakisha maendeleo katika nchi, hivyo naomba wembe huu hakuna kurudi nyuma bali kusonga mbele na kuwa wabunifu zaidi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri na Naibu Waziri wake na timu nzima Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri mmeonyesha *capability* yenu vizuri sana. *Keep up the good job,* msilewe sifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, hongera sana Mawaziri, Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote.

Mheshimiwa Spika, nashauri utafutwe utaratibu wa kupeleka mawasiliano kwa vijiji ambavyo havina mawasiliano kabisa.

Mheshimiwa Spika, nahitaji kijiji cha/au vijiji katika Kata ya Kalembo na Sanje vina uchumi mzuri sana na mahitaji ya mawasiliano ni makubwa sana. Katika Wilaya ya Ileje shida kubwa ipo katika Kata ya Kalembo, Kata ya Lubanda, Kata ya Ikinga na Kata ya Sange. Naomba sana ufanyike utaratibu ili minara iwekwe katika kata hizi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ifanye juhudi ili Shirika letu la *TTCL* lipatiwe asilimia 100 ya hisa zote zimilikiwe na Serikali kupitia Shirika hili ili liweze kufanya kazi zake kwa uhuru wa kuwaletea Watanzania maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfuko wa mawasiliano kwa wote, ushauri wangu Serikali itoe fedha za kutosha kwa mfuko huu ili tupate mawasiliano kwa kasi kubwa zaidi.

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Mheshimiwa Spika, ninaanza kuchangia hoja hii kwa maandishi kwa kuishukuru Wizara hii kwa kazi na umahiri wao wa kuisimamia Wizara hii nyeti.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya maendeleo ya shughuli za mfuko wa mawasiliano kwa wote hadi Aprili, 2014, sikuweza kuiona Kata ya Nguliguli ya Wilaya ya Maswa katika Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Nguliguli ni Kata yenye wakazi wengi wanaojishughulisha na kilimo cha pamba, mpunga, choroko, dengu kwa wingi kuliko maeneo yote ya Mkoa wa Simiyu, wanazalisha pia mbaazi kwa wingi sana. Kata hii pia ni ya wafugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo kwa wingi sana.

Mheshimiwa Spika, Kata hii yenye uchumi mkubwa wenye tija kwa Wilaya ya Maswa na Mkoa wa Simiyu na Taifa kwa kutopatiwa minara ama mnara ni sawa na kutokuthamini umuhimu wa uchumi mkubwa unaozalishwa na wakazi wa Kata hii ya Nguliguli.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa natambua juhudi za Waziri na Naibu wake ninayo imani kuwa Kata hii iliyosahauliwa kuwekwa kwenye mpango wa kuwekewa minara ama mnara pamoja na kuwa niliituma kwa kuiombea kwa Wizara iwekwe kwenye mpango, naamini kufanya kosa si sawa, naamini kata hii itawekwa katika mpango wa kujengewa minara/mnara.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wa Wizara hii kwa kufanya kazi nzuri katika nyanja hii ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mawasiliano, tunashukuru kwa kupata mnara katika Kata ya Kihungu na Ukata. Naomba mkandarasi/wahusika waweke mitambo hii ili mawasiliano yawe hai. Kata ya Mperai inayosomeka katika ukurasa wa 92 wa kitabu cha hotuba ya bajeti bado mnara huo haujaanza kujengwa.

Ipo shida kubwa ya mawasiliano katika Kata na vijiji vya Ngima karibu tu na Mji wa Mbinga; Kata ya Litumbandyosi hasa kijiji cha Litumbandyosi na Kingole; Kata ya Langiro kijiji cha Lungomba na Mkoha na Kata ya Kihangi Mahuka kijiji cha Lupumba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya TEHAMA katika shule zetu, katika Wilaya ya Mbinga elimu hii bado duni. Ningependa kuona elimu inaanzishwa katika shule za msingi na sekondari. Wizara inaweza kusaidia namna gani na Halmashauri ya Mbinga angalau kuanza kama *satellite* tu. Nitashukuru sana

kupata ushirikiano. Nitafurahi kama nitakaribishwa kwa mazungumzo juu ya ombi hili.

Mheshiiwa Spika, naomba pia katika programu hii ya uanzishwaji wa vituo vya kijamii vya mawasiliano Mbinga pia iwemo.

Mheshimiwa Spika, naikaribisha pia Wizara kuisaidia Halmashauri ya Mbinga kuanzisha utaratibu mpya wa anuani za makazi.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma upo mpakani mwa nchi ya Burundi, hivyo mara nyingi wananchi wanaoishi mpakani mawasiliano kwa njia ya simu ni ya shida sana, mara nyingi sana mitandao inayoonyeshwa kwenye simu zao ni ya Burundi, hata hivyo wanakuwa hawawezi kupiga wala kupokea simu. Maeneo hayo ni vijiji vya Kitanga, Heru Ushingo, Buhigwe na vijiji vingine vingi ambavyo sikuvitaja hivyo naomba Serikali iweze kutusaidia kushawishi makampuni ya simu yaweze kutuwekea minara ya simu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma eneo kubwa la barabara limetawaliwa na misitu mikubwa, hivyo mara nyingi majambazi hujificha katika misitu maeneo hayo na kufanya vitendo vya unyang'anyi na utekaji wa magari, katika maeneo hayo hakuna mawasiliano ya simu. Naomba hilo nalo litizamwe na kupewa kipaumbele eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yao yote kwa kazi nzuri sana ya kujenga, kukuza na kuratibu vyema shughuli zote za Wizara na zaidi kupanua matumizi ya TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri *TCRA* mbali na kuanza kudhibiti mapato lakini pia idhibiti matumizi ya mtandao kwa watu wanao-*download* picha za ngono. Tumeona baadhi ya nchi za Kiarabu huwezi ku-*download* picha za ngono.

Mheshimiwa Spika, aidha naiomba Wizara idhibiti wizi unaofanywa na makampuni ya simu hasa katika kudhibiti wizi na mawimbi wanayotumia watu. *Money transaction* na mawasiliano ya kutoka simu moja hadi nyingine Wizara mbali na kuanzisha *tele medevice* pia iharakishe *electronic recurement* kwani Serikali hutumia wastani wa asilimia 70 ya bajeti yake kutoka manunuzi.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya Mkongo yameleta manufaa sana katika kuboresha matumizi ya TEHAMA, ni vyema Wizara kubuni njia za kuratibu mashirika na taasisi nyingine ambazo zina mikongo kama *TANESCO*, Reli na kadhalika. Matumizi mazuri ya rasilimali za nchi sio tu kutapunguza gharama, bali kutatoa fursa ya matumizi mazuri ya rasilimali za nchi.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa wataalam wa wanasayansi, ni vyema Serikali ikawa na *data* juu ya mahitaji ya wanataaluma wa sayansi kwa nchi nzima, yaani kujua mahitaji ya wataalam katika kipindi cha miaka mitano hadi 10 - 15 - 25. Wataalam waliopo sasa katika kila sekta ya sayansi na uzalishaji wa wataalamu hao sasa na mpango wa kuziba pengo lililopo.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi zinazoendelea duniani zimejipanga kuzalisha wakati wote wanataaluma wa sayansi wasiopungua asilimia 60, hivyo ni vyema tukawa na *data*, maandalizi toka shule za msingi, vyuo vya *VETA* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuzinunua hisa za mbia wa *TTCL Bharti Airtel*, lakini kumekuwa na kigugumizi cha kumaliza kukokotoa mahesabu ili TTCL iweze kumilikishwa asilimia 35 ya Bharti Airtel.

Mheshimiwa Spika, namuomba Waziri alielezee Bunge hili ni lini ununuzi wa kina utakamilika

Mheshimiwa Spika, kampuni za simu kujiunga na Soko la Mitaji Dar, pamoja na sheria ya kuyataka makampuni ya simu katika kipindi cha miaka mitatu kujiunga na Soko la Mitaji kama hatua ya kuwapa fursa Watanzania kumiliki hisa ndani ya makampuni hayo hadi sasa hakuna taarifa ya utekelezaji wa sheria hii.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Katika miradi wa UCAF, Wilaya ya Ulanga ilipanga kujenga minara mitatu, katika Kata za Itete, Iragua na Ngoheranga, lakini hadi leo minara imejengwa miwili tu katika Kata ya Itete na Iragua, lakini bado kuunganisha mitambo ya mawasiliano, naiomba Serikali iharakishe kukamilisha mawasiliano katika minara hii ambayo imejengwa na *TTCL* na Tigo.

Mheshimiwa Spika, ni lini mnara na Ngoheranga utaanza kujengwa kwani ilikuwepo katika awamu ya kwanza ya *UCAF* lakini haikufanikiwa kupata

mkandarasi. Wananchi wa Kata ya Ngoheranga wanateseka sana kwa kukosa mawasiliano ya simu na mitandao ya *internet* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali aidha kupitia *UCAF* au sekta binafsi itajenga mnara katika kata iliyosahaulika, Kata ya Sofi ambayo haimo katika mpango wa Serikali katika *UCAF*.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* naiomba ipatie kipaumbele utafiti wa kilimo hasa katika mazao ya mpunga ambapo sasa zao hilo linakabiliwa na magonjwa mengi yakiwa ya virusi ambao yanawasumbua sana wakulima. Hivyo nashauri Serikali kuongeza bajeti inayotengwa kwa *COSTECH* kwa ajili ya utafiti na sayansi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze kuwapongeza Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya na pia kuwasilisha bajeti yao ili tuanze kuijadili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufinyu wa bajeti inasikitisha sana kuona bado Serikali haijaweza kuona umuhimu wa kutenga fedha ya kutosha katika Wizara hii. Wizara hii ni nyeti lakini pamoja na kupatiwa bajeti ndogo sana bado fedha hazifiki kwa wakati na kusababisha miradi mingi ya maendeleo kutokukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hakuna nchi duniani inapata maendeleo bila kutumia utafiti wa ubunifu kwa nini Serikali haioni hilo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Mkongo wa Taifa niipongeze sana Serikali kwa mradi huu. Ni imani yangu Mkongo huu utakapokamilika utasaidia sana kushusha gharama na kuongeza ubora wa mawasiliano na hata umeweza pia kuunganisha nchi zote jirani hasa zile ambazo hazipakani na bahari. Wasiwasi wangu pamoja na umuhimu wa mradi huu wa usuaji wa Serikali kuwekwa fedha ya kutosha katika ujenzi wa mradi huu kutasaidia kweli kufikia malengo? Je, ni mkakati gani umewekwa wa Serikali katika kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika kwa wakati?

Mheshimiwa Spika, kuhusu kodi katika sekta ni kubwa sana ukilinganisha nchi za jirani za Kenya, Rwanda na Burundi, bado nchi yetu kodi ya sekta ya simu ni kubwa, kwa nini Serikali isipunguze *excise duty* kutoka 17% hadi 14% iwe kama ilivyokuwa mwaka 2012/2013. Kwa sababu ukubwa wa kodi hiyo unasababisha gharama za simu na mitandao inakuwa ghali sana kwa

watumiaji. Na vilevile kuwepo kwa kodi hii kubwa inasababisha uwekezaji mdogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utafiti wa maendeleo inasikitisha sana kuona bado Serikali haijaweza kuona umuhimu wa kuweka fedha za kutosha katika kitengo cha utafiti, nchi ambayo haina utafiti haina maendeleo.

Nchi zote ambazo zimeendelea ni nchi ambazo zimetoa kipaumbele katika utafiti. Lipo azimio la kutenga 1% ya Pato la Taifa na kupeleka katika utafiti, je, Serikali imeweza kutekeleza azimio hili? Ni kwa nini azimio hilo halitekelezeki?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfuko wa mawasiliano kwa wote *(UCAF)* lengo la kuanzishwa kwa Mfuko huu wa Mawasiliano kwa Wote, lakini tumeona katika mfuko huu zipo changamoto nyingi sana ambazo zinasababisha dhamira hii kutotimia kwa wakati ambazo ni pamoja na ufinyu wa bajeti na fedha kutopatiwa kwa wakati, maeneo mbalimbali yasiyokuwa na mvuto wa biashara makampuni ya simu kutowekeza. Ni kwa nini Serikali isichukue mikopo ya Kimataifa ili kumaliza tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Posta, Mradi wa Posta na Simbo za Posta *(Postal code)* ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi kiuchumi, kibiashara, kisiasa na katika utoaji wa huduma mbalimbali, kwa nini bado Serikali haijatoa umuhimu katika mradi huu?

Ushauri wangu pamoja na kuwa Serikali haijaweza kupeleka fedha za kutosha katika mradi huu lakini ili mradi huu uende haraka ni vyema Wizara hii ingeshirikiana na Wizara ya TAMISEMI kwa sababu kama Halmashauri zetu zitasimamia miradi hii na kushughulikia uwekaji majina ya mitaa na namba za nyumba kwa haraka kutasaidia sana mradi huu kwenda kwa haraka zaidi, bajeti iliyopita ya mwaka 2013/2014 ilitengwa shilingi 1,000,000,000/= lakini zilitolewa shilingi 300,000,000/= tu, ni vyema fedha zote zilizotengwa zitolewe na pia zitakazotengwa kwa bajeti ya mwaka huu 2014/2015 zitolewe zote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kampuni ya Simu *(TTCL)* moja ya changamoto kubwa inayokabili *TTCL* ni madeni ambayo imekuwa ikidai katika taasisi za Serikali. Hadi kufikia Februari, 2014 inadai shilingi 2,431,040,809.37 na dola 1,488,153.88 na pia inadai hata katika taasisi zisizo za Kiserikali, je, mkakati gani umewekwa ili kuhakikisha shirika hili linakamilika? Mheshimiwa Spika, naunga mkono.

**MHE. CELINA O. KOMBANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Wizara kwa kazi nzuri mnayojenga ya kusambaza mawasiliano katika nchi hii. Naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 90 hadi wa 91 Kata zisizopata wazabuni ukurasa 91 Mkoa wa Morogoro - Ulanga Kata ya Itete na Iragua, Kata zote hizi zipo Ulanga Magharibi.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 94 hadi wa 96 Kata zilizopata wazabuni angalia ukurasa wa 96, Morogoro - Ulanga haipo.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 99 hadi wa 103 Kata zilizopata wazabuni awamu "B" angalia ukurasa wa 102, Morogoro Ulanga haipo.

Ninapenda kutoa masikitiko yangu kwamba Jimbo langu la Ulanga Mashariki halina mawasiliano ya simu katika Kata zipatazo 10, Kata hizo ni pamoja na Ruaha, Sali, Euga, Chirombola, Ketaketa, Ilonga, Mbuga, Lukande, Msogezi na baadhi ya maeneo katika Kata ya Nawenge na Lyandu.

Mwaka 2013/2014 niliahidiwa kwamba utajengwa mnara katika Kata ya Sali ambayo ipo juu sana kutoka usawa wa bahari, mnara huo ungejengwa ungeweza kusambaza mawasiliano katika Kata jirani za Ruaha, Euga na Chirombola na hata Kata za jirani za Sofi katika Jimbo la Ulanga Magharibi.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka Waziri mwenyewe ulinielekeza nimuone Bwana Ulenga ili anisaidie na nilifanya hivyo, Serikali hadi leo hakuna matokeo yoyote. Kwa hiyo naomba Wizara yako ifikirie hilo Jimbo lenye Kata 16 na kati yake ni sita (6) tu ndiyo zenye mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kutoa taarifa kwamba umeme wa *REA* umefika katika baadhi ya Kata kama Chirombola, Ruaha na Euga. Naomba mnara ujengwe katika Kata ya Ruaha na Sali.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wa Wizara hiyo kwa kazi nzuri wanazofanya katika kuboresha mawasiliano nchini na kuhamasisha matumizi ya sayansi kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, natambua kwamba kuna upungufu mkubwa wa wanasayansi hasa katika nyanja za sayansi, teknolojia na ubunifu ambao ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Je, Wizara ina mkakati gani ili kuongeza wanasayansi nchini?

Mheshimiwa Spika, utafiti wa maendeleo *(R&D)* ni muhimu sana katika kuharakisha maendeleo nchini. Mwaka 2008 ilikubaliwa kuanza kutenga angalau shilingi bilioni 30 kuelekea kufikia kiasi cha asilimia 1.0 ya Pato ghafi la

Taifa kwa ajili ya utafiti na maendeleo, je, kwa sasa tumefikia asilimia ngapi ya lengo hilo?

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kilolo maeneo ya Nyanzwa (Mahenge), Kising'a (Ukwega), Kimala, Irole, Image, Ibumu, Masisiwe, Ibofure na Kitelewasi yamekosa mawasiliano ya simu kwa muda mrefu licha ya maombi ya mara kwa mara. Je, ni lini sasa maeneo hayo yatapata mawasiliano kwa maendeleo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, napenda kusema kuwa ninaunga mkono hoja hii iliyopo mbele yetu leo.

Napenda pia nimpongeze Waziri mwenye dhamana na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya ambapo wameonyesha kuimudu vizuri Wizara hii. Aidha napenda pia kumpongeza Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, hali ya mawasiliano Wilayani kwangu Nanyumbu Mkoa wa Mtwara bado ni duni sana na hii imeathiri sekta mbalimbali za huduma za jamii hivyo kuzorotesha maendeleo.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi ndani ya Wilaya ya Nanyumbu hayajafikiwa na mawasiliano ya simu za mkononi na hii inatokana na ukosefu wa minara ya simu. Maeneo ambayo hayapati mawasiliano au hayasikiki kupitia simu za mkononi ni kama yafuatayo:-

(i) Kata ya Nandete ni katika vijiji vya Chivirikiti, Nakole na Ngalole.
(ii) Kata ya Likokona ni katika vijiji vya Likokona, Namaka na Mwambo.
(iii) Kata ya Lumesule ni katika vijiji vya Lumesule, Mchenjeuka na Changwale.
(iv) Kata ya Napacho ni katika vijiji vya Napacho, Kazamoyo na Mpombe.
(v) Kata ya Maratani ni katika vijiji vya Maratani na Lipupu.
(vi) Kata ya Mnanje ni katika vijiji vya Mnanje na Mikuva.
(vii) Kata ya Mikangaula ni katika vijiji vya Chitandi, Mkoromwana na Mkambata.
(viii) Kata ya Nangomba katika kijiji cha Nangomba.
(ix) Kata ya Chipuputa katika vijiji vya Chipuputa, Namasogo, Mkohora, Namaguluvi na Nakatete.
(x) Kata ya Sengenya katika vijiji vya Nawavupi, Masyalele na Chinyanyira.
(xi) Kata ya Mkonona katika vijiji vya Marumba, Wanika na Namaromba.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara hii ifanye taratibu za kupeleka au kujenga minara ya kutosha ili maeneo niliyoyataja yaweze kupata mawasiliano ya simu za mkononi ili wananchi walio kwenye maeneo hayo waweze kupata mawasiliano?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu na ndiyo maana Azimio la Abuja pamoja na lile la *SADC* zilipitisha kutenga asilimia moja ya Pato la Taifa kwa ajili ya sayansi na teknolojia kwa nchi za Afrika ili ziweze kukua na kuondoka kuwa nchi maskini duniani.

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti ya mwaka 2013/2014, Serikali ilitengewa shilingi takribani bilioni 30 kwa maendeleo. Cha kusikitisha Serikali hadi leo wametoa shilingi bilioni tatu tu sawa na asilimia 10 tu ya fedha za ndani, lakini pia fedha za nje zilikuwa ni shilingi bilioni 1.7 ikiwa ni asilimia 31 tu ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, hii inakatisha tamaa na wanasayansi wanajiuliza kama kweli Serikali inatilia maanani suala zima la kukuza sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji mdogo unaathiri sana kazi nzuri ya Tume ya Taifa ya Sayansi ambayo inafanya kazi nzuri sana kuendeleza tafiti mbalimbali kwenye kilimo, lakini pia kwenye afya na mazingira. Ni muhimu sasa Wizara iangalie ni jinsi gani Tume iwe na vyanzo vya mapato. Ni kwa nini basi Serikali isiweke *Technology Development Levy* ili fedha hizo ziende moja kwa moja *COSTECH*?

Mheshimiwa Spika, *Atomic Energy Agency* ni muhimu sana kwa usalama wa Watanzania, wenzetu nchi zilizoendelea na za kati pamoja na kutumia mionzi kwenye *x-ray* na matibabu ya kansa, lakini pia inatumika kwenye kuhifadhi nafaka na matunda na kuzuia uharibifu wa vyakula mbalimbali ili kuongeza tija kwa mwananchi.

Mheshimiwa Spika, ninatoa wazo kubuniwe vyanzo vingine vya mapato ili kuongeza makusanyo ya taasisi ili iweze kutoa huduma hiyo muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu na maisha bora ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze taasisi hizi zote, maana pamoja na fedha ndogo inayotolewa bado wanafanya kazi vizuri na wamekuwa wabunifu

wa kutafuta fedha. Taasisi hizo ni zote zikiwemo *TCRA*, *COSTECH*, *Atomic Energy Agency*, *TTCL* na zote nyingine.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TCRA ifanye jitihada kuendelea kudhibiti matumizi mabaya ya simu. Natambua ni kazi nzito na wanapambana na kila aina ya mbinu mpya, lakini ni dhahiri kuwa ili nchi iendelee kuwa na amani na utulivu ni lazima *TCRA* ipambane na ifanikiwe kudhibiti.

Mheshimiwa Spika, itakuwa vizuri Wizara ikasema imejipanga vipi kudhibiti maana ni suala ambalo wananchi wanataka kulisikia, hivyo ni vyema Wizara ikaeleza.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, jitihada za kuboresha huduma za mawasiliano zinazoendelezwa na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia 2013/2014 na 2014/2015 ni kubwa na za kuvutia.

Hata hivyo napenda kuonyesha huzuni kubwa kwa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga kutopatiwa ongezeko la hata kijiji kimoja tangu mwaka 2013/2014 na katika bajeti hii 2014/2015, nilijaza fomu kuonyesha matatizo ya vijiji muhimu sana na kuweka maelezo ya umuhimu wake, hivyo narudia tena leo kwa hata kata moja na vijiji vitatu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kata ya Zirai, Tarafa ya Amani vijiji vya Zirai - Antakae - Kambai Kata hii ipo katika milima ya Amani lenye hifadhi ya msitu wa Amani na mashamba makubwa ya chai. Eneo la hifadhi ni kivutio kikubwa cha utalii (wanaofika bila kupata mawasiliano). Pia mashamba ya chai yanayopatia Taifa letu fedha za kigeni kwa mauzo ya chai na miwa inayosaidia vijana ajira ya mauzo ya miwa miji ya Muheza /Tanga/Dar es Salaam. Mfumo huo wa biashara unapokosa mawasiliano ni sawa na kudhoofisha mapato ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vodacom walijenga mnara mmoja mrefu sana Amani eneo la kata ya Amani kijiji cha Shebomeza lakini kutokana na mfumo wa hali ya muinuko na mabonde katika mazingira ya maeneo ya milimani, bado maeneo mengi hayapati mawasiliano kabisa na sehemu nyingine mawasiliano kuwa dhaifu.

Naomba kuwasilisha ombi hili maalum licha ya kuwepo maeneo mengine kama niliyoorodhesha katika fomu nilizojaza awali kwa ajili ya Wilaya ya Muheza. Nimeona Kiambatanisho Namba 8; Kiambatanisho Namba 9 na Kiambatanisho Namba 10. Wilaya ya Muheza haipo wakati maeneo mengine yamepata Kata tano na vijiji 18 – 30.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote hayo naunga mkono hoja kwa manufaa ya Taifa la Tanzania.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Aidha, naomba pia kumpongeza Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa na Naibu wake Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Katibu Mkuu wa Wizara pia timu yote ya Wizara kwa kazi nzuri ambayo inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Mbeya Vijijini kuna vijiji vingi ambavyo vina matatizo ya mawasiliano na hivyo kuwaletea matatizo ya mawasiliano kwa wananchi. Aidha, vijiji hivyo ni vile vilivyopo Kata ya Ilungu, Isato, Iwiji, Ulenje na Ilambo pamoja na Ikukwa. Kuna vijiji vingi vilivyotajwa katika hotuba yako ambavyo vimepangwa kuboresha mawasiliano.

Naomba Mbeya Vijiji Ikambakwe katika Kata nilizotaja kupewa huduma hiyo, Mbeya Vijijini ina jiografia ya milima mingi na hivyo kufanya mawasiliano kuwa shida katika vijiji vingi, kwa hiyo utafiti wa kubainisha matatizo ya mawasiliano ni vizuri ukapunguza.

Mheshimiwa Spika, huduma ya mawasiliano ni bora ikatenga katika maeneo ambayo huduma mbalimbali zinatolewa hususani katika shule za sekondari za Kata zilizo vijijini, zahanati, shule za msingi na kadhalika ili kuwafanya wahudumu wote waliopo maeneo hayo wapate huduma hii muhimu.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri wa Wizara hii pamoja na Naibu wake, pia watendaji wote waliopo chini ya Wizara hii kwa mchango wao mkubwa wa uchumi na mawasiliano ya Watanzania. Hata hivyo nina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mosi Wilaya ya Tandahimba ina kero kubwa za ukosefu wa mawasiliano ya uhakika kwenye Kata za Mihambe, Mkoreha, Naputa, Maundo, Namikupa, Chaume na Michenjele. Tafadhali jitihada zifanyike kutoa adha ya ukosefu wa huduma hiyo kwenye Kata hizi.

Mheshimiwa Spika, pili nchi ina shida kubwa ya kukithiri kwa wizi na utapeli katika mitandao, TCRA wawe na utaratibu mahsusi wa kudhibiti na kusimamia kadhia hiyo.

Mheshimiwa Spika, tatu fedha za kusimamia huduma za mawasiliano kwa nini hazipelekwi kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili kusaidia vijiji na hata miji kufikiwa kwa haraka badala ya kupelekwa Serikalini kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, nne kufuatia taarifa kuwa Rasimu ya Sheria za Usalama wa Mtandao, Sheria ya Kulinda Taarifa Binafsi na Sheria ya Kudhibiti Uhalifu wa Mtandao na Kompyuta kuwa tayari, ni rai yangu kwa Serikali kuharakisha mapitio ya rasimu za Sheria hizo ili sheria hizo ziwasilishe Bungeni haraka iwezekanavyo ili kusaidia kudhibiti hatari ya maovu wayapatayo Watanzania kutokana na ukosefu wa sheria hizo nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri. Naomba kupata utekelezaji katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, niliomba minara kwa vijiji vya Gwata, Vikumbui, Kusui, Kitanga na Kihare lakini hadi leo toka mwaka 2011 nilipopeleka maombi na kujaza fomu maalum ya kuomba minara bado ombi hili halijatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, naomba haraka iwezekanavyo kwa kijiji cha Gwata na Vikumburu, kwani changamoto ya mawasiliano imekuwa kubwa zaidi kwa maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, nawatakia utekelezaji mwema wa maombi yangu na kazi za Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa nia ya kuwawezesha Watanzania kuwa katika ulimwengu wa kileo.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo dogo katika suala hili la kupata mawasiliano katika baadhi ya maeneo hasa vijijini. Nakuomba Mheshimiwa Waziri uhakikishe kwamba minara ya Tigo inawekwa zaidi ili nikiwa kwetu kijijini Pandani nisiwe na usumbufu kwa mitandao yote.

Mheshimiwa Spika, nakuomba sana iwepo Sheria ya Kuzuia Kutumia Mitandao kwa njia zisizoendana na mila, silka na tamaduni zetu za Kitanzania kuonyesha picha za ngono sio jambo jema kwenye mitandao.

Ni vizuri kuwajenga vijana wetu katika tamaduni zenye heshima. Siyo vizuri kufungua simu ghafla unakuta picha za ngono za jinsia moja, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri hili jambo tulitafutie dawa ya kuweza kudhibiti hii hali kwani jamii yetu inaelekea kubaya sana.

Mheshimiwa Spika, wizi wa fedha kwenye matumizi ya simu naomba pamoja na kazi nzuri mnayofanya hili liangaliwe kwa umakini mkubwa kwani makampuni haya ya simu yanawaibia sana Watanzania maskini, walipakodi wawahurumie.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya simu ni maongezi ya watu wawili, lakini utashangaa kuona kwamba mazungumzo yote wanayajua wafanyakazi na *sms* zote wanazijua je, inakuwaje? Naomba kueleweshwa. Zaidi ya hayo unajitahidi na timu yako, ila upewe fedha za kutosha ili ukamilishe malengo.

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza sana kwa dhati Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa - Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, vilevile Naibu Waziri Mheshimiwa January Yusuf Makamba kwa namna wanavyoshirikiana na moyo wao wa uzalendo kwa Watanzania na nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, makampuni ya Zantel na Vodacom yanaongoza kuwaibia Watanzania kwani *voucher* zao hutumika muda mfupi tofauti na fedha ambazo wateja wamenunua na kuweka. Vilevile *promotions* mbalimbali zinalenga katika kuwaibia wananchi kwa kuwapatia ushindi watu kidogo sana, kadhalika hii inafanywa na makampuni yote yanayotoa huduma za simu za mkononi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kupitia *TCRA* wayabane makampuni haya yasiwanyonye Watanzania. Pia *TCRA* iyabane makampuni yanayoachia ujumbe *(sms)* zinazosambazwa zenye ujumbe wa uchochezi, kashfa, fitina na kadhalika yahakikishe vitu kama hivyo haviendelei kusambazwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, namuomba Waziri asaidie kupatikana kwa huduma nzuri ya mawasiliano kwa Shehia yangu ya Bumbwisudi katika Jimbo la Dole, Shehia ya Mwera hasa katika kijiji cha Misufini, Kimara vyote vikiwa ndani ya Jimbo la Dole.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Kata 72 zilizopata wazabuni kwa Mkoa wa Simiyu na ile Wilaya ya Meatu, napenda kushauri kwamba kwa kuwa tayari kuna mnara wa Airtel kwenye Kata ya Mwabuzo na wanapata mawasiliano vizuri, naishauri Wizara ihamishe mnara

utakaojengwa hapo Mwabuzo uhamishiwe Kata ya Imalaseko ambayo haina mtandao kabisa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, kwa kufuatana na jina la Wizara na mimi nachangia kwa njia hiyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu na Watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, bajeti ni ndogo sana, imeshuka sana kwa upande wa maendeleo kwa 21% hii ni kama fedha itapatikana, wasiwasi wangu ni mipango yote mizuri itashindwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCAF)* mimi napenda kwanza na naomba nisisitize athari ya watu wanaoishi sehemu ya watu wanaishi kwa maeneo yasiyofikiwa na simu *(remote areas inaccessible by phone)*, watu kukosa kuwasiliana na wengine hata wakati wa hatari ya ugonjwa, wafugaji kuibiwa ng'ombe, kutokea vita vya vikundi kama kule Kiteto na Yaeda Chini na Mbulu.

Mheshimiwa Spika, pili nashukuru kwa miradi niliyopata kwenye Kata tatu Wilayani Mbulu, Kata 17 hazikuwa na mawasiliano kabisa, kuna ahadi za Kata za Kainam, Muray Tumati, Tlawi na Daudi ambayo nne za kwanza hali ni mbaya sana, naomba Wizara ifanye mpango mbadala ili tupate mtandao wa simu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikutano kwa kutumia TEHAMA naipongeza Serikali kwa kuamua kuanzisha jambo hili kwa njia hii ya mikutano mingi itafanya kwa bei ndogo sana, *big up.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano naishauri Serikali ifanye juhudi zaidi ya kuunganisha sehemu za nchi ambazo hazijaungwa na Mkongo huu ziungwe ili zipate mawasiliano ya simu, *TV and Internet* kamili kwa mfano hivi sasa Wilaya ya Mbulu aina *internet service* kwa sababu haina 3G.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. RIZIKI SAID LULIDA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani na pongezi za dhati kwa Waziri Mheshimiwa Makame Mnyaa Mbarawa, Naibu Waziri Mheshimiwa January Makamba na Katibu Mkuu. Mawasiliano ni

maendeleo hivyo sehemu zinazofikishwa huduma za mawasiliano maendeleo huwa ya haraka sana.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Lindi upo nyuma kuliko mikoa yoyote Tanzania hivyo kwa maana hii, Mkoa wa Lindi utadumaa kimtazamo wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto kwa kuwa Mkoa wa Lindi tupo nyuma kwa kuwekewa minara na watu kupanda juu ya miti kutafuta mawasiliano ningeomba yafuatayo:-

*(i)* *Airport* ya Lindi na eneo la jirani upelekwe mnara.
(ii) Lindi vijijini imeathirika sana hakuna mawasiliano na maeneo yafuatayo:-
(a) Ngongo – Milola;
(b) Mchinga- Kijiwai;
(c) Chikongi – Nangaro;
(d) Mkwajuni – Mbwakuru – Mipingo – Matapwa; na
(e) Nyangamara – Nahukahuka – Mandwanga.
(iii) Kilwa – Nangurukuru – Mbwemkuru - Rushungi – Kilabijeranje.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nianze na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kwa kuwa Serikali imeridhia na kukubali uwepo wa Chuo Kikuu hicho huko Mbeya ni vyema Serikali ikaonyesha utayari wa kukiendeleza Chuo hicho kama ilivyofanya kwa Chuo cha Nelson Mandela – Arusha au Chuo Kikuu Dodoma *(UDOM)* kukamilisha ujenzi na mahitaji ya majengo mengineyo kupitia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Kwa umuhimu na uhitaji wa chuo hicho na hususan Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuwa na chuo cha mfano tunaitaka Serikali kujiangalia upya na kuridhia chuo kuendelezwa aidha kulipa fidia kwa wananchi walionyang'anywa ardhi zao kupisha ujenzi wa chuo hiki Mbeya.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa mapato kutokana na Mtambo wa Kuhakiki na Kusimamia Huduma za Mawasiliano *(TTMS)* mapato ambayo yanapelekwa Hazina, ni vyema sasa fedha hizo zikapelekwa moja kwa moja katika Mfuko wa Mawasiliano Vijijini *(UCAF)* ili mfuko uwe na nguvu ya kuimarisha mawasilino vijijini badala ya kutegemea wahisani na makampuni ya simu na watakodisha minara yao watakayojenga kwa makampuni na mfuko utakuwa endelevu kuweza kukarabati au kujenga minara pale itakapohitaji na jambo hili likikamilika mapato hayo yatarejeshwa tena Hazina.

Mheshimiwa Spika, Serikali kutokutoa kipaumbela katika Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia kwa kuiwezesha kifedha kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais, Tume imekuwa ikipata fedha kidogo sana ikiwemo pia *DIT* na *TAEC*, haya

ni maeneo muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Hivyo basi lazima yatizamwe kwa namna ya kipekee na kuwezeshwa ili kutimiza malengo yao kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua hatua ya mazungumzo ya hisa za *TTCL/Airtel* yamefikia wapi kwani kuchelewa kufikia maamuzi mapema kunakatisha tamaa na kuchelewesha *TTCL* kujiimarisha.

Mheshimiwa Spika, kadhalika napenda kulipongeza Shirika la Posta na Simu pamoja na mabadiliko makubwa kutokana na maendeleo ya teknolojia lakini wanaendelea kuwepo ndani ya ushindani. Hivyo Serikali isaidie juhudi za Shirika la Posta.

Mheshimiwa Spika, mwisho anuani za makazi hakika mchango wa TCRA katika mradi huu ni wa kupongezwa sana na sasa inaonekana ni jukumu la *TCRA* na Serikali kujitoa hii siyo sahihi kabisa, Serikali lazima itimize wajibu wake wa kutoa fedha kwa mradi huu ili ukamilike kwa haraka na kwa gharama stahiki, tunavyochelewa ni kuongezeka kwa gharama za mradi pia.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, mimi nilitaka kupata majibu kutoka Wizara hii kwamba ni kwa nini Halmashauri karibu zote nchini hazilipwi *service levy* ya minara ya simu inayowekwa kwenye Halmashauri husika? Nataka kupata majibu Wizara itaendelea kuzinyonya Halmashauri hizi mpaka lini na kwa nini hakuna hatua ambazo zinachukuliwa ili kumaliza utata huu, huku wamiliki wa uwanja wakalipwa dola 750 – 100 kwa mwezi?

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya kwenye Wizara hii. Jitihada zao zinaonekana, hongereni sana endeleeni kuchapa kazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zao bado kuna baadhi ya maeneo hayana mawasiliano ya kutosha kwa mfano Wilaya ya Pangani kuna kijiji kina biashara kubwa sana ya samaki lakini mawasiliano yako *very poor. Airtel* ilikuwa inapatikana zamani lakini leo mpaka utegee sehemu, Vodacom hawapatikani kabisa na Tigo nayo inapatikana kwa mashaka mno. Ninaiomba Wizara katika maeneo mtakayoyapendekeza kuboresha mawasiliano na eneo hilo mlipe kipaumbele kwani kuna biashara kubwa sana watu wasizunguke na fedha mikononi.

Mheshimiwa Spika, vilevile naiomba Wizara iangalie sana maeneo hatarishi ambayo hayana mtandao kabisa na majambazi huwa wanatega maeneo hayo na kuwateka watu na magari mara kwa mara kwa mfano eneo lililopo kati ya Mikumi na Iringa wanateka sana magari na sababu kubwa

hakuna mawasiliano. Tafadhali naiomba Wizara itoe kipaumbele kwenye eneo hilo muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iangalie gharama za mawasiliano ya simu za viganjani hususani kwa mitandao tofauti, hali ambayo watu wamekuwa wakimiliki kazi za simu zaidi ya moja.

Mimi mwenyewe nina *line* nne za simu. Pia kudhibiti utozaji tofauti kati ya kampuni moja na nyingine kwani *TCRA* ipo na ndiyo kazi yake ingawa *TCRA* nao wanafanya kazi nzuri sana sasa hivi lakini waliangalie na hilo.

Mheshimiwa Spika, mimi nimalizie kwa kuwapongeza zaidi Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi zao nzuri ingawa wanapewa fedha ndogo lakini kazi zao zina matumaini.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na tulivyoweza kupata wote waliotakiwa kuchangia katika Wizara hii wameweza kuchangia isipokuwa wale waliojadili zaidi kama akina Mheshimiwa… *(Kicheko)*

Naomba sasa nimuite Naibu Waziri. Wamegawana muda kwamba Naibu Waziri dakika 30 na Waziri dakika 45. Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa shukrani. Kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, vilevile nashukuru na kukupongeza kwa uongozi wako mahiri wa taasisi hii nyeti hasa katika kipindi hiki kigumu ambacho demokrasia ya vyama vingi imechachamaa

Mheshimiwa Spika, unatuongoza vizuri, umepasua dari na wapo wasichana wengi ambao wanataka kuingia kwenye siasa kwa sababu ya uongozi wako. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda niwashukuru wana Bumbuli, wapiga kura wangu kwa kuendelea kuniamini, wamenibeba katika mabega yao hadi Watanzania wengine wakaniona, hadi Rais akaniona, nawashukuru sana. Nisingeweza kusimama hapa leo bila wao.

Napenda niwahakikishie kwamba zile changamoto zetu ikiwemo kiwanda chetu cha chai kilichofungwa zitakwisha, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliniahidi kwamba atakuja ataongoza na mimi kuja Mponde tumalize hilo tatizo. Napenda niwahakikishie kwamba mpaka mwakani kila kijiji Bumbuli kitapata umeme, watoto wetu watapata viatu vya kuendea shule, mikopo itaendelea, kwa hiyo tupo pamoja, niko nanyi.

Mheshimiwa Spika, napenda niishukuru familia yangu, mke wangu na watoto wangu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri…kabisa kabisa. Wanajua tu kama wewe upo.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda niwashukuru Waziri, Katibu Mkuu, hawa ni Maprofesa, Waziri ni Profesa, Katibu Mkuu Profesa, mimi nimekaa katikati siyo Profesa, lakini kwa namna tunavyofanya kazi wamenifanya na mimi niwe Profesa mdogo, sioni kama nanyanyasika.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru vilevile watendaji wa Wizara na taasisi za Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya, tunafanya kazi kwa upendo na ushirikiano mzuri, hakuna migogoro, kazi zinaenda ingawa katika mazingira magumu kama walivyoyasema Wabunge waliochangia hoja yetu.

Vile vile napenda kuishukuru Kamati inayoongozwa na Mheshimiwa Peter Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini. Lakini vile vile napenda kuwashukuru Wabunge wote kwa kweli kwa kuonesha ushirikiano kwetu, kwa kuonesha dhamira ya kutusaidia, kwa kutambua umuhimu wa Sekta yetu, kwa kutambua mazingira yetu magumu.

Kwa kweli tumefarijika sana kwa namna mlivyochangia hoja yetu na kwa kweli ni kielelezo cha mahusiano mazuri yaliyopo baina yenu na sisi kama mnavyofahamu.

Tumezipokea pongezi nyingi mlizotupa leo. Lakini tumezipokea pongezi hizi siyo kama sifa bali kama deni. Tunalo deni kwenu kutekeleza yale mnayoyategemea kutoka kwetu.

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kujibu hoja zilizolewa. Lakini kabla ya hapo naomba vile vile nitoe pole kwa misiba inayoongozana inayotokea katika tasinia ya filamu Tanzania. Hivi majuzi wenzangu hawa, rafiki zangu walifiwa na mwenzao Bwana Kuambiana, wakafiwa na binti, mwenzetu, rafiki yetu Rachel na jana mwendeshaji, mtengenezaji picha mashuhuri George Tyson alifariki kwa ajali ya gari akitokea hapa Dodoma. Kwa hiyo, nataka niwape pole vijana wenzangu kwenye tasinia ya filamu hii niwambie tuko pamoja katika misiba hii mizito.

Mheshimiwa Spika, ninayo maeneo mawili matatu ya kujibu kwenye hoja. La kwanza, lililochangiwa na Wabunge wengi na kwa kweli karibu wote walioachangia hoja yetu, na lenyewe ni la mawasiliano vijijini.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia katika kipindi cha miaka 6, 7, 8 iliyopita mapinduzi makubwa sana kwenye sekta ya mawasiliano. Sekta yetu inaongoza kwa ukuaji, mwaka huu tu peke yake imekua kwa asilimia 22 na wastani wa ukuaji katika miaka mitano iliyopita ni karibu asilimia 19, 20. Sekta yetu imetoa mchango mkubwa sana katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Sekta yetu ni sekta ya uchumi kwa maana ya sekta inayoajiri, sekta inayozalisha, sekta inayolipa kodi. Lakini vile vile ni kiwezeshi cha sekta nyingine za uchumi. Sasa hivi hakuna sekta yoyote ya uchumi iwe mabenki, iwe sekta ya fedha, sekta ya uzalishaji viwandani, sekta ya utalii ambayo haitegemei mawasiliano. Kwa hiyo sisi tunafarijika kwamba tunasimamia shughuli muhimu sana ambayo imebadilisha sura ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini mapinduzi haya katika sekta ya mawasiliano hayana maana yoyote kama yatawaacha baadhi ya Watanzania wenzetu nje, hasa Watanzania wanaoishi maeneo ya vijijini. Sasa kwa kubaini hilo, Serikali ilianzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili utoe huduma, utoe ruzuku kwa makampuni ya simu kupeleka mawasiliano kule ambapo makampuni ya simu yamesema au yanadhani kwamba hakuna mvuto wa kibiashara.

Mfuko huu ulianzishwa hapa Bungeni kwa Sheria ya Bunge mwaka 2009. Lakini wote mnafahamu kwamba mfuko huu ulichelewa kuanza kazi mpaka 2009/2010. Sasa bahati mbaya sana katika mara kadhaa ambazo tumejaribu kuweka mazingira ya kuweka ruzuku kwa kupitia fedha za mkopo wa Benki ya Dunia, makampuni ya simu yamekuwa hayaonyeshi mwamko mkubwa sana katika kuingia hizo zabuni. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Bwana Ussi leo asubuhi na ni kweli kwamba tulivyotoa zabuni ya kwanza ya Kata 152, ni Kata 52 tu zilizopata wazabuni.

Kwa hiyo, kwa sababu utaratibu huu ni wa hiari, kwa hiyo pamoja na Serikali kuweka mpango wa ruzuku kuyaongezea makampuni fedha yaende kule ambapo yanadhani kujenga ni gharama kuliko biashara iliyopo pale, bado makampuni yale yamekuwa yanasuasua. Tumekuwa tunaendelea kuzungumza nao na kuwahimiza kwamba wapeleke mawasiliano vijijini. Sasa Waheshimiwa Wabunge mmekuwa mnasema hapa na mmekuwa wa kweli kwamba utaratibu huu unachelewa sana. Sasa sisi mwaka jana tuliamua kwamba utaratibu ule wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote wa zile tenda peke yake hautoshi.

Lazima tuchukue hatua kubwa zaidi na za haraka zaidi ukizingatia umuhimu wa mawasiliano kwa nchi yetu ili tuweze kuimaliza kazi hii mapema.

Mheshimiwa Spika, hata sisi tunafadhaika sana kwamba hapa bungeni anasimama Mbunge anaomba kupata mawasiliano kwenye maeneo ya Jimbo lake na anaiomba Wizara, lakini bahati mbaya Wizara haina fedha za kupeleka mawasiliano, haijapangiwa fedha na Bunge za kupeleka mawasiliano. Kwa hiyo, unaniomba mimi, unamuomba Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri anachofanya na yeye anaenda kuomba tena kwa watu wengine. Sasa tulidhani kwamba hiyo siyo sahihi, kwa sababu tunapoahidi hapa lazima tuwe na uhakika kwamba ile ahadi mmetupa uwezo wa kuitekeleza.

Anaposimama hapa Waziri wa Maji au Waziri wa Nishati anaposema kwamba tunapeleka umeme kwenye vijiji kadhaa, anaongea kwa uhakika kwa sababu fedha mmempangia ninyi Bunge. Sasa sisi siyo hivyo. Sasa lakini tukaona kwamba hatuwezi kuendelea kunung'unika, kulia lia kwamba mnatuomba minara hatuna fedha.  Kwa hiyo, tukaamua tutafute hizo fedha sisi kama Wizara na tuliamua kutengeneza andiko. Kwanza, la kubaini maeneo yote yasiyo na mawasiliano nchini, je, yanahitaji minara kiasi gani na hiyo minara ina thamani gani.

Kwa andiko lile kubwa lilitueleza kwamba ili nchi yote ipate mawasiliano ya simu za mkononi, inahitajika shilingi bilioni 328. Sasa bahati mbaya hali ya fedha hapa mnaifahamu Hazina hawana hiyo fedha. Kwa hiyo tulichoamua ni sisi kuanza kuhangaika kutafuta hizo fedha kwa namna nyingine.

Kwa hiyo mimi mwenyewe nikasafiri nikaenda India kwenda kufanya mambo mawili. Kwanza kutafuta teknolojia rahisi ya kupeleka mawasiliano vijijini, kwa sababu teknolojia inabadillika kila siku.

Teknolojia ya sasa inategemea minara inayoendeshwa kwa genereta za *diesel* na asilimia 40 ya kuendesha mnara inatumiwa na mafuta ya *diesel* ambayo yanaibiwa mengine hayafiki.  Kwa hiyo, watoaji huduma wanaposema kwamba minara ni ghali kuliko wateja walioko kwenye eneo hilo au uwezo wa uchumi wa watu waliopo kwenye eneo hilo, wakati mwingine wanalinganisha kwa gharama ambazo ni kubwa kuliko ambavyo inaweza kuwa.

Kwa hiyo, nikaenda nikatembea katika vijiji vya India kuona wenzetu wanafanyaje, kwa sababu wao wamejitahidi sana kupeleka mawasiliano vijijini. Tukafanikiwa kupata teknolojia rahisi ya kupeleka mawasiliano vijijini ambayo inatumia minara inayoendeshwa kwa sola. Kwa hiyo, kazi ya kwanza ya kutafuta teknolojia rahisi.

Ya pili, kutafuta fedha, kwamba wenzetu wa India wanao mfuko, wanayo *facility* wanaita ya mikopo ya gharama nafuu kwenye miradi kama hii.

Kwa hiyo, tulipeleka andiko letu tukitaka mkopo wa dola milioni 154 na mimi binafsi nikazungumza na viongozi wa Serikali ya India na mazungumzo yalienda vizuri na tulikubaliwa kupewa zile fedha kuja kujenga minara nchi nzima. Lakini bahati mbaya tulivyokubaliana ndiyo uchaguzi ukaingia India, kwa hiyo, inangojewa Serikali mpya ikae iingie madaraka ili hatimaye fedha zile ziweze kutolewa.

Kwa hiyo, tunategemea tukipata hizo fedha dola milioni 154 zitatuwezesha kwa kiwango kikubwa kuifanya kazi hii. Lakini hatua ya pili tuliyochukua, wacha kutafuta fedha hizo, ni kubadilisha utaratibu wa kutoa zabuni kwa makampuni haya ya simu kwa ajlli ya minara.

Huko mwanzo tulikuwa tunatoa zabuni kwa makampuni ya simu halafu yenyewe yanatafuta wajengaji minara. Kwa hiyo kunakuwa na manunuzi ya mara mbili, manunuzi kutoka Mfuko kwenda kwenye Makampuni ya simu na manunuzi kutoka makampuni ya simu kwenda kwa makampuni yanayojenga minara.

Kwa hiyo, utaratibu mpya sasa hivi ni kufanya manunuzi moja kwa moja, kutoa zabuni moja kwa makampuni yanayojenga minara ili mradi yatuhakikishie kwamba tayari yapo makampuni ya simu ambayo yatatumia minara hiyo na sisi tunafanya kazi ya kuzungumza na kampuni ya simu ili yatumie minara itakayojengwa katika utaratibu huu mpya.

Hatua ya tatu, tunayochukua ni kutafuta fedha nyingine ya ziada na tunapenda kuishukuru sana Kamati ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Peter Serukamba na Wajumbe wote kwa kuunga mkono na kupendekeza kwamba zile fedha ambazo zilikuwa zinatoka kwenye Mtambo wa Ufuatiliaji wa Mawasiliano *(Telecommunication Traffic Monitoring System)* ambazo zimeanza kwenda Hazina takribani shilingi 1,700,000,000/= kwa mwezi basi ziende kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili tuweze kupata fedha za ziada kwa ajili ya kujenga minara.

Sisi pendekezo hili tumelipenda kwa sababu tunahitaji hizo fedha, lakini tunapenda kuwahakikishia wenzetu kwamba hili siyo jambo la daima. Ni kwamba ni mwaka mmoja au miwili halafu tutakapokuwa tumemaliza kazi ya ujenzi wa minara basi wenzetu wataendelea kuchukua fedha hizi na wakati huo zitakuwa zimeongezeka.

Mheshimiwa Spika, jambo la nne ambalo tunafanya katika kuhakikisha tunaharakisha upatikanaji wa mawasiliano vijijini ni kuimarisha Shirika letu la Simu *TTCL.* Huko nyuma *TTCL* ilikuwa inatumia teknolojia ambayo haitumiwi na watu wengi, kwa hiyo minara mingi ya *TTCL* ilikuwa imekaa tu bila kutumika.

Kwa hiyo, Serikali ikaamua kutoa masafa mapya kwa Kampuni hii ya Simu masafa ya *GSM* ambayo ni sawa na masafa ya kampuni nyingine zote tunazotumia sasa hivi za *Vodacom, Airtel, Zantel* na *Tigo* na nyinginezo ili kampuni hii iweze kushindana na kutoa huduma ambayo itatumiwa na Watanzania walio wengi.

Kazi hii imekamilika, na pale ambapo *TTCL* inajenga minara wananchi wasiwe na wasiwasi watapata mawasiliano ya mitandao yote kwa sababu *TTCL* inaingia kwenye makubaliano ya *roaming* na makampuni haya mengine. Lakini vilevile bado iko shughuli nyingine ya kuimarisha zaidi *TTCL* zaidi ya masafa na hiyo tutaizungumza hapo baadaye, ikiwemo kuondokana na ile ndoa na *Airtel.*

Lakini hatua nyingine ambayo mimi inanipa matumaini makubwa ni kwamba Serikali sasa ipo kwenye mazungumzo na mazungumzo hayo yako kwenye hatua za mwisho na Kampuni ya Simu inayomilikiwa na Serikali ya Vietnam inaitwa *VIETTEL*. Hawa walikuja miaka ya nyuma kutaka kushirikiana na *TTCL* lakini ikashindikana. Kwa hiyo sasa hivi wamekuja wenyewe na walichokuja kutuambia ni kwamba sisi ni mashuhuri na ni wataalam wa kupeleka mawasiliano vijijini ndiyo shughuli tunayofanya Vietnam na kwenye nchi ambazo tunafanya kazi.

Wakasema kwamba wao namna yao ya kusambaza mawasiliano ni kujenga mkongo wa mawasiliano nchi nzima. Wame-*commit* kujenga kilometa 13,000 za *fiber optic network* na sisi Serikali tunazo 7,500 tumezijenga katika miaka mine, wao wanasema ndani ya mwaka mmoja wanajenga kilometa 13,000 wanafikisha mkongo huu kwenye kila Wilaya na mnara kwenye kila kijiji.

Sasa walivyoleta hii habari nikasema mbona hii ni nzuri kuliko uhalisia. Kwa hiyo, tukafanya uchunguzi kwamba kampuni hii imewahi kufanya kazi wapi. Imewahi kufanya kazi Msumbiji na ni kweli wanayosema kwamba Msumbiji miaka kadhaa iliyopita kwenye *ranking* ya nchi zilizoeneza mawasiliano Afrika ilikuwa iko chini chini, lakini sasa hivi ni namba 3 kutokana na wao kwenda kule na sasa hivi kampuni ile ni namba moja kwa mawasiliano Msumbiji. Kwa hiyo na sisi tunazungumza nao na kama tutakubaliana mkataba wetu, makubaliano yetu ni kazi hii ya kupeleka mawasiliano nchi nzima wawe wameimaliza ndani ya mwaka mmoja na wao wameahidi kwa maandishi kwamba wataweza kufanya hivyo.

Kwa hiyo, pamoja na hatua zote hizi hii kampuni mpya kama tutafikia makubaliano, basi Waheshimiwa Wabunge muwe na uhakika kabisa kwamba katika mwaka mmoja nchi yetu itapata mawasiliano kwenye kila kijiji kama ilivyofanya kule Msumbiji.

Hatua nyingine ambayo tunachukua ni kuweka mpango maalumu wa kuweka mawasiliano katika mipaka ya nchi yetu. Wote tunafahamu na Wabunge kadhaa hapa wamezungumza kwamba mawasiliano siyo shughuli ya uchumi tu hasa katika maeneo ya mipaka yetu, lakini shughuli ya kiusalama. Na sisi tunakubali kwamba yapo maeneo nchi yetu ina mipaka mingi, inapaka na nchi nyingi na kwamba ni muhimu na baadhi ya mipaka iko mbali na miji.

Lakini lazima mipaka hii ihakikishiwe usalama na kwa sababu mipaka hii inalindwa, lazima wale wanaolinda mipaka hii wawe na uwezo wa kuwasiliana na wenzao katika kuhakikisha kazi yao ya ulinzi wa mipaka inafanyika vizuri.

Sasa kutokana na umuhimu huo wa kuhakikisha kwamba nchi yetu inalindwa na mipaka yetu iko salama, tumeamua kuweka mpango maalum sasa wa kupeleka mawasiliano mipakani na hii haitaenda kwa zabuni. Ni kwamba Serikali moja kwa moja italipia gharama asilimia 100 za kujenga minara katika maeneo haya.

Tumeshaanza, baadhi ya makampuni yameshachagua maeneo kwa sababu tumeorodhesha maeneo yote ya mipakani ikiwemo maeneo katika majimbo ya Masasi, Ngara, Karagwe, Manyovu, Kigoma Kusini, Mpanda, Kalambo, Nkasi, Nyasa, Ludewa, Kyela, Longido na kwingineko. *(Makofi)*

Sasa hili ni muhimu, ni muhimu sana kwa ulinzi na ulama wetu. Kwa hiyo tupo kazi hiyo tunaendelea nayo na nawahakikishia kwamba kutokana na umuhimu wa usalama wa mipaka yetu, Serikali itagharamia minara hiyo kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nataka nimalize hili suala la minara kwa kusema jambo lifuatalo:- Kwamba Wizara yetu ina mambo mengi makubwa, mazuri na mengi yanaenda kimya kimya, mambo ya utafiti, mambo ya uvumbuzi. Tunacho chuo kikubwa kabisa pale Nelson Mandela ukienda pale unajisikia fahari kuwa Mtanzania. Kazi kubwa inafanyika pale *Dar Tech. (Dar es salaam Institute of Technology.*

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kinaanza kunawili na chenyewe tumekitengea fedha kwa ajili ya kukiendeleza zaidi. Na mambo mengine mengi pale *COSTECH* kazi nyingi nzuri inafanyika sana. Taasisi ya *Nuclear* pale Arusha wanafa kazi nzuri. Kwa hiyo, yapo mambo mengi, mengi, mengi mazuri yanayoendelea. *(Makofi)*

Tunafahamu kwamba Watanzania wengi katika Wizara yetu wanaangalia suala la mawasiliano na michango mingi iliyotolewa hapa na

Wabunge inahusu masuala ya mawasiliano, na sisi tunajua kwamba tutapimwa mimi na Mheshimiwa Waziri na Watendaji kutokana na kupatikana kwa mawasiliano kwenye nchi hii. Sasa siyo vema kama ni mwanasiasa kijana na unajaribu kufanya kazi yako ukashindwa kwa shughuli ndogo kama ya kupeleka mawasiliano kwa nchi nzima. Kwa hiyo, kwa kufahamu kwamba tutapimwa kwa hili, tafsiri yake ni kwamba tutahakikisha linafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika nataka niwaambie Watanzania wote wanaonisikiliza kwamba msiwasulubu Waheshimiwa Wabunge kwa ahadi walizotoa kwenye minara kwa sababu ahadi zile wamezitoa kutokana na sisi tulivyowaambia. Kwa hiyo, hakuna Mbunge aliyetoa ahadi hewa. Ahadi iliyotolewa ni kutokana na ahadi yetu sisi. Kwa hiyo, na sisi tutajitahidi kuitimiza kuhakikisha kwamba Wabunge hawa waliotoa ahadi na chama chetu hakishindwi kutokana na kutokuwepo kwa mawasiliano. Hili tutalifanya kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nizungumzie suala lingine linalohusu ubora wa huduma za mitandao pamoja na udanganyifu unaofanyika kwenye mitandao ya simu. Waheshimiwa Wabunge wamelizungumza sana na wamelijadili katika michango yao. Ni kweli kwamba teknolojia hii imeleta changamoto. Teknolojia ni sawa na kisu. Kisu unaweza ukakitumia kukata nyanya, kukata nyama, na kukusaidia kwenye shughuli za nyumbani. Lakini kisu vilevile unaweza ukakitumia kumdhuru mtu. Kwa hiyo, wapo watu wanaotumia teknolojia vibaya. Sasa sisi Serikali wajibu wetu ni kuhakikisha kwamba teknolojia hizi zinatumika katika madhumuni yaliyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa Wabunge wamelalamikia na wamezungumzia na wako sahihi kabisa, kuhusu wananchi kupata huduma na kukatwa fedha kwa huduma ambazo hawakuziomba, miito ya milio, nyimbo na huduma nyinginezo, hili ni tatizo kubwa. Sasa sisi tumefanyaje?

Mheshimiwa Spika, tumeanza kutengeneza Kanuni ambazo zitalazimisha makampuni ya simu kutomkata mtu bila ridhaa yake ya maandishi na tumepeleka Mamlaka ya Mawasiliano agizo la kuanza mchakato wa utengenezaji wa Kanuni hizo. Na kwa sababu, lazima ukae na wadau uzungumze nao, dhamira yetu ni kuweka adhabu pale ambapo unapata huduma na unakatwa bila ya wewe kuafiki au kukubali kwa maandishi kwa hiyo, hilo tutalifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tunafahamu kwamba, wananchi wengi wanalalamika kwamba, pale wanapokuwa na malalamiko kuhusu huduma hawapati majibu, simu hazipokelewi na wanabaki wanajisikia wanyonge, kwamba, umedhulumiwa hauna pakwenda. Ukipiga simu kwenye kampuni ya simu inaita tu halafu unakatwa.

Sasa cha kwanza ambacho tumeamua kufanya ni kuongeza jitihada za elimu kwa umma kuhusu namna ya kutoa malalamiko. Maana tulichobaini ni kwamba, watu wengi hawalalamiki katika njia fasaha. Kwa mfano, kuanzia Julai 2013 mpaka Mwezi Machi, malalamiko yaliyopokelewa rasmi ni 193. Sasa haya ni machache ulikilinganisha na malalamiko ambayo watu wanayatoa.

Kwa hiyo, tumeamua sasa kufungua kituo mahsusi kabisa cha kupokea malalmiko hayo kitakachokuwepo wazi saa 24.

Mheshimiwa Spika, watu wameajiriwa, kitengo kipo tayari. Lakini vilevile tutaongeza ukaguzi kwa sababu makampuni ya simu na yenyewe yana vituo vya kupokea malalamiko, hiki ni kituo cha *TCRA,* yana vituo vya kupokea malalamiko *(customer service centres)* na ukaguzi unafanyika kila baada ya miezi mitatu. Tumewaagiza *TCRA* na tunawaagiza kwamba waongeze ukaguzi wa mara kwa mara, ikiwezekana ukaguzi wa ghafla na ukaguzi wa mwezi mara moja ili kuona kama wananchi kweli wanahudumiwa na hivi vituo vya kupokea malalamiko.

Mheshimiwa Spika, lakini tunatumia teknolojia na iko mitambo ya namna tatu/nne ambayo tumeinunua kwa ajili ya kusaidia kupunguza kero na ulaghai na udanganyifu na uhalifu kwenye mitandao. Ya kwanza, ni kwamba tunao mtambo sasa ule wa *TTMS* ambao niliuzungumza, lakini una sehemu zake kwa mfano, upo mtambo unaitwa *Anti Fraud System* ambao kazi yake ni kubaini mawasiliano ya ulaghai. Mtambo huu umeanza kazi. Tumeshawakamata watu watatu ambao walitaka kuiibia Serikali karibu shilingi bilioni nane, kesi ziko mahakamani.

Vilevile kuna mtambo mwingine ambao unaanza kazi mwezi Juni unaitwa *Central Equipment Identification Register.* Mtambo huu kazi yake ni kujua kila kifaa, kila *handset* au *Ipad* au *computer* inayotumika nchini na kuitambua kama imetumika katika matumizi ya kihalifu, aidha ya wizi au uchochezi au matusi au kashfa. Na kifaa hicho (mtambo huo) una uwezo wa kuzima kwa mbali *handset* au kifaa kilichotumika na siyo kuzima tu, hata kukifuatilia hadi kilipo. Mtambo huo ni mzuri na wa kisasa na utasaidia sana kupunguza kero na hujuma na wizi na ulaghai uliopo kwenye mitandao. Lakini vilevile tunafahamu kwamba, kuna tatizo kubwa sana kwenye uhamishaji fedha, kule watu wengi ndiyo wanaibiwa.

Kwa hiyo, tunao mtambo mwingine unaitwa *Mobile Money Transactions Monitoring System* ambao una-*record* miamala yote inavyohamishwa kila siku na kila saa na taarifa hizo ni za papo kwa papo na unaweza ukajua miamala iliyohamishwa kwa njia ambayo ni ya kidanganyifu na kufuatilia pale mtu anapokuwa ameibiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tunayo *system* nyingine ambayo tunaianza katika mwaka ujao wa fedha inaitwa *Mobile Number Portability*. Kwamba, unaweza kuhama kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine ukiwa na namba yako hiyo hiyo ya simu. Kama una namba ya *Voda,* kwa mfano, unaweza kuhamia *AirTel, Tigo, Zantel* na kwingineko bila kuibadilisha namba hiyo. Na hiyo ni teknolojia mpya, tumeanza majaribio mwezi Juni na mpaka mwisho wa mwaka wote hapa mtaweza kuhama mtandao bila kuhama namba.

Mheshimiwa Spika, lakini nyingine ambayo nadhani ni muhimu, ni mfumo mzima wa usajili wa namba. Sasa kama Serikali, tumeamua kuwa *serious* kidogo kwenye hili jambo. Kwa sababu, udanganyifu mwingi unafanyika kutokana na kutokuwepo na mfumo mzuri wa usajili wa namba. Tuliamua kama nchi kwamba, kila aliye na namba ya simu isajiliwe; haukuwa uamuzi rahisi kwa sababu ulipingwa, lakini tukafanikiwa na tukatoa mwisho wa tarehe ya kusajili. Na tulitoa ruhusa ya mwezi kwa mtu ambaye hajasajili kwamba, unaweza kununua simu leo ukakaanayo mwezi ndiyo uende kusajili, tumeondoa kile kipindi kwa sababu kuna watu walikuwa wananunua simu ndani ya mwezi anafanya udanganyifu halafu anaitupa, kile kipindi tumekiondoa.

Mheshimiwa Spika, sasa moja ya tatizo kubwa ni utaratibu wetu wa vitambulisho. Imani yetu ni kwamba, tutakapopata vitambulisho vya Kitaifa, tutakuwa na uwezo wa kuwa na taarifa sahihi za usajili, lakini la pili ni uaminifu kwa wale wanaosajili kwa sababu kazi ya kusajili hatukuwa tunaifanya sisi Serikali, tuliyaachia makampuni ya simu, lakini kumetokea udanganyifu na tumechukua hatua.

Mwezi uliopita Wakurugenzi wa makampuni yote ya simu, karibu yote, walikamatwa na Polisi wakawekwa ndani kwa sababu walikiuka sheria hii ya usajili na tukafika mahali tukaelewana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda nikushukuru tena na niwashukuru Wabunge. Nawashukuru kwa kutuunga mkono na naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, kwa kunijalia kusimama hapa na mimi kuanza kutoa mchango wangu kwenye hoja hii muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe mwenyewe pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya. Vilevile naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa umakini wake katika kusimamia shughuli za Serikali. Aidha, napenda kuwashukuru Wabunge wote waliochangia hoja yetu hii ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa kutuletea michango mizuri na makini ambayo inaendeleza sekta ya mawasiliano, sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingi zimetolewa na hii ni dalili ya kwamba, Wabunge na Watanzania kwa ujumla sasa wanaelewa umuhimu wa sekta ya sayansi na teknolojia katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Aidha, katika michango hiyo imedhihirika wazi kuwa sekta ya sayansi, mawasiliano na teknolojia, hasa mawasiliano ya simu, imekuwa sasa ni kitu muhimu na miundombinu muhimu kama ilivyo Bandari, Barabara au Reli, Watanzania hawawezi kuishi bila ya teknolojia hii ya mawasiliano ya simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile imeonekana dhahiri kuwa, masuala ya utafiti ni muhimu sana katika nchi yetu, hasa tukiangalia kwamba, nchi yetu iko katika mpango wa kutoka kwenye kundi la maskini kwenda kundi la uchumi wa kiwango cha kati, ambayo ile haiwezi kufanikiwa bila kuwa na sayansi na teknolojia hapo inapofika mwaka 2020/2025. Aidha, uendelezaji wa Vyuo Vikuu vya Sayansi na Teknolojia ni muhimu sana katika nchi yetu, ili kukuza maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu imechangiwa na wachangiaji wengi. Waliochangia kwa maandishi ni 62 na kwa kuzungumza ni 25. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge wote ilikuwa ni mizuri sana na imesheheni mapendekezo, ushauri na busara za namna bora ya kuendeleza sekta ya mawasiliano, sayansi na teknolojia. Aidha, siyo rahisi kujibu kila hoja hapa, lakini tutakalolifanya ni kwamba tutatayarisha majibu yote kwa maandishi halafu tuwapelekee Waheshimiwa Wabunge kwa hoja walizozitoa.

Mheshimiwa Spika, ushauri na maoni ya Kamati ya Kudumu umezingatiwa. Vilevile maoni na ushauri kutoka kwa Kambi ya Upinzani tumeupokea na tutauzingatia. Hata hivyo, ningependa nitumie muda huu mfupi nitolee ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa hapa bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nizungumzie hoja za Kamati ya Kudumu ya Miundombinu:-

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ambayo ilitolewa na Kamati ni kuhusu Bajeti kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2014/2015 imeshuka kutoka bilioni 28 ikilinganishwa na bilioni 35 kwa mwaka uliopita. Je, Serikali inatoa kipaumbele gani katika masuala ya sayansi na teknolojia?

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha unategemea na hali ya uchumi wa nchi yetu.

Na sisi kama Serikali, kila uchumi unapoturuhusu tutahakikisha kwamba tunatenga fedha za kutosha kwa ajili ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba, suala la kutenga 1% ya pato ghafi la Taifa ni changamoto kubwa kwa sababu, *GDP* ya Tanzania leo hii ni trilioni 54. Sasa 1% ya *GDP* ni bilioni 540 kwa kweli, kwa uchumi wa Serikali yetu unavyokwenda haitakuwa rahisi kwa hii miaka ya hivi karibuni kuweza kutenga shilingi bilioni 540.

Mheshimiwa Spika, *percentage* ya *GDP* kuhusu utafiti inavyoangaliwa Kimataifa, siyo mchango wa Serikali peke yake, ni mchango wa Serikali na *private sector*. Mfano mzuri Korea, asilimia karibu 65 ya pesa za utafiti zinatoka kwenye *private sector,* inatoka kwenye *LG,* inatoka kwenye *Samsung* na makampuni mengine. Sasa hapa kwetu tuna changamoto na sisi Serikali kwa kulijua hilo ndiyo tukaanzisha mfumo mwingine kuhusu utafiti wa sayansi na teknolojia na utafiti ambao utajaribu kuhamasisha wadau mbalimbali, ili waweze kuchangia sekta ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, tunaamini mfumo huu utaanza kutumika mapema mwakani, ili kuhakikisha kwamba, *private sector* na wadau wengine wote wanaweza kufanya kazi ya kuchangia kwenye Mfuko wa Sayansi na Teknolojia. Taasisi yetu ya *COSTECH* imeanza kufanya kazi nzuri kuhusu jambo hili, kama mnavyofahamu mwezi mmoja uliopita wamepata pesa kutoka Shirika la Misaada la Uingereza karibu bilioni 83.8 ambazo ni kwa ajili ya utafiti.

Tunaamini kwamba, tukiendelea na utaratibu huu huko mbele tutakuwa tunajitegemea sana bila kutegemea pesa nyingi kutoka Serikalini, kwa sababu, kama tunavyojua Serikali yetu ina changamoto nyingi za kifedha.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyotolewa; fedha zilizoidhinishwa na Bunge zitolewe kama ilivyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuwasiliana kwa karibu sana na Wizara ya Fedha ili kuhakikisha kwamba fedha hizo zinapatikana.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu iliyotolewa na Kamati ambayo hata Mheshimiwa Naibu Waziri ameizungumza; Kamati inashauri Senti 7 za Kimarekani zinazopatikana kutoka *TTMS* kwa kila dakika zinazopelekwa Serikalini, sasa zipelekwe kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote.

Mhesimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mimi na Mheshimiwa Waziri wa Fedha tumekubaliana kwamba tutapeleka baadhi ya pesa hii kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili kutatua changamoto za mawasiliano huko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kuchangia pesa za utafiti, kama inavyoonekana kwamba pesa za utafiti mwaka huu hazikutoka, tumekubaliana tena na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba pesa kutoka kwenye *TTMS* mwezi wa Mei na mwezi wa Juni tuzipeleke kwenye Mfuko wa *COSTECH* kwa ajili ya kuendeleza utafiti.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nne iliyotolewa inasema *TCRA* iendelee kusimamia miamala ya fedha kupitia simu za mkononi inayofanywa na makampuni ya simu ili kutambua mapato yanayopatikana kutokana na miamala hiyo ya fedha.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, *TCRA* kupitia mtambo wetu ule wa *TTMS* uko katika hatua ya mwisho ya kujenga *platform* ambayo tunaita *Mobile Money Transaction System* ambayo kazi yake itaweza kutambua miamala yote na kiasi gani Serikali inatakiwa ipate kodi yake kutokana na miamala hiyo na vilevile mtambo huo utaweza kuiarifu Benki Kuu miamala gani inatembea kwenye mitandao yetu.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyotolewa na Kamati ya Miundombinu kwamba *TCRA* itoe elimu kwa wananchi watumiaji wa huduma za simu kuhusu namna nzuri ya kutumia mitandao ili kuepukana na adha ya utapeli na kuondoa dhana iliyojengeka kuwa, kampuni za simu wamekuwa wakiiba fedha kupitia miamala ya wananchi.

Mheshimiwa spika, hili kwa kweli, ni suala ambalo ni gumu na sisi tunalijua na watu wengi linawagusa, Watanzania wengi wamepata matatizo haya, lakini *TCRA* tunaweka mikakati mizuri ambayo kwa kuweka huu mtambo tutajua kila pesa inakwenda sehemu gani. Vilevile tunahakikisha kwamba, makampuni ya simu yote yanafuata Kanuni ambazo zinaweka utaratibu mzuri, ili kuilinda mali au fedha za watu wanaotumia mitandao hiyo.

Mheshimiwa Spika, kabla kampuni ya simu kupewa leseni, kwanza wanapewa leseni mbili; leseni ya mwanzo inatoka Mamlaka ya Mawasiliano ya Simu kwa ajili ya mawasiliano ya simu na leseni ya pili inatoka *BOT* kwa ajili ya miamala ya fedha, kutuma fedha kwenye mitandao.

Baada ya kupata leseni, kampuni ya simu inatakiwa lazima iweke *deposit* kwenye benki kuhakikisha kwamba, wanalinda pesa za watumiaji. Baada ya hapo kuna utaratibu ambao *BOT* kila baada ya muda inahakikisha inapitia makampuni ya simu kuhakikisha kwamba, yanafuata kanuni na sheria zote za utumaji wa pesa. *TCRA* tukishirikiana na Benki Kuu tunaendelea kulisimamia hili kwa makini na tunaamini kwamba tutalisimamia vizuri na tutafanikiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia, kuna hoja ambayo inazungumzia kuhusu utuamiaji wa mitandao. Kweli kuna malalamiko mengi kwamba, mitandao yetu inaonesha mambo machafu, kwa hiyo, iko haja ya Mamlaka ya Mawasiliano kuwasimamia.

Mheshimiwa Spika, naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba, Mamlaka ya Mawasiliano iko katika mchakato wa kuandika Kanuni, tunaziita *Regulations Online Content* ambazo zitakuwa zinasimamia hasa hiyo mitandao ya simu na mitandao ya *internet* kuhakikisha kwamba mambo yote machafu yanayopita pale tunayasimamia vizuri. Vinginenvyo, hatutaki kuona kwamba, jamii ya Kitanzania inaharibikiwa. Kwa hiyo, hili tunalisimamia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna *issue* inayohusu Serikali isimamie kikamilifu zoezi la usajili wa *line* za simu. Kweli hili ni tatizo na tunalisimamia kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri. Na tatizo kubwa kwa kweli, liko kwa mawakala. Mawakala wanaopewa kazi ya kusajili *line* za simu wao ndiyo wanafanya udanganyifu mkubwa, lakini tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba, na hili tukishirikiana na Jeshi la Polisi kwamba tunalisimamia vizuri.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine inasema Serikali ihakikishe mawasiliano ya simu yanakuwa na ubora, hususan katika suala la usikivu. Kwa kweli, hili ni tatizo sasa hivi kwa sababu zifuatazo:- Kwanza sasa hivi makampuni ya simu yamekuwa na huduma nyingi, sasa hivi kumekuwa na *M-Pesa,* kumekuwa na *video streaming,* kumekuwa na *Internet,* mambo yamekuwa mengi na masafa tuliyowapa ndiyo yaleyale. Sasa kwa kutatua tatizo hilo kuanzia mwakani tuaanza kutoa masafa mengine ya *ATE* ambayo yatapunguza kidogo huu msongamano kwenye mitandao ya makampuni ya simu na hapo tutaweza kupata mambo mazuri. Wakati huohuo tumejenga mtambo wa *TTMS* ambao

utaweza kupima ubora wa masafa na ubora wa huduma katika makampuni ya simu.

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo limezungumzwa kwa urefu kuhusu Kamati hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa Mradi wa *Postal Code* na *Symbol* za Posta. pesa zinazokwenda kwenye mradi huu ni kidogo, lakini mradi huu naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba ni mradi ambao unatekelezwa baina ya Wizara ya Mawasiliano na Halmashauri.

Halmashauri wana jukumu lao na wao wanatakiwa watayarishe majina ya mitaa, watayarishe namba za nyumba na sisi tukishirikiana pamoja ndiyo tunalikamilisha zoezi hili. Kwa hiyo tunaendelea kuhamasisha Halmashauri tukae nao pamoja kuhakikisha kwamba zoezi hili la *post code* zlinafanikiwa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja inasema Kamati inashauri kasi iongezwe katika kutekeleza mradi wa *video conferencing.* Kama nilivyosema kwenye hotuba yangu leo asubuhi kwamba Mikoa 21 kati ya 25 ya Tanzania Bara tayari imefungiwa mitambo hiyo, pia tuko katika hatua za mwisho za kuifungia Mikoa mitano huko Zanzibar vile vile na Ofisi ya Rais wa Zanzibar itakuwa imefungiwa mitambo hiyo ya *video conferencing*. Tunaamini mchakato huu utapofika mwisho wa mwaka huu itakuwa yote imekamilika na mitambo hiyo itakuwa inafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali katika kutekeleza mradi wa *E-School* iweze kufanya haraka ili maendeleo yawafikie Watanzania wote. Mradi huu kweli unafanywa na Wizara yetu lakini tunashirikiana na Wizara ya Elimu na Wizara ya Elimu iko katika mpango wa kuchukua mkopo mkubwa huko China ili kuhakikisha kwamba mradi huu unakwenda sehemu zote hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja inasema kasi ya utoaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Mkongo wa Taifa hairidhishi kwani hadi sasa fedha kiasi cha shilingi milioni 300 zimetolewa kati ya bilioni 1.1. Kweli tuna changamoto hapa, lakini Mkongo wa Taifa ni mkongo ambao wenyewe unaweza kujiendesha.

Mkongo wa Taifa sasa hivi unaweza kutengeneza pesa nyingi na tunazo pesa nyingi, naweza kusema mamilioni ya dola kwenye akaunti ya Mkongo wa Taifa na tumeomba kibali kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha ili tuweze kutumia fedha za Mkongo wa Taifa.

Mara baada ya kupata kibali hicho tatizo hili litakuwalimekwisha na ninaamini kabisa kwamba Waziri wa Fedha ataweza kutekeleza kazi hiyo mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, suala linalofuata; Serikali iendelee kushirikisha na kushawishi makampuni ya simu yaendelee kupeleka mawasiliano vijijini. Hii Mheshimiwa Naibu Waziri ameijibu vizuri, tunaifanya kazi hiyo. Mwaka 2012/2013 ni Kata 52 tu ndiyo ziliweza kupata wakandarasi lakini leo hii Kata 215 zimepata wakandarasi. Tunaamini mwaka huu unaokuja tutakwenda mara tano ya hilo ili Watanzania wengi waweze kupata huduma hii ya mawasiliano hasa walioko vijijini na kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, tuko katika mazungumzo ya hali ya juu ya kuzungumza na *VIETTEL* ambayo yenyewe inataka kuingia ubia na *Egotel* ya Tanzania ili kuweza kujenga mawasiliano vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya *TTCL* ambayo Kamati inauliza je, lini Serikali itaweza kumaliza tatizo la ubia wa *TTCL* na *Bharti Airtel*. Kwa kweli mazungumzo yanaendelea na tumekaa pamoja baina ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Fedha na *TTCL* na *Bharti Airtel* kuona jinsi gani ambavyo tutaweza kutatua hilo.

Katika kikao kilichopita kidogo hatukukubaliana bei kwa sababu Serikali tunaamini kwamba *Bharti Airtel* haikuwekeza chochote na haistahili kupata kitu au inastahili kupata sifuri, lakini vile vile *Bharti Airtel* inasema hapana kwa vile wamekwenda kufanya hesabu tena, tunaamini katikati ya mwezi unaokuja Juni watakaa pamoja ili tuweze kupata jawabu sahihi ili kuona kwamba *TTCL* inaondokana na ubia huu wa *Bharti Airtel*.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja iliyotolewa kwamba Kamati inashauri Fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya chuo cha *MUST* pamoja na ufinyu wake zitolewe kwa wakati ili ziweze kusaidia utekelezaji wa miradi na maendeleo kwani hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu ni shilingi milioni 500 tu ndiyo zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, mpaka hivi sasa kiasi cha shilingi bilioni 2.5 kilichokuwa kimetengwa katika mwaka wa fedha 2013/2014 kimetolewa na Serikali. Fedha hizi zimetolewa katika awamu mbili, awamu ya kwanza kiasi cha shilingi 543,637,500 kimetolewa katika robo ya kwanza, ambapo kiasi cha bilioni 1.955 kimetolewa katika robo ya nne. Kwa hiyo, tunaamini tatizo la pesa la *MUST* litakuwa limemalizika.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inashauri kwamba fedha kwa ajili ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela yaani shilingi milioni 300 zilizotolewa kati ya bilioni 4.5 zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha ni kidogo sana. Ushauri huu tumeuchukua na tunaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha ili kuhakikisha kwamba pesa hiyo inatolewa kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja inazungumzia kwamba Kamati inashauri taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu vipewe uhuru wa kutafuta wafanyakazi na walimu wa vyuo vikuu hivi wenyewe kwani kuingizwa kwenye uajiri wa pamoja wa Wizara Utumishi inachelewesha.

Jibu la hoja hii ni kama ifuatavyo; Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma kupitia Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kupitia tangazo namba 70 la tarehe 14 Machi, mwaka huu imeruhusu taasisi za elimu ya juu kuendesha mchakato wa ajira badala ya Sekretarieti ya Ajira. Kwa hiyo, tatizo hilo limemalizika na sasa tunaweza kuifanya kazi hiyo bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja inayosema pamoja na bajeti ya fedha za utafiti kuwa kidogo pia hazitolewi kwa wakati.

Kamati inashauri Serikali kutoa fedha iliyoidhinishwa na Bunge kabla ya kuisha mwaka wa fedha 2013/2014 ili Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* iweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kuna uwezekano wa kupata fedha hizo za maendeleo, pesa ambayo ilikuwa ipelekwe Hazina kwa ajili ya mwezi wa Mei ambayo ni karibuni bilioni 1.7 kutoka *TTMS,* sasa itapelekwa *COSTECH* na vilevile pesa ya Juni itapelekwa *COSTECH* na Mheshimiwa Waziri bado anafanya mipango mingine kuona jinsi gani ataweza kupeleka pesa zaidi huko *COSTECH*.

Mheshimiwa Spika, hizo ndiyo zilikuwa hoja ambazo zilitolewa na Kamati ya Kudumu.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja chache zilizotolewa na Kambi ya Upinzani ambazo zinatoka kwa ndugu yangu Mheshimiwa Mnyaa, nitaomba nizipitie kidogo hapa. Hoja ya kwanza, kwa nini taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume isijumuishwe katika majukumu ya msingi ili kuweza kunufaika na huduma ikiwemo na ujenzi, kwa nini isiwekwe kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano?

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipounda Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia siyo taasisi zote zilihamia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Kama ilivyo Arusha *Technical College* ambayo imebaki chini ya Wizara ya Elimu, pia na Karume imebaki chini ya Wizara ya Elimu Zanzibar. Kile ni chuo ambacho kimeanzishwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyingine ambayo inasema kwa nini Zanzibar ina taasisi moja tu iliyojumuishwa katika mradi wa kuunganisha taasisi za elimu ya juu na utafiti yaani *Last Mile Connectivity Step*. Mradi huu wakati unaanzishwa, Karume haikuwa Chuo Kikuu, Chuo Kikuu kilikuwepo cha Serikali ambacho ni SUZA na SUZA kimewekwa kwenye mpango huo na sasa hivi nafikiri unatekelezwa.

Wakati Chuo cha Tunguu hakikuwekwa, lakini vile vile tuna mradi mwingine, awamu nyingine inakuja ambayo tutaweka Chuo *Zanzibar University* pamoja na Chuo cha Karume kuhakikisha nao wanapata huduma hii.

Mhehimiwa Spika, hoja ya tatu je, ni sababu zipi zimetumika hata ikawa taasisi ya Karume na vyuo vingine visijumuishwe kwenye mradi huu! Nimeshaizungumza hiyo kwa sababu wakati tumeanza mradi, Karume hakikuwa chuo ilikuwa ni *college* tu, lakini sasa hivi imekuwa na tutaingiza kwenye awamu inayokuja na Zanzibar *University* vile vile tutaingiza.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja inasema Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kuwa na sura ya Muungano. Hili suala mara nyingi Mheshimiwa Mnyaa amelizungumza kwa jazba na vishindo, lakini kwa kweli hili suala anajua yeye mwenyewe kwamba taasisi zote za Wizara yangu zilizoko Zanzibar zina sura ya Muungano, nikianzia *TTCL*, Posta, *TCRA* ofisi ya Zanzibar wafanyakazi wote ni kutoka Zanzibar na sasa hivi tumefungua ofisi nyingine ya *COSTECH* ambayo msimamizi mwenyewe ni dada yake Mheshimiwa Mnyaa, Dkt. Afua. Na vilevile tumeanzisha *TAEC*, wafanyakazi wote ni kutoka Zanzibar.

Kwa hiyo, Mheshimiwa tutaendelea kulifanyia kazi na kama una maoni yoyote usisite kutuambia Mheshimiwa Mnyaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mohammed vilevile alitaka kujua, Kambi ya Upinzani ilitaka kufahamu ufafanuzi wa mtiririko wa fedha kwa kipindi cha miaka mitatu kwa fedha za matumizi ya kawaida. Mtiririko wa fedha wa matumizi ya kawaida zilizopatikana kwa miaka mitatu 2011 hadi 2013/2014 uliwasilishwa katika randama husika kama ifuatavyo:-

Mwaka 2011/2012 fedha zilizoidhinishwa ni bilioni 23.799, pesa iliyopatikana ni bilioni 19.966 sawa na 83%.

Mwaka 2012/2013 fedha zilizoidhinishwa ni bilioni 20.055, fedha iliyopatikana ni bilioni 18.073. Mwaka 2013/2014 fedha iliyoidhinishwa ni bilioni 27 fedha iliyopatikana ni bilioni 24. 057 sawa na asilimia 88.4.

Mheshimiwa Spoika kuna hoja nyingine; Je, lini kanda ngapi kati ya hizo saba zilizokamilisha mradi wa anuani za makazi kwa Posta.

Kama nilivyosema kwenye hotuba yangu kwamba mradi huu ulianza kwa majaribio hapa Dodoma na Arusha. Sasa hivi mradi huu unakwenda kutengenezwa, kuanzishwa hasa huko Dar es Salaam na tunategemea Mkoa wa Dar es Salaam tutamaliza ifikapo mwisho wa mwaka huu.

Kwa upande wa Zanzibar kuna maeneo mawili Zanzibar hasa Pemba, kuna sehemu moja Shehia ya Selemu na Limbani kule Wete pia zimepata mradi huu. Kwa upande wa Zanzibar kwenye Shehia ya Chwaka pia nayo itafikia kwenye mradi huu ambapo pesa zimeshatengwa kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na *issue* ambayo suala jingine linasema kwa nini mradi wa anuani za makazi na simbo za Posta na mradi wa vitambulisho vya Taifa unasuasua je, miradi hii itakamilika lini? Suala la vitambulisho vya Taifa sitaligusia hapa, lakini suala la mradi wa anuani za makazi na misimbo ya Posta nimeshalieleza kwa nini na fedha zinachelewa. Halafu kuna suala kwa nini jengo la Makao Makuu ya *PAP* halijajengwa hadi hivi sasa na kwa nini halijaripotiwa na Wizara?

Mheshimiwa Spika, jengo la *PAP* ambalo lipo huko Arusha ndiyo Makao Makuu ya *PAP* linajengwa kwa ubia kati ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na *PAP*. Sasa hivi mkandarasi ameshapatikana, kazi kubwa iliyobaki kwa sasa ni *PAP* kutafuta jengo la muda ili wawze kufanyia kazi zao pale kwa sababu kazi ya ujenzi itachukua miaka mitatu, sasa kwa wakati huo inabidi tutafute ofisi nyingine ambayo *PAP* wanaweza kufanya kazi zao. Kiutaratibu kutokana na sheria za nchi *Foreign Affairs* inatakiwa iwapatie ofisi hiyo kwa ajili ya kazi zao za *PAP*.

Wiki iliyopita tu alifika *Secretary General* wa *PAP* ofisini kwangu ili kuona kunifahamisha maendeleo haya na jinsi gani tutaweza kusaidia ili aweze kupata hiyo ofisi ya muda. Kwa hiyo, suala hilo lipo makini na tunalisimamia kwa umakini sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyaa amehoji kwa nini Mkongo wa Taifa umeunganishwa na mikongo miwili tu; *C-com, EZ*, vipi mikongo mingine *Uhurunet*, *Umojanet* na *TIMs*? Mkongo wa Mataifa umeunganishwa na mikongo mine, umeunganishwa na *C-com*, umeunganishwa na *EZ*, umeunganishwa na *SIZ* ambao unatoka Dar es Salaam kwenda Seychelles, Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani halijui hilo najua, pia umeunganishwa na TIMs kutoka Mombasa kupitia Tanga, Horohoro. Kwa hiyo, hiyo inafanywa vizuri na tunaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyingine kwa nini kuna udhaifu wa mawasiliano kuhusu kupatikana kwa picha katika runinga kuonesha vivuli, kuganda *and so on and so forth.* Kwa kweli kuna teknolojia mbili zinatumika kwenye utangazaji wa *television*. Kwenye digitali kama kuna matatizo ya mvua utapata mgando wa picha, lakini kwenye mfumo wa analojia utapata chengachenga, iko hivyo. Sasa duniani kote wanaotumia *satellite* na mifumo hii lazima ikitokea mvua kama kuna hitilafu yoyote itatokea kugandaganda kwa picha.

Hili tatizo lipo na lilikuwepo Dar es Salaama, lakini sisi kwa kulitambua hilo tukawaambia wataalamu wale waliofunga hii mitambo ya digitali waweke kitu kinaitwa *gap fillers* kuondoa huo mgandomgando ambao unatokea. Hata sasa hivi ukiangalia *DSTV* tatizo utalikuta lipo hasa kama kunatokea mvua utaona huo mgandomgando, lakini kama una analojia unaona chenga tupu na huwezi kuona kabisa. Kwa hiyo, hilo suala lipo na sisi tumelifanyia kazi kwa kuweka hizo *gap fillers* katika maeneo mengi kuanzia Dar es Salaam na sehemu nyingi ili kuondoa matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyaa anasema kwa nini kuwe na viwango tofauti baina ya makampuni ya simu! Nafikiri alikuwa nazungumzia viwango vya bei hapa. Lakini nilitaka nimwambie kwa sababu alizungumzia vilevile kwa nini mkongo umekuja lakini haukuwa na faida yoyote.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla; Mwaka 2009 Tanzania tulikuwa hatuna mkongo, tumeanza kujenga mkongo mwaka 2009. Mkongo ulianza kutumika awamu ya kwanza mwaka 2010 na kuanzia hapo bei za simu zilishuka. Mwaka 2009 bei za simu kupiga mtandao mmoja *on nets* kwa dakika moja ya wastani ilikuwa shilingi 147 mwaka 2009. Baada ya kuunganishwa mkongo mwaka 2010 bei ikashuka mpaka shilingi 93 kwa dakika moja. Mwaka 2011 bei iliendelea kushuka mpaka kufika shilingii 59 kwa dakika moja. Ukiangalia hilo ni punguzo la kwanza karibu asilimia 36, ni punguzo kubwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009 maeneo mengi kulikuwa hakuna hata mawasiliano. Kule kwetu Mkanyageni hata mawasiliano yalikuwa hakuna, lakini leo kila mtu Mkanyageni *alhabdulillah* ana mawasiliano bwana! Hizi ni faida za teknolojia na kanuni nzuri na sheria tulizoziweka. Kwa hiyo mimi nafikiri unaona kuna faida kubwa. Pia kwa upande wa *off net, off net* ni kupiga mawasiliano kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine yaani *Airtel to Zantel* au *Tigo to Vodacom* bei kabla ya Mkongo wa Taifa ilikuwa ni shilingi 292 kwa dakika moja,

mwaka 2010 ikashuka 263, mwaka 2011 bei hiyo imeshuka na kuwa shilingi 187 kwa dakika, karibu kulikuwa na punguzo la asilimia 10 na 29.

Mheshimiwa Spika, leo hii kupiga simu mtandao mmoja kwenda mwingine makampuni ya simu hawapendi hivyo ndiyo wanaanza kuleta vifurushi kwa sababu sisi Serikali tuliangusha *interconnection fee* kutoka shilingi 115 mpaka shilingi 34 kwa dakika, ndiyo sababu leo unaona kila kampuni ya simu inazungumza vifurushi.

Mheshimiwa Spika, ukichukua kifurushi kimoja kwa mfano cha *Airtel* mimi natumia sana vifurushi, shilingi 3,000 unakuwa na dakika 65 kupiga mtandao wowote kwa wiki, unakuwa na *sms* 2,000, pia unakuwa na *GB* 300. Ukifanya mahesabu utaona jinsi gani bei ilivyoshuka. Kwa hiyo, siyo sahihi kuwaambia wananchi kwamba baada ya kujengwa Mkongo bei hazijashuka, siyo sahihi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa upande wa *Internet* kabla ya mwaka 2009 bei ya *broadband* ya *gigabyte* mbili ilikuwa ni sh. 100,000/=. 2012/2013 ilikuwa ni sh. 30,000/=. Leo hii unaweza kupata kifurushi hicho hicho kwa sh. 10,000/= au 15,000/= inategemea kampuni gani unakwenda.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika gharama za huduma za furushi cha *broadband* cha *gigabyte* 40 kwa makampuni 2009, ilikuwa shilingi milioni moja mwaka 2009, leo hii imekuwa sh. 360,000/=, utaona kwamba bei imeshuka sana sana baada ya kuweka mkongo.

Mheshimiwa Spika, leo hii unaona watu wengi wanatumia *smart phones* hapa, wanatumia *Viber,* hii yote imetokana na mkongo, bila mkongo kazi hii isingeweza kufanyika, lakini tunaona kwamba Serikali imefanya kazi kubwa na tutaendelea kufanya kazi kubwa kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya Mheshimiwa Waziri Kivuli kwamba, kwa nini kuna masafa mengi hayajagawika, mpaka sasa hatujagawa masafa na tuna mpango gani. Kuna utaratibu wa kisheria unaotumika katika kugawa na kunyang'anya masafa. Huwezi tu ukakurupuka leo wewe kama Waziri ama watendaji kwenda kunyang'anya masafa ya mtu. Kuna kampuni moja pale *HITS* ilikuwa haikutimiza masharti na tumenyang'anya masafa.

Mheshimiwa Spika, kuna masafa ya *eighteen hundred megabyte,* tumeyanyang'anya masafa hayo, tumeipa *TTCL* ambayo Naibu Waziri muda

mfupi alizungumza. Kwa vile tunaendelea na utaratibu huo na tutahakikisha kwamba masafa hayo yanagawika.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kambi ya Upinzani inataka kujua kuna mpango gani wa *4G, LTG*, tunafanya nini masafa haya. Kuna utaratibu wa aina tatu wa kugawa masafa, kwanza kabisa kuna *auction*, kuna wa *high breed* wenyewe wanasema wataalam, halafu kuna *beauty contest*. *Beauty contest* mtu anakuja tu anaomba, akishatimiza masharti yale, unaweza kuumpa masafa. Halafu kuna utaratibu mwingine kwa ajili ya *auction* mnafanya mnada.

Mheshimiwa Spika, sasa tukianza kugawa hayo masafa mwakani, tutaanza kufanya *auction,* sasa hivi tumeanza kufanya stadi na tunaandika Sera ya kusimamia kugawa masafa hapa nchini. Hili ni jambo muhimu, lazima tulisimamie vizuri. Hatuwezi tu kugawa masafa kwa sababu amekuja, amekwenda, hapana na mpaka sasa hivi tumegawa masafa ya *eighteen hundred* kwa kampuni tatu na hayo masafa yamegawiwa zamani.

Mheshimiwa Spika, wakati masafa hayo yamegawika si kwa *LTG* iligawiwa kwa *Wi-Max*, hiyo ni *4G,* halafu na *smile* na kampuni nyingine. Kwa vile teknolojia inakua kila siku, masafa hayo sasa yameweza kutumika kwa *LTE*. Ukiangalia leo Dar es Salaam pale tayari mtandao wa *LTE* umeanza ambao *smile communication* inafanya. Sisi masafa ambayo tunataka kuyagawa ni masafa ambayo tutayapata baada ya kuhama kwenye mfumo wa analojia kwenda digitali, ndiyo sababu Serikali ikahimiza sana lazima tuhame kutoka kwenye mfumo wa analojia kwenda dijitali. Leo hii ninaposimama hapa wale wananchi wa kule Kahama wameanza kupata huduma ya dijitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi, Waziri Kivuli aliuliza, lakini hili suala moja ambalo linahusu ubora wa ving'amuzi. Vinga'muzi kwanza vinavyotumika kwanza na *AGAPE, Star Media* na *Basic Transmission* vina ubora unaokubalika na vinga'muzi hivi vinatakiwa vioneshe *Channel* zile za Kitaifa bure bila ya *charge* yoyote na vinafanya hivyo. Lakini kinga'muzi kwa mfano cha *Azam* na king'amuzi cha *ZUKU* vile ni ving'amuzi vilivyoko kwenye *satellite*.

Mheshimiwa Spika, kitaratibu *satellite* na wao wanatakiwa wakianza waoneshe *free to air* bila malipo na sasa hivi tunakaa pamoja kutengeneza mwongozo ambao tutawapeleka ili na wao waweze kuifanya kazi hiyo ya kuwaonesha wananchi *channel* hizo tano, bila ya malipo yoyote. Kwa vile kazi inaendelea vizuri, naomba Mheshimiwa Mnyaa uwe na amani na mambo yatakwenda vizuri tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja imetolewa na Mheshimiwa Rajab Mteketa, yeye anasema katika Kijiji chake cha Mtanganyika kuna wanawake wenye

tatizo la *Fistula* na bahati mbaya sana hakuna mtandao wa simu. Tunajua kweli kuna maeneo kuna akinamama wana tatizo hili na hakuna mitandao ya simu kwa vile hawezi kupata zile huduma zinazotoka kwenye *VODACOM*. Sasa nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote wenye matatizo haya au kwenye akinamama wenye matatizo haya kwenye Majimbo yao na hawana mitandao kule waje wawasiliane na mimi ili tupange kuonana na *VODACOM* na wao waweze kupata huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna hoja ya Mheshimiwa Naomi, anazungumzia mteja anapopiga simu kuna makato gani, analalamika kwamba akipiga simu anakatwa pesa. Kikawaida unapopiga simu hutakiwi ukatwe pesa, hata kama kuna muziki unakuja, ule muziki unakuja kama ni matangazo, lakini hatakiwi ukatwe pesa. Pesa itaanza kukatwa pale utakapoanza kusikia sauti ya mtu ambaye umemuita au labda kuwe na *voice message*, tena ukikubali *voice message*, hapo utakatwa pesa kama unaongea kawaida. Kwa hiyo, hili ni tatizo, nitalichukua, tutalizungumza vizuri na Makampuni ya Simu.

Mheshimiwa Spika, analalamika vile vile akinunua kifurushi, ameweka kifurushi leo, kesho pesa zake zimekwisha. Nafikiri Waheshimiwa Wabunge hapa kuna tatizo moja, wengi hapa tunatumia *smart phone* na *smart phone* hizi kuna *application* nyingi sana na wakati wote *smart phone* zile *application* ziko *on*. Sasa ukitia pesa na zile *application* zinakua *upgraded automatically* kwenye *system*. Sasa kama umeunganisha na mtandao, wakati wowote akikuuliza *upgrade* ukisema ndiyo, ndiyo pesa yako inakwisha.

Mheshimiwa Spika, sasa nawashauri kwamba ukiwa na *smart phone* zile *application* zote ziweke *off* kwa muda angalau uweze kupungua na utaona hilo tatizo la pesa yako haiwezi kwenda kwa urahisi kama unavyofikiria. Imeshawahi kunikuta hiyo, nimeweka pesa, dakika moja mtoto wangu amekwenda kwenye mtandao, aka-*download,* dakika mbili pesa yote imekwisha. Kwa hiyo, naomba wale wenye *smart phone* kama wana shida wakutane na Makampuni ya Simu watawaeleza jinsi ya kufanya ili waweze kuepukana na changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, pia amelalamika kwamba anakwenda kwenye misururu mikubwa ya foleni kubwa, namshauri tu Mheshimiwa Mbunge kama kuna shida namna hiyo atumie *M-pesa, TIGO* pesa, anaweza kutoa kwenye akaunti yake zaidi ya mabenki 20, hakuna haja ya kwenda benki na kukaa foleni anaweza kukaa huko na akatoa pesa yake bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Kaihula, mteja anapopiga simu hakuna, hiyo ndiyo nimeshaijibu.

Mheshimiwa Spika, kuna Mheshimiwa Haroub vile vile ameleta malalamiko yake ambayo kwa kweli ni ya msingi na sisi kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri tunaweka utaratibu ambao tutakuwa na kituo maalum kwa ajili ya malalamiko yote yanayotokea, kituo kile kitafanya masaa 24, siku saba kwa wiki, siku 36 kwa mwaka kuhakikisha kwamba mtu yeyote anaweza kupiga simu, simu zitakuwa za bure ama anaweza kutuma *sms* bure ili kuhakikisha kwamba Watanzania matatizo yote waliyonayo tunaweza kuyatatua kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 68 – WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Kif. 1001 – *Administration and Human Resource Management*… … ..Sh. 2,009,257,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Habib Mnyaa! Naomba tuwe *brief* jamani, tunatumia muda mwingi bila mafanikio makubwa.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa kweli nimpongeze Profesa kwa kuweza kujibu hizi hoja vizuri na kwa kweli sina haja sasa ya kutoa shilingi yake, isipokuwa ningependa aeleze *commitment*. Nilipozungumza haya Mashirika kuwa na sura ya Muungano nilikusudia si katika kuwa na uongozi kwa wengine na uwakilishi wa Bodi tu. Mengine kiutendaji hayana na mfano mzuri *TCRA* na ule uwakilishi wa *COSTECH*, tushukuru kwanza ni kwa juhudi za Bunge hili, hapo mwanzo hayakuwepo, lakini hivi sasa angalau imeazimwa ofisi huko katika ofisi ya Makamu wa Rais na jengo liko linatayarishwa Maruubi, lakini utendaji wa kazi mpaka sasa hivi ukitizama kile kitengo chenyewe Zanzibar, bado hakiko katika ile *level* yenyewe kama kilivyo kitengo kilichoko Dar es Salaam na sehemu zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunataka *commitment* za Mheshimiwa Waziri, je, kitengo cha *COSTECH* na cha *Atomic* kuondolewa Ikulu na kupatiwa maeneo yake na utendaji na uwakilishi ulio kamili siyo kama wa Kikanda tu

kupata picha kabisa kwamba, hizi uwakilishi wake ni sawasawa na unawakilisha Jamhuri ya Muungano vizuri. Nataka *commitment* ni lini na ana ahadi gani kuhusu uongozi na vitendea kazi vyote yakiwemo maabara. Naomba ufafanuzi Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi!

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kumjibu Mheshimiwa Mnyaa kwamba Roma haikujengwa siku moja. Hiyo kazi tumeanza mwaka jana na tunaifanya vizuri lakini aelewe kwamba hatuwezi tukajenga ofisi mkubwa Zanzibar kama Bara, kwa sababu Zanzibar Vyuo vya Utafiti ni viwili; Kizimbani na *SUZA* mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, hatuwezi kujenga *center* kama iliyoko Dar es Salaam, hata mtu yeyote ukimwambia hivyo hiyo haingii akilini. Hata hivyo, tutajenga kitu kizuri na tutahakikisha kwamba kinafanya kazi kwa maslahi ya wananchi wote wa Watanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri naye pia ni Mnyaa, kwa hiyo wanajuana kwa vilemba hao.

Mheshimiwa Profesa Kahigi! Naomba tuwe *brief* jamani, leo lazima tuanze Wizara nyingine tafadhali endelea.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru sana sote tunatambua mchango wa Wizara hii katika maendeleo na pia tunatambua mchango wa Waziri na watumishi wote katika Wizara na wataalam mbalimbali Maprofesa walio katika taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nataka kumuuliza Waziri, ni kama Wizara ina mpango mkakati wa maendeleo ya sayansi na teknolojia kuelekea kwenye uchumi wa kiwango cha kati. Kwa sababu lengo ni kwenda kwenye uchumi huo. Je, Wizara ina mpango mkakati huo? Pia ni kwamba, mpango mkakati huo ndiyo utakaowianisha ufundishaji wa aina gani ambao utatufika huko, utafiti wa aina gani ambao utatufikisha huko, ugunduzi wa aina gani utakaotufikisha huko na uhawilishaji wa sayansi na teknolojia wa aina gani utakaotufikisha huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni swali tu la kutaka kufahamu kama mnao na kama hamna je, mnaweza kuanza kufikiria kuwa nao? Kwa sababu bila mpango huo, itakuwa kila mtu anafanya kitu chake tu.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara tunao mpango wa *Science and Technology Innovation Reform (STIR)* na pesa kwenye bajeti ya mwaka huu tumepanga.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie atueleze ni chombo gani ambacho yeye mwenyewe anakiamini kwa sababu haya makampuni ambayo yanachukua milio ya sauti kwa ajili ya kwenda kuuzia Makampuni ya Simu, milio ile ambayo inauzwa na Makampuni ya Simu halafu mauzo yale, msanii mwenyewe mwenye wimbo wake hapati chochote kutoka kwenye mlio ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mlio ule unapouzwa, unaambiwa sasa umeingiziwa wimbo wako umekatwa sh. 400, baada ya siku mbili, tatu umekatwa Sh. 400, lakini zile hela haziendi kwa msanii. Nakusudia kutoa shilingi, naomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini atayaambia makampuni yaweze kulipa haki asilimia 10 kwa wasanii. Naomba aniambie sasa hivi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kumekuwa na tatizo kubwa….

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti sasa.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kumekuwa na tatizo kubwa sana kwenye eneo hili. Nianze kwa kusema kwamba sekta yetu hii imeleta fursa kubwa kubwa sana kwa vijana wetu kutafuta namna nyingine ya kusambaza muziki wao na wapo vijana ambao wanalipwa mpaka milioni 30, 40, 50 kwa mwezi. Pia ni kweli kabisa Mheshimiwa yuko sahihi, ukiangalia kiwango cha manunuzi na kiwango ambacho wanapata hakuna uwazi dhahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulichoamua kufanya kwanza ni kutengeneza kanuni ambazo zitaweka uwazi kwenye mapato ya Kampuni ya Simu kwa sababu mpaka sasa hivi hakuna uwazi, ni kwa kiasi gani ambacho Makampuni haya ya Simu yanapata kutokana na biashara ya milio peke yake. Kwa sababu Makampuni ya Simu yana biashara nyingi; kuna *SMS*, kuna za kupiga, kuna *M-pesa* na nini, kwa hiyo kinachopatikana mahususi kwenye milio ya simu. Tutakapojua hapa tutajua ukubwa wa soko la hii biashara, kwa hiyo hicho cha kwanza kuweka uwazi na kanuni ziseme hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambaye anaingia mkataba na wasanii siyo Makampuni ya Simu kuna mtu wa katikati hapa ambaye anaitwa *aggregator* ambaye yeye ndiyo anakusanya nyimbo za wanamuziki wote, anaikatata vipande anaiweka kwenye *system,* halafu yeye yule ndiye anauzia Makampuni ya Simu. Kwa hiyo kikubwa kwa kweli na tulishaongea na *TCRA* kuhusu hili na tulishaanza vikao Wizara pale kati ya Wasanii, Makampuni ya Simu na hao wanaofanya biashara ya katikati *aggregators* ili kujua ni kwa kiasi gani wao wanapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishe Mheshimiwa Martha Mlata, najua hili jambo amelisimamia kwa muda mrefu kwa sababu yeye ni msanii, anajua kilio hicho. Naomba tuendelee kushirikiana katika hili jambo kwa sababu nami pia nina dhamira ya kuwasaidia vijana wenzangu ili jambo hili liishe.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza nataka kujua hizo kanuni…..

**MWENYEKITI:** Sasa tuelewane.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi.

**MWENYEKITI:** *Okay*, hapo unabidi uwe *specific*.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Ndiyo, Ninachokitaka ni kwamba, ni kwa nini sasa Serikali pamoja na kwamba wanasema watatunga kanuni ambazo hatufahamu watatunga lini. Ni kweli kuna mikataba wasanii wanalipwa vizuri, nafahamu ni Kampuni moja tu ya *Push Mobile* ambayo wao wanalipa vizuri watu wao ambao wameingia nao mkataba, lakini makampuni mengine yote yanawaibia wasanii.

Je, ni kwa nini msanii asilipwe *direct* kutoka kwenye Kampuni ya Simu, ili aweze kupata? Kwa sababu makampuni mengi hayalipi. Kwa hiyo, ninachotaka kumuuliza Waziri kwa nini msanii asilipwe kiwango chake cha asilimia 10 kutoka kwenye Kampuni ya Simu moja kwa moja kama ni *VODACOM*, alipwe msanii mwenyewe, kuliko zile hela zipitie kwenye hayo makampuni madogo madogo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo niseme kwamba linahusu wadau wengi, kwa sababu jambo la haki miliki za kazi za wasanii halihusu Wizara yetu, linahusu Wizara ya Viwanda na Biashara na pale wako *COSOTA*. Vile vile linahusu Wizara ya Habari, Utamaduni, Vijana na Michezo, pia linahusu Makampuni ya Simu na linahusu *TRA* na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kabisa mwaka jana nilisimamia uanzishaji wa vikao vya wadau wote hao ili kulitazama kwa kina kwa sababu siyo jambo dogo. Napenda kumshawishi Mheshimiwa arudishe shilingi yake ili tuweze kuendelea na ile kazi ambayo tumeanza ili tuweze kulimaliza, kwa

sababu sheria hiyo anayoisema ya asilimia 10 ni sheria iliyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria yenyewe hiyo bado kwa kweli kwa jinsi ilivyo inahitajika kufanyiwa marekebisho, kwa sababu wasanii wanapaswa kulipwa hata muziki wao unapopigwa kwenye *TV* na kwenye redio kila siku, hata unapolia kwenye simu. Kwa hiyo, ni lazima kuweka mifumo mahususi ya kuweza kufahamu wakati gani muziki umepigwa, ni wakati gani redio hiyo imesikilizwa na redio hiyo inasikika na watu wangapi ili kuweza kupata asilimia sahihi kwa wasanii.

Kwa hiyo, ni jambo la kiteknolojia na la kisheria kwa upande mwingine. Kazi hii tunayo dhamira ya kuifanya na kuimaliza. Hivyo, namshawishi Mheshimiwa kwamba arudishe shilingi ili tuendelee na kazi hii na kanuni tutazitengeneza pale tutakapokuwa tumemaliza mjadala. Kwa sababu kwenye vikao vya mwanzo hatukukubaliana mambo mengi sana tulikuwa tunapishana, lakini tulikuwa tunakwenda vizuri na nitamualika Mheshimiwa naye ashiriki vikao hivi.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ambayo anasema kwamba, watatengeneza mfumo utakaoweza kusimamia malipo haya na kushirikiana na ile Sheria ya *COSOTA*. Hata hivyo, naomba kwa sababu *TCRA* wao wako *very smart* kwenye kusimamia mambo haya na tumeona kwamba kuna mtambo ambao unaweza ukawa unatambua kazi zetu zilizotumika ama kwenye redio ama kwenye *TV* au kwenye simu ili malipo haya yaweze kuwanufaisha wasanii kwa sababu ni ajira. Naomba nirudishe shilingi, nitasubiri mwaliko wake na kama itashindikana basi nitakuja na hoja binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Unajua Wizara hii nimewapa muda mrefu kusema kwa sababu mkiangalia ninyi wenyewe mlivyojadili ukiacha mimi simu kwangu kule, mtandao nini na nini, vingine hatukujadili. Hata hivyo, alivyoeleza Waziri mbona tumejifunza mengi. Kwa hiyo, ni Wizara muhimu sana na ni vizuri tukapata haya mafunzo pengine katika hali ya kawaida tusingeyapata. Kwa hiyo, ndiyo maana ukiniona hapa nampa nafasi nyingi zaidi Waziri kwa sababu haya mambo ni masomo.

Sasa nakuja kwa Mheshimiwa *Engineer* Athumani Mfutakamba.

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilitegemea Mheshimiwa Waziri atazungumzia suala hili la *ICT, business processing packs,* naona bajeti mwaka jana haikuwa imetengewa pesa zozote. Hata hivyo, suala hili ni muhimu sana katika matumizi ya *ICT* katika kukuza uchumi wetu hasa kwa njia ya ku-*outsource business contract.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Kenya wameanzisha *ICT industrial harbour* ambayo wamekaribisha makampuni mbalimbali ya *IT* kuja kuwekeza pale. Sasa sijui Mheshimiwa Waziri pamoja na ufinyu wa bajeti kuna mpango gani wa kusaidia suala hili. Kwa sababu mkongo uko tayari na TEHAMA inafika mpaka vijijini. Mtu unaweza kuwa na Komputa tu hata kama uko Igalula, kuna umeme wa Mheshimiwa Muhongo, mkongo upo na Komputa yako unaweza kupewa *contract* za kufanya New York, *contract* za kufanya **Silicon** *Valley* California , ukaweza kufanya zile kazi uka-*process* na ukaweza kulipwa wakati uko Igalula, hiyo ndiyo faida ya Mkongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze kidogo, utaratibu gani au *alternative* pamoja na ufinyu wa bajeti kupata hii *ICT business processing Industrial pack*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwenye bajeti ya safari hii hatukuweka *ICT Pack*, lakini sisi tuna *believe* hiyo inaweza kufanyika kwa kutumia *private sector*. Hatuwezi kila kitu ambacho kinaweza kufanyika kwa kutumia *private sector* tukapeleka kwenye pesa za Serikali ambako pesa zenyewe hazitoshi, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tayari tumeshapa eneo kule Kigamboni heka 340 ambayo ni ushirikiano baina ya EPZ na *COSTECH* na tatu tunatayarisha sera kwa ajili ya *business processing outsourcing* ambayo mwaka huu sera hiyo itakuwa imekwisha.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu nilisema Mkoa wa Kigoma tumepakana na nchi ya Burundi. Vipo vijiji ambavyo vipo mpakani kabisa, mawasiliano ni ya shida na mara nyingi wananchi wanaoishi maeneo yale minara wanayotumia ni kutoka Burundi. Hata hivyo, hiyo haiwasaidii kwa sababu hawawezi kupiga simu wala kupokea simu. Nataka kujua, Waziri anaweza kutusaidia kwa haraka zaidi akatupa kipaumbele ili maeneo hayo yaweze kupatiwa minara haraka iwezekanavyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza wakati nachangia hoja kwamba Serikali imeamua kuweka mpango mahususi kabisa wa kujenga minara katika maeneo ya mipaka ya nchi yetu kama moja ya hatua za kuimarisha ulinzi wa mipaka ya nchi yetu. Tumeshabainisha maeneo kadhaa katika Majimbo ya Masasi, Ngara, Karagwe, Manyovu, Kigoma Kusini, Mpanda, Kalambo, Nkasi, Nyasa, Ludewa, Kyela na kwingineko Rombo kule. Kama Mheshimiwa ana uhakika kabisa kwamba kuna eneo la mpakani na kama anataka kuthibitisha kuwa limo basi aje atuone ili tuweze kuhakikisha lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wetu huu ni kujenga hii minara kwa asilimia mia moja kwa fedha za Serikali bila hata kusubiri mchango wa makampuni binafsi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khalfan Aeshi hayupo, Mheshimiwa Betty E. Machangu!

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali langu liko kwenye vifurushi na natilia shaka utendaji na uadilifu wa hawa wanaotoa hivi vifurushi. Kwa mfano, niseme *VODACOM* wanatoa kifurushi kinaitwa *Chekazogo*, inakwambia utalipa sh. 495 kwa dakika 30/24. Hata hivyo, najiunga *let say* saa tatu usiku, natumia *like five minutes*, dakika tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile hela, yaani muda unakwisha, kwa nini dakika 25 haziwi *carried forward* na kwa nini hawakwambii *break down* kwamba umetumia dakika ngapi na umebakia na dakika ngapi badala yake inakwisha hivi hivi. Ukiamka asubuhi kama ni *24 hours* unatarajia *the next day* usiku *24 hours* iishe au hata kesho yake uweze kupiga simu, lakini hakuna, ukifika asubuhi saa kumi na mbili basi. Kwa hiyo, naomba nipate maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Mheshimiwa Waziri alikuwa anaongea sh. 3,000/=, utaongea *60 minutes for a week*. Niseme labda wanampa yeye kwa vile wanajua ni simu ya Waziri, kwa sababu gani? Hata hizo *message* wanazokwambia 200, *once* umemaliza kuongea, zile *message* 200 umeahidiwa, *message* moja haiendi kama ile hela imekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hili jambo la kifurushi sisi ndiyo tumeleta, kwa sababu ilikuwa

kupiga simu mtandao mmoja kwenda mwingine ni pesa nyingi sana, sh. 115 kwa dakika, sisi tukaona tuteremshe *inter connection fee* ije mpaka sh. 34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya hivyo, Makampuni ya Simu yakaona hapana, hakuna faida sasa hivi kuanza kupiga mtandao mmoja kwenda mwingine, ndiyo wakaanzisha hivyo vifurushi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mimi ni mtumiaji mkubwa wa vifurushi, natumia dakika 65 kwa sh. 3,000 na inafanya kazi vizuri, lakini niko *Airtel,* hivyo la Mheshimiwa nitalichukua kwa sababu mimi siyo mtumiaji wa *Vodacom,* ili kuangalia tatizo liko wapi.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKUMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Sina nia ya kuondoa shilingi na ingawa Naibu Waziri amekuwa akiitaja taja Ngara, lakini nimeona nieleze kwamba katika mchango wangu wa maandishi nimemkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba, tangu mwaka jana nilimwandikia barua kwamba Ngara inapakana na Rwanda na Burundi na mipaka ile haiko shwari na kwamba Wilaya kama Ngara ingewekwa kwenye *priority list* ya kupata minara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barua hiyo haikujibiwa, lakini nimeona wenzangu hata majirani zangu hapa wanajibiwa, wanapewa *commitment* kwa maandishi na Waziri. Mimi nimekulia Serikalini, najua Serikali inafanya kazi kwenye makaratasi, naandika, wengine hawaandiki lakini wanapewa *serious commitment* kwa barua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nimeeleza kwamba vijiji ambavyo viko mpakani mwa Burundi na Rwanda katika Wilaya ya Ngara, Kata za Nyakisasa, Mabawe, Mganza, Ntobeye, Bukililo, Mbuva, Keza hazina usikivu kabisa wa simu, lakini nimekuwa nikieleza, sijapata maandishi yoyote wenzangu wanapata *commitment*, kumbe nimeona kwamba kwenye siasa *its doesn't pay to be a gentleman.* Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** *In fact*, sana sana wajibu kwa nini hawakujibu barua, lakini kama ni suala la sera ni lile alilouliza Mheshimiwa Josephine Genzabuke, kwamba mipakani kungepewa ulinzi wa kutosha zaidi, labda hilo la kutokujibu barua.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuliamua kwamba pale ambapo tutakuwa tumepata *commitment* ya Kampuni ya Simu, tumepata Mkandarasi, basi tunamwandikia Mheshimiwa Mbunge kumueleza kwamba sehemu yako imepata mawasiliano.

Nimekuwa naongea na Mheshimiwa Mzee wangu Ntukumazina mara nyingi sana kuhusu maeneo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nimueleze kwamba, wiki iliyopita sisi tumepata barua kwa sababu maeneo yake aliyotupa barua yake aliyotupa tumeifanyia kazi, tulitaka tumpe majibu ambayo tumeyafanyia kazi. Nafahamu kwamba wakati mwingine ni sahihi kuandika kwamba umepokea barua, lakini barua yake tumeifanyia kazi na tumewapelekea Makampuni ya Simu kuhusu umuhimu wa kupeleka minara kwenye maeneo yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata barua kutoka *Tigo* ambao wameji-*commit* kujenga mnara Keza na kwa maana hiyo sasa, tutamwandikia kwa sababu barua hii ya Tigo tumeipata wiki iliyopita. Tutamwandikia kumwambia kwenye ile barua aliyotuandikia, *Tigo* wameamua kuja. Maeneo mengine tunangoja majibu kutoka *Vodacom* kwa sababu na wenyewe tuliwaambia kwamba mkijenga mnara kwenye maeneo haya ya Ngara Serikali italipa fedha zote. *Tigo* wamechukua Keza, tunasubiri wengine na tutamjibu barua yake kwa majibu mazuri.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kupata maelezo ya Serikali kuhusiana na *issue* ya mtambo ambao unaratibu kujua *transactions* za simu, kwa sababu kumekuwa kuna malalamiko makubwa. Mara nyingi sana tumekuwa tunauliza maswali hapa ndani ya Bunge. Hivi Serikali inakusanya kodi kiasi gani kupitia Makampuni ya Simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi zipo taarifa kwamba mtambo huu umeshakuwa *installed,* lakini ni kwamba wanaweza kujua *transaction* za simu za kimataifa, simu za ndani kwamba bado hawajaweza kufanya kazi hiyo.

Sasa naomba Serikali waweze kutupa maelezo. Je, taarifa hii ni sahihi kwamba wanafanya *monitoring* kwenye simu za Kimataifa kwa maana ya simu za nje au ni pamoja na simu za ndani. Ningeomba niweze kupata maelezo ya Serikali kuhusiana na suala hili na kama nitakuwa sikuridhika nitaomba kutoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Wewe mwenyewe huna uhakika kama ni ya nje tu au ya ndani, mbona huna uhakika utatoaje shilingi.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Hilo ni moja halafu la pili ni kuhusiana na mtambo kuwa *installed* kwa sababu Serikali iliahidi…

**MWENYEKITI:** Hakuna la pili, Mheshimiwa Waziri jibu hilo swali ili utufundishe sisi wote.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mtambo tulivyouweka una maeneo nane ya kutazama. La kwanza, ni idadai kamili ya simu zinazopigwa nchini kwa siku, kwa wiki, kwa mwezi. Idadi ya dakika zote na sekunde zote na *sms* zote zinazopingwa nchini, kupata volume ya *traffic* ya *telecoms* nchini ni kitu cha kwanza na cha msingi kwa sababu ni muhimu Serikali kuwa na taarifa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, huko nyuma kulikuwa na wizi mkubwa kwenye simu zinazotoka nje ya nchi na zinazoingia ndani ya nchi, kwa sababu simu zinazopigwa kutoka nje zinapokuja ndani kuna mageti, zinaitwa *gateways*. Kwamba kuna biashara ya *termination*, kwamba unaweza wewe ukaanzisha biashara leo ya kupokea simu kutoka nje, zinakuja kwenye *terminal* yako, wewe ndiyo unazipeleka kule zilikopigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa watu wengi walikuwa na hizi mashine za *termination,* wanapokea simu kutoka nje wanazi-*terminate* kwa watu wala Serikali haijui, simu hizo kiasi gani na Serikali haipati pesa na hata Makampuni ya Simu na yenyewe hayapati pesa kwa sababu biashara hiyo ilikuwa inafanyika kinyemela.

Kwa hiyo, sisi kwenye ule mtambo na yako maeneo mengi, ule mtambo unaweza kujua wizi, unaweza kujua ubora wa mawasiliano katika maeneo yote. Hivyo, tuliona tuanze na hili eneo rahisi kwanza la kuzuia hizi *termination fraud.* Tumefanikiwa, huko nyuma hatukuwa na pesa, lakini sasa hivi tunapata karibu shilingi bilioni moja na milioni mia nane kwa mwezi ambazo nyuma hazikuwepo. Hii ilikuwa ni biashara inayofanyika kihuni ya ku-*terminate* hizi simu. Tumekamata watu watatu waliokuwa wanafanya biashara hizo ambao wameibia Serikali karibu bilioni nane na watu hao wamepelekwa Mahakamani. Hayo ni matokeo ya haraka tu, kwa sababu tumeanza majuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vingine vinaitwa *add-ons,* vitu ambavyo tutaviongeza kwenye ule mtambo kwa sababu unaweza. Kwa hiyo, kuanzia mwezi uliopita vimefanyika vikao kati ya *TCRA* na *TRA* kwenda kwenye hatua ya pili ya kutazama simu za ndani zinazopigwa ndani. Hii *system* inaitwa *airtime revenue monitoring system,* ni sehemu ya huu mtambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mtambo huu ni mkubwa na ni *complex,* ni lazima ujenge uwezo wa watu wetu kabla hujaongeza kitu. Kwa hiyo, hilo pia linafanyika kwamba watu wanakwenda kuwa *trained* ndiyo mnakwenda kwenye hatua inayofuata. Matumaini yetu ni kwamba tutafika kote huko ikiwemo kutazama miamala na vitu vinginevyo. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi nzuri sana inafanyika pale na ni kazi ya kujivunia sana ambayo itaisaidia sana Serikali kuokoa fedha.

**MWENYEKITI:** Jamani ilikuwa elimu hakuna kitu! Kifungu hiki kinaafikiwa.
**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa bado nahitaji ufafanuzi…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa vitu vingine ni elimu, hatuwezi kubishana kitu ambacho ni kipya.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na majibu yaliyotolewa na Serikali.

**MWENYEKITI:** Sipendi, ndiyo ninaye-*manage,* naomba sasa ukae, mimi ndiye ninaye-*manage* kikao hiki.

**MHE. MOSES J. MCHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, u-*dictator* huo!

**MWENYEKITI:** Najua umeandika barua nyingi sana, ndiyo laana zenyewe. Ameandika barua nyingi sana kunilaumu ninavyoendesha kikao na nimenyamaza. Hatuwezi kubishana kitu ambacho tunapata elimu, mtambo una siku tatu. Mimi ningedhani…

Haya tuendelee, fungu linaafikiwa!

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*… … … … Sh. 341,335,000/=

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru niko kwenye Kifungu 1002, Uhasibu na Fedha kwenye kasma 221100, *Travel out of country* yaani usafiri wa nje. Kwa mujibu wa randama inaeleza katika fedha hizi sh. 25,500,000/= ambazo zimetengwa mwaka huu, hizi ni fedha kwa ajili ya posho za watumishi, wanaotarajia kuhudhuria mafunzo ya Kimataifa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo, kutoka shilingi milioni tano kwa mwaka 2013/2014 mpaka milioni ishirini na tano laki tano, kuna ongezeko karibu la shilingi ishirini milioni, ni safari za nje. Sawa, lakini ningependa kujua Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi, ongezeko la shilingi ishirini milioni, pamoja na kwamba ni safari za nje, ni nchi zipi na mnakwenda wapi! Naomba ufafanuzi wa kina.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni kwa ajili ya posho ya watumishi watatu wanaotarajiwa kuhudhuria masomo ya uandaaji wa taarifa za fedha kwa kutumia mfumo wa Kimataifa nje ya nchi na mtumishi mmoja anayetarajia kuhudhuria mkutano wa kitaalam nje ya nchi. Ongezeko la tengeo linatokana na kuongezeka kwa idadi ya watumishi wanaotarajiwa kuhudhuria mafunzo hayo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Planning*… … … … … Sh. 625,952,000/=

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nataka kuulizia kidogo kuhusu *subvote 1003,* katika kasma ya 221400, kwamba hii *hospitality, supplies and services*, naona imepanda mno. Mwaka juzi ilikuwa milioni moja, mwaka jana milioni moja laki mbili, lakini mwaka huu zimetengwa milioni tisa na laki sita. Ulaji gani huu au hicho chakula kinatoka Kempinski safari hii.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zinaombwa kwa ajili ya kulipa gharama za vitafunio na vinywaji kwa vikao vya kitengo, ambavyo sasa hivi tuna Wakurugezi Wasaidizi watatu wapya tumewaajiri, zamani hao wote hawakuwepo. *(Makofi)*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko hapo hapo kwenye sera na mipango, *subvote 1003,* katika *item* 22100, *travel in Country,* safari za kikazi kwa watumishi wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana, 2013/2014, kulikuwa na sh. 25,200,000/=, mwaka huu fedha ambazo zimetengwa ni sh. 46,000,000. Kwa mujibu wa maelezo ya randama, yanavyoeleza, kwamba safari za kikazi kwa watumishi wa ndani, sh. 20,800,000, ni ongezeko la Wakurugenzi watatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hofu yangu na mashaka yangu, ni juu ya ongezeko la Wakurugenzi watatu kupewa shilingi ishirini milioni na laki nane. Naomba ufafanuzi wa kina juu ya fedha hizi, isionekane kuna ongezeko

dogodogo la hizi fedha, ikawa zinakwenda kwenye uchaguzi wa Serikali za mitaa. Nashukuru na naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Hebu ondoa maneno mengine, wewe uliza kazi yake ni nini, hayo maneno mengine ni ya kwako.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Kazi yake ni nini, naomba ufafanuzi wa kina.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema, fedha hizi ni kwa ajili ya kulipia gharama za safari za kikazi za watumishi ndani ya nchi. Ongezeko la milioni 20, linatokana na idara kupata Wakurugenzi watatu wapya, lakini kuna miradi mingi wataitembelea; Miradi ya Mkongo, Vyuo vyetu vile vya Nelson Mandela, *Mbeya University of Science and Technology* na miradi mingine iliyoko kwenye mikoa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 - *Internal Audit Unit*… … … … … … Sh.188,646,000/=

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko katika *subvote* 1004, katika *item* au kasma 230400, *routine maintenance and repair of vehicles and transportation equipment*. Mwaka jana mwaka 2013/2014, fedha ambazo zilikuwa zimetengwa ilikuwa ni sh. 2,000,000/=, mwaka huu kuna sh. 16,500,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa randama, inaeleza kwamba ni kutengeneza gari la kitengo, siyo magari ya kitengo, gari la kitengo na amesema maelezo ya ziada kwenye randama, kwamba ongezeko linatokana na gharama kubwa, kutokana na gari kuwa chakavu.

Matengenezo haya ambayo yapo, ongezeko la shilingi milioni karibu 14, yaani kumi na tatu milioni na laki tano, ni kwa sababu ya matengezo kwa gari hili ambalo limekuwa ni chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza, hivi jamani, gari lenyewe kama ni chakavu pengine hatujui shilingi ngapi lilinunuliwa kipindi hicho, milioni 30 au 35. Mara hii mnatenga sh. 16,500,000/=, kwa sababu ya uchakavu wa hili gari kulitengeneza, hamliuzi? Naomba ufafanuzi wa kina. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema, kiasi hiki kinaombwa kwa gari chakavu, lakini

kabla ya hapo, ilikuwa fedha hizi zinatengwa kwenye kifungu cha utawala, lilikuwa chini ya utawala gari hilo. Kwa hiyo, fedha zilikuwa zinatengwa kule, lakini sasa hivi wamepewa kwenye idara yenyewe walisimamie.

Kif.1005 - *Legal Unit*… … … … … … … … … Sh. 44,718,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1006 - *Government Communications Unit*… … … … … … … … … … …Sh. 129,823,000/=

**MWENYEKITI:** Mnakaa kwanza, halafu tunakuita baada ya kusoma kifungu.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko kwenye *subvote* 1006, kasma 220800. Kwa mujibu wa randama, inasema fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya mafunzo ndani ya nchi, lakini mafunzo yenyewe ni kulipia gharama za mafunzo kwa ajili ya utoaji wa taarifa za Serikali. Naomba ufafanuzi, ni taarifa gani na fedha hizi ambazo miaka miwili ya nyuma, hakuna fedha iliyotengwa, mwaka huu ndiyo kumetengwa milioni moja. Je, kipindi cha nyumba kulikuwa hakuna mafunzo yoyote yanayotolewa na ni mafunzo ya aina gani! *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto kubwa Serikalini ni kuhusu kuhifadhi, uandishi na utoaji wa taarifa za Serikali. Sisi tunaamini kwamba kazi hii inahitaji ujuzi na weledi mkubwa na kwa kweli kiasi cha milioni moja kilichopangwa hapa hakitoshi. Kwa hiyo, tunaamini kwamba, hii *justified* na kwamba *in fact* tungependa iwe nyingi zaidi ya hii iliyokuja. Vile vile kwa sababu mwaka uliopita haikupangiwa fedha, haimaanishi kwamba kuna makosa mwaka huu kupanga fedha.

**MWENYEKITI:** Uliomba na wewe, nilimwona mmoja tu. Mheshimiwa Masoud!

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko *subvote1006,* niko katika *item* 221200, *Communications and information*. Katika habari na mawasiliano, kwa mwaka jana kulikuwa na sh.13,500,000/=, mwaka huu kuna sh. 33,000,000/= na kwa mujibu wa randama, inaeleza kwamba hizi ni fedha kwa ajili ya kugharamia machapisho, majarida, vitini na kuelimisha, lakini

katika machapisho hayo ya majarida, vitini na kuelimisha, kuna ongezeko la karibu sh. 20,000,000/= milioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunajiuliza, haya machapisho, majarida, vitini na vikorombwezo vingine, Mheshimiwa *Engineer* na Mheshimiwa mwenzake, ni yapi na ya aina gani mwaka huu! Ongezeko ni kubwa sana, la sh. 20,000,000/=, mna mpango gani, mtandao gani, maeneo yapi! Hebu watupe elimu ya kujua haya machapisho na vitini vyao na majarida ambayo mnataka kuelimisha zaidi. Naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu ujao wa fedha, Wizara italeta Miswada isiyopungua minne ya Sheria hapa Bungeni na itaandika Sera zisizopungua tatu na mchakato mzima wa uandishi wa hizi Sera, Sheria, mikutano na wadau na kuelimisha umma kuhusu shughuli tunazofanya pamoja na hizi Sheria tunazotunga, zinahitaji fedha za kutosha kwa sababu tunao wajibu kama Wizara, kwa sababu huwa tunasemwa kwamba shughuli za Wizara zetu hazifahamiki, hazijulikani. Kwa hiyo, pale tunapoomba fedha ili shughuli hizo zifahamike na zijulikane, tunaomba mridhie. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1007-*Procurement and Management Unit*… … … … … … … … … … … … Sh. 228,361,000/=
Kif. 1008 - *Management Information System*… … … … … … … … … … … Sh. 136,914,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Communication Division*… … … ..Sh. 542,099,000/=

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kuniona. Pamoja na kwamba kuna kifungu kingine nilisimama huko nyuma, sikupata nafasi. Hoja yangu iko kwenye kifungu kidogo cha 210500, *Personal Allowances In Kind.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kabisa kwamba kitengo hiki cha mawasiliano ni muhimu, lakini kifungu hiki kinaonekana kwamba, ukilinganisha na mwaka uliopita, kimeongezeka kwa takribani asilimia 71. Kwa hiyo, nataka

kujua tu kwamba ni kwa nini kifungu hiki kimeongezewa fedha nyingi kwa kiwango hicho.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki ni kweli kimeongezeka, ni kwa ajili ya stahili kwa viongozi za posho za nyumba, simu, maji na umeme. Ongezeko la shilingi hizo, linatokana na kuwepo kwa watumishi watatu kwenye idara hii ambao wana stahili hizo na bei za umeme zimeongezeka.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Information, Communication and Technology… … … … … … …*Sh. 440,129,000/=

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi hii ili niweze kuhoji sehemu moja tu. Niko kwenye kasma 221200 - *Communication and Information*. Maeneo mengi ya mipakani, likiwemo Jimbo la Ileje, Vijiji vingi kama vile Kalembo, Malangali, Kafule na Ikinga, hata maeneo mengine ya Wilaya ya Rungwe, kule Mwakaleli na kwa mzee wangu Mheshimiwa Mwandosya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kyela, hakuna mawasiliano ya *TBC*, hata vipindi hivi vinavyoendelea, wananchi hawasikii. Nadhani kwamba kwenye eneo hili, Mheshimiwa Waziri angeweza kuniambia kwamba pengine inahusika kurekebisha mitambo ili iweze kufika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo ya Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Hizi fedha ni za nini ndiyo swali lenyewe, hayo yote mengine... Haya, tupe maelezo hizi milioni nane. Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunalo jibu la swali la Mheshimiwa...

**MWENYEKITI:** Jibu hili hapa.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA :**Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha ni kwa ajili ya kulipia huduma ya *internet* kwenye Ofisi ya Mradi wa Jengo la Posta. Mwaka uliopita tulikuwa tunalipa kwa kupitia mradi wa *RSIP* uliokuwa unafadhiliwa na Benki ya Dunia, ambao unakwisha Februari, mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Ileje, tumeongea na *TBC*, wamekwenda, wamefanya *survey*...

**MWENYEKITI:** Yaani hizi fedha ndiyo za hayo unayoyasema.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana.

**MWENYEKITI:** Tunakwenda kwenye vifungu. Kifungu hiki kinaafikiwa, aaa, *no*, kuna Mheshimiwa Mshama nilimwandika. Mheshimiwa Mshama!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, nilitaka kuuliza, kwa sababu na sisi hatupati mawasiliano.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. *3003 - Science and Technology* … … … … … … … … … … … … … …Sh. 33, 157,434,000/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi, sina dhamira ya kuondoa shilingi, kuhusu kasma 270300, *Current Grants to Non Financial Public Units (Academic Institutions)*. Nafahamu kwamba, kasma hii ni kwa ajili ya utoaji wa ruzuku na fedha za uendeshaji kwa Chuo Kikuu cha Mbeya cha Sayansi na Teknolojia, bilioni 11.7; Taasisi ya Nelson Mandela, Arusha, bilioni 9.3 na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, bilioni 14.19 na kuendelea, kati ya fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kifungu hiki, kimeongezeka, kutoka bilioni 19.3 mpaka bilioni 26.5. Kumekuwepo na malalamiko katika Chuo cha Sayansi na Teknolojia, Taasisi ya Sayansi ya Teknolojia pale Dar es Salaam, *(DIT),* juu ya fedha za wanafunzi kwa ajili ya chakula na fedha za wanafunzi kwa ajili ya mafunzo ya vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limeelezwa vile vile na Kamati katika ukurasa wa 19, ambao Kamati inasema, kwa mwaka jana ambapo chuo kilitengewa bilioni 2.5, hadi kufikia Aprili, 2014, fedha zilizotolewa zilikuwa milioni 843 peke yake! Sasa ningependa kupata ufafanuzi, iwapo nyongeza ya safari hii ya fedha, italenga kwenda kuhakikisha kwamba matatizo pale ya chakula na matatizo ya mafunzo ya vitendo, pale Chuo cha *DIT* sasa yanamalizika na ningeomba ufafanuzi kutoka kwa Waziri kwa kuzingatia ufinyu wa mwaka

uliopita, sasa tunaongeza fedha zaidi, kama watahakikisha zinafika kwa ajili ya malengo hayo.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mnyika kwamba, fedha hizi tumetenga tukiwa na maana kwamba, zitatosha kwa kuwahudumia wanafunzi, ndiyo tukaongeza hiki kiwango ili kiweze kuwasaidia wanafunzi wetu.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali langu liko katika kasma 270300, fedha zilizotengwa kwa ajili Taasisi ya Nelson Mandela...

**MWENYEKITI:** Aaa, hiyo ndiyo tuliyoimaliza sasa hivi na Mheshimiwa.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ameulizia *DIT*...

**MWENYEKITI:** Ndiyo hiyo, kifungu ni hicho kimoja tu. Mheshimiwa Jafo!

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nipate ufafanuzi tu kidogo katika kasma namba 221200, *Communication and Information*. Naona tuna *variation* kubwa, kutoka milioni saba, tumekwenda mpaka milioni 146. Sasa nataka nipate *clarification* vizuri, ni kwa nini una tofauti kubwa sana ya fedha hapo katika mwaka huu wa fedha!

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli kuna *variation* kubwa kwa sababu Wizara tumeona iko haja ya kuanzisha *dedicated channel* kwa ajili ya sayansi na teknolojia. *Channel* ya *TV* ambayo madhumuni makubwa yatakuwa ni kuhamasisha sayansi na teknolojia nchini.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niko katika kasma ya *Travel in Country,* 221000, ambayo imeonekana kwamba imekwenda maradufu zaidi ya fedha zilizotengwa mwaka jana. Kiwango cha sh. 99,200,000/= mwaka jana na mwaka huu iko Sh. 258,850,000/=. Kitu gani kilichosababisha fedha hizo kupanda kiasi hicho kwa *travel* ndani ya nchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri au Naibu, mmekiona hicho.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *experience* yetu katika mwaka uliopita wa fedha, ni kwamba

tulipata changamoto kubwa sana ya kufanya kazi zetu na kuitisha mikutano na kuzunguka nchi nzima, katika kutekeleza majukumu tuliyopangiwa. Kuna baadhi ya kazi tuliacha kuzifanya kutokana tu na ukweli kwamba hakukuwa na fedha za kwenda huko kufanya kazi yenyewe.

Kwa hiyo, sisi tunaamini kwamba kiwango hiki cha fedha tulichopanga mwaka huu kitatusaidia kuweza kutimiza majukumu yetu kama Wizara na Mheshimiwa Sanya anatoka Zanzibar, Wizara hii kuna baadhi ya mambo ni ya Muungano, Zanzibar hoteli bei ghali, kwa hiyo, itatuwezesha kufika Zanzibar na kutekeleza majukumu yetu katika kiwango kinachoridhisha.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 68 – Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia**

*Kif.* 1003 - *Policy and Planning* … … … … … Sh. 300,000,000/=

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye randama kifungu hiki kimeainishwa kwamba ni kwa ajili ya utathimini na kwa ajili ya kufuatilia miradi…

**MWENYEKITI:** Kiseme kifungu chenyewe.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Abee!

**MWENYEKITI:** Kiseme kifungu chenyewe.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote* 1003, kasma 4383 ambacho kimetengewa Shilingi milioni mia tatu, kimeainishwa kwamba ni kwa ajili ya tathmini na kufuatilia miradi. Sasa nataka kujua kama mojawapo ya kazi ambayo itakwenda kufanyika ni kufuatilia mradi wa huu mtambo wa kudhibiti mawasiliano ya ndani. Kwa sababu tumeona kwa mawasiliano ya nje tu, Serikali imeweza kupata kwa miezi mitatu bilioni sita *point* nane. Sasa ni imani yangu kama tukiboresha, wakifuatilia wakaboresha mtambo huu, tunaweza tukapata hela nyingi sana kwa mawasiliano ya ndani. Sasa nataka nijue, je kifungu hiki pia kitahusika kwa asilimia kubwa zaidi kuweza kufuatilia na kuhakikisha kwamba mawasiliano ya ndani nayo yanadhibitiwa?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri! Hela hizi ni za kazi gani, ndilo swali.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa hizi ni kwa ajili ya ufuatiliaji wa miradi yote. Katika mwaka huu wa fedha tulipanga miradi mingi ya nje ya Dar es Salaam , mikoani na kwingineko na miradi mingine ni ambayo inatokana na ufadhili, mingine inatokana na fedha zetu za ndani ambayo inahitaji kufuatilia ili utekelezaji uwe sahihi; ikiwemo na aliyosema Mheshimiwa Matiko. Vile vile kufuatilia kama masafa ya redio yanatumika kama inavyopaswa na mambo ya *tele-centers* na mambo ya *e-schools* ndiyo kazi yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mshama huwezi kuitwa kwa sababu ni kifungu hicho hicho.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Communication Division* … … …Sh. 2,434,813,000/=

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hii *subvote* 2001, kifungu kidogo 4287 ambacho ni cha *UCAF* au Mfuko kwa wote zimetengwa milioni mia moja pale. Sasa nataka kujua kwamba *UCAF* walikuwa wamewateua *TiGO* kuweka minara kwenye vijiji vya upande wangu vya Mwintiri, Glansoni, Kinyampembee na kadhalika ambao mpaka sasa hawajaanza ile kazi na wanatakiwa wamalize kazi hii mwezi Machi, wakati wenzao wa *Airtel* walishafanya kazi hiyo na wanakamilisha. Sasa je, fedha hili zitasaidia kumtaka *TiGO* afanye hiyo kazi, labda hakulipwa pesa au ni ukorofi wa *TiGO*.

**MWENYEKITI:** Jem hizo ndizo hela za kazi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Missanga na jirani yake pale Mheshimiwa Hamoud Mbunge wa Kibaha kwa ufuatiliaji mahiri kabisa wa maeneo yao.

Pesa hizi, kama mnavyoona, nilisema kwamba, kwa umuhimu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na kwa kweli kwa bajeti kupangiwa milioni mia moja tu ambayo haitoshi hata kujenga mnara mmoja ni pesa kidogo sana. Kwa hiyo, pesa hizi ni kwa ajili ya ufuatiliaji na shughuli nyingine ndogo ndogo ikiwemo ufuatiliaji wa ujenzi wa mnara katika Jimbo la Mheshimiwa Missanga na Jimbo la Mheshimiwa Hamoud pale.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ilikuwa kwenye kasma hiyo ambayo Mheshimiwa ameulizia…

**MWENYEKITI:** Nashukuru, kama ilikuwa ni hiyo basi.

**GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nitakwenda katika fungu linalofuata…

**MWENYEKITI:** Aaa, Mheshimiwa Mshama, Mheshimiwa Jafo!

**MHE. SELEMANI SAIDI JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hoja yangu iko katika kifungu kidogo 4285*, new post code and addressing System*, ambapo nimeona mwaka huu tumetenga Sh. 500,000,000/=, lakini najua kwamba eneo hili ndipo tunaposema kwamba suala zima la kuainisha, suala zima la mitaa, hizi *post code,* sasa naona *investments* hapa imekuwa ndogo na nikiangalia sasa hata suala zima la vitambulisho vya Uraia vinataka angalau watu kujua kwamba wanaishi maeneo gani. Sasa nataka nipate *clarification*, je, hela hii itaweza kuwekeza katika eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli huu ni mradi muhimu sana ambao utabadilisha sana namna Watanzania wanavyoendesha shughuli zao kwa sababu kila mtu atakuwa na *address* ambapo vitu vinaweza kumfikia nyumbani kwake au kwenye eneo lake la kazi au biashara. Fedha hizi hazitoshi kabisa kwa sababu zinazotakiwa ni bilioni mia moja na hamsini na nane.

Kwa hiyo, fedha hizi zimewekwa hapa ni kwa sababu ya *ceiling*. Matumaini yetu ni kwamba, tutazungumza ndani ya Serikali kwa sababu shughuli hii vile vile inahusu sana TAMISEMI na wenyewe wawe wanapanga kwa ajili ya shughuli hii.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Niko kwenye kasma 4284, *information society and ICT project*. Mwaka huu kasma hii imetengewa Sh. 300,000,000/= fedha za ndani na Sh. 1,300,000,000/= fedha za nje kutoka Finland. Katika ufafanuzi wa Randama, pamoja na mambo mengine, kasma hii inakusudiwa kuwezesha uanzishaji wa miradi midogo midogo pamoja na kuratibu uibuaji, ubunifu katika sekta ya TEHAMA miongoni mwa vijana. Sasa ukiangalia, mwaka wa jana vile vile kasma hii ilitengewa milioni mia moja tisini na tano fedha za ndani na bilioni mbili fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu sana kupitia makabrasha ya maelezo ya utekelezaji wa miradi mikubwa ambayo Wizara imeifanya, mradi huu sijaona mchanganuo wa utekelezaji wake. Ningeomba ufafanuzi, kwa fedha ambazo tunatenga hivi sasa zinalenga kwenda kufanya nini? Naelewa, maelezo ya

jumla imeelezwa kuwa ni ubunifu wa miradi hiyo ya sekta ya TEHAMA miongoni mwa vijana, kufanya nini hasa na vijana wakitaka kuzipata pesa hizi wanawezaje kuzipata. Hizi tunazotenga sasa na hizi za mwaka ambao tunaendelea nao hivi sasa ambao haujakamilika bado. Naomba ufafanuzi kutoka kwa Wizara hii.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mradi mmoja mzuri sana na wenzetu wa Serikali ya Finland na wenyewe ni kuhamasisha uvumbuzi pamoja na kuatamia uvumbuzi wa vijana katika sekta ya TEHAMA ili uwe biashara. Vile vitu wanavyovumbua vijana viwe biashara. Mradi huu maelezo yake yapo kwenye maelezo ya utekelezaji wa miradi ya Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* kwa sababu mradi huu unatekelezwa kupitia *COSTECH*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale *COSTECH* na vijana wanaopenda mambo hayo wanafahamu, kila mwaka tunachukua maombi ya vijana ambao wana mawazo na fikra ya uvumbuzi wanakwenda pale, wanaingia kwenye semina, wanafundishwa. Ambao wanafanikiwa wanawekwa pale, wanalipiwa nafasi ya ofisi, wanapata walezi, mawazo yao na zile *ideas* zao za uvumbuzi zinachakatwea kwa namna nzuri ili yawe mawazo ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata matunda mazuri sana, nadhani mnafahamu kampuni inaitwa *Max* Malipo ambayo ni maarufu sana. *Max* Malipo yule ametokana na shughuli kama hii, alikuwa na wazo tu, akaja pale, akakaa tukafanya naye kazi, sasa hivi imekuwa ni kampuni kubwa na ameondoka na wapo wengine wengi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Information, Communication and Technology*… … … … … ..Sh. 1,000,000,000/=

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma hiyo ya 4283. Mkongo wa Taifa, kipande kile kinachokwenda Namanga na baadaye kuunganisha na wenzetu wa Kenya kinapita katika Wilaya yangu mimi. Hata hivyo, kwa bahati mbaya, tofauti na *utilities* nyingine kama maji, umeme ambapo pale inapopita wananchi wanaopitiwa wananufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi katika Wilaya yangu kwa sehemu kubwa hawana mawasiliano ya simu na nimeangalia katika vitabu hivi, kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri na hiki kitabu cha Mfuko wa *UCAF,* hakuna hata mradi mmoja uliotekelezwa katika Wilaya yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, wananchi wale wanauona mkongo unapita kwao na wanaulinda, lakini hawanufaiki nao. Sasa nataka kujua, kwamba je, kutokana na fedha ambazo zimetengwa hapa, Shilingi billioni moja, ni kwa kiasi gani Serikali itasaidia wananchi wa maeneo hayo, wakiwemo wa Oldonyosambu, kule Losinoni, kule Mwandet, Olukokola, Musa kuteremka mpaka kule chini Bwawani, ambao hawana mawasiliano, kama katika fedha hizi nao watawezeshwa kupata mawasiliano. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Na kengele imegonga, hizi bilioni moja hapa ni kazi gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mradi mkubwa wa mkongo wa Taifa ambao sasa hivi tuko awamu ya tatu, ambapo tunaanza kwenda kujenga *data center*, na pesa hizi zitatumiwa kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi ambao watasimamia mradi huo. Hata hivyo, kwa suala lake Mheshimiwa tutahakikisha kwamba tunachukua…

**MWENYEKITI:** Tumemaliza, tunajibu mambo ya hapa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3003 - *Science and Technology*… … Sh. 25,641,520,000/=

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii. Kifungu hicho hicho 3003, kifungu kidogo 6345 zimetengwa kwa ajili ya *COSTECH*, kiasi cha bilioni kumi na sita na kiasi hicho hicho ndicho kinachopangwa miaka yote. Kifungu hiki ni muhimu sana kwa utafiti na utafiti ni kitu muhimu sana. Sasa je, hela hizi mbona naona haziongezeki, hazipungui, hizi tafiti ni za aina moja tu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa pesa hizi haziongezeki na sisi kama Wizara tulikuwa tunataka pesa hizi ziongezeke, lakini kutokana na *ceiling* tuliyopewa hatuwezi kuongeza pesa hizo.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nipate ufafanuzi katika kifungu namba 61, kasma namba 6352, *construction of Radiation Waste Facility*. Nimeona mwaka huu tumetenga shilingi milioni mia tano, lakini kiuhalisia sasa hivi nchi yetu inaingiza vifaa vingi sana vyenye mionzi. Ukiangalia *computer* zinaingia, simu zinaingia, sasa tunaingia katika janga kubwa sana na katika hali ya hatari katika nchi yetu. Sasa, hii maana yake tunahatarisha maisha ya wananchi wetu hapa nchini.

Sasa kama hatuna mipango muafaka kuhakikisha kwamba haya mabaki ya mionzi inayokuja nchini mwetu jinsi gani tunayadhibiti, tutakuwa katika janga kubwa sana. Sasa nataka niwaulize Wizara, je, pesa hii mnavyofikiri na *importation* ya vifaa vya mionzi inavyoingia nchini kwetu itaweza kusaidia ujenzi wa taasisi hiyo? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli pesa hii haitoshi, lakini ndiyo *ceiling* ilivyo na hatuwezi kufanya kitu, isipokuwa tutatafuta njia nyingine ya kuhakikisha kwamba tunaendelea na kazi hiyo.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Niko kwenye *item* 6281 - *joint program on capacity strengthening*. Ukizingatia kwamba Wizara hii inahusika kwa kiasi kikubwa na mambo ya sayansi, lakini Tanzania si kisiwa. Nataka kujua, hapa naona hakuna pesa iliyotengwa, pale ni *zero* kabisa. Je, tutakwendaje katika hali hii wakati huu ambapo tunatakiwa kushirikiana na wenzetu duniani katika mambo ya kukuza sayansi na teknolojia katika nchi yetu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ulikuwepo mwaka wa jana wa fedha, muda wake umekwisha, kwa hiyo mradi huu haupo tena.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kupata ufafanuzi katika kasma 4358, Chuo cha Nelson Mandela, Arusha; wametenga bilioni moja laki tano na chuo kile kina matatizo makubwa ya maji, je, fedha hizo zitakwenda kufanya kazi hiyo?

**MWENYEKITI:** Na uliliongelea hilo, Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya matumizi ya fedha hizi ni hizo, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wenzetu pale wa uongozi wa chuo kile, wamefanya ubunifu mkubwa sana katika kutafuta fedha za kumaliza matatizo ya pale, ikiwemo na mimi nimeshiriki kikamilifu kutafuta *Professional Fund Raiser* na kubuni mfuko, *Endowment Fund* kwa ajili ya uendeshaji wa chuo kwa kufahamu changamoto zilizopo Serikalini kwenye kupata fedha. Nimetembelea pale na wanayo dhamira kabisa ya kumaliza tatizo la maji kwa fedha hizi ambazo tunawapangia.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwenye kasma 6333, sina dhamira ya kuondoa shilingi. Mbeya *Institute of Science and*

*Technology*, mwaka wa jana kilitengewa bilioni mbili *point* tano na mwaka huu kimetengewa shilingi bilioni mbili. Kulikuwa na malalamiko ya wananchi ya kudai fidia na tathmini ilifanyika na ikabainika wanatakiwa kulipwa fidia ya bilioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari hii kumetengwa bilioni mbili, lakini ni kwa ajili ya ujenzi wa maktaba na miundombinu mingine. Sasa ningependa kupata ufafanuzi kutoka kwa Wizara, kwa fedha ambazo zilitengwa mwaka uliotangulia za chuo hiki kwa upande wa Mbeya, bilioni mbili *point* tano, ni kwa nini hazijalipa fidia ile ya wananchi na ni kwa vipi uendelezaji wa miundombinu utaendelea wakati ambapo kuna madai ya fidia ya wananchi. Kwa hiyo, ningependa kupata ufafanuzi kuhusu hatma ya fidia ya wananchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda pale Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, niliona tatizo na tulikuja Serikalini tukasukumana. Fedha zile zimepatikana na wakati wowote kuanzia sasa hivi wale watu watalipwa kwa sababu fedha zimepatikana. Hii ni ya uhakika kwamba zimepatikana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mheshimiwa Mtoa hoja, taarifa.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya matumizi na kuyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2014/2015, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano,*

*Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2014/2015 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Nadhani wote wameafiki. Kwanza kabisa tunaomba tuwapongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake. Siyo tu kwa kazi mnayoifanya, lakini kwa Semina ambayo mmeifanya leo humu ndani, wote tumeisikiliza vizuri sana. Kwa sababu michango ya Waheshimiwa Wabunge toka kipindi cha asubuhi, ilielekea kwenye mambo fulani fulani tu, lakini nyie mliweza kuyafafanua sana na wengi tumeelewa. Tunawaomba kwa uzalendo wenu, muendelee kufanya kazi pamoja na wataalam wenu kwa sababu nchi hii itajengwa na watu wenye moyo na siyo vinginevyo. Fedha hazitoshi, lakini kazi kubwa mnaifanya. *(Makofi)*

Nadhani ni kusudio letu baadaye tuweze kuangalia vizuri eneo hili pia. Kwa hiyo tunawapongezeni sana na tunawatakia kila la heri. *(Makofi)*

## Makadirio ya Serikali ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 - Wizara ya Maji Kama ilivyosomwa Bungeni

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limepokea Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa Peter Mahamoud Msolwa, kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara. Naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa kupokea, kuchambua, taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa Mwaka 2014/2015. Maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa wakati wa Maandalizi ya Bajeti ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, hali ya Sekta ya Maji Nchini; Sekta ya Maji ni moja ya sekta sita (6) zilizopewa kipaumbele katika utekelezaji wa Miradi ya Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa au *BRN*. Awamu ya kwanza ya Mpango huo ya miaka mitatu (3) yaani mwaka 2013/2014 – 2015/2016. Ni mwelekeo chanya katika kuyafikia malengo tuliyojiwekea ya kuwafikishia wananchi huduma ya maji, safi na salama, hususan katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango huo, jumla ya Miradi 1,810, itakayogharimu kiasi cha shilingi trilioni 1.45, inatarajiwa kujengwa na

itakapokamilika, wananchi wapatao milioni 15.4 na zaidi watapata huduma ya maji na kufikisha idadi ya wananchi wanaopata huduma ya maji safi na salama, kufikia milioni 30.6 sawa na asilimia 74 (74%) ya wakazi wote vijijini.

Mheshimiwa Spika, rasilimali za maji; hali ya upatikanaji wa maji imeendelea kutofautiana katika maeneo mengi nchini, kutokana na tabia tofauti za hali ya hewa katika maeneo hayo. Baadhi ya Mabonde yalipata mvua nyingi na mengine mvua kidogo kulingana na viwango vya mvua katika mwaka uliopita. Hata hivyo, mvua zilizomyesha mwaka huu, zimeongeza uwingi wa maji kwenye vyanzo vya maji katika maeneo yaliyopata mvua nyingi za masika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ahueni hiyo, hali ya upatikanaji wa maji inaendelea, kuathiriwa na uharibifu wa vyanzo vya maji unaotokana na ukataji wa miti mingi, uharibifu wa mazingira, mabadiliko ya matumizi ya ardhi, athari za mabadiliko ya tabia nchi, ongezeko la shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya vyanzo vya maji na kasi kubwa ya ongezeko la watu na shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, takwimu za Kitaifa za rasilimali za maji zilizopo zinaonesha kuwa kiasi cha maji tulichonacho kwa sasa kwa kila Mtanzania ni wastani wa mita za ujazo 1,952 kwa mwaka. Kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa kila mtu kwa kila mwaka, kinachokubalika Kimataifa ni wastani wa mita za ujazo 1,700. Utafiti unaonesha kuwa, endapo hatua madhubuti za kutunza vyanzo vya maji hazitachukuliwa, kiasi hicho kinatarajiwa kupungua hapa nchini na kufikia mita za ujazo 883 ifikapo mwaka 2035. Wizara ya Maji, kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya maji, inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na hali hiyo, ili nchi yetu isifikie kiwango hicho hatarishi, katika upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuwapatia maji safi na salama, wananchi waishio maeneo ya vijijini katika umbali usiozidi mita 400 kutoka kwenye makazi yao kama sera ya maji ya mwaka 2002 inavyoelekeza. Wizara ya Maji kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo, Serikali za Mitaa, wananchi, sekta binafsi na wadau wengine, inaboresha huduma ya maji vijijini kwa kujenga, kupanua na kukarabati miundombinu ya maji chini ya Mpango wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango huo, ulianza rasmi mwezi Julai, 2013, umeboresha kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini ambapo idadi ya wakazi wanaopata huduma ya maji safi na salama imeongezeka

kutoka wakazi 15,200,0000 mwezi Julai, 2013 hadi kufikia 17,840,000 mwezi Machi 2014, ikiwa ni sawa na ongezeko la watu 2,640,000.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Maji Mijini; Mamlaka za Maji za Miji Mikuu na Mikoa zinaendeshwa chini ya usimamizi wa Bodi za Wakurugenzi, ambazo huteuliwa na Waziri mwenye dhamana ya Maji kwa kushirikiana na Mikoa husika. Hadi mwezi Machi, 2014 zimeundwa Mamlaka 23 za Maji Mikuu ya Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka 13 kati hizo yaani Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Moshi na Mtwara, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Tanga, Songea na Musoma, zipo katika daraja *"A"* kwa maana zinajitegemea kabisa kwa shughuli zake. Mamlaka nne za Bukoba, Kigoma, Singida na Sumbawanga, ziko daraja *"B"* na zinapata ruzuku ya kulipia sehemu ya gharama za umeme na uendeshaji wa Mitambo. Mamlaka zilizoko kwenye daraja *"C"* ni Mpanda, Njombe, Bariadi, Geita na Babati na Lindi na kuna miradi nane ya maji ya Kitaifa na Mamlaka 96, za ngazi ya Wilaya ambazo nazo ziko katika daraja *"C"* na hulipiwa na Serikali sehemu ya gharama za umeme, uendeshaji wa mitambo na mishahara.

Mheshimiwa Spika, wastani wa kiwango cha utoaji wa huduma ya maji safi kwenye miji mikuu ya mikoa imeendelea kuimarika. Hiyo inatokana na ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya maji safi katika Mamlaka zote za Miji Mikuu ya Mikoa. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 utoaji wa huduma ya maji kwenye Miji Mikuu 19, umefikia wastani wa asilimia 86. Upatikanaji wa huduma ya maji kwa miji minne, Mpanda, Njombe, Geita na Bariadi ni wastani wa asilimia 53. Utekelezaji wa Miradi inayoendelea sasa na ile iliyopangwa kwa mwaka 2014/2015, itaongeza upakanani wa maji katika miji hiyo minne kufikia angalau asilimia 70 baada ya miradi hiyo kukabidhiwa mwishoni mwa mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekekezaji wa Bajeti ya mwaka 2013/2014 na Mpango wa bajeti kwa mwaka 2014/2015. Rasilimali za Maji; katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu ilisimamia na kuendeleza rasilimali za maji, ikiwemo kuchunguza, kutathimini na kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji nchini, pamoja na rasilimali za maji, shirikishi na kuimarisha Bodi za Maji za Mabonde ili zisimamie kikamilifu, rasilimali hizo. Kazi nyingine ni kuandaa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kusanifu na kusimamia ujenzi wa miundombinu ya kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji; katika kutekeleza mikakati ya kuhifadhi vyanzo vya maji. Wizara yangu imeendelea kuvitambua, kuviwekea mipaka na kuvitangaza kuwa maeneo tengefu vyanzo

vipya vya maji. Katika mwaka 2013/2014, jumla ya vyanzo 153, vilitambuliwa kuwa katika hatari ya kuharibiwa na kuathiriwa kwa sababu mbalimbali ikiwemo ongezeko la shughuli za kibinadamu. Kati ya hivyo, vyanzo 59, vimebainishwa na kuandaliwa ili vitangazwe kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maji, inaandaa mpango maalum wa miaka mitano, wa kuhifadhi na kutunza vyanzo vya maji utakaoanza kutekelezwa katika mwaka 2014/2015. Mpango huo umeainisha maeneo ya utekelezaji, ili kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya maji kwa maendeleo endelevu ya sasa na vizazi vijavyo. Mpango huo utahusisha utoaji elimu kwa umma na kuimarisha ushiriki wa wadau katika shughuli za uhifadhi, utunzaji na ulinzi wa rasilimali za maji.

Mheshimiwa Spika, kudhibiti uchafuzi wa Vyanzo vya Maji; udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya Maji, ni muhimu katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, ukaguzi ulifanywa katika bonde la kati kwenye maeneo tisa ya viwanda, migodi 46 na hoteli tatu katika bonde la Pangani. Ukaguzi pia ulifanyika katika mifumo ya utoaji Maji taka, ya Viwaanda vitatu na kuangalia utendaji wa kazi au *Performance Assessment* wa Mabwawa ya maji taka wa Mamlaka ya Maji ya Arusha. Ukaguzi huo ulibaini baadhi ya viwanda kutozingatia taratibu za utiririshaji wa maji taka kwenda kwenye vyanzo vya maji na hatua zimechukuliwa kushughulikiwa viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliendelea kutafiti maji chini ya ardhi, kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa maji ya matumizi majumbani na hata kwa ajili ya umwagiliaji. Utafiti ulibaini maeneo 501, yanayofaa kuchimbwa visima vya maji, katika mabonde ya Mto Rufiji, Bonde la Kati, Bonde la Pangani, Wami, Ruvu, Ziwa Victoria, Ziwa Rukwa, Ziwa Tanganyika na Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya watu wa China ilichimba visima 53, kati ya visima 55 vilivyopangwa kuchimbwa katika Wilaya ya Kisarawe na Wilaya ya Kilosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Uendelezaji wa Rasilimali za Maji; Bodi za Maji za Mabonde zinaendelea kutayarisha mipango itakayosimamia na kuendeleza rasilimali za maji hapa nchini. Hadi mwezi Machi, 2014, rasimu za mwisho za mipango katika mabonde ya Ruvuma na Pwani ya Kusini, Bonde la Kati, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa zimefanyiwa marekebisho na wataalam washauri, baada ya kupokea maoni ya marekebisho kutoka kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, Wataalam Washauri katika Bonde la Ziwa Rukwa, Pangani na Rufiji, wamewasilisha *interim reports* na Wizara imetoa maoni kuhusu taarifa hizo kwa ajili ya maekebisho. Katika bonde la Wami, taarifa ya mwisho ya mpango shirikishi wa usimamizi wa undelezaji wa rasilimali za maji katika bonde hilo imekamilika na kuwasilishwa Wizarani mwezi Desemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Rasilimali za Maji Shirikishi; Wizara yangu imeendelea kushirikiana na nchi nyingine zinazochangia rasilimali za Maji Shirikishi kwa kuunda vyombo vya pamoja na kuimarisha vilivyopo ili kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali hizo. Mabonde saba ya maji kati ya tisa, yaliyopo nchini, yanavuka mipaka ya nchi yetu na hivyo kutulazimu kushirikiana na nchi nyingine 17 majirani. Nchi hizo ni Angola, Botswana, Namibia, Zambia, Zimbabwe, Malawi, Msumbiji, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Sudan, Sudan Kusini, Uganda na Eritrea.

Mheshimiwa Spika, ushikirikiano wa kitaasisi na nchi hizo, unatekeleza kama ifuatavyo: Bonde la Mto Nile; Umoja wa Ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile, yaani *Nile Basin Initiative* unahusisha nchi 11 ambazo ni Burundi, Ethiopia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Misri, Rwanda, Sudan, Sudan Kusini, Uganda na Tanzania na nchi ya Eritrea ikiwa mtazamaji. Nchi saba za Burundi, Ethiopia, Uganda, Rwanda, Kenya, Sudan Kusini na Tanzania, zilisaini Mkataba wa kudumu wa ushirikiano wa nchi hizo, utakaoanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Nile.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa nchi ya Ethiopia na Rwanda, tayari zimeridhia mkataba huo na Tanzania ipo katika hatua za kukamilisha taratibu za kuridhia. Kulingana na matakwa ya Mkataba huo, nchi sita, zitakapokamilisha kuridhia Kamisheni ya Bonde la Mto Nile inaanzishwa. Katika mwaka ujao wa fedha nchi ambazo zilisaini mkataba huo zitakamilisha taratibu za kuridhia, kwa kuzingatia Sheria za nchi zao. Tanzania inaendelea kufuatilia kwa karibu suala hili ambalo lina manufaa makubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Hifadhi ya Mazingira wa Ziwa Victoria; Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali za Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda, ziliendeleza awamu ya pili ya mradi wa usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria, yaani *RIVAMP II.* Taassisi zinazohusika na hifadhi ya maji na samaki, zinatekeleza miradi ya ukarabati ya mifumo ya kusafisha maji taka, katika Miji ya Mwanza, Musoma na Bukoba, vilevile Halmashauri za Maswa, Itilima, Busega, Bariadi, Magu, Meatu, Kwimba, Sengerema, Geita, Chato, Muleba, Karagwe, Kyerwa na Misenyi, zimeingizwa kwenye awamu ya pili ya utekelezaji wa Mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bonde la Mto Zambezi; Wizara yangu inaendelea kutekeleza Mkataba wa Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi, uliokuwa ukitekelezwa rasmi kisheria tangu mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, Bonde la Mto Ruvuma; Mradi wa Maji Shirikishi wa Bonde la Mto Ruvuma, unatekelezwa kwenye Wilaya tano (5), katika Mikoa ya Mtwara na Ruvuma ambazo ni Tandahimba, Nanyumbu, Songea Vijijini, Tunduru na Mbinga. Katika mwaka 2013/2014, Miradi miwili (2) ya kijamii na mitambo miwili ya gesi asilia inayotokana na samadi kwa ajili ya matumizi ya kupikia na kuwashia taa inatekelezwa katika Wilaya ya Tunduru. Vile vile *scheme* ya umwagiliaji ya Namatuhi, iliyoko katika Wilaya ya Songea Vijijini inatekelezwa. Bonde la Mto Songwe; Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Malawi inatekeleza awamu ya pili ya program ya kuendeleza rasimu za Bonde la Mto Songwe. Awamu hiyo inahusu usanifu wa kina wa miradi ya rasilimali za maji itakayojengwa kwa ajili ya kuzalisha umeme, kilimo cha umwagiliaji na kuzuia mafuriko.

Mheshimiwa Spika, huduma za ubora wa maji na usafi wa maji; usimamizi wa rasilimali za maji nchini unahusisha uhakiki wa wingi na ubora wa maji kutoka katika vyanzo vyake vyote. Jukumu kuu la Wizara yangu ni kuhakikisha ubora, usafi na usalama wa maji katika vyanzo vya maji na mitandao ya usambazaji wa maji vijijini na mijini.

Katika mwaka 2013/2014 sampuli 4,673 za maji zilikusanywa na kuhakikiwa ubora wake. Kati ya hizo, sampuli 3,200 za maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani zilihakikiwa na kuhakikishwa kwamba zina ubora unaostahiki.

Mheshimiwa Spika, uondoaji madini ya Fluoride katika maji. Katika hotuba yangu ya mwaka 2013/2014 nilieleza Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu inaandaa mkakati wa usambazaji wa teknolojia ya kuondoa madini ya *fluoride* katika maji ya kunywa na kupikia kwa kutumia mkaa wa mifupa ya ng'ombe au *borne charcoal*. Sasa hivi matumizi ya teknolojia hii yako katika ngazi za kaya na jamii katika Mikoa ya Arusha zinanufaika na teknolojia hiyo.

Mheshimiwa Spika, huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini. Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa miradi ya huduma ya maji safi na usafi wa mazingira vijijini chini ya mpango wa *Big Results Now,* ambapo jumla ya Shilingi bilioni 236 zilikasimiwa. Aidha, kiasi kingine cha Shilingi bilioni 108 kilikasmiwa moja kwa moja kupitia mafungu ya Mikoa kwa ajili ya Halmashauri, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI na Wizara zinazoshiriki katika kutekeleza kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira vijijini.

Mpango wa *BRN* unahusisha utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo manne ambayo ni ujenzi wa miradi mipya, ukarabati wa miradi chakavu, upanuzi wa miradi iliyopo na uendeshaji na matengenezo. Ujenzi wa miradi mipya unahusisha miradi ya vijiji 10 kwa kila Halmashauri pamoja na miradi ya kimkakati. Miradi ya upanuzi na ukarabati inajumuisha utekelezaji wa miradi ya matokeo ya haraka kutoka kwenye vyanzo vya mabwawa, visima virefu, vyanzo vidogo vya maji juu ya ardhi, miradi ya kitaifa na miradi inayohitaji matengenezo. Aidha, uendeshaji na matengenezo unahusisha kuvijengea uwezo vyombo vya watumia maji na ukusanyaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 jumla ya vijiji 1,538 vilipangwa kutekelezwa kupitia mradi wa vijiji 10 kwa kila Halmashauri. Hata hivyo, wakati wa utekelezaji vijiji 17 zaidi viliongezwa na kufikia jumla ya vijiji 1,555. Mradi huo ukikamilika vituo 32,274 vya kuchotea maji vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi wapatao milioni 8,068,500 vitakuwa vimejengwa kwenye Halmashauri 167 kati ya Halmashauri 168. Vijiji vya Halmashauri iliyobaki ya Musoma vitapata huduma ya maji kutokana na mradi wa maji unaojengwa katika mji huo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza pango huo wa vijiji 10, hadi mwezi Machi, 2014 miradi 228 kwenye vijiji 247 imekamilika ambapo jumla ya vituo 9,594 vya kuchotea maji vyenye uwezo wa kuhudumia watu 2,398,500 vimejengwa. Aidha, miradi 538 kwenye vijiji 583 itakayokuwa na vituo 9,630 vyenye uwezo wa kuhudumia watu 2,407,500 inaendelea kujengwa.

Mikataba ya miradi 707 kwa ajili ya vijiji 725 itaanza kutekelezwa mara baada ya kupokea fedha. Miradi hiyo itakuwa na vituo 13,050 vyenye uwezo wa kuhudumia watu 3,262,500. Hivyo, miradi hiyo yote 1,473 itakapokamilika katika vijiji vyote 1,555 itahudumia jumla ya watu 8,068,500. Katika mwaka 2014/2015 Serikali itakamilisha miradi hiyo.

Aidha, Serikali imepanga kutumia jumla ya Shilingi bilioni 142.72 kutekeleza miradi ya maji katika vijiji 10 katika Halmashauri ambapo kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 73.65 zitapitia Wizara ya Maji na Shilingi bilioni 69.07 zitapitia mafungo ya mikoa kwa ajili ya Halmashauri na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, miradi ya kimkakati. Mradi wa maji wa Masoko unaojengwa katika Wilaya ya Rungwe ulisimama baada ya Halmashauri kusitisha mkataba wa mkandarasi aliayeshindwa kutekeleza kazi kulingana na viwango vya usanifu. Mradi utakapokamilika utanufaisha wakaazi 15,158 katika

vijiji 15. Katika mwaka 2014/20154 Serikali itaendelea kukamilisha mradi huo wa maji wa Masoko katika vipande.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan inatekeleza mradi wa maji katika vijiji 20 kwenye Wilaya zote saba za Mkoa wa Tabora. Mradi una awamu mbili; na awamu ya kwanza ulianza mwezi Septemba, 2009 na kukamilika mwezi Machi, 2014. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukarabati visima virefu 46 vya pampu za mkono katika Wilaya sita; kuandaa mpango mahususi wa maji vijijini kwa Mkoa unaohusisha maeneo ya kipaumbele ya kutekeleza miradi ya maji; kufanya upembuzi yanikifu na usanifu wa mradi wa vijiji 20 na kuandaa makadirio, gharama za ujenzi pamoja na makabrasha ya zabuni. Awamu ya pili ya mradi huo ilianza kutekelezwa mwezi Aprili, 2014 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2016. Mradi ukikamilika, utanufaisha wananchi 45,000.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Serikali kwa kushirikiana na *World Vision International* iliendelea na kazi ya upanuzi na ukarabati wa mradi wa Bungu katika Wilaya ya Korogwe. Hadi mwezi Machi, 2014 jumla ya vituo 22 vya kuchotea maji vilijengwa na kukarabatiwa katika vijiji vya Bunku, Manka, Msasa ambapo wakazi 9,909 wanaendelea kupata huduma ya maji. Katika mwaka unaofuata ujenzi wa mradi huu utaendelezwa na kukamilishwa.

Mheshimiwa Spika, kati ya vijiji 18 vinavyohudumiwa na mradi wa maji wa Ntomoko, ujenzi wa maji katika vijiji vinne umefikia katika hatua mbalimbali za utekelezaji na Wakandarasi katika miradi ya vijiji 10 wamepatikana na wanajiandaa kufanya kazi. Katika mwaka 2014/2015 mradi huo utakamilika.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma ya maji katika mradi wa Chiwambo Wilaya ya Masasi, Wizara yangu inakarabati miundombinu ya maji, hadi mwezi Machi, 2014 kazi ya kulaza bomba kuu la kilomita 11 kutoka kwenye chanzo cha maji hadi kwenya matanki ya Nagaga umefikia kilomita 9.7. Katika mwaka wa fedha unaofuata, mradi huu utaendelezwa na ni mategemeo yangu kwamba mradi huu utakamilika.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Shilingi bilioni 45 zitatumika kwa ajili ya kuendeleza, kutekeleza miradi inayotarajiwa kuleta matokeo ya haraka. Katika miradi hiyo jumla ya vituo 4,808 vya kuchotea maji vimejengwa kwa ajili ya kuhudumia wananchi milioni 1,253,101. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 10 zitatumika kusambaza maji kutoka kwenye mabwawa na Shilingi bilioni 35 zilizobaki zitatumika katika kutekeleza miradi yenye kuleta matokeo ya haraka iliyoainishwa kwenye kutumia vyanzo vingine vya maji ikiwa ni visima virefu na vyanzo vya maji juu ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji vijijini yanapatikana kwenye ukurasa wa 45 hadi 63 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilitekeleza *program* ya maji safi na usafi wa mazingira mijini; kujenga, kukarabati na kupanua mifumo ya majisafi na majitaka pamoja na kuzijengea uwezo mamlaka za maji mijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa *AFD*, Serikali ya Ujerumani na Umoja wa nchi za Ulaya inatekeleza miradi ya kukidhi mahitaji ya maji katika miji saba ya Bukoba, Musoma, Lindi, Kigoma, Sumbawanga, Mtwara na Babati.

Kazi zinazotekelezwa katika Manispaa ya Musoma na Bukoba ni kujenga mitambo ya kusafisha na kusukuma maji pamoja na kulaza mabomba ya usambazaji wa maji katika miji hiyo. Miradi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2014. Katika miji ya Lindi, Kigoma na Sumbawanga Wakandarasi wanaendelea na kazi ya uchimbaji wa visima, ujenzi wa mabanio, ujenzi wa matanki na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji. Miradi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2015.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Wizara yangu ilianza kutekeleza mradi wa ukarabati wa miundombinu ya maji na maboresho ya kituo cha maji cha Igombe Mjini Tabora kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 4.84. Mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano na Serikali ya Uswiss kupitia Shirika lake la *SECO*.

Mheshimiwa Spika, aidha, ukarabati na upanuzi wa chujio la maji katika Kituo cha Igombe Mjini Tabora unaogharamiwa na *program* ya Sekta ya Maji unaendelea kwa kazi ya ufungaji wa pampu tatu na kulaza bomba kuu la mita 240 kutoka Bwawani hadi kwenye chujio. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2015 na mradi huo utakapokamilika, utaleta maji ya kutosheleza mahitaji ya Mji wa Tabora kuanzia sasa mpaka mwaka 2032.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji safi na usafi wa mazingira katika Chuo Kikuu cha Dodoma, Wizara yangu inatekeleza mradi wa ujenzi wa kituo cha kusukuma maji kwenda Chuo Kikuu cha Dodoma na ujenzi wa matanki matatu yenye ujazo wa lita milioni 12. Aidha, mradi wa ujenzi wa mfumo wa uondoaji wa majitaka unaogharamu Shilingi bilioni 27.7 unaendelea kujengwa katika chuo hicho. Mradi huo unajumuisha ujenzi wa mtandao wa kusukuma majitaka wenye urefu wa kilomita 32 na ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia inaendelea na juhudi za kuwapatia wananchi wa Manispaa ya Dodoma majisafi na salama kwa kushirikiana na Serikali ya Korea kwa gharama ya Shilingi bilioni 49.62. Visima viwili vimekamilika kukarabatiwa kati ya visima 21 na visima viwili vimeshachimbwa kati ya visima vitatu na kazi inaendelea ya kulaza mabomba kutoka Mzakwe kuja Dodoma.

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji Mjini Singida. Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kiarabu pamoja na Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta, yaani *OPEC* ilikamilisha ujenzi wa mradi wa kuboresha miundombinu ya majisafi na salama Mjini Singida. Ujenzi wa miradi hiyo ilihusu uchimbaji wa visima saba ambavyo tayari vimekamilika katika maeneo ya Mwankoko na Iriyo. Kati ya usambazaji wa maji kufikia wateja inaendelea na maji yanayopatikana mjini Singida ni ya kutosha mpaka mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi ya ukarabati wa chanzo cha maji cha Mto Ruhira mjini Songea imeanza mwezi Aprili, 2014 na kazi hiyo ni kujenga banio la maji. Mradi huo utagharimu Shilingi bilioni 2.6 mpaka kukamilika. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza upatikanaji wa maji wakati wa kiangazi katika Mji wa Songea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko la shughuli za kiuchumi katika Mji wa Mtwara, Serikali inaendelea kutafuta vyanzo vipya vya maji vitakavyohudumia Manispaa ya Mtwara. Katika mwaka 2013/2014 Serikali iliingia mkataba na Mhandisi mshauri kwa ajili ya usanifu wa mradi mpya wa kutoa maji mto Ruvuma kwenda Manispaa ya Mtwara. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2014 na ujenzi wa mradi huo utaanza katika mwaka 2014/2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, iko mradi mingi ambayo imeelezwa katika kitabu chetu cha hotuba ya kupeleka maji katika Miji ya Geita, Sengerema na Nansio. Mradi wa maji wa Ziwa Victoria unaotekelezwa na mgodi wa dhahabu wa Geita kwa kushirikiana na Serikali, mradi mpya katika eneo la ziwa ambao unahusisha uwekezaji wa Serikali kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ufaransa *AFD* na utekelezaji wa mradi huo utaresha huduma ya maji pamoja na usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza pamoja na Miji ya Musoma, Bukoba, Magu, Misungwi na Lamadi na katika utekelezaji wa mradi huo jumla ya Euro milioni 104.5 zitatumika ambapo Serikali ya Tanzania itachangia Euro milioni 14.5, Benki ya Maendeleo ya Ulaya pamoja na *AFD* watachangia kwa pamoja Euro milioni 90.

Mheshimiwa Spika, iko pia miradi ya maji safi na usafi wa mazingira ya Miji inayozunguka Ziwa Tanganyika. Mradi wa maji na usafi wa mazingira kwa eneo

la Ziwa Tanganyika unatekelezwa katika nchi za Zambia, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Tanzania kwa kusimamiwa na Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa *UN Habitant*. Kwa upande wa Tanzania, mradi unatekelezwa katika Miji ya Kigoma, Kasulu, Mpanda, Namanyere, Uvinza na Kasanga. Mradi huo ulifanyiwa upembuzi yakinifu mwaka 2011 na hata hivyo utekelezaji wake ulichelewa kutokana na kutopatikana kwa fedha.

Kazi zinazotarajiwa kutekelezwa ni pamoja na usambazaji wa maji safi na usafi wa mazingira; ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua na uondoaji wa takangumu pamoja na kuzijengea uwezo taasisi zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Mikoa mipya, imeelezwa katika hotuba yangu ya bajeti katika Miji ya Mpanda, Mji wa Njombe na Mji wa Bariadi. Aidha, usanifu wa miradi ya majisafi na majitaka imeelezwa katika hotuba kwa ajili ya miji mbalimbali ikiwemo Biharamuro, Muleba, Ngara, Kayanga Umurushaka, Chato, Bunazi, katika Mkoa wa Kagera, Kakonko katika Mkoa wa Kigoma, Miji ya Namanyere, Chala, Laila kwa upande wa Rukwa, Miji ya Manyoni, Kiomboi kwa upande wa Singida na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi ya maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka maji katika maeneo mbalimbali inahusu kutoa maji Ziwa Victoria na kuyapeleka Bariadi, Mwanuhunzi, Langabilili, Maswa ambapo pia utanufaisha vijiji 40 vilivyopo kandokando ya bomba kubwa. Kazi ya kusanifu mradi huu inaendelea na tunategemea kwamba fedha zikipatikana mradi huu utatekelezwa katika mwaka 2014/2015.

Miji mingine itakayopatiwa maji kutoka Ziwa Victoria ni Mji wa Kagongwa, Isaka na Tinde na utekelezaji utaanza katika mwaka 2014/2015 na maji kutoka Muhalo kwenda Runere na Ngudu karibu unakamilika na katika bajeti ya mwaka huu tumepanga mradi wa kutoa maji kutoka Ngudu kwenda Sumve na Malya pamoja na vijiji vilivyoko kando kando ya Bomba na kutoa maji kutoka Mji wa Shinyanga kwenda katika Miji ya Maganzo, Kolandoto, Mwadui na Muhunze.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliendelea kutekeleza miradi mbalimbali iliyopangwa ili kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam. Hadi mwezi Machi, 2014 miradi iliyokuwa inaendelea kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, usanifu wa Bwawa la Kidunda pamoja na usanifu wa barabara ya kuingia kwenye eneo la bwawa umekamilika. Tathmini ya athari za kimazingira na kijamii katika maeneo ya miradi ya bwawa Kidunda na barabara

inayoelekea kwenye bwawa hilo inaendelea. Mkandarasi wa ujenzi wa barabara kuelekea kwenye eneo la Bwawa anatarajiwa kuanza kazi mara baada ya kukamilika kwa tathmini ya kijamii na kimazingira na ulipaji fidia kwa watakaoathirika na mradi huo.

Katika mwaka 2014/2015 Wizara yangu inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za ujenzi wqa bwawa hilo na hivi sasa tupo katika mashauriano kati ya Benki ya Uwekezaji ya Afrika Kusini Afrika Kusini ikishirikiana na Benki ya Rasilimali ya Tanzania na Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi huo. Ninategemea kwa hatua tuliyofikia, ujenzi huo utaanza katika mwaka 2014/2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi wa uchimbaji wa visima virefu vinane vya uchunguzi wa mwenendo wa maji chini ya ardhi amekamilisha uchimbaji wa visima viwili katika maeneo ya Mwasonga na Mkuranga. Majaribio ya uwingi *(output)* wa maji katika visima hivyo na matokeo ya vipimo vya ubora wa maji yameonesha dalili za kuwa na maji mengi yenye ubora unaofaa kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Mkandarasi anachimba kisima cha tatu eneo la Kibada na amefikia mita 200 kati ya mita 600 na kisima hicho kilitaratajiwa kukamilika mwezi Mei mwaka huu 2014.

Visima vingine vitano vitaendelea kuchimbwa na matarajio yetu ni kwamba, vitakamilika mwezi Novemba, 2014. Mkandarasi wa kuchimba visima 20 vya kuzalisha maji anaendelea na maandalizi ya vitendea kazi *(Mobilization)* na ataanza kazi ya kuchimba visima hivyo mwezi Juni.

Mheshimiwa Spika, nililielezea Bunge lako hatua iliyofikiwa katika kujiandaa katika ujenzi wa Mtambo huu katika Bunge hili. Utekelezaji wa miradi hiyo miwili ya kujenga na kukarabati Mtambo wa kuchujia maji na ulazaji wa bomba kuu kutoka Mlandizi kuja Dar es Salaam ukikamilika utaongeza upatikanaji wa maji kutoka lita milioni 82 za sasa hadi kufikia lita milioni 196 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *Millenium Challenge Corporation* la Marekani, imekamilisha upanuzi wa mradi wa maji wa Ruvu Chini. Kwa sasa Mkandarasi anafanya majaribio ya mitambo. Hadi mwezi Machi, 2014, kazi ya ulazaji wa bomba kuu kutoka mitambo ya Ruvu Chini hadi kwenye matanki ya Chuo Kikuu cha Ardhi lenye urefu wa kilomita 55.93 imekamilika kwa asilimia 62.87 sawa na kilomita 35.16. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi ujao.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi kati ya Jiji la Dar es Salaam na Mji wa Bagamoyo unahusisha kuunganisha wateja kutoka Tegeta kwenda Mpiji na Mpiji kwenda Bagamoyo. Mradi huo unajumuisha ulazaji wa mabomba ya urefu wa kilomita 732. Mtaalam Mshauri hivi sasa anaandaa nyaraka za zabuni kumwajiri Mkandarasi wa Mradi wa kuunganisha mabomba ya usambazaji maji ya urefu wa kilomita 300 kwenye eneo la Mbezi hadi Kiluvya na kuunganisha wateja 10,000 na ujenzi wa magati 30.

Mheshimiwa Spika, iko miradi mbalimbali ambayo imeorodheshwa katika kitabu cha bajeti ikiwa ni pamoja na ukamilishaji wa mradi mkubwa wa maji kutoka Masasi hadi Nachingwea na utekelezaji wa mradi wa maji wa Bunda.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Waarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA)* na *OFID* inatarajia kuanza kujenga mradi wa majisafi utakaohudumia Mji wa Orkesumet. Hivi sasa Mhandisi Mshauri anapitia upya *detailed design review* kwa ajili ya kutayarisha makabrasha ya zabuni na kupata kibali cha *BADEA* kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mradi huo.

Aidha, tumeeleza ujenzi wa mradi wa Muheza, mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji Karatu na miradi ya maji ya Miji Midogo. Ningependa kusema kwamba, katika mwaka ujao Serikali imetenga Shilingi bilioni 17.1 kwa ajili ya kukarabati na kupanua miundombinu ya maji katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji midogo 42. Fedha hizo zitatumika kutekeleza miradi inayoendelea sasa na miradi ambayo italeta ahueni kubwa ya shida ya maji katika Miji hiyo midogo.

Aidha, katika hotuba yangu tumeeleza mradi wa Mji wa Longido na miradi ya kitaifa ya maji ambayo inajengwa katika kukabiliana na upungufu wa maji katika miradi ya kitaifa na kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya miradi hiyo. Wizara yangu itatumia Shilingi bilioni 11.6 katika kufanya kazi kwenye miradi hiyo ikiwa ni pamoja na miradi ya Makonde, Maswa, Mugango, Kyabakari, Wanging'ombe, Chalinze, Masasi, Nachingwea, na KASHWASA.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee Taasisi zilizoko kwenye Wizara yangu. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)* inaendelea kutathmini na kuidhinisha bei za huduma ya maji kwa mamlaka mbalimbali za majisafi na usafi wa mazingira nchini. Katika mwaka 2013/2014, *EWURA* iliidhinisha bei mpya *za* huduma za maji kwa mamlaka 23 za Miji ya Babati, Moshi, Musoma, Kilwa Masoko, Kahama, Arusha, Bariadi, Dodoma, Dar es Salaam, Iringa, KASHWASA, Kigoma, Lindi, Mbeya, Morogoro, Mpanda, Mtwara, Mwanza, Shinyanga, Singida, Songea, Tabora na Tanga. *(Makofi)*

Mabadiliko hayo yanatokana na ongezeko la gharama za uendeshaji hususan gharama ya umeme. Aidha, *EWURA*, ilipokea na kupitisha mipango ya kibiashara *(Business Plans)* ya miaka mitatu kutoka mamlaka za maji za Kisarawe, Songea na Mtwara. Tumeelezea pia juu ya Wakala wa Uchimbaji wa visima ambaye katika mwaka huu amechimba visima 100 na tunategemea kwamba mpaka mwisho wa Juni mwaka huu visima virefu 150 vitakuwa vimekamilika. Tuko katika juhudi za kuboresha shirika hili kwa kulipatia vifaa vipya ili liweze kushiriki kikamilifu katika kutekeleza miradi ya maji mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Awamu ya Pili iliyohusisha wadau wa Sekta ya Maji ilifanyika mwezi Februari hadi Mei, 2013. Tathmini hiyo ilipitia maeneo yote yanayohitaji maboresho kwa ajili ya awamu ya pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambayo inaandaliwa kwa mwaka 2014/2015 – 2018/2019). Mapendekezo hayo yalihusu kuimarishwa kwa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; mipango ya ujenzi wa miradi ya maji Mijini na vijijini na mipango mingine kama ambavyo imeelezwa katika hotuba yangu ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2013/2014, Wizara yangu ilikabiliana na changamoto mbalimbali pamoja na mafanikio ambayo nimeyaeleza. Changamoto hizo ni pamoja na upatikanaji wa fedha, kupungua kwa rasilimali za maji, upotevu wa maji katika Miji na Vijijini, upungufu wa Wataalam katika Sekta ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyofikiwa katika kuendeleza Sekta ya Maji yametokana na michango inayoendelea kutolewa na Wadau mbalimbali. Hivyo, napenda sasa kutumia fursa hii kidogo kuwashukuru wale wote waliochangia na kuwezesha kufanikisha majukumu ya sekta hii.

Ninaamini kuwa mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2013/2014 ni kutokana na jitihada za pamoja, ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, zikiwemo na nchi wahisani, mashirika ya misaada ya Kimataifa, Taasisi zisizo za Kiserikali, Mashirika ya Kidini na Taasisi za Kifedha. Napenda kuzishukuru nchi rafiki zikiwemo Serikali za Ujerumani, Uholanzi, Uingereza, Marekani, Japan, Ufaransa, China, Uswisi, Ubeligiji, Ireland, Korea ya Kusini, Sweden, Denmark, Norway, India na Misri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia, kuzishukuru Taasisi za Kifedha za Kimataifa na Mashirika ya Kimaendeleo kwa misaada ya fedha na ushirikiano wa kitaalam katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

Taasisi hizo ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KFW),* Benki ya Ufaransa *(AFW),* Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya, Benki ya Kiarabu ya Maendeleo kwa Afrika *(BADEA)*, Mfuko wa Maendeleo wa nchi zinazotoa Mafuta, Mfuko wa Maendeleo wa Saudia, Umoja wa Ulaya, Shirika la Marekani la Changamoto za Milenia*,* Shirika la Misaada ya Maendeleo la Norway *(NORAD)* na Taasisi ya Maendeleo ya Uingereza *(DFID)*.

Mengine ni Shirika la Maendeleo la Ujerumani *(GIZ),* Mpango wa Umoja wa Mataifa (*UNDP),* Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan *(JICA)*, Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Makazi Duniani *(UN HABITAT)*, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF),* Shirika la Misaada ya Maendeleo la Sweden *(SIDA),* Shirika la Misaada ya Maendeleo la Canada *(CIDA),* Shirika la Misaada ya Maendeleo la Denmark *(DANIDA)* na Shirika la Misaada la Marekani (*USAID)*. *(Makofi)*

Aidha, tumeorodhesha mashirika mengine ya kidini ambayo yameshiriki katika kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, ningependa niwataje watu wachache ambao wametusaidia kwa kiwango kikubwa kabisa katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Kwa namna ya pekee naomba nitumie fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Naibu Waziri wa Maji; Mhandisi Bashir Mrindoko, Katibu Mkuu; Mhandisi Mbogo Futakamba, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi wote na Wakuu wa Vitengo; Maafisa na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Aidha, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Mhandishi Dkt. Bilinith Saatano Mahenge na ambaye tulianza kazi hii ya kuwapelekea wananchi wa Tanzania maji vijijini na mijini. Leo ninayo furaha kumpongeza Dkt. Mahenge kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).

Napenda pia nimshukuru aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii, Ndugu Christopher Nestory Sayi, ambaye amestaafu kwa heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kuchukua fursa hii kuishukuru familia yangu, hasa Mke wangu mpenzi Kudra Maghembe na watoto wangu Dkt. Ngwalu Maghembe, Dkt. Mwanamkuu Maghembe, Namcheja Maghembe na Namvumo Maghembe, kwa upendo wao na kunipa kila msaada ninaohitaji ili kuniwezesha kukamilisha kazi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo na kuwatambua watu hao, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh.

520,906,475,000/= kwa ajili ya matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2014/2015, ili Wizara hii iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni Sh. 30,899,443,000/= ambayo ni kama asilimia sita ya matumizi yote. Kwa hiyo, asilimia 94 ya fedha hizi ni kwa ajili ya miradi yenu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizi Sh. 15,514,444,000/= ni fedha za Matumizi Mengineyo *(OC)* na Sh. 15,384,999,000/= ni Mishahara ya Watumishi *(PE)*. Jumla ya Bajeti ya Maendeleo ni Sh. 490,007,032,000/= ambapo kati ya fedha hizo Sh. 312,066,164,000/= ni fedha za ndani na Sh. 177,940,868,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba tena nitoe shukurani zangu kwako wewe binafsi, uongozi wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara yangu ambayo ni *www.maji.go.tz*. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante. Hoja hii imeungwa mkono.

**Hotuba ya Wizara wa Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2014/2015 Kama Ilivyowasilishwa Mezani**

## HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI MHE. PROF. JUMANNE ABDALLAH MAGHEMBE (MB.) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA 2014/2015

### *1.0 UTANGULIZI*

1. **Mheshimiwa Spika,** leo hii Bunge lako Tukufu limepokea taarifa ya Mwenyekiti wa **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mbunge wa Kilolo,** kuhusiana na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maji. Naomba sasa kutoa hoja

kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2014/2015.

**2. Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati hiyo kwa kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2014/2015. Maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa wakati wa maandalizi ya Bajeti ya Wizara yangu.

**3. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee nampongeza **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dr. Jakaya Mrisho Kikwete** kwa kuongoza kwa umahiri mkubwa hatua mbalimbali za mchakato wa kupata Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni pamoja na kuunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba na hatimaye kuteua Wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba.

Aidha, napenda kumpongeza Rais wetu kwa kupata ***Tuzo ya Heshima ya Kiongozi Mwenye Mchango Mkubwa zaidi katika Maendeleo Barani Afrika kwa mwaka 2013***.

**4. Mheshimiwa Spika**, vilevile nawapongeza **Mhe. Samwel Sitta, Mbunge wa Urambo Mashariki** kwa kuchaguliwa kuwa **Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba** na **Mhe. Samia Suluhu Hassan, Mbunge wa Makunduchi** kuwa **Makamu Mwenyekiti** pamoja na Wajumbe wote wa Bunge hilo kwa kuteuliwa kwao kushiriki katika mchakato wa kupata Katiba mpya. Watanzania wana matumaini makubwa ya kuwa na Katiba mpya ambayo itakayozingatia matakwa ya kizazi cha sasa na kijacho.

**5. Mheshimiwa Spika,** naomba nitumie fursa hii, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa kuwa Mawaziri na Manaibu Waziri ili kuziongoza Wizara mbalimbali. Vilevile, nawapongeza Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wapya wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge waliochaguliwa hivi karibuni. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana nao katika kutekeleza majukumu yetu kwa maendeleo ya Taifa letu.

**6. Mheshimiwa Spika,** niungane na wenzangu walionitangulia katika kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya **Mhe. Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga** na **Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Chalinze** waliochaguliwa kujiunga na Bunge lako Tukufu. Nawatakia heri na mafanikio katika kazi yao hiyo mpya.

**7. Mheshimiwa Spika,** napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza Waziri Mkuu, **Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb) kwa hotuba**

**yake inayo**toa **mwelekeo wa utekelezaji wa kazi za Serikali. Vile**vile, nawapongeza Mawaziri walionitangulia kuwasilisha hoja zao.

**8. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu ilipokea kwa mshtuko na masikitiko makubwa, taarifa za vifo vya Waheshimiwa Wabunge wenzetu, Marehemu **William Augustao Mgimwa**, aliyekuwa **Waziri wa Fedha na Mbunge wa Kalenga** na Marehemu **Saidi Bwanamdogo**, aliyekuwa **Mbunge wa Chalinze**.

Nachukua nafasi hii kutoa pole kwako wewe Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, familia za marehemu, ndugu na wananchi wa majimbo ya Kalenga na Chalinze kwa misiba hiyo mikubwa. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. **Amin**.

**9. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwasilisha hotuba yangu ya Bajeti yenye maeneo makuu manne (i) hali ya Sekta ya Maji nchini; (ii) mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014; (iii) mpango wa bajeti kwa mwaka 2014/2015; na (iv) shukrani kwa wadau wa Sekta ya Maji na maombi ya fedha kwa mwaka 2014/2015. Maelezo yatakayotolewa katika maeneo yaliyoainishwa yamezingatia sera na mikakati ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa; sheria, kanuni na miongozo inayohusiana na Sekta ya Maji; na mgawanyo wa kazi kisekta zinazoongoza usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini.

***2.0 HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI***

**10. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA II); Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015; Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016); Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa "Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa (*Big Results Now - BRN*)" na Ahadi za Serikali. Wizara inatekeleza miradi mbalimbali katika Sekta ya Maji kulingana na Sera ya Maji ya mwaka 2002, Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Maji (2006 – 2015), Sheria na Kanuni za Maji, na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*).

**11. Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuboresha hali ya maisha ya wananchi wake kupitia Sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Maboresho makubwa ya kimfumo na kiutendaji katika sekta zote nchini (*Sector reforms*) yanaendelea kutekelezwa. Aidha, Sekta ya Maji ni moja ya sekta sita zilizopewa kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya "Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa" – BRN. Awamu ya Kwanza ya Mpango huo wa miaka mitatu (2013/2014 – 2015/2016) ni mwelekeo chanya katika kuyafikia malengo

tuliyojiwekea ya kuwafikishia wananchi huduma ya maji safi na salama, hususan katika maeneo ya vijijini.

Katika Mpango huo jumla ya miradi **1,810** itakayogharimu kiasi cha **shilingi trilioni 1.45** inatarajiwa kujengwa na itakapokamilika wananchi wapatao **milioni 15.4** zaidi watapata huduma ya maji na kufikisha idadi ya wananchi wanaopata huduma ya majisafi na salama kufikia **milioni 30.6** sawa na **asilimia 74** ya wakazi wote wa vijijini. Miradi inayotekelezwa kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji imejumuishwa kwenye Mpango wa *BRN* ili kuharakisha utekekezaji wa miradi ya maji nchini. Naomba nikiri kwamba tumepata hamasa kubwa katika utekelezaji wa *BRN* na nichukue fursa hii niwapongeze Serikali za Mitaa kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

**12. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambayo ilizinduliwa mwaka 2006/2007 na kuanza kutekelezwa mwaka 2007/2008. Programu hiyo inatekelezwa katika vipindi vya miaka mitano mitano hadi mwaka 2025/2026 na imegawanywa katika programu ndogo nne ambazo ni; Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji, Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini, Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini, na Kuimarisha na Kuzijengea Uwezo Taasisi zinazotekeleza Programu ya Maji. Hadi sasa hali halisi ya utekelezaji katika Sekta ya Maji imefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

### *2.1 RASILIMALI ZA MAJI*

**13. Mheshimiwa Spika**, Rasilimali tuliyonayo inatumika majumbani, kilimo cha umwagiliaji, uzalishaji wa nishati, mifugo, uvuvi, viwanda, uchimbaji wa madini, usafirishaji, utalii, ujenzi pamoja na maendeleo ya miji. Aidha, Rasilimali za maji zinatumika pia kwa ajili ya kupokea majitaka yaliyosafishwa na kufikia viwango vinavyokubalika baada ya matumizi. Usimamizi wa vyanzo vya maji nchini unafuata taratibu za mipango shirikishi ya usimamizi wa rasilimali za maji kwenye Bodi za Maji za mabonde tisa yaliyopo nchini, ambapo **saba** katika hayo yanahusisha majishirikishi kati ya nchi yetu na nchi jirani.

**14. Mheshimiwa Spika**, inakadiriwa kuwa rasilimali za maji juu ya ardhi zinazofaa kwa matumizi mbalimbali (*annual renewable surface water resources*) ni wastani wa **kilomita za ujazo 87** kwa mwaka. Aidha, hifadhi ya rasilimali za maji chini ya ardhi inakadiriwa kuwa **kilomita za ujazo 38**. Hata hivyo, mtawanyiko na upatikanaji wa rasilimali hizo nchini hauko sawa katika maeneo yote kutokana na tofauti ya hali ya hewa, jiografia na jiolojia.

**15. Mheshimiwa Spika**, Changamoto kubwa iliyopo kwenye usimamizi wa rasilimali za maji ni kupungua na kuharibika kwa vyanzo vya maji kutokana na shughuli za kibinadamu katika maeneo ya vyanzo vya maji na katika misitu ya hifadhi ya maji (*catchments forests and wetlands*). Hifadhi hizi zinawezesha upatikanaji wa maji juu na chini ya ardhi. Takwimu za kitaifa za rasilimali za maji zilizopo zinaonesha kuwa kiasi cha maji kwa sasa kwa kila mtanzania ni wastani wa **mita za ujazo 1,952** kwa mwaka. Endapo hatua madhubuti za utunzaji wa vyanzo vya maji hazitachukuliwa mapema, kiasi hicho kinatarajiwa kupungua hadi kufikia **mita za ujazo 883** mwaka 2035. Kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa kila mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa ni **mita za ujazo 1,700**. Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Maji inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na hali hiyo ili nchi yetu isifikie kiwango hicho cha upatikanaji wa maji kwa kila Mtanzania.

**16. Mheshimiwa Spika**, wastani wa mvua katika mabonde ya maji nchini ulikuwa unatofautiana kutokana na tabia tofauti za hali ya hewa katika maeneo hayo. Baadhi ya mabonde yalipata mvua kidogo na mengine mvua nyingi kulinganisha na viwango vya mwaka uliopita kwa mujibu wa taarifa ya mwaka wa kihaidrolojia (Novemba, 2012 – Oktoba 2013). Kwa ujumla kiasi cha mvua kilikuwa chini ya wastani katika maeneo mengi ambapo **asilimia 67** ya vituo vya mvua vilionesha kiwango cha mvua chini ya wastani. Kiwango cha mvua katika mabonde **sita (6)** kati ya **tisa (9)** ulikuwa kama ifuatavyo: Bonde la Pangani **milimita 720** ikilinganishwa na wastani wa **milimita 782** ya mwaka uliopita; Bonde la Rufiji **milimita 1,144** ikilinganishwa na **milimita 846.0;** Bonde la Wami/Ruvu **milimita 979** ikilinganishwa **milimita 1,150**; Bonde la Ziwa Tanganyika **milimita 895** ikilinganishwa na **milimita 705**; Bonde la Ziwa Victoria **milimita 968** ikilinganishwa na **milimita 1,175**; na katika Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini wastani wa **milimita 730** ikilinganishwa na **milimita 917.**

**17. Mheshimiwa Spika**, kulingana na mvua zilizonyesha katika kipindi hicho, viwango vya maji kwenye mito pia vimetofautiana kutokana na kiasi cha mvua pamoja na mitiririko ya maji kuelekea katika mito mbalimbali nchini. Viwango vya maji katika baadhi ya mito nchini vilikuwa kama ifuatavyo:- Mto Kikuletwa katika Bonde la Pangani ulikuwa na **mita za ujazo 14.66** kwa sekunde ikilinganishwa na kiasi cha **mita za ujazo 21.85** kwa sekunde kilichopatikana mwaka uliopita; Mto Ruaha Mkuu ulioko Bonde la Rufiji ulikuwa na wastani wa mita za **ujazo 9.93** kwa sekunde ikilinganishwa na mita za **ujazo 12.90** kwa sekunde; Mto Wami mita za **ujazo 18.69** kwa sekunde ikilinganishwa na mita za **ujazo 89.41** kwa sekunde; na Mto Ruvu mita za **ujazo 36.21** kwa sekunde, ikilinganishwa na wastani wa mita za ujazo **42.90** kwa sekunde. Vilevile, wastani wa mtiririko wa maji kwenye baadhi ya mito katika bonde la Ziwa Victoria ulikuwa ni mita za **ujazo 66.55** kwa sekunde katika Mto Mara na mita za **ujazo**

**27.46** kwa sekunde kwa Mto Simiyu ikilinganishwa na mita za **ujazo 102.37** na **74.78** kwa sekunde kwa mwaka uliopita katika mito hiyo kwa mtiririko huo.

**18. Mheshimiwa Spika,** hali ya maji kwenye baadhi ya mabwawa makubwa tuliyonayo haikuwa ya kuridhisha japo kulikuwa na ongezeko dogo la kina cha maji katika mabwawa hayo. Katika Bonde la Pangani bwawa la Nyumba ya Mungu usawa wa maji ulikuwa **mita 683.94** juu ya usawa wa bahari, ikilinganishwa na usawa wa **mita 683.20** mwaka uliopita na bwawa la Mabayani lilikuwa na usawa wa maji wa **mita 91.20** ikilinganishwa na **mita 91.10** juu ya usawa wa bahari. Katika mabwawa yaliyopo Bonde la Rufiji, usawa wa maji ulikuwa kama ifuatavyo; Kihansi (**mita 1,144.69**), Mtera (**mita 691.18**) na Kidatu (**mita 446.33**) juu ya usawa wa bahari ikilinganishwa na **mita 1,145.30** (Kihansi), **mita 689.19** (Mtera) na **mita 444.57** (Kidatu) kwa mwaka uliopita. Kiwango cha maji katika Bwawa la Mtera ambalo pia hutegemewa na Bwawa la Kidatu katika uzalishaji wa umeme kimeendelea kuwa chini ya kiwango. Kiwango kinachotakiwa kwa ajili ya kuendesha mitambo ya umeme katika Bwawa la Mtera ni **mita 690.00** juu ya usawa wa bahari.

**19. Mheshimiwa Spika,** usawa wa maji katika bwawa la Mindu ni **mita 506.45** juu ya usawa wa bahari ikilinganishwa na **mita 506.82** ya mwaka uliopita. Aidha, usawa wa maji katika Ziwa Victoria ulikuwa **mita 1,133.22** juu ya usawa wa bahari ikilinganishwa na **mita 1,133.06** mwaka uliopita, Ziwa Tanganyika lilikuwa wastani wa **mita 774.6** ikilinganishwa na **mita 774.3** juu ya usawa wa bahari, na Ziwa Nyasa lilikuwa na wastani wa **mita 474.48** ukilinganisha na **mita 475.71** juu ya usawa wa bahari.

**20. Mheshimiwa Spika,** kulingana na takwimu hizo, uhaba wa maji umeendelea kuyaathiri maeneo mengi nchini kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo upungufu wa mvua katika maeneo mengi hasa yale yanayotegemea mvua za msimu mmoja, kupungua kwa uwezo wa ardhi kuhifadhi maji wakati yakitiririka kuelekea mitoni kutokana na ukataji miti kwa wingi na uharibifu wa mazingira, mabadiliko ya matumizi ya ardhi, athari za mabadiliko ya tabianchi, ongezeko la shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya vyanzo vya maji na kasi kubwa ya ongezeko la watu. Hata hivyo mvua zilizonyesha mwezi Aprili 2014 ziliongeza wingi wa maji kwenye mito, mabwawa na maziwa. Katika baadhi ya mito, takwimu zinaonesha wastani wa mtiririko wa maji uliongezeka kama ifuatavyo:- Mto Mara, **mita za ujazo 260** kwa sekunde, Mto Simiyu **mita za ujazo 141.37** kwa sekunde, Mto Wami **mita za ujazo 337.63** kwa sekunde, Mto Rufiji **mita za ujazo 800** kwa sekunde na Mto Ruvu ni zaidi ya **mita za ujazo 453** kwa sekunde. Hali hiyo imedhihirika pia katika vina vya mabwawa ya Mtera **mita 693.38** juu ya usawa wa bahari, Nyumba ya Mungu **mita 684.25** na Mindu **mita 507**. Vilevile, vina vya maji kwenye maziwa nchini vimeongezeka ambapo kwa Ziwa Victoria kilikuwa **mita 1133.25**, Ziwa Nyasa **mita 476.02** na Ziwa Tanganyika

**mita 775.13** juu ya usawa wa bahari. Mvua hizo zimeongeza wingi wa maji kwenye vyanzo vya maji katika maeneo yaliyopata mvua za kutosha.

### *2.2 HUDUMA YA MAJI VIJIJINI*

**21. Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuwapatia maji safi na salama wananchi waishio vijijini katika umbali usiozidi mita 400 kutoka kwenye makazi yao kama Sera ya Maji ya mwaka 2002 inavyoelekeza. Kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, Serikali za Mitaa, Wananchi, Sekta Binafsi na Wadau wengine, Serikali inaboresha huduma za maji vijijini kwa kujenga, kupanua na kukarabati miundombinu ya maji. Jukumu la Wizara ni kutafuta fedha, kuandaa miongozo ya utekelezaji na kutoa ushauri wa kitaalam. Sekretarieti za Mikoa husimamia na kutoa ushauri wa kiufundi kwa Halmashauri katika kutekeleza miradi ya maji vijijini.

**22. Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa kina uliofanyika wakati wa matayarisho ya mpango wa *BRN* ulibaini vituo vingi vya miradi iliyokamilika kuwa havitoi huduma kutokana na miradi hiyo kutofanyiwa matengenezo ya mara kwa mara kama inavyotakiwa. Aidha, baadhi ya miradi, pampu na vipuri vimeibiwa, au miradi mingine uwezo wa vyanzo vyake umepungua kutokana na uharibifu wa mazingira katika vyanzo kama vile ukataji miti au kilimo katika vyanzo hivyo, hii ikiwa ni pamoja na mahitaji ya maji kuongezeka kutokana na kuongezeka kwa watu ukilinganisha na uwezo wa vyanzo vya miradi hiyo.

### *2.3 HUDUMA YA MAJI MIJINI*

**23. Mheshimiwa Spika,** huduma za majisafi na usafi wa mazingira mijini zinasimamiwa na kutekelezwa na Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini. Mamlaka hizo zilianzishwa mwaka 1998 chini ya **Sheria Na.8 (***Water Works Act*) ya mwaka 1997**,** kwa sasa zinasimamiwa na Sheria **Na. 12** ya mwaka 2009 ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira. Mamlaka hizo za Maji ziko kwenye miji mikuu ya mikoa na wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa.

### (a) Huduma ya Majisafi katika Miji Mikuu ya Mikoa

**24. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za maji za miji mikuu ya mikoa zinaendeshwa chini ya usimamizi wa Bodi za Wakurugenzi ambazo huteuliwa na Waziri mwenye dhamana ya maji kwa kushirikiana na uongozi wa mikoa husika. Lengo la utaratibu huo ni kuziwezesha Mamlaka hizo zijiendeshe kibiashara na hatimaye kuwa endelevu na kujitegemea kwa gharama zote za uendeshaji, matengenezo na uwekezaji kutokana na maduhuli ya mauzo ya maji. Hadi mwezi Machi, 2014 zimeundwa Mamlaka **23** za Miji Mikuu ya Mikoa**.** Mamlaka

kati ya hizo yaani **Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Moshi, Mtwara, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Tanga, Songea na Musoma** zipo **Daraja 'A'**. Mamlaka hizo zinajitegemea kwa gharama zote za uendeshaji na matengenezo, ikiwemo mishahara ya watumishi na gharama za umeme wa kuendesha mitambo ya kusukuma maji na uwekezaji mdogo. Mamlaka **nne** za **Bukoba, Kigoma, Singida** na **Sumbawanga** ziko **Daraja 'B'** na zinapata ruzuku ya kulipia sehemu ya gharama za umeme wa kuendesha mitambo. Mamlaka zilizo kwenye **Daraja 'C'** ni **Mpanda, Njombe, Bariadi, Geita**, **Babati** na **Lindi** ambazo zinaendelea kupata ruzuku ya mishahara kwa baadhi ya wafanyakazi wake pamoja na kulipia gharama za umeme wa kuendesha mitambo na uwekezaji.

**25.** **Mheshimiwa Spika,** wastani wa kiwango cha utoaji huduma ya majisafi kwenye miji mikuu ya mikoa imeendelea kuimarika. Hali hiyo imetokana na ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya majisafi katika mamlaka zote za maji za miji mikuu ya mikoa. Hadi mwezi Machi, 2014 upatikanaji wa huduma ya maji kwenye mamlaka za maji **19** isipokuwa *DAWASA* na Mamlaka za miji **minne** ya Mikoa mipya imefikia wastani wa **asilimia 86**. Upatikanaji wa huduma ya maji kwa miji minne ya Mpanda, Njombe, Geita na Bariadi ni wastani wa **asilimia 53.** Aidha, idadi ya wateja waliounganishwa kwenye mitandao ya majisafi mijini imeongezeka kutoka wateja **311,478** mwezi Machi, 2013 hadi kufikia wateja **336,898** ambalo ni ongezeko la **asilimia 8**.

**26.** **Mheshimiwa Spika,** uzalishaji wa majisafi kwa Mamlaka zote **23** za miji mikuu ya mikoa uliongezeka kutoka wastani wa lita **milioni 348.76** kwa siku mwezi Machi 2013 hadi kufikia wastani wa lita **milioni 376.07** mwezi Machi 2014. Ufungaji wa dira za maji umeongezeka hadi kufikia dira za maji **316,018** ukilinganisha na **dira 284,861** mwezi Machi *2013,* sawa na **asilimia 94 ya wa**teja wote **336,898**. Lengo ni kufikia **asilimia 100** ya ufungaji wa dira za maji kwa wateja ifikapo mwezi Desemba 2014. Wastani wa upotevu wa maji (*Non Revenue Water – NRW*) kwenye mifumo ya usambazaji maji umefikia **asilimia 38.**Upotevu huu wa maji unatokana na uchakavu wa miundombinu ya usambazaji wa maji na wizi wa maji**.** **Wastani wa** makusanyo ya maduhuli yatokanayo na mauzo ya maji kwa mwezi kwa Mamlaka zote za maji mijini isipokuwa *DAWASCO*, yameongezeka hadi kufikia **shilingi bilioni 6.36** (kwa mwezi) mwezi Machi 2014 kutoka wastani wa **shilingi bilioni 5.58,** mwezi Machi 2013. Ongezeko hili ni sawa na **asilimia 14**. Kuongezeka kwa maduhuli hayo, kumeziwezesha Mamlaka kuboresha huduma zinazotolewa ikiwa ni pamoja na kukarabati miundombinu na kugharamia shughuli za uendeshaji. Wizara itaendelea kuimarisha Mamlaka za maji ili kuongeza maduhuli ziweze kufikia malengo yaliyoainishwa kwenye Mikataba ya Utendaji kazi waliosaini na Wizara na *EWURA*.

### (b) Huduma ya Majisafi katika Miradi ya Kitaifa, Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo

**27. Mheshimiwa Spika,** miradi **nane** ya kitaifa ya *KASHWASA, Handeni Trunk Main–HTM*, Maswa, Mugango-Kiabakari, Chalinze, Wanging'ombe, Makonde na Masasi-Nachingwea inasimamiwa na Wizara yangu chini ya kifungu **Na. 41** cha Sheria ya Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009. Aidha, huduma za majisafi kwa Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo hutolewa na Mamlaka za maji za miji hiyo ambazo husimamiwa na Bodi za Wakurugenzi zinazoteuliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na kusimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwa sasa miradi ya maji ya kitaifa na mamlaka **96** ngazi ya Wilaya na Miji Midogo zipo daraja C. Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI inaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka hizo ili zipande daraja kutoka C hadi madaraja ya B na A. Nia yetu ni kuziwezesha kujiendesha kibiashara na hivyo kupunguza mzigo kwa Serikali.

### (c) Huduma ya Majisafi katika Jiji la Dar es Salaam

**28. Mheshimiwa Spika,** mmiliki na msimamizi wa usambazaji wa huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka Jijini Dar-es-Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo ni *Dar es Salaam Water Supply and Sewerage Authority–DAWASA*. Serikali kupitia *DAWASA* iliingia Mkataba wa kukodisha shughuli za uendeshaji wa huduma ya majisafi na majitaka na Shirika la Usambazaji Maji Jijini Dar es Salaam (*Dar es Salaam Water Supply and Sewerage Corporation- DAWASCO*). Lengo ni kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za utoaji huduma ya majisafi na majitaka.

**29. Mheshimiwa Spika,** idadi ya wakazi wanaopata huduma ya majisafi sasa katika Jiji la Dar es Salaam ni **asilimia 68** kwa wastani wa **saa tisa (9)** kwa siku**.** Kati ya hao**, asilimia 55** wanapata huduma ya maji kutoka kwenye mitandao ya mabomba na wanaobaki wanapata huduma ya maji kutoka kwenye visima, magati na huduma ya magari (*water bowsers*). Lengo la Serikali ni kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji hadi kufikia **asilimia 75** mwezi Juni, 2016. Mahitaji ya maji kwa hivi sasa ni lita **milioni 450** kwa siku ikilinganishwa na uwezo wa mitambo wa kuzalisha maji lita **milioni 300** kwa siku.

Hata hivyo, mwezi Machi 2014, uzalishaji wa maji ulishuka na kufikia wastani wa lita **milioni 260** kwa siku. Upungufu huo wa uzalishaji unatokana na tatizo la kuharibika kwa mara kwa mara kwa mitambo ya kusukuma maji (pampu kubwa za Ruvu Juu), muda mrefu wa matengenezo, miundombinu chakavu na hitilafu za umeme. Aidha, mpaka mwezi Machi, 2014 wateja **137,856** walikuwa wameungiwa huduma ya maji na kufungiwa mita, ikilinganishwa na wateja **118,942** mwezi Machi, 2013, hilo ni ongezeko la **asilimia 16**. Ongezeko la wateja

limeongeza wastani wa makusanyo ya maduhuli yanayotokana na mauzo ya maji kutoka **shilingi bilioni 3.38** kwa mwezi Machi, 2013 hadi kufikia **shilingi bilioni 3.57** mwezi Machi, 2014. Pamoja na kuwepo kwa changamoto kubwa inayotokana na uvujaji, uchakavu wa miundombinu, wizi wa maji na uharibifu unaoweza kutokea wakati wa ukarabati wa miuondombinu ya barabara huharibu miundombinu ya maji. na kuongeza upotevu wa maji na kupunguza upatikanaji wa huduma ya maji. Serikali inaendelea kukabiliana na changamoto hizi na kuzipatia ufumbuzi hatua kwa hatua.

**(d) Huduma ya Uondoaji wa Majitaka Mijini**

**30. Mheshimiwa Spika,** takwimu zilizopo zinaonesha kwamba, huduma ya uondoaji majitaka ni **asilimia 18** kufikia mwezi Machi 2014, ikilinganishwa na malengo ya MKUKUTA II ya kuongeza kiwango cha huduma ya majitaka kufikia **asilimia 22** ifikapo 2015. Miji yenye mitandao ya majitaka ni Arusha, Moshi, Tanga, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Iringa, Songea, Tabora, Morogoro na Dar es Salaam. Hali ya huduma ya uondoaji wa majitaka mijini siyo ya kuridhisha.

Aidha, idadi ya wateja waliounganishwa kwenye mtandao wa majitaka imeongezeka kutoka **21,775** mwezi Machi, 2013 hadi kufikia wateja **22,976** mwezi Machi, 2014. Pamoja na ongezeko hilo, bado wastani wa huduma ya uondoaji majitaka mijini ni **asilimia 18** tu. Hali hiyo inasababishwa na mwamko mdogo wa wananchi kujiunga kwenye mtandao wa majitaka katika miji hiyo. Vilevile, miundombinu ya majitaka kwa baadhi ya miji ni chakavu na inahudumia maeneo machache.

## *2.4 KUJENGA UWEZO WA TAASISI ZIILIZO CHINI YA PROGRAMU YA MAENDELEO YA SEKTA YA MAJI*

**31. Mheshimiwa Spika**, kulingana na mahitaji ya rasilimali watu ya kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji na Mpango wa *BRN*, Wizara inahitaji wataalam **8,749** kwa kipindi chote cha utekelezaji wa Programu (2006/2007 hadi 2025) ili kutekeleza majukumu kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Hivi sasa, Sekta ya Maji ina jumla ya wataalam **1,538.** Kwa mwaka wa kwanza (2013/2014) wa utekelezaji wa Mpango wa *BRN*, jumla ya wataalam **835** walihitajika kuajiriwa kwenye Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini. Kati ya Wataalam hao, wahandisi ni **302** na mafundi sanifu **533**. Katika mwaka 2013/2014 Serikali imeiidhinisha ajira ya wataalamu (wahandisi) **125** wapya na mafundi sanifu (*FTC*) **350**.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA 2013/2014 NA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2014/2015

**32. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu ilitekeleza miradi inayohusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini na mijini na masuala mtambuka. Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2013/2014 na malengo ya mwaka 2014/2015 kwa Sekta ya Maji unaelezwa katika sura hii ya Bajeti.

## 3.1 RASILIMALI ZA MAJI

**33. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014 Wizara yangu ilisimamia na kuendeleza rasilimali za maji, ikiwemo kuchunguza, kutathmini na kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji nchini pamoja na rasilimali za majishirikishi (*transboundary water resources*); na kuimarisha Bodi za Maji za Mabonde ili zisimamie kikamilifu rasilimali hizo. Kazi nyingine ni kuandaa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, kusanifu na kusimamia ujenzi wa miundombinu ya kipaumbele, yakiwemo mabwawa.

### 3.1.1 Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

### (a) Mwenendo wa Rasilimali za Maji

**34. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kuimarisha vituo vya kupima wingi na ubora wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi ili kuboresha upatikanaji wa takwimu na upatikanaji wa taarifa sahihi. Katika mwaka 2013/2014, jumla ya vituo **29** vya kupima mtiririko wa maji mitoni, vituo **14** vya hali ya hewa, vituo **sita (6)** vya ufuatiliaji maji chini ya ardhi, vituo **vitatu (3)** vya kupima maji kwenye maziwa na vituo **saba (7)** vya kupima mvua vilijengwa. Vituo hivyo vipo katika mabonde ya Wami-Ruvu, Pangani, Ziwa Rukwa, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini. Aidha, ukarabati ulifanyika katika vituo **80** vya kupima mtiririko wa maji kwenye mito, vituo **18** vya hali ya hewa, vituo **viwili (2)** vya ufuatiliaji wa maji chini ya ardhi, vituo **vitatu (3)** vya kupima maji kwenye maziwa, vituo vitano (5) vya kupima maji kwenye mabwawa na vituo **sita (6)** vya kupima mvua. (**Jedwali Na.1**)

**35. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha upatikanaji wa takwimu sahihi za hali ya maji nchini, Bodi za Maji za Mabonde zimekusanya na kuchanganua takwimu za hali ya maji katika vituo mbalimbali. Vituo hivyo vinajumuisha vituo **203** vya kupima mtiririko wa maji mitoni, **vituo 12** vya kupima usawa wa maji katika maziwa na mabwawa, vituo **122** vya kupima mvua, na vituo **29** vya kupima hali ya hewa. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea

kujenga na kukarabati **vituo 134** vya kupima mtiririko wa maji mitoni, **vituo 17** vya hali ya hewa, **vituo 35** vya mvua na **vituo 52** vya kupima maji chini ya ardhi pamoja na kukusanya takwimu kwenye mabonde yote nchini.

**36. Mheshimiwa Spika**, takwimu na taarifa zinazokusanywa kutoka kwenye vituo hivyo husaidia kutambua hali ya maji kwa nyakati tofauti kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini, hivyo kuwezesha maandalizi ya mipango na kutoa maamuzi sahihi ya ugawaji wa rasilimali za maji kwa matumizi mbalimbali. Aidha, takwimu na taarifa hizo hutumika katika usanifu na ujenzi wa miundombinu ya miradi ya maji, mabwawa na madaraja pamoja na utafiti wa mabadiliko ya tabianchi.

**(b) Kuhifadhi wa Mazingira na Vyanzo vya Maji**

**37. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza mikakati ya kuhifadhi vyanzo vya maji, Wizara yangu imeendelea kuvitambua, kuviwekea mipaka na kuvitangaza kuwa maeneo tengefu. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya vyanzo **153** vilitambuliwa kuwa katika hatari ya kuharibiwa na kuathiriwa kwa sababu mbalimbali ikiwemo ongezeko la shughuli za kibinadamu. Kati ya hivyo, vyanzo **59** vimebainishwa na na kuandaliwa ili vitangazwe kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji. Hadi mwezi Machi 2014, mapendekezo ya vyanzo **saba (7)** kati ya vyanzo vilivyobainishwa katika Bonde la Ziwa Rukwa viko tayari kutangazwa rasmi kuwa maeneo tengefu. Maeneo hayo ambayo hayakuhitaji fidia ni maeneo ya vyanzo vya maji chini ya ardhi yaliyoko Chokaa, Kidole, Kiswaga, Matundasi A, Matundasi B, Mkola na Bwawa la Milala.

**38. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea na taratibu za kutangaza vyanzo vya maji vilivyobainishwa kuwa maeneo tengefu likiwemo Bwawa la Mtera katika Bonde la Rufiji. Vilevile, katika Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini vyanzo vya maji vya chemichemi za Mbwinji, Ndanda, Mwena na Liputu kwenye miteremko ya milima ya Makonde vimewekewa mipaka kwa ajili ya kuvihifadhi. Uchoraji wa ramani za maeneo husika unaendelea na utakapokamilika yatatangazwa kuwa maeneo tengefu. Aidha, uwekaji wa mipaka unaendelea kwenye vyanzo vya maji vya Mitema-Kitangari kwa lengo la kuvihifadhi. Wizara yangu itaendelea kubaini na kuweka mipaka maeneo mengine ya vyanzo vya maji ili kuyakinga dhidi ya uharibifu wa mazingira.

**39. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maji imeandaa Mpango Maalum wa miaka mitano wa Kuhifadhi na Kutunza Vyanzo vya Maji utakaoanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2014/2015. Mpango huo umeainisha maeneo ya utekelezaji ili kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya maji kwa maendeleo endelevu ya sasa na vizazi vijavyo. Mpango huo utahusisha kutoa elimu kwa umma na kuimarisha ushiriki wa wadau katika shughuli za uhifadhi, utunzaji na ulinzi wa rasilimali za maji;

kujenga uwezo wa wadau wa sekta ya maji katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji; na kusaidia shughuli mbadala za kiuchumi ili kupunguza shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya vyanzo vya maji. Shughuli hizo ni pamoja na ukataji miti, kilimo cha "vinyungu" na kilimo katika kingo za mito. Wizara kwa kushirikiana na wadau hao itaendelea kuhakikisha kwamba vyanzo vya maji vinatunzwa na kulindwa.

**40.** **Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji, hadi mwezi Machi 2014, jumla ya Jumuiya **99** za Watumiaji Maji ziliundwa. Kati ya hizo Jumuiya **18** zimeundwa katika kipindi cha mwaka 2013/2014. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaunda Jumuiya za Watumiaji Maji **20** na Kamati **13** za kulinda misitu katika vyanzo vya maji (*catchment areas*) na kuendelea kuimarisha zilizopo. Taarifa ya tathmini ya athari kwa mazingira kwa mabwawa sita ya Itobo, Uchama, Nkiniziwa, Leken, Enguikument I na Enguikument II yaliyopo katika Bonde la Kati imekamilika na kuwasilishwa *NEMC* kwa hatua zaidi. Kazi ya tathmini za athari kwa mazingira kwa ajili ya miradi ya mabwawa ya Farkwa na Ndembera zinaendelea. Vilevile, tathmini ya athari kwa mazingira ya mradi wa bwawa la Kidunda pamoja na barabara inayoelekea kwenye bwawa inaendelea.

### (c) Kudhibiti Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji

**41.** **Mheshimiwa Spika**, udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji ni muhimu katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, ukaguzi ulifanyika katika Bonde la Kati kwenye maeneo **tisa (9)** ya viwanda, migodi **46** na hoteli **tatu (3)** na katika Bonde la Pangani, ukaguzi ulifanyika katika mifumo ya utoaji majitaka ya viwanda **vitatu (3)** na kuangalia utendaji kazi (*performance assessment*) wa mabwawa ya majitaka ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi Mazingira, Arusha.

**42.** **Mheshimiwa Spika,** vilevile, Bodi ya Maji ya Bonde la Pangani ilikagua maeneo mbalimbali yaliyopo katika Mkoa wa Kilimanjaro ili kubaini na kuorodhesha shughuli zinazoathiri ubora wa vyanzo vya maji (*Inventory of polluting activities*). Maeneo yafuatayo yalibainishwa:- Viwanda vya kahawa, viwanda vya mkonge, kiwanda cha chokaa, mashamba ya maua, maeneo ya kutengeneza na kuoshea magari na maeneo ya vyanzo vya maji yanayochafuliwa kwa kuweka makazi na kutupa taka ngumu.

**43.** **Mheshimiwa Spika**, ukaguzi huo ulibaini baadhi ya viwanda kutokuzingatia taratibu za utiririshaji wa majitaka kwenda kwenye vyanzo vya maji. Wizara iliviagiza viwanda hivyo kutengeneza mifumo ya kusafisha majitaka kabla ya kuyatiririsha kwenda kwenye vyanzo vya maji kwa kuzingatia Sheria **Na. 20** ya mwaka 2004 ya Usimamizi wa Mazingira. Wizara kwa kushirikiana na

*NEMC* itaendelea kufanya ukaguzi kwenye maeneo ya viwanda na migodi na kuchukua hatua stahiki. **Jedwali Na. 2** linaonesha matokeo ya ukaguzi wa vyanzo vya maji unaotokana na majitaka kutoka viwandani na migodini.

**(d) Kutafuta Vyanzo Vipya vya Maji**

**44. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imeendelea na kuhakikisha vyanzo vipya vya maji vilivyobainishwa vinafanyiwa tathmini na usanifu ili viweze kujengwa na kuongeza upatikanaji wa maji nchini. Katika mwaka 2013/2014, Mtaalam Mshauri amekamilisha kazi ya uchunguzi wa kina wa miamba na ameendelea na kazi ya usanifu kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Farkwa kwenye Mto Bubu, Wilaya ya Chemba. Mradi huo unatarajiwa kuwapatia maji wakazi wa Manispaa ya Dodoma pamoja na Miji ya Chamwino, Bahi na Chemba. Aidha, Wizara inaendelea na maandalizi ya ujenzi wa Bwawa la Ndembera katika Bonde la Rufiji litakalotumika kudhibiti mwenendo na mtiririko wa maji katika kipindi cha mwaka mzima kwenye Mto Ruaha Mkuu. Bwawa hilo pia linatarajiwa kutumika kwa shughuli za kilimo cha umwagiliaji na kuzalisha umeme. Vilevile, Mtaalam Mshauri amewasilisha taarifa ya upembuzi yakinifu na anaendelea na kazi ya usanifu wa kina.

**45. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, hatua za awali za ujenzi wa bwawa la Kidunda zimekamilika ambapo Mtaalam Mshauri anaandaa taarifa ya mwisho ya usanifu na uandaaji wa zabuni (*Final Design Report & Tender Documents*). Taratibu za ununuzi wa Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya kuelekea kwenye eneo la bwawa zinatarajiwa kuanza mara baada ya kukamilika kwa mapitio ya Tathmini ya Athari za Kimazingira na Kijamii *(Environmental and Social Impact Assessment-ESIA)* na kulipa fidia kwa watakaoathirika na mradi. Katika mwaka 2014/15, Wizara imetenga fedha za kulipa fidia, na kujenga barabara.

**46. Mheshimiwa Spika,** kwa mradi wa visima vya kuchunguza mwenendo wa maji chini ya ardhi katika maeneo ya Kimbiji na Mpera, Wizara yangu ilipanga kuchimba visima **nane (8)**. Hadi mwezi Machi, 2014 visima **viwili (2)** vya uchunguzi vimekamilika na kisima cha tatu kinachimbwa na kimefikia mita **200**. Inatarajiwa kuwa kufikia mwezi Novemba, 2014 visima vyote vitakuwa vimekamilika. Katika mwaka 2014/2015 Serikali italipa fidia kwa wananchi watakaoathirika na uchimbaji wa visima ili kukamilisha mradi wa visima wa Kimbiji na Mpera kama ilivyopangwa. Baada ya kulipa fidia kwenye eneo la mita 60 kuzunguka kila kisima katika maeneo ya Kimbiji na Mpera kukamilika, Serikali imekamilisha uhakiki wa fidia katika maeneo ya Luzando na Kisarawe II na ulipaji wa fidia umeanza kwa eneo litakapojengwa tanki la Kisarawe II pamoja na kwa eneo la Luzando. Vilevile, uthamini katika maeneo ya ujenzi wa njia za mabomba za barabara kuelekea kwenye visima umeanza, na maombi

ya kupata Wathamini yamewasilishwa kwenye Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali.

**47. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliendelea kutafiti maji chini ya ardhi kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa maji. Utafiti ulibaini maeneo **501** yanayofaa kuchimbwa visima vya maji katika mabonde ya Rufiji **(33)**, Bonde la Kati **(39)**, Pangani **(149)**, Wami-Ruvu **(18)**, Ziwa Victoria **(40)**, Ziwa Rukwa **(73)**, Ziwa Tanganyika **(80)** na Ruvuma na Pwani ya Kusini **(69)**. Wizara yangu pia ilisimamia uchimbaji wa visima vya utafiti **152** katika mabonde ya Rufiji **(40)**, Bonde la Kati **(3),** Pangani **(4)**, Ruvuma na Pwani ya Kusini **(42)** Wami-Ruvu **(55)**, Ziwa Victoria **(4)** na Ziwa Tanganyika **(4)**. Kwa mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea kutafiti maji chini ya ardhi katika maeneo mengine zaidi.

**48. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kushirikiana na Serikali ya Misri katika utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa uchimbaji wa visima **70**; kati ya hivyo, maandalizi ya uchimbaji wa visima **30** yameanza katika maeneo ya Wilaya za Kiteto **(10)**, Same **(8)**, Mwanga **(1)**, Bariadi **(2)** na Itilima **(9)** ambapo Mkandarasi amekabidhiwa maeneo ya kazi. Vilevile, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ilichimba visima **53** kati ya visima **55** vilivyopangwa katika Wilaya za Kisarawe na Kilosa. Visima **25** vilichimbwa katika Wilaya ya Kilosa na visima **28** Wilaya ya Kisarawe. Visima hivyo viko katika hatua za mwisho za ufungaji wa pampu. Katika mwaka 2014/2015, kazi ya uchimbaji wa visima vilivyobaki itakamilishwa katika Wilaya ya Kisarawe.

**49. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu ilisajili kampuni **mbili (2)** za uchimbaji visima vya maji kati ya kampuni **sita (6)** zilizoomba. Kampuni **nne (4)** hazikukidhi vigezo kulingana na Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya Mwaka 2009. Uratibu huo unalenga kuhakikisha kwamba taratibu za kitaalam zinafuatwa ili kuhakikisha visima vina ubora kwa matumizi endelevu. Hadi mwezi Machi 2014, kampuni binafsi **137** zilikuwa zimesajiliwa. Aidha, jumla ya visima vya maji **546** vilichimbwa katika maeneo mbalimbali nchini. Kati ya hivyo, visima **100** vilichimbwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*DDCA*) na visima **446** vilichimbwa na kampuni binafsi**.**

### (e) Matumizi Bora ya Rasilimali za Maji

**50. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu kupitia Bodi za Maji za Mabonde imeendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu umuhimu wa usimamizi endelevu wa rasilimali za maji, hususan kutoa vibali vya matumizi ya maji na utiririshaji wa majitaka. Hadi mwezi Machi 2014, jumla ya vibali vipya **586**

vilitolewa katika mabonde ya Pangani **(105)**, Rufiji **(92)**, Wami-Ruvu **(112)**, Ruvuma na Pwani ya Kusini **(21)**, Bonde la Kati **(3)**, Ziwa Victoria **(37)**, Ziwa Rukwa **(66),** Ziwa Tanganyika **(56)** na Ziwa Nyasa **(94)**. Jumla ya maombi **223** yalipokelewa katika mabonde ya Ziwa Rukwa **(19)**, Ziwa Tanganyika **(50)**, Wami-Ruvu **(77)**, Ziwa Nyasa **(60)** na Ruvuma na Pwani ya Kusini **(17)**. Vilevile, usajili wa vibali vya zamani (*re-registration)* ulifanyika ambapo vibali **479** kutoka katika mabonde ya Ziwa Nyasa **(4)**, Ziwa Victoria **(370)** na Wami-Ruvu **(105)** vilihakikiwa na kusajiliwa upya kulingana na matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji **Na. 11** ya mwaka 2009..

**51. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, vibali **15** vya kutiririsha majitaka vilitolewa katika mabonde ya Ziwa Victoria **(10),** Ziwa Rukwa **(3)** na Pangani **(2)**. Aidha, zoezi la kuwatambua watumiaji maji kwa matumizi mbalimbali lilifanyika ili waweze kupatiwa elimu na hatimaye kuweza kufuata taratibu za kisheria za matumizi endelevu ya maji. Jumla ya watumiaji maji **835** walibainishwa katika mabonde ya Pangani **(513),** Ziwa Victoria **(27)**, Ziwa Tanganyika **(162)**, Ziwa Nyasa (24), Ruvuma na Pwani ya Kusini **(19)** na Wami-Ruvu **(90)**.

### (f) Mipango ya Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

**52. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliendelea na utayarishaji wa Mipango itakayo simamia na kuendeleza Rasilimali za Maji (*IWRM&D Plans*) na kuwahusisha wananchi katika mabonde yote tisa. Hadi mwezi Machi 2014, rasimu za mwisho za mipango katika mabonde ya Ruvuma na Pwani ya Kusini, Bonde la Kati, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa zilifanyiwa marekebisho na Wataalam Washauri baada ya kupokea maoni na marekebisho kutoka kwa wadau. Wataalam Washauri katika bonde la Ziwa Rukwa, Pangani na Rufiji wamewasilisha *Interim Reports* na Wizara imetoa maoni kuhusu taarifa hizo kwa ajili ya maboresho.

**53. Mheshimiwa Spika,** katika Bonde la Wami-Ruvu, taarifa ya mwisho ya mpango shirikishi wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji imekamilika na kuwasilishwa wizarani mwezi Desemba, 2013.

Mpango Shirikishi wa Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika Ziwa Victoria upo katika hatua za awali za ukusanyaji wa takwimu na taarifa muhimu kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea na utayarishaji wa Mpango Shirikishi wa Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika Ziwa Victoria. Aidha,

Wizara itafanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii kabla ya utekelezaji wa mipango iliyoainishwa na (*IWRM&D*).

**(g) Kuimarisha Bodi za Maji katika Mabonde**

**54. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imeendelea kuzijengea uwezo Bodi za Maji za Mabonde kwa kutoa mafunzo kwa watumishi, kujenga ofisi na kununua vitendea kazi. Katika mwaka 2013/2014, watumishi **81** wa mabonde **nane** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na semina mbalimbali kama ifuatavyo; Bonde la Kati **(3)**, Ziwa Nyasa **(8)**, Pangani **(36)**, Ruvuma na Pwani ya Kusini **(6)**, Wami-Ruvu **(2)**, Ziwa Victoria **(10)**, Rufiji **(3)** na Bonde la Ziwa Rukwa **(13)**. Mafunzo yalihusu jinsi ya kushirikisha wadau na jamii katika utunzaji na usimamizi wa rasilimali za maji, usimamizi wa takwimu, sheria mpya ya ununuzi, mfumo wa maamuzi (*Decision Support System - DSS*), mifumo ya teknolojia ya *Quantum GIS*, *Google earth and ArcGIS software - conservation strategies* na usimamizi wa mazingira (*Environmental Management System - EMS*). Mafunzo hayo yalilenga kuongeza ujuzi na ufanisi katika utendaji wa kazi.

**55. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa jengo jipya la ofisi ya Bonde la Ziwa Nyasa umekamilika na litakabidhiwa mwezi Julai 2014. Aidha, ujenzi wa Ofisi za Bodi za Maji za Mabonde ya Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Bonde la Kati umeanza. Taarifa za usanifu wa majengo ya Ofisi za Bodi za Maji za Mabonde yaliyobaki ya Wami-Ruvu, Ruvuma na Pwani ya Kusini, Rufiji, Pangani, na Ziwa Rukwa, zimekamilika na kuwasilishwa kwa uhakiki. Kwa mwaka 2014/2015, taratibu za kuwapata Wakandarasi wa ujenzi wa ofisi zilizobaki zitakamilika na ujenzi kuanza.

**56. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inaimarisha Bodi za Maji za Mabonde ili ziweze kufanya tafiti za rasilimali za maji kwa lengo la kupata ufahamu zaidi kuhusu rasilimali zetu na katika usimamizi na uendelezaji wake. Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa imefanya utafiti (*Bathymetry)* katika Ziwa Rukwa, na Ziwa hilo litakuwa la nne kufanyiwa utafiti wa aina hiyo hapa nchini baada ya Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa.

**(h) Makusanyo ya Maduhuli**

**57. Mheshimiwa Spika,** Bodi za Maji za Mabonde hukusanya maduhuli yatokanayo na ada za matumizi ya maji na kutumia mapato hayo (*retention*) katika usimamizi, utunzaji na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini. Hadi mwezi Machi 2014, jumla ya **shilingi 1,527,245,592** zilikusanywa. Makusanyo hayo ni sawa na **asilimia 86.34** ya lengo la **shilingi 1,768,887,117** zilizopangwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2013/2014. Katika mwaka 2014/2015, Bodi za Maji za Mabonde zimelenga kukusanya kiasi cha **shilingi 2,576,000,000** kutoka

vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwa ni pamoja na ongezeko la Ada ya matumizi ya maji kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 3.**

**(i) Kudhibiti Migogoro Miongoni mwa Watumiaji wa Maji**

**58. Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa majukumu ya Bodi za Maji za Mabonde ni kusuluhisha migogoro katika matumizi ya maji kwa kushirikiana na Jumuiya za Watumiaji Maji na inapobidi vyombo vya sheria hutumika. Katika mwaka 2013/2014, migogoro **29** ya watumiaji maji ilijitokeza, ambapo migogoro **21** kati ya hiyo ilisuluhishwa katika Mabonde ya Maji ya Pangani **(5),** Wami/Ruvu **(10),** Ziwa Victoria **(2)**, Rufiji **(2)** Ziwa Nyasa **(1)**, na Ruvuma na Pwani ya Kusini **(1).** Migogoro mingine **sita (6)** katika Bonde la Kati **(4)** na Ziwa Victoria **(2)** ipo katika hatua mbalimbali za mashauriano nje ya mahakama;**.** Migogoro **miwili (2)** iliyobaki katika Bonde la Pangani iko mahakamani. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea kusuluhisha migogoro ya watumiaji maji kama itakavyojitokeza na kutoa elimu ya ugawanaji na utunzaji wa rasilimali za maji.

**(j) Usimamizi wa Rasilimali za Majishirikishi**

**59. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kushirikiana na nchi nyingine zinazochangia rasilimali za maji shirikishi kwa kuunda vyombo vya pamoja na kuimarisha vilivyopo ili kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali hizo. Azma ya ushirikiano huo ni kuhakikisha kunakuwepo na mifumo ya uwazi na usawa ya uendelezaji na utumiaji wa rasilimali za maji. Mabonde **saba (7)** ya maji kati ya **tisa (9)** yaliyopo nchini yanavuka mipaka ya nchi yetu na hivyo kuwa na ulazima wa kushirikiana na **nchi** nyingine **17** majirani. Nchi hizo ni Angola, Botswana, Namibia, Zambia, Zimbabwe, Malawi, Msumbiji, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Sudan, Sudan Kusini, Uganda na Eritrea. Ushirikiano wa kitaasisi na nchi hizo unatekelezwa kama ifuatavyo:-

**(i) Bonde la Mto Nile**

**60. Mheshimiwa Spika**, Umoja wa Ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile (*Nile Basin Initiative – NBI*) ulianzishwa rasmi mwaka 1999. Umoja huo ni chombo cha mpito kuelekea kwenye uundwaji wa Kamisheni ya Bonde la Mto Nile. Madhumuni ya kuanzishwa kwa umoja huo ni kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji, mazingira, nishati, kilimo, mafunzo na kujenga uwezo kwa taasisi zilizopo katika nchi husika. Jumla ya **nchi 11** zinaunda umoja huo ambazo ni Burundi, Ethiopia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Misri, Rwanda, Sudan, Sudan Kusini, Uganda na Tanzania na nchi ya Eritrea ikiwa ni mtazamaji (*observer*).

**61.** **Mheshimiwa Spika**, Nchi **saba** za Burundi, Ethiopia, Uganda, Rwanda, Kenya, Sudan Kusini na Tanzania zilisaini Mkataba wa Kudumu wa Ushirikiano wa nchi hizo utakaoanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Nile. Hadi sasa, nchi za Ethiopia na Rwanda tayari zimeridhia Mkataba huo na Tanzania ipo katika hatua za kukamilisha taratibu za kuridhia. Aidha, nchi za Misri, Sudan na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo zinaendelea na misimamo yao ya kutosaini Mkataba huo. Kulingana na matakwa ya Mkataba huo, nchi **sita (6)** zikikamilisha kuridhia Kamisheni ya Bonde la Mto Nile itaanzishwa. Katika mwaka 2014/2015, nchi ambazo zilisaini Mkataba huo zitakamilisha taratibu za kuridhia kwa kuzingatia sheria za nchi zao. Tanzania itaendelea kufuatilia kwa karibu suala hili ambalo ni la manufaa kwa nchi yetu.

**(ii) Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria**

**62.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali za Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda zinatekeleza Awamu ya Pili ya Mradi wa Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria *(LVEMP II)*. Lengo la mradi ni kuimarisha usimamizi wa pamoja wa rasilimali za Bonde la Ziwa Victoria kwa kudhibiti uharibifu wa mazingira katika ziwa hilo. Aidha, nchi yetu inanufaika na mradi huo kwa kuimarisha Taasisi zinazohusika na hifadhi ya maji na samaki; ukarabati wa mifumo ya kusafisha majitaka katika miji ya Mwanza, Musoma na Bukoba. Vilevile, Halmashauri za Wilaya za Maswa, Itilima, Busega, Bariadi, Magu, Meatu, Kwimba, Sengerema, Geita, Chato, Muleba, Karagwe, Kyerwa na Misenyi zimeingizwa kwenye awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huo.

**63.** **Mheshimiwa Spika**, jumla ya miradi midogo ya kijamii **176** yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 4.5** inatekelezwa katika eneo la mradi. Hadi mwezi Machi 2014, miradi **48** imekamilika na itakabidhiwa kwa jamii. Vilevile, miradi **22** mikubwa ya kijamii yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 5.5** imeanza kutekelezwa katika Halmashauri za Wilaya za Musoma Mjini, Maswa, Bariadi, Kwimba, Magu, Meatu na Jiji la Mwanza. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo na kuhakikisha Wataalam Washauri wanakamilisha kazi zao ambazo ni pamoja na kuoanisha Sera, Sheria, Kanuni na Viwango vya utupaji majitaka katika rasilimali za maji zilizopo kwenye Bonde la Ziwa Victoria.

**(iii) Bonde la Mto Mara**

**64.** **Mheshimiwa Spika,** Bonde la Mto Mara, ni moja kati ya mabonde ya mito inayoingiza maji katika Ziwa Victoria na linahusisha nchi **mbili** za Kenya (inayomiliki **asilimia 65** ya bonde) na Tanzania **asilimia 35**. Bonde hilo ni eneo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi pamoja na bayoanuai zilizopo. Utekelezaji wa miradi na shughuli mbalimbali katika Bonde hilo kikanda

unasimamiwa na Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria *(Lake Victoria Basin Commission-LVBC).* Katika kuimarisha ushirikiano uliopo katika nchi zetu mbili, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Maadhimisho ya "Siku ya Mara" ambayo lengo lake ni kushirikisha Wakazi wa Bonde hilo katika kulinda, kusimamia na kuendeleza rasilimali asili za Bonde kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vijavyo. Sherehe hizo zilifanyika Mjini Mugumu, Serengeti ambapo mgeni rasmi alikuwa **Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**65. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu ilianza uratibu wa Mradi wa masuala ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (*Planning for Resilience in East Africa through Policy, Adaptation, Research and Economic Development-PREPARED*). Miji iliyopewa kipaumbele katika utekelezaji wa mradi huo ni Halmashauri za Itilima katika Mkoa wa Simiyu, Bunda (Mkoa wa Mara) pamoja na Chato (Mkoa wa Geita). Aidha, taratibu za kuandaa Hati ya Makubaliano *(MoU)* kwa ajili ya usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji katika ikolojia ya Bonde la Mto Mara zinaendelea kati ya nchi shirikishi chini ya uratibu wa *Nile Basin Initiatives*. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea kuratibu miradi mbalimbali itakayotekelezwa kupitia Mradi wa "*PREPARED*" ili kusaidia wananchi wanaoishi maeneo ya Bonde la Mto Mara kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**66. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu kwa kupitia Mradi wa Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika Bonde la Mto Mara, ulio chini ya Umoja wa Ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile imeendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa bwawa la Borenga litakalojengwa kwenye mpaka wa Wilaya za Serengeti na Tarime. Bwawa hilo ni kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo, nishati ya umeme na kilimo cha umwagiliaji katika vijiji **16** vilivyopo katika Wilaya za Butiama, Serengeti na Tarime. Inakadiriwa kuwa **hekta 8,340** zitamwagiliwa na maji kutoka katika bwawa hilo ambalo litakuwa na **mita za ujazo milioni 20**. Aidha, mradi unaendelea na uandaaji shirikishi wa mipango ya usimamizi wa hifadhi ya maji katika sehemu ya Bonde la Mto Mara (*Sub Catchment Management Plans*) ya Tobora (**kilomita za mraba 364**) na Somoche (**kilomita za mraba 682**). Hifadhi hizo za maji zipo katika bonde la Mto Mara Wilayani Serengeti. Vilevile, katika mwaka 2013/2014, mradi ulitoa mafunzo ya uendeshaji na matengenezo wa vifaa vinavyopima wingi wa maji mitoni na ziwani na hali ya hewa (*hydro-metereological equipment*) kwa Mafundi Sanifu wa Bonde la Ziwa Victoria.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi wa ujenzi wa bwawa la Borenga na kuandaa zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi.

**(iv) Bonde la Mto Zambezi**

**67. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu iliendelea kutekeleza Mkataba wa Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi *(Zambezi Watercourse Commission-ZAMCOM*) ulioanza kutekelezwa rasmi kisheria mwaka 2011. Madhumuni ya kuanzisha Kamisheni hiyo ni kusimamia kwa pamoja rasilimali za maji za Bonde la Mto Zambezi. Jumla ya nchi **saba (7**) zinatekeleza Mkataba wa Kamisheni hiyo ambazo ni Angola, Botswana, Msumbiji, Namibia, Zambia, Zimbabwe na Tanzania.

Nchi ya Malawi haijaridhia Mkataba huo hadi sasa. Baada ya Sekretarieti ya muda (*Interim ZAMCOM Secretariat*) kumaliza muda wake tarehe 31 Desemba, 2013, Sekretarieti ya Kudumu ya Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi imeanza kazi rasmi na Makao Makuu yake yapo Mjini Harare Zimbabwe.

**68. Mheshimiwa Spika**, majukumu mengine ya Sekretarieti ya Kudumu ya *ZAMCOM* ni kuandaa mikakati ya utekelezaji wa mipango ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji za Bonde la Mto Zambezi kwa kuzingatia maamuzi ya vikao vya Baraza la Mawaziri wa Maji wa *SADC* na lile la nchi wanachama wa *ZAMCOM*. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kuratibu kazi za Kamisheni hiyo zinazofanyika hapa nchini.

**(v) Bonde la Mto Ruvuma**

**69. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Maji Shirikishi wa Bonde la Mto Ruvuma unahusisha nchi za Msumbiji na Tanzania na kuratibiwa na Sekretarieti ya *SADC*. Mradi huo umeanzishwa ili kuhakikisha rasilimali za maji za Bonde hilo zinasimamiwa vizuri na kutumiwa kwa manufaa ya nchi hizo mbili. Hapa nchini mradi unatekelezwa katika Wilaya **tano (5)** za Mikoa ya Mtwara na Ruvuma ambazo ni Tandahimba, Nanyumbu, Songea Vijijini, Tunduru na Mbinga. Katika mwaka 2013/2014, miradi **miwili** ya kijamii inatekelezwa katika Wilaya ya Tunduru ambapo jumla ya miche ya **miti 5,733** imepandwa katika vijiji **viwili** vya Daraja Mbili na Lelolelo kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa ardhi na kutunza vyanzo vya maji. Vilevile, mitambo **miwili (2)** ya gesi asilia inayotokana na samadi imejengwa katika vijiji vya Nandembo na Majimaji kwa ajili ya matumizi ya kupikia na kuwashia taa.

**70. Mheshimiwa Spika**, katika skimu ya umwagiliaji ya Namatuhi iliyoko Wilaya ya Songea Vijijini, Mkandarasi anaendelea na kazi ya ujenzi wa mifereji midogo yenye urefu wa **mita 550** na mradi utakamilika mwezi Juni, 2014. Aidha, uchimbaji wa kisima kirefu cha **mita 150** na usambazaji wa maji katika kijiji cha Mihambwe, Wilaya ya Tandahimba umekamilika. Aidha, utekelezaji wa mradi wa kusambaza maji katika kijiji cha Mahande, Wilaya ya Mbinga umekamilika.

Kupitia mradi huo wananchi wa vijiji hivyo wamepatiwa huduma ya maji safi na salama.

**71. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu kwa kushirikiana na taasisi nyingine itakamilisha miradi ya maji ya kijamii, kuelimisha na kuhamasisha wadau kuhusu utunzaji wa vyanzo vya maji na ufungaji wa vituo vya hali ya hewa. **Jedwali Na. 4** linaonesha orodha ya miradi inayotekelezwa katika Bonde la Mto Ruvuma.

**(vi) Bonde la Mto Songwe**

**72. Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Malawi inatekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya Kuendeleza Rasilimali za Bonde la Mto Songwe. Awamu hiyo inahusu usanifu wa kina wa miundombinu ya rasilimali za maji itakayojengwa kwa ajili ya kuzalisha umeme, kilimo cha umwagiliaji na kuzuia mafuriko.

Aidha, mpango unaandaliwa kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Kusimamia Programu na kujenga uwezo kwa watekelezaji wa programu katika ngazi za Halmashauri hadi Taifa. Hadi mwezi Aprili 2014, Mtaalam Mshauri amekamilisha na kuwasilisha rasimu zifuatazo:-Dira ya Maendeleo ya Programu ya Kuendeleza Rasilimali za Maji za Bonde la Mto Songwe, upembuzi yakinifu wa miradi ya kipaumbele na tathmini ya athari za kimazingira na kijamii kuhusu miradi itakayojengwa.

Vilevile, amekamilisha rasimu ya mwisho ya mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya Kamisheni ya Pamoja ya Kusimamia Programu ya Mto Songwe. Kazi hizo zinatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2015. Mkakati wa elimu na mawasiliano umekamilika na kuanza kutekelezwa kwenye Halmashauri za Wilaya za Mbeya na Momba kwa upande wa Tanzania, na kwa upande wa Malawi katika Wilaya za Karonga na Chitipa.

**73. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, usanifu wa awali wa mabwawa **matatu (3)** katika Bonde la Mto Songwe umekamilika.

Lengo la kujenga mabwawa hayo ni kwa ajili ya kudhibiti mafuriko na kuhamahama kwa mto, matumizi ya maji majumbani, kilimo cha umwagiliaji na uzalishaji umeme. Jumla ya **hekta 5,635** zinatarajiwa kutumika kwa kilimo cha umwagiliaji ambapo kwa upande wa Tanzania ni **hekta 3,005** na Malawi **hekta 2,630.**

Vilevile, **megawati 175** za umeme zinatarajiwa kuzalishwa kutoka bwawa moja *(Lower Dam)* litakaloanza kujengwa kati ya mabwawa hayo. Katika mwaka

2014/2015, uandaaji wa muundo wa kitaasisi, usanifu wa kina na makabrasha ya zabuni utakamilika. Serikali itaendelea kushirikiana na Serikali ya Malawi kuratibu utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi huo.

**(vii) Ziwa Tanganyika**

**74. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kushirikiana kwa karibu na nchi wanachama wengine wa Mamlaka ya Bonde la Ziwa Tanganyika ambazo ni Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Zambia katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali ya maji ya Ziwa Tanganyika. Tanzania na *DRC* zinamiliki kwa pamoja **asilimia 86** ya Ziwa hilo. Changamoto ya kupungua kwa kina cha maji ya Ziwa Tanganyika imeathiri sana bandari za Kigoma upande wa Tanzania na Kalemie, Uvira na Moba zote za *DRC*. Aidha, chanzo cha maji kwa ajili ya mji wa Kigoma/Ujiji kiliathirika na kulazimika kuongeza urefu wa bomba kutoka kwenye banio (*intake*) umbali wa **mita 60** ndani ya ziwa. Miongoni mwa sababu zinazochangia tatizo la kupungua kwa kina cha maji ni kubomoka kwa banio la Mto Lukuga ulioko *DRC* unaotoa maji kutoka Ziwa Tanganyika kupeleka Mto Kongo.

**75. Mheshimiwa Spika**, katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dr.Jakaya Mrisho Kikwete** alituma ujumbe maalum mara mbili, mwezi Agosti, 2010 na Machi, 2014 kwa Rais wa *DRC*, **Mhe. Joseph Kabila Kabange** kuhusu umuhimu wa Tanzania na *DRC* kushirikiana (*bilaterally*) katika kukarabati banio la Mto Lukuga.

**76. Mheshimiwa Spika**, kufuatia hatua nilizozitaja, usanifu wa kina wa banio husika umekamilika mwezi Desemba, 2013 kwa ufadhili wa *COMESA*. Jumla ya **Dola za Marekani milioni 65** zinahitajika kutekeleza miradi ya kudhibiti kupungua kwa kina cha Ziwa kwa kujenga upya banio hilo. Aidha, Wizara yangu ilimwalika Waziri wa Maji na Umeme wa *DRC* kuja Tanzania mwezi Aprili, 2014 kwa lengo la kujadili namna tutakavyo washirikisha wadau wa maendeleo ili kupata fedha za kujenga upya banio hilo. Mkutano wetu ulikuwa wa mafanikio na kwamba tutaunda timu ya pamoja ya Wataalam kutoka Sekta za Maji, Mazingira na Usafirishaji kushughulikia changamoto zilizopo. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itajenga ushirikiano imara na nchi za DRC, Zambia na Burundi kuhifadhi rasilimali za maji ya Bonde la Ziwa Tanganyika.

**(viii) Ziwa Chala, Ziwa Jipe na Mto Umba**

**77. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inaratibu uandaaji wa Mpango Shirikishi wa Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika ekolojia ya Maziwa ya Chala na Jipe; na Mto Umba. Hati ya Makubaliano (*MoU*) kati ya Kenya na Tanzania kuhusu utunzaji na uendelezaji wa ekolojia ya maziwa hayo ilisainiwa mwezi Februari, 2013. Makubaliano hayo yanasisitiza kusimamia na kuendeleza

rasilimali zilizoko katika maeneo hayo ili matumizi yake yawe endelevu, ikiwa ni pamoja na kulinda mifumo ya ekolojia kwa ustawi wa wananchi wa nchi hizo.

**78. Mheshimiwa Spika,** kikao cha pamoja kati ya Tanzania na Kenya kilifanyika Mjini Taveta mwezi Machi, 2014 na kufikia makubaliano ya kuandaa mpango wa kitaalam wa kutumia maji ya Ziwa Chala kwa ajili ya matumizi ya majumbani na kilimo cha umwagiliaji kwa wakazi wanaozunguka ziwa hilo, kwa kuzingatia kuwa eneo linalozunguka ziwa hilo ni kame. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na nchi ya Kenya kutekeleza makubaliano hayo. Lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa miradi ya kuboresha maisha ya jamii inatekelezwa, hususan miradi ya maji kwa matumizi ya majumbani. Vilevile, kilimo cha umwagiliaji kitaanza kwa eneo dogo, hatua kwa hatua kwa kuzingatia usawa wa maji ziwani (*trend monitoring*).

### 3.1.2 Huduma za Ubora na Usafi wa Maji

**79. Mheshimiwa Spika**, usimamizi wa rasilimali za maji nchini unahusisha utambuzi na ufuatiliaji wa wingi na ubora wa maji kutoka katika vyanzo vya maji. Jukumu kuu la Wizara yangu ni kuhakiki ubora, usafi na usalama wa maji katika vyanzo vya maji na mitandao ya usambazaji maji vijijini na mijini kwa lengo la kulinda afya na ustawi wa wananchi. Kama tunavyofahamu, afya ya wananchi inaweza kuathirika vibaya kama maji yanayotumika hayakidhi viwango kutokana na kuchafuliwa na mifumo asilia au shughuli za kibinadamu, hivyo ni muhimu kuwa na takwimu za ubora wa maji zitakazosaidia kuweka mifumo madhubuti ya kuhifadhi na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji.

**80. Mheshimiwa Spika**, Maabara za maji nchini zinafuatilia na kuchunguza ubora wa maji katika vyanzo na mitandao ya usambazaji maji. Aidha, maabara hutoa ushauri wa kitaalam kwa mamlaka za maji, vyombo vya watumiaji maji, Bodi za maji za mabonde, taasisi na watu binafsi kuhusu umuhimu wa kuzingatia viwango vinavyokubalika kwa matumizi yaliyokusudiwa. Katika mwaka 2013/2014, Wizara ilipanga kukagua vyanzo vya maji kwa kuchunguza **sampuli 8,000** za maji ili kuhakiki ubora wake. Vilevile, **sampuli 1,000** za majitaka zilipangwa kuchunguzwa kwa lengo la kuhakiki ubora wake kabla ya kurudishwa kwenye mazingira ili kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji na kuepusha athari za kiafya kwa wananchi na mfumo wa ekolojia. Takwimu hizo ni muhimu katika kuandaa mikakati ya kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji.

**81. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi, 2014, sampuli **4,673** za maji zilikusanywa na kuhakikiwa ubora wake. Kati ya hizo, sampuli **3,200** ni za maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani; sampuli **382** kwa matumizi ya viwandani; sampul**i 712** ni za kuratibu mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo (mito, chemichemi, maziwa na mabwawa); sampuli **341** za utafiti; na sampuli **38** kwa

ajili ya shughuli za umwagiliaji. **Jedwali Na. 5** linaonesha mwelekeo wa sampuli za maji zilizokusanywa na kuchunguzwa ubora wake kuanzia mwaka 2009/2010 hadi Machi, 2014.

## (a) Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Majumbani

**82.** **Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeleza hapo awali, wananchi wote wa vijijini na mijini wanatakiwa kutumia maji safi na salama ili kulinda afya zao kwa ustawi wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Sheria ya Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira **Na. 12** ya mwaka 2009 inavitaka vyombo vinavyohusika na huduma hii kuhakikisha maji yanayosambazwa yana ubora unaokubalika. Matokeo ya uchunguzi wa sampuli **2,880** sawa na **asilimia 90** yameonesha kuwa maji hayo yalikidhi viwango vinavyokubalika. Sampuli **320**, maji yake hayakukidhi viwango kutokana na uwepo wa kiwango kikubwa cha chumvichumvi, madini-chuma (*iron), manganese* na *fluoride*. Maji yaliyoonekana kuwa na madini-chuma na *manganese,* ushauri ulitolewa maji hayo yawekwe katika hali ya kuongezewa hewa ya Oxgen (*aeration*) ambayo huwezesha madini chuma kutuama kama masimbi, au kutafuta vyanzo mbadala.

Kwa vyanzo vilivyobainika kuwa na kiwango kikubwa cha madini ya *fluoride*, hatua zimeanza kuchukuliwa kutafuta vyanzo mbadala vya kukidhi mahitaji pamoja na kutumia teknolojia ya kuondoa madini ya *fluoride* kwenye maji ya kunywa na kupikia. Aidha, ushauri ulitolewa wa kutumia madawa ya kutibu maji yanayokidhi viwango na kukagua mitambo ya kusafisha maji mara kwa mara kwa kuzingatia mabadiliko ya ubora wa maji yanayotokana na misimu ya mwaka. **Jedwali Na. 6** linaonesha maeneo ambayo maji hayakukidhi viwango vinavyokubalika.

**83.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Shirika la Afya Duniani (*WHO*) kutekeleza Mpango wa Usalama wa Maji (*Water Safety Plan*) kwa maeneo mbalimbali nchini. Mpango huo una lengo la kuboresha shughuli za usimamizi wa ubora wa maji kwa mamlaka za maji na vyombo vya watumiaji maji vijijini (*COWSOs*) kuanzia kwenye chanzo cha maji hadi kwa mtumiaji.

## (b) Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Viwanda

**84.** **Mheshimiwa Spika,** shughuli za viwanda zinahitaji maji yanayokidhi viwango vya ubora kwa lengo la kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa au kusindikwa zinakidhi viwango. Kwa kuzingatia hilo, jumla ya sampuli **382** kutoka viwanda mbalimbali vya kuzalisha bidhaa zilikusanywa na kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara. Kati ya hizo, sampuli **358** zilitoka viwanda vya samaki katika Miji

ya Bukoba, Musoma, Tanga, Mafia, Mwanza na Dar es Salaam na matokeo ya uchunguzi huo yalionesha maji kukidhi viwango vya kimataifa. Sampuli **24** kutoka viwanda vya sukari-Kagera, saruji na Pepsi Mkoani Mbeya zilichunguzwa na matokeo kuonesha kuwa maji yana ubora unaokubalika kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**(c) Kuratibu Mwenendo wa Ubora wa Maji katika Vyanzo**

**85. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu kupitia Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria (*LVEMP*) hufuatilia mwenendo wa ubora wa maji na udhibiti wa ongezeko la magugu maji katika Ziwa Victoria. Hadi mwezi Machi, 2014, kwa upande wa Tanzania ufuatiliaji (*cruise monitoring*) kwenye vituo **28** ulifanyika na jumla ya sampuli **334** zilikusanywa na kuchunguzwa. Matokeo yalionesha kuwa hali ya uwepo wa virutubisho vya *nitrate* na *phosphorus* kwenye vituo vya pembezoni mwa ziwa bado ni mkubwa kutokana na shughuli za kibinadamu ikilinganishwa na vituo vya katikati ya ziwa ambapo hali ya wingi wa virutubisho inapungua. Aidha, sampuli za maji katika mabonde ya Wami-Ruvu **(124)**, Ziwa Tanganyika **(56),** Ziwa Rukwa **(41),** Rufiji **(27)**, Bonde la Kati **(86),** Pangani **(8)**, Ziwa Nyasa **(8)** na Pwani ya Kusini **(28)** zilipimwa kwa ajili ya kutoa takwimu zinazotumika katika usimamizi wa rasilimali za maji. Matokeo yalionesha maji kutoka kwenye vyanzo hivyo kuwa na ubora unaokubalika kwa ustawi wa viumbe hai na kuendelezwa kwa matumizi mbalimbali.

**(d) Ubora wa Maji kwa ajili ya Umwagiliaji na Utafiti**

**86. Mheshimiwa Spika,** maji yanayotumika kwa ajili ya umwagiliaji yanatakiwa kukidhi viwango vya ubora kutegemeana na aina ya udongo na aina ya mazao yanayomwagiliwa ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao hayo. Hadi mwezi Machi 2014, sampuli **38** za maji kwa ajili ya umwagiliaji kutoka maeneo ya Kiloka, Mikindo (Morogoro), Mlowa, Matali (Iringa), Matiganjola, Kivavi, Igongolo (Njombe), Litapwasi, Peramiho (Ruvuma) na Kibiti (Pwani). zilichunguzwa na kuonesha kukidhi ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa. Aidha, Wizara hupima sampuli za maji kwa ajili ya shughuli za utafiti kutoka kwenye taasisi na watu binafsi. Sampuli **341** za maji zilipokelewa na kuchunguzwa na ushauri ulitolewa kulingana na mahitaji ya utafiti.

**(e) Ubora wa Majitaka Yanayorudishwa kwenye Mazingira**

**87. Mheshimiwa Spika,** moja ya sababu za uchafuzi wa vyanzo vya maji ni majitaka yanayozalishwa viwandani na majumbani. Hadi mwezi Machi 2014, sampuli **630** za majitaka kutoka kwenye mabwawa ya majitaka ya Miji ya Dodoma, Morogoro, Mwanza, Dar es Salaam, Tanga na Iringa; na kutoka viwanda vya sukari, samaki, nguo, bia na tumbaku zilikusanywa na

kuchunguzwa. Kati ya hizo sampuli **120** zilichunguzwa kuangalia uwezo wa mifumo ya kusafisha majitaka na uchunguzi wa sampuli **510** ulilenga kuhakiki ubora wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira. Matokeo yalionesha kuwa **asilimia 85** yana ubora usiosababisha uchafuzi wa vyanzo vya maji na ushauri wa kitaalam wa kuboresha utendaji wa mabwawa na mitambo ya kusafisha majitaka ulitolewa kwa taasisi husika.

**88. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea itaimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa ubora wa maji kwenye vyanzo kwa ajili ya matumizi ya majumbani, viwandani, kilimo na mazingira. Katika kutekeleza majukumu hayo, sampuli **8,000** za maji na sampuli **1,000** za majitaka zitakusanywa na kuchunguzwa. Takwimu zitakazopatikana zitatumika kushauri hatua za kuchukua kabla ya kutumia maji kutoka kwenye chanzo husika.

Aidha, takwimu hizo zitawezesha utekelezaji wa Mkakati wa Kusimamia Ubora wa Maji na Kudhibiti Uchafuzi wa Maji (*Water Quality Management and Pollution Control Strategy*) ambapo moja ya shughuli zilizoainishwa ni ufuatiliaji wa mwenendo wa kiwango cha madini tembo (*heavy metals*) aina ya zebaki (*mercury*), *arsenic*, urani (*uranium)* na *cyanide* katika vyanzo vya maji kwenye maeneo ya migodi.

**(f) Ubora wa Madawa ya Kusafisha na Kutibu Maji**

**89. Mheshimiwa Spika,** ni wajibu wetu kuhakiki madawa ya kutibu na kusafisha maji ili kuthibitisha ubora wake katika kupata maji safi na salama. Jumla ya sampuli **50** za madawa ya kusafisha na kutibu maji kutoka Morogoro, Tanga, Chalinze na *DAWASCO* zilihakikiwa ubora wake. Kati ya sampuli hizo, sampuli za shabu (*Aluminium Sulphate*) zilikuwa **16**, *sodium bicarbonate* **nne (4)** na *Polyaluminium Chloride* **(15)** ambazo hutumika kusafisha maji; na *Calcium Hypochlorite* (**15)** inayotumika kuua vijidudu. Matokeo yalionesha kuwa sampuli **33** zilikuwa na viwango vinavyokubalika na ushauri wa kitaalam ulitolewa kuhusu matumizi sahihi ya madawa hayo. Sampuli **17** ambazo ni za *Calcium Hypochlorite* **nne (4)**, *Aluminium Sulphate* **sita (6)** *na Polyaluminium Chloride* **saba (7)** zilibainika kuwa na viambata hafifu visivyotosheleza kutibu maji katika kiwango kinachotakiwa. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kuhakiki ubora wa madawa na kukagua ufanisi wa mitambo ya kusafisha na kutibu maji pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam kwa vyombo vinavyotoa huduma ya majisafi vijijini na mijini.

**(g) Uondoaji wa Madini ya Fluoride katika Maji ya Kunywa na Kupikia**

**90. Mheshimiwa Spika,** katika hotuba yangu ya mwaka 2013/2014 nililielezea Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu imeandaa mkakati wa usambazaji wa teknolojia ya uondoaji madini ya *fluoride* katika maji ya kunywa na kupikia kwa

kutumia mkaa wa mifupa ya ng'ombe (*bone* char). Hadi Machi, 2014, tanuru **mbili (2)** zenye uwezo wa kuchoma tani **nne (4)** za mifupa ya ng'ombe kwa mara moja zimejengwa na majaribio ya kubaini ufanisi wa uchomaji katika matanuru hayo yanaendelea. Vilevile, *mould* kwa ajili ya kuzalisha mitambo ya kuondoa madini ya *fluoride* katika maji ya kunywa na kupikia kwa ngazi ya kaya imenunuliwa na uzalishaji wa mitambo **1,000** kwa ajili ya kuisambaza kwenye kaya za maeneo yenye vyanzo vya maji yenye kiwango kikubwa cha *fluoride* unaendelea kufanyika. Lengo ni kuhamasisha wananchi kutumia teknolojia ya mkaa wa mifupa ya ng'ombe ili kuondoa madini ya *fluoride* katika maji ya kunywa na kupikia na hivyo kupunguza athari hasa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

**91. Mheshimiwa Spika,** mwezi Novemba 2013, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilitembelea Kituo cha Utafiti wa *Fluoride* kilichopo Ngurdoto Mkoani Arusha na jamii inayotumia vifaa vya kuondolea madini hayo katika maji ya kunywa vilivyobuniwa na kituo hicho. Lengo la ziara hiyo, lilikuwa kutoa fursa kwa Kamati hiyo ya Bunge kutathmini utafiti unaofanyika na kupata taarifa ya hatua iliyofikiwa ya matumizi ya teknolojia ya chengachenga za mkaa wa mifupa ya ng'ombe *(Bonechar filter media)*. Matumizi ya teknolojia ya kuondoa madini ya *Fluoride* imetumika kwa zaidi ya miaka mitatu sasa katika ngazi ya kaya katika **kaya 22** kwenye maeneo ya Ngaramtoni **(9)**, Kijenge **(1)**, Leganga **(1)**, Kiwawa **(1)**, Ngongongare **(6)**, Arusha Mjini **(1)**, Njiro **(2)** na Olasiti (**1**), Mkoani Arusha. Vilevile, kwa ngazi ya jamii **11**, Mkoa wa Arusha na jamii **moja (1)** maeneo ya Mwando, Mkoa wa Singida. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea na mkakati wa usambazaji wa teknolojia ya mkaa wa mifupa ya ng'ombe na kutayarisha ramani (*fluoride mapping*) itakayoainisha maeneo yenye kiwango kikubwa cha *fluoride* katika maji ili kuyatambua maeneo hayo wakati wa kuibua miradi ya maji.

### (h) Maabara za Maji kupata Ithibati (*Accreditation*)

**92. Mheshimiwa Spika,** vigezo vinavyotumika kwa taasisi zinazohusika na vipimo na uchunguzi wa kimaabara kutambulika kimataifa ni kupata Ithibati (*Accreditation*). Kupatikana kwa Ithibati kutawezesha Maabara zetu kutambulika kimataifa na hivyo, kukidhi miongozo ya Sheria **Na. 11** ya mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sheria **Na.12** ya mwaka 2009 ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira na Sheria **Na. 20** ya mwaka 2004 ya Usimamizi wa Mazingira. Maabara ya Maji Mwanza imekamilisha uandaaji wa mwongozo wa utendaji kazi (*Quality Manual*) na kuwasilisha kwa taasisi inayosimamia shughuli hizo kimataifa (*SADCAS)* kwa ajili ya kufanyiwa tathmini. Lengo la Wizara yangu ni kuziwezesha maabara zote kukidhi vigezo vya kupata Ithibati na hivyo kuwa na maabara zenye viwango.

**93. Mheshimiwa Spika**, hatua hiyo inawezesha maabara zetu kushiriki kwenye majaribio ya kujipima uwezo wa utendaji kazi za kimaabara (*Laboratory Performance Evaluation or Proficiency Testing*) yanayoandaliwa na taasisi za kimataifa. Majaribio hayo hufanyika kila mwaka na kwa mwaka 2013/2014 majaribio yaliyofanywa ni:-

(i) Mwezi Julai 2013, Maabara **saba (7)** za Iringa, Mwanza, Arusha, Morogoro, Mbeya, Tanga na Maabara Kuu Dar es Salaam zilishiriki katika jaribio la kujipima uwezo linaloratibiwa na *Southern Africa Development Community Measurement Traceability* (*SADCMET*).

(ii) Mwezi Agosti 2013, Maabara **tisa (9)** za Mwanza, Iringa, Mbeya, Tanga, Arusha, Dodoma, Mtwara, Bukoba na Maabara Kuu Dar es Salaam zilishiriki katika jaribio la kujipima uwezo chini ya Programu ya *Global Environmental Monitoring System/Water (GEMS/Water)*.

Tathmini ya matokeo ya majaribio hayo imeonesha kuwa maabara zilizoshiriki zimefanya vizuri kwa wastani wa asilimia **65** kwa vielelezo vya kemikali na asilimia **92** ya upimaji wa vimelea vya vijidudu (*bacteria*) kwenye maji. Tathmini hiyo inaonesha kuwa maabara zinaongeza ufanisi katika utendaji kimaabara baada ya kujengewa uwezo wa kupatiwa vitendea kazi. **Jedwali Na. 7** linaonesha matokeo ya majaribio ya kujipima uwezo wa maabara za maji kwa ajili ya kupata ithibati.

**94. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inaendelea na ukarabati wa Maabara Kuu ya Wizara na maabara za mikoa. Uboreshaji huo utaongeza ufanisi katika utendaji kazi na hivyo kutoa huduma yenye tija zaidi. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuzijengea uwezo maabara zake kwa kuweka mazingira mazuri kwa wataalam kufanya kazi za uchunguzi katika hali bora na salama kama inavyoelekezwa kwenye viwango vya kimataifa ***(ISO 17025)***.

### 3.2 HUDUMA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI

#### 3.2.1 Mpango Maalum wa "Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa" (*Big Results Now – BRN*)

**95. Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza katika utangulizi wa hotuba hii, Sekta ya Maji ni moja kati ya sekta **sita (6)** zinazotekeleza mpango maalum wa **"Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa"** (*Big Results Now*) ulioandaliwa na Serikali chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dr. Jakaya Mrisho Kikwete.** Katika Sekta ya Maji, tathmini ya *BRN* juu ya hali ya huduma ya maji vijijini iliyofanyika mwezi Februari, 2013 ilibaini hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kushuka kutoka **asilimia 57.8** hadi kufikia **asilimia 40**.

Sababu za kushuka kwa huduma hiyo ni pamoja na kuharibika kwa baadhi ya miundombinu ya maji kulikosababishwa na ukosefu wa matengenezo ya mara kwa mara ya miundombinu hiyo. Utekelezaji wa mpango wa *BRN* ulioanza rasmi mwezi Julai 2013, umeboresha kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini hadi kufikia **asilimia 49** mwezi Machi 2014. Lengo ni kufikia **asilimia 74** ifikapo mwezi Juni 2016. Mpango huo unaelekeza maeneo manne (4) ya utekelezaji ambayo ni ujenzi wa miradi mipya (*new construction*), ukarabati wa miradi chakavu (*rehabilitation*), upanuzi wa miradi iliyopo (*extension*) na uendeshaji na matengenezo (*operation and maintenance*).

**96. Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa miradi mipya unahusisha miradi ya vijiji **10** kwa kila Halmashauri pamoja na miradi ya kimkakati (*strategic projects*). Miradi ya upanuzi na ukarabati inahusisha utekelezaji wa miradi ya matokeo ya haraka kutoka kwenye vyanzo vya mabwawa, visima virefu, vyanzo vidogo vya juu ya ardhi, miradi ya kitaifa na miradi inayohitaji matengenezo. Aidha, uendeshaji na matengenezo unahusu kuvijengea uwezo vyombo vya watumiaji maji na ukusanyaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi.

### 3.2.2 Utekelezaji wa *BRN*

**97. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu–TAMISEMI kusimamia utekelezaji wa *BRN* kulingana na mipango na vipaumbele kama ilivyoainishwa kwa kila Halmashauri. Katika kuhakikisha miradi ya maji vijijini inatekelezwa kwa haraka na ufanisi, Wizara imepeleka wataalam wazoefu katika Sekretarieti za Mikoa ili kuwajengea uwezo Wahandisi wa Mikoa na Halmashauri. Vilevile, Wizara imeondoa vibali (*No-Objection*) ili kupunguza muda wa ununuzi wa Wataalam Washauri na Wakandarasi. Hatua nyingine ni kuhusu ujenzi wa miradi kuanza hata kama fedha zote za mradi hazijaifikia Halmashauri na hata kama michango ya wananchi haijakamilika. Michango hiyo inatumika wakati wa uendeshaji wa miradi baada ya ujenzi kukamilika.

**98. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu ilikasimiwa **shilingi bilioni 236** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji vijijini. Aidha, kiasi kingine cha **shillingi bilioni 108** kilikasimiwa kupitia mafungu ya mikoa kwa ajili ya Halmashauri, OWM-TAMISEMI na Wizara zinazoshiriki katika kutekeleza kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira vijijini. Hadi kufikia Machi 2014, Serikali imezipatia Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa **shilingi 137,904,598,951** kwa ajili ya utekelezaji na usimamizi wa mradi wa maji wa vijiji 10 kwa kila Halmashauri. Vilevile, jumla ya **shilingi 10,610,746,989** zimeelekezwa kwenye miradi mingine ya maji vijijini kama vile miradi ya yenye kuleta matokeo ya haraka, ujenzi wa mabwawa, vijiji 100 kutoka bomba la KASHWASA, Same-Mwanga-Korogwe na gharama za ziada za usimamizi na ufuatiliaji wa miradi. **Jedwali Na. 8** linaonesha mgao wa fedha zilizotumwa kwenye Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa.

**99. Mheshimiwa Spika,** kwa kutumia fedha hizo, jumla ya miradi ya maji **248 yenye jumla ya v**ituo vya kuchotea maji **10,560** imejengwa kwenye **Halmashauri 98** na kunufaisha vijiji **270. Juhudi hizo zimeo**ngeza idadi ya wakazi vijijini wanaopata huduma ya maji safi na salama kutoka wakazi **15,200,000** mwezi Juni, 2013 hadi kufikia wakazi **17,840,000,** sawa na ongezeko la wakazi **2,640,000** . Ongezeko hilo limeboresha huduma ya upatikanaji wa maji vijijini kutoka **asilimia 40** hadi kufikia **asilimia 49**. Lengo la Serikali kulingana na Mpango huo, ni kuwapatia huduma ya maji wananchi **milioni 22** waishio vijijini ifikapo mwezi Juni 2014. Hata hivyo uwezekano wa kufikia lengo hilo unaendelea kufifia kutokana na upatikanaji wa fedha mdogo.

### 3.2.3 Mpango wa *BRN* kwa mwaka 2014/2015

**100. Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, katika bajeti ya Serikali ya mwaka 2014/2015, Wizara yangu imepanga kuendelea kutekeleza miradi ya maji vijijni chini ya Mpango wa *BRN*. Kazi zitakazotekelezwa ni ujenzi na upanuzi wa miradi ya maji pamoja na ukarabati wa miundombinu ya maji. Fedha zilizopangwa kutumika ni **shilingi bilioni 270.97**, ambapo **shilingi bilioni 166.81** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 104.16** ni fedha za nje. Fedha hizo zitatekeleza miradi kwenye vijiji **1,239** na itakapokamilika itakuwa na vituo **28,031** vya kuchotea maji vitakavyohudumia jumla ya wakazi **7,007,628** wanaoishi vijijini.

**(a)Ujenzi wa Miradi Mipya**

**(i) Ujenzi wa Miradi ya Vijiji 10 kwa kila Halmashauri**

**101. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatekeleza Mradi wa Maji wa Vijiji 10 ambapo katika mwaka 2013/2014, vijiji **1,538** vilipangwa kupatiwa huduma ya maji. Hata hivyo, wakati wa utekelezaji vijiji **17** zaidi viliongezwa na kufikia jumla ya vijiji **1,555**.

Mradi huo ukikamilika, vituo **32,274** vya kuchotea maji vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi wapatao **8,068,500** vitakuwa vimejengwa kwenye **Halmashauri 167** kati ya **Halmashauri 168** nchini. Vijiji vya Halmashauri iliyobaki ya Manispaa ya Musoma vitapata huduma ya maji kutoka katika mradi wa maji na usafi wa mazingira unaoendelea kutekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Musoma.

**102. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza mpango huo wa vijiji 10, miradi ya maji **766** kwenye **vijiji 830** imeendelea kutekelezwa katika Halmashauri zote nchini. Hadi mwezi Machi 2014, kati ya miradi hiyo, miradi **228** kwa ajili ya vijiji **247** imekamilika. Kukamilika kwa miradi hiyo kumeongeza upatikanaji wa

huduma ya maji safi na salama kwa wakazi **2,398,500** zaidi waishio vijijini. Aidha, **miradi 538** kwenye **vijiji 583** itakayokuwa na **vituo 9,630** yenye uwezo wa kuhudumia **watu 2,407,500** inaendelea kujengwa; mikataba ya ujenzi wa **miradi 707** kwa ajili ya **vijiji 725** itakayokuwa na **vituo 13,050** vyenye uwezo wa kuhudumia **watu 3,262,500** imesainiwa.

**103. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, Serikali imepanga kutumia jumla ya **shilingi bilioni 148.12** kujenga miradi ya maji ya vijiji 10 kwenye vijiji **725** katika Halmashauri **167** ambapo jumla ya vituo **13,050** vya kuchotea maji vinatarajiwa kujengwa vyenye uwezo wa kuhudumia wakazi wapatao **3,262,500**.

**(ii) Miradi ya Kimkakati**

**Mradi wa Maji Masoko**

**104. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Maji Masoko unaojengwa katika Wilaya ya Rungwe ulisimama baada ya Halmashauri kusitisha Mkataba wa Mkandarasi aliyeshindwa kutekeleza kazi kulingana na viwango vya usanifu. Kazi za mradi huo zinahusisha ujenzi wa banio la maji, chujio la maji, matanki **matatu (3)** ya kuhifadhia maji yenye ujazo wa **lita 90,000** kila moja, vituo **122** vya kuchotea maji, ununuzi wa pampu na ulazaji wa mabomba.

Mradi unalenga kunufaisha wakazi **15,158** wa vijiji 15 vya Bulongwe, Igembe, Ngaseke, Ntandabala, Lupando, Bujesi, Lufumbi, Busisya, Mbaka, Isabula, Lwifwa, Ikama, Itagata, Nsanga na Nsyasya. Awali mradi huo ulikadiriwa kugharimu kiasi cha **shilingi 4,754,773,420**. Gharama ya kazi zilizofanyika ni **shilingi 1,713,445,750**. Hata hivyo, hadi Mkataba unasitishwa Mkandarasi huyo alikuwa amelipwa kiasi cha **shilingi 1,269,851,102.**

**105. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali itaendelea kukamilisha Mradi wa Maji wa Masoko kwa vipande (*lots*) kwa kadri fedha zitakavyopatikana. Hii ni kutokana na gharama za kukamilisha mradi huo zinazotolewa na wakandarasi kuwa mara mbili zaidi ya gharama zilizokadiriwa kwenye usanifu wa mradi. Mradi huo utajengwa na Halmashauri kwa kutumia Wakandarasi wadogo na ujenzi utasimamiwa na Wataalam wa Wizara wakishirikiana na Wataalam wa Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya na Wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ili kuharakisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Masoko.

**Mradi wa Maji wa Same – Mwanga - Korogwe**

**106. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo inatekeleza mradi wa Same-Mwanga-Korogwe unaolenga kupeleka maji katika

miji ya Mwanga na Same. Mchango wa *BADEA* wa **Dola za Marekani milioni 10**, *OFID* **Dola za Marekani milioni 12** na Serikali **Dola za Marekani milioni 13.76** zitatumika kujenga sehemu ya mradi kutoka kwenye chanzo katika bwawa la Nyumba ya Mungu, mtambo wa kutibu maji eneo la Njia Panda na kulaza bomba kubwa la **milimita 900** au **inchi 35** hadi kwenye matanki ya kituo cha kusukuma maji Kisangara. Tangazo la kupata Mkandarasi kwa ajili ya kazi hiyo limetolewa tarehe 1 Mei, 2014 na Mkandarasi anategemewa kuanzia kazi mwezi Agosti, 2014.

**107.** 106. **Mheshimiwa Spika**, Mkataba wa kupata fedha (*Financing Agreement*) kati ya Serikali na *Kuwait Fund* (**Dola za Marekani milioni 34**), *Saud Fund* (**Dola za Marekani milioni 25**), *BADEA* (**Dola za Marekani milioni 12**) na *OFID* (**Dola za Marekani milioni 15**) utasainiwa mwezi Septemba, 2014. Fedha hizi ni za kujenga sehemu ya mradi kutoka Kisangara hadi Mwanga na Same kupitia kwenye matanki mawili yenye ujazo **lita milioni 7.5** kila moja eneo la Kiverenge. Mkandarasi anategemewa kupatikana na kuanza kazi mwezi Machi, 2015. Mradi huu utakapokamilika utahudumia wananchi **456, 931**.

**108. Mheshimiwa Spika,** katika awamu ya pili, Washirika wa Maendeleo walioahidi kutoa fedha ni *Kuwait Fund* **Dola za Marekani milioni 34,** *Saudi Fund* **Dola za Marekani milioni 25,** *BADEA* **Dola za Marekani milioni 12** na *OFID* **Dola za Marekani milioni 15.** Fedha hizo zinatarajiwa kupatikana mwezi Septemba, 2014 na ujenzi wa awamu ya pili utaanza mwezi Machi, 2015.

**Mradi wa Maji Vijijini katika Mkoa wa Tabora**

**109. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan inatekeleza mradi wa maji katika **vijiji 20** kwenye Wilaya zote **saba** za Mkoa wa Tabora. Mradi una awamu mbili; awamu ya kwanza ilianza mwezi Septemba, 2009 na kukamilika mwezi Machi, 2014. Awamu ya pili imeanza kutekelezwa mwezi Aprili, 2014 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2016. Katika awamu ya kwanza, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukarabati visima virefu na vifupi **46** vya pampu za mkono katika Wilaya **sita**; kuandaa Mpango Mahsusi wa Maji Vijijini kw*a* Mkoa unaoanisha maeneo ya kipaumbele ya kutekeleza miradi ya maji; kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi ya maji katika **vijiji 20**; na kuandaa makadirio ya gharama za ujenzi pamoja na makabrasha ya zabuni.

**110. Mheshimiwa Spika,** awamu ya pili ya mradi imeanza kutekelezwa mwezi Aprili, 2014 na itaendelea hadi mwaka 2016. Mradi ukikamilika utanufaisha zaidi ya wananchi **45,000**. Kampuni ya *KONOIKE* ya Japan imepewa kazi ya kutekeleza mradi kwa gharama ya **Yeni za Kijapan 1,560,000,000** sawa na **shilingi bilioni 25**. Awamu hiyo inahusisha kazi zifuatazo:-

i. Ujenzi wa miradi **minne** (**4)** ya usambazaji maji katika vijiji **vinne** (**4)** vya Isanga (Nzega), Mpumbuli na Mabama (Uyui) na Kakola (Manispaa ya Tabora);

ii. Ujenzi wa visima virefu **114** vya pampu za mkono katika Wilaya **saba** za Mkoa katika vijiji vya Busomeke na Kalemela (Igunga); Isanga, Kitangili, Makomelo na Wela (Nzega); Kasandalala, Usunga na Mpombwe (Sikonge); Mabama, Ufuluma na Mpumbuli (Uyui); Kakola, Misha na Kalumwa (Manispaa ya Tabora); na vijiji vya Imalamakoye, Kapilula, Kalembela, Kiloleni na Usungwa katika Wilaya ya Urambo/Kaliua; na

Mafunzo kwa Wataalam wa Maji kuhusu uendeshaji na matengenezo ya miradi na mafunzo kwa vitendo kuhusu matumizi ya vifaa vya utafiti wa maji chini ya ardhi.

**(iii) Mradi wa Maji na usafi wa Mazingira Mkoa wa Kigoma (*Water and Sanitation Kigoma Region Project - WaSKiP*)**

**111. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Ubelgiji imekubali kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kutekeleza miradi ya maji vijijini katika Mkoa wa Kigoma. Miradi hiyo itaongeza upatikanaji wa maji safi na salama vijijini na inatarajiwa kugharimu **shilingi bilioni 20.6**. Kati ya hizo **shilingi bilioni 18.13** sawa na **Euro milioni 8** zitatolewa na Serikali ya Ubelgiji wakati **shilingi bilioni 2.44** zitatolewa na Serikali ya Tanzania. Mradi huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano, kuanzia mwaka 2014/2015. Kwa mwaka huu wa fedha, kiasi cha **shilingi milioni 90.63** ambacho kitatolewa na Serikali ya Ubelgiji kimetengwa ili kuwezesha kufanya mapitio ya *master plan* ya mkoa, kutayarisha mpango wa utekelezaji, kupata orodha ya vijiji vitakayotekelezwa *(identification study)* na kufanya usanifu. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2015/16.

**(iv) Miradi yenye Matokeo ya Haraka (*Quickwins*)**

**Mradi wa Maji Vijiji 100 Kandokando ya Bomba la Ziwa Victoria hadi Kahama-Shinyanga**

**112. Mheshimiwa Spika,** Wizara inatekeleza Mradi wa Maji wa vijiji **100** vilivyoko kandokando ya bomba kuu kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama-Shinyanga. Hadi mwezi Machi, 2014 upimaji na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika vijiji **31** vilivyoko Halmashauri za Wilaya za Msalala na Shinyanga Vijijini umekamilika. Ujenzi wa miradi katika vijiji **vinne** vya Magobeko, Nyashimbi, Kakulu na Butegwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala umeanza. Taratibu za kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa miradi katika vijiji vingine zinaendelea.

**113. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara itakamilisha usanifu kwenye vijiji vingine vilivyobaki kufikia **vijiji 100** na ujenzi wa miradi katika **vijiji 40** utakamilika ifikapo mwezi Juni, 2015. Utekelezaji huo utagharimu kiasi cha **shilingi 2,586,819,387** na matarajio ni kuwa na **vituo 664** vya kuchotea maji vitakavyohudumia zaidi ya wananchi **115,430**. **Jedwali Na. 9** linaonesha utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji 40 kandokando ya bomba kuu la maji toka Ziwa Victoria hadi Kahama-Shinyanga.

**Mradi wa Maji Bungu**

**114. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *World Vision* iliendelea na kazi za upanuzi na ukarabati wa mradi wa maji wa Bungu katika Wilaya ya Korogwe. Hadi mwezi Machi, 2014, jumla ya **vituo 22** vya kuchotea maji vimejengwa na kukarabatiwa katika vijiji vya Bungu, Manka na Msasa ambapo **wakazi 6,909** wanapata huduma ya maji. Vilevile, bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 10.4** kutoka chanzo cha maji kilichopo Sakare hadi kitongoji cha Sinai limejengwa; na mtandao wa kusambaza maji kutoka tanki la Gare hadi kijiji cha Msasa wenye urefu wa **kilomita 4** umekamilika. Aidha, mtandao wa kusambaza maji katika kijiji cha Manka wenye urefu wa **kilomita 6** umekamilika na matanki **mawili** yenye ujazo wa **lita 90,000** kila moja yamejengwa katika vijiji vya Manka na Gare.

**115. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huo utaendelea katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 ambapo tanki lenye ujazo wa **lita 90,000** litajengwa katika kijiji cha Sinai na mtandao wa mabomba utajengwa katika vijiji vya Bungu-Msiga, Ngulu, Kwemshai na Mlungui. Mradi huo utakapokamilika jumla ya **wakazi 18,460** wa vijiji **saba (7)** vilivyokusudiwa vya Bungu, Bungu Msiga, Kwamshai, Ngulu, Mlungui, Msasa na Manka watanufaika na huduma ya maji safi na salama.

**Mradi wa Ntomoko katika Halmashauri za Kondoa na Chemba**

**116. Mheshimiwa Spika,** kati ya vijiji **18** vinavyohudumiwa na mradi wa maji wa Ntomoko, ujenzi wa miundombinu katika vijiji **vinne (4)** vya Jenjeluse, Goima, Mtakuja na Mlongia upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambazo ni **asilimia 88** kwa kijiji cha Jenjeluse, Goima **asilimia 62**, Mtakuja **asilimia 8** na Mlongia **asilimia 20**. Wakandarasi kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya maji katika vijiji **10** vya Makirinya, Kirere cha Ng'ombe, Lusangi, Hamai, Songolo, Madaha, Churuku, Kimkima, Jinjo na Jangalo wamepatikana na utafiti kwa ajili ya kuchimba visima katika vijiji vya Igunga, Itolwa, Mapango na Chandama umekamilika. Halmashauri husika zimekubaliana kuwa mikataba iliyoingiwa na Wilaya mama ya Kondoa ihamishiwe Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ili kuongeza ufanisi wa usimamizi.

**Mradi wa Chiwambo**

**117. Mheshimiwa Spika,** huduma ya maji katika mradi wa Chiwambo, Wilaya ya Masasi imekuwa duni kutokana na kuchakaa kwa miundombinu. Katika kuboresha huduma ya maji kwenye maeneo hayo, Wizara inakarabati miundombinu ya maji ikihusisha ulazaji wa bomba kuu la **kilomita 11** kutoka kwenye chanzo cha maji cha chemchemi ya Lulindi hadi kwenye matanki ya kijiji cha Nagaga, kukarabati bomba lenye kipenyo cha **milimita 110** kutoka Nagaga hadi Chiungutwa umbali wa **kilomita 16** na kukarabati bomba lenye kipenyo cha **milimita 110** kutoka Nagaga hadi Mitesa umbali wa **kilomita 10**. Vilevile, ukarabati na upanuzi wa mradi huo unahusisha ulazaji wa mabomba yenye urefu wa **kilomita 50**, ujenzi wa matanki **10** ya kuhifadhi maji na vituo **78** vya kuchotea maji. Kukamilika kwa mradi huu kutanufaisha wakazi wapato **32,570** wanaoishi katika kata saba za Lulindi, Mbuyuni, Namalenga, Nachungutwa, Sindano, Mchauru na Lupumbulu.

**118. Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Machi 2014, kazi ya kulaza bomba kuu la **kilomita 11** kutoka kwenye chanzo cha maji hadi kwenye matanki ya Nagaga umefikia **kilomita 9.7**. Aidha, bomba la **milimita 200** limelazwa umbali wa **kilomita mbili** kutoka kwenye chanzo hadi matanki ya Nagaga ili kuongeza wingi wa maji katika eneo la mradi. Bomba la **milimita 110** la urefu wa **kilomita mbili** limelazwa kutoka Nagaga kwenda Chiungutwa na kutoka Nagaga kwenda Mitesa limelazwa kwa umbali wa **kilomita 1.5**. Ujenzi wa matanki **mawili** kwenye eneo la mradi umeanza na ukarabati wa matanki **manne** unaendelea. **Vituo 11** vya kuchotea maji vimejengwa. Mikataba kwa ajili ya kazi za ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji kwenye vijiji vyote vya mradi huo imesainiwa.

**(v) Usambazaji wa Maji kutoka kwenye Mabwawa na Miradi ya Matokeo ya Haraka**

**119. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, jumla ya **shilingi bilioni 45.74** zitatumika kwa ajili ya kuendelea kutekeleza miradi inayotarajiwa kuleta matokeo ya haraka. Miradi hiyo itahusisha ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji kutoka kwenye mabwawa, visima virefu na vyanzo vingine vinavyoweza kusambaza maji kwenye vijiji zaidi ya kimoja. Katika miradi hiyo, jumla ya **vituo 4,808** vya kuchotea maji vitajengwa kwa ajili ya kuhudumia wananchi **1,253,101**.

**120. Mheshimiwa Spika**, kati ya **shilingi bilioni 45.74** kiasi cha **shilingi bilioni 10.18** zitatumika upande wa usambazaji maji kutoka kwenye mabwawa kwenye vijiji **30** vitakavyokuwa na vituo vya kuchotea maji **993** vyenye uwezo wa kuhudumia watu **257,166**. Mradi utatumia vyanzo vya maji kutoka mabwawa **10** ya Mti Mmoja (Monduli), Looderkes (Simanjiro), Salama Kati

(Bunda), Nyambori (Rorya), Kawa (Nkasi), Mihama (Nzega), Ulyanyama (Sikonge), Kwa Maligwa (Kilindi), Masuguru (Bagamoyo) na Nkoma (Itilima). Aidha, **shilingi bilioni 35.56** zilizobaki zitatumika kutekeleza miradi yenye kuleta matokeo ya haraka iliyoainishwa kwa kutumia vyanzo vingine vya maji ikiwa ni visima virefu na vyanzo vya juu ya ardhi. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kushirikiana na OWM-TAMISEMI katika kujenga uwezo wa Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa ili kuharakisha utekelezaji wa miradi hiyo. (**Majedwali Na. 10.1** na **10.2)** yanaonesha mchanganuo wa fedha zilizopangwa kutumwa kwenye Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa kwa mwaka 2014/2015.

### (vi) Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Kitaifa

**121. Mheshimiwa Spika,** Mpango wa *BRN* umeainisha miradi mitatu ya kitaifa itakayokarabatiwa na kupanuliwa mifumo ya usambazaji kwa kipindi cha miaka mitatu. Miradi itakayohusika ni:-

i. Mradi wa kitaifa wa Makonde ambao utahusisha vijiji vya Wilaya za Newala, Tandahimba na Mtwara Vijijini;

ii. Mradi wa maji wa Wanging'ombe utakaohusisha uunganishaji wa vijiji vilivyo kandokando ya bomba kuu hadi Wilaya ya Mbarali Mkoani Mbeya; na

iii. Handeni Trunk Main (HTM) utakaohusisha Wilaya za Handeni, Korogwe na Kilindi.

Katika mwaka 2014/2015 Serikali itatumia kiasi cha **shilingi bilioni 1.6** kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa miradi hiyo**.** Kati ya fedha hizo, mradi wa maji wa Makonde umepangiwa **shilingi milioni 800**, Wanging'ombe **shilingi milioni 300** na HTM **shilingi milioni 500.**

**122. Mheshimiwa Spika**, ili miradi ya maji iwe endelevu na kutoa huduma iliyokusudiwa, Serikali imeweka taratibu zitakazohakikisha kuwa miradi hiyo inakuwa endelevu ikiwa ni pamoja na kuunda wa Vyombo vya Watumiaji Maji (*COWSOs*), kuongeza idadi ya wataalam kwenye miradi, na kutoa mafunzo kwa wasimamizi wa skimu za miradi ya maji.

### 3.2.4 Ujenzi wa Miradi Mingine ya Maji Vijijini

**123. Mheshimiwa Spika**, Serikali inashirikiana na mashirika na taasisi zisizo za kiserikali kujenga miradi ya maji katika juhudi za kuboresha na kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji vijijini.

**(i) Uvunaji wa Maji ya Mvua**

**124. Mheshimiwa Spika,** uvunaji wa maji ya mvua ni muhimu sana kwa nchi yetu kutokana na hali duni ya upatikanaji wa maji hasa maeneo kame ya vijijini. Halmashauri zinatekeleza agizo la Serikali la kuandaa mpango wa miaka mitano na kutunga sheria ndogo zinazohakikisha kuwa michoro ya nyumba zote zinazojengwa zinajumuisha mifumo ya miundombinu ya kuvuna maji ya mvua kabla ya kuidhinishwa ujenzi wake. Hadi mwezi Machi, 2014 Serikali kupitia Halmashauri imejenga jumla ya matanki **675** ya uvunaji wa maji kwenye maeneo mbalimbali zikiwemo taasisi kama shule, zahanati na taasisi nyingine.

**(ii) Ujenzi wa Mabwawa**

**125. Mheshimiwa Spika**, yapo maeneo hapa nchini yenye ukame na kutokuwa na vyanzo vya maji vya uhakika juu ya ardhi na visima vingi vilivyochimbwa kukosa maji.

Aidha, maeneo mengine yana vyanzo vyenye uwezo mdogo sana wa kutoa maji. Hali hiyo imeilazimu Wizara kujenga na kukarabati mabwawa kwenye maeneo hayo ili kuwapatia wananchi huduma endelevu ya maji. Ujenzi huu unahusu mabwawa ya:-

**(a) Bwawa la Sasajila**

**126. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa bwawa la Sasajila lililopo wilayani Chamwino, mkoa wa Dodoma ulisimama kutokana na Mkandarasi wa awali kuondoka eneo la mradi kinyume na Mkataba. Kwa sababu hiyo, Wizara imeajiri Mkandarasi mwingine ambaye ameanza kazi mwezi Novemba, 2013. Hadi mwezi Machi, 2014 ujenzi wa bwawa umefikia **asilimia 62.5.** Katika mwaka 2014/2015, kazi za ujenzi zilizobaki zitakamilishwa.

**(b) Bwawa la Iguluba**

**127. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa bwawa la Iguluba, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa Vijijini, ulikamilika kulingana na kazi zilizoainishwa kwenye Mkataba. Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika ulibaini ongezeko la kazi ambazo hazikuwemo kwenye mkataba huo. Kazi ambazo hazijakamilika ni kujenga *crest weir,* miundombinu ya mawe kuzuia mmomonyoko wa udongo; kupanda nyasi upande wa nje wa tuta na kupanga mawe upande wa ndani wa tuta, ujenzi wa miundombinu ya kutolea maji kwenye bwawa na ujenzi wa *sand traps* **3** za

kupokea mchanga na kuondoa mchanga ndani ya Bwawa. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itakamilisha kazi za ziada zilizojitokeza.

### (c) Mabwawa ya Habiya, Seke Ididi na Matwiga

**128. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeanza kutekeleza ujenzi wa mabwawa ya Habiya (Itilima, Simiyu), Seke Ididi (Kishapu, Shinyanga) na Matwiga (Chunya, Mbeya) ambayo ujenzi wake ulisimama baada ya Wakandarasi husika kushindwa kazi na kuondoka kwenye maeneo ya miradi. Hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kusitisha mikataba ya Wakandarasi hao baada ya kwenda kinyume na mikataba. Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*DDCA*) ameteuliwa kukamilisha ujenzi wa mabwawa hayo. Mikataba ya kukamilisha ujenzi wa mabwawa hayo imesainiwa tarehe 28.2.2014 na ujenzi utaanza mwezi Juni, 2014 baada ya msimu wa mvua.

### (d) Bwawa la Kawa

**129. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa Bwawa la Kawa (Nkasi, Rukwa) umefikia **asilimia 95**. Mkandarasi aliyekuwa akiendelea na ujenzi wa bwawa hilo aliondoka eneo la mradi. Aidha, Wizara imeajiri Mkandarasi mwingine kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji kutoka katika bwawa kupeleka maji katika vijiji vya Nkundi, Kalundi na Fyengerezya. Ujenzi wa mradi huo umesimama kwa muda ili kupisha usanifu wa kituo cha kutibu maji. Hadi mwezi Machi, 2014 ujenzi wa miundombinu hiyo ulikuwa umefikia **asilimia 20**.

Vilevile, Wizara inajadiliana na Mkandarasi huyo ili akamilishe kazi ya ujenzi wa bwawa zilizoachwa na Mkandarasi wa awali. Mradi huo ukikamilika jumla ya **wananchi 13,500** watanufaika na huduma ya maji.

### (e) Bwawa la Wegero

**130. Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa Bwawa la Wegero (Butiama, Mara) ulikamilika mwaka 2010 kwa mujibu wa mkataba wa awali. Hata hivyo kuongezeka kwa shughuli za kijamii hasa kilimo katika eneo linalozunguka bwawa kumesababisha bwawa hilo kujaa tope katika muda mfupi na kushindwa kutumika ipasavyo. Wizara ilifanya upimaji mwezi Novemba, 2013, na kuonekana kuwa bwawa linaweza kufanyiwa ukarabati ili kuongeza wingi wa maji kwa mita za ujazo 32,000. Kazi hiyo zitafanyika katika mwaka wa fedha 2014/2015.

### (f) Bwawa la Mwanjoro

**131. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa bwawa la Mwanjoro (Meatu, Simiyu) umekamilika kwa **asilimia 78.** Ujenzi huo kwa sasa umesimama baada ya Mkandarasi kuondoka eneo la kazi kinyume na Mkataba. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaajiri Mkandarasi mwingine ili kukamilisha kazi zilizobaki.

**(g) Bwawa la Kidete**

**132. Mheshimiwa Spika,** Bwawa la Kidete (Kilosa, Morogoro) lilijengwa kabla ya Uhuru kwa lengo la kuthibiti mafuriko kwenye eneo la Reli ya Kati. Bwawa hilo lilibomoka kutokana na mafuriko ya mwaka 2003, hivyo kuilazimu Serikali kulijenga upya. Gharama ya ujenzi ilikadiriwa kuwa **shilingi bilioni 4.48**. Ujenzi umesimama kutokana na matatizo ya kimkataba ambayo yanashughulikiwa ili ujenzi uweze kukamilishwa katika mwaka 2014/2015.

### 3.2.5 Uendeshaji na Matengenezo

**(i)Mfumo wa Takwimu za Miundombinu ya Maji**

**133. Mheshimiwa Spika,** ili kupata takwimu sahihi zinazohusiana na huduma ya maji vijijini, Wizara yangu imetekeleza mradi wa kuainisha vituo vya kuchotea maji vijijini unaotumia mfumo wa kompyuta. Kuainishwa kwa vituo hivyo kumewezesha kufahamika kwa usahihi zaidi takwimu za uendeshaji wa miundombinu na kuandaa ramani za vituo vya maji (*water point mapping*). Takwimu zilizopatikana zinawezesha Halmashauri kufahamu hali ya upatikanaji wa maji katika vijiji.

**134. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi, 2014 takwimu za vituo **88,913** vya kuchotea maji katika Halmashauri 168 zimekusanywa. Aidha, Wizara imetoa mafunzo maalum ya utumiaji wa vifaa kwa ajili ya kutoa na kuboresha taarifa (*data up-dating*) ya vituo vya kuchotea maji kwa wahandisi wote wa Sekretarieti za mikoa; na wahandisi wa maji wa Wilaya, mafundi sanifu na wasajili wa vyombo vya watumia maji wa Halmashauri zote nchini. Mafunzo hayo yalitolewa kwenye vituo **vinne (4)** vya Moshi, Mbeya, Mwanza na Morogoro na kukamilika mwezi Aprili 2014. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri zote za Wilaya itaendelea kuboresha mfumo wa ukusanyaji takwimu kwa kutoa mafunzo, kununua vifaa na matumizi ya teknolojia mpya kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati.

**(ii)Uundaji na Usajili wa Vyombo vya Watumiaji Maji**

**135. Mheshimiwa Spika,** kulingana na **Kifungu Na. 31** cha **Sheria Na. 12** ya mwaka **2009** ya Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Halmashauri

zinaelekezwa kusajili vyombo vya watumiaji maji *(COWSOs*) ili kuhakikisha kuwa uendeshaji na usimamizi wa miradi ya maji unafanyika kwa mujibu wa sheria. Wizara yangu, imetoa miongozo ya usajili ikiwemo uteuzi wa Wasajili katika Halmashauri na namna vyombo vitakavyoendeshwa. Kupitia sheria na miongozo hiyo, wananchi wanawajibika kuunda vyombo hivyo na kuvisajili rasmi.

**136. Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Machi, 2014, idadi ya vyombo vya watumiaji maji vilivyosajiliwa kisheria imefikia **373** kutoka vyombo **147** ya mwaka uliopita.

Aidha, Wizara yangu imetoa mafunzo mbalimbali kwa Halmashauri kwa ajili ya vyombo hivyo ikiwa ni pamoja na mafunzo ya uendeshaji, utunzaji wa fedha, matengenezo madogo madogo ya mradi na njia mbalimbali za utoaji wa taarifa za maendeleo ya mradi.

Katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea kutoa mafunzo, kuhimiza uundwaji zaidi wa vyombo vya watumiaji maji na kusisitiza wasajili kuongeza kasi ya usajili kwa miradi iliyopo na mingine itakayojengwa.

Vilevile, Halmashauri zinatakiwa ziandae mipango kazi ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kuanzisha na kusajili vyombo na kutoa taarifa ya utekelezaji wa mipango hiyo kila robo mwaka.

## *3.3 HUDUMA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MIJINI*

**137. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ilitekeleza Programu ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini kujenga,kukarabati na kupanua mifumo ya majisafi na majitaka pamoja na kuzijengea uwezo Mamlaka za maji mijini.

Lengo la utekelezaji huo ni kuwapatia wananchi wengi zaidi huduma nzuri katika Jiji la Dar es Salaam, miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya, miji midogo, na miradi ya maji ya kitaifa.

### 3.3.1 Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

#### (a) Miradi ya Maji ya Kukidhi Mahitaji ya Muda wa Kati katika Miji Saba

**138. Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya inatekeleza miradi ya

kukidhi mahitaji ya maji katika miji saba ya Bukoba, Musoma, Lindi, Kigoma, Sumbawanga, Mtwara na Babati.

**139. Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Manispaa za Musoma na Bukoba unaotekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*) unaendelea. Hadi mwezi Machi, 2014 utekelezaji wa miradi hiyo ambayo inagharimu kiasi cha **Shilingi bilioni 68.2** umefikia **asilimia 50** kwa Manispaa ya Musoma na **asilimia 40** kwa Bukoba. Kazi zinazotekelezwa ni kujenga mitambo ya kusafisha na kusukuma maji pamoja na kulaza mabomba ya usambazaji wa maji katika miji hiyo. Miradi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2014.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya imeanza utekelezaji wa miradi katika Miji ya Lindi, Kigoma na Sumbawanga yenye gharama ya **Euro milioni 62.59.** Wakandarasi wanaendelea na ujenzi wa miradi hiyo na wanatazamiwa kukamilisha kazi mwezi Aprili, 2015. Utekelezaji wa miradi hiyo unahusu uchimbaji wa visima, ujenzi wa mabanio, ujenzi wa matanki, ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya usambazaji, ujenzi wa chujio na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji.

**140. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Ser**i**kali ya Ujerumani kupitia *KfW* ilitenga **Euro milioni 8.72** kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika Mij**i ya Mtwara na Baba**ti chini ya programu ya *Millenium Development Goal Initiative (MDGI-EU)*. Kufuatia kumalizika kwa upembuzi yakinifu imebainika kuwa fedha hizo hazitatosha kwa ajili ya ujenzi wa miradi hiyo. Wizara yangu inakamilisha taratibu za kumtafuta Mtaalam Mshauri kwa ajili ya usimamizi wa utekelezaji wa Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa miji hiyo ambaye ataainisha kazi ambazo zitafanyika kulingana na kiasi cha fedha kilichopo huku Serikali ikiendelea na kutafuta jibu la muda mrefu katika Miji hiyo.

### (b) Miradi ya Maji ya Kukidhi Mahitaji ya Muda Mrefu

### (i) Mradi wa Maji Tabora

**141. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu ilitekeleza mradi wa ukarabati wa miundombinu ya maji na maboresho ya kituo cha maji cha Igombe Mjini Tabora kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 4.84.** Mradi huo unatekelezwa kwa kushirikiana na Serikali ya Uswisi kupitia Shirika lake la Maendeleo (*SECO*). Hadi mwezi Machi, 2014, mradi umekamilika kwa **asilimia 96** na unatarajiwa kukamilika na kukabidhiwa ifikapo mwezi Juni, 2014. Aidha, ukarabati na upanuzi wa chujio la maji katika kituo cha Igombe Mjini Tabora unaogharamiwa na Mfuko wa Pamoja wa Sekta ya Maji unaendelea kwa kufunga pampu kubwa mpya tatu na kulaza bomba kuu la urefu wa **mita 240**

kutoka bwawani hadi kwenye chujio. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2015. Kukamilika kwa mradi huo kutawapatia wakazi wa Manispaa ya Tabora Maji ya kutosha hadi mwaka 2032.

**(ii) Mradi wa Maji Mjini Dodoma**

**142. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha kiwango cha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Chuo Kikuu cha Dodoma, Wizara yangu inatekeleza mradi wa ujenzi wa kuongeza majisafi. Mradi huo unahusisha ujenzi wa kituo cha kusukuma majisafi kwenda Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) na ujenzi wa matanki **matatu (3)** ya ujazo wa lita **milioni 12.** Aidha, mradi wa ujenzi wa mfumo wa uondoaji majitaka unaogharimu **shilingi bilioni 27.7** unaendelea. Mradi huo unajumuisha ujenzi wa mtandao wa kukusanya majitaka wenye urefu wa **kilomita 32** na ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka. Hadi mwezi Machi, 2014 utekelezaji wa kazi za mradi wote umefikia **asilimia 54**, na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2014. Kukamilika kwa mradi huo kutaondoa kero ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na kufurika kwa majitaka katika maeneo mbalimbali ya chuo.

**143. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inaendelea na juhudi za kuwapatia wananchi wa Manispaa ya Dodoma majisafi na salama kwa kuendeleza Mradi ulioanza mwezi Desemba 2012, unaotekelezwa kwa kushirikiana na Serikali ya Korea Kusini kwa gharama ya **shilingi bilioni 49.62**. Hadi mwezi Machi 2014, **visima 15** vimekarabatiwa kati ya **visima 21** vilivyopangwa na visima vipya **viwili (2)** vimechimbwa kati ya visima **vitatu (3).** Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 35**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2015 na utaongeza kiwango cha utoaji huduma kutoka **asilimia 87** hadi kufikia **asilimia 90.**

**144. Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na mahitaji makubwa ya maji yanayotokana na ongezeko la watu pamoja na shughuli za kiuchumi na kijamii katika Manispaa ya Dodoma, Serikali imeajiri Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kusanifu Bwawa la Farkwa na tayari amewasilisha taarifa ya awali ya usanifu (*interim report I)* imewasilishwa na anaendelea na usanifu. Pia, bwawa hilo litakuwa chanzo cha maji kwa Miji ya Kondoa, Chamwino, Chemba na Bahi ili kukidhi ongezeko la mahitaji ya maji katika miji hiyo. Gharama za usanifu wa bwawa hilo ni **shilingi bilioni 1.6.** Usanifu huo unaotarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2014 utaonesha gharama halisi za ujenzi wa bwawa hilo pamoja na kiwango cha maji kitakachopatikana.

**(iii) Mradi wa Maji Jijini Arusha**

**145. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Serikali imeanza kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Jiji la Arusha. Utekelezaji huo unahusu uchimbaji wa kisima kirefu na ujenzi wa tanki la maji katika maeneo ya kata ya Moshono. Hadi mwezi Machi 2014, uchimbaji wa kisima umefikia **asilimia 75** na kinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2014. Ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita milioni 2.5** umeanza na unatarajiwa kujengwa na kukamilika mwezi Desemba, 2014. Mradi huo utakapokamilika utahudumia wakazi wapatao **28,124** wa Kata za Moshono na Engutoto**.**

**(iv) Mradi wa Maji Mjini Singida**

**146. Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kiarabu (*BADEA*) pamoja na Mfuko wa Maendeleo wa Nchi zinazozalisha Mafuta (*OPEC Fund for International Development-OFID*) ilikamilisha ujenzi wa mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya majisafi Mjini Singida. Ujenzi huo ulihusu uchimbaji wa visima virefu **10**, kati ya hivyo visima **saba (7)** vilikamilika na tayari vinatumika katika maeneo ya Mwankoko **viwili (2)** na Irao **vitano (5).** Visima **vitatu (3)** kati ya **10** havikuwa na maji ya kutosha.

Aidha, kazi za ujenzi wa matanki **mawili (2)** katika maeneo ya *Airport;* kulaza bomba kuu la maji hadi kwenye matanki; na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji katika eneo la Mandewa zilikamilika. Mradi huo uligharimu **shilingi bilioni 32.53**. Kukamilika kwa mradi huo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka lita **milioni 8** kwa siku kwa sasa hadi kufikia lita **milioni 17.76** na utakidhi **asilimia 100** ya mahitaji ya wakazi wa Mji wa Singida.

**(v) Mradi wa Maji Morogoro Mjini**

**147. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi wa kupanua na kuboresha upatikanaji wa majisafi katika Manispaa ya Morogoro unaendelea. Hadi mwezi Machi 2014, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukarabati matanki **matatu (3)**, ulazaji wa bomba kuu la maji la urefu wa **kilomita 1.8**, kupanua chujio la maji la Mafiga na kujenga mtambo wa kusafisha maji wa Mambogo. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 92** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2014. Mradi huo unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Shirika la MCC la Marekani na utagharimu **shilingi bilioni 10**. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita **milioni 23** kwa siku za sasa hadi lita **milioni 33**.

**(vi) Mradi wa Maji Songea Mjini**

**148. Mheshimiwa Spika**, kazi ya ukarabati wa chanzo cha Mto Ruhira, Mjini Songea imeanza mwezi Aprili, 2014. Kazi hiyo ni kujenga banio la maji (*weir)* ili kukabiliana na upungufu wa maji wakati wa kiangazi. Gharama ya kukamilisha

mradi ni **Shilingi bilioni 2.6**. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea na utekelezaji wa mradi huo ambao utakapokamilika unatarajiwa kuongeza uhifadhi wa maji kutoka lita **milioni 3.4** za sasa hadi kufikia lita **milioni 6.5** wakati wa kiangazi.

**(vii) Mradi wa Kutoa Maji Mto Ruvuma Kupeleka Mtwara-Mikindani**

**149. Mheshimiwa Spika,** Kutokana na ongezeko la shughuli za kiuchumi katika Manispaa ya Mtwara, Serikali inaendelea kutafuta vyanzo vingine vitakavyohudumia Manispaa hiyo. Katika mwaka 2013/2014 Serikali illingia mkataba na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi mpya wa kutoa maji mto Ruvuma kwenda Manispaa ya Mtwara na vijiji vitakavyopitiwa na bomba kuu. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2014 na ujenzi utaanza mwaka wa fedha 2014/2015 ambapo Serikali imetenga shilingi milioni 800 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huu.

**(viii) Mradi wa Maji katika Miji ya Geita, Sengerema na Nansio**

**150. Mheshimiwa Spika,** awamu ya pili ya Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Ziwa Victoria (*LVWATSAN II*) unatekelezwa katika miji **15** iliyoko kwenye nchi **tano (5)** za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*).

Kwa upande wa nchi yetu mradi unatekelezwa katika Miji ya Geita, Sengerema na Nansio kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 30.4** na unasimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (*MWAUWASA*).

**151. Mheshimiwa Spika,** kazi zinazoendelea kutekelezwa ni za vipindi vya muda mfupi na muda mrefu ambazo ni kujenga na kuboresha miundombinu ya majisafi, mifumo ya utoaji wa huduma ya usafi wa mazingira, mitaro ya maji ya mvua na kuzijengea uwezo Mamlaka za maji za Miji ya Geita, Sengerema na Nansio. Mtaalam Mshauri wa kusanifu na kusimamia kazi za ujenzi wa mradi huo amewasilisha taarifa ya usanifu wa mradi.

**152. Mheshimiwa Spika,** kazi ambazo tayari zimetekelezwa chini ya mpango wa muda mfupi ni ununuzi wa magari **matano (5)** na kugawiwa kwa mamlaka za maji za Geita **(1)**, Sengerema **(1),** Nansio **(1)** na kwa *MWAUWASA* **(2)**; ununuzi wa pikipiki **nane (8)** kwa Geita **(3),** Sengerema **(3)** na Nansio **(2)**; ununuzi wa trekta na tela zake **tisa** (**9**) kwa Geita **(3)**, Sengerema **(3)** na Nansio **(3)**; Ununuzi wa magari makubwa ya majitaka **matano (5)** kwa Geita **(2),** Sengerema **(2)** na Nansio **(1)**; na ununuzi wa magari madogo ya majitaka **matatu (3)** kwa Geita **(1),** Sengerema **(1)** na Nansio **(1)**. Aidha, mamlaka hizo zimegawiwa vifaa vya kukusanyia taka ngumu **vikiwemo kontena na toroli,** Geita **(40),** Sengerema **(37)** na Nansio **(27)**. Mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya maji amepatikana

na Mikataba ya ujenzi wa miradi hiyo itasainiwa kabla ya mwezi Agosti, 2014 na ujenzi utakamilika mwezi Desemba, 2015.

**(ix) Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria Unaotekelezwa na Mgodi wa Dhahabu wa Geita (*GGML*) kwa Kushirikiana na Serikali**

**153. Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ya Mji wa Geita kwa kushirikiana na Mgodi wa Dhahabu wa Geita (*Geita Gold Mining Limited – GGML*) wamekamilisha kazi ya ujenzi wa chanzo, chujio la maji, kulaza bomba kuu na tanki moja lenye ujazo wa **lita milioni 1.2** kwa gharama za **Dola za Marekani milioni 5.4**, fedha ambazo zimetolewa na *GGML*. Katika mwaka 2014/2015, kazi ya ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji itatekelezwa na mradi utagharimu kiasi cha **Dola za Marekani milioni 1.4** kati ya hizo mchango wa Serikali ni **Dola za Marekani 400,000** na *GGML* ni **Dola za Marekani milioni 1.** Maandalizi ya Hati ya Makubaliano (*Limited Distribution Network Agreement*) kati ya Wizara yangu, *GGML*, Halmashauri ya Geita na Mamlaka ya Majisafi Geita yapo kwenye hatua za mwisho na inatarajiwa kusainiwa baada ya ridhaa ya Mwanasheria Mkuu. Mradi huo utakapokamilika utazalisha lita **milioni 4.8** za maji kwa siku na kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 3.5** hadi **asilimia 40**. Aidha mwaka wa fedha 2014/2015 Serikali imetenga Shilingi billioni 2.5 kwa ajili ya kupanua mtandao wa usambazaji maji katika mji wa Geita.

**154. Mheshimiwa Spika,** mradi wa maji ya mtiririko wa Ihako unaofadhiliwa na *UN HABITAT* kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliibuliwa kutokana na uhaba wa maji uliokuwepo katika miji ya Muleba na Mutukula. Kwa upande wa Muleba, mradi umelengwa kutekelezwa katika awamu mbili. Awamu ya Kwanza ulihusisha ujenzi wa chanzo cha Ihako chenye uwezo wa kuzalisha maji **lita 544,000** kwa siku; tanki la kuhifadhi maji lenye ujazo wa **lita 680,000**; ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 10.1**; na ujenzi wa **vituo 19** vya kuchotea maji**.** Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huo umekamilika kwa gharama ya **shilingi bilioni 1.39**.

**155. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015. Wizara yangu itakamilisha utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi huu kwa kulaza mabomba ya usambazaji maji yenye urefu wa **kilomita 21.5**; uchimbaji wa kisima kirefu na kufunga pampu. Mradi huo ukikamilika utahudumia zaidi ya wakazi **29,000** ambapo kwa sasa mradi unahudumia wakazi wapatao **11,563** na kati ya hao wakazi **10,063** ni wa mji wa Muleba na **1,500** ni wa vijiji vya Bwata, Kamishango, Kabare na Katanga.

**156. Mheshimiwa Spika,** katika mji wa Mtukula, kazi zilizokamilika ni ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 2.1**, kulaza mabomba ya kusambaza maji lenye urefu wa **kilomita 5.3**, uchimbaji wa visima **viwili (2)**, ujenzi wa vituo **16** vya

kuchotea maji na ujenzi wa tanki la ujazo wa **lita 120,000.** Gharama za mradi ni **shilingi milioni 653.29**. Kazi zilizobaki ni kupeleka umeme kwenye visima **viwili (2)** na ufungaji wa pampu. Mradi huo utakapokamilika utahudumiwa wakazi wapatao **5,000** wa mji wa Mtukula.

### (x) Miradi Mipya katika Eneo la Ziwa Victoria

**157. Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya *(European Investment Bank-EIB*) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*French Development Agency-AFD*) itatekeleza mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji pamoja na usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza, pamoja na Miji ya Musoma, Bukoba, Magu, Misungwi na Lamadi.

Katika utekelezaji wa mradi huo, jumla ya **Euro milioni 104.5** zitatumika ambapo Serikali itatoa **Euro milioni 14.5,** *EIB* na *AFD* kwa pamoja watatoa jumla ya **Euro milioni 90**. Mikataba ya kifedha ilisainiwa tarehe 23/12/2013 na tarehe 5/03/2014 hivyo fedha ziko tayari. Hatua za manunuzi zimeanza na Mtaalam Mshauri anatarajiwa kupatikana mwezi Juni, 2014.

**158. Mheshimiwa Spika,** kukamilika kwa mradi huo kutaongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 35** hadi **asilimia 90** kwa Mji wa Magu; **asilimia 5** hadi **asilimia 90** kwa Mji wa Lamadi; na **asilimia 45** hadi **asilimia 90** kwa Mji wa Misungwi. Aidha, katika Jiji la Mwanza mradi unategemewa kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi katika maeneo ya miinuko sambamba na kuboresha usafi wa mazingira kwenye maeneo hayo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyoo katika shule za msingi na maeneo ya vituo vya mabasi.

**159. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014 Wizara yangu iliendelea kutekeleza miradi ya majitaka kwa Miji ya Bukoba na Musoma. Usanifu na uandaaji wa makabrasha vya zabuni kwa mifumo ya majitaka unaendelea na mkataba wa kupata fedha (*loan agreement*) za kutekeleza miradi hiyo kati ya Serikali na *AFD* utasainiwa mwezi Mei, 2014. Ujenzi wa miradi utaanza baada ya kukamilika kwa taratibu za zabuni na kumpata Mkandarasi. Miradi ikikamilika itahudumia **asilimia 15** ya wakazi wa Bukoba na **asilimia 20** ya wakazi Mji wa Musoma.

### (xi) Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji Inayozunguka Ziwa Tanganyika

**160. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira kwa eneo la Ziwa Tanganyika (*LT-WATSAN*) unatekelezwa katika nchi za Zambia, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda na Tanzania, na kusimamiwa na Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa (*UN-HABITAT*).

Kwa upande wa Tanzania, mradi unatekelezwa katika miji ya Kigoma, Kasulu, Mpanda, Namanyere, Uvinza na Kasanga. Mradi huo ulifanyiwa upembuzi yanikifu mwaka 2011, hata hivyo, utekelezaji wake haukuanza kutokana na kutopatikana kwa fedha. Kwa sasa gharama za utekelezaji zimeongezeka ikilinganishwa na makadirio ya awali, hivyo, nchi wanachama walielekezwa wapitie upya gharama za ujenzi ili kupata gharama halisi za sasa. Baada ya mapitio, gharama hizo kwa Tanzania zimekadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 39.18,** ambazo zimepangwa kama ifuatavyo:-

Mji wa Kigoma ni **Dola za Marekani milioni 19.10**; Kasulu **Dola za Marekani milioni 5.39**; Mpanda **Dola za Marekani milioni 4.33;** Namanyere **Dola za Marekani milioni 3.79;** Uvinza **milioni 3.01** na Kasanga **milioni 3.56.** Kazi zinazotarajiwa kutekelezwa ni pamoja na usambazaji wa majisafi na usafi wa mazingira, ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua na uondoaji wa taka ngumu pamoja na kuzijengea uwezo taasisi husika. Wafadhili wa mradi huo wanatarajiwa kupatikana baada ya majadiliano yetu katika Kikao cha Mawaziri wa Maji wa nchi zetu kilichofanyika Mjini Bujumbura, mwezi Aprili, 2014

### 3.3.2 Uboreshaji wa Huduma ya Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa Mipya

**161. Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuboresha huduma ya majisafi katika miji mikuu ya mikoa mipya ya Mpanda, Njombe na Bariadi. Miradi inayoendelea kutekelezwa katika miji hiyo ni:-

**(i) Mji wa Mpanda**

**162. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatarajia kutumia **shilingi bilioni 2.6** kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji kwa kujenga miradi mbalimbali katika Mji wa Mpanda. Katika mwaka 2013/2014 Serikali imetuma kiasi cha **shilingi bilioni 1.5** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika mji huo. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na kulaza bomba kutoka maeneo ya Ikolongo hadi Kazima urefu wa **kilomita 13.6**; ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita milioni moja;** nyumba **mbili** za watumishi Ikolongo na Kazima na kufungwa *solar panel;* ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji urefu wa **kilomita 48** yenye kipenyo cha **milimita 110** maeneo ya Kawajense, Kazima, Nsemulwa, Ilembo na Makanyagio; na ununuzi wa dira za maji **4,000** na viungio vyake.

**163. Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Machi 2014, utekelezaji wa kazi hizo, ni kama ifuatavyo:-

i. Mtaro wa urefu wa **kilomita 12.4** umechimbwa kati ya **kilomita 13.6** na kulaza bomba urefu wa **kilomita 1.3**. Kazi hizo zinatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2014;

ii. Ujenzi wa nyumba **mbili** na tanki la maji lenye ujazo **lita milioni moja** umeanza na kazi hii itakamilika mwezi Agosti, 2014; na

iii. Ununuzi wa viungio kwa ajili ya ufungaji wa dira za maji umekamilika. Aidha, ununuzi wa vifaa vyote vya mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2014.

Mradi utakapokamilika utaongeza kiasi cha lita **milioni tano** za maji kwa siku. Vilevile, idadi ya watu wapatao **50,000** watanufaika na huduma hiyo ambapo upatikanaji wa maji utaongezeka kutoka **asilimia 38.8** ya sasa hadi kufikia **asilimia 72**. Katika mwaka 2014/2015, Serikali imetenga **shillingi billioni 3** kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa mradi kutoka chanzo cha maji cha mtiririko Ikolongo II awamu ya pili utakaoongeza upatikanaji wa maji kutoka **asilimia 72** hadi **asilimia 82**.

**(ii)Mji wa Njombe**

**164. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014 Serikali imetuma kiasi cha **shilingi bilioni 1.2** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji katika Mji wa Njombe. Kazi zinazoendelea kufanyika ni ujenzi wa intake ya maji na kulaza bomba kuu la maji kwa gharama ya **shilingi bilioni 1.75** na ujenzi wa matanki **matatu** ya lita **135,000** kila moja kwa gharama ya **shilingi milioni 321**. Kazi zote zinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2014. Mradi huo ukikamilika, kiasi cha maji kitaongezeka kutoka lita **milioni 3.66** hadi lita **milioni 5.77** kwa siku. Wananchi watakaonufaika na mradi wataongezeka kutoka **20,734** hadi **32,734**. Na mradi utakidhi mahitaji ya maji toka **asilimia 41** za sasa na kufikia **asilimia 58**. Katika mwaka 2014/2015 mradi huu utapanuliwa ili ufikie **asilimia 79** ya mahitaji ya Mji wa Njombe. Kiasi cha **shilingi bilioni 3.5** kimetengwa kwa kazi hiyo.

**(iii)Mji wa Bariadi**

**165. Mheshimiwa Spika,** kazi zilizopangwa kutekelezwa katika Mji wa Bariadi ni kuchimba visima **sita** na kufunga pampu; kujenga tanki la maji lenye ujazo wa **lita 45,000**; kupanua mtandao wa maji; kukarabati tanki la Somanda; kuunganisha umeme kwa ajili ya visima vya Somanda, Sanungu, Isanzu na Kidinda; na kujenga ofisi ya mamlaka ya maji. Mradi huo utagharimu **shilingi bilioni 2.** Hadi mwezi Machi 2014, mtaro wenye urefu wa **kilomita 6.8** kati ya **kilomita 7.6** umechimbwa na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa **kilomita 2.1**

umekamilika kati ya **kilomita 7.6** zilizopangwa. Nguzo za umeme tayari zimefika katika eneo la ujenzi. Katika mwaka 2013/2014, Wizara imetuma **shilingi bilioni 1.2** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. Mradi ukikamilika, kiasi cha maji kitaongezeka kutoka lita **861,000** hadi lita **1,560,000** kwa siku na huduma ya upatikanaji maji itaimarika kutoka **asilimia 17** hadi **asilimia 30.** Katika mwaka 2014/15 Serikali imetenga **shilingi bilioni 3.5** ili kuendelea na ujenzi na upanuzi wa mradi wa maji wa Mji wa Bariadi kutoka **asilimia 30** kufikia **asilimia 75** ya mahitaji ya kila siku.

#### 3.3.3 Usanifu wa Miradi ya Majisafi na Majitaka

**166. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea na usanifu wa kina na kuandaa vitabu vya zabuni kwa miradi ya maji katika miji midogo na miji mikuu ya Wilaya za Biharamulo, Muleba, Ngara, Karagwe, Chato na Bunazi (Kagera). Mtaalam Mshauri ameajiriwa tarehe 27/12/2013 na anaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu**.** Taratibu za kuwapata Wataalam Washauri katika mji wa Kakonko (Kigoma) na Miji ya Namanyere, Chala na Laela (Rukwa) zinaendelea. Kwa upande wa Miji ya Manyoni na Kiomboi (Singida), Mtaalam Mshauri ameanza kazi tarehe 21/08/2013 na anatarajiwa kukamilisha mwezi Juni, 2014. Usanifu unaendelea kwa miradi ya maji ya Miji ya Mombo, Songe, Lushoto, Kasela, Korogwe na Handeni Trunk Main - *HTM* katika Mkoa wa Tanga; na mradi wa kutoa maji Mto Ugala hadi Miji ya Urambo na Kaliua. Katika Mkoa wa Tabora. Katika mwaka **20**14/2015, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi hiyo.

#### 3.3.4 Miradi ya Maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka katika Miji Mbalimbali

**167. Mheshimiwa Spika,** maandalizi ya ujenzi wa miradi ya maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka katika miji mbalimbali yanaendelea. Mradi wa kupeleka maji katika Miji ya Bariadi, Mwanhuzi, Lagangabilili na Maswa utakapokamilika utanufaisha **vijiji 40** vilivyo umbali wa **kilomita 12** kandokando ya bomba kuu kutoka kwenye Ziwa Victoria. Katika mwaka 2014/2015, kiasi cha **shilingi bilioni 3.5** zimepangwa kwa ajili ya mradi huo, na upembuzi yakinifu utaanza mwezi Mei, 2014. Kwa upande wa Miji ya Magu kwenda Kwimba, mradi utakapokamilika utahudumia vijiji na miji ya njiani litakapopita bomba kuu ikiwemo miji midogo ya Sumve na Malya na kiasi cha **shilingi bilioni 4** zimepangwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Vilevile, Miji ya Kagongwa, Isaka hadi Tinde itapata huduma ya maji kutoka bomba kuu la Kahama-Shinyanga kutoka Ziwa Victoria. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu imepanga kutumia kiasi cha **shilingi bilioni 8** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

**166. Mheshimiwa Spika**, mradi wa upanuzi wa mtandao wa bomba kuu la maji la Mamlaka ya Maji ya *KASHWASA* kutoka tanki la maji lililopo katika kijiji cha Mhalo kwenda katika Mji wa Ngudu unatekelezwa na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2014. Mradi huu unasimamiwa na Mamlaka ya *KASHWASA*. Kazi zilizokamilika hadi sasa ni uchimbaji wa mtaro na kulaza bomba kutoka kijiji cha Runere hadi Mjini Ngudu umbali wa **kilomita 24.6**; na ukarabati wa tanki la maji lililopo Ngudu; na **chemba 13** kati ya **75** zimejengwa. Mradi upo katika hatua nzuri ya utekelezaji, ambapo majaribio ya kupeleka maji kutoka Mhalo hadi Runere yamefanyika. Maandalizi ya kazi za majaribio ya kupeleka maji kutoka Runere hadi Ngudu yanaendelea.

### 3.3.5 Mradi wa Maji wa Chalinze

**168. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu iliendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa maji Chalinze, utakaotoa huduma ya majisafi katika vijiji **47** vya mikoa ya Pwani **(42)** na Morogoro **(5)**. Mradi huo unaotekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na *BADEA*, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na Mfuko wa Pamoja wa Sekta ya Maji, utawanufaisha wakazi **197,684** wa Wilaya **tatu** za Bagamoyo, Kibaha na Morogoro. Wizara yangu inaendelea kutekeleza awamu hiyo ya mradi inayotegemewa kukamilika mwezi Septemba, 2014. **Jedwali Na. 11** linaonesha viwango vya utekelezaji wa sehemu mbalimbali za mradi huo.

**169. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Serikali iliingia Mkataba na Mtaalam Mshauri ili kufanya mapitio ya usanifu na kusimamia utekelezaji wa mradi wa Chalinze awamu ya tatu utakaogharimu **Dola za Marekani milioni 49.** Kazi hiyo ilianza mwezi Agosti, 2013 na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2014. Katika mwaka 2014/2015 Serikali itaanza ujenzi wa mradi baada ya kumpata Mkandarasi. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwaka 2016. Kazi zitakazotekelezwa ni ukarabati wa chanzo, kujenga matanki ya kuhifadhia maji katika vijiji 20, kupanua mitandao ya bomba kuu na bomba la usambazaji, kujenga tanki kubwa la kuhifadhi maji katika Mlima Mazizi na kujenga vituo vya kuchotea maji katika maeneo ambayo hayakufikiwa na ujenzi wa awamu za I na II.

### 3.3.6 Miradi katika Jiji la Dar es Salaam

**170. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliendelea kutekeleza miradi mbalimbali iliyopangwa ili kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam. Hadi mwezi Machi, 2014 miradi inayoendelea kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

**(a) Ujenzi wa Bwawa la Kidunda**

**171. Mheshimiwa Spika**, Mtaalam Mshauri aliyepewa kazi ya kutathmini athari za kimazingira na kijamii (*ESIA*) zitakazotokana na ya ujenzi wa barabara kuelekea eneo la ujenzi wa bwawa la Kidunda amewasilisha rasimu ya mwisho ya kazi hiyo tarehe 24 Februari, 2014. Serikali imekamilisha taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa barabara kuelekea kwenye eneo la bwawa na ujenzi unatarajiwa kuanza mara baada ya kukamilika tathmini ya *ESIA* na ulipaji fidia kwa watakaoathirika na mradi.

**172. Mheshimiwa Spika**, upande wa malipo ya fidia, Mthamini wa Serikali amekamilisha mapitio ya uthamini ili kuongeza thamani ya fidia baada ya kuchelewa malipo. Kulingana na Sheria ya Ardhi **Na. 4** ya mwaka 1999, thamani ya fidia imeongezeka kwa **asilimia 8**. Vitabu vipya vimetayarishwa na rasimu ziliwasilishwa tarehe **28/2/2014.** Taratibu za kupata fedha za kulipia fidia hiyo ambayo ni **shilingi bilioni 7.9** zinaendelea. Katika mwaka 2014/2015, Serikali imepanga kutumia kiasi cha **shilingi bilioni 7.0** kwa ajili ya maandalizi na ulipaji wa fidia. Aidha, Wizara inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za ujenzi wa bwawa na hivi sasa yapo mashauriano kati ya Benki ya Uwekezaji ya Afrika Kusini ikishirikiana na Benki ya Rasilimali ya Tanzania, na Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi wa bwawa hilo.

### (b) Visima Virefu vya Kimbiji na Mpera

**173. Mheshimiwa Spika**, mradi wa visima virefu vya Kimbiji na Mpera unahusisha uchimbaji wa visima **20** vya uzalishaji na visima **vinane (8)** vya kubaini mwenendo wa rasilimali za maji chini ya ardhi. Hadi mwezi Machi, 2014 Mtaalam Mshauri wa kusimamia kazi ya uchimbaji wa **visima 20** vya Kimbiji na Mpera ametoa maoni yaliyowasilishwa na Mkandarasi kuhusu uagizaji vifaa vya kuchimbia visima pamoja na mabomba (*casings and screens*) yatakayotumika katika uchimbaji wa visima hivyo. Mkandarasi anaendelea kukamilisha maandalizi ya vitendea kazi na mabomba *(equipment mobilization*) na anategemewa kuanza kazi mwezi Juni, 2014. Uchimbaji wa visima hivyo unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2014.

**174. Mheshimiwa Spika**, mkandarasi wa uchimbaji wa visima virefu **vinane (8)** vya uchunguzi wa mwenendo wa maji chini ya ardhi amekamilisha uchimbaji wa visima **viwili (2)** eneo la Mwasonga na Mkuranga. Majaribio ya uwingi (*output*) wa maji katika visima hivyo na matokeo ya vipimo vya ubora wa maji yameonesha dalili za kuwa na maji mengi yenye ubora unaofaa kwa matumizi ya binadamu. Kwa sasa Mkandarasi anachimba kisima cha tatu eneo la Kibada na amefikia mita **200** kati ya mita **600**. Aidha, Mtaalam Mshauri anayetathmini athari za kimazingira na kijamii (*ESIA*) amewasilisha rasimu ya tatu ya taarifa ya *ESIA* tarehe 24/3/2014 na kupelekwa Benki ya Dunia tarehe 26/03/2014 kwa ajili ya kuridhiwa.

**175. Mheshimiwa Spika**, baada ya ulipaji wa fidia kwenye eneo la **mita 60** kuzunguka kila kisima katika maeneo ya Kimbiji na Mpera kukamilika, Serikali ilikamilisha uhakiki wa fidia katika maeneo ya Luzando na Kisarawe II. Ulipaji wa fidia kwa eneo litakapojengwa tanki la Kisarawe II ulianza tarehe 20/8/2013 na kwa eneo la Luzando tarehe 29/10/2013. Vilevile, uthamini katika maeneo ya ujenzi wa njia za mabomba na barabara kuelekea kwenye visima umeanza, na maombi ya kupata Wathamini kutoka Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali yamewasilishwa. Kwa sasa Mtaalam Mshauri anakamilisha usanifu wa kazi hiyo. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kutekeleza mradi wa kuchimba visima katika eneo la Kimbiji na Mpera.

**(c) Upanuzi wa Mtambo wa Ruvu Juu**

**176. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto ya ukuaji wa kasi wa Miji ya Mlandizi, Kibaha na Jiji la Dar es Salaam, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya India inajenga na kupanua mtambo wa kuzalisha maji Ruvu Juu na ulazaji wa bomba kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara kuanzia tarehe **15/02/2014**.

Mradi huo unatarajiwa kukamilika baada ya miezi 18. Mradi utakapokamilika utagharimu **Dola za Marekani milioni 39.7** kwa ajili ya upanuzi wa mtambo na **Dola za Marekani milioni 59.3** kwa ulazaji wa bomba kuu. Kukamilika kwa upanuzi wa mradi kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita **milioni 82** hadi lita **milioni 196** kwa siku. Aidha, wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya Jiji ambayo miundombinu ya usambazaji maji ilikarabatiwa na haikuwa na maji kwa kipindi kirefu watapata huduma hiyo.

**(d) Upanuzi wa Mradi wa Maji wa Ruvu Chini**

**177. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Serikali kwa kushirikiana na *MCC*, imekamilisha upanuzi wa mradi wa maji wa Ruvu Chini. Kwa sasa Mkandarasi anafanya majaribio ya mitambo. Hadi mwezi Machi 2014, kazi ya ulazaji wa bomba kuu kutoka mitambo ya Ruvu Chini hadi kwenye matanki ya Chuo Kikuu cha Ardhi lenye urefu wa **kilomita 55.93** imekamilika kwa **asilimia 62.87** sawa na **kilomita 35.16**. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2014. Aidha, kazi ya ujenzi wa kingo za Mto Ruvu katika eneo la Kidogozero ulikamilika mwezi Novemba, 2013 na umekabidhiwa kwa *DAWASA*, kwa sasa Mkandarasi yuko kwenye kipindi cha uangalizi (*defects liability period*).

**(e) Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi**

**178. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi kati ya Jiji la Dar es Salaam na Mji wa Bagamoyo

unahusisha kuunganisha wateja kutoka Tegeta hadi Mpiji na Mpiji hadi Bagamoyo. Mradi huo unajumuisha ulazaji wa mabomba ya urefu wa **kilomita 732** ya kusambaza maji yatakayounganisha wateja **24,400** na kujenga magati **30** kati ya Bagamoyo na Tegeta. Mtaalam Mshauri atakayesanifu na kusimamia ujenzi amepatikana.

Kwa sasa Mtaalam Mshauri huyo anaandaa nyaraka za zabuni za ujenzi wa mradi (*pre-qualification document*) na tayari amewasilisha rasimu ya kwanza ya nyaraka za kuwatafuta Wakandarasi watakaoshiriki zabuni. Aidha, kwa mradi wa kuunganisha mabomba ya usambazaji maji ya urefu wa **kilomita 300** kwenye eneo la Mbezi hadi Kiluvya uliendelea kutekelezwa. Jumla ya wateja **10,000** wataunganishwa na magati **30** yatajengwa. Kazi hiyo inahusu miradi ya mabomba madogo madogo na kuunganisha wateja kwenye eneo kati ya Mbezi hadi Kiluvya. Mtaalam Mshauri anaandaa nyaraka za zabuni.

**179. Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kuboresha hali ya huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam ili iwe endelevu, Wizara yangu imefikia makubaliano ya awali na Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*) ili kuwekeza kwenye mradi wa ukarabati na upanuzi wa mfumo wa usambazaji maji katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa sasa Mtaalam Mshauri ameanza kazi ya upembuzi yakinifu na kuandaa makadirio ya gharama za mradi ili zitumike kutayarisha Mkataba wa kifedha. Pamoja na majadiliano yanayoendelea na *TIB*, Kampuni za *AVIC International* na *China Machinery and Engineering Corporation* kutoka nchini China zimeonesha nia ya kufadhili baadhi ya miradi ikiwemo upanuzi wa miundombinu ya majitaka. Wizara yangu inaendelea na taratibu za awali za kufikia mikataba ya kifedha.

### (f) Miradi Mingine ya Kuboresha Huduma ya Maji Jijini Dar es Salaam

**180. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (*BTC*) na Umoja wa Nchi za Ulaya imekamilisha miradi **tisa (9)** kati ya miradi **15** ya kujenga mifumo ya usambazaji maji katika maeneo ya Jiji la Dar es Salaam. Kazi zilizokamilika ni pamoja na kuchimba visima **14**; na kujenga vituo **194** vya kuchotea maji na matanki **15** ya kuhifadhia maji. Miradi **sita (6)** iliyobaki katika maeneo ya Tabata Darajani, Minazi mirefu, Kinyerezi, Mwanamtoti, Yombo Dovya - Msakala na Tandale inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2014 baada ya kuwasha mitambo na kupima msukumo wa maji (*pressure test*). Vilevile, mradi huo umejenga vyoo bora **21** vya mfano katika maeneo ya jumuiya (shule **6** za msingi, zahanati **4**, soko **1** na katika Ofisi za Serikali za Mitaa **10**). Vyoo hivyo vimejengwa kwa lengo la watu kujifunza jinsi ya kujenga vyoo bora katika makazi yao. Pamoja na ujenzi wa vyoo hivyo vipya, mradi umekarabati vyoo vya zamani katika shule **tisa (9)**. Vilevile, mradi umetoa elimu

ya maji, afya na usafi wa mazingira kwa wananchi na wanafunzi wa shule husika katika eneo la mradi. **Jedwali Na. 12** linaonesha utekelezaji wa uchimbaji wa visima katika maeneo mbalimbali ya mradi Jijini Dar es Salaam

**181. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliendelea kutekeleza miradi ya uchimbaji wa visima katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam ili kupunguza kero ya maji wakati wa kusubiri utekelezaji wa Mradi Maalum wa Kuboresha Upatikanaji wa Huduma ya Majisafi na Uondoaji Majitaka katika Jiji la Dar es Salaam. Hadi mwezi Machi 2014, *DAWASA* imechimba visima **44** kati ya **visima 46** vilivyopangwa. Kati ya visima hivyo, visima **21** vimekamilika na kuanza kutumika. Visima **nane (8)** vipo Kimara, katika maeneo ya Mavurunza A, Kilungule A, Kilungule B, King'ongo I, King'ongo II, King'ongo III, Saranga I na Saranga II; Visima **vitano (5)** vipo Keko/Chang'ombe maeneo ya Keko Magurumbasi, Keko Mwanga A, Chang'ombe A, Unubini na Chang'ombe Toroli; na visima **vitatu (3)** vipo Sandali katika maeneo ya Sandali, Mpogo na Mwembe Ladu. Vilevile, visima vingine **viwili (2**) vilivyokamilika vinatumika Mburahati maeneo ya *Mburahati National Housing* na Shule ya Msingi Muungano; na kisima **kimoja kimoja** katika maeneo ya Mwaninga-Kigamboni, Kipunguni na *FFU* yaliyoko Ukonga. Katika mwaka 2014/2015, *DAWASA* itaendelea na kazi ya ufungaji wa pampu ili kukamilisha visima vilivyobaki.

### (g) Mradi wa Maji ya Bomba kwenda Mloganzila

**182. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanza ujenzi wa Kampasi mpya ya Chuo Kikuu cha Udaktari na Sayansi Shirikishi katika eneo la Mloganzila. Ili kurahisisha ujenzi, Wizara yangu inajenga mradi wa Bomba la Maji kwenda eneo la upanuzi. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu imekamilisha usanifu wa mradi, ununuzi wa mabomba na pampu, ukarabati wa tanki la zamani kwenye kituo cha kusukumia maji na ujenzi wa mnara wa tanki jipya litakalopokea maji kutoka kwenye chanzo cha Ruvu Juu. Kazi zote zilikamilika mwezi Oktoba, 2013. Uchimbaji wa mtaro wenye urefu wa **kilomita 1.94** umekamilika ambapo mabomba yenye urefu wa **kilomita 1.0** yamelazwa. Kazi ya kulaza mabomba yenye urefu wa **kilomita 0.94** zilizobaki inaendelea na mradi utakamilika mwezi Juni, 2014.

## 3.3.7 Huduma ya Maji katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa

### (a) Miradi ya Maji katika Miji ya Kibiti na Kibaigwa

**183. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu ilikamilisha ujenzi wa miradi ya maji katika Miji ya Kibiti na Kibaigwa katika mwaka 2013/2014. Mradi wa Kibiti ambao uligharimu **shilingi bilioni 5.3** ulizinduliwa rasmi tarehe 5/10/2013 na **Mhe. Dr.**

**Jakaya Mrisho Kikwete**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi huo unatoa huduma kwa wakazi wapatao **29,931** wa Kata **mbili** za Kibiti na Mtawanya. Aidha, mradi wa Kibaigwa uliogharimu **shilingi bilioni 2.27** ulizinduliwa na **Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Maji tarehe 17/3/2014. Kukamilika kwa mradi huo kumewezesha **asilimia 90** ya wananchi wa Kibaigwa kupata maji safi na salama ukilinganisha na **asilimia 48** kabla ya mradi.

**(b) Miradi ya Maji katika Miji ya Kisarawe, Ikwiriri, Kilosa, Turiani, Mahenge, Mvomero na Gairo**

**184. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza miradi ya maji katika Mji wa Kisarawe, Wizara imekamilisha uchimbaji wa visima **vitano (5)** katika maeneo ya Kwala, Mtunani, Chole-Samvula, Yombo-Lukinga I na Yombo-Lukinga II. Aidha, Wizara imeendelea na ujenzi wa miradi ya maji katika miji midogo ya Ikwiriri, Kilosa, Turiani, Mahenge, Mvomero na Gairo. Hadi mwezi Machi 2014, ujenzi wa miradi ya maji katika miji hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:- Ikwiriri **asilimia 100**, Kilosa **asilimia 80**, Turiani **asilimia 77,** Mahenge **asilimia 77**, Mvomero **asilimia 81** na Gairo **asilimia 86**. Miradi hiyo inatarajiwa kukamilika mwaka 2014/2015.

**(c) Miradi ya Maji Masasi/Nachingwea na Bunda**

**185. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu imekamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji wa Masasi-Nachingwea. Mradi huo umekamilika mwezi Julai, 2013 na unahudumia Miji ya Masasi na Nachingwea pamoja na vijiji vya Likwachu na Chinongwe vilivyopo Wilaya ya Ruangwa na vijiji vya Chiumbati Shuleni na Chiumbati Miembeni vilivyopo Wilaya ya Nachingwea. Kazi ya kuunganisha wateja na ufungaji wa dira za maji inaendelea. Hadi mwezi Machi, 2014 jumla ya wateja **2,972** wameunganishwa kwenye mtandao wa majisafi. Vilevile, huduma kwa wakazi wasio na maji majumbani inatolewa kwenye magati **68** yaliyojengwa maeneo mbalimbali ya Miji ya Masasi na Nachingwea.

**186. Mheshimiwa Spika,** katika Mji wa Bunda, hadi mwezi Machi, 2014 Mkandarasi amekamilisha kazi ya ukarabati wa matanki **mawili (2)** kati ya matanki **matatu (3)** yenye ujazo **wa lita 225,000** kila moja. Vilevile, ujenzi wa Ofisi ya Mtaalam Mshauri na ununuzi wa magari **mawili** umekamilika. Kazi ya ulazaji wa bomba inaendelea na imefikia **asilimia 40**, ambapo **kilomita 9.3** kati ya **kilomita 25.4** zimekamilika. Katika mwaka 2014/2015 ujenzi huo utaendelea na kutumia **shilingi bilioni 3** kukamilisha ulazaji wa bomba na kujenga mfumo wa kusambaza maji katika Mji wa Bunda.

**(d) Mradi wa Maji Orkesumet**

**187. Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Nchi za Kiarabu *(BADEA*) na *OFID* inatarajia kujenga mradi wa majisafi utakaohudumia Mji wa Orkesumet. Katika utekelezaji wa mradi huo, *BADEA* watatoa **Dola za Marekani milioni 8**, *OFID* **Dola za Marekani milioni 8** na Serikali **Dola za Marekani milioni 2.4**.

Mtaalam Mshauri anaendelea na kufanya mapitio (*review*) ya usanifu uliofanywa hapo awali na kutayarisha vitabu vya zabuni kwa ajili ya kumtafuta Mkandarasi wa ujenzi. Hadi mwezi Machi, 2014 Mtaalam Mshauri ameshawasilisha taarifa ya mapitio ya usanifu wa kina (*detail design review*), kwa ajili ya kuhakikiwa. Katika mwaka 2014/2015, ujenzi wa mradi huo utaanza baada ya kumpata Mkandarasi.

**(e) Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi Muheza**

**188. Mheshimiwa Spika,** katika kupunguza kero ya upatikanaji wa majisafi na salama katika Mji wa Muheza, Wizara yangu imetuma **shilingi milioni 350** ili kuboresha miundombinu ya maji ya visima virefu **vitatu (3)** maeneo ya soko la Michungwani, *NHC-tank* na Kwasemwaiko.

Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni ununuzi na ufungaji wa pampu na viungio vyake, ujenzi wa chemba **mbili (2)** na vituo **viwili (2)** vya kuchotea maji, uchimbaji mtaro, ulazaji wa mabomba na ununuzi wa vifaa vya ujenzi na umeme. Ujenzi huo ukikamilika kwenye kisima cha *NHC-tank* kitakuwa na uwezo wa kusukuma maji **lita 2,000** kwa saa (saa 22 kwa siku), kisima cha Kwasemwaiko kikikamilika kitasukuma maji **lita 2,500** kwa saa (saa 22 kwa siku).

**(f) Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi Karatu**

**189. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Serikali ilitekeleza mradi wa maji wa dharura katika Mji wa Karatu unaogharimu **Shilingi milioni 930**. Mradi huo umezinduliwa rasmi tarehe 22/04/2014 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dr. Jakaya Mrisho Kikwete**. Kazi zilizokamilika hadi sasa ni ujenzi wa tanki **moja** lenye **ujazo wa lita 225,000**; ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 2.9**; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa **kilomita 4.4**; ujenzi wa **vituo 12** vya kuchotea maji; ujenzi wa njia kuu ya umeme yenye urefu wa **kilomita 1.2**; na ufungaji wa transfoma na pampu. Kazi hizo zimegharimu **shilingi milioni 609.9** na kuongeza upatikanaji wa maji kwa kiasi cha **lita 720,000** kwa siku na hivyo kufikia **asilimia 34.5** ya mahitaji ya maji kwa Mji wa Karatu. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu imepanga kutumia

**shilingi milioni 250** kuendelea kutekeleza kazi zilizobaki ambazo ni pamoja na:- Ujenzi wa tanki **moja** lenye **ujazo wa lita 225,000**; ulazaji wa mabomba ya usambazaji wa maji yenye urefu wa **kilomita 3.8**; na uchimbaji wa mitaro na ulazaji wa mabomba ya kupeleka maji eneo la G-lambo.

**(g) Miradi ya Maji ya Miji Midogo**

**190. Mheshimiwa Spika,** Serikali imetenga **shilingi bilioni 17.1** kwa ajili ya kukarabati na kupanua miundombinu ya maji katika miji mikuu ya wilaya na miji midogo **46**. Fedha hizo zitatumika kutekeleza miradi inayoendelea na ambayo italeta ahueni kubwa ya maji kwa wakazi wa Miji hiyo. Miradi hiyo imeorodheshwa kwenye **Jedwali Na. 13** linaonesha mchanganuo wa fedha zitakazotumwa kwenye Mamlaka za Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo.

**(h) Mradi wa Maji Longido**

**191. Mheshimiwa Spika,** Mji wa Longido unakadiriwa kuwa na wakazi **21,000** na mifugo ipatayo **13,000**. Mahitaji ya maji kwa sasa ni wastani wa **lita milioni 1.2** kwa siku wakati uzalishaji wa maji kwa siku ni wastani wa **lita 240,000.** Utafiti uliofanyika awali umeonesha kuwa maeneo ya karibu na Mji hayana vyanzo vya maji vinavyoweza kutosheleza mahitaji ya maji kwa Mji huo. Kutokana na hali hiyo, Wizara yangu imefanya utafiti wa kina na kubaini kuwa chanzo pekee ambacho kitatosheleza mahitaji ni Mto Meru. Katika mwaka 2014/2015, Wizara imetenga **shilingi bilioni 3** kutekeleza mradi wa kutoa maji Mto Meru hadi Mji wa Longido ili kutatua tatizo la maji katika Mji huo.

### 3.3.8 Miradi ya Maji ya Kitaifa

**192. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na upungufu wa maji katika Miradi ya Kitaifa na kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma katika maeneo ya miradi hiyo, Wizara yangu ilituma **shilingi milioni 870** kwa ajili ya ununuzi wa pampu, mabomba na ukarabati wa miundombinu ya maji. Mgao wa fedha ulikuwa kama ifuatavyo:-

*Handeni Trunk Main - HTM* **shilingi milioni 50**, Makonde **shilingi milioni 60**, Maswa **shilingi milioni 200**, Mugango-Kiabakari **shilingi milioni 250**, Wanging'ombe **shilingi milioni 50,** Chalinze **shilingi milioni 60,** Masasi-Nachingwea **shilingi milioni 150**, na KASHWASA **shilingi milioni 50**.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu imepanga kutumia jumla ya **shilingi bilioni 11.6** kukarabati miundombinu ya maji katika miradi hiyo ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma iliyo bora na endelevu.

**193. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaajiri Mtaalam Mshauri wa kufanya mapitio ya usanifu na usimamizi wa mradi wa miundombinu ya maji katika Mradi wa Kitaifa Mugango-Kiabakari na vijiji vilivyopo umbali wa **kilomita 12** kando ya bomba kuu.

Mradi huo utatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA)* na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*Saudi Fund for Development - SFD)* kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 30.69**. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa chanzo, ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kusukuma maji, kujenga matanki matatu, kulaza mabomba kutoka Mugango hadi Kiabakari na Butiama urefu wa **kilomita 32**, kukarabati mitambo ya kusukuma maji ya Kiabakari na kulaza mabomba ya mtandao wa usambazaji maji Butiama hadi Bisalye. Kukamilika kwa mradi huo kutanufaisha wananchi wapatao **80,000** katika eneo hilo.

### 3.3.9 Kuzijengea Uwezo Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

**194. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu imeendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini ili ziongeze ufanisi katika utoaji wa huduma kwenye maeneo yao. Ujenzi wa ofisi za Mamlaka za maji za Miji ya Utete na Mpwapwa umekamilika. Ujenzi wa ofisi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Babati unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2014. Katika Mamlaka ya maji Tunduma, ujenzi wa ofisi utakamilika mwezi Novemba, 2014. Aidha, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kuziimarisha mamlaka za maji ngazi ya mikoa, wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa kwa kuzijengea mazingira mazuri zaidi ya kazi ili zitoe huduma bora kwa wananchi.

**195. Mheshimiwa Spika**, ili kuijengea uwezo miradi ya kitaifa na mamlaka za maji za daraja B na C, Wizara yangu imetoa jumla ya **shilingi milioni 435** kwa ajili ya kulipia sehemu ya ankara za umeme wa mitambo ya kuzalisha maji. Katika mwaka 2014/2015 Wizara yangu, itaendelea kuchangia gharama za uendeshaji wa miradi ya kitaifa na Mamlaka za daraja B na C ili hatimaye ziweze kujiendesha zenyewe na hivyo kuipunguzia Serikali mzigo wa kuchangia gharama hizo.

**196. Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuwekeza kwenye miundombinu ya maji na kuzijengea uwezo Mamlaka za maji za ngazi ya wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa ili kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo ya mamlaka hizo.

## 3.4 TAASISI CHINI YA WIZARA YA MAJI

### (a) Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)*

**197. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu imeendelea kuisimamia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*) ili iweze kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Kifungu **Na. 414** cha Sheria **Na.11** ya *EWURA* ya mwaka 2001. Sheria hiyo inaitaka *EWURA* kudhibiti utoaji wa huduma kwenye Sekta za umeme, mafuta ya petroli, gesi asilia, majisafi na majitaka nchini. Kwa mujibu wa sheria hiyo, *EWURA* ina majukumu ya kutoa leseni, kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni, kudhibiti ubora na ufanisi wa utoaji huduma, kutathmini na kupitisha bei za huduma na kutatua migogoro baina ya watoa huduma na wateja wao. Kwa upande wa sekta ya Maji, *EWURA* imeendelea na udhibiti wa huduma za maji zinazotolewa na Mamlaka za Maji **129** nchini. Kati ya Mamlaka hizo, **23** ni za miji mikuu ya mikoa, **96** za miji mikuu ya wilaya na miji midogo, *DAWASA, DAWASCO* na miradi ya maji **minane (8)** ya kitaifa.

**198. Mheshimiwa Spika,** *EWURA* iliendelea kutathmini na kuidhinisha bei za huduma ya maji kwa mamlaka mbalimbali za majisafi na usafi **w**a mazingira nchini. Katika mwaka 2013/2014, *EWURA* iliidhinisha bei mpya *za* huduma za maji kwa mamlaka 23 za maji za Babati, Mo**s**hi, Musoma, Kilwa Masoko, Kahama, Arusha, Bariadi, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, KASHWASA, Kigoma, Lindi, Mbeya, Morogoro, Mpanda, Mtwara, Mwanza, Shinyanga, Singida, Songea, Tabora na Tanga. Mabadiliko ya bei hizo yanatokana na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji hususan gharama ya umeme. Aidha, *EWURA*, ilipokea na kupitia Mipango ya Kibiashara (*Business Plans*) ya miaka mitatu kutoka mamlaka za maji za Miji ya Kisarawe, Songea na Mtwara. Mamlaka zilizobaki zinaendelea kutekeleza mipango yao ya kibiashara.

**199. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, *EWURA* ilitoa taarifa ya utendaji wa Mamlaka za Maji kwa mwaka 2012/13. Taarifa hiyo inaonesha kuwa mamlaka za maji zimepiga hatua katika ufungaji wa dira za maji, kuongezeka kwa idadi ya wateja wa majisafi na majitaka na ukusanyaji wa maduhuli. Aidha, katika mwaka 2013/2014, jumla ya malalamiko **12** yalipokelewa *EWURA*. Malalamiko hayo yalihusu ankara za majisafi na majitaka zilizokosewa, ukosefu wa maji, kukatiwa huduma ya maji kimakosa na huduma hafifu kwa wateja (*poor customer service*). Kati ya malalamiko yaliyowasilishwa, **sita (6)** yamepatiwa ufumbuzi na **sita (6)** yaliyobaki yapo katika hatua mbalimbali za utatuzi.

**200. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014 *EWURA* imeendelea kusimamia Sekta Ndogo za Umeme, Petroli na Gesi Asilia, hususan katika masuala ya kusimamia ubora wa huduma ya umeme, kukagua miundombinu ya umeme, gesi asili na mafuta ili kuhakikisha ubora na usalama wa huduma

hizo. *EWURA* imeendelea kuandaa kanuni na taratibu zinazovutia uwekezaji na kutoa leseni **mbili (2)** kwa wawekezaji wa miradi midogo midogo isiyozidi Megawati **10** (makampuni ya Mapembasi ya Njombe na Bwelui ya Mbeya). Katika Sekta ndogo ya Petroli jumla ya leseni **15** kwa ajili ya wauzaji wa jumla wa mafuta ya petroli zilitolewa. Vilevile, leseni **19** kwa ajili ya wauzaji wa rejareja wa mafuta hayo zilitolewa. Aidha, EWURA imeendelea kukagua miundombinu ya kuchakata, kusafirisha na kusambaza gesi asilia na kubainika kuwa ni salama kwa matumizi na mazingira.

**201. Mheshimiwa Spika,** ili kuimarisha udhibiti wa huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka inayotolewa na mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira nchini, katika mwaka 2014/2015 vipaumbele vifuatavyo vitazingatiwa:-

(i) Kuhimiza uwekezaji kwa mamlaka za maji kwa kuandaa miongozo ya jinsi ya kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma za majisafi na majitaka;

(ii) Kuendelea kufuatilia utendaji wa mamlaka za maji nchini kwa kuchambua na kuhakiki taarifa za utendaji kazi na kukagua miundombinu na utendaji wa mamlaka za maji;

(iii) Kuandaa miongozo ya viwango vya ubora wa huduma zinazotolewa na mamlaka za maji;

(iv) Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa mipango yao ya kibiashara (*Business Plans*) kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa na *EWURA*;

(v) Kuandaa na kutekeleza mipango ya kuhimiza ubora wa huduma wa mamlaka za maji katika miji midogo, miji mikuu ya wilaya na miradi ya kitaifa; na

(vi) Kuandaa na kutekeleza hatua zitakazosaidia kupunguza gharama za kuunganisha huduma za maji kwa wateja.

**202. Mheshimiwa Spika,** EWURA ni mamlaka ya udhibiti wa Sekta kuu mbili za Nishati na Maji. Ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi, nimeiagiza EWURA iendeleze ushirikiano wa karibu na kupokea na kutekeleza miongozo inayotolewa na Wizara zinazosimamia Sekta hizo kulingana na Sheria zilizopo.

### (b) Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji

**203. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu la Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji la kujenga uwezo wa kitaalam wa fani za ufundi zinazohitajika kwenye Sekta ya Maji, Chuo kilidahili wanafunzi **412** wa mwaka

wa kwanza wa Stashahada (*water technicians)* na wanafunzi **69** wa Shahada ya Kwanza ya Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji (*Bachelor of Engineering in Water Resources and Irrigation*). Udahili huo umeongeza idadi ya wanafunzi wote kufikia **1,020** ikilinganishwa na **757** mwaka 2012/2013.

**204. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Novemba 2013, wanafunzi **144** walihitimu mafunzo katika fani za ufundi sanifu wa mifumo ya usambazaji wa majisafi na usafi wa mazingira **(80)**, utafutaji wa maji chini ya ardhi na uchimbaji wa visima vya maji (*Hydrogeology and water well drilling*) **(22)**, haidrolojia na hali ya hewa **(26)** na teknolojia ya maabara ya uchunguzi wa ubora wa maji (*Water Quality Laboratory technology*) wanafunzi **(16)**. Katika jitihada za kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike kujiunga na fani za ufundi, Mamlaka ya Elimu Tanzania (*TEA*) ilifadhili wanafunzi **52** wa kike katika kozi za kuwawezesha kujiunga na masomo ya stashahada. Hii imewezesha kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike kutoka **67** mwaka 2012/2013 hadi **79** katika mwaka 2013/2014.

**205. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Chuo kimeendelea kutoa ushauri juu ya ubora wa maji kwa wateja **136** waliowasilisha sampuli za maji na kupima pamoja na kushauri juu ya upatikanaji wa maji ardhini katika maeneo ya Makambako (Njombe), Ilula (Iringa); Kiwalani, Kibamba na Kigamboni (Dar es Salaam); Gairo (Morogoro); Sikonge (Tabora), Korogwe (Tanga) na Makongo (Pwani). Aidha, washiriki **135** walipewa mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali zinazohusu Sekta ya Maji.

**206. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mazingira ya utoaji wa mafunzo, Chuo kimesaini mikataba ya ununuzi wa vifaa ikiwa ni pamoja na samani na vitendea kazi vya maabara za *hydraulics*, ubora wa maji, usambazaji maji, hali ya hewa, na udongo. Katika kukabiliana na upungufu wa watumishi, Chuo kiliajiri watumishi **wanane (8)** na watumishi **70** walipatiwa mafunzo ya masuala ya ununuzi. Katika mwaka 2014/2015 chuo kitaendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Stashahada (*Water Technician*) kwa wanafunzi **1,056**, sambamba na mafunzo ya ngazi ya Shahada kwa wanafunzi **135**. Mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki **300** yatatolewa. Vilevile, Chuo kitafanya utafiti na kutoa ushauri katika masuala yanayohusu Sekta ya Maji. Ili kukabiliana na upungufu wa ofisi na madarasa, Chuo kitakarabati majengo yaliyopo na kuanza ujenzi wa jengo la ghorofa sita lenye madarasa, maabara, maktaba na kumbi za mikutano.

### (c) Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*DDCA*)

**207. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*DDCA*) uliendelea na uchimbaji wa visima virefu katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi mwezi Machi, 2014 visima virefu **100** vilikamilika na ifikapo mwezi Juni, 2014 visima vingine **150** vinatarajiwa kuchimbwa katika maeneo

mbalimbali nchini. Aidha, uchunguzi wa maji chini ya ardhi kwa ajili ya uchimbaji visima virefu umekamilika katika maeneo **184** na ifikapo mwezi Juni, 2014 maeneo **244** yatachunguzwa. **Jedwali Na. 14** linaloonesha orodha ya visima vilivyochimbwa na *DDCA* katika mwaka 2013/2014.

**208. Mheshimiwa Spika,** Wakala umekamilisha mradi wa ujenzi wa mnara wa kubeba tanki la kuhifadhi maji na ujenzi wa miundombinu ya maji katika ghala la kuhifadhi madawa *MSD*-Kizota (Dodoma).

Vilevile, Wakala unaendelea kutekeleza kazi ya ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji NHC-Kibada (Kigamboni, Dar es Salaam) kazi ambayo imefikia **asilima 90.** Kazi hiyo itakamilika ifikapo mwezi Juni, 2014. Kazi ya upembuzi yakinifu wa miradi ya mabwawa katika maeneo **manne (4)** ya bwawa la *Aviv Estate* Wilayani Songea, bwawa la *Saadani National Park* Wilayani Pangani, bwawa la *Pande Game Reserve* Wilayani Bagamoyo na bwawa la Mfilisi (Mbegesela) Wilayani Kilosa nayo imekamilika. Ujenzi wa bwawa la umwagiliaji la *Aviv Estate* – Lipokera, Songea utakamilika ifikapo mwezi Juni, 2014.

Aidha, ukarabati wa mabwawa **matatu (3)** ya Seke Ididi Wilayani Kishapu, Habiya Wilayani Itilima na Matwiga Wilayani Chunya umeanza.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea na mpango wa kuujengea uwezo Wakala kwa kununua mitambo mbalimbali ya uchimbaji visima na ujenzi wa mabwawa ili kuongeza kasi ya kuchunguza maji chini ya ardhi, uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa nchini.

Wizara imeiagiza Wakala kuandaa mkakati wa kujitegemea *(Exit Strategy*), lengo likiwa ni kuwa na Wakala wenye weledi mkubwa na pia inayojitegemea katika kugharamia shughuli zake zote.

**(d) Bohari Kuu ya Maji**

**209. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake, Bohari Kuu ya Maji inaendelea kununua, kuhifadhi na kusambaza vifaa na madawa ya kusafisha na kutibu maji kwenye Halmashauri mbalimbali, Mamlaka za Maji na Miradi ya Kitaifa. Katika mwaka 2013/2014, vifaa mbalimbali vilisambazwa vikiwemo pampu za maji, mabomba na viungio vyake. Aidha, Bohari Kuu ya Maji imekamilisha ujenzi wa uzio na ukarabati wa ghala la kuhifadhi vifaa vya ujenzi. Wizara yangu katika mwaka 2014/2015, itaendelea kuijengea uwezo Bohari Kuu ya Maji ili iweze kununua vifaa vya ujenzi wa miradi ya maji kwa wingi (*Bulk Purchase*) na kurahisisha upatikanaji wa vifaa hivyo katika Halmashauri, Mamlaka za Maji na Miradi ya Kitaifa ili kwenda sambamba na Mpango wa "Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa". Aidha, nimeiagiza Bohari Kuu ya Maji

kubuni Miradi ya Ubia (*Public Private Partnership-PPP)* ili kupunguza utegemezi wake kwa Serikali.

### 3.5 MASUALA MTAMBUKA

#### (a) Sheria

**210. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kutoa ushauri wa kisheria na elimu kuhusu utekelezaji wa sheria mbalimbali na hatua za kuchukua dhidi ya ukiukwaji wa sheria hizo. Elimu na ushauri umetolewa katika ngazi ya Wizara, Bodi za Maji za Mabonde, Mamlaka za Maji, Halmashauri, Vyombo vya Watumiaji Maji na Wadau wa Sekta ya Maji kupitia mikutano, kongamano, warsha na mafunzo mbalimbali. Jumla ya nakala **478** za Sheria **Na.11** ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Sheria **Na.12** ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira za mwaka 2009 na kanuni zake zimesambazwa. Aidha, mikataba **110** zikiwemo Randama za Makubaliano (*MoU*) zilipitiwa na kutolewa ushauri wa kisheria.

**211. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilikamilisha utayarishaji wa kanuni **saba (7)** za Sheria za Maji ambazo ni:- Usalama wa Mabwawa (*The Water Resources Management (Dam Safety) Regulations, 2013),* iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali **Na. 237** la tarehe 02/08/2013; Usambazaji wa Maji (*The Water Supply Regulations 2013*) na Mfuko wa Taifa wa Uwekezaji wa Maji (*The National Water Investment Fund Regulations 2013*), Gazeti la Serikali **Na. 236** la tarehe 02/08/2013; Usimamizi wa Maji chini ya Ardhi (*The Ground Water (Exploration and Drilling) Licensing Regulations, 2013),* Gazeti la Serikali **Na. 219** la tarehe 02/07/2013; Uunganishaji wa Mamlaka za Maji (*Water Supply and Sanitation (Clustering of Water Authorities) Regulations, 2013)* Gazeti la Serikali **Na 437** la tarehe 06/12/2013; Uteuzi na Sifa za Wajumbe wa Bodi (*EWURA (Appointment and Qualifications of Board Members) Regulations 2013),* Gazeti la Serikali **Na 255** la tarehe 23/8/2013; Uteuzi na Ukomo wa Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Watumiaji **(***EWURA (Appointment and Tenure of Members of the Consumer Consultative Council) Regulations, 2013)* Gazeti la Serikali **Na 256** la tarehe 23/8/2013**;** na Baraza la Ushauri kwa Serikali (*EWURA (Government Consultative Council) Regulations 2013),* Gazeti la Serikali **Na. 254** la tarehe 30/08/2013. Nakala **95** za Kanuni hizo zilisambazwa kwa jamii na pia zinapatikana kupitia tovuti ya Wizara ya Maji (www.maji.go.tz)**.**

**212. Mheshimiwa Spika,** utayarishaji wa rasimu ya kanuni za Bodi ya Leseni (*The Water Supply and Sanitation (Licensing Board) 2014*) umekamilika. Rasimu ya tafsiri za Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji **Na.11** ya mwaka 2009 na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira **Na. 12** ya mwaka 2009 kwa

lugha ya Kiswahili zimekamilika na kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

**213. Mheshimiwa Spika,** ili kukabiliana na changamoto za kisheria katika utekelezaji wa Sheria za Maji, Wizara imetayarisha rasimu za marekebisho (*amendment)* ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji **Na.11** ya mwaka 2009, Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira **Na. 12** ya mwaka 2009 na Sheria ya *DAWASA* Na. 20 ya mwaka 2001. Maoni ya wadau yanaendelea kukusanywa na kufanyiwa kazi. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kisheria kuhusu utekelezaji wa sheria za maji na kuendelea kutayarisha kanuni sita za sheria za maji.

### (b) Mfuko wa Maji

**214. Mheshimiwa Spika**, uanzishwaji wa Mfuko wa Maji (*National Water Investment Fund*) unalenga kuongeza fedha za uwekezaji katika Sekta ya Maji kwa mujibu wa Sheria **Na. 12** ya mwaka 2009 ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira. Katika kufanikisha azma hiyo, Wizara yangu imekamilisha Kanuni za uendeshaji wa Mfuko wa Maji (*National Water Investment Fund Regulations, 2013*) na kuzichapisha kwenye Gazeti la Serikali **Na**. **236** la tarehe 02/08/2013, na zimeanza kutumika. Maandalizi ya kuuwezesha Mfuko kuanza kazi yamekamilika na kwa mwaka 2013/2014 Serikali ilitenga kiasi cha **shilingi milioni 100** kama kianzio (*seed money*) kwa ajili ya Mfuko. Serikali itaendelea kuutunisha Mfuko huo kwa kubaini vyanzo vingine vya mapato ikiwa ni pamoja na ada na tozo mbalimbali.

### (c) Habari, Elimu na Mawasiliano

**215. Mheshimiwa Spika**, elimu na taarifa kuhusu maendeleo ya Sekta ya Maji ni muhimu kwa jamii kama njia mojawapo ya kuelezea masuala ya usimamizi na uendelezaji wa miradi ya maji nchini. Katika mwaka 2013/2014, Wizara iliendelea kutoa elimu kwa wananchi kupitia maonesho, warsha, tovuti na vyombo mbalimbali vya habari. Vilevile, mwezi Agosti 2013, Wizara yangu ilishiriki kikamilifu katika maonesho ya Kilimo ya Nanenane yaliyofanyika Nzuguni Mjini Dodoma ambapo vipeperushi, majarida na machapisho mbalimbali yanayohusu shughuli zinazotekelezwa kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji vilisambazwa kwa jamii. Pia, elimu ya Sera ya Maji kwa lugha nyepesi ilitolewa kwa wananchi kupitia majarida na santuri za maigizo ili kuifahamu mipango na mikakati ya Wizara. Aidha, katika Maadhimisho ya Wiki ya Maji yaliyofanyika kitaifa Mkoani Dodoma mwezi Machi, 2014, Wizara yangu ilitoa jumla ya machapisho **5,000** na vipindi **saba (7)** vya redio na luninga.

**216. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilitoa vipindi maalum kupitia vyombo vya habari kuhusiana na hali ya maji Mkoani Dodoma; mradi wa maji wa kitaifa wa Masasi-Nachingwea; upanuzi wa mradi wa maji wa Ruvu Chini; mradi wa maji wa Kahama-Shinyanga; na kituo cha utafiti cha kuondoa madini ya *fluoride* kwenye maji kilichopo Ngurdoto, Mkoani Arusha. Vipindi hivyo vililenga katika kufafanua na kuelimisha jamii katika masuala mbalimbali ya Sekta ya Maji.

Pia, makala mbalimbali zilitolewa magazetini na kwenye mitandao ya kijamii ya mawasiliano kuelezea kazi mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kuelimisha wananchi na kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu Sekta ya Maji; kuandaa na kutangaza vipindi katika luninga na redio; na kuboresha tovuti ya Wizara ili wananchi wengi zaidi waitumie.

### (d) Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

**217. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu imeendelea kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuboresha utoaji wa huduma na utendaji kazi. Uimarishaji wa matumizi ya TEHAMA ulihusu masuala yafuatayo:-

(i) Kuboresha mfumo wa kielektroniki wa takwimu na taarifa (*Water Sector Management Information system*) ili kusaidia masuala ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango na miradi kwenye Sekta ya Maji (*scaling up/out MIS to cover M&E functions – physical aspects*). Vilevile, mafunzo ya mfumo huo yametolewa kwa watumishi **40** kutoka Makao Makuu ya Wizara, **72** kutoka Halmashauri za Wilaya mpya, **nane (8)** Mikoa mipya, **62** Mamlaka za Majisafi na Majitaka na watumishi **18** wa Bodi za Maji za Mabonde. Matumizi ya mfumo huo yameboresha usimamizi wa fedha za utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji;

(ii) Matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa takwimu na utambuzi wa vituo vya kuchotea maji vijijini (*Water point mapping*) kwa kutumia TEHAMA (www.wpm.maji.go.tz). Hadi mwezi Machi 2014, mafunzo ya mfumo huo yametolewa kwa watumishi **50** kutoka Makao Makuu ya Wizara, Wahandisi wa Maji **155** wa Halmashauri, Wahandisi wa maji **26** kwenye Sekretarieti za Mikoa, Wasajili **163** wa Vyombo vya Watumiaji Maji kwenye Halmashauri na Maafisa Maji wa Mabonde **watatu (3)**;

(iii) Kuendeleza juhudi za Serikali za utekelezaji wa Serikali Mtandao (*e-Government*) kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao (*e-Government Agency*) katika utayarishaji wa mikakati ya kutekeleza '*Open Data.'*

Mikakati hiyo itahusisha kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi katika matumizi ya Serikali Mtandao ili kutoa taarifa mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya maji na matumizi ya fedha kwa uwazi zaidi.

**218. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ukusanyaji na uchambuzi wa kina wa takwimu pamoja na kutathmini hali halisi ya upatikanaji wa maji vijijini.

Tathmini ya hali halisi itafanyika baada ya kukamilisha ukusanyaji wa takwimu na utayarishaji wa ramani za vituo vya kuchotea maji vijijini (*Water Point Mapping*). Aidha, Wizara itaendeleza juhudi za kujenga uwezo wa Halmashauri za Wilaya na Sektretarieti ya Mikoa katika kutumia mfumo huo.

**219. Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na:- kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa takwimu na taarifa ili kusaidia masuala ya ufuatiliaji na tathmini; kutekeleza Mpango wa '*Open Data*' ili kuwezesha utoaji wa takwimu na taarifa za Sekta ya Maji kwa uwazi.

Lengo ni kurahisisha ushiriki wa wananchi na wadau katika kuendeleza Sekta ya Maji nchini kwa kuzingatia maeneo ambayo yataonekana kuwa na mapungufu zaidi ya huduma za maji; kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi katika matumizi ya TEHAMA ili kuboresha huduma ndani ya Sekta ya Maji.

**(e) Jinsia**

**220. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imeendelea kuzingatia umuhimu wa kuwepo kwa uwiano wa kijinsia baina ya wanawake na wanaume katika ngazi za uongozi na maamuzi. Katika mwaka 2013/2014, asilimia ya wanawake katika vyombo vya maamuzi kwenye ngazi ya Wizara na Taasisi zake ni zaidi ya **asilimia 30** kama ifuatavyo:- Wizara **(asilimia 39)**, Bodi ya Taifa ya Maji **(asilimia 33**), Bodi za Mabonde ya Maji (**asilimia 34),** Bodi za Mamlaka za Maji Mijini (**asilimia 31)**, na Bodi za Wakala **(asilimia 50)**. Pia, kwa upande wa vyombo vya watumia maji, suala la ushiriki wa wanawake kwa **asilimia 50** linaendelea kuzingatiwa kulingana na mwongozo uliotolewa na Wizara.

**221. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu imeshirikiana na wadau wa masuala ya jinsia (Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; *TGNP*; na *TaGLA*) kutoa mafunzo kwa watumishi kwa awamu ili kujenga

uwezo wa uongozi katika kusimamia na kutekeleza masuala ya jinsia. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (*GIZ)* inaandaa Mkakati na Mwongozo wa masuala ya jinsia ambao utatumika katika kupanga mipango madhubuti na kubaini changamoto zinazohusu jinsia mahala pa kazi na kuzipatia ufumbuzi. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaandaa benki ya takwimu ya masuala ya jinsia kwa lengo la kuwa na takwimu sahihi za ushiriki unaozingatia jinsia katika mipango, ufuatiliaji na usimamizi wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

**(f) UKIMWI**

**222. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu imetoa elimu kuhusu UKIMWI kwa watumishi **580** wa Wizara. Kati ya hao, watumishi **160** walipata ushauri nasaha na kukubali kupima VVU kwa hiari ili kujua afya zao. Aidha, Dawati la UKIMWI la Wizara lilishiriki katika maonesho ya Wiki ya Maji yaliyofanyika kitaifa Mjini Dodoma kuanzia tarehe 16 - 22/3/2014 kwa kutoa elimu, ushauri nasaha pamoja na upimaji wa hiari kwa jamii. Katika mwaka 2014/2015, kwa kuzingatia maelekezo ya Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania *(TACAIDS)* Wizara yangu itaandaa Mpango wa Ukimwi Mahali pa Kazi *(HIV Plan at Work Place)* kwa kutekeleza yafuatayo:- kutathmini hali ya UKIMWI katika Wizara; kutoa mafunzo elekezi kwa waelimisha rika na watumishi kwa ujumla; kutenga bajeti ya masuala ya ukimwi; kuandaa mpango wa mafunzo utakaoonesha aina ya mafunzo yatakayotolewa; na kuzingatia mahitaji halisi ya watumishi wanaoishi na VVU kama yalivyoainishwa katika sheria ya kazi na mwongozo wa utumishi wa umma. Aidha, Wizara yangu imeendelea kutoa lishe kamili kwa watumishi wake **10** waliojiweka wazi kuwa wanaishi na VVU.

**(g) Maendeleo ya Rasilimali Watu**

**223. Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Aprili 2014, Wizara imepokea watumishi **22** kutoka Sekretarieti ya Ajira. Kati ya hao, Mhasibu Msaidizi **mmoja (1)**, Wahaidrolojia **watatu (3)**, Wakemia **wanne (4)**, Mhudumu wa Afya **mmoja (1)**, Mafundi Sanifu **sita (6)** katika fani ya ujenzi**, wawili (2)** fani ya haidrolojia na **watano (5)** wa fani ya haidrojiolojia. Katika mwaka 2014/2015, Wizara inatarajia kuwapandisha vyeo watumishi **367** na kuwaajiri watumishi wapya **429** wa kada mbalimbali. Aidha, Wizara inaendelea kufuatilia kibali cha ajira mbadala kwa ajili ya kujaza nafasi **28** zilizo wazi za watumishi wa kada mbalimbali waliostaafu, waliofariki au kuacha kazi.

**224. Mheshimiwa Spika,** mwezi Januari, 2014 watumishi **42** walipatiwa mafunzo elekezi kuhusu utumishi wa umma. Vilevile, mwezi Februari na mwezi Aprili 2014, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (*GIZ*) ilitoa

mafunzo kwa viongozi **36** wa Wizara pamoja na Maafisa Watendaji Wakuu wa taasisi zilizo chini yake kwa ajili ya kuimarisha uongozi na utendaji kazi. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kutekeleza mpango wa kuwapatia watumishi mafunzo ya muda mrefu na ya muda mfupi ili kukidhi sifa za miundo ya kada zao na kuongeza ufanisi katika utendaji wa kazi. Mafunzo hayo yatatolewa kwa kuzingatia Mpango wa Mafunzo wa Wizara.

**(h) Mapambano Dhidi ya Rushwa**

**225. Mheshimiwa Spika**, tathmini ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo mbalimbali nchini imeonesha kupungua kwa malalamiko ya kushuka kwa maadili kutokana na vitendo vya rushwa na watumishi wasiokuwa waaminifu kuhujumu miradi na miundombinu ya maji. Mwanzoni mwa mwezi Machi 2014, Wizara yangu kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi ilitoa mafunzo ya maadili kwa viongozi wote wa Wizara na taasisi zake za *EWURA, DAWASA, DAWASCO, DDCA*, Bohari Kuu ya Maji na Chuo cha Maji. Katika mwaka 2014/2015, mafunzo ya aina hiyo yanatarajiwa kutolewa kwa watumishi wengine wa Wizara ili kujenga uelewa wa pamoja.

**(i) Uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji**

**226. Mheshimiwa Spika,** Wizara inatekeleza Sera ya Maji ya Mwaka 2002 ambayo imeweka mfumo madhubuti na endelevu wa kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji nchini. Hii ni pamoja na kuandaa na kutekeleza taratibu za kisheria na kuweka muundo wa kitaasisi wenye uwezo wa kutekeleza Sera. Muundo huo unaohusisha ushirikishwaji wa Wadau wa Sekta ya Maji katika hatua mbalimbali za utekelezaji ikiwa ni pamoja na kubuni, kupanga, kusanifu, kujenga, kusimamia, kuendesha na matengenezo miradi ya maji pamoja na kuchangia gharama za huduma za maji. Sera hiyo inatekelezwa kupitia Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Maji (2006-2015) na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (2006-2025).

**227. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*Water Sector Development Programme – WSDP*) ni ya kipindi cha miaka 18 kuanzia mwaka 2006 hadi 2025. Awamu ya kwanza ya miaka mitano ya utekelezaji wa Programu ilianza mwezi Julai, 2007 na ilipangwa kukamilika mwezi Juni, 2012. Ili kukamilisha miradi iliyopangwa, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo iliamua kuongeza muda wa utekelezaji wa awamu ya kwanza kutoka Juni, 2012 hadi Juni, 2014. Kulingana na Hati ya Makubaliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo, Wizara yangu imeendelea kuandaa taarifa za utekelezaji wa Programu na kuratibu maandalizi ya mikutano ya majadiliano kati ya Serikali, Washirika wa Maendeleo na Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayohusiana na Sekta ya Maji.

**228. Mheshimiwa Spika**, lengo la uratibu wa Programu ni kuhakikisha kuwa Programu ya Maji inatekelezwa kulingana na makubaliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo ikiwemo kuhakikisha kuwa taarifa za utekelezaji na taarifa za matumizi ya fedha zinaandaliwa kwa wakati. Pia, kuhakikisha kuwa ushirikiano wa kiutendaji unakuwepo muda wote wa utekelezaji wa Programu kati ya Wizara ya Maji na OWM-TAMISEMI, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Fedha na Wizara nyingine ambazo ni watumiaji wakubwa wa maji, mfano, Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Kilimo. Aidha, ushirikiano wa kiutendaji kati ya ngazi ya Wizara hizo, Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri, Bodi za Maji za Mabonde, Mamlaka za Maji Mijini na Miradi ya Kitaifa unakuwepo muda wote wa utekelezaji ili kuhakikisha kuwa viwango na kasi ya utekelezaji kwa kuzingatia thamani ya fedha inayotumika vinafanyika kwa ufanisi wa hali ya juu. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kutoa taarifa mbalimbali za utekelezaji wa Programu na kuratibu majadiliano baina ya wadau wa sekta.

### (j) Maandalizi ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Awamu ya Pili

**229. Mheshimiwa Spika,** tathmini ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Programu iliyohusisha wadau wa Sekta ya Maji ilifanyika mwezi Februari hadi Mei, 2013. Tathmini hiyo ilipitia maeneo yote yanayohitaji maboresho kwa ajili ya Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (2014/2015 – 2018/2019). Mapendekezo hayo yalihusu kuimarishwa kwa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; mipango ya ujenzi wa miradi ya maji katika miji mikuu ya wilaya na miji midogo na kuboresha huduma za maji katika miji mikuu ya mikoa; na mipango ya ujenzi wa miradi ya maji vijijini inayohusisha uwekezaji, ukarabati, upanuzi, ujenzi wa miradi mipya na uendeshaji na matengenezo ya miradi katika Halmashauri. Pia, tathmini ilibainisha umuhimu wa kuzijengea uwezo taasisi zinazotekeleza Programu ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo wa kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira kwa kuhusisha maeneo yote ya vijijini na kwenye taasisi za huduma za jamii zikiwemo shule na vituo vya huduma ya afya kwa kushirikiana na sekta nyingine.

**230. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imepokea maoni na ushauri kutoka kwa Wadau kuboresha rasimu ya awamu ya pili ya Programu. Kikosi-kazi kimekamilisha kazi hiyo na kitabu cha awamu ya pili ya Programu kipo tayari kutumika kama mwongozo wa mipango ya utekelezaji na bajeti ya kila mwaka kuanzia 2014/2015 hadi mwaka 2018/2019.

## 3.6 CHANGAMOTO NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA

**231. Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2013/2014, Sekta ya Maji imeendelea kukabiliana na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo na hatua zinazochukuliwa ili kukabiliana nazo ni kama ifuatavyo:-

**(a) Kuongezeka kwa Mahitaji ya Maji Yasiyowiana na Uwekezaji kwenye Miradi ya Sekta ya Maji**

**232. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inakabiliwa na changamoto ya kuongezeka kwa idadi ya watu, hususan mijini. Miji hiyo inakua kwa kasi kubwa sana wakati miundombinu ya kusambaza maji imeendelea kubaki ile ya zamani. Idadi ya watu mijini imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa **asilimia 4.5** ambapo kwa vijijini ni **asilimia 2.3** kwa mwaka. Kwa Jiji la Dar es Salaam idadi ya watu inakua kwa wastani wa **asilimia 5.6** kwa mwaka. Ongezeko hilo la watu linasababisha mahitaji makubwa ya maji yasiyowiana na uwezo wa Serikali kuwekeza kwenye miundombinu ya maji. Aidha, kwa upande wa vijijini upungufu wa huduma ya maji umesababishwa na uwekezaji mdogo wa miundombinu ya maji katika baadhi ya maeneo nchini. Sababu nyingine ni kuharibika kwa miundombinu ya maji pamoja na vituo vya kuchotea maji vilivyojengwa.

**233. Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara yangu imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji kwa kukarabati, kupanua na kujenga miradi mipya mijini na vijijini. Kwa upande wa uboreshaji wa huduma za maji mijini, ujenzi wa miradi ya maji unaendelea katika miji mikuu ya mikoa na wilaya, miji midogo pamoja na miradi ya kitaifa. Katika Jiji la Dar es Salaam upanuzi wa mitambo ya kuzalisha maji ya Ruvu Chini na Ruvu Juu, ujenzi wa bomba kuu kutoka Bagamoyo hadi kwenye matanki ya Chuo Kikuu cha Ardhi, uchimbaji wa visima vya Kimbiji na Mpera na ujenzi wa Bwawa la Kidunda unaendelea. Aidha, kwa upande wa vijijini, Serikali imeendelea kukarabati na kujenga miradi ya kipaumbele ambayo inatoa huduma kwa wananchi wengi zaidi ikiwa ni pamoja na kuendelea kwa ujenzi wa mradi wa maji wa vijiji **10** kila Halmashauri**.**

**234. Mheshimiwa Spika**, uwekezaji kwenye maeneo haya niliyoyaainisha kwa kiasi kikubwa umeathiriwa na uhaba mkubwa wa fedha. Uhaba huu unatokana na kukasimiwa bajeti ndogo ambayo haikidhi mahitaji ya uwekezaji katika miundombinu ya maji. Fedha inayotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji huwa ni kidogo ikilinganishwa na kiasi kinachokasimiwa. Kwa miaka mitatu mfululizo fedha za maendeleo za ndani zilizotolewa kwa Fungu la Wizara ya Maji zilikuwa ni kidogo kulinganisha na fedha zilizokasimiwa.

**235. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2011/2012, fedha zilizokasimiwa zilikuwa ni **shilingi 41,565,045,000** na kiasi kilichotolewa ni **shilingi 24,746,549,522** ambayo ni pungufu kwa **asilimia 40.5**. Kwa mwaka 2012/2013 jumla ya **shilingi 140,015,967,000** zilikasimiwa ambapo fedha zilizotolewa zilikuwa ni **shilingi 104,000,000,000** ambayo ni pungufu kwa **asilimia 25.7**; na kwa mwaka 2013/2014, kiasi cha **shilingi 312,066,164,000** zilikasimiwa na kiasi kilichopatikana hadi mwezi Machi, 2014 ni **shilingi bilioni 86**sawa na upungufu wa asilimia **72.4**. **Jedwali Na. 15** linaonesha mwenendo wa upatikanaji wa fedha za ndani za maendeleo tangu kuanza kwa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

**236. Mheshimiwa Spika**, Serikali hujenga miradi ya maji vijijini na baada ya kukamilika huikabidhi kwa wananchi kwa ajili ya kuiendesha. Uendeshaji na usimamizi wa miradi hiyo umekuwa ni changamoto kubwa kwa maeneo mengi vijijini kutokana na kutokuwa na taaluma na uwezo wa kugharamia matengenezo pindi miradi inapoharibika. Kwa hali hiyo, miradi mingi vijijini imeshindwa kutoa huduma kama ilivyokusudiwa na kupunguza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji safi kwa wananchi. Kukabiliana na changamoto hiyo, Halmashauri zimeelekezwa kuunda na kusajili vyombo vya watumiaji maji kwenye miradi ya maji vijijini ili kuwepo na usimamizi wa karibu katika kuendesha miradi hiyo. Aidha, vyombo hivyo vimejengewa uwezo wa mafunzo kuhusu usimamizi na utunzaji wa fedha zinazotokana na mauzo ya maji; na uendeshaji na matengenezo ya miradi ili kuifanya huduma hiyo kuwa endelevu.

**237. Mheshimiwa Spika**, ongezeko la mahitaji ya huduma ya maji halilingani na upatikanaji wa vifaa na vitendea kazi vya kutekeleza miradi ya maji na hivyo, kusababisha miradi kutokamilika kwa wakati.

Kutokana na hali hiyo, Wizara inajadiliana na Wadau mbalimbali walioonesha nia ya kuwekeza kwenye miradi ya maji na usafi wa mazingira ili kutekeleza miradi hiyo kupitia ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Public Private Partinership - PPP*). Hadi sasa usanifu unaendelea kwa miradi ya *PPP* ikiwemo uvunaji wa maji ya bahari (*desalination project*) kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam na *Handeni Trunk Main - HTM*. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu itaendelea kushawishi wawekezaji wengi zaidi ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira kupitia *PPP*.

**238. Mheshimiwa Spika,** hatua zinazoendelea kuchukuliwa kukabiliana na uhaba wa fedha ni pamoja na Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kutafuta fedha zaidi kutoka Washirika wa Maendeleo, na kuhakikisha kuwa fedha zinazokasimiwa zinatolewa kama zilivyopangwa na kwa wakati. Hadi mwezi Machi 2014, Washirika wa Maendeleo wameahidi kuongeza jumla ya **Dola za Marekani milioni 73** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Sekta ya Maji.

Wizara inaendelea kujadiliana na Washirika wa Maendeleo ili watoe fedha walizoahidi kulingana na makubaliano.

**(b) Kupungua kwa rasilimali za maji**

**239. Mheshimiwa Spika,** upungufu wa rasilimali za maji nchini ni miongoni mwa changamoto zinazoikabili Sekta ya Maji na kusababisha maeneo mengi kukumbwa na uhaba wa maji. Miongoni mwa sababu za upungufu huo ni pamoja na mabadiliko ya tabianchi, uvamizi katika vyanzo vya maji kwa ajili ya shughuli za kiuchumi, uchafuzi wa vyanzo vya maji na matumizi holela ya maji.

**240. Mheshimiwa Spika**, athari za mabadiliko ya tabianchi katika rasilimali za maji ni pamoja na kutotabirika kwa urahisi majira ya mwaka na mtawanyiko wa mvua. Hali hii husababisha mvua kunyesha kwa uchache au wingi na hivyo kusababisha maeneo kuwa kame na wakati mwingine kukumbwa na mafuriko. Matukio yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi yanaathiri vyanzo vya maji pamoja na miundombinu yake.

**241. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Wizara yangu imeendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo kuwekeza katika ujenzi na uendelezaji wa vyanzo vya maji na kuhifadhi maeneo oevu. Hatua hizo zinalenga kuboresha upatikanaji wa maji kwa kipindi chote cha mwaka. Aidha, Wizara yangu imeandaa mipango shirikishi ya uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji kwa Bodi za Maji za Mabonde kama njia mojawapo ya kukabiliana na athari za mabadaliko ya tabianchi. Utekelezaji wa mipango hiyo, unahusisha sekta na wadau mbalimbali nchini katika kupanga na kutumia rasilimali za maji kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**242. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeandaa mpango mkakati wa kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi ili kutekeleza shughuli za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika Sekta ya Maji. Vilevile, kupitia Jukwaa la Majadiliano ya athari za mabadiliko ya tabianchi katika Sekta ya Maji, Wizara yangu imekuwa ikishirikiana na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali pamoja na wadau wa sekta katika utambuzi wa mbinu za kukabiliana na athari hizo kupitia taarifa za shughuli zinazotekelezwa na wadau hao na tafiti mbalimbali zinazofanyika nchini kuhusiana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye Sekta ya Maji. Pia, Serikali inaendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya teknolojia ya uvunaji na uhifadhi wa maji ya mvua katika ngazi ya kaya ili kuongeza upatikanaji wa maji kwa wananchi.

**243. Mheshimiwa Spika**, uvamizi na uchafuzi wa vyanzo vya maji umechangia kwa kiasi kikubwa upungufu katika vyanzo vya maji nchini. Hali hii imechangiwa

na ukosefu wa mipango endelevu ya matumizi bora ya ardhi na hivyo maeneo mengi ya vyanzo vya maji kutumika katika shughuli za uzalishaji mali hususan kilimo. Shughuli hizo zisizozingatia matumizi bora ya ardhi zimesababisha vyanzo vingi kuharibiwa na kuchafuliwa hatimaye kupoteza wingi na ubora wa maji. Vilevile, kumekuwa na matumizi yasiyozingatia vibali vya matumizi vinavyotolewa na mamlaka husika na hivyo kusababisha upungufu wa rasilimali hiyo adimu kwa watumiaji wengine na kusababisha migogoro ya mara kwa mara katika maeneo mbalimbali nchini.

**244. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Serikali imeendelea kuviimarisha vyombo vya kisheria vya usimamizi wa rasilimali za maji ili viweze kusimamia sheria, kanuni na miongozo iliyowekwa. Vyombo hivyo vinaendelea kutekeleza majukumu yao na kuhakikisha rasilimali za maji zilizopo maeneo husika zinagawanywa na kutumiwa kwa mujibu wa sheria. Aidha, maeneo ya vyanzo vya maji yamebainishwa na utaratibu wa kuyawekea mipaka unaendelea ili kulinda maeneo hayo yasiharibiwe na kuchafuliwa na shughuli mbalimbali za binadamu.

### (c) Kiwango Kikubwa cha Upotevu wa Maji

**245. Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa changamoto ambazo Mamlaka za maji katika miji mikuu ya mikoa, wilaya, miji midogo pamoja na miradi ya Kitaifa inazokabiliana nazo ni kiwango kikubwa cha upotevu wa maji (*NRW*). Hali hii inasababisha kutofikiwa kwa malengo ya makusanyo ya maduhuli na hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli za uendeshaji kutokana na uhaba wa fedha. Kwa mamlaka za miji mikuu ya mikoa isipokuwa *DAWASCO*, makadirio ya kiwango cha maji yasiyolipiwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2011/2012 hadi 2013/2014 yanaonesha mamlaka hizo zinapoteza wastani wa zaidi ya **shilingi milioni 30** kwa kila mamlaka kwa mwaka, sawa na **asilimia 34.2** ya upotevu wa maji. Kwa upande wa *DAWASCO***,** wastani wa upotevu wa maji kwa kipindi hicho ni **asilimia 52** ambapo ni sawa na **shilingi bilioni 50.** Upotevu huo wa maji unatokana na sababu zifuatazo:-

### (i) Uchakavu wa Miundombinu

**246. Mheshimiwa Spika,** mamlaka nyingi za maji bado zina miundombinu ambayo ilijengwa miaka mingi iliyopita, hali hiyo imesababisha miundombinu hiyo kuzidiwa uwezo na msukumo mkubwa wa maji yanayotoka kwenye mitambo na kusababisha kuwepo kwa upotevu mkubwa wa maji.

Vilevile, uwekezaji wa miundombinu ya maji katika baadhi ya miradi mipya hususan miradi ambayo uwekezaji wake ulilenga bomba kuu pekee na kuacha miundombinu ya usambazaji. Uwekezaji wa aina hiyo umesababisha mabomba

ya zamani ya usambazaji kushindwa kuhimili msukumo mkubwa wa maji kutoka mradi mpya na kusababisha kupasuka mara kwa mara kwa mabomba hayo. Upasukaji huo umeongeza upotevu mkubwa wa maji. Mfano wa matokeo hayo ya uwekezaji ni kwenye mradi mpya wa Mamlaka ya majisafi na usafi wa mazingira, Iringa ambayo upotevu wake wa maji ulifikia **asilimia 60** baada ya kukamilika kwa mradi.

**247. Mheshimiwa Spika,** Serikali inachukua hatua za kukarabati miundombinu ya maji katika mamlaka mbalimbali na kuhakikisha wakati wa kuanzisha miradi ya uzalishaji maji, usanifu unazingatia mfumo wa mabomba ya usambazaji maji. Vilevile, Wizara imeziagiza mamlaka hizo kuviimarisha vitengo vya matengenezo ili viweze kukarabati mitandao ya maji kwa wakati pindi mivujo inapojitokeza.

**(ii) Wizi wa Maji**

**248. Mheshimiwa Spika,** upotevu wa maji umeendelea kuwa changamoto kubwa kwenye Mamlaka za maji mijini kutokana na baadhi ya wateja wasiokuwa waaminifu kujipatia huduma ya maji kinyume na taratibu (*by-pass, and illegal connection*).

Aidha, udanganyifu wa wateja kuchezea dira za maji ili kubana matumizi ya maji nao umechangia upotevu huo.

**249. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za maji kwa kushirikiana na Manispaa za miji husika zimeweka mikakati ya kufuatilia wizi huo wa maji.

Vilevile, Wizara kwa kuzingatia matakwa ya Sheria **Na. 12** ya mwaka 2009 ya Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira pamoja na Kanuni zake, inazitaka mamlaka hizo kutumia wanasheria wao na vyombo vingine vya usalama kufuatilia wizi wa maji na hujuma kwenye miundombinu ya maji.

Kwa sasa Wanasheria wa Wizara, *DAWASA* na *DAWASCO* wanaendelea na taratibu za kuziboresha sheria hizo ili kuzipa nguvu katika utekelezaji wake. Aidha, Kikosi Kazi cha kufuatilia na kubaini wezi wa maji katika Jiji la Dar es salaam kimeundwa na kinaendelea na kazi hiyo kwa ufanisi. Hadi mwezi Machi 2014, jumla ya **watu 107** walituhumiwa kuwa ni wezi wa maji na wamefikishwa mahakamani na kesi zao ziko kwenye hatua mbalimbali za kisheria.

**(iii) Hujuma kwenye Miundombinu ya Maji**

**250. Mheshimiwa Spika**, miundombinu ya usambazaji wa maji na uondoaji majitaka imeendela kuhujumiwa kutokana na kushamiri kwa biashara ya chuma chakavu. Biashara hiyo imeleta athari kubwa katika maendeleo ya Sekta ya Maji ambapo wahujumu hao wamefikia hatua ya kuharibu mitandao

ya usambazaji majisafi na majitaka kwa kuiba mabomba ya majisafi, mifuniko ya majitaka, pampu, dira na viungio mbalimbali vya mabomba ya maji na hatimaye kuuza vifaa hivyo kama vyuma chakavu. Kutokana na hujuma hizo, kero ya uhaba wa maji kwa wananchi imeongezeka na pia kusababisha uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

**251. Mheshimiwa Spika,** hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kupitia vyombo mbalimbali vya habari juu ya utunzaji wa miundombinu ya maji na kusisitiza ulinzi shirikishi wa miundombinu hiyo. Aidha, Mamlaka zinashirikiana na Sekretarieti za Mikoa, Serikali za Mitaa pamoja na Jeshi la Polisi kudhibiti biashara hiyo ya chuma chakavu. Hatua hiyo imesaidia kukamatwa kwa watuhumiwa na kufikishwa katika vyombo vya Sheria katika Mikoa ya Dodoma, Tabora, Mbeya, Moshi na Dar es Salaam na kesi zao ziko katika hatua mbalimbali za kusikilizwa. Kuanzia mwaka 2010 hadi mwezi Machi, 2014 hasara iliyopatikana kwa Mamlaka za majisafi mijini kutokana na kuibiwa kwa mitandao ya usambazaji maji inakadiriwa kufikia kiasi cha **shilingi bilioni 1.5** ambapo *DAWASA* pekee ni **shilingi milioni 700**.

### (d) Upungufu wa Wataalam katika Sekta ya Maji

**252. Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Maji inakabiliwa na upungufu mkubwa wa wataalam **7,211**, unaotokana na Serikali kutoajiri kwa muda mrefu, kuongezeka kwa idadi ya Mikoa, Wilaya, Halmashauri pamoja na kustaafu kwa baadhi ya watumishi. Idadi ya wataalam wanaohitajika kwenye Sekta ya Maji katika ngazi ya Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri ni **8,749**. Wataalam waliopo kwenye Sekta ya Maji ni **1,538**. Mchanganuo wa mahitaji ya Wataalam wa kada mbalimbali katika Sekta ya Maji umeainishwa katika **Jedwali Na. 16**.

**253. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara yangu iliomba kibali cha ajira Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma mwezi Desemba, 2013. Napenda kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge kwamba mnamo mwezi Machi, 2014 Ofisi hiyo imetoa kibali cha nafasi **475** kwa ajili ya kuajiri Wahandisi wa maji **125** na Mafundi Sanifu **350** ambao watafanya kazi kwenye miradi ya maji iliyopo kwenye Halmashauri. Hatua za kuajiri wataalam hao zinaendelea kufanywa na Wizara yangu kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Ajira.

**254. Mheshimiwa Spika**, usimamizi wa mikataba inayosainiwa na Wakandarasi ni muhimu katika kuhakikisha miradi ya maji inajengwa na kukamilika kwa wakati na kwa kuzingatia viwango vinavyotakiwa. Hata hivyo, kutokana na upungufu wa wataalam katika Sekta ya Maji, usimamizi wa mikataba hiyo umekuwa hafifu na kusababisha miradi mingi kuchelewa na kwa wakati mwingine, kujengwa chini ya viwango na kutumia gharama kubwa. Katika

kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya maji, Wizara imewasilisha maombi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kuajiri kwa mkataba Wataalam wa maji wenye uzoefu kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wataalam wapya watakaoajiriwa. Vilevile, baadhi ya wahandisi wazoefu kutoka Wizarani wamehamishiwa kwenye Sekretarieti za Mikoa ili kuongeza uwezo wa usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maji kwenye Halmashauri mbalimbali nchini.

### (e) Upatikanaji wa Taarifa Sahihi na kwa Wakati kutoka kwa Watekelezaji

**255. Mheshimiwa Spika,** katika kuratibu utekelezaji wa miradi ya maji kumekuwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa taarifa sahihi kutoka kwa watekelezaji wa miradi hiyo hususan Halmashauri. Aidha, taarifa hizo zimekuwa hazifiki kwa wakati na hivyo kuchelewesha maamuzi na utekelezaji wa miradi inayofuata. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imeanza kutumia Mfumo wa Taarifa za Mikataba ya Miradi na Fedha (*Management Information System - MIS*) ambapo mafunzo maalum yametolewa kwa watekelezaji wa miradi ya maji. Serikali pia, inaandaa mfumo wa kompyuta kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za hali ya vituo vya kuchotea maji (*water point mapping system*) utakaounganishwa kwenye Halmashauri zote kwa ajili ya kuweka na kuboresha kumbukumbu.

### (f) Mawasiliano kati ya Wizara na Wadau wa Sekta ya Maji

**256. Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo mawasiliano hafifu baina ya Wizara na wadau wengine wanaotekeleza miradi ya majisafi na usafi wa mazingira tangu kuanza kwa awamu ya kwanza ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Hali hii inasababisha pamoja na mambo mengine, upatikanaji wa taarifa sahihi kuwa mgumu na ucheleweshaji wa utoaji wa maamuzi ya utekelezaji. Mathalan, kwa kipindi kirefu upatikanaji wa taarifa za matumizi ya fedha za utekelezaji wa Programu zimekuwa hazipatikani kwa usahihi na kwa wakati kutokana na kutokuwepo kwa miundombinu ya uhakika ya mawasiliano katika baadhi ya maeneo nchini.

**257. Mheshimiwa Spika,** vilevile, kutokuwepo kwa mawasiliano ya karibu kati ya Sekta ya Maji na Sekta nyingine imesababisha utekelezaji wa miradi ya maji kukwama au kucheleweshwa kwa muda mrefu. Tumeshuhudia utekelezaji wa miradi kama vile ujenzi wa mabomba makuu ya maji kuchelewa kujengwa kutokana na matakwa ya kuomba vibali vya kukatiza katika hifadhi za barabara na zuio za kimahakama. Vilevile, upatikanaji wa vibali au kumalizika kwa kesi za mahakama kunachukua muda mrefu na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya maji kukamilika katika muda uliopangwa. Hali hiyo mara nyingi

inawavunja moyo wananchi kwa kukosa huduma ya maji pamoja na Washirika wetu wa maendeleo wanaochangia miradi ya maji, hivyo kupunguza michango yao ya uwekezaji katika Sekta ya Maji.
**258. Mheshimiwa Spika,** vilevile, kumekuwepo na mawasiliano hafifu na wadau wengine wanaotoa mchango wa kuendeleza utoaji wa huduma ya maji ikiwa ni pamoja na Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Mashirika ya Dini na Watu Binafsi. Upungufu huo umesababisha Wizara kukosa taarifa za miradi ya maji inayotekelezwa na wadau hao ili kujua hali halisi ya huduma ya upatikanaji wa maji kwenye maeneo husika.

**259. Mheshimiwa Spika,** hatua zinazochukuliwa katika kukabiliana na changamoto hiyo ni pamoja na kuimarisha mawasiliano na wadau hao kwa kuwashirikisha katika vikao mbalimbali vinavyojadili masuala ya Sekta ya Maji ili kubadilishana uzoefu na kupanga mikakati ya pamoja kukabiliana na changamoto zilizopo. Aidha, Wizara inaendelea kuboresha Mfumo wa Menejimenti ya Taarifa na Takwimu za Sekta ya Maji. Mfumo huo utarahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati.

## 4.0 SHUKRANI

**260. Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyofikiwa katika kuendeleza Sekta ya Maji yametokana na michango inayoendelea kutolewa na Wadau mbalimbali, hivyo napenda sasa kutumia fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia na kutuwezesha kufanikisha majukumu ya sekta.

Naamini kuwa mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2013/2014 ni kutokana na jitihada za pamoja, ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, ikiwa ni pamoja na nchi wahisani, mashirika ya misaada ya kimataifa, taasisi zisizo za kiserikali, mashirika ya kidini na taasisi za kifedha. Napenda kuzishukuru nchi rafiki zikiwemo Serikali za Ujerumani, Uholanzi, Uingereza, Marekani, Japan, Ufaransa, China, Uswisi, Ubeligiji, Ireland, Korea ya Kusini, Sweden, Denmark, Norway, India na Misri.

**261. Mheshimiwa Spika,** napenda pia, kuzishukuru taasisi za fedha za kimataifa na mashirika ya kimaendeleo kwa misaada ya fedha na ushirikiano wa kitaalam katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu. Taasisi hizo ni pamoja na:-

Benki ya Dunia *(WB)*, Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW),* Benki ya Maendeleo ya Ufaransa (*AFD*)**,** Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya *(EIB)*, Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA)*, Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta *(OPEC Fund for*

*International Development-OFID)*, Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*SFD*), Umoja wa Ulaya (*EU*), Shirika la Marekani la Changamoto za Milenia (*MCC*), Shirika la Misaada ya Maendeleo la Norway *(NORAD),* Taasisi ya Maendeleo ya Uingereza *(DFID),* Shirika la Maendeleo la Ujerumani *(GIZ),* Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo (*UNDP),* Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan *(JICA)*, Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Makazi Duniani *(UN HABITAT)*, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF),* Shirika la Misaada ya Maendeleo la Sweden *(SIDA),* Shirika la Misaada ya Maendeleo la Canada *(CIDA),* Shirika la Misaada ya Maendeleo la Denmark *(DANIDA),* na Shirika la Misaada la Marekani (*USAID).*

**262. Mheshimiwa Spika,** aidha, michango ya mashirika ya kidini imeongeza hamasa katika kuyafikia malengo tuliyojiwekea. Hivyo, napenda kuyashukuru mashirika hayo ya kidini ambayo ni:- *World Islamic League,* Shirika la *Ahmadiya Muslim Jamaat Tanzania, Islamic Foundation,* Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Kanisa la Kilutheri la Ujerumani, Baraza Kuu la Waislam Tanzania, Kanisa Katoliki Tanzania, Kanisa la Kianglikana Tanzania, *Catholic Agency for Overseas Aid and Development (CARITAS)*, *Adventist Development Relief Agency (ADRA), Norwegian Church Aid* na *Livingwater International*.

Pia, nazishukuru taasisi zisizo za kiserikali za *Tanzania Water and Sanitation Network (TAWASANET);* Wahamasishaji wa Maji, Maendeleo na Afya *(WAMMA); Southern Highlands Participatory Organizasition (SHIPO); WaterAid*; *World Vision*; *Plan International*; *Concern Worldwide*; *Netherlands Volunteers Services (SNV);* Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili na Mali Asili (*IUCN*); *World Wide Fund for Nature (WWF*); *African Medical Research Foundation (AMREF); Clinton HIV Aids Initiative (CHAI); Bill and Melinda Gates Foundation;* na wale wote ambao wameendelea kuisaidia Wizara ya Maji kufanikisha malengo yake.

**263. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee kabisa naomba nitumie fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa **Mhe. Amos Gabriel Makalla (Mb)**, Naibu Waziri wa Maji; **Mhandisi Bashir Juma Mrindoko,** Katibu Mkuu; **Mhandisi Mbogo Futakamba,** Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi wote na Wakuu wa Vitengo; Maafisa na Watendaji Wakuu wa Mashirika, Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu; na Wataalam na Watumishi wote kwa ushirikiano wanaonipatia pamoja na kujituma kwao katika kusimamia utekelezaji wa majukumu tuliyopewa.

**264. Mheshimiwa Spika,** Napenda nimshukuru sana **Mhe. Dr. Mhandisi Bilinith Saatano Mahenge (Mb)** na ambaye tulianza kazi hii ya kuwapelekea maji watanzania kwa nguvu mpya. Leo ninayo furaha kumpongeza Dr. Binilith S.

Mahenge (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira). Napenda pia nimshukuru aliyekuwa Katibu Mkuu, **Mhandisi Christopher Nestory Sayi** ambaye amestaafu kwa heshima. Ni matumaini yangu kuwa huko waliko kwa sasa wataendelea kuwa mabalozi wazuri wa Sekta ya Maji.

## 5.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2014/2015

**265. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya **shilingi 520,906,475,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2014/2015**,** ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni **shilingi 30,899,443,000** ambapo **shilingi 15,384,999,000** ni Mishahara ya Watumishi **(PE),** na **shilingi 15,514,444,000** ni fedha za Matumizi Mengineyo **(OC).** Jumla ya Bajeti ya Maendeleo ni **shilingi 490,007,032,000** ambapo kati ya fedha hizo **shilingi 312,066,164,000** ni fedha za ndani na **shilingi 177,940,868,000** ni fedha za nje.

**266. Mheshimiwa Spika,** naomba tena nitoe shukurani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anwani: *www.maji.go.tz*.

**267. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Sasa pamoja na tatizo la muda, lakini nitamwita Mwenyekiti wa Kamati aweze kusoma hotuba yake. Mheshimiwa Profesa Msolla.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa Fedha 2013/2014; na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, maji ni hitaji la msingi la maisha na uhai kwa viumbe vyote. Aidha, shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa umeme na bidhaa za viwandani, matumizi ya majumbani na usafi wa mazingira, zinategemea uwepo wa maji ya kutosha. Katika nchi yetu huduma ya maji bado haijatosheleza mahitaji hayo.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilikutana na Wizara ya Maji tarehe 2 – 3 Mei, 2014 katika Ukumbi wa Mikutano ya Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere ili kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti, utekelezaji wa maoni ya Kamati, changamoto zilizojitokeza kwa mwaka 2013/2014 na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali. Kwa ujumla Kamati haikuridhika na utekelezaji wa miradi mbalimbali. Hali hii imesababishwa na upungufu mkubwa wa fedha pamoja na ucheleweshaji wa fedha kidogo zinazopatikana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara katika kutekeleza majukumu yake, Wizara inakumbana na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa ni kikwazo kikubwa katika kufikia malengo iliyojiwekea. Baadhi ya changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

(a) Kutopatikana fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji;

(b) Kutopatikana fedha kwa wakati imekuwa ni changamoto kubwa na hivyo kuathiri kasi ya utekelezaji wa miradi ya Wizara;

(c) Utaratibu wa kupeleka fedha za maendeleo kutoka Hazina kupitia Benki Kuu hadi kufikia Halmashauri umekuwa na urasimu mkubwa. Utaratibu huu huchukua hadi miezi mitatu kabla ya fedha kuingizwa kwenye akaunti husika wakati zinasomwa kwenye mtandao;

(d) Kuna upungufu mkubwa wa Wataalamu. Kati ya wataalamu 8,749 wanaohitajika katika ngazi ya Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya ni wataalamu 1,538 tu, ndio waliopo;

(e) Kuongezeka kwa idadi ya watu na shughuli za kiuchumi na za kijamii nchini huku baadhi ya miundombinu ya maji ikibaki kuwa ya zamani na chakavu, hivyo kusababisha wananchi wengi kutofikiwa na huduma ya maji;

(f) Kutopatikana kwa takwimu sahihi na taarifa za utekelezaji wa miradi ya maji kwa wakati kutokana na program kushirikisha Taasisi mbalimbali ambazo Wizara ya Maji haina mamlaka ya kiutawala moja kwa moja;

(g) Hujuma mbalimbali kwenye miundombinu ya maji ikiwa ni pamoja na wizi wa mabomba ya maji kwa biashara ya vyuma chakavu, kujiunganishia maji safi na maji taka; na

(h) Mabadiliko ya tabianchi yamesababisha kutotabirika kwa msimu na mtawanyiko wa mvua. Mabadiliko ya tabianchi yamesababisha ukame wa muda mrefu na kukauka kwa vyanzo vya maji kwa baadhi ya maeneo. Maeneo mengine yamekumbwa na mafuriko.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ya Maji chini ya Fungu 49 inaomba jumla ya Sh. 520,906,475,000/=. Kati ya fedha hizo Sh. 490,007,032,000/= ni fedha za maendeleo na Sh. 30,837,043,000/= ni fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za maendeleo, Sh. 312,066,164,000/= ni fedha za ndani na Sh. 177,940,868,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, sasa nielezee maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

(i) Utoaji wa fedha za ndani za nyongeza za miradi ya maji katika mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuwa wakati wa Vikao vya Bunge la Bajeti ya mwaka jana yaani 2013/2014, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, baada ya kujiridhisha kuwa bajeti ya Wizara ya Maji isingekidhi matarajio ya kuboresha huduma za maji hasa vijijini, ilipendekeza na Bunge likapitisha nyongeza ya Shilingi bilioni 184.5 kwenye fungu la Wizara ya Maji.

Kati ya hizo, Shilingi bilioni 173.8 zilipangwa kutekeleza miradi ya maendeleo na Shilingi bilioni 10.7 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengine *(OC)*. Nyongeza ya Shilingi bilioni 173.8 za maendeleo ilifanya Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Maji kwa vyanzo vya ndani kuongezeka kutoka Shilingi bilioni 138.3 iliyokuwa imepangwa awali, hadi Shilingi bilioni 312.1.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitika kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, pamoja na Bunge kupitisha bajeti ya nyongeza ya Shilingi bilioni 173.8 za miradi ya maendeleo, fedha zilizopokelewa na Wizara ni Sh. 46,590,392,417/= sawa na asilimia 27 tu ya fedha zote, hivyo kuwa na upungufu wa Sh.127,209,607,583/=. Aidha, Wizara ilipanga kukamilisha miradi 1,473 lakini hadi sasa miradi iliyokamilika ni 228 tu.

Mheshimiwa Spika, bila ya fedha hizi kutolewa kwa Wizara na kwa wakati, hakuna muujiza utakaotokea wa kufikia malengo ya kufikisha huduma ya maji

kwenye maeneo mbalimbali na hususan maeneo ya vijijini ambako tatizo ni kubwa zaidi. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, Kamati inasisitiza Serikali itoe fedha hizo kama Bunge lilivyoidhinisha ili Wizara iweze kutekeleza malengo yaliyokusudiwa.

(ii) Utoaji wa fedha nyingine za maendeleo kutoka vyanzo vya ndani.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa kabla ya fedha za nyongeza zilizopendekezwa na Kamati Bungeni, Wizara ya Maji ilikuwa imetengewa na Serikali jumla ya Shilingi bilioni 138.3 fedha za maendeleo kutoka vyanzo vya ndani. Kati ya fedha hizo, hadi mwezi Aprili, 2014, ni kiasi cha Sh. 39,409,607,583/= tu kilikuwa kimetolewa, sawa na asilimia 28. Hali hiyo imesababisha uwepo upungufu wa Shilingi bilioni 98.9. Kamati inasisitiza fedha hizi zitolewe ili Wizara itekeleze majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, viwango hivi vidogo vya utoaji fedha za maendeleo kwa Wizara ya Maji ukilinganisha na viwango vilivyoidhinishwa na Bunge, vina athari zifuatazo:-

· Baada ya Bajeti hiyo kuidhinishwa na Bunge, Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yao walitangaza kuhusu neema ya ongezeko hilo na wananchi walipata matumaini makubwa kuwa miradi iliyokuwa haijatekelezwa kwa kipindi kirefu, hatimaye itaanza kutekelezwa kwa kasi kubwa. Kutotolewa kwa fedha hizo kunasababisha wananchi wavunjike moyo na wasiiamini mipango ya Serikali kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji. *(Makofi)*

· Wakandarasi wengi ambao walisaini mikataba ya ujenzi wa miradi ya maji, hasa baada ya kuzinduliwa kwa Mpango wa Serikali wa *Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa*, wamesimamisha utekelezaji kwa sababu ya ukosefu wa fedha, na ipo hatari ya Serikali kupata hasara kutokana na kuongezeka kwa madeni, hususan yanayotokana na kuongezeka kwa riba kwa mujibu wa mikataba yao. Hatua hii itaathiri zaidi bajeti zijazo kwa sababu madeni yatazidi kuongezeka. *(Makofi)*

· Kutotolewa kwa fedha hasa za miradi ya maendeleo kama zilivyokuwa zimeidhinishwa na Bunge, kutasababisha wananchi kutokuwa na imani na viongozi wao; na

· Uhaba wa fedha za matumizi mengine *(OC)* ambazo nazo hazijatolewa kama ilivyotarajiwa, umesababisha Wizara ya Maji iendelee kulimbikiza madeni ya watumishi, madeni ya umeme hasa kwenye mitambo ya kusukuma maji pamoja na kutofuatilia ipasavyo utekelezaji wa Programu ya

Maji ambao ni muhimu sana katika kusimamia viwango vya utekelezaji wa miradi kwa kulinganisha na thamani ya fedha inayotumika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo haya, na hali halisi ya tatizo la maji hasa vijijini, Kamati inashauri Bunge lako Tukufu liazimie kuitaka Serikali, iwe imetoa fedha zote za ndani za miradi ya maendeleo, yaani Shilingi bilioni 226.1 ambazo hazijatolewa hadi sasa. Hii inajumlisha Shilingi bilioni 127.2 kutoka kwenye fedha za nyongeza na Shilingi bilioni 98.9 kutoka kwenye fedha zilizokuwa zimepangwa kabla ya nyongeza ifikapo leo, tarehe 31 Mei, 2014. *(Makofi)*

Aidha, pendekezo la azimio hili, linahusu pia utoaji wa fedha zote za matumizi mengineyo, yaani *(OC)* ambapo Wizara ya Maji haijapewa hadi sasa.

(iii) Utaratibu wa Utoaji Fedha za Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya utaratibu wa sasa wa utoaji wa fedha za maendeleo kutoka Hazina kupitia Benki Kuu kwenda Halmashauri na miradi mingine ili kupunguza urasimu.

(iv) Kutokamilika kwa Miradi Mikubwa ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kuna miradi mikubwa ya maji ambayo imechukua muda mrefu bila ya kukamilika. Miradi kama ya Kimbiji na Mpera, mradi wa Kidunda, mradi wa maji wa Ruvu Juu na Ruvu Chini, ni ya muda mrefu na bado haijakamilika. Kamati inashauri Serikali kuwa miradi mikubwa ambayo imeanzishwa ikamilishwe kabla ya kuanza mingine. *(Makofi)*

(v) Uhaba wa Wataalamu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu mkubwa wa wataalamu katika Sekta ya Maji, Kamati inaishauri Serikali iajiri wataalamu wa kutosha katika ngazi zote. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kupanua udahili wa wanafunzi katika fani ya maji.

(vi) Hujuma za Miundombinu ya Maji.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na ongezeko la hujuma za miundombinu ya maji, Kamati inaishauri Serikali ije na Sheria itakayowadhibiti wahujumu wa miundombinu hiyo. *(Makofi)*

(vii) Kodi za Madawa ya Maji.

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa mara kadhaa imeishauri Serikali kuondoa kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* kwenye madawa ya kutibia maji. Kamati inasisitiza Serikali hii sikivu kufuta kodi hii ya 9.9% na kuwa 0%, yaani iwe *zero rated* ili gharama za maji kwa watumiaji zipungue.

(viii) Uchimbaji wa Visima.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa wananchi wanaochimba visima binafsi hawafikii viwango vya ubora wa maji yanayofaa kwa matumizi ya binadamu. Maeneo mengine maji yana madini ambayo siyo salama kwa matumizi.

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa. Kwa mujibu wa kanuni ya 28, kanuni ndogo ya (5) naongeza muda wa dakika 30. Mheshimiwa Profesa Msola endelea.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa watu wenye visima sehemu mbalimbali mijini na vijijini wanapata leseni ya uchimbaji visima na visima hivyo viwe vinakidhi viwango vya ubora wa maji vinavyotakiwa kwa kufanya ukaguzi wa mara wa mara.

(ix) Vyanzo vya Maji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikalikwa kushirikiana na wananchi kuwe na utaratibu wa kutunza vyanzo vya maji vilivyopo. Aidha, kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo hayatabiriki, utunzaji wa vyanzo vya maji uhusishe wananchi wote wakiongozwa na Halmashauri za Wilaya kwa sababu vyanzo vya maji vinaharibiwa na shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, ufugaji, ukataji miti na uchomaji moto hovyo.

(x) Uvunaji wa Maji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali iendelee kuhimiza na kuhamasisha jamii kwa kutoa elimu ya uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa, malambo na uvunaji wa maji ya paa. Aidha, Serikali ihimize Halmashauri kutunga sheria ndogo ili kutoa elimu ya uvunaji wa maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Maji, Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe na Naibu Waziri Mheshimiwa Amosi Makala, kwa ushirikiano wao mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni na kisheria ya Kamati.

Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Eng. Bashiri Mrindoko na Naibu Katibu Mkuu Eng. Mbogo Futakamba pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Elieka Saanya na Angelina Sanga kwa kuihudumia Kamati vizuri na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji Fungu 49 kwa mwaka wa fedha 2014/2015 yenye jumla ya Sh. 520,906,475,000/=.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Ah, bwana hebu kaa kwanza! Mwongozo wako nataka uwe dakika mbili tu Mheshimiwa Mnyika.

**MHESHIMIWA JOHN J. MNYIKA:** Mheshimwia Spika, nitatumia dakika mbili tu.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa sababu kwa mujibu wa taarifa yako ukurasa wa saba, Kamati inataka Bunge lipitishe Azimio ya

kwamba kabla ya tarehe 31 Mei, Serikali iwe imetoa hizi fedha na tunajua tarehe 31 Mei ni lini. Lakini cha kushangaza, mwishoni Kamati imeunga mkono hoja na inataka Bunge lipitishe haya makadirio.

Mheshimiwa Spika, ningeomba mwongozo wako ili pendekezo hili la Kamati liweze kutekelezwa Serikali itakiwe kutoa kauli kabla ya mjadala huu kuendelea juu ya hoja hii iliyotolewa na Kamati ya kwamba tarehe 31 Mei ambayo ni leo na Mwenyekiti wa Kamati amesema leo, fedha ziwe zimeingizwa ili Upinzani ukizungumza na hata Wajumbe wengine wawe tayari wameshapata jibu iwapo Serikali ipo tayari au la kutekeleza Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2014/2015 – Wizara ya Maji – Kama ilivyowasilishwa Mezani**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA FEDHA 2014/2015**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

**1.2 Mheshimiwa Spika,** maji ni hitaji la msingi la maisha na uhai wa viumbe vyote. Aidha, shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa umeme na bidhaa za viwandani, matumizi ya majumbani na usafi wa mazingira zinategemea uwepo wa maji ya kutosha. Katika nchi yetu huduma ya maji bado haijatosheleza mahitaji hayo.

**1.3 Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilikutana na Wizara ya Maji tarehe 2-3Mei,2014 katika Ukumbi wa mikutano ya Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere ili kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti, utekelezaji wa

maoni ya Kamati, changamoto zilizojitokeza kwa mwaka 2013/2014 na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali. Kwa ujumla Kamati haikuridhikanautekelezaji wa miradi mbalimbali. Hali hii imesababishwa upungufu mkubwa wa fedha pamoja na ucheleweshaji wa fedha kidogo zinazopatikana.

## 3.0 CHANGAMOTO

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara katika kutekeleza majukumu yake, Wizara inakumbana na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa ni kikwazo kikubwa katika kufikia malengo iliyojiwekea. Baadhi ya changamoto hizo ni:-

a) Kutopatikana fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji;

b) Kutopatikana fedha kwa wakati imekuwa ni changamoto kubwana hivyo kuathiri kasi ya utekelezaji wa miradi ya Wizara;

c) Utaratibu wa kupeleka fedha za maendeleo kutoka Hazina kupitia Benki Kuu hadi kufikia Halmashauri umekuwa na urasimu mkubwa, utaratibu huu huchukua hadi miezi mitatu kabla ya fedha kuingizwa kwenye akaunt husika wakati zinasomwa kwenye mtandao;

d) Kuna upungufu mkubwa wa Wataalamu; kati ya wataalamu**8,749**wanaohitajika katikakatika ngazi ya Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya ni wataalamu **1,538** tu waliopo;

e) Kuongezeka kwa idadi ya watu na shughuli za kiuchumi na za kijamii nchini huku baadhi ya miundombinu ya majiikibaki kuwa ya zamani na chakavu hivyo kusababisha wananchi wengi kutofikiwa na huduma ya maji;

f) Kutopatikana kwa takwimu sahihi na taarifa za utekelezaji wa miradi ya maji kwa wakati kutokana na programukushirikisha taasisi mbalimbali ambazo wizara ya maji haina mamlaka ya kiutawala moja kwa moja;

g) Hujuma mbalimbali kwenye miundombinu ya maji ikiwa ni pamoja na wizi wa mabomba ya maji kwa biashara ya vyuma chakavu, kujiunganishia maji safi na maji taka n.k; na

h) Mabadiliko ya tabianchi yamesababisha kutotabirika kwa msimu na mtawanyiko wa mvua. Mabadiliko ya tabianchiyamesababisha ukame wa muda mrefu na kukauka kwa vyanzo vya maji kwa baadhi ya maeneo. Maeneo mengine yamekumbwa na mafuriko.

## 4. 0 MALENGO NA MAOMBI YA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ya Maji chini ya **Fungu 49** inaomba jumla ya**shilingi 520,906,475,000.** Kati ya fedha hizo**shilingi 490,007,032,000/=**ni fedha za maendeleo na **shilingi 30,837,043,000/=** ni fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za maendeleo, **shilingi 312,066,164,000** ni fedha za ndani na **shilingi177, 940,868,000** ni fedha za nje.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

### i) Utoaji wa fedha za ndani za nyongeza za miradi ya maji katika mwaka wa fedha 2013/2014

**Mheshimiwa Spika**, utakumbuka kuwa wakati wa vikao vya Bunge la Bajeti ya mwaka 2013/2014, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, baada ya kujiridhisha kuwa bajeti ya Wizara ya Maji isingekidhi matarajio ya kuboresha huduma za maji hasa vijijini, ilipendekeza na Bunge likapitisha nyongeza ya **Shilingi bilioni 184.5** kwenye fungu la Wizara ya Maji. Kati ya hizo, **Shilingi bilioni 173.8** zilipangwa kutekeleza miradi ya maendeleo na**Shilingi bilioni 10.7** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengine (OC). Nyongeza ya **Shilingi bilioni 173.8** za maendeleo ilifanya Bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Maji kwa vyanzo vya ndani kuongezeka kutoka **Shilingi bilioni 138.3** iliyokuwa imepangwa awali, hadi Shilingi **bilioni 312.1**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasikitika kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, pamoja na Bunge kupitisha bajeti ya nyongeza ya**shilingi 173,800,000,000** za miradi ya maendeleo, fedha zilizopokelewa na Wizara ni **shilingi 46,590,392,417** sawa na **asilimia 27** tu ya fedha zote, hivyo kuwa na upungufu wa **shilingi**

**127,209,607,583**. Aidha, Wizara ilipanga kukamilisha **miradi 1473** lakini hadi sasa miradi iliyokamilika ni**228** tu.

**Mheshimiwa Spika**, bila ya fedha hizi kutolewa kwa Wizara na kwa wakati, hakuna muujiza utakaotokea wa kufikia malengo ya kufikisha huduma ya maji kwenye maeneo mbalimbali na hususan maeneo ya vijijini ambako tatizo ni kubwa zaidi.Kutokana na hali hiyo, Kamati inasisitiza Serikali itoe fedha hizo kama Bunge lilivyoidhinisha ili Wizara iweze kutekeleza malengo yaliyokusudiwa.

**ii) Utoaji wa fedha nyingine za maendeleo kutoka vyanzo vya ndani.**

**Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kuwa kabla ya fedha za nyongeza zilizopendekezwa na Kamati Bungeni, Wizara ya Maji ilikuwa imetengewa na Serikali jumla ya **Shilingi bilioni 138.3** fedha za maendeleo kutoka vyanzo vya ndani. Kati ya fedha hizo, hadi mwezi Aprili 2014, ni kiasi cha **Shilingi 39,409,607,583/=** tu kilikuwa kimetolewa, sawa na **asilimia 28.** Hali hiyo imesababisha uwepo upungufu wa**Shilingi bilioni 98.9**. Kamati inasisitiza fedha hizi zitoleweili Wizara itekeleze majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, viwango hivi vidogo vya utoaji fedha za maendeleo kwa Wizara ya Maji ukilinganisha na viwango vilivyoidhinishwa na Bunge, vina athari zifuatazo:-

· Baada ya Bajeti hiyo kuidhinishwa na Bunge, waheshimiwa wabunge katika maeneo yao walitangaza kuhusu neema ya ongezeko hilo na wananchi walipata matumaini makubwa kuwa miradi iliyokuwa haijatekelezwa kwa kipindi kirefu, hatimaye itaanza kutekelezwa kwa kasi kubwa. Kutotolewa kwa fedha hizo kunasababisha wananchi wavunjike moyo na wasiiamini mipango ya Serikali kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji;

· Wakandarasi wengi ambao walisaini mikataba ya ujenzi wa miradi ya maji, hasa baada ya kuzinduliwa kwa **Mpango wa Serikali wa *Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa*;** wamesimamisha utekelezaji kwa sababu ya ukosefu wa fedha, na ipo hatari ya Serikali kupata hasara kutokana na kuongezeka kwa madeni, hususan yanayotokana na kuongezeka kwa riba kwa mujibu wa mikataba yao. Hatua hii itaathiri zaidi bajeti zijazo kwa sababu madeni yatazidi kuongezeka;

· Kutotolewa kwa fedha hasa za miradi ya maendeleo kama zilivyokuwa zimeidhinishwa na Bunge, kutasababisha wananchi kutokuwa na imani na viongozi wao; na

· Uhaba wa fedha za matumizi mengine (OC) ambazo nazo hazijatolewa kama ilivyotarajiwa, umesababisha Wizara ya Maji iendelee kulimbikiza madeni

ya watumishi, madeni ya umeme hasa kwenye mitambo ya kusukuma maji pamoja na kutofuatilia ipasavyo utekelezaji wa Programu ya Maji ambao ni muhimu sana katika kusimamia viwango vya utekelezaji wa miradi kwa kulinganisha na thamani ya fedha inayotumika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia maelezo haya, na hali halisi ya tatizo la maji hasa vijijini, Kamati inashauri Bunge lako tukufu liazimie kuitaka Serikali, iwe imetoa fedha zote za ndani za miradi ya maendeleo (**Shilingi bilioni 226.1**) ambazo hazijatolewa hadi sasa (**shilingi bilioni 127.2** kutoka kwenye fedha za nyongeza na**Shilingi bilioni 98.9** kutoka kwenye fedhazilizokuwa zimepangwa kabla ya nyongeza) ifikapo **tarehe 31 Mei, 2014**. Aidha, pendekezo la azimio hili, linahusu pia utoaji wa fedha zote za matumizi mengineyo (OC) ambazo Wizara ya Maji haijapewa hadi sasa.

**iii) Utaratibu wa Utoaji Fedha za Maendeleo**

**Mehimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya utaratibu wa sasa wa utoaji wa fedha za maendeleo toka hazina kupitia Benki Kuu kwenda halmashauri na miradi mingine ili kupunguza urasimu.

**v) Kutokamilika kwa Miradi Mikubwaya Maji**

**Mheshimiwa Spika,** kuna miradi mikubwa ya maji ambayo imechukua muda mrefu bila ya kukamilika. Miradi kama ya Kimbiji na Mpera, mradi wa Kidunda, mradi wa maji wa Ruvu Juu na RuvuChini ni ya muda mrefu na bado haijakamilika. Kamati inashauri Serikali kuwamiradi mikubwa ambayo imeanzishwa ikamilishwe kabla ya kuanza mingine.

**vi) Uhaba wa Wataalamu**

Kutokana na upungufu mkubwa wa wataalamu katika sekta ya maji, Kamati inaishauri Serikali iajiri wataalamu wa kutosha katika ngazi zote. Aidha, kamati inaishauri Serikali kupanua udahili wa wanafunzi katika fani ya maji.

**vii) Hujuma za Miundombinu ya Maji**

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na ongezeko la hujuma za miundombinu ya maji, Kamati inaishauri Serikali ije na Sheria itakayowadhibiti wahujumu wa miundombinu hiyo.

**viii) Kodi za Madawa ya Maji**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati kwa mara kadhaa imeishauri Serikali kuondoa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye madawa ya kutibia maji. Kamati inasisitiza Serikali hii sikivu kufuta kodi hiiya 9.9% na kuwa 0% (zero rated) ili gharama za maji kwa watumiaji zipungue.

**ix) Uchimbaji wa Visima**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa wananchi wanaochimba visima binafsi hawafikii viwango vya ubora wa maji yanayofaa kwa matumizi ya binadamu. Maeneo mengine maji yana madini ambayo siyo salama kwa matumizi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa watu wenye visima sehemu mbalimbali mijini na vijijini wanapata leseni ya uchimbaji visima na visima hivyo viwe vinakidhi viwango vya ubora wa maji vinavyotakiwa kwa kufanya ukaguzi wa mara wa mara.

**x) Vyanzo vya Maji**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikalikwa kushirikiana na wananchi kuwe na utaratibu wa kutunza vyanzo vya maji vilivyopo. Aidha, Kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo hayatabiriki, utunzaji wa vyanzo vya majiuhusishe wananchi wote wakiongozwa na Halmashauri za Wilaya kwa sababu vyanzo vya maji vinaharibiwa na shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, ufugaji, ukataji miti na uchomaji moto hovyo.

**xi) Uvunaji wa Maji**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali iendelee kuhimiza na kuhamasisha jamii kwa kutoa elimu ya uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa, malambo na uvunaji wa maji ya paa. Aidha, Serikali ihimize Halmashauri kutunga sheria ndogo ili kutoa elimu ya uvunaji wa maji ya mvua.

## 6. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na kazi nzuri wanayofanya. Wajumbe wa Kamati ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Prof Peter Mahamudu Msolla, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Said Juma Nkumba, Mb Makamu- Mwenyekiti
3. Mhe. Prof. David Homeli Mwakyusa, Mb- Mjumbe
4. Mhe.Subira Khamis Mgalu, Mb “
5. Mhe. Asaa Othman Hamad, Mb “

6. Mhe. Abdulsalaam Seleman Ameir,Mb "
7. Mhe. Abdalla Haji Ali, Mb "
8. Mhe. Namelok Edward Sokoine, Mb "
9. Mhe. Dr. Christine Gabriel Ishengoma, Mb "
10. Mhe. Sylvestry Francis Koka, Mb "
11. Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb "
12. Mhe.Kheri Khatib Ameir, Mb "
13. Mhe. Meshack Jeremia Opulukwa, Mb "
14. Mhe. Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mb "
15. Mhe. Sadifa Juma Khamis, Mb "
16. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb "
17. Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb "
18. Mhe. Donald Kelvin Max, Mb "
19. Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya, Mb "
20. Mhe. Haji Juma Sereweji, Mb "
21. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb "
22. Mhe. Dkt Lucy Sawere Nkya, Mb "
23. Mhe. Dkt. GoodluckJoseph Ole- Medeye "

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Maji, Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe (Mb) na Naibu waziri Mhe. Amosi Makala, (Mb) kwa ushirikiano wao mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni na kisheria ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Eng. Bashiri Mrindoko na Naibu Katibu Mkuu Eng. Mbogo Futakamba pamoja na watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wao.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Elieka Saanya na Angelina Sanga kwa kuihudumia vizuri Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.
**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji **Fungu 49** kwa mwaka wa fedha **2014/2015**yenye jumla ya **shilingi 520,906,475,000.**

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Prof. Peter M. Msolla, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**

**SPIKA:** Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani! Mheshimiwa Sakaya!

**MHESHIMIWA MAGDALENA H. SAKAYA – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya na nguvu ya kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu ili kusoma maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Aidha, kwa heshima kubwa na mshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa imani yake kwangu na kunipa jukumu hili la kuwa Waziri Kivuli na Msemaji Mkuu wa Kambi katika Wizara hii muhimu ambayo ni muhimu sana kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nachukua nafasi hii shukrani kwa uongozi mzima wa Vyama vyetu kwa kuunda ushirikiano wa UKAWA ndani na nje ya Bunge kwa ajili ya maslahi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maji ni rasilimali muhimu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa nchi yoyote. Upatikanaji wa maji safi, salama na ya kutosha una mchango mkubwa katika kuboresha maisha ya jamii husika na kusaidia katika ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, maji ni kiashiria mojawapo katika kufikia Dira ya Maendeleo ya 2025. Aidha Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano, umebainisha maji kama kipaumbele kimojawapo katika kukuza uchumi hasa kwa kuchangia katika uzalishaji wa umeme, kilimo cha umwagiliaji, viwanda na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya 11 kwa kuwa na mito mingi duniani. Ziwa kubwa kuliko yote Afrika liko Tanzania ambalo ni Ziwa Viktoria; Ziwa lenye kina kirefu kuliko yote Afrika liko Tanzania ambalo ni ziwa Tanganyika. Kwa maana hiyo, Tanzania ina inaongoza katika Afrika kwa kuwa na vyanzo vingi vya maji na vya uhakika.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya *SYNOVET* ya mwaka 2009 imeeleza kuwa kero namba moja Tanzania ni maji. Kukosekana kwa maji ya uhakika na salama kwa jamii ya Watanzania walio wengi siyo kwamba inachelewesha maendeleo na kufifisha juhudi za kuondoa umasikini, bali pia inadumaza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Nchi nyingine kama Misri hawana vyanzo vya maji zaidi ya Mto Nile, lakini wananchi wake hawana shida ya maji safi na Salama kama wananchi wa Tanzania. Hii ni aibu kwa nchi ya Tanzania ambayo inatumia mabilioni ya Shilingi katika sherehe ya wiki ya maji kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Tanzania kuwa na rasilimali za maji za kutosha, mgawanyo wa raslimali hizo haupo katika uwiano sawa katika maeneo mengi nchini, hivyo kuwa na uhaba mkubwa wa maji katika maeneo kame. Mahitaji ya maji yanazidi kuongezeka siku hadi siku kutokana na ongezeko la watu nchini, ukuaji wa shughuli za uzalishaji mali katika sekta mbalimbali hususan kilimo cha umwagiliaji, uzalishaji umeme, uzalishaji viwandani, utalii, uchimbaji madini, ufugaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, kama Serikali inashindwa kutoa hata nusu ya bajeti iliyoidhinishwa mwaka jana ambayo Bunge ilishauriwa na wataalamu, ni kwa vipi tunaweza kuondokana na matatizo makubwa ya maji yanayotukabili katika nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza Sera ya Maji ya mwaka 2002 ambayo imeweka mfumo madhubuti na endelevu wa kuendeleza na kusimamia rasilimali za maji nchini. Sera inatelekeza ushirikishwaji wa wadau wa Sekta ya Maji katika hatua mbalimbali za utekelezaji ikiwa ni pamoja na kubuni, kupanga, kujenga, kusimamia, kuendeleza na kuifanyia matengenezo miundombinu ya maji pamoja na kuchangia gharama za huduma za maji.

Mheshimiwa Spika, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2015 inalenga kufikisha huduma ya maji safi na salama kwa wananchi waishio mijini kwa asilimia 100 na asilimia 90 kwa wananchi waishio vijijini ifikapo mwaka 2015.

Aidha, kwa mujibu wa MKUKUTA II 2010/2011 - 2014/2015, Sekta ya maji imepewa jukumu la kuwapatia wananchi maji safi na salama karibu na makazi yao kwa kuongeza idadi ya wananchi waishio mijini wanaopata huduma hiyo kutoka asilimia 57.8 ya mwaka 2009 hadi asilimia 65 ifikapo mwaka 2015. Pia kwa Miji Mikuu kwa mikoa 19 kutoka asilimia 84 ya mwaka 2010 hadi asilimia 95 ifikapo mwaka 2015, na kwa Jiji la Dar es Saalam, Kibaha na Bagamoyo huduma kuongezeka kutoka asilimia 68 ya mwaka 2010 hadi asilimia 75 ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa katika utafiti wa Kitaifa katika eneo la Sekta ya Maji *(National Key Results Area)* inaonyesha kuwa kwa sasa wananchi wanaopata maji safi na salama ni asilimia 40 tu na siyo asilimia 57.8 kama ilivyorekodiwa katika taarifa za MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, kwa utafiti huo mpya unatoa tafsiri kwamba takwimu nyingi ambazo zinatolewa kuna uwezekano mkubwa kuwa haziakisi hali halisi na hivyo kuzidisha tatizo kwani watawala wanazidi kutangaza mafanikio ambayo hayapo. Jambo hili ni baya sana kwani linaendelea kuwanyima wananchi haki zao za kupatiwa huduma. Hivyo basi,

tunaitaka Serikali kufanya marejeo katika takwimu zinazotolewa katika Sekta za Huduma za Jamii na hivyo kupanga kulingana na hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Spika, gharama za maji hapa nchini zimekuwa zikipanda kila leo hivyo kuongeza mzigo na ugumu wa maisha kwa wale wanaopata huduma ya maji hali inayosababisha wengine kushindwa kulipia bili zao na kukatiwa maji.

Kuongezeka kwa gharama hizo kunasababishwa na kodi ya ongezeko la thamani kwenye umeme na madawa. Serikali ina wajibu wa kuhakikisha maji yanayotumiwa na Watanzania wote ni safi na salama ili kulinda afya za wananchi wake. Madawa yanayotumiwa kusafisha na kuuwa wadudu yamekuwa yakiuzwa ghali sana kiasi kwamba Mamlaka za Halmashauri za Miji na Wilaya zinashindwa kununua madawa ya kutosha hivyo kupelekea watumiaji wa maji kutumia maji yasiyo salama.

Mheshimiwa Spika, madawa hayo yameongezeka bei kutokana na ongezeko la Thamani (VAT) kwenye madawa ya kutibu maji.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri kwamba ongezeko la *VAT* liondolewe kabisa kutoka 18% mpaka 0% ili gharama za maji zipungue pia Watanzania wapate maji safi na salama kwa gharama nafuu. Hii pia itapunguza magonjwa mengi yatokanayo na wananchi kutumia maji machafu na hivyo kuokoa gharama za matibabu kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Serikali ilikubali kuiongezea Wizara ya Maji kiasi cha Shilingi bilioni 184.5 na hivyo kuifanya bajeti ya maendeleo kwa Wizara hii kwa fedha za ndani kuongezeka kwa asilimia 122.9, yaani kutoka Shilingi bilioni 140.01 mpaka Shilingi bilioni 312.06.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ni kwamba kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kwa fedha za maendeleo Sekta ya Maji ilitengwa Shilingi bilioni 683.65 ambapo kati ya hizo fedha za ndani zilikuwa Shilingi bilioni 312.06 sawa na asilimia 45.6 ya fedha za maendeleo na Shilingi bilioni 371.6 fedha za nje, sawa na asilimia 54.4

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014 kwa kipindi cha Julai hadi Desemba inaonesha kwamba mbali na fedha zilizotengwa kwa fungu 49, Wizara ya Maji pia ilikuwa na fedha nyingine jumla ya Shilingi bilioni 130.41 zilizotengwa katika mafungu kama inavyoonekana kwenye taarifa yangu.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Serikali inaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Aprili, 2014, ni kiasi cha Shilingi bilioni 46.59 tu kilikuwa kimetolewa, ikilinganishwa na fedha za nyongeza Shilingi bilioni 173.9 zilizokuwa zimeidhinishwa kwa ajiliya miradi ya maendeleo, sawa na asilimia 27 tu. Hali hiyo imesababisha kuwepo na upungufu wa Shilingi bilioni 127.21 kwenye miradi iliyokuwa imepangwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako, kati ya fedha hizo zilizotengwa katika fungu 49 na mafungu mengine kama yalivyotajwa hapo awali, ni kiasi gani cha fedha kilichotolewa kwa ajili ya maendeleo hadi kipindi kilichoishia mwezi Machi, 2014?

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge inayosimamia Wizara hii, baada ya kubaini tofauti kubwa ya kibajeti kwa ajili ya maji Mijini na Vijijini ilipendekeza Serikali itenge bajeti ya maji vijijini ili kupunguza tatizo kubwa la maji linalokabili maeneo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inasema imezingatia ushauri huo kwa kuongeza fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji vijijini.

Kwa mwaka 2013/2014, asilimia 53 zimetengwa kwa ajili ya huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini; 34% ni kwa ajili ya huduma ya maji na usafi wa mazingira mijini; na 9% ni kwa ajili ya utunzaji wa vyanzo vya maji na 4% ni kwa ajili ya kujenga uwezo na kuimarisha Taasisi zinazotekeleza *WSDP*.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ilianza rasmi mwaka 2007 hadi mwaka 2025. Programu hii inatekelezwa kwa awamu nne za miaka mitano kwa kila awamu. Utekelezaji wa awamu ya kwanza ulianza Julai, 2007 na utakamilika mwaka Juni, 2014 baada ya kuongeza miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya Programu hii inakadiriwa kugharimu Dola za Marekani milioni 434. Programu hii inatekelezwa kupitia mfuko wa pamoja *(basket funding)* na kwa kupitia Wahisani wanaofadhili miradi maalum *(earmarked funding)*.

Mheshimiwa Spika, lengo lilikuwa ni kuwapatia wananchi wapatao milioni nane maji safi na salama kwa kujenga vituo 44,900 katika kipindi cha miaka mitano. Fedha zilizotengwa mpaka Mei, 2013 ni Dola za Marekani milioni 340.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa awamu ya kwanza imemalizika na nusu ya awamu ya pili. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wananchi miradi hiyo imefikia wapi? Kwani kwa hali halisi, kuna mwingiliano mkubwa katika matumizi ya fedha za maji na mwisho unakuta mradi mmoja

unatekelezwa na program mbili au tatu jambo ambalo tathmini inakuwa siyo sahihi kwa mradi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa sana la upotevu wa maji hapa nchini kutokana na miundombinu chakavu na wizi wa maji unaofanywa na baadhi ya watu katika maeneo mbalimbali yakiwepo mahoteli, kujiunganishia maji bila kufuata utaratibu. Hali hii imesababisha hasara kubwa kwa Serikali, wakati huo huo wananchi wa maeneo mengine wanakosa maji.

Taarifa zinaonyesha uvujaji na upotevu wa maji kwa mamlaka za maji umeendelea kupungua kutoka asilimia 51 Julai, 2001 hadi kufikia asilimia 36.3 Juni, 2013. Hata hivyo, kiasi hicho bado ni kikubwa sana ukizingatia kwama Watanzania walio wengi hawapati huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* inaonyesha kuwa kuna upotevu mkubwa wa mapato katika Mamlaka za Maji unaotokana na wateja kutokuwa na mita au upotevu wa maji.

Kwa mfano, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bukoba ilipoteza kiasi cha asilimia 56.6 ya mapato yatokanayo na maji wakati Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya walipoteza kiasi cha asilimia 35.16.

Aidha, kulikuwa na upotevu wa fedha wa kiasi cha Shilingi milioni 314 katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Songea. Ukaguzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga, uligundua kuwepo kwa limbikizo la deni la ankara za maji la jumla ya Shilingi milioni 147 ambazo hazikulipwa na Taasisi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ankara nyingi wateja wanagoma kulizilipa kutokana na ukweli kuwa maji hayafiki kwenye nyumba zao lakini maji yanatoka kwenye chanzo na kuishia njiani. Sambamba na hili ni kwamba *DAWASA* iliweza kurekodi maji ambayo yalipotea kwa uwiano wa asilimia 53 ya kiasi cha maji yote yaliyosambazwa ambayo ni asilimia 28 juu zaidi ya kiwango kinachokubalika cha asilimia 25 kilichokadiriwa kufikia fedha za Kitanzania bilioni 8.947. Vile vile mamlaka ilipata hasara ya Shilingi bilioni 17.159 na kufikia tarehe 30 Juni, 2013 madeni ya muda mrefu ya mamlaka yalizidi mali za mamlaka za muda mfupi kwa Shilingi bilioni 19.624.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya upinzani inaitaka Serikali kueleza, kuna mkakati gani endelevu uliyopangwa kufanya marekebisho kwenye miundombinu ya maji kwa muda maalum ili kuokoa maji yanayopotea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na Serikali kutokuwa na mpango mzuri na mikakati makini ya kutunza vyanzo vya maji, vyanzo vingi vimeharibiwa na vingine vimekauka; wakulima kulima mpaka kwenye kingo za maji; mifugo kuchungwa mpaka kwenye vyanzo vya maji; na wananchi kukata miti ya asili kwenye vyanzo vya maji. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ni kwa namna gani inavyoshirikisha wananchi kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji vinavyowazunguka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo cha mikaratusi kwa ajili ya biashara ya mbao imechangia kwa kiasi kikubwa uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji na maji kupungua kwa kiwango kikubwa. Kutokuwepo kwa mpango wa kudhibiti hali hiyo, kunachangia na kuleta hofu na hatari hapo mbeleni kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka ilieleze Bunge kuwa Watumiaji wakubwa wa maji hapa nchini wakiwemo wenye viwanda, mahoteli makubwa na mashirika makubwa kama *TANESCO* na kadhalika, yanashirikishwaje kwenye kulinda vyanzo vya maji?

Ni mkakati gani endelevu wa kuhakikisha maeneo yote yenye vyanzo vya maji yanalindwa? Kwa ujumla Serikali ina idadi ya wataalamu; waliopo ni 1,538 katika ngazi za Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri ni ndogo sana sawa na asilimia 17 tu ukilinganisha na mahitaji ambayo ni 8,749.

Kambi Rasmi ya upinzani inaitaka Serikali kueleza Bunge, upungufu huu mkubwa wa wataalamu unaondolewaje kwa muda mfupi?

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji vijijini uliofadhiliwa na *World Bank* ulileta matumaini makubwa sana kwa Watanzania, wananchi wa vijijini na kuona kuwa utawakomboa kutokana na adha kubwa ya maji wanayoipata. Mradi umekuwa ni kiini toka mwaka 2007 mradi ulipoanza mpaka 2014 hakuna hata Wilaya moja ambayo vijijini vyake vimekamilika.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Mei, 2013, Halmashauri 118 zimeanza ujenzi wa miundombinu ya maji kwenye vijiji 10. Halmashauri 10 zipo katika hatua mbalimbali za kutangaza kupata Wakandarasi wa ujenzi na Halmashauri tatu zimepata wataalam washauri.

Mheshimiwa Spika, jumla ya miundombinu ya miradi ya maji kwenye miradi ya maji kwenye vijiji 535 ipo katika hatua ya ujenzi. Pamoja na wananchi kupokea mradi kwa furaha kubwa na kujinyima sana ili wachangie 5% iliyotakiwa ili mradi uanze, fedha yao mpaka leo haijazaa matunda. Kwa vijiji vingi, fedha zao zimewekwa benki na mpaka leo hawajapata maji na hawajui hatima ya fedha zao.

Mheshimiwa Spika, vijiji vingine vimechimbwa visima, maji yameonekana tangu mwaka 2010 mpaka leo hayajasambazwa kwa wananchi, wameishia kuyaangalia tu. Baadhi ya visima vilivyoonekana kuwa na maji wakati wananchi wanasubiri, Wahandisi wa Wilaya wamefika kwenye visima hivyo na kueleza kwamba wataweka pampu za mikono na siyo kusambazwa kwa wananchi kama ambavyo mradi ulilenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mfano mzuri ni Kijiji cha Ushokora na Kazoroho Wilaya ya Kaliua, walileteWa mpaka mabomba, na baadaye mabomba hayo yamehamishwa kwa maelezo kwamba maji yaliyoko pale hayatoshi kuwasambazia wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo ya kina iweje mradi wa milioni 210, uliofanyiwa utafiti wa kutosha na wataalam, na Wakandarasi kupewa kazi ya uchimbaji na wananchi kuelezwa kwamba maji ni mengi, na sasa wanasubiri kusambaziwa, leo Serikali inakuja na kauli kwamba maji ni kidogo. Huko siyo kuwahadaa wananchi?

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya 2012/2013 Serikali iliahidi Bunge kukamilisha Mradi wa Vijiji kumi kwa kila Wilaya na fedha zilitengwa jumla ya Shilingi bilioni 75.34. Hata hivyo, fedha zilizotolewa kwenye mradi wa vijiji kumi ni Shilingi bilioni 34.3 tu.

Mheshimiwa Spika, hivi kweli Serikali ina nia ya dhati ya kuondoa kero ya maji kwa wananchi wa Tanzania? Utaratibu uliotumika katika mchakato wa mradi wa vijiji 10 ulilenga kuharibu fedha za wananchi walio wengi. Aidha, kwenye Miradi ya Vijiji 10 kuna wizi mkubwa umefanyika na ndiyo maana kwa miaka zaidi ya saba sasa hakuna hata mradi mmoja ambao umekamilika. Wahandisi washauri walioteuliwa na Wizara kwenda kufanya utafiti Vijijini walienda kutafiti maji wakalipwa fedha zote.

Mheshimiwa Spika, Wachimbaji walipokwenda kuchimba maji kwenye vijiji hivyo, zaidi ya asilimia 70 ya maeneo yaliyofanyiwa utafiti hayakuonekana kuwa na maji. Mpaka leo hakuna hatua zozote zilizochukuliwa kwa Wahandisi hawa. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo ya kina toka kwa Serikali; nini hatima ya vijiji vilivyochimbwa visima vya maji na maji hayakuonekana?

Pia Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ichukue hatu za kisheria ikiwemo kuwafikisha Mahakamani kwa kufanya kazi chini ya viwango na kusababisha hasara kwa Taifa na Watanzania wanaendelea kuteseka kwa kukosa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nielezee kuhusu changamoto katika utekelezaji wa miradi. Miradi mingi imekuwa inachukua muda mrefu kutekelezwa na mingine kutotekelezwa kabisa kutokana na mipango mibovu na urasimu uliopo Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kuna mifano halisi, kwa namna miradi mingi inavyochelewa na hivyo wananchi kuendelea kutaaabika kwa kukosa maji, mfano ni mradi wa maji Mkoa wa Tabora; mradi unaotakiwa kutoa maji Ziwa Viktoria kwenda Nzega, Igunga hadi Tabora, tangu mwaka 2010 zilipotolewa fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu, mpaka leo upembuzi yakinifu haujakamilika kwa miaka minne.

Mradi mwingine ni ule wa maji kutoka Ugala kupeleka Wilaya ya Kaliua na Wilaya ya Urambo; Bajeti ya mwaka 2013/2014, Serikali ilitenga fedha Shilingi milioni 450 kwa ajili ya usanifu na upembuzi yakinifu. Kwa mwaka mzima kazi hiyo haikufanyika kwa sababu mshauri mwelekezi hakupatikana.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inauliza, ikiwa usanifu na upembuzi yakinifu unachukua miaka minne haujakamilika: Je, utekelezaji wa mradi utachukua miaka mingapi kukamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kasi ya utekelezaji wa miradi ni ndogo sana! Hii inatokana na miradi kutekelezwa na kusimamiwa na Serikali Kuu kwa kiasi kikubwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Serikali kuweka utaratibu wa kushirikisha mamlaka za maji na Wahandisi wa Mikoa kurahisisha utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, hadi Juni, 2013 hali halisi ya upatikanaji wa maji vijijini, huduma ya maji vijijini ni asilima asilimia 40 tu. Kiasi hiki ni kidogo sana ukizingatia zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanaishi vijijini na hivyo wengi wao hawapati huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuja na mipango mbalimbali ikiwepo miradi ya kimkakati, matokeo ya haraka *(Quick Win Projects)*, Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa *(Big Result Now)*, Serikali hiyo hiyo imeshindwa kutoa fedha za kutekeleza miradi ya maji Vijijini na hivyo wananchi kuendelea kuteseka. Miradi mingi utekelezaji wake unakwenda taratibu sana, miradi inasuasua, hivyo kusababisha hata gharama za miradi hiyo kuendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2013/2014 miradi ya maji na usafi wa mazingira vijijini ilianza kutekelezwa kwa utaratibu wa Tekeleza sasa kwa matokeo makubwa *(Big Result Now)*.

Utaratibu huu ulilenga kuongeza kasi katika utekelezaji wa miradi ili kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi waishio vijijini kutoka asilimia 40 iliyoko sasa mpaka asilimia 74.

Mpango wa *Big Result Now* ulihusisha utekelezaji katika ujenzi wa miradi mipya, ukarabati wa miradi chakavu, upanuzi wa miradi iliyopo na uendeshaji na matengenezo *(Operation and Maintenance)*.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kupata ufafanuzi wa kina, ni miradi mingapi ilifanyiwa ukarabati wa miundombinu chakavu kwa mwaka 2013/2014, na ni maeneo yapi; na ni wapi?

Mheshimiwa Spika, matatizo ya ukosefu wa maji safi na salama yaliyoibuliwa na wananchi katika tafiti shirikishi ya mwaka 2010/2014 maeneo mbalimbali; Kambi Rasmi ya Upinzani kwa miaka mingi imeendeleza Serikali matatizo ya maji yaliyopo katika Mikoa mbalimbali nchini. Hata hivyo, wakati mwingine Wizara ya Maji imebeza taarifa hizo ikitoa majibu yenye kuashiria kutokutambua ukubwa wa matatizo yaliyopo na haja ya kuchukua hatua za haraka. *(Makofi)*

Aidha, hotuba za Kambi Rasmi ya Upinzani zimekuwa zikibezwa kwa vigezo kwamba kazi ya upinzani ni kupinga tu na kwamba Wizara ya Maji inaendelea kutekeleza miradi yenye Matokeo Makubwa Sasa *(Big Results Now)* kwenye kuwezesha wananchi kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kwamba malalamiko juu ya matatizo ya maji tunayoyawasilisha ni kwa niaba ya wananchi na ni kwa maslahi ya nchi. Kwa kuthibitisha hilo, katika hotuba hii, tumeamua kuwaletea ushuhuda wa maelezo na ushahidi wa picha unaotokana na utafiti Shirikishi uliofanywa na Mtandao wa Jinsia Tanzania *(TGNP)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatarajia kwamba Wizara ya Maji haitabeza utafiti huu kama inavyofanya kwa hotuba za Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuzingatia kwamba *TGNP* ni Shirika lisilo la Kiserikali lisilofungamana na Chama chochote cha siasa, lenye shabaha ya kuchochea kujenga kwa usawa na uwiano wa jinsia; kukuza uwezo wa wanawake na makundi mengine yaliyoko pembezoni; kustawisha na kubadilisha mfumo wa Kijamii ambao unamkandamiza mwanamke kwa hali na mali. Wahanga wa matatizo makubwa ya wa maji nchini ni wakina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini kupitia utafiti huu ambao natoa mwito kwa Wabunge wote walioshiriki warsha ya uchambuzi wa bajeti kijinsia *(Gender Budget Analysis)* na Wabunge wote wa Mikoa ambayo utafiti huu umefanyika

ya Mbeya, Shinyanga, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam; mtasimama kidete kuhakikisha Wizara ya Maji inatimiza wajibu wa kuwezesha wananchi kupata huduma hii ya msingi kwa maisha ya binadamu na uchumi wa nchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshiwa Spika, nichukue mifano michache kutoka katika baadhi ya tafiti walizozifanya kati ya mwaka 2010 mpaka mwaka huu 2014 zenye kuonyesha ukubwa wa matatizo ya maji katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, utafiti shirikishi umetoa ushuhuda na ushahidi kwamba katika eneo la Maneromango, Kiluvya Na Visegese, maji ni tatizo gumu sana na sugu. Hivyo, limepewa kipaumbele katika ngazi zote kwa mtu binafsi, familia na hata jamii. Maana hawana uhakika wa kupata maji kwa urahisi licha ya kwamba siyo salama na safi. Maji yanapatikana mbali na kuna milima mikali.

Pamoja hayo, bado siyo hakika sana mtu kupata, hasa wakati wa kiangazi. Wanawake wamekuwa wakiamka usiku wa manane wakati mwingine kulala kwenye foleni za maji, wakati huo njia wanazopita siyo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, nitaomba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard* kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, wamelalamika kuwa shughuli nyingi sana zinakwama kwa ajili ya maji. Maana inabidi wasitishe kwenda kulima kwa wakati, ama kufanya shughuli nyingine wa ajili ya kutafuta maji.
Mheshimiwa Spika kwingine ni Mkambarani (Morogoro), Songwa (Kishapu) na Njombe (Mbeya Vijijini). Katika Kata zote tatu za utafiti Shirikishi, tatizo la maji limejitokeza kwa upana sana. Katika Kata ya Songwe katika baadhi ya maeneo yote ya **Maganzi**, Seseko, Ikonogo, Mpumbula na Masagala hawana huduma ya maji kabisa. Katika Kijiji cha **Magonze** gharama za maji ni kubwa kwa mwananchi wa kawaida, ni kati ya Sh. 500/= na Sh. 1,000/= kwa lita 20 za maji safi. Wanawake hutumia muda mwingi kutafuta maji na kuacha shughuli zao za kujitafutia kipato mfano biashara zao na ufundi cherehani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Njombe inaelezwa kuwa shida ni kubwa mno kwani maji wanayochota ni machafu sana.

Kwa hali hiyo, huwafanya wanafunzi wa kike kuchelewa kwenda shuleni na mara nyingine hutokea ubakaji wanapofuatilia maji. Lakini pia wanapochelewa kurudi hupigwa na waume zao wakihofiwa kuwa walikuwa kwa mahawara zao. Wanafunzi nao hasa wa kike huchelewa kusoma kwa sababu ya kufuatilia maji. Washiriki walisema kuwa kwa jinsi hali ya maji ilivyo

mbaya, wana hofu ya kuchota magonjwa, hata wamama wajawazito wanapokwenda kuchota maji. Kwa hiyo, kuna hofu ya wao kuzalia njiani lakini hawana la kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kisaki (Morogoro), Kishapu na Mbeya Vijijini, Serikali irejee maelezo ya utafiti kwamba, maji ni suala ambalo linagusa nyanja zote za maendeleo ikiwa ni pamoja na afya, uzalishaji katika kilimo, ardhi endelevu, elimu na fursa mbalimbali za elimu kwa wanawake na watoto, amani na utulivu, pamoja na uzalishaji uchumi. Katika mchakato wa uraghbishaji katika Kata zote tatu, suala la ukosefu wa maji safi na salama limejitokeza na limechangia kwa kiasi kikubwa kurudisha nyuma maendeleo na kuwa kikwazo kikubwa kwa wanawake na wasichana. Katika Kata ya Kishapu, suala hili limechukua nafasi kubwa sana. Kwa kiasi kikubwa sehemu hii ni kame na hivyo maji hupatikana kwa wingi kipindi cha mvua na baada ya hapo hufuatiwa na kipindi cha ukame mkali. Kwa hali hiyo sehemu kubwa upatikanaji wa maji ni changamoto kubwa.Wanawake wamekuwa na mzigo mkubwa wa kuamka usiku wa manane na kutembea usiku wa manane wakipita misitu mizito, kupanda vilima na kwa ajili ya kutafuta maji, umbali wa kilometa 8 - 10 kufuata maji. Pamoja na umbali wote huo, vyanzo vya maji vimechafuliwa na uwekezaji wa mashamba, viwanda pamoja na shughuli za kila siku za binadamu na kunywesha wanyama. Kwa upande wa Kisaki tatizo la maji kusababishwa na kuongezeka kwa idadi ya watu katika eneo hili. Hii ni kutokana na shughuli za biashara ya mazao na utalii. Vilevile uanzishwaji wa Shule ya Sekondari ya Kata pia imechangia ongezeko la watu.

Mheshimiwa Spika, changamoto hii ya maji imepelekea matatizo mengi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa matumizi katika familia, kwani pesa nyingi hutumika kununua maji, wanawake na wasichana kubakwa; ubakaji kwa wanawake na wasichana na hivyo kupewa mimba zisizotarajiwa. Pia wanawake kukutana na vipigo kutoka kwa wapenzi wao kwa ajili ya kuchelewa kurudi nyumbani.

Mheshimiwa Spika, uleaji hafifu wa watoto na famiia kwa ujumla kwa kuwa muda mwingi mama hutumia kwenye kusaka maji, ushiriki mdogo katika shughuli za kiuchumi unaosababishwa na kupoteza muda mwingi kufuatilia maji na hivyo umaskini endelevu. Imeathiri hali ya kiuchumi ya akina mama kiuongozi, kipato na fursa za ajira. Matokeo yake ni kwamba, wanawake wengi wameshindwa kushiriki nafasi zao za ajira mfano, kilimo na biashara ndogo ndogo; familia kusambaratika, inaathiri matumizi ya muda kwa wanawake; kiwango cha elimu kushuka; ndoa za mapema na zisizotarajiwa; vile vile kuna masuala ya ujinsi ambapo wanawake hushindwa kufurahia ndoa zao/ngono kwa sababu ya kuamka usiku wa manane kufuata maji lakini pia kukosa maji ya

kuoga kujiandaa kwa ajili ya kufurahia mapenzi na waume zao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mifano ni mingi kuna Nyamaraga (Tarime), Mondo Kishapu, Morogoro na kadhalika. Mifano ni mingi, Waheshimiwa Wabunge watasoma kwenye taarifa yangu. Hali ni mbaya, tunaiomba tena Serikali iangalie tena suala hili.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia wakati wa mvua maji mengi yanapotea ardhini na kuleta maafa na uharibifu wa Miundombinu ya barabara, Reli na hata kuteketeza makazi ya wananchi. Baada ya msimu wa mvua…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ni kengele ya pili.

**MHESHIMIWA MAGDALENA S. SAKAYA- MSEMAJI MKUU KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Afadhali umalize, usije ukatukana bure baadaye. *(Makofi/Kicheko)*

**Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2014/2015, kama ilivyowasilishwa Mezani**

---

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHESHIMIWA MAGDALENA H.SAKAYA (MB) WIZARA YA MAJI KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15**

***(Inatolewa chini ya Kanuni 99(9) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2013)***

1. **UTANGULIZI:**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya na nguvu ya kusimama mbele ya Bunge hili kusoma maoni ya Kambi Rasmi ya

Upinzani. Aidha, kwa heshima kubwa na mshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa imani yake kwangu na kunipa jukumu hili la kuwa Waziri Kivuli na Msemaji Mkuu wa Kambi katika Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu ni shukrani kwa uongozi mzima wa vyama vyetu kwa kuunda ushirikiano wa UKAWA ndani na nje ya Bunge kwa ajili ya maslahi ya watanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Maji ni rasilimali muhimu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa nchi yeyote. Upatikanaji wa maji safi, salama na ya kutosha una mchangi mkubwa katika kuboresha maisha ya jamii husika na kusaidia katika ukuaji wa uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Maji ni kiashiria mojawapo katika kufikia Dira ya Maendeleo ya 2025, aidha Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano, umebainisha maji kama kipaumbele kimojawapo katika kukuza uchumi hasa kwa kuchangia katika uzalishaji wa umeme, kilimo cha umwagiliaji, viwanda na kupunguza umaskini.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni nchi ya kumi na moja kwa kuwa na mito mingi Duniani, ziwa kubwa kuliko yote Afrika liko Tanzania ambalo ni ziwa Viktoria, Ziwa lenye kina kirefu kuliko yote Afrika liko Tanzania ambalo ni ziwa Tanganyika. Kwa maana hiyo, Tanzania ina inaongoza katika Afrika kwa kuwa na vyanzo vingi vya maji na vya uhakika.

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti ya SYNOVET 2009 imeeleza kuwa kero namba moja Tanzania ni maji. Kukosekana kwa maji ya uhakika na salama kwa jamii ya watanzania walio wengi sio kwamba inachelewesha maendeleo na kufifisha juhudi za kuondoa umasikini bali pia inadumaza uchumi wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Nchi nyingine kama Misri hawana vyanzo vya maji zaidi ya Mto Nile, lakini wananchi wake hawana shida ya maji safi na Salama kama wananchi wa Tanzania. Hii ni aibu kwa nchi inayotumia mabilioni ya shilingi katika kusherekea wiki ya maji.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na Tanzania kuwa na rasilimali za maji za kutosha, mgawanyo wa raslimali hizo haupo katika uwiano sawa katika maeneo mengi nchini, hivyo kuwa na uhaba mkubwa wa maji katika maeneo kame. Mahitaji ya maji yanazidi kuongezeka siku hadi siku kutokana na ongezeko la watu nchini, ukuaji wa shughuli za uzalishaji mali katika sekta mbalimbali hususan

kilimo cha umwagiliaji, uzalishaji umeme, uzalishaji viwandani, utalii, uchimbaji madini, ufugaji n.k.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya matokea ya maji kwa maeneo mbalimbali nchini( National key Results Area) inaonyesha kwamba ili kuondokana na matatizo ya maji yanaowakabili watanzania. Tunahitaji kutenga fedha za kutosha kama ifuatavyo:-

i. 2013/14 bilioni 437.3 kati ya hizo shilingi bilioni 195.1 ni fedha za ndani;

ii. 2014/15 bilioni 563.2 kati hizo bilioni 332.0 ziwe fedha za ndani;

iii. 2015/16 bilioni 451.9 kati hizo bilioni 206 ziwe fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, kama Serikali inashindwa kutoa hata nusu ya bajeti inayopitishwa na Bunge ambayo haifikii ile ilishauriwa na wataalamu. Ni kwa vipi tunaweza kuondokana na matatizo makubwa yanayotukabili ya maji?

## 2. MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA YA MAJI

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji ina majukumu yafuatato:

i. Kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa sera, mikakati na Programu ya Maendeleo ya sekta ya maji;
ii. Kutayari na kusimamia sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia sekta ya maji;

iii. Kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji;

iv. Kukusanya na kuchambua,kutafsiri na kuhifadhi takwimu muhimu za sekta ya maji;

v. Kutoa miongozo ya utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira mijini na vijijini;

vi. Kutoa miongozo ya kusimamia matumizi endelevu ya raslimali za maji;

vii. Kutoa mafunzo kwa wataalam wa sekta ya maji katika ngazi na kada mbalimbali za utekelezaji;

viii. Kuendeleza tafiti kuhusu teknolojia zinazotumika katika kutoa huduma ya maji; na

ix. Kuratibu majukumu na kutekeleza ushauri wa Bodi ya Taifa ya Maji.

## 3. MADHUMUNI YA WIZARA KWA MWAKA 2012/13-2014/15

**Mheshimiwa Spika,** Randama inasema wazi kuwa Wizara ya Maji kwa kipindi tajwa ilikuwa na madhumuni yafuatayo**:-**

a) Kuhakikisha raslimali za maji zinasimamiwa na zinatumika kwa njia endelevu na shirikishi na utunzaji wa mazingira kwa manufaa ya kijamii na kiuchumi;

b) Kuhakikisha makundi ya jamii vijijini,mijini na pembezoni mwa miji yanapata huduma ya maji safi na usafi wa mazingira;

c) Kusimamia kazi,uwajibikaji na kudhibiti mianya ya rushwa; n.k

**Mheshimiwa Spika,** Wizara inatekeleza Sera ya Maji ya mwaka 2002 ambayo imeweka mfumo madhubuti na endelevu wa kuendeleza na kusimamia rasilimali za maji nchini. Sera inaelekeza ushirikishwaji wa wadau wa sekta ya maji katika hatua mbalimbali za utekelezaji ikiwa ni pamoja na kubuni, kupanga, kujenga, kusimamia, kuendesha na kuifanyia matengenezo miundombinu ya maji pamoja na kuchangia gharama za huduma za maji.

**Mheshimiwa Spika,** Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2015 inalenga kufikisha huduma ya maji safi na salama kwa wananchi waishio mijini kwa asilimia 100 na asilimia 90 kwa wananchi waishio vijijini ifikapo mwaka 2015. Aidha kwa mujibu wa MKUKUTA II 2010/2011-2014/2015, Sekta ya maji imepewa jukumu la kuwaptia wananchi maji safi na salama karibu na makazi yao kwa kuongeza idadi ya wananchi waishio vijijini wanaopata huduma hiyo kutoka asilimia 57.8 ya mwaka 2009 hadi asilimia 65 ifikapo mwaka 2015. Pia kwa miji mikuu kwa mikoa 19 kutoka asilimia 84 ya mwaka 2010 hadi asilimia 95 ifikapo mwaka 2015, na kwa Jiji la Dar, Kibaha na Bagamoyo huduma kuongezeka kutoka asilimia 68 ya mwaka 2010 hadi asilimia 75 ifikapo mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa katika utafiti wa Kitaifa katika eneo la sekta ya maji (National Key Results Area) inaonyesha kuwa kwa sasa wananchi wanaopata maji safi na salama ni asilimia 40 tu na sio asilimia 57.8 kama ilivyorekodiwa katika taarifa ya MKUKUTA.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani, kwa utafiti huo mpya unatoa tafsiri kwamba takwimu nyingi ambazo zinatolewa kuna uwezekano mkubwa kuwa

haziakisi hali halisi na hivyo kuzidisha tatizo kwani watawala wanazidi kutangaza mafanikioa ambayo hayapo.

Jambo hili ni baya sana kwani linaendelea kuwanyima wananchi haki zao za kupatiwa huduma. Hivyo basi, tunaitaka Serikali kufanya marejeo katika takwimu zinazo au zilizotolewa katika sekta za huduma za jamii na hivyo tupange kulingana na hali halisi ilivyo.

**4. GHARAMA ZA MAJI NA UBORA WA MAJI**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ina wajibu wa kuhakikisha maji yanayotumiwa na wanzania wote ni safi na salama ili kulind afya za wananchi wake. Madawa yanayotumiwa kusafisha na kuuwa wadudu yamekuwa yakiuzwa ghali sana kiasi kwama Mamlaka za Wilaya zinashindwa kununua madawa ya kutosha hivyo kupelekea watumiaji wa maji kutumia maji yasiyo salama.

**Mheshimiwa Spika,** Madawa hayo yameongezeka bei kutokana na ongezeko la Thamani (VAT) kwenye madawa ya kutibia maji. Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali iondoe kabisa VAT (Ongezeko la Thamani) kutoka 18% hadi 0% ili gharama za maji zipungue pia watanzania wapate maji yaliyo safi na salama kwa gharama nafuu.

**5. PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA MAJI**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha kuwa raslimali maji inatunza, inaendelezwa na inawafikiwa wananchi wote, Serikali ilianzisha Programu ya Kuendelea sekta ya maji mwaka 2006 hadi 2025. Awamu ya kanza inatarajiwa kukamilika mwezi Juni mwaka 2014. Aidha Programu hiyo inatekelezwa kupitia Programu ndogo 4:

a) Programu ya usimamizi na uendelezaji wa raslimali za maji kwa mabonde 9 ya maji nchini;

b) Programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini- Iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI;

c) Programu ya maji safi na usafi wa mazingira mijini- Iko chini ya Wizara ya Maji katika mamlaka za maji za miji mikuu ya mikoa,miji mikuu ya wilaya, miji midogo na katika miradi ya maji ya kitaifa;

d) Programu ya kuzijengea uwezo na kuimarisha Taasisi zinazosimamia na kuratibu Progamu za Maji.

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Programu hiyo kwa awamu ya kwanza ulihitaji kiasi cha dola za Marekeni milioni 1,691.8, kati ya hizo Serikali ilitakiwa kuchangia dola za Marekani milioni 540.2 na wahisani waliahidi kuchangia kiasi cha dola za Marekani milioni 1,151.0. Hadi mwezi Machi, 2014 kiasi cha Dola za Marekani milioni 1,156.8 zilikwishatolewa, kati ya fedha hizo Serikali ilitoa dola milioni 255.7 na wahisani wametoa dola milioni 901.1, hivyo wahisani hawajatimiza ahadi ya dola milioni 250.5.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kufanikisha program hii Serikali bado inadaiwa kiasi cha Dola za Marekani milioni 284.5. Hoja ni Je, zinalipwa lini kwani mwisho wa utekelezaji wa Programu hii ni mwezi wa Sita Mwaka huu?

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2013/14 Serikali ilikubali kuiongezea Wizara ya Maji kiasi cha shilingi bilioni 184.5 na hivyo kuifanya bajeti ya maendeleo kwa wizara hii kwa fedha za ndani kuongezeka kwa asilimia 122.9 yaani kutoka shilingi bilioni 140.01 mwaka 2013/13 hadi shilingi bilioni 312.06 kwa mwaka 2013/14.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla ni kwamba kwa mwaka wa fedha 2013/14 kwa fedha za maendeleo sekta ya maji zilitengwa shilingi bilioni 683.65 ambapo kati ya hizo fedha za ndani zilikuwa shilingi bilioni 312.06 sawa na asilimia 45.6 ya fedha za maendeleo na shilingi bilioni 371.6 fedha za nje, sawa na asilimia 54.4

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2013/14 kwa kipindi cha Julai hadi Desemba inaonesha kwamba mbali na fedha zilizotengwa kwa fungu 49 wizara ya maji, pia kulikuwa na fedha zingine jumla ya shilingi bilioni 130.41 zilizotengwa katika mafungu kama ifuatavyo:-

a. Mafungu ya Mikoa na Halmashauri shilingi bilioni 96.148 kwa ajili ya utekelezaji wa program ya majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini;

b. Fungu 46(Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi) shilingi bilioni 4.208-Kampeni ya usafi wa Mazingira mashuleni;

c. Fungu 52(Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii) shilingi bilioni 8-kampeni ya Afya na Usafi wa Mazingira Vijijini;

d. Fungu 50(Wizara ya fedha) shilingi bilioni 21.75 kugharamia miradi ya maji chini ya MCC; na

e. Fungu 56(TAMISEMI) shilingi milioni 300 kugharamia ufuatiliaji wa itekelezaji wa WSDP.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya Serikali inaonesha kuwa hadi kufikia mwezi April 2014, ni kiasi cha shilingi bilioni 46.59 tu kilikuwa kimetolewa, ikilinganishwa na shilingi za nyongeza shilingi bilioni 173.9 zilizokuwa zimeidhinishwa, sawa na asilimia 27 tu. Hali hiyo imesababisha kuwepo na upunufu wa shilingi bilioni 127.21 kwenye mkiradi iliyokuwa imepangwa.

**Mheshimiwa Spika**,Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itueleze imewezaji kutekeleza majukumu yake hadi kufikia kuwapatia maji safi na salama watu 2,390,000 waishio vijijini kwa kulinganishwa na wananchi 300,000 hadi 500,000 ambao walikuwa wanapatiwa maji safi na salama hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako, kati ya fedha hizo zilizotengwa katika fungu 49 na mafungu mengine kama yalivyotajwa hapo awali, ni kiasi gani cha fedha kimetolewa kwa ajili ya maendeleo hadi kipindi kilichoishia mwezi Machi mwaka 2014?

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bunge inayosimamia Wizara ya Maji baada ya kubaini tofauti kubwa ya kibajeti kwa ajili ya maji mijini na vijijini ilipendekeza kuwa Serikali itenge/iongeze bajeti ya maji vijijini ili **kupunguza tatizo kubwa la maji linalokabili maeneo mengi ya nchi.**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inasema kuwa imezingatia ushauri huo kwa kuongeza fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji vijijini. Kwa mwaka 2013/2014 asilimia 53 zimetengwa kwa ajili ya huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini, asilimia 34 ni kwa ajili ya huduma ya maji na usafi wa mazingira mijini, na asilimia 9 ni kwa ajili ya utunzaji wa vyanzo vya maji na asilimia 4 ni kwa ajili ya kujenga uwezo na kuimarisha taasisi zinazotekeleza WSDP.

Usambazaji wa Maji:

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji umehamasisha kuongezwa kwa rasilimali katika sekta ya maji. Kupitia miradi yake ya kutoa matokeo ya haraka, kumekuwa na ongezeko la vituo vya kuzaliza maji 8,285 vilivyoendelezwa na kuwezesha usambazaji wa maji kwa watu zaidi ya 1.89 milioni. Kutokana na mpango huu, usambazaji wa huduma ya maji umeongezeka kutoka asilimia 55 mwaka 2005 hadi kufikia asilimia 58.7 mwezi Desemba 2009.

Kumekuwa na maendeleo katika usambazaji wa huduma ya maji katika miji mikubwa ambapo vituo vya usambazaji wa maji vinaongozwa na mamlaka za maji safi na maji taka (UWASA), kwa kuendeleza vyanzo vipya vya maji, kukarabati na kupanua mifumo ya usambazaji wa maji. Hii imewezesha kuwepo

kwa ongezeko la maeneo yanayopata maji kutoka asilimia 74 mwaka 2005 mpaka kufikia asilimia 84 mnamo Desemba 2009.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, upatikanaji wa maji katika maeneo ya makao makuu ya wilaya na miji midogo bado ni changamoto kubwa kwani kunahitajika uwekezaji mkubwa kwenye vyanzo vipya vya maji, ukarabati pamoja na upanuzi wa mifumo. Vivyo hivyo, huduma za usambazaji maji katika Jiji la Dar es Salaam umebakia kuwa asilimia 68 toka mwaka 2005 mpaka sasa, kutokana na uzalishaji usiokidhi mahitaji hasa ikilinganishwa na ukuaji wa idadi ya watu ya asilimia 8 kwa mwaka.
**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi ya vifaa (kwa mujibu wa utafiti) kabla ya Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji, utafiti wa kaya unaonyesha kupungua kwa huduma ya usambazaji wa maji mijini kutoka asilimia 90 katika mwaka 2000/01 hadi kufikia asilimia 79 katika mwaka 2007, na kutoka asilimia 46 katika mwaka 2000/01 hadi kufikia asilimia 40 katika mwaka 2007 katika maeneo ya vijijini. Kuna haja ya kufanya tafiti kubaini sababu za kupungua kwa uwezo wa kusambaza, ingawa sababu mojawapo yaweza kuwa ukarabati duni wa miundombinu iliyopo na kutokuwa na mikakati endelevu ambayo imesababisha miundombinu iliyopo kutofanya kazi kwa kiwango kilichokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa uwiano wa usawa, jamii maskini inatumia kiasi kikubwa cha nguvu na muda (maeneo ya vijijini) na sehemu kubwa ya mapato katika kupata maji ikilinganishwa na jamii maskini ziishizo mijini ambazo zinatumia fedha nyingi ili kupata huduma ya maji. Uelewa mzuri wa mahusiano kati ya kiwango cha uwekezaji uliofanywa na kuongezeka kwa upatikanaji wa maji ni muhimu katika kutambua umuhimu na ufanisi katika uwekezaji katika sekta maji.

## 6. PROGRAMU YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI

**Mheshimiwa Spika,** Programu ya maji na usafi wa Mazingira Vijijini ilianza rasmi kuanzia mwaka 2007 hadi mwaka 2025. Programu hii inatekelezwa kwa awamu nne za miaka mitano kwa kila awamu. Utekelezaji wa awamu ya kwanza ulianza Julai, 2007 na utakamilika mwaka Juni, 2014 baada ya kuongeza miaka 2.

**Mheshimiwa Spika,** Awamu ya kwanza ya Programu hii inakadiriwa kugharimu Dola za Marekani 434 millioni. Programu hii inatekelezwa kupitia mfuko wa pamoja (*basket funding*) na kwa kupitia Wahisani wanaofadhili miradi maalum *(earmarked funding*).

**Mheshimiwa Spika,**Lengo lilikuwa ni kuwapatia wananchi wapatao **milioni 8** maji safi na salama kwa kujenga **vituo 41,900** katika kipindi cha miaka mitano. Fedha zilizotolewa mpaka Mei, 2013 ni Dola za Marekani 340 millioni.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa sasa awamu ya kwanza imemalizika na nusu ya awamu ya pili, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wananchi miradi hiyo imefikia wapi, kwani hali halisi kuna muingiliano mkubwa katika matumizi ya fedha za maji na mwisho unakuta mradi mmoja unatekelezwa na program mbili au tatu jambo ambalo tathmini inakuwa siyo sahihi kwa mradi husika.

## 7. UPOTEVU NA WIZI WA MAJI

**Mheshimiwa Spika,** Lipo tatizo kubwa sana la upotevu wa maji hapa nchini kutokana na miundombinu chakavu na wizi wa maji unaofanywa na baadhi ya watu maeneo mbali mbali yakiwepo mahoteli kujiunganishia maji bila kufuata utaratibu. Hali hii imesababisha hasara kubwa kwa serikali wakati huo huo wananchi wa maeneo mengine wanakosa maji. Taarifa zinaonyesha uvujaji na upotevu wa maji kwa mamlaka za maji umeendelea kupungua kutoka asilimia 51 july 2001 hadi kufikia asilimia 36.3 June 2013. Hata hivyo kiasi hicho bado ni kikubwa sana ukizingatia watanzania walio wengi hawapati huduma ya maji safi na salama.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa taarifa ya CAG inaonyesha kuwa kuna upotevu mkubwa wa mapato katika mamlaka za maji unaotokana na wateja kutokuwa na mita au upotevu wa maji.

Kwa mfano, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bukoba ilipoteza kiasi cha asilimia 56.6 ya mapato yatokanayo na maji wakati Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya walipoteza kiasi cha asilimia 35.16. Aidha, kulikuwa na upotevu wa fedha wa kiasi cha shilingi milioni 314 katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Songea. Ukaguzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), uligundua kuwepo kwa limbikizo la deni la ankara za maji la jumla ya Shilingi milioni 147 ambazo hazikulipwa na taasisi mbalimbali za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Ankara nyingi wateja wanagoma kulizilipa kutokana na ukweli kuwa maji hayafiki kwenye nyumba zao lakini maji yanatoka kwenye chanzo na kuishia njiani. Sambamba na hili ni kwamba DAWASA iliweza kurekodi maji ambayo yalipotea kwa uwiano wa asilimia 53 ya kiasi cha maji yote yaliyozalishwa ambayo ni asilimia 28 juu zaidi ya kiwango kinachokubalika cha asilimia 25 kilichokadiriwa kufikia fedha za kitanzania bilioni 8.947. Vile vile mamlaka ilipata hasara ya shilingi bilioni 17. 159 (2012 shilingi bilioni 21.052) na

hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2013 madeni ya muda mfupi ya mamlaka yalizidi mali za mamlaka za muda mfupi kwa shilingi bilioni 19.624.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi ya upinzani inaitaka serikali kueleza mkakati gani endelevu uliyopangwa kufanya marekebisho kwenye miundo mbinu ya maji kwa muda maalum ili kuokoa maji yanayopotea?

## 8. ULINZI NA UHIFADHI WA VYANZO VYA MAJI

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na Serikali kutokuwa na mpango mzuri na mikakati makini ya kutunza vyanzo vya maji, Vyanzo vingi vimeharibiwa, na vingine vimekauka . wakulima kulima mpaka kwenye kingo za maji, Mifugo kuchungwa mpaka kwenye vyanzo vya maji,wananchi kukata miti ya asili kwenye vyanzo vya maji .

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serilkali kueleza ni kwa namna gani inavyoshirikisha wananchi kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji vinavyowazunguka?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serkali ieleze Bunge watumiaji wakubwa wa maji hapa nchini vikiwepo viwanda, mahoteli makubwa, mashirika mfano TANESCO nk yanashirikiswaje katika kulinda vyanzo vya maji?

Ni mkakati gani endelevu wa kuhakikisha maeneo yote yenye vyanzo vya maji yanalindwa?

## 9. WATAALAM KATIKA SEKTA YA MAJI

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuwepo na ufanisi na utekelezaji mzuri wa majukumu ya Sector ya maji kunahitajika wataalam wa kutosha, wenye ujenzi wa kutosha na ubunifu ili kuendeleza sector hii.
Kwa mujibu wa taarifa za Serikali zinaonesha kuwa wataalam katika nyanja ya maji ni kama ifuatavyo:

i. *Ngazi ya Halmashauri:* kuna Wahandisi **150** na technicians **182;**

ii. *Ngazi ya Mikoa:* kuna Wahandisi 50; na

iii. *Sekta binafsi*: Kuna kampuni 145 za Wataalam Washauri, Kampuni 179 za Wakandarasi na Kampuni 33 za uchimbaji. Kampuni hizi ni zile zinazofanya kazi za maji[1].

**Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla Serikali ina** idadi ya wataalam waliopo 1538 katika ngazi ya Wizara, Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri ni ndogo sana ukilinganisha na mahitaji ambao ni 8,749. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge mapungufu haya makubwa ya wataalam yanaondolewaje?

### 10. MRADI WA VIJIJI KUMI UNAOFADHILIWA UNAOFADHILIWA NA BANK YA DUNIA

**Mheshimiwa Spika,** Mradi uhuu ulileta matumaini makubwa sana kwa watanzania/wananchi wa vijiji na kuona utawakomboa kutokana na adha kubwa ya maji wanayoipata. Mradi umekuwa ni kiini macho – tangu mwaka 2007 mradi ulipoanza mpaka leo 2014 hakuna hata Wilaya moja ambayo vijiji vyake vimekamilika.

---

[1] G. J. Kisaka - Mpango wa utekelezaji wa miradi ya maji vijijini mwaka 2013/2014 - terehe 3.6.2013

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Mei 2013, Halmashauri 118 zimeanza ujenzi wa miundombinu ya maji kwenye vijiji 10. Halmashauri 10 zipo katika hatua mbalimbali za kutangaza kupata wakandarasi wa ujenzi na Halmashauri, Halmashauri 3 zimepata wataalam Washauri na ziko katika hatua za utafiti wa vyanzo vya maji na kufanya usanifu wa miradi na halmashauri ya Wilaya ya Morogoro bado haijapata Mtaalam Mshauri.

**Mheshimiwa Spika,** Jumla ya miundombinu ya miradi ya maji kwenye vijiji 535 ipo katika hatua ya ujenzi.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na wananchi kupokea mradi kwa furaha kubwa na kujinyima sana ili wachangie asilimia 5% iliyotakiwa ili mradi uanze, fedha yao mpaka leo haijazaa matunda. Kwa vijiji vingi fedha yao wameweka bank na mpaka leo hawajapata maji na hawajui hatma ya fedha yao.

**Mheshimiwa Spika,** Vijiji vingine vimechimbwa visima maji yakaonekana tangu 2010 mpaka leo hayajasambawa kwa wananchi wameishia kuyaangalia tu. Baadhi ya visima vilivyonekana kuwa na maji wakati wananchi wanasubiri wasambaziwe wasaidizi wa Wilaya wamefika kwenye visima hivyo na kueleza

kwamba vitawekwa Pump ya mkono na siyo kusambazwa kwa wananchi kama ambavyo mradi ulivyolenga.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano mzuri ni Kijiji cha Usholola na Kazoroto (W) Kaliua waliletewa mpaka mabomba, na baadae mabomba hayo yamehamishwa kwa maelezo kwamba maji yaliyoko pale hayatoshi kusambazwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo ya kina iweje mradi wa milioni mia mbili na kumi, uliofanyiwa utafiti wa kutosha na wataalam, na wakandarasi kupewa kazi ya uchimbaji na wananchi kuelezwa maji ni mengi sana wasubiri kusambaziwa. Leo Serikali inakuja na kauli kwamba maji ni kidogo huko siyo kuwahadaa wananchi?
**Mheshimiwa Spika,** Katika Bajeti ya 2012/2013 Serikali iliahidi Bunge kukamilisha Mradi wa Vijiji kumi kwa kila mwaka na fedha zilitengwa jumla ya shilingi Bilioni 75.34. Hata hivyo fedha zilizopelekwa kwenye mradi wa vijiji kumi ni Tsh. Bilioni 34.3 tu.

**Mheshimiwa Spika,** Hivi kweli Serikali ina nia ya dhati ya kuondoa kero ya maji kwa wananchi wa Tanzania. Utaratibu uliotumika katika mchakato wa mradi wa vijiji 10 ulilenga kuharibu fedha za wananchi. Mhandisi mshauri alifanya utafiti maeneo yenye maji.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa vijiji 10 kuna wizi mkubwa umefanyika na ndio maana kwa miaka zaidi ya 7 sasa haikamiliki. Mhandisi mshauri aliyeteuliwa na Wizara kwenda kufanya utafiti vijiji vilivyoingia kwenye mradi na kuthaminisha maeneo yenye maji, walilipwa fedha yote.

**Mheshimiwa Spika,** Wachimbaji walipokwenda kuchimba maji, zaidi ya 70% ya maeneo yaliyofanyiwa utafiti na kuonekana yana maji yalipochimbwa hayakutoa maji. Matokeo yake mpaka leo hakuna hatua zozote zilizochukuliwa kwa wahandisi hawa. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali iwafikishe mahakamani kwa kufanya kazi chini ya viwango na kusababisha hasara kwa Taifa na wananchi wanaendelea kuteseka kwa kukosa maji.

## 11. CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MRADI WA VIJIJI KUMI

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa taarifa ya Serikali inaonyesha kuwa kuna changamoto kadhaa katika utekelezaji wa mradi wa maji wa vijiji kumi, nazo ni zifuatazo:

1. Ucheleweshaji wa kupata vibali vya usanifu na Mtaalam Mshauri;

2. Kampuni inayopima eneo la kuchimba visima kuwa tofauti na kampuni itakayochimba hivyo kusababisha visima vingi kulipiwa bila kuwa na maji;
3. Mikoa kutokuwa na nguvu ya uwajibikaji katika miradi inayotekelezwa kwenye Halmashauri;
4. Gharama za miradi zinakuwa juu kutokana na baadhi ya watekelezaji kutokuwa waaminifu (*high unit cost);*
5. Ufuatiliaji na usimamiaji hafifu unaofanywa na watekelezaji;
6. Miradi mingi imekuwa inachukua muda mrefu kutekelezwa na mingine kutotekelezwa kabisa kutokana na mipango mibovu na urasimu unaofanywa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kuna mifano halisi kwa namna miradi mingi inakuwa inachelewa na hivyo wananchi kuendelea kutaaabika kwa kukosa maji, mfano ni mradi wa maji mkoa wa Tabora unaotakiwa kutoa maji Ziwa Viktoria - Nzega - Igunga hadi Tabora, Tangu mwaka 2010 zilipotolewa hela kwa ajili ya upembuzi yakinifu mpaka leo upembuzi yakinifu haujakamilika kwa miaka minne.

Mradi mwingine ni ule wa maji kutoka Ugalla kupeleka wilaya ya Kaliua na Wilaya ya Urambo. Bajeti ya mwaka jana 2013/14 Serikali ilitenga fedha milioni 450 kwa ajili ya usanifu na upembuzi yakinifu, kwa mwaka mzima kazi hayo haikufanyika kwa sababu mshauri mwelekezi (Consultant) hakupatikana.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi ya Upinzani inauliza, ikiwa usanifu na upembuzi yakinifu unachukua miaka minne haujakamilika, je utekelezaji wa mradi utachukua miaka mingapi kukamilika?

**Mheshimiwa Spika,** kasi ya utekelezaji wa miradi ni ndogo sana, na hii inatokana na miradi kutekelezwa na kusimamiwa na Serikali Kuu. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Serikali kuweka utaratibu wa kushirikisha mamlaka za maji na waandisi wa mikoa kurahisisha utekelezaji wa miradi.

**12. HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI**

**Mheshimiwa Spika,** Hadi June, 2013 hali halisi ya upatikanaji wa maji vijijini (Huduma ya maji vijijini ni asilima 40%. Kiasi hiki ni kidogo sana ukizingati zaidi ya asilimia 80 ya watanzania wanaoishi vijijini na hivyo wengi wao hawapati huduma ya maji safi na salama.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na Serikali kuja na mipango mbalimbali ikiwepo miradi ya kimkakati, matokeo ya haraka (Quick win Projects) Miradi ya matokeo makubwa sasa (Big Result Now) Serikali hiyo hiyo imeshindwa kutoa fedha za kutekeleza miradi ya maji Vijijini na hivyo wananchi kuendelea kuteseka - Miradi mingi utekelezaji wake unakwenda taratibu sana (Miradi inasuasua) hivyo kusababisha hata gharama za miradi hiyo kuongezeka.

**Mheshimiwa Spika,** Kuanzia mwaka wa fedha 2013/2014 miradi ya maji na usafi wa mazingira vijijini ilianza kutekelezwa kwa utaratibu wa Tekeleza sasa kwa matokeo makubwa (Big Result Now – BRN). Utaratibu huu ulilenga kuongeza kasi kaatika utekelezaji wa miradi ili kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi waishio vijijini kutoka 40% Juni, 2013 hadi asilimia 74% ifikapo mwezi Juni, 2016. Mpango wa Big Results Nowa ulihusu utekelezaji katika ujenzi wa miradi mipya, ukarabati wa mradi chakavu, Upanuzi wa miradi iliyopo na uendeshaji na matengenezo (Operation and Maintenance).

**Mheshimiwa Spika,** Kambi ya Upinzani inapenda kupata ufafanuzi wa kina ni miradi mingapi ilifanyiwa ukarabati wa miundombinu chakavu kwa mwaka 2013/2014 na ni maeneo yapi/wapi?

**Mheshimiwa Spika,** Mwaka wa fedha 2013/14 Serikali ilitenga fedha shilingi 345,005,362,000 kwa ajili ya maji vijijini. Kati ya fedha hizo 45,750,840,000 ni fedha za ndani na Tsh. 129,254,522,000 ni za nje. Hadi Machi, 2014 fedha zilizotolewa kwa miradi ya maji vijijini ni shilingi 148,515,345,941 (Sawa na 43% ya Bajeti).
Katika fedha hizo Sh. 137,904,598,957 zimeelekezwa kwenye miradi ya vijiji 10 kwa Halimashauri za Wilaya ambapo kati ya hizo Tsh. 34,311,371,348 (15.9% fedha ya ndani ) ni fedha za ndani na Tsh. 103,593,227,603 (sawa na 80% ya fedha za nje)

## 13. MATATIZO YA UKOSEFU WA MAJI SAFI NA SALAMA YALIYOIBULIWA NA WANANCHI KATIKA TAFITI SHIRIKISHI 2010-2014 MAENEO MBALIMBALI

**Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani kwa miaka mbalimbali imeieleza Serikali matatizo ya maji yaliyopo katika mikoa mbalimbali nchini.

Hata hivyo, wakati mwingine Wizara ya Maji imebeza taarifa hizo ikitoa majibu yenye kuashiria kutokutambua ukubwa wa matatizo yaliyopo na haja ya kuchukua hatua za haraka.

Aidha, Hotuba za Kambi Rasmi ya Upinzani zimekuwa zikibezwa kwa visingizio kwamba kazi ya upinzani ni kupinga tu na kwamba Wizara ya Maji inaendelea kutekeleza miradi yenye Matokeo Makubwa Sasa (Big Results Now) kwenye kuwezesha wananchi kupata maji.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kwamba malalamiko juu ya matatizo ya maji tunayoyawasilisha ni kwa niaba ya wananchi na ni kwa maslahi ya nchi.

Kwa kuthibitisha hilo, katika Hotuba hii, tumeamua kuwaletea ushuhuda wa maelezo na ushahidi wa picha uliotokana na utafiti shirikishi uliofanywa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

**Mheshimiwa Spika;** Tunatarajia kwamba Wizara ya Maji haitabeza utafiti huu kama inavyofanya kwa hotuba za Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuzingatia kwamba TGNP ni shirika lisilo la kiserikali lisilofungamana na chama chochote cha siasa lenye shabaha ya kuchochea kujengeka kwa usawa na uwiano wa jinsia, kukuza uwezo wa mwanamke na makundi mengine yaliyoko pembezoni, kustawisha na kubadilisha mfumo wa kijamii ambao unamkandamiza mwanamke kwa hali na mali. Wahanga wa matatizo makubwa ya wa maji nchini ni wakina mama.

**Mheshimiwa Spika;** Tunaamini kupitia utafiti huu ambao natoa mwito pia kwa picha kuonyeshwa bungeni wakati ninapoendelea kuwasilisha maoni haya ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, wabunge wote walioshiriki warsha ya uchambuzi wa bajeti kijinsia (gender budget analysis) na wabunge wote wa mikoa ambayo utafiti huu umefanyika ya Mbeya, Shinyanga, Morogoro, Pwani na Dar Es Salaam mtasimama kidete kuhakikisha Wizara ya Maji inatimiza wajibu wa kuwezesha wananchi kupata huduma hii ya msingi kwa maisha ya binadamu na uchumi wa nchi kwa ujumla.

**Mheshiwa Spika**; nichukue mifano michache kutoka katika baadhi ya tafiti walizozifanya kati ya mwaka 2010 mpaka mwaka huu 2014 zenye kuonyesha ukubwa wa matatizo ya maji katika maeneo mbalimbali:

### 13.1. MANEROMANGO, KILUVYA NA VISEGESE ( KISARAWE)

**Mheshimiwa Spika;** Utafiti shirikishi umetoa ushuhuda na ushahidi kwamba katika eneo hili maji ni tatizo gumu sana na sugu. Na hivyo limepewa kipaumbele katika ngazi zote kwa mtu binafsi, familia na hata jamii. Maana hawana uhakika wa kupata maji, kwa urahisi licha ya kwamba si salama na safi. Maji yanapatikana mbali na kuna mlima mkali sana. pamoja hayo bado si hakika sana mtu kupata, hasa wakati wa kiangazi. Wanawake wamekuwa

wakiamka usiku ama wakati mwingine kulala kwenye foleni za maji, wakati huo njiani si salama sana.

Wamelalamika kuwa shughuli nyingi sana zinakwama kwa ajiili ya maji. Maana inabidi wasitishe kwenda kulima kwa wakati, ama kufanya shughuli nyingine wa ajili ya kutafuta maji.

**Figure 1 Madimbwi ya maji yanayotumika na wananchi wa Maneromango Kisarawe**

### 1.1. MKAMBANI (MOROGORO), SONGWA (KISHAPU) NA (IJOMBE MBEYA VIJIJINI)

**Mheshimiwa Spika;** Katika kata zote tatu za utafiti shirikishi tatizo la maji limejitokeza kwa upana sana. Katika kata ya Songwa katika baadhi ya maeneo yote ya Maganzo, Seseko, Ikonongo, Mpumbula na Masagala hawana huduma ya maji kabisa. Katika kijiji cha Maganzo gharama za maji ni kubwa kwa mwananchi wa kawaida, ni kati ya sh. 500 na 1000 kwa lita 20 za maji masafi. Wanawake hutumia muda mwingi kutafuta maji na kuacha shughuli zao za kujitafutia kipato mfano biashara zao na ufundi cherehani.

**Mheshimiwa Spika,** Maji yanayotumiwa na wakazi wa kijiji cha Songwa hayasafishwi wala kuwekwa dawa, wakati yale yanayotumiwa na wakazi wa Williamson Diamonds (Mwadui) yanatiwa dawa, yote yanatoka kwenye chanzo kimoja cha mabwawa ya Songwa. Hali hii imewafanya wazazi wakati mwingine hawaogi kabisa kwa kukosa maji katika zahanati ya Maganzo.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa kata ya Mkambarani utafiti unaeleza kuwa maji yanapatikana katika kijiji cha Mkambarani tu ambapo wakazi hawa wamejichangisha na kuvuta maji toka chanzo cha maji ili kufikisha gharama ya asilimia 5% na asilimia 95% ya gharama zimefadhiliwa na Benki ya Dunia (WB). Wanakijiji huchota maji kwa sh 50 kwa ndoo ya lita 20 na kwa wanaotoka vijiji vya jirani huchota maji sh 100 kwa ndoo. Vilevile maji haya yamefikishwa kwenye vituo vya maji ambavyo viko vinne katika kijiji kizima na kama alivyosema mkazi wa Mkambarani.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa Ijombe inaelezwa kuwa shida ni kubwa mno kwani maji wanayochota ni machafu sana. Kwa hali hiyo huwafanya wanafunzi wa kike kuchelewa kwenda shuleni, na mara nyingine hutokea ubakaji wanapofuatilia maji. Lakini pia wanapochelewa kurudi hupigwa na waume zao wakihofiwa kuwa walikuwa kwa mahawara zao. Wanafunzi nao hasa wa kike huchelewa masomo kwa sababu ya kufuatilia maji. Washiriki

walisema kuwa kwa jinsi hali ya maji ilivyo mbaya wanahofu ya kuchota magonjwa, hata mama wajawazito wanakwenda kuchota maji kwa hiyo kuna hofu ya wao kuzalia njiani lakini hawana la kufanya.

**Figure 2 watoto wa kike ni wathirika wa tatizo la ukosefu wa maji vijijini na mjini, hawa ni kutoka kijiji cha Ijombe, Mbeya Vijijini**

### 1.1. KISAKI (MOROGORO), KISHAPU (KISHAPU) NA MSHEWE (MBEYA VIJIJINI)

**Mheshimiwa Spika;** Serikali irejee maelezo ya utafiti kwamba maji ni suala ambalo linagusa Nyanja zote za maendeleo ikiwa ni pamoja na afya, uzalishaji katika kilimo na ardhi, elimu na fursa mbalimbali za elimu kwa wanawake na watoto, amani na utulivu, pamoja na uzalishaji kiuchumi. Katika mchakato wa uraghbishi katika kata zote tatu suala la ukosefu wa maji safi na salama limejitokeza, na limechangia kwa kiasi kikubwa kurudisha nyuma maendeleo na kuwa kikwazo kikubwa kwa wanawake na wasichana kufikia. Katika kata ya Kishapu suala hili limechukua nafasi kubwa sana. Kwa kiasi kikubwa sehemu hii ni kame na hivyo maji hupatikana kwa wingi kipindi cha mvua na baada ya hapo hufuatiwa na kipindi cha ukame mkali. Kwa hali hiyo kwa sehemu kubwa upatikanaji wa maji ni changamoto kubwa.

**Figure 3 wananchi wa mji wa Munze Kata ya Kishapu wakitafuta maji**

**Figure 4 vijana wanaojishughulisha na biashara ya maji wakihangaika mjini Kishapu**

Wanawake wamekuwa na mzigo mkubwa wa kuamka usiku wa manane na kutembea usiku wa manane wakipita misitu na vichaka kupanda vilima na miamba (hili limeonekana zaidi Mshewe katika kijiji cha Ilota), umbali wa kilometa 8-10 kufuatilia maji. Pamoja na umbali wote huo, vyanzo vya maji vimechafuliwa na uwekezaji wa mashamba na viwanda pamoja na shughuli za kila siku za binadamu na kunywesha wanyama. Kwa upande wa Kisaki tatizo la maji linasababishwa na kuomhezeka kwa idadi ya watu katika eneo. Hii ni kutokana na shughuli za biasharaya mazao na utalii. Vilevile uanzishwaji wa shule ya sekondari ya kata umewezesha vijana wengi kutoka vijiji na kata jirani kuhamia hapo. Matatizo ya maji yanajionesha zaidi kwenye makazi mapya.

**Figure 5 Wanakijiji wa Ilota kata ya Mshewe, Mbeya vijijini wakitoka kuchota maji**

**Mheshimiwa Spika;** Changamoto hii ya maji imepelekea matatizo mengi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa matumizi katika familia kwani pesa nyingi hutumika kununua maji; wanawake na wasichana kubakwa, ubakaji kwa wanawake na wasichana na hivyo kuwepo na mimba zisizotarajiwa;

wanawake kukutana na vipigo kwa ajili ya kuchelewa kurudi kwenye maji na wivu wa mapenzi kutoka kwa wenzi wao; hatari ya wanyama wakali kama vile chatu, chui, fisi, nk; uleaji hafifu wa watoto na famiia kwa ujumla kwa kuwa muda mwingi mama huutumia kwenye kusaka maji; ushiriki mdogo katika shughuli za kiuchumi unaosababishwa na kupoteza muda mwingi kufuatilia maji na hivyo umaskini endelevu; imeathiri hali ya kiuchumi ya akina mama kiuongozi, kipato na fursa za ajira. Na matokeo yake ni kwamba, wanawake wengi wameshindwa kushikilia nafasi zao za ajira mfani kilimo, biashara ndogo ndogo; familia kusambaratika; inaathiri matumizi ya muda kwa wanawake, kiwango cha elimu kushuka, ndoa za mapema na zisizotarajiwa, vile vile kuna masuala ya ujinsi ambapo wanawake hushindwa kufurahia ndoa zao/ngono kwa sababu ya kuamka usiku wa manane kufuata maji lakini pia kukosa maji ya kuoga kujiandaa kwa ajili ya kufurahia mapenzi/ngono.

### 1.1. NYAMARAGA (TARIME), MONDO KISHAPU, KIROKA (MOROGORO) NA KIGOGO (DSM)

**Mheshimiwa Spika;** Tatizo la maji ni la nchi nzima, vijijini na mijini. Kata ya Kigogo Dar Es Salaam tatizo la maji linaathiri jamii hasa mwanamke, watoto wa kike kuchelewa kwenda shuleni na wakinamama kuchelewa kufanya majukumu yao yanayowahusu pia kulingana na maumbile ya mwanamke ni rahisi kupata magonjwa ya UTI kwa vile maji yanayopatikana sio salama na safi, pia kusababisha kupata magonjwa ya homa ya matumbo( typhoid) na magonjwa ya milipuko. Sababu ya tatizo hili la maji ni miundo mbinu chakavu inayochangia kupateza maji mengi bila sababu na kusababisha maji taka kuingia kwa baadhi ya sehemu za bomba iliyopasuka , pia wanaouza maji kwa kuvuta kwa motor pia ni tatizo na wanaohusika kufanya hivyo ni baadhi yao ni viongozi.

**Figure 6 wananchi wenyewe kwenye utafiti walichora picha kuonesha jinsi wanavyouziwa maji na matajiri**

**Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa vijijini, Changamoto katika upatikanaji na ufikiwaji wa rasilimali ya maji katika kata ya Nyamaraga na vijiji vyake inalingana karibu kila kijiji. Katika kata hii hakuna mradi wowote wa maji, wakazi wa kata hii wanategemea visima na mito kupata maji ambayo mara nyingi sio safi na salama.

**Mheshimiwa Spika,** Maji yanapatikana kwenye chemchemi na makorongo ambayo yapo mbali na makazi ya watu, kumejaa hatari na wasiwasi kwa wnawake na wasichana wanapoenda kutafuta maji, changamoto kubwa ni

kwatoto wa shule pale wanapolazimika kuamka alfajiri kutafuta maji ndipo waende shule.

Visima vingi na kwenye mito kumezingirwa na vichaka, huko tinabakwa na kusumbuliwa sana, hakuna pakushitaki, utamwambia nani na watu ni walewale? Msichana na mwanamke wa Nyamaraga yupo hatarini, tumechagua viongozi lakini suala la maji limekuwa kama ajenda yao ya, kuombea kura kila mwaka wa uchaguzi, halijawahi kufanyiwa kazi. Kazi ya kuchota maji katika jamii ya kikurya ni kazi ya mwanmke mzigo huu umetuelemea hatuna pakupumlia.

**Mheshimiwa Spika,** Kilimo cha mikaratusi kwa ajili ya biashara ya mbao imechangia uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji na maji kupungua kwa kiwango kikubwa. Kutokuwepo kwa mpango wa kudhibiti hali hiyo kunachangia hofu na hatari hapo mbeleni.

Kwa vijiji vya Gwitiro na Kitagasembe katika suala hili la maji ni kwamba kuna changamoto kubwa zaidi, ili kupata maji inawalazimu kutembea na kupita maeneo ya hatari sana kufuata maji. Hali hii imepelekea adha kubwa mno kwa wanawake/wasichana wa vijiji hivi, ikiwemo kutumia muda mwingi sana kwa ajili ya maji, kuishi kwa hofu na wasiwasi wa vipigo na unyanyasaji kijinsia kutoka kwa waume au wenzi zao. Lakini pia kudhalilishwa na kubakwa wanapoenda kutafuta maji.

Wananchi wanaonyesha kuchoshwa na kukata tamaa kwani kwa pamoja wako tayari kujitolea, hakuna jitihada za viongozi zozote wasio tayati kutatua kero ya maji katika vijiji vyao Wamesusia shughuli za maendeleo kwa sababu hawana imani na viongozi. Wanapanga ajenda wao wanapotuita wanataka kujadili wanayotaka wao tu, tukiuliza mapato na matumizi inakuwa ugomvi.

***Mheshimiwa Spika;*** *Maji ni hitaji la msingi katika uhai wa binadamu kwani yanatumika kwa njia mbili. Licha ya matumizi ya kunywa/kupikia na usafi/kufua, pia yanatumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Vijiji vingine vina mtandao wa maji wenye vituo vichache vya maji ambavyo vinafanya wanawake/wasichana kutembea mwendo mrefu na muda kwenda kuchota maji. Matatizo katika upatikanaji wa maji safi na salama zinatofautiana kulingana na vyanzo vya maji vilivyopo.*

***Mheshimiwa Spika,*** *Mwanamke anapata wakati mgumu kwa kupigwa na mume wake pale anapochukua muda mrefu kwenda kuchota maji huku akijua kabisa maji ni shida. Lakini tu kutaka kujulikana kuwa yeye ni mwanamme ni lazima ampige mke wake. Wasichana wanapoenda kuchota maji ndipo wanapokutana na vijana na kuwarubuni kwa kuwa hana stadi za maisha*

*kujikuta wameingia kwenye mahusiano ya mapenzi na matokeo yake ni mimba au magonjwa ya zinaa kama VVU.*

Maeneo mengine wanatumia maji ya visima ambavyo wamechimba wenyewe kwa mikono ambavyo viko mbali na makazi. Lakini walipata mradi wa maji ambao walichimba visima bila kushirisha jamii bali viongozi pekee na mradi ukafa.

Wakati vijiji vilivyo kando kabisa na mlima (Bamba) changamoto yao juu ya maji ilikuwa ni ukosefu wa maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Katika uchambuzi ilionesha kuwa kuna uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji unaofanywa na kilimo cha milimani, ukataji kuni na uchomaji wa mkaa. Pia washiriki walilalamikia jinsi maji yalivyouzwa kwenda Kijiji cha Mkambarani na wao kuambulia vituo viwili tu vya maji.

**Mheshimiwa Spika;** Tatizo la maji lilichukua nafasi kubwa sana wakati wa mchakato wa uraghbishi katika kata ya Mondo hasa katika kijiji cha Buchambi.Tatizo la maji ni la vizazi na vizazi kwani tangu uhuru hawajawahi kupata maji safi na salama.

**Mheshimiwa Spika,** Wanajamii wa kata ya Mondo wanategemea maji kutoka katika bwawa la Songwa ambalo liko katika kata ya Songwa na wanatumia takriban muda wa masaa manne kutembea kwa miguu. Kijiji cha Buganika ni moja wapo ya vijiji 8 vilivyo katika mzunguko, yaani viko pembeni ya mgodi wa Wiliamson Diamond. Hakuna chanzo cha maji zaidi ya maji kutoka bwawa la Songwa ambayo yanatumika katika migodi (Wiliamson Diamond) na kuyarudisha bwawani na hali wanajuwa kuwa watu wanayatumia katika shughuli za majumbani. Changamoto hii ya maji inatokana na uhaba wa mvua ikiwa ni hali ya kijografia ya nchi. Lakini pia katika eneo hili hakuna chanzo cha uhakikika cha maji safi na salama zaidi ya ziwa Victoria.

**Mheshimiwa Spika;** Adhari za kukosekana kwa maji ni kubwa kwa wanawake na watoto kwa mfano ukatili wa kijinsiaikiwemo ubakaji,wanyama wakali na ajali za kugongwa na magari,pikipiki na baiskeli.Pia eneo la kupatia maji ni mbali na unatembea kwa saa nne.Lakini pia maji ya bwawa ambayo hutumika kunyweshea wanyama,matumizi ya nyumbani wakati huohuo maji hayo hutumika kuoshea almasi kutoka mgodini na kurudishwa bwawani kwani maji siyo safi na salama.Wanafunzi wa shule ya msingi hubeba maji kwa ajili ya matumizi ya shule,wengi wao wanatoka mbali hivyo ni mateso makubwa.Wanawake wanapokwenda kujifungua wanabeba maji kwani hakuna maji katika zahanati iliyoko katika kijiji cha Bughanika.

Figure 7wasichana wakitoka kusaka maji Kishapu

**Mheshimiwa Spika;** nimechukua mifano michache kati ya mingi ya ushuhuda na ushahidi wa matatizo ya maji nchini ili kutoa picha halisi nikiamini kwamba walau mwaka huu Wizara ya Maji itakuguswa na ukubwa wa tatizo na kuacha kutoa majibu mepesi ya kutaja orodha ya miradi utekelezaji ukiwa hafifu na kuacha wananchi kuendelea kupata shida. Wabunge ni vizuri kukumbuka kwamba Sera ya maji ya mwaka 2002 inaeleza kuwa madhumuni ya jumla ya sera kuhusu utoaji wa huduma ya maji ni kuboresha afya ya jamii na kusaidia kuondoa umaskini vijijini ikiwa ni pamoja na kuboresha upatikanaji wa maji safi salama na yakutosha.

**Mheshimiwa Spika;** Maji ni uhai na inatambulika kuwa maji ni hitaji la msingi na haki ya kila mtu,upatikanaji wa maji safi na salama ni hitaji la msingi na haki ya kila mtu. Hata hivyo haki hii haipo kwa wakazi wa vijijini na miji midogo.Hili limekuwa ni dai na kilio cha wanajamii wa maeneo ambayo utafiti shirikishi umefanyika na hitaji la wananchi wa maeneo mengi nchini. Kwa kuzingatia hali hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ni kwanini mpaka sasa imeshindwa kutekeleza kwa ukamilifu Sera ya Maji iliputungwa na ni hatua gani za haraka zinachukuliwa na Serikali kuboresha upatikanaji wa maji kwa wananchi nchini? Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa mwito kwa wananchi kuanza maandalizi ya kuindoa CCM kuanzia kwenye chaguzi za vitongoji, vijiji na mitaa kama adhabu ya kushindwa kushughulikia matatizo ya maji tangu chama hicho kilipoanzishwa na viongozi wake kuchukua dhamana ya kusimamia miradi michache na mibovu ya maji katika maeneo mbalimbali.

1. **UVUNAJI WA MAJI**

**Mheshimiwa Spika,** Tumeshuhudia wakati wa mvua maji mengi yanapotea ardhini na kuleta maafa na uharibifu wa Miundombinu ya bara bara, Reli na hata Kuteketeza makazi ya wananchi. Baada ya msimu wa mvua kilio cha mahitaji ya maji hufuata kila kona.

Hakuna Mipango/Mikakati ya Serikali kukusanya maji kwenye mabwawa ili yatumike kwa kilimo na mifugo. Serikali kwa miaka mitatu mfululizo imeahidi kujenga mabwawa katika Wilaya zote, utekelezaji wake unakwenda taratibu sana na kwingine hakuna kabisa utekelezaji uliofanyika.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la kutoa elimu na miongozo ya uvunaji wa maji ya mvua limeachwa kwenye halmashauri za Wilaya. Kwa kuwa hakuna yeyote anayeona umuhimu wa swala hili na hivyo limeachwa kama lilivyo. Pamoja na maelekezo kutolewa hakuna hata sheria ndogo ndogo iliyoundwa kusimamia suala la uvunaji maji ya mvua.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni mpango gani kwa nchi nzima wa kuhakikisha maji ya mvua yanavunwa kwa ajili ya matumizi ya akiba?

## 2. TEKELEZAJI WA MPANGO MAALUM WA KUTATUA MATATIZO YA MAJI KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM NA MAENEO MENGINE YA DAWASA YA KIBAHA NA BAGAMOYO MKOANI PWANI

**Mheshimiwa Spika;** Tarehe 22 Aprili 2013 Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliwasilisha Hotuba ya maoni juu ya mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2012/2013 na kuwasilisha maoni juu ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2013/2014 juu ya pamoja na mambo mengine Mpango Maalum wa kutatua Matatizo la Maji katika eneo la Mamlaka ya Majisafi na Majitaka (DAWASA).

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani ilifanya hivyo kwa kuzingatia athari za matatizo ya maji wanayopata wananchi katika eneo la DAWASA lenye kuhusisha Jiji la Dar Es Salaam na baadhi ya maeneo ya Kibaha na Bagamoyo ambao ni zaidi ya asilimia kumi ya wananchi wote wa Tanzania lakini wanaishi kwenye maeneo ambayo upatikanaji wa maji chini ya wastani wa kitaifa wa mijini. Katika majumuisho ya mjadala juu ya makadirio hayo, Wizara ya Maji iliahidi kwamba majibu ya michango iliyotolewa yangetolewa kwa maandishi.

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo, mpaka nipowasilisha maoni haya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haijapatiwa kitabu au bango kitita la majibu ya hoja za wabunge; hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa mwito kwa Spika wa Bunge kabla ya mjadala huu kuendelea kumtaka Waziri wa Maji kutoa maelezo ni kwanini hakutekeleza ahadi hiyo na aagizwe asambaze nakala za majibu ya michango ya mwaka 2013/2014 kabla ya wabunge kuendelea kutoa michango mipya juu ya makadirio ya mwaka 2014/2015.

**Mheshimiwa Spika;** Pamoja na kutopata majibu ya michango kuhusu makadirio ya mwaka 2013/2014, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepitia Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2014/2015 Fungu 49 uliowasilishwa Bungeni juu ya "uboreshaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dar Es Salaam" na haijaridhika na maelezo yaliyotolewa.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Maji na inatoa mwito kwa wabunge kurejea Mpango Maalum wa Kuboresha Huduma ya Majisafi na Majitaka eneo la DAWASA ulionza kutekelezwa mwezi Machi 2011, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano, kauli ya Waziri wa Maji Bungeni ya tarehe 7 Novemba 2012 na maelezo ya Waziri wa Maji aliyoyatoa kufuatia Hoja Binafsi ya Mheshimiwa John Mnyika (Mb) tarehe 4 Februari 2013 juu ya Hatua za

Haraka za Kuboresha Upatikanaji wa Majisafi na kushughulikia uondoaji wa maji taka katika Jiji la Dar Es Salaam na nchini.

**Mheshimiwa Spika;** Wizara ya Maji na wabunge walinganishe ahadi za Serikali katika nyaraka hizo zilizowasilishwa Bungeni na maelezo ya utekelezaji yaliyopo kwenye randama na hotuba ya Waziri ambapo inaonyesha wazi kwamba hatua za haraka za uboreshaji wa huduma za maji katika Jiji la Dar Es Salaam na maeneo mengine ya DAWASA ya Kibaha na Bagamoyo bado hazichukuliwi kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia hali hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Waziri wa Maji kujieleza bungeni ni sababu zipi zilimfanya atoe maelezo ya uongo Bungeni tarehe 4 Februari 2013 na kufanya mabadiliko yaliyosababisha kuondolewa kwa hoja binafsi ambayo iwapo ingejadiliwa ingeliwezesha Bunge kupitisha maazimio ya kuisimamia Serikali kuwezesha hatua za haraka kuchukuliwa.

Hali hii ya matatizo kuendelea inajidhihirisha katika muongozo ulioombwa Bungeni tarehe 12 Mei 2014 na Kauli ya Serikali kuhusu matatizo ya uzalishaji wa maji katika mtambo wa maji wa Ruvu juu iliyotolewa na Waziri wa Maji katika Mkutano huu wa Bunge. Aidha, hali hiyo inajidhihirisha kwenye udhaifu kuhusu Bwawa la Kidunda mkoani Morogoro ambapo mpaka sasa ujenzi haujaanza.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kukumbuka kwamba Mpango huo Maalum ulipitishwa na Baraza la Mawaziri mapema mwaka 2011 hivyo, kusuasua kwa utekelezaji wake ni ishara ya udhaifu wa Rais kuwasimamia Mawaziri na Mamlaka zingine kuweza kutekeleza maamuzi ya chombo hicho muhimu ambacho Rais ni mwenyekiti wake.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani inafahamu kwamba mwezi Machi 2013 Rais alinukuliwa kwenye vyombo vya habari kwamba angeitisha kikao Ikulu kukutana DAWASA, DAWASCO, Mkuu wa Mkoa wa Dar Es Salaam, Wabunge na Wizara ya Maji kuwezesha hatua za haraka kuchukuliwa. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inataarifa kwamba kikao hicho hakijafanyika mpaka hivi zaidi ya mwaka mmoja ukiwa umepita hali inayodhihirisha udhaifu wa usimamizi wa Rais na ofisi katika suala muhimu kwa maisha ya wananchi wa Jiji la Dar Es Salaam na maeneo mengine yanayohudumiwa na DAWASA.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Waziri Mkuu aagize kwa mujibu wa mamlaka na madaraka yake yanayotajwa kwenye ibara ya 52, Serikali itoe maelezo wakati wa majumuisho ya mjadala wa makadirio ya

mapato na matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2014/2015 ni kwanini kikao hicho hakijafanyika mpaka hivi sasa na ni lini hasa kikao hicho kitafanyika.

**Mheshimiwa Spika;** Maelezo hayo yawezeshe Serikali kushughulikia kasoro zilizopo katika muda uliobaki kabla ya kufika mwisho wa mwezi wa Juni 2014 ambapo ni mwisho wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/2014 pamoja na kuhakikisha bajeti ya Serikali kwa mwaka 2014/2015 imezingatia kikamilifu Mpango wa Taifa wa Maendeleo katika vipaumbele na mahitaji halisi ya utatuzi wa haraka wa matatizo ya maji katika Jiji la Dar Es Salaam na maeneo ya Mkoa wa Pwani yanayohudumiwa na DAWASA.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali izingatie kwamba mradi wa upanuzi wa Ruvu Chini ulipaswa kukamilika kabla ya mwezi Machi 2013; hata hivyo kutokana na udhaifu mbalimbali mradi huo haukukamilika kwa wakati. Aidha, kumekuwepo na udhaifu katika utekelezaji wa mradi wa ulazaji wa Bomba Kuu la kipenyo cha milimeta 1,800 kutoka mtambo wa Ruvu chini hadi Jijini Dar Es Salaam ambapo ilipaswa maji yawe yamefika jijini ikiwemo katika Jimbo la Ubungo Januari 2014 kwa gharama za Shilingi bilioni 192.68.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa upande mwingine, pamoja na Serikali ya Tanzania kupata fedha kutoka Serikali ya India dola za Kimarekani milioni 178.125 sawa na Shilingi bilioni 289.45 kwa ajili ya upanuzi wa chanzo cha maji Ruvu Juu kumekuwepo na udhaifu wa utekelezaji ambao Wizara ya Maji na DAWASA wanapaswa kutoa maelezo kwa Bunge na kwa Rais. Mradi huo unahusisha ulazaji wa bomba kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara; na Ujenzi wa tanki kubwa katika eneo la Kibamba; usanifu na ujenzi wa mabomba ya usambazaji katika maeneo ambayo hayana mtandao wa maji. Ujenzi wa mradi huo ulipaswa kuanza toka Agosti 2013, hata hivyo mwezi huo ulipita bila ujenzi kuanza hali ambayo imechelewesha hatua za haraka za kuboresha upatikanaji wa maji safi.

**Mheshimiwa Spika;** Hivyo majibu ya Wizara ya Maji na kikao na Rais kinapaswa kuwezesha ujenzi kufanyika kwa haraka zaidi kama ambavyo Ofisi ya Rais inasukuma ujenzi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara mpaka Dar Es Salaam umbali mrefu zaidi. Usanifu na utayarishaji wa vitabu vya zabuni kwa ajili wa ujenzi wa bwawa la Kidunda Mkoani Morogoro ambalo litachangia kuboresha upatikanaji wa maji katika mkoa huo na mikoa ya Pwani na Dar Es Salaam haukukamilika mapema 2013 kama ambavyo Wizara ya Maji iliahidi. Aidha, kumekuwa na ucheleweshaji wa ulipaji fidia za wananchi hatua ambayo imekwamisha ujenzi wa bwawa kuanza mwezi Oktoba 2013 kama ilivyopangwa baadaye baada ya kuwa na udhaifu mkubwa katika utekelezaji wa mpango kwa mujibu wa ratiba ya awali. Wizara ya Maji imekuwa ikisuasua kutenga kwa

ukamilifu fedha za ujenzi wa bwawa tajwa zinazokadiriwa kufikia Shilingi bilioni 179.7 hali inayohitaji msukumo wa Rais.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa miaka mingi kumekuwepo pia udhaifu katika kuchukua hatua za kupunguza uvujaji wa maji na maji yasiyolipiwa (non-revenue water) ambapo ilipaswa toka mwaka 2010 kupunguzwa kutoka katika ya 50-60 mpaka asilimilia 25 lakini mpaka sasa utekelezaji ni hafifu. Tafsiri ya hali hii ni kwamba kwa kuondoa tu upotevu wa maji unaohusisha pia ufisadi na biashara haramu, bila hata kuongeza kiwango cha uzalishaji nusu ya tatizo la maji katika Jiji la Dar Es Salaam ingeweza kupungua au walau hata robo. Hatua hii inahitaji shilingi bilioni 17 tu ambazo Wizara ya Maji, DAWASA na DAWASCO wamekuwa wakisuasua kuzitenga na kutekeleza mipango kwa wakati. Iwapo hatua zote hizo za haraka na zingine zingechukuliwa maeneo ambayo mabomba yalilazwa na kukarabatiwa ambayo hayapati maji na maeneo yote ambayo hayana mtandao wa maji kwa sasa yangepata maji ya kutosha.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka hatua hiyo ingeambatana na kuhakikisha maeneo mengine yanajengewa mtandao mpya wa mabomba ya majisafi hususani Kiluvya, Kibamba, Mbezi Luisi, Mbezi Msumi, Msakuzi, Makabe, Mpiji Magohe, Saranga, Malambamawili, King'ong'o, Matosa, Bonyokwa, Kibangu, Kinzudi, Goba, Kinyerezi, Kipawa, Kiwalani, Vinguguti, Uwanja wa Ndege, Ukonga, Gongolamboto, Pugu, Chanika, Tegeta, Bahari Beach, Boko, Bunju, Salasala, Mbezi Juu, Madale, Kisota, Mabwepande, Mpiji, Vikawe, Mapinga, Zinga, Kilombo, Bagamoyo, Kibaha na Mlandizi ambayo hayakufikiwa na miradi ya awali katika maeneo yanayohudumiwa na DAWASA.

**Mheshimiwa Spika;** Kutokana na matatizo ya maji kuendelea kinyume na maelezo ya Waziri aliyoyatoa bungeni tarehe 4 Februari 2013, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Waziri wa Maji kueleza Bunge hatua gani amechukua katika kutekeleza mapendekezo ya maazimio yafuatayo yaliyotolewa kwenye hoja iliyowasilishwa bungeni:

"NA KWAMBA, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) afanye ukaguzi maalum wa matumuzi ya fedha matumizi ya bilioni 96.4 za mradi wa maji safi na mazingira vijijini katika Jiji la Dar es salaam na Halmashauri zingine na kuwezesha hatua za ziada kuchukuliwa.

NA KWAMBA, Kufuatia kauli iliyotolewa bungeni tarehe 7 Novemba 2012 kuhusu Mpango Maalum wa kutatua tatizo la maji katika Jiji la Dar es salaam uliopitishwa mwezi Machi 2011 Serikali izingatie makisio ya awali ya gharama za mpango huo na kuingiza mahitaji yaliyobaki kwenye Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2013/2014 na Bajeti ya mwaka 2013/2014.

NA KWAMBA, Mpango wa dharura wa kupunguza kero ya maji ulionza kutekelezwa na Wizara ya Maji kwa kushirikiana na DAWASA kuanzia Juni 2010 unaohusisha uchimbaji wa visima 29 uliopaswa kukamilika Oktoba 2011 uwekewe muda wa ukomo wa kukamilika kwa dharura katika maeneo ambayo miradi haijakamilika mpaka hivi sasa ikiwemo iliyozinduliwa Oktoba 2012 yenye kuhitaji miundombinu ya ziada kufikia wananchi zaidi.

NA KWAMBA, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) afanye ukaguzi wa thamani ukilinganisha na ufanisi (Value for Money) wa Mradi wa ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya Majisafi na Majitaka Jijini Dar es salaam na maeneo ya Bagamoyo na Kibaha (Dar es salaam Water Supply and Sanitation Project-DWSSP) kwa kurejea ukaguzi wa kiufundi (technical Audit) uliofanywa na kampuni ya Howard Humphreys.

NA KWAMBA, EWURA ifanye ukaguzi wa kiufanisi (performance audit) wa miradi ya visima vya maji takribani 200 ambavyo vilichimbwa na serikali na kukabidhiwa kwa DAWASCO, jumuiya za wananchi na taasisi mbalimbali lakini haitoi huduma inavyostahili kwa kadiri ya malengo ya awali.
NA KWAMBA, EWURA iharakishe kukamilisha mchakato ulioanza wa kutunga kanuni za udhibiti wa ubora na bei ya huduma ya maji kwa upande wa sekta binafsi katika Jiji la Dar es Salaam.

NA KWAMBA, Kamati husika ya Bunge ijadili taarifa ya ukaguzi wa ufanisi kuhusu usimamizi wa usambazaji wa maji katika maeneo ya mijini (performance audit report on the management of water distribution in urban areas) ya Januari 2012 ili maoni na mapendekezo yazingatiwe wakati wa kujadili na kushauri kuhusu mapendekezo ya mpango wa taifa na bajeti ya nchi.

NA KWAMBA, Serikali iwasilishe bungeni haraka iwezekanavyo muswada wa sheria ya marekebisho ya sheria mbalimbali za majisafi na majitaka (Water Supply and Sanitation Miscellaneous Amendment Bill) ili kushughulikia upungufu uliojitokeza katika utekelezaji wa sheria zilizopo na kuweka mfumo thabiti wa usimamizi wa sekta ya maji nchini."

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani nawashukuru wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji na Waheshimiwa wabunge wengine kwa taarifa zao zilizoniwezesha kuandaa maoni haya ya Kambi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**Magdalena Sakaya (Mb)**

**Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-Wizara ya Maji**

**31.05.2014**

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge kadhaa walisimama)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae chini.

Mheshimiwa Mnyika alikuwa ameomba mwongozo kuhusiana na hotuba ya Kamati. Hii hotuba ya Kamati iliandikwa tarehe 12 Mei, ni wakati ule ambapo Wizara hii ilikuwa ianze. Lakini tukashauriwa kwamba tuisogeze mbele. Sasa naomba Waziri Mkuu uzungumze, tuliisogeza kwa sababu gani? Anaweza akasema Waziri Mkuu ama yeyote. Tuliisogeza mbele ili kusudi tufanye nini? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nimesimama tu kwakweli kusema kwa kifupi kwamba nimeona taarifa ya Kamati, lakini watu wanashauriana hapa kwamba sisi tulikuwa tunaendelea na utaratibu wa kawaida, lakini kwenye mwezi Mei huu, tulikuwa tunatarajia kuweka kama Shilingi bilioni 80 kuanzia wiki ijayo, kwakuwa tunajua mwaka unafungwa mwezi Juni. Ndiyo maana nilitoa juzi maelezo kwamba tulikuwa tunatarajia kwamba tujaribu kukokotoa tena kwenye maeneo mengine ili tuone ni namna gani tunaweza tukawezesha bajeti hii kuweza kupata fedha zinazotakiwa.

Nikumbushe tu pia kwamba, siyo Wizara hii tu ambayo tuna matatizo ya kifedha, kuna Wizara nyingine vilevile ambazo nazo ni lazima tuzipe umuhimu wake. Kwa hiyo, kwakweli kwa maana ya mwezi Mei, hiki ni kiasi ambacho tutaweka kwanzia wiki ijayo, lakini kwa maana ya *budget process,* matarajio yetu ni kwamba mpaka Juni tutaweza kuwa tumepata fedha nyingine tena ambazo tutaongezea kwenye bajeti hiyo, pamoja na kukokotoa vile viposho vingine, inawezekana tukafikia hapo.

Mheshimiwa Spika, kama tutashindwa, basi Waheshimiwa Wabunge, tutaomba mtuelewe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kuna nini Mheshimiwa Rukia? Tusirudie mambo ambayo tumemaliza!

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nilikuwa naomba mwongozo wako kuhusu kanuni namba 68 (7).

Mheshimiwa Spika, leo tumepewa ratiba hii ya kuwa siku ya Jumatatu tarehe 9 Juni, 2014 kutakuwa na Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Bunge, nafasi

iliyoachwa na Mheshimiwa Jenista. Lakini kwakuwa kwa mujibu wa kanuni yetu, Wenyeviti ni watatu, lakini tunayemwona anayefanya kazi hapa ni Mheshimiwa Zungu. Huyu Mwenyekiti mmoja hatujawahi kumwona akifanya kazi.

Naomba mwongozo wako, ikiwa hii nafasi hawezi kuifanyia kazi ajiondoe na badala yake tuchague Mwenyekiti mwingine. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kufuatana na kanuni hizo hizo, Wenyeviti wanafanya kazi kwa kuagizwa ama na Spika ama na Naibu Spika. Kwa hiyo, tunaendelea. Nadhani mlielewa kuwa hii tunafanya kwa kuwaagiza, anaagiwa na Spika ama na Naibu Spika. *Full stop! (Makofi)*

Kwa hiyo, naomba niwatambue wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Maji. Kwanza kabisa kuna familia yake ikiongozwa na mke wake, Mrs Kudra Maghembe. Ahsante! Halafu tunaye Katibu Mkuu Ndugu Bashiri Mrindoko, halafu na Naibu Katibu wake Mkuu, ni Engineer Mbogo Futakamba. *(Makofi)*

Kwa hiyo, watumishi wengine wote kwenye Wizara yao wapo wote hapa, ingawa sikupata familia ya Naibu Waziri, labda tutatangaza Jumatatu. Baada ya kusema hivyo Waheshimiwa naomba niwashukuru sana. Kazi ilikuwa nzito wiki hii na mmefanya kazi kwa uvumilivu sana.

Sasa naomba niwatakie Jumapili njema ya mapumziko, tukutane siku ya Jumatatu, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 2.30 Usiku Bunge lilihairishwa Mpaka siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 2 Juni, 2014 Saa Tatu Asubuhi)*